MAISHA MATAKATIFU
YA
SEYYIDNA AHMAD[AS]

Na

Hadhrat Sheikh Abdul Qadir
(Saudagar Mal – jina la zamani)

MAISHA MATAKATIFU YA SEYYIDNA AHMAD[AS]

Swahili Translation of Hayat-e-Tayyaba (Urdu)

Mwandishi:
Hadhrat Sheikh Abdul Qadir (Saudaagar Mal ─ jina la zamani)

Mfasiri: Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1960
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2020

Kwa maelezo zaidi:

Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dare es Salam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi, Kenya. Simu: +254222111031

Kimechapwa na: Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031

Cover design: Farhan Naseer

ISBN: 978-1-84880-560-6
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

FAHARISI

Faharisi....3
Maelezo ya Mwenezi....21
Neno la Mwandishi....23
Maisha Matakatifu....27
Maisha Matakatifu Dibaji....29
Mlango wa kwanza....31
Ukoo wa Seyyidna Ahmad[as]....31
Mirza Hadi Beg....32
Habari za ukoo alizoandika Seyyidna Ahmad[as] Mwenyewe....32
Bwana Mirza Faidh Muhammad....33
Bwana Mirza Gul Muhammad....34
Bwana Mirza Ataa Muhammad....36
Bwana Mirza Ghulam Murtadhaa....37
Ushahidi wa Sir Lepel Griffin....38
Muhtasari wa habari za kuhamishwa kwa ukoo wa Ahmad kutoka Qadian....39
Shajara ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad Qadiani[as]....41
Harusi ya Hadhrat Mirza Ghulam Murtadhaa....42
Watoto wa Hadhrat Mirza Ghulam Murtadhaa....42
Kuzaliwa kwa Seyyidna Ahmad[as]....43
Utoto wa Seyyidna Ahmad[as]....44
Masomo ya Seyyidna Ahmad[as]....45
Akashiriki katika michezo ya kawaida ya zama zile....46
Harusi yake ya kwanza....46
Upweke wake....47
Kutalii sana....48
Kufuatilia mashtaka....49
Mifano michache ya unyenyekevu wake na khulka zake njema....52
Kamwona Mtume Mtukufu[saw]....53
Ushindani baina ya baba na mwana....55
Kazi mjini Sialkot....56
Kuajiriwa ni gereza....57
Tukio la kimwujiza la hifadhi ya Mungu....57
Baadhi ya habari za muda wa kukaa Sialkot....57

Nia imara ya kuitanasarisha India na mchango wa Sialkot ndani yake 58
Jinsi padri Taylor M.A. alivyoathirika na Seyyidna Ahmad[as] 59
Kuzuia mafuriko ya ukristo yaendeleayo kuzidi. 60
Ushahidi wa kwanza wa Maulana Seyyid Mir Hasan kuhusu Seyyidna Ahmad[as] kukaa sialkot 60
Ushahidi wa pili wa maulana Seyyid Mir Hasan kuhusu Seyyidna Ahmad[as] 64
Ushahidi wa bwana Munshi Sirajuddin 66
Amri ya baba kuacha kazi na kurudi Qadian 67
Kifo cha mama yake mzazi, mwaka 1868 67
Mwelekeo wa Hadhrat Mirza Ghulam Muratadhaa kwenye mambo ya akhera 68
Kakataa kuwa ofisa wa Idara ya Elimu katika utawala wa Kapurthala 70
Kamwomba baba aruhusiwe kukaa mbali kabisa na shughuli za kidunia 70
Ufunuo wa kwanza sawa na utafiti wa hivi sasa na bishara ya mustakabali wenye shani 71
Wingi wa ruya na kashfi, na ishara kwa Mabaniani wa Qadian 73
Kakutana na watawa wa zamani katika kashfi 75
Saumu za miezi 8 au 9 na kuteremka kwa nuru za kimbingu 75
Kakutana na Maulawii Abdullah Ghaznawii na baadhi ya watawa wengine 77
Kifo cha baba yake, Juni 1876 78
Matunzo ya Mungu baada ya kifo cha baba 79
Mazishi ya baba katika kona ya Masjid Aqsa 81
Baadhi ya ruya kuhusu kudumu heshima ya ukoo huu 83
Mwanzo wa maongezi na Mwenyezi Mungu kwa wingi 84
Zama za usimamizi wa kaka yake Mirza Ghulam Qadir 84
Taii amekuja 85
Mirza A'zam Beg kashtaki ili kushiriki katika milki ya mababu ya Seyyidna Ahmad[as] 86
Kesi ya posta 87
Akapona kimujiza katika maradi ya hatari 89

Bishara ya kurejeshwa kazini kwa jaji Nawab Sardar Muhammad Hayat Khan aliyekuwa amesimamishwa kazi 90
Usiku wa mapinduzi ya kiroho yasiyo na kifani 91
Mlango wa Pili 93
Tangu kuandika Barahine Ahmadiyya mpaka baiati ya kwanza 93
Mandhari nyuma ya Barahine Ahmadiyya 93
Kushindwa kwa mwendeleo wa Barhamu Samaj 95
Kuandika na kuchapisha Barahine Ahmadiyya 96
Maoni juu ya Barahine Ahmadiyya 98
1. Rai ya kiongozi maarufu wa Ahle Hadith, Maulawii Muhammad Husain Batalawii 99
2. Maoni ya Sufii Ahmad Jan wa Ludhiana 99
3. Maoni ya Maulawii Muhammad Sharif Bengalori 101
Zama za uchapaji wa baadhi ya sehemu za Barahine Ahmadiyya 102
Juhudi yake kwa kueneza Barahine Ahmadiyya 102
Mwendo wa ajabu wa Nawab Siddik Hasan Khan 103
Kuahirishwa kwa Barahine Ahmadiyya 104
Ufunuo wa kwanza kuhusu kuwa Mujadidi na kutumwa kwake . 105
Kifo cha Bwana Mirza Ghulam Qadir, mwaka 1883 108
Ufaulu wa Bwana Mirza Sultan Ahmad katika mtihani wa 'afisa mapato' 108
Harusi yake ya pili 109
Ishara ya vitone vyekundu, 10 Julai 1885 113
Mwito kwa kuonyesha Ishara, na tangazo la kuwa Mujadidi na kutumwa 115
Utabiri kuhusu ahali na watoto wa binamu zake, 5 Agosti 1885 . 116
Ishara ya vimondo 117
Ishara ya kutokeza kwa nyota 118
Baadhi za habari za kutisha kuhusu Maharaja Dalip Singh na Marehemu Sir Seyyid 118
Maharaja Dalip Singh 119
Safari ya Hoshiarpur na bishara kuhusu Muslih Mau'udi 119
Ishara ya Rehema, yaani bishara kumhusu Muslih Mau'udi 122
Bishara kumhusu yeye mwenyewe, familia yake na wapenzi wake 124
watoto wa Hudhur[as] 126

Utabiri kuhusu Mirza Ahmad Beg na wengineo ─ mwaka 1888.127
Mlango wa Tatu.....129
Tangazo la baiati hadi upanuzi wa Masjid Mubarak 129
Tangazo la Baiati, 1 Desemba 1888.....129
Masharti ya Baiati.....131
Sababu ya kuahirisha tangazo la masharti ya Baiati 132
Ishara iliyofichika katika kujumuika pamoja kuanzishwa Jumuiya na kuzaliwa Muslih Mau'udi 133
Safari ya Ludhiana na Hoshiarpur 134
Baiati ya kwanza, 23 Machi 1889 135
Darul baiati 135
Siku ya baiati.....136
Taratibu ya wafanyao baiati 136
Maneno ya baiati 137
Safari ya aligarh 138
Kurudi Ludhiana.....138
Baiati ya Hadhrat Pir Sirajul Haq Nu'mani, 23 Desemba 1889 ...139
Baiati ya Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan, mtawala wa Malerkotla, 19 Novemba 1890.....139
Madai ya kuwa Masihi Mau'udi, mwishoni mwa mwaka 1890.....139
Uchapaji wa "Fat'he Islam" na "Taudhihe Maraam".....140
Maulawii Muhammad Husain Batalawii katika kambi ya wapinzani 140
Maulawii Muhammad Husain kataka kufanya mjadala 141
Mambo machache kutoka katika barua.....142
Kuandikiana na Maulawii Muhammad Husain kwakoma 144
Mbinu nyingine ya Maulawii Muhammad Husain.....145
Tangazo muhimu.....145
Kukoma kwa kuandikiana na Maulawii Muhammad Hasan pia..146
Safari ya Amritsar na kupatikana sababu za mjadala wa Ludhiana 147
Mjadala wa Ludhiana.....147
Maelezo ya Hadhrat Pir Sirajul Hak Nu'mani.....147
Ghadhabu ya Maulawii Muhammad Husain na hatua ya kamishna mdogo wa Ludhiana.....151
Baiati ya Maulawii Nidhamud Din.....151

Ushahidi wa Gulab Shah Darweshi.....154
Kaandika na kuchapisha Izala Auham 155
Changamoto kuhusu maana ya neno Tawaffi na zawadi ya rupia elfu moja 157
Mada zingine za Izala Auham 158
Tangazo la Hadhrat Mir Nasir Nawab.....159
Baiati ya Hadhrat Maulawii Ghulam Nabii Khushabi.....159
Safari ya Delhi, 28 Septemba 1891 163
Zawadi kwa kuthibitisha uhai wa Masihi kutoka Kurani na Hadithi 167
Taarifa kwa muhtasari ya mkutano wa mjadala wa 20 Oktoba 1891 167
Silaha ya maulamaa wa Delhi ya kukufurisha na kuchochea.....172
Mjadala na Maulawii Muhammad Bashir Bhupalawii, 23 Oktoba 1891 173
Hotuba ya Hudhur[as] kwa Maulawii Muhammad Bashir.....174
Kukaa Patiala wakati wa kurudi 176
Mwito kwa uamuzi wa kimbinguni.....177
Fatuwa ya ukafiri.....178
Maoni ya Hudhur[as] juu ya fatuwa ya kufuru 180
Mkutano wa kwanza wa mwaka, Desemba 1891.....183
Vitabu vya 1890-91.....184
Mwingereza kasilimu, 13 januari 1892.....185
Safari ya Lahore, 20 Januari 1892 185
Hotuba ya Hadhrat Alhaj Maulana Hafiz Hakim Nurud Din[ra] wa Bhera 186
Tukio moja la subira kubwa ya Hudhur[as].....187
Baiati ya baadhi ya ndugu wa Lahore 188
Mdai fulani wa umahdi kamshabulia 188
Hadhrat Seyyid Muhammad Ahsan Amrohi aja kuungana na Jumuiya, Februari 1892 189
mjadala kwa Sheikh Abdul Hakim Kalanorii 189
Mwanzo wa Maulawii Muhammad Husain Batalawii kupungukiwa heshima machoni mwa watu 190
Safari ya Sialkot 191
Maulawii Muhammad Husain Batalawii pia afika Sialkot 192

Safari ya Kapurthala.....193
Sifa za jumuiya ya Kapurthala 193
Safari ya Jalandhar.....195
Safari ya Ludhiana.....195
Faida za safari hizo 195
Mahubiri ya kiroho kwa watafutao haki.....196
Uhamiaji wa Hadhrat Maulawii Abdul Karim[ra], mwishoni mwa mwaka 1892.....198
Vitabu vya mwaka 1892 199
Mkutano wa mwaka 1892.....199
Hadhrat Mir Nasir Nawab kashiriki katika mkutano wa mwaka 1892 199
Uchapaji wa Aina Kamalate Islam, Februari 1893 200
Ziara ya Mtume Mtukufu[saw] mara mbili wakati wa kuandika kitabu hicho.....200
Mahubiri.....201
Mwito wa Islam kwa Malkia Victoria.....201
Wasiwasi wa mapadri.....201
Kuzaliwa kwa Hadhrat Mirza Bashir Ahmad, 20 Aprili 1893.....202
Mwito mwingine kwa Maulawii Muhammad Husain Batalawii kushindana naye kiamali na kiroho.....203
Mwito wa mubahala kwa wasiokuwa waislamu 204
Kuandika kijitabu Barakaatud Dua, 20 Aprili 1893.....206
Utabiri kuhusu Maulawii Muhammad Husain Batalawii, 4 Mei 1893 207
Habari za mjadala "Vita Takatifu".....208
Deputy Abdullah Atham hakushikamana na masharti ya mjadala 214
Tukio moja la ajabu 215
Utabiri kuhusu Abdullah Atham.....215
Baiati wakati wa mjadala 216
Maulawii Muhammad Husain Batalawii kakimbia mubahala, na Sheikh Abdul Hak Gaznawii kaelekea 217
baiati ya Hafidh Muhammad Yakub.....218
Athari ya mubahala.....218

Masheikh wa Amritsar katika chumba cha chini cha Masjid Muhammad Jan....220
Mwenendo wa masheikh....222
hali ya Bwana Atham....222
Kafundishwa maneno asilia elfu arobaini ya lugha ya kiarabu katika usiku mmoja....226
Kuhama kwa Hadhrat Alhaji Maulana Hakim Nuruddin[ra]....227
Vitabu vilivyoandikwa mwaka 1893....228
Kuahirishwa kwa mkutano wa mwaka 1893....229
Ujaji wa Maulana Hasan Ali katika Qadian pamoja na Hadhrat Seth Abdur Rahman Haji Allah Rakha Madrasi....230
Ishara ya jua na mwezi kupatwa, Aprili 1894....235
Baiati ya Khwaja Kamaluddin, mwaka 1894....236
Kutimiza hoja juu ya Maulawii Rusul Baba....236
Maulawii Rusul Baba kafa kwa tauni, 8 Desemba 1902....238
Vitabu vya mwaka 1894....238
Mkutano wa mwaka 1894....239
Kuzaliwa kwa Hadhrat Mirza Sharif Ahmad, 24 Mei 1895....239
Katuma ujumbe kwenda Srinagar kwa kutafiti kaburi la Masihi[as]240
Tanbihi kwa Waaria na Wakristo kwa kurekebisha mijadala ya kidini na ukumbusho kwa serikali, 22 Septemba 1895....244
Safari ya kwenda Dera Baba Nanak, 30 Septemba 1895....245
Vtabu vya mwaka 1895....248
Pendekezo la kutoa ruhusa siku ya Ijumaa, 1 Januari 1896....249
Mwito kwa Wakristo kwenye uamuzi kwa njia bora, 14 Desemba 1896....249
Taarifa ya mkutano wa dini zote, Desemba 1896....252
Vitabu vya mwaka 1896....259
Zawadi ya rupia elfu moja, 28 Januari 1897....259
Kuvunja msalaba na laana, 6 Machi 1897....260
Mwito wa Hudhur[as] wa mubahala kwa wanazuoni wapinzani kwa kutaja majina, kuhusu kufunuliwa kwake na kuongolewa na Mungu....261
Majina ya Masheikh....266
Majina ya Masufii....266

Usadikisho wa Hadhrat Mian Ghulam Farid wa Chachran Sharif 266
laana ya Sheikh Ghulam Dastgir Kusuri na athari yake, mwaka 1897 268
Mwito kwa Masheikh wapinzani kushindana katika ishara 269
Utabiri kuhusu kifo cha Pandit Lekhram.....271
Matukio baada ya kuuawa.....274
Upekuzi wa nyumba ya Hudhur[as] 274
Shauri jema kwa anayemdhania Hudhur[as] kuwa mshiriki katika njama ya uuaji.....274
Ujasiri wa Ganga Bishan.....275
Mwito wa kiapo kwa Maulawii Muhammad Husain Batalawii.....278
Ushahidi mmoja kuhusu uuaji wa Lekhram 279
Faida moja ya kisiasa ya uuaji huo 280
Tukio la ghera ya dini ya Hudhur[as] 280
Kuzaliwa kwa Hadhrat Mubaraka Begam, 2 Machi 1897, sawa na 27 Ramadhan 1314 Hijria 281
Ujaji wa Husain Kami, balozi wa uturuki, katika Qadian, 10-11 Mei 1897 282
Kufichuliwa aibu ya balozi wa Uturuki.....282
Toba ya mzee wa gazeti Chaudawin Sadii 283
Mahubiri kwa mfalme wa Afghanistan:.....284
Amin ya Mahmud, 7 Juni 1897 284
Sherehe ya jubilii ya miaka sitini ya Malkia Victoria, 19 Juni 1897 285
Ombi kwa masheikh na watu wema kwa kuapisha kiapo cha Mungu mwenye shani, 15 Julai 1897.....285
Upanuzi wa Masjid Mubarak.....286
Mlango wa Nne.....287
Kuanzia kesi ya kujaribu kuua hadi kudhihirika tauni 287
Padre Dkt. Henry Martin Clark kamshtaki Hudhur kwa kujaribu kumwua, 1 Agosti 1897.....287
fitina ya Abdul Hamid.....287
maelezo ya Abdul Hamid.....289
Ushahidi wa Maulawii Muhammad Husain Batalawii.....289
Uwakili wa wakili Mwaria Pandit Ram Bhajdat 290

Mungu katawala moyo wa Kapteni Douglas.....291
Uamuzi wa kesi, 23 Agosti 1897.....292
Ujasiri wa kihulka wa Kapteni Douglas.....292
Kauli ya Fadhluddin wakili wa mahakama kuu ya Panjab, kuhusu hulka ya hali ya juu ya Hudhur[as].....293
kapteni Douglas kaathirika mno na dhati tukufu ya Hudhur[as].....295
kuanzisha shule Ta'Limul Islam, Qadian.....296
Safari ya Multan, mwanzoni mwa Oktoba 1897.....296
Kuanzisha gazeti la 'Al-Hakam' kutoka Qadian.....297
Hati ya maombi kwa Viceroy wa India ili kurekebisha hitilafu za dini, Septemba 1897.....297
vitabu vya mwaka 1897.....299
Mkutano wa mwaka 1897.....300
Tangazo la kumtolea fidia ya rupia 20,000 atakayeleta hadithi ya kupaa na kushuka kwa Hadhrat Masihi[as].....301
Utabiri wa kuenea tauni katika Panjab.....302
Kumbukumbu kuhusu kitabu cha "Ummahatul Muminin", 4 Mei 1898.....303
Mwongozo kwa Jumuiya kuhusu kuoana, 7 Juni 1898.....304
Kesi ya kodi ya mapato 1898.....305
Mwito wa mubahala kwa Maulawii Muhammad Husain Batalawii.....305
Matangazo ya Maulawii Abul Hasan Tibeti Na Ja'Far Zatalli.....306
dua ya Hudhur[as], 21 Novemba 1898.....306
Uamuzi wa Mungu kadhihiri.....307
Upekuzi wa polisi.....308
Ombi la kutoa fatuwa.....309
Kuomba fatuwa.....310
Fatuwa za maulamaa.....311
Fatuwa ya Maulawii Abdul Hak Ghaznawii aliye mwanafunzi wa Hadhrat Maulawii Abdullah Ghaznawii.....311
Fatuwa ya Sheikh Abdul Jabbar Bin Adullah Ghaznawii.....311
Fatuwa ya Sheikh Ghulam Muhammad Bugwi, Imamu wa Shahi Masjid Lahore.....312

Fatuwa ya Mufti Muhammad Abdullah, Profesa Wa Oriental College Lahore, mwenyekiti wa Anjuman Himayate Islam Lahore na katibu wa Anjuman Mustasharul Ulamaa.....312
Fatuwa ya Sheikh Abdul Aziz Ludhianawii.....312
sheikh Ahmadullah Amritsari.....312
Fatuwa ya Sheikh Seyyid Nadhir Husain Delhawii:.....313
Kufichuka aibu ya kielimu ya Maulawii Muhammad Husain.....314
Kesi ya kulinda amani na dhamana.....315
Dhila ya Maulawii Muhammad Husain ilikamilika kwa kila jiha..316
Vitabu vya mwaka 1898.....318
Kuzaliwa kwa Mubarak Ahmad, 14 Juni 1899.....320
Kwa njia ya kumbukumbu, serikali iliombwa kuitisha mkutano wa dini zote, 27 Septemba 1899.....320
Ujumbe kwa Nasibin.....322
Mahubiri kwa mabaniani kwa njia ya fonogarafu.....322
Mfululizo wa masomo ya kufundisha kiarabu.....323
Vitabu vya mwaka 1899.....323
Mirza Imamuddin na nidhamuddin wakajenga ukuta mbele ya Masjid Mubarak, 7 January 1900.....325
Ikadhihiri ishara ya kimwujiza katika kesi hiyo.....327
Shule ya Tta'limul Islam iliyokuwa mpaka darasa la nane ikafanywa kuwa mpaka darasa la kumi, 1 Februari 1900.....329
Hotuba ya ki-ufunuo siku ya Idul Adhha, 11 Aprili 1900, sawa na mwaka 1317 hijria.....329
Uchapaji wa Khutba Ilhamiah, 17 Oktoba 1902.....331
Changamoto kwa askofu wa Lahore.....331
Tangazo la kutoa mchango wa Manaratul Masihi, 28 Mei 1900..335
Kuweka jiwe la msingi wa Manaratul Masihi, mwaka 1903.....337
Fatuwa ya kukataza jihadi ya upanga, 7 Juni 1900.....337
Changamoto kwa Pir Mehr Ali Shah Golarawii kwa kumkabili Hudhur[as] ili kuandika maelezo ya Kurani, 20 Julai 1900.....338
Jibu la bwana Pir Mehr Ali Shah.....340
Ujanja mwingine wa Bwana Pir.....342
Ujio wa bwana Pir katika Lahore, 24 Agosti 1900.....342
Barua kwa bwana Pir.....343
Kimya cha bwana Pir.....344

Kutimiliza hoja ya mwisho juu ya bwana Pir 344
Bwana Pir karejea Golra 345
Uandishi wa Ijazul Masihi.....345
Uchapaji wa Ijazul Masihi, 20 Februari 1901 346
bwana Pir kakikosoa "*Ijazul Masihi*" 348
Wizi wa kimaandishi wa bwana Pir 349
Sensa ya mwaka 1901, na Jumuiya kupewa jina 'Musalman Firka Ahmadiyya' ─ waislamu wa dhehebu la Ahmadiyya 355
Vitabu vya mwaka 1900 356
Kwa nini ilikatazwa kusali nyuma ya imamu asiye mwahmadiyya 359
Pendelezo la kuanzisha jarida 'Review of Religions' 360
Dhihirisho la tauni, machi 1901 361
Pendekezo la kuwatahini wenye busara wa Jumuiya 363
Mlango wa Tano.....365
Uandishi wa "Kuondoa Kosa Moja", safari ya kwenda Delhi na kurudi 365
Amin ya Bashir Ahmad, Sharif Ahmad na Mubaraka Begam, 30 Novemba 1901.....376
'Al Manar' 380
Vitabu vya mwaka 1901 381
Nidhamu ya michango ya Jumuiya, 5 Machi 1902.....381
Ishara ya tauni na maendeleo makubwa ya Jumuiya.....382
Ahadi ya kulinda Addar.....386
Tukio kumhusu la Maulawii Muhammad Ali 386
Kashti-e-Nuh, 5 Oktoba 1902 387
Mfuasi kamili hana haja ya kudungwa sindano 387
Kifo kwa nadra hakiwezi kupunguza hadhi ya ishara.....388
Hilaki ya charagh din jammuni.....389
Ndoa ya Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, Oktoba 1902 391
Kuanzisha gazeti Al-Badr 391
Mjadala wa Mudd, wilaya ya Amritsar, 29-30 Oktoba 1902.....392
Uandishi wa 'Ijaze Ahmadi'.....393
Kalamu za wapinzani zikavunjika 395
Maoni juu ya mjadala baina ya Batalawii na Chakralawii 395

Vitabu vya mwaka 1902 397
Ujaji wa Maulawii Thanaullah Amritsari katika Qadian, 10 Januari 1903 398
Safari ya kwenda Jhelum kwa kesi ya Maulawii Karmuddin, 15 Januari 1903 399
Utabiri wa kuondolewa kwa kesi na uenezaji wa utabiri 400
Uamuzi wa ombi la uangalizi la Maulawii Karmuddin 403
Kesi tatu dhidi ya Maulawii Karmuddin 404
Kesi ya Maulawii Karmuddin 405
Maombi ya uhamisho wa kesi 405
Utabiri kuhusu hatima ya kesi, 29 Juni 1903 408
Ombi la kuhamisha kesi lilikataliwa 410
Kashtakiwa rasmi 413
Lala Chandu La'l kashushwa cheo 414
Hakimu mpya Lala Atmaram alivyomtendea Hudhur[as] 415
Ushahidi wa Maulawii Thanaullah 415
Juhudi ya suluhu 415
Uamuzi wa kesi, 18 Oktoba 1904 416
Kurekebisha kosa moja la kihistoria 419
Kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo 419
Kuzaliwa kwa Amatun Nasiir, 28 Januari 1903 420
Ujenzi wa Baitud-Du'aa 420
Hadhrat Sahibzada Abdul Latif Shahid[ra] 421
Bwana Sahibzada arejea nchini mwake na njiani kakaa katika Lahore 421
Kifo cha kishahidi cha Hadhrat Sahibzada Abdul Latif, 14 Julai 1903 423
Matokeo ya mauaji hayo pasipo haki 428
Amir Habibullah Khan kauawa, 20 Februari 1919 429
Mwisho wa Sardar Nasrulla Khan 429
Mwisho wa daktari mpanjabi Abdul Ghani 429
Mwisho wa kadhi Sheikh Abdur Razzak 430
Utawala ukaitoka familia ya Amiri Habibullah Khan 430
Tukio la kimwujiza la kukubaliwa dua, 25 Oktoba 1903 431
Vitabu vya mwaka 1903 432
Tadhkiratush Shahadatain, 16 Oktoba 1903: 433

Kuzaliwa kwa Amatul Hafiidh Begam, 25 Juni 1904: 433
Safari ya Lahore, 20 Agosti 1904 433
Maji hayakunajisika 434
Hotuba ya kuzidisha imani, na wengi walifanya baiati 434
Hotuba yaLahore, 3 Septemba 1904 434
Safari ya Sialkot, 27 Oktoba 1904 435
Ukarimu wa wanajumuiya wa Sialkot 436
Mapokezi 436
Hotuba ya Hudhur[as] baada ya sala ya Ijumaa 437
Pendekezo la hotuba katika mkutano wa hadhara 437
Kwenda mkutanoni 438
Hotuba ya mwenyekiti, Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin 439
Hotuba ya Hudhur[as] 439
Watu wengi walifanya baiati 440
Baiati ya Hadhrat Chaudhari Nasrullah Khan 440
Kurudi Qadian, 3 Novemba 1904 442
Mazungumzo na padri mmoja kwenye stesheni ya Wazirabad 442
"Nguvu moja ya mashariki na hali ya hatari ya Korea," mwaka 1904 takriban 443
Vitabu vya mwaka 1904 444
Zilizala ya kangra, 4 Aprili 1905 444
Hudhur[as] alikaa katika bustani, Aprili hadi Juni 1905 445
Tangazo la ombi muhimu kwa kuzingatiwa na serikali 446
Ujaji katika Qadian wa bwana Abun-Nasr Maulana Ghulam Yasin Aah, nduguye Maulana Abul Kalam Azad, Aprili 1905 447
Matangazo mengine kuhusu matetemeko ya ardhi 449
Tangazo la utabiri wa tetemeko la ardhi 449
Utabiri wa vita kuu, Aprili 1905 450
Maana ya tetemeko lililoahidiwa 454
Wakati wa zilizala kubwa umeahirishwa 455
Utabiri wa zilizala kishairi 456
Ufunuo "Aah, Nadir Shah kaenda wapi", 3 Mai 1905 456
Tafsiri mbili za utabiri 460
Maradhi ya Hadhrat Maulawii Abdul Karim Sialkoti, Agosti 1905 461
Kifo cha Hadhrat Maulawii, 11 Oktoba 1905 462

Juhudi ya kumtibu.....463
Kifo cha Hadhrat Maulawii Burhanuddin Jhelumi, 3 Desemba 1905.....463
Pendekezo la kuanzisha Madrasa Ahmadiyya Qadian.....463
Safari ya Delhi, 22 Oktoba 1905.....464
Dua kwenye kaburi la Khwaja Baki Billah[rh].....465
Akiona Jami‘ Masjid Delhi.....466
Kamwita Hadhrat Maulawii Nuruddin aje Delhi.....466
Kwa nini ni lazima kumwamini?.....466
Watu wanaopaswa nikutane nao.....467
Kuzuru makaburi.....467
Mirza Hairat, mhariri wa Karzan Gazette kamtupia Hudhur[as] changamoto.....468
Kuondoka Delhi, 4 Novemba 1905.....468
Kawasili Ludhiana, 5 Novemba 1905.....469
Hotuba ya Ludhiana, 6 Novemba 1905.....469
Awasili Amritsar, 7 Novemba 1905.....470
Kufika Qadian, 10 novemba 1905.....471
Mlango wa Sita.....473
Kuanzia funuo za kukaribia kifo, mpaka Hudhur[as] kufariki.....473
Funuo za kukaribia kifo, Desemba 1905.....473
Kuanzisha Bahishti Makbara.....475
Masharti ya kuzikwa katika Bahishti Makbara.....475
Kuanzisha kamati ya wasimamizi wa masilahi ya makbara.....476
Maana ya unaibu wa Sadr Anjuman.....476
Vitabu vya mwaka 1905.....477
Limetokea tetemeko katika kasri ya Kisra.....478
Kuwafariji wabangali, 11 februari 1906.....479
Kuanzisha jarida Tash-hizul Adh-han, 1 Machi 1906.....480
Padri Ahmad Masihi kakataa kufanya mubahala, Mei 1906.....480
Harusi ya Hadhrat Mirza Bashir Ahmad, 10 Mei 1906.....482
Dkt. Abdul Hakim Khan kaondolewa katika Jumuiya, mwaka 1906.....482
Ndoa ya Hadhrat Mirza Sharif Ahmad, 15 Novemba 1906, sawa na 27 Ramadhan 1324 Hijria.....489
Ishara ya Mungu kuhusu Mian Abdul Karim, mwaka 1906.490

Ishara kuhusu Hadhrat Seth Abdur Rahman Madrasi, Mei 1906 491
Ishara kuhusu Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan, chifu wa Maler Kotla, mwaka 1906 492
Ishara kuhusu Hadhrat Mir Muhammad Is′hak, mwaka 1906 493
Baadhi ya matukio mbali mbali ya mwaka 1906 495
Vitabu vya mwaka 1906 495
Saadullah Ludhianawii kaangamia, 3 Januari 1907 496
Hudhur[as] aeleza ishara kuhusu Saadullah, Novemba 1906 499
Kifo cha mmiliki na mhariri wa gazeti 'Shubh Chintak' 500
Lala Sharmpat na Malavamal walikimbia kuapa 501
Maulawii Thanaullah Amritsari kauogopa mubahala na kukataa 503
Jibu la upinzani huu kwamba tangazo la Hudhur[as] halikuwa Muswada wa mubahala 513
Marejeo ya Hudhur[as] ya uamuzi wa mwisho 514
Maangamio ya Alexander Dowie, 9 Machi 1907 514
Mwisho wa Dowie 521
Maoni ya Hudhur[as] juu ya kifo cha Dowie 522
Maoni ya magazeti ya Marekani juu ya kifo cha Dkt. Dowie 525
Kamheshimu mkewe mheshimiwa 525
Maradhi ya Hadhrat Mirza Mubaraka Ahmad, 21 Agosti 1907 526
Ndoa ya Mubarak Ahmad, – 30 Agosti 1907 527
Kifo cha Mubarak Ahmad, 16 Septemba 1907 527
Makala ya Hudhur[as] na mkutano wa Aria Samaj ya Wach-chowali, Lahore, 2-4 Desemba 1907 528
Mkutano wa mwaka 1907 529
Vitabu vya mwaka 1907 530
Ndoa ya Hadhrat Nawab Mubaraka Begam, 17 Februari 1908 530
hadhrat Nawab Mubaraka Begam asimulia kuhusu kupanga mahari 531
Harusi, 14 Machi 1909 531
Karamu ya walima, 15 Machi 1909 532
Baadhi ya funuo za Hudhur[as] zikatimia kwa ndoa hiyo 532
Ujio wa kamishna wa fedha katika Qadian, 21 Machi 1908 532
Ujio wa watalii wawili wamerekani katika Qadian, 7 Aprili 1908 533

Safari ya Lahore na kukaririwa kwa funuo za kifo, 27 Aprili 1908 534
Profesa Clement Wragge alikutana na Hudhur[as].....535
Wakili Mian Fadhl Husain kaonana na Hudhur[as], 15 Mei 1908...536
Mwaliko kwa machifu na waheshimiwa viongozi wa Lahore na Mahubiri ya mwongozo, 17 Mei 1908.....538
Kuondoa kosa la Akhbare Aam kupitia barua, 23 Mei 1908.....539
pendekezo la kutoa hotuba katika mkutnao wa hadhara, na "Paighame Sulh".....540
Nasaha ya mwisho 540
Vitabu vya 1908.....541
Mwito wa kushindana katika kukubaliwa dua: 541
Maradhi alimofia 543
Usimuliza wenye kuongeza imani 544
Kifo, 26 Mei 1908 545
Umri wake.....546
Subira ya watu wa nyumbani 547
Huzuni kwa kifo cha ghafla 547
Hali ya wapinzani 547
Kumwosha na kumkafinisha 548
Jeneza likafikishwa Qadian 549
Tangazo kutoka kwa Sadr Anjuman.....551
Maoni ya baadhi ya magazeti wakati wa kifo cha Hudhur[as].....554
Mlango wa Saba.....559
Sifa za Hadhrat Masihi Mau'udi[as] 559
Sura takatifu.....559
Mwili na kimo.....560
Rangi yake.....560
Nywele zake.....562
Ndevu.....562
Mnili na hina.....563
Uso wake.....563
Paji la uso na kichwa.....564
Midomo.....564
Shingo.....565
Mavazi 565

Kiasi cha chakula 569
Nyakati zake 570
Jinsi alivyokula chakula.....571
Alikuwa akila nini.....572
Kunawa mikono.....577
Kujinyima kula 577
Ufunuo.....578
Madawa 578
Maisha kwa kifupi ya mwandishi wa kitabu cha maisha matakatifu581

MAELEZO YA MWENEZI

Hazina nyingine ya kiroho twawaletea wasomaji wetu wa lugha ya Kiswahili kwa sura ya 'Maisha Matakatifu ya Seyyidna Ahmad[as].

Kitabu hiki ni tafsiri ya kitabu 'Hayate Tayyiba' kilichoandikwa na Hadhrat Abdul Qadir ambaye zamani alikuwa Baniani na aliitwa jina Saudagar Mal. Baada ya kuingia katika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya alijitolea wakfu kutumikia dini maisha mazima. Kitabu chenyewe kiliandikwa kwa Kiurdu na kimefasiriwa na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani aliyekuwa zamani Amir na Mbashir Mkuu wa Jumuiyya ya Tanzania. Nami binafsi nikaidurusu na kurekebisha huko na huko.

Nionavyo, kitabu hiki chatosha kabisa kwa mtu mtulivu akisomaye kwa makini sana kutambua ukweli wa Seyyidna Mwanzilishi wa Jumuiyya ya Waislamu Waahmadiyya.

Sheikh Ansar Hussain alijibidiisha kufanya kazi ya fometi. Mwenyezi Mungu Awapatie malipo bora wote walioishughulikia tafsiri hii kutoa kwa sura ya kitabu. Twamwomba Mungu Mwenye Enzi kukifanya kitabu hiki kiwanufaishe wasomaji wote. Amin.

Jamil R. Rafiq
Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan. 15 Oktoba 2019

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ وَعَلٰی عَبۡدِہِ الۡمَسِیۡحِ الۡمَوۡعُوۡدِ

NENO LA MWANDISHI

Katika mwaka 1938 Hadhrat Mirza Bashir Ahmad M.A., Mungu Ampe umri mrefu, Nadhir Talif-o-Tasnif wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Qadian Darul Amaan, aliwaagiza vijana wachache kutunga baadhi ya vitabu sawa na mahitaji ya Jumuiya yanayozidi siku hadi siku. Mimi nikapewa jukumu la kuandika Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad[saw] na Maisha ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as]. Siku hizo nilikuwa ninakaa Karachi kuhusiana na shughuli za kubashiri, na huko huko nikaitayarisha miswada ya vitabu vyote viwili sawa na agizo lake.

Ni maelfu ya ihsani za Mwenyezi Mungu kwamba katika kupitia muswada wa 'Maisha ya Mtume Mtukufu[saw]' Hadhrat Dkt. Mir Muhammad Ismail pia pamoja na mwalimu wangu Hadhrat Maulana Muhammad Ismail walishiriki vizuri na kurekebisha ipasavyo. Na Hadhrat Sahibzada Mirza Sharif Ahmad, Mungu Amweke salama, pia alitoa mashauri yafaayo baada ya kusikiliza baadhi ya sehemu zake. Hadhrat Maulana alikuwa amegharamia kuchapisha kitabu hicho mara ya kwanza katika Qadian Darul Amaan, nacho kikawa kwa miaka mingi katika masomo ya Nusrat Girls High School. Baada ya uhamiaji, kitabu hicho kilipohitajika sana, Bwana Malik Fadhl Husain akakichapisha mara ya pili. Mwenyezi Mungu Ampe malipo mema.

Katika siku hizo hizo ambapo Hadhrat Amirul Muminin Khalifatul Masihi wa Pili, Muslih Mau'udi, Mungu Amsaidie, alienda Karachi kubadilisha hewa kwa manufaa ya afya, mimi nikampa muswada wa 'Maisha ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as]'. Hudhur akausoma kikamilifu na kufanya marekebisho yafaayo sana.

Nasikitika sana kwamba wakati wa uhamiaji, muswada huo wenye thamani ukapotea huko huko Qadian. Baadaye nikapata moyoni mwangu wazo mara kwa mara kwamba maisha hayawezi

kutegemewa. Mwenyezi Mungu Aliniwezesha kuandika Maisha ya Mkuu wa Manabii s.a.w., yafaa nijaribu tena kuandika maisha ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as]. Basi papo hapo sababu yake ikapatikana kwamba mwisho wa mwezi Aprili 1959 mimi nilipokuwa nimeenda Sheikhupura kwa ajili ya mahubiri, Bwana Chaudhry Muhammad Anwar Husain, Wakili na Mwenyekiti wa jamii ya mawakili mjini Sheikhupura na Amiri wa Jumuiya Ahmadiyya katika mji na wilaya ya Sheikhupura alikuwa ameitisha kikao cha wawakilishi wa Jumuiya za wilaya nzima siku ya Jumapili. Katika kikao hicho aliweka jambo hili pia katika mpango wa mwaka ujao kwamba wanajumuiya, hasa vijana wetu, wanapaswa kutalii sana maisha ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as]. Mimi nikakaa kimya wakati huo, lakini nikaamua kabisa moyoni mwangu kwamba baada ya kurudi tu kutoka huko kwenda Lahore, inshallah nitaanza kazi ya kuandika kitabu juu ya maisha yake.

Sababu ya pili ikawa hii pia kuwa tangu muda fulani wakati wa usiku nikilala nilikuwa nasikia sana sauti "Ujitayarishe kwa mtihani. Ujitayarishe kwa mtihani." Kwa hiyo pia nikaelewa kwamba pengine ninafahamishwa tu kwamba nijikusanyie masurufu kwa ajili ya safari ya Akhera. Hivyo, kutokana na mambo hayo nikaamua kuwa yafaa nianze mara moja kazi ya kuandika juu ya maisha yake. Kwa hiyo, leo tarehe mosi Mei 1959, siku ya Ijumaa, katika Msikiti wa Ahmadiyya, ***Delhi Darwaza*** mjini Lahore, ambapo naishi kama mbashiri wa Jumuiya, nimeinua kalamu ili kukamilisha shabaha hii baada ya kufanya dua pamoja na baadhi ya wazee[1]. [2] وَأَرْجُوا مِنَ اللّٰهِ خَيْرًا وَّأَتَوَكَّلُ عَلَيْهِ

Sina nia ya kuandika kitabu kikubwa cha historia, bali kusudio langu ni hili tu kuwa vijana wa Jumuiya na wale marafiki wanaofanya utafiti kuihusu Jumuiya wapatiwe kitabu kimoja kamili mikononi mwao juu ya maisha ya Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya, ambacho kukisoma

[1] Wazee hawa ni Bwana Sheikh Rahmatullah, katibu wa fedha wa eneo la Delhi Darwaza, na Bwana Sufii Ataa Muhammad. Mwenyezi Mungu Awajaze jaza bora. Hawa walipoanza kuomba, basi baada ya dakika mbili tu Bwana Sheikh Rahmatullah akitamka 'Amin' akasema kitabu kimeshakubaliwa na Mwenyezi Mungu, kwa kuwa nilipoinua tu mikono Hadhrat Masihi Mau'udi[as] akaja mbele yangu. Alhamdu lillahi.

[2] Ninatarajia heri kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ninamtegemea Yeye.

waweze kukisia kuwa yule mtu aliyepewa kazi yenye shani adhimu ya kufufua dini ya Uislamu mara ya pili sawa na bishara za Mtume Mtukufu[saw], mtu huyo ni wa daraja gani na maarifa gani, basi tu. Hivyo, kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu naanza kazi hii na kumwomba Yeye tu kuwa Anisaidie kwa Roho Mtakatifu. Amin! Ee Mungu, Amin!

Abdul Qadir

1 Mei 1959

MAISHA MATAKATIFU

Siku hizi kitabu kimoja juu ya maisha ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as] kiitwacho 'Hayate Tayyiba' kilichoandikwa na Bwana Sheikh Abdul Qadir kimetolewa. Mimi hadi sasa sijaweza kusoma kitabu hiki kizima. Lakini sehemu zozote ambazo nimeziona, kutokana na hizo naweza kusema kwamba kitabu hiki kwa fadhili za Mwenyezi Mungu ni nyongeza nzuri sana katika vitabu vyetu. Labda mpaka wakati huu hakijaandikwa kitabu kinachojumuisha katika jalada moja maisha ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as] na kuyaratibisha hivyo. Utafiti na uchunguzi wa matukio uliofanywa sawa na uwezo, na utaratibu na kutoa maoni yapasayo huko na huko yameongeza thamani ya kitabu hiki ... Anayesoma kitabu hawezi kubaki bila kuathirika na dhati tukufu sana ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as] na juhudi zake zenye jadhba za kubashiri Uislamu. Uchapaji pia ni mzuri.

Nionavyo, kitabu hiki siyo tu kinastahili kusomwa na wanajumuiya wenyewe, bali na kienezwe sana baina ya wasiokuwa wanajumuiya. Naomba kwamba Mwenyezi Mungu Akifanye kitabu hiki kuwa chenye kuwanufaisha watu wote na Ampatie malipo mema mwandishi. Amin!

Mirza Bashir Ahamd, Rabwah

12 Januari, 1960

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [3] نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ [4]

وَلَنُحۡیِیَنَّکَ حَیٰوۃً طَیِّبَۃً ثُمَّ لَنَزِیۡنَنَّ حَوۡلًا اَوۡ قَرِیۡبًا مِّنۡ ذٰلِکَ

Tafsiri: Na Tutakujaalia maisha matakatifu miaka themanini au karibu yake.

(Ufunuo wa Hadhrat Masihi Mau'udi[as])

MAISHA MATAKATIFU

DIBAJI

Imeandikwa na Hadhrat Mirza Sharif Ahmad, Rahman Amweke salama.

(Nadhir Islaho Irshad wa ziada, Rabwah)

Kuhusiana na maisha ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as], kitabu hiki kinachochapishwa kwa jina la "Maisha Matakatifu" kimeandikwa na mbashiri wa Jumuiya Ahmadiyya, Sheikh Abdul Qadir (Sodagar Mal, jina la zamani).

Kwa muda mrefu haja ilikuwa ikisikika katika Jumuiya na nje ya Jumuiya kuwa kiandikwe kitabu kwa Kiurdu kielezacho kinaganaga wasifu na maisha ya Mwanzilishi wa Jumuiya Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian. Ingawaje, maudhui yote yanayohusikana moja kwa moja au kwa njia fulani na mada hii yapo katika vitabu mbalimbali vya Jumuiya, hata hivyo hakikuwepo kitabu kimoja mahususi kilichojumuisha na kukusanya yote hayo pamoja ambacho kiweze kuwa toshelevu kikamilifu. Basi, Alhamdulillahi mwandishi wa kitabu hiki kwa bidii yake yenye ikhlasi na juhudi yake ametimiza kwa kiasi kikubwa haja hii muhimu. [5] فَجَزَاہُ اللّٰہُ اَحۡسَنَ الۡجَزَاء

Nionavyo, kitabu hiki kwa njia hii pia kitawafaidisha zaidi wasomaji kwamba ingawaje shabaha yake ilikuwa kuandika maisha, hata hivyo kwenye sehemu zifaazo yameelezwa pia matukio yaongezayo imani

[3] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[4] Twamhimidi Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

[5] Mwenyezi Mungu Ampe malipo mema. Mwenezi.

ambayo bila kuongeza ukubwa wa kitabu yanatia mwanga sana kwenye sera tukufu za Hadhrat Mwanzilishi[as]. Vivyo hivyo mahali pafaapo funuo mbalimbali, bishara, vitabu, safari na mijadala ya Hudhur[as] imeelezwa kwa namna ambavyo kana kwamba muhtasari wenye thamani na kiini cha elimu ya hoja za kimantiki iliyoletwa na Hadhrat Masihi Mau'udi[as] chabainika. Basi, kwa jumla, kitabu hiki kwa yakini ni chenye kuongeza elimu pia na kuzidisha imani vile vile.

Dua yangu ni kwamba Mwenyezi Mungu Azitilie baraka bidii za mwandishi na kukifanya kitabu hiki kiwe chenye kuwaongoza viumbe wa Mungu. Amin!

Mirza Sharif Ahmad

15 Desemba 1959

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [6] نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ [7]

MLANGO WA KWANZA

(Tangu Kuzaliwa Hadi Azimio La Kuandika Barahine Ahmadiyya)

UKOO WA SEYYIDNA AHMAD[AS]

Hadhrat Masihi Mau'udi[as] alitokana na kaumu maarufu Barlaas ya Waajemi. Mkuu wa kaumu hii, jina lake Karachar, aliyepita katika karne ya sita Hijria, alipata kusilimu. Bwana Karachar alikuwa waziri wa mfalme Chughtai na jemedari mashuhuri. Alikalisha kaumu yake vitongojini mwa mji wa Kish, maili thelathini takriban kutoka Samarkand, upande wa kusini. Mjukuu wake Barkaal alipata wavulana wawili, mmoja wao aliitwa Taraghe na mwingine Haji Barlaas. Mfalme mashuhuri wa Irani Taimur[8] Sahibkiran[9] alikuwa mtoto wa Taraghe. Serikali ya Kish aliirithi Haji Barlaas, lakini kijana wa nduguye Taimur alipopata nguvu, Haji Barlaas alilazimika kuondoka sehemu hii.

Kutokana na historia ya wakati ule inaonekana kwamba maeneo yote kuanzia Valga mpaka bahari ya Faris, na kuanzia Afghanistan na Balochistan hadi Bukhara yaliitwa Faris. Bali sawa na kauli ya wengine sehemu nyingi ya Afghanistan na Balochistan ya siku hizi, na toka chanzo cha mto Ganges hadi maeneo ya kaskazini mpaka kwenye Kashghar, yalikuwemo katika Faris, na Kish pia imo katika eneo hilo, lakini katika zama za Makhalifa wa Kiabbasi eneo hili lilihesabiwa kuwa sehemu ya *Mawara unnahr*.[10]

---

[6] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[7] Twamhimidi Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

[8] Taimur alikuwa Mkuu wa ukoo wa mfalme Dhahiruddin Babur, mwanzilishi wa Dola la Kimughali.

[9] Sahibkiran: Ni lakabu ya mfalme Taimur, maana yake 'mshindi'.

[10] Annajmuth thakib, jalada 2, uk. 182

MIRZA HADI BEG

Taimur alipomfukuza babake mdogo Barlaas katika serikali yake, yeye alikimbilia Khurasaan na akatawafu huko. Kisha, baadaye, Taimur alishinda sehemu ya Khurasaan na akawakabidhi sehemu hiyo watoto wa babake mdogo. Kwa hiyo wakaendelea kuishi huko huko.

Lakini baada muda fulani mzee mmoja wa ukoo huo, Mirza Hadi Beg, pamoja na familia yake alirudi kwao Samarkand. Na baada ya kukaa huko muda fulani, akahama watani wake kwa sababu zisizojulikana, na kuelekea India.

Seyyidna Ahmad[as] akitaja kuhama kwake alisema:

> "Katika enzi ya mfalme Babur, aliyekuwa mwanzilishi wa serikali ya Kichughtai, mababu zangu wakahama Samarkand[11] na kuwasili Delhi pamoja na jamii kubwa kwa sababu isiyoelezwa. Kwa hakika jambo hili halikuwa wazi kutokana na nyaraka zile ya kuwa waliwasili India pamoja na Babur au mara baadaye. Wakafika pamoja naye au siku chache baadaye, lakini yathibitika kwa uwazi kwa kuchunguza nyaraka nyingi kuwa walikuwa na uhusiano maalum na ukoo wa kifalme ambao kwa sababu yake walihesabiwa miongoni mwa machifu waheshimiwa machoni mwa serikali. Kwa hiyo, wakapewa na mfalme vijiji kadha kumiliki na wakawa wamiliki wa mashamba makubwa."[12]

HABARI ZA UKOO ALIZOANDIKA SEYYIDNA AHMAD[AS] MWENYEWE

Hapa yafaa kunukuu zile habari za ukoo wake alizoandika Seyyidna Ahmad[as] mwenyewe katika baadhi ya vitabu vyake. Hudhur[as] Anasema:

> "Kaumu yetu ni Mughal Barlaas. Kutokana na nyaraka za zamani za wazee wetu zilizohifadhiwa mpaka sasa yaonekana

[11] Nchini Turkistan

[12] Izala Auhaam, uk 121, 122 katika maelezo ya pembeni.

kwamba walifika katika nchi hii kutoka Samarkand pamoja na watu wapatao mia mbili, wafuasi, mahudumu na ahali zao. Aliingia katika nchi hii kama chifu mhashamu na kuishi katika mji huu uliokuwa ni pori wakati ule, uliokuwa kama maili sabini kutoka Lahore upande wa Kaskazini Mashariki. Waliujenga na kuuita Islampur, uliojulikana baadaye kwa jina la Islampur Qadhi Majhi. Polepole neno la Islampur likasahaulika, na mahali pa Qadhi Majhi likabaki Qadhi pekee ambalo hatimaye likawa Qadi ambalo likageuka likawa Qadian.[13] Na sababu ya kuitwa Qadhi Majhi imeelezwa kwamba eneo lote hili ambalo urefu wake ni maili 90 liliitwa Majha. Pengine sababu ya kuitwa majha ilikuwa ni kuwa katika nchi hii nyati walipatikana kwa wingi, na katika lugha ya Kihindi nyati anaitwa Majh. Kwa vile wazee wetu walipewa utawala pia pamoja na vijiji kadha, kwa hiyo waliitwa ma-Kadhi. Sijui kabisa kwa nini na kwa sababu gani wazee wetu walihamia hapa kutoka Samarkand, lakini nyaraka zinaonyesha kwamba katika nchi hiyo pia walikuwa miongoni mwa matajiri na watawala waheshimiwa na wakalazimika kuacha nchi ile kwa sababu ya uadui na mfarakano fulani. Baada ya kufika katika nchi hii, mfalme wa wakati ule aliwapa vijiji vingi vikiwa miliki yao, basi wakawa na utawala wa kudumu katika maeneo haya."[14]

BWANA MIRZA FAIDH MUHAMMAD

Baada ya kifo cha Mirza Hadi Beg, ukoo wake uliendelea kuzidi katika adhama na heshima hata kwamba katika kizazi cha 9, wakati wa enzi ya Mirza Faidh Muhammad, ukoo huu ukawa na uhusiano mkubwa zaidi na serikali ya Kimughal. Basi, katika mwaka 1716 mfalme Farrukh Seyar alimpa Mirza Faidh Muhammad cheo cha 'Haft Hazaari'[15] na lakabu ya '*Adhdud*

[13] Qadian kutoka Batala ni maili 12, kutoka Amritsar maili 36 na kutoka Lahore maili 70. (Mwandishi)

[14] Kitabul Bariyya, maelezo ya pembeni, uk. 121, 122. Chapa ya kwanza.

[15] Haft Hazaari, maana yake 'mwenye Elfu saba', muradi wake ni 'kamanda wa maaskari elfu saba'.

Daula'[16]. Hiyo ilimaanisha kwamba alikuwa na madaraka ya kuwa na jeshi la vijana 7000, na heshima hii walikuwa wakipewa katika zama zile wenye kutegemewa na kuaminika sana na serikali.

BWANA MIRZA GUL MUHAMMAD

Seyyidna Ahmad[as] katika kitabu chake, Kitabul Bariyya, ameandika:

> "Katika zama za mwanzo za Masingasinga, baba ya babu yangu Bwana Mirza Gul Muhammad alikuwa chifu mashuhuri wa maeneo hayo, aliyekuwa mmiliki wa vijiji 85 wakati ule. Vijiji vingi vilitwaliwa kwa kushambuliwa na Masingasinga. Hata hivyo, hali ya ukarimu wake ilikuwa ni kwamba aliwapa baadhi ya machifu Waislamu wenye shida vijiji kadha kutoka katika vijiji hivi vichache, ambavyo bado hao wanavyo mpaka sasa. Ilmuradi, katika zama za machafuko na kukosekana serikali hasa, yeye alikuwa chifu wa kujitegemea wa maeneo yake. Daima watu wapatao 500, pengine wakapungua au kuzidi, walikuwa wakila chakula pamoja naye. Na wanachuoni karibu mia moja, watawa na mahafidhi wa Kurani walikuwa wakikaa naye waliokuwa wakipewa mishahara mikubwa. Na katika baraza lake, aya za Kurani na Hadithi za Mtume[saw] zilikuwa zikitajwa sana, na miongoni mwa mahadimu na wahusika wote hakuwa hata mmoja asiyekuwa anasali. Bali hata wanawake wenye kazi ya kusaga unga walikuwa wakisali sala tano na sala ya Tahajudi pia. Waheshimiwa Waislamu wote wa maeneo haya ambao wengi wao walikuwa Maafghani, walikuwa wakiiita Qadian, iliyoitwa wakati huo Islampur, kuwa Makka. Kwani, wakati ule wa vurugu, mji huo wenye baraka ulikuwa kimbilio la kila Mwislamu, na katika sehemu nyingi zingine ilionekana kufuru, ufasiki na dhuluma, ilihali Qadian ilikuwa ikinukia Islam, uchamungu, utakaso na uadilifu. Mimi mwenyewe nimewaona wale walioona zama zilizo karibu na zama hizo, hao walikuwa wakiisifu sana Qadian, kana kwamba hiyo ilikuwa bustani katika zama zile ambamo mlikuwemo mamia ya mimea

[16] 'Adhdud Daula, maana yake 'Mkono wa Dola', yaani Nguvu ya Dola.

ya wasaidizi wa dini, mawalii, wanachuoni, waungwana na mashujaa. Katika maeneo hayo habari hizi zinajulikana kwamba marehemu Bwana Gul Muhammad alikuwa miongoni mwa wazee wataalamu wa zama hizo na mwenye kuonyesha karama, ambaye kwa kukaa naye waja wa Mungu, watawa na wanachuoni wengi walijumuika katika Qadian. Na ni ajabu kubwa sana kwamba karama zake nyingi zinatambulikana kiasi hiki kwamba hata kundi kubwa la wapinzani wa dini pia liliendelea kutoa ushahidi wake. Ilmuradi, zaidi ya Uchifu na Uamiri, alipata umashuhuri katika sifa zake za uaminifu, uchamungu, ushujaa, uthabiti, kuihami dini na kuwahurumia Waislamu. Na masahibu wake wote walikuwa wacha Mungu, wema, wenye ghera ya Kiislamu, wenye kujiepusha na ufasiki na maovu, mashujaa na wenye heba. Nilisikia kutoka kwa baba yangu mara kadha kwamba katika zama hizo waziri mmoja wa serikali ya Kimughal alifika Qadian aliyeitwa Ghiyathud Din. Yeye akajionea njia za busara ya Mirza Gul Muhammad, na hima na uthabiti, uimara, akili, fahamu na kuihami Islam, jadhba ya kuisaidia dini, uchamungu, utakaso na adabu ya baraza, na akakuta Baraza lake dogo limejaa wenye akili, wema na mashujaa, hapo akiwa na machozi machoni akasema, kama ningalijua habari hii mapema kwamba katika pori hili yupo mtu wa ukoo wa Kimughal ambaye anazo sifa zote za lazima za kutawala, basi ningalijaribu kuulinda utawala wa Kiislamu kwa kumkabidhi kiti cha kifalme cha Delhi katika siku za uzembe na kukosekana kipawa na hali mbovu za wafalme wa Kichughtai.

"Hapa itafaa kuandika pia kwamba baba mzazi wa babu yangu yaani Bwana Mirza Gul Muhammad alifariki kwa maradhi ya kwikwi pamoja na matatizo mengine pia. Wakati wa kuzidi maradhi, matabibu kwa kauli moja walisema kuwa kama akitumia kileo kwa siku chache pengine kitamsaidia, lakini hawakuthubutu kumwambia. Hatimaye baadhi yao kwa maneno laini wakamweleza. Hapo akasema kwamba Mwenyezi Mungu Akitaka kuniponya, basi dawa Alizoumba zipo nyingi, sitaki kutumia kitu hiki kichafu na nipo radhi juu ya kudra ya Mungu.

Hatimaye baada ya siku chache akafariki na maradhi hayo.[17] Kifo kilikuwa kimekadiriwa, lakini njia yake hii ya uchamungu ikawa kumbukumbu kwa kudumu kwamba alikubali kifo kuliko kutumia kileo. Kwa kuepuka mauti, mtu anajichagulia njia yoyote ile, lakini yeye aliona afadhali kifo kuliko kumwasi Mungu. Ni masikitiko juu ya hali ya hawa malodi, matajiri na machifu ambao katika maisha haya ya siku chache wasipomjali Mungu na amri zake wanamwasi kwa kuvunjilia mbali mahusiano yote na Mungu. Wanakunywa pombe kama maji na hivyo wakichafua sana na kunajisi maisha yao, na wakikosa umri wao wa kawaida pia wanakufa haraka kwa maradhi ya hatari na wanawaachia vizazi vyao mfano mbaya."

BWANA MIRZA ATAA MUHAMMAD

"Kwa kifupi, sasa, ni kwamba alipofariki baba wa babu yangu, pahali pake babu yangu Bwana Mirza Ataa Muhammad alishikilia nafasi yake. Katika enzi yake, kwa hekima na masilahi ya Mungu, Masingasinga walishinda vita. Babu yangu marehemu kwa kulinda maeneo yake alitumia mbinu zote, lakini akashindwa mpaka akabakiwa na mji wa Qadian pekee. Qadian wakati ule ilikuwa ni mji kama ngome[18] iliyokuwa na buruji nne na ndani ya buruji walikaa wanajeshi na ilikuwepo mizinga michache. Ukuta wa mji ulikuwa na urefu wa kwenda juu futi 22, na upana wake ulikuwa kiasi hiki hata kwamba marukwama matatu yaliweza kupita sambamba. Na ikawa hivi kwamba kundi moja la masingasinga liitwalo Ram Garhia liliingia katika Qadian kwa idhini kiujanja, kisha wakajitwalia bila haki. Wakati huo wazee wetu wakafikiwa na maangamio makubwa, wakashikwa kama wafungwa kama wana wa Israeli, na wakanyang'anywa mali zao zote. Misikiti mingi na nyumba nzuri zilibomolewa, bustani zikakatwa kwa ujahili na bughudha.

[17] Bwana Mirza Gul Muhammad akafariki labda mwaka 1800, sawa na Siratul Mahdi, sehemu ya kwanza, uk.129.

[18] Ngome ya Qadian ilikuwa na malango manne, majina yao ni haya: Lango la Ki-Batala, lango la mlimani, lango la Mauri na lango la Nangli.

Baadhi ya misikiti ambayo mmojawapo mpaka sasa umeshikiliwa nao, iligeuzwa kuwa Dharamsala, yaani nyumba ya ibada ya Masingasinga. Siku hiyo maktaba pia ya wazee wetu yalichomwa moto, ambamo mlikuwa na nakala mia tano za Kurani Tukufu zilizoandikwa kwa mkono, nazo zilichomwa kwa utovu wa adabu. Hatimaye, Masingasinga kwa kufikiria jambo fulani wakawaamuru wazee wetu kuondoka humo. Basi, wote, wanaume kwa wanawake, wakafukuzwa kwa marukwama.[19] Wakakimbilia utawala fulani[20] wa Panjab. Baada ya muda mfupi, kwa njama ya hao maadui babu yangu alipewa sumu.

BWANA MIRZA GHULAM MURTADHAA

"Kisha katika mwisho wa zama za Ranjit Singh babangu, Bwana Mirza Ghulam Murtadhaa, alirudi Qadian na akarudishiwa vijiji vitano kutoka vijiji vya babake, kwani katika muda huo Ranjit Singh aliimarisha utawala wake mkubwa kwa kuzishinda tawala ndogo ndogo. Hivyo vijiji vyetu vyote pia akavimiliki Ranjit Singh, na kutoka Lahore mpaka Peshawar, na upande mwingine mpaka Ludhiana, utawala wake ulipanuka. Ilmuradi, utawala wetu wa zamani ulipotea isipokuwa vilibaki vijiji vitano tu mkononi mwetu. Hata hivyo, kwa sababu ya kuwa ukoo wa zamani, babangu Bwana Mirza Ghulam Murtadhaa alikuwa chifu maarufu katika eneo hilo. Katika Baraza la Gavana alikuwa anakaribishwa akiwa miongoni mwa machifu wenye kupewa kiti. Hata Sir Lepel Griffin amemtaja katika kitabu chake, "Historia ya Machifu wa Panjab". Ilmuradi, alipendwa sana na watawala na mara nyingi kwa kumfariji wakuu wa serikali wa wakati ule, Naibu wa Kamishna na Kamishna, walikuwa wakimtembelea nyumbani kwake."[21]

[19] Mnamo mwaka 1802, Qadian, uk. 79.

[20] Utawala wa Kapurthala

[21] Kitabul Bariyya, uk. 134-146

USHAHIDI WA SIR LEPEL GRIFFIN

Naona itafaa kunukuu hapa aliyoandika Sir Lepel Griffin katika kitabu chake kilichotajwa juu, "Kumbukumbu la Machifu wa Panjab", kuhusu ukoo wa Hadhrat Ahmad[as] wa Qadian. Anaandika:

> "Katika mwaka wa mwisho wa zama za utawala wa mfalme Babur, yaani mwaka 1530, Mughali mmoja aitwaye Hadi Beg, mkazi wa Samarkand, akiacha kwao akaja Panjab na kukaa katika Wilaya ya Gurdaspur. Yeye alikuwa ameelimika kiasi fulani na alifanywa kadhi ama hakimu wa vijiji sabini[22] vya vitongojini mwa Qadian. Inasemekana kwamba yeye alianzisha Qadian na akaiita jina Islampur Kadhi ambalo likigeuka-geuka likawa Qadian.[23] Kwa vizazi kadha ukoo huu ulikuwa na vyeo vyenye heshima katika zama za utawala wa kifalme, na katika zama za Masingasinga tu ulifilisika. Bwana Gul Muhammad na mwanaye Bwana Ataa Muhammad waliendelea kupigana na Masingasinga wa dhehebu la Ram Garhia na Kanayya Musal waliokuwa wamejitwalia maeneo ya Qadian, na hatimaye baada ya kunyang'anywa maeneo yake yote Ataa Muhammad alimkimbilia Sardar Fateh Singh wa Ahluwalia huko Begowal na akaishi huko kwa amani kwa miaka 12. Baada ya kifo chake, Bwana Ranjit Singh, aliyejitwalia maeneo yote ya kabila la Ram Garhia, alimwita Bwana Ghulam Murtadhaa aje Qadian[24], na akamrudishia sehemu kubwa ya maeneo ya babu zake. Hapo Bwana Ghulam Murtadhaa pamoja na ndugu zake alijiunga na jeshi la Maharaja na kutumikia sana mipakani mwa Kashmir na sehemu zingine. Katika enzi za Naunihal Singh, Sher Singh na utawala wa Lahore, Bwana Ghulam Murtadhaa daima alitumikia jeshini. Mnamo mwaka 1841, yeye akatumwa pamoja na jemedari Wanchora, aende Mandi na Kullu, na katika mwaka

[22] Hii si sahihi. Kwa hakika vilikuwa vijiji 85 kama ilivyoelezwa juu. Mwandishi.

[23] Katika maelezo ya pembeni ya "Kumbukumbu la Machifu wa Panjab" imeandikwa kwamba katika lugha ya Kiarabu herufi *dhad* inatamkwa *dal* katika lugha ya Kipanjabi.

[24] Hili ni tukio la mwaka 1834 sawa na kitabu: "Qadian", uk. 79

1843 akiwa kamanda wa kikosi cha waenda miguu alitumwa kwenda Peshawar. Katika machafuko ya Hazara alifanya kazi kubwa sana, na wakati wa uasi wa mwaka 1848 aliendelea kuwa mwaminifu wa serikali yake na kuipigania. Wakati huo nduguye, Bwana Ghulam Muhyiddin, pia alitoa huduma bora. Wakati Bwana Maharaj Singh alipokuwa anaelekea Multan pamwe na jeshi lake kumsaidia Diwan Mulraj, hapo Bwana Ghulam Muhyiddin na makabaila wengine wa Langar Khan Sahiwal na Sahib Khan Tiwana waliwachochea Waislamu na kwa kuungana na jeshi la Bwana Misr Sahibdial walipigana na waasi na kuwashinda kabisa. Waasi hawakupata njia ya kukimbilia popote isipokuwa mto Chenab ambamo watu mia sita wakafa maji.

"Wakati wa mwungano,[25] ardhi ya ukoo huu ilitwaliwa, lakini Bwana Ghulam Murtadhaa na ndugu zake walipewa pensheni ya Rupia mia saba, lakini Qadian na vijiji vya vitongojini mwake vilibaki katika miliki yao. Ukoo huu ulitoa huduma nzuri katika mwaka 1857. Bwana Ghulam Murtadhaa akaandika watu wengi jeshini. Na mwanaye Bwana Ghulam Qadir alikuwa katika jeshi la Bwana General Nicholson alipowaua huko Trimmu Ghat waasi wa askari wenyeji wa kikosi cha waenda miguu Na. 46, waliokimbia Sialkot. Bwana General Nicholson alimpa Bwana Ghulam Qadir hati ambamo akaandika kuwa mnamo mwaka 1857 ukoo huu wa Qadian, Wilaya ya Gurdaspur, uliendelea kuwa mwaminifu kuliko koo zote nyingine."[26]

MUHTASARI WA HABARI ZA KUHAMISHWA KWA UKOO WA AHMAD KUTOKA QADIAN

Hapo juu, mahali fulani, katika maelezo ya pembeni, imeishaelezwa kwamba Bwana Mirza Gul Muhammad alifariki mnamo mwaka 1800. Baada ya kifo chake katika zama za Bwana Mirza Ataa Muhammad, Masingasinga kwa kisingizio cha kuonana kirafiki na

[25] Yaani Panjab ilipounganishwa na sehemu iliyotawaliwa na Waingereza. Mwandishi.

[26] Kumbukumbu la machifu wa Panjab, J. 2, uk. 67,68

Mirza Ataa Muhammad waliingia ndani, na kuitwaa Qadian[27], na Bwana Mirza aliyetajwa juu pamoja na familia yake alilazimika kukimbilia mjini Begowal katika Utawala wa Kapurthala. Hii ikatokea mnamo mwaka 1802 au 1803. Hizi ni habari za siku zile ambapo mtawala wa Kapurthala alikuwa Raja Fateh Singh. Raja Fateh Singh akamtendea vizuri kwa moyo mkunjufu na akataka kumpatia vijiji viwili vya kuponea, lakini Bwana Mirza alikataa akisema tukikubali vijiji hivi, kizazi chetu kitakosa hima na watasahau kuendeleza mapokeo ya ukoo wao.

Bwana Mirza Ataa Muhammad katika zama za uhamisho akivumilia shida nyingi kwa miaka 11 mfululizo akafariki huko Kapurthala mnamo mwaka 1814.[28] Mwanaye Bwana Mirza Ghulam Murtadhaa alileta jeneza lake Qadian saa za usiku, na juu ya Masingasinga kuzuia alimzika kwa ushujaa sana katika makaburi ya familia yake. Baada ya kifo chake, familia hiyo haikubakiwa na mtu wa kumtegemea, na hali hii iliendelea karibu miaka ishirini. Lakini kwa vile wakati wa kuzaliwa kwa Masihi Mau'udi ulikuwa unasogelea karibu, kwa hiyo Mwenyezi Mungu Alipanga kwa ghaibu mpango wa kurudi Qadian. Ikawa hivi kwamba mnamo mwaka 1834 au 1835, Maharaja Ranjit Singh alimrudishia babake Bwana Mirza Ghulam Murtadhaa vijiji vitano vya utawala wa Qadian vilivyobaki mkononi mwake mpaka utawala wa Masingasinga, yaani kwa miaka 14 mfululizo. Lakini, tarehe 29 Machi 1849 jimbo la Panjab lilipochukuliwa na Waingereza, hapo pamoja na maeneo ya viongozi waasi, Qadian pia ilinyang'anywa na kwa kufariji pensheni kidogo ya Rupia 700 iliwekwa kwa familia hii. Utawala wa Waingereza ulipoimarika katika Panjab, basi kama ilivyotajwa juu, Hadhrat Mirza Ghulam Murtadhaa alisaidiana kikamilifu na serikali mpya sawa na desturi yake ya zamani. Habari zake zilizobaki zitaendelea kuelezwa mbele pamoja na maisha ya Masihi Mau'udi[as].

Kwa vile, sasa, yaanaza kuandikwa maisha ya Mtukufu Hudhur[as], kwa hiyo yafaa shajara ya ukoo wake itiliwe hapa chini:

[27] Kuhusu jambo hili baadhi ya wenyeji wasiokuwa Waislamu hawakuonyesha uaminifu.

[28] 'Qadian', uk. 78

SHAJARA YA HADHRAT MIRZA GHULAM AHMAD QADIANI[AS]



Tanbihi 1: Kwa vile Seyyidna Ahmad[as] alitokana na kizazi cha Muhammad Sultan, kwa hiyo shajara ya wazao wake tu umetiwa kwa kifupi. Kwa maelezo zaidi angalieni Siratul Mahdi, sehemu ya kwanza, uk. 116, utungo wa Hadhrat Mirza Bashir Ahmad.

Tanbihi 2: Habari za baada ya Mirza Faidh Muhammad zinajulikana zaidi kiasi fulani, kwa hiyo shajara ya baada yake imetiwa kikamilifu.

HARUSI YA HADHRAT MIRZA GHULAM MURTADHAA

Baba mzazi wa Seyyidna Ahmad[as], Hadhrat Mirza Ghulam Murtadha, alioa kutoka katika ukoo wenye heshima wa Kimughali wa huko Aimma, Wilaya ya Hoshiarpur. Mamake Mtukufu Hudhur aliitwa Charagh Bibi. Yeye alijaa sifa za ukinaifu, ukarimu na kuwasaidia maskini. Alikuwa anatia umuhimu sana kuwalisha maskini na alikuwa akiwatimizia mahitaji ya wahitaji. Hii ilikuwa kawaida yake kwamba maskini yeyote alipofariki, yeye alikuwa anaipeleka sanda nyumbani kwake.

WATOTO WA HADHRAT MIRZA GHULAM MURTADHAA

Hadhrat Charagh Bibi alimzalia Hadhrat Mirza Ghulam Murtadhaa watoto watano:

1. Murad Bibi: Yeye aliolewa na Mirza Muhammad Beg wa Hoshiarpur. Yeye alikuwa mwenye kupata kashfi na ufunuo.
2. Mirza Ghulam Qadir: Yeye alikuwa kaka wa Seyyidna Ahmad[as]. Alikuwa na vyeo mbalimbali katika serikali ya Kiingereza. Pia alikuwa Mkurugenzi katika ofisi ya Wilaya yake, yaani Gurdaspur. Atatajwa sehemu mbalimbali katika kurasa zijazo.
3. Mvulana mmoja alizaliwa, akafariki baada muda mfupi.
4. Jannat Bibi: Yeye alikuwa pacha wa Seyyidna Ahmad[as], na alifariki haraka.
5. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad Qadiani, Masihi Mau'udi na Mahdi Mtakatifu ambaye sasa takdiri zihusuzo dunia zinaambatana naye.

KUZALIWA KWA SEYYIDNA AHMAD[AS]

Alizaliwa katika zama za utawala wa Masingasinga ambapo ilikuwa haihifadhiwi taarifa ya tarehe ya kuzaliwa, na pia familia yake ilikuwa katika matatizo, kwa hiyo hakuna hati maalum ya tarehe ya kuzaliwa kwake. Hata hivyo, Hadhrat Mirza Bashir Ahmad M.A. alikisia kutokana na baadhi ya maandishi na masimulizi kwamba alizaliwa tarehe 13 Fabruari 1835, sawa na 14 Shawwal 1250 Hijria, siku ya Ijumaa wakati wa sala ya Alfajiri. Jambo hili lafaa kutajwa kwamba pamoja na kuzaliwa kwake zama za ugenini na ukata wa familia yake zikaisha kwa kurudishwa Qadian.

Imeshatajwa nyuma kwamba yeye alizaliwa pacha. Binti aliyemtangulia alifariki baada ya siku chache. Kuashiria kwenye tukio hili, yeye wakati mwingine alikuwa akisema, "Nafikiri kwa njia hii Mwenyezi Mungu Aliniondolea tabia ya kike. Kuzaliwa kwake pacha kulikuwa na hekima hii pia kwamba kwa sababu hiyo ilitimia bishara ile iliyoandikwa katika baadhi ya maandiko ya Kiislamu kwamba Mahdi Mau'udi atazaliwa pacha.[29]

Miaka michache kabla ya kuzaliwa kwake, Mujadidi wa karne ya 13 Hadhrat Seyid Ahmad Brelawii na Hadhrat Ismaili shahidi walikwisha kuwa mashahidi katika Balakot, Wilaya ya Hazara, na kwa sababu ya utawala wa serikali ya Kiingereza, mafuriko ya Ukristo yalienea kote kote katika India kwa kuacha Panjab. Katika Panjab, kwanza kabisa Wakristo walifungua kituo chao cha mahubiri mjini Ludhiana mnamo mwaka 1835, yaani katika mwaka wa kuzaliwa kwa Seyyidna Ahmad[as]. Ni ajabu ya kudra ya Mungu kwamba dini ya msalaba ilipoanzisha mfumo wa mahubiri yake katika Panjab, ndipo Mwenyezi Mungu akamfanya mvunja msalaba azaliwe katika Wilaya moja ya karibu ili kuponda kichwa cha fitina iliyokuwa inaibuka. Na alipoamrishwa huyo Mvunja msalaba kupokea Baiati, yeye alichagua mji huo huo wa Ludhiana kwa kuchukua Baiati ya kwanza.

[29] Fususul Hikam, cha Hadhrat Muhyiddin ibni Arabi, uk. 36. Tafsiri ya Maulana Al-Fadhil Muhammad Mubarak Ali, chapa ya 1308 Hijria.

UTOTO WA SEYYIDNA AHMAD[AS]

Kuna methali maarufu ya Kiurdu inayomaanisha kwamba mtu mkubwa anatambulika tangu utotoni. Sawa na methali hii, utoto pia wa Seyyidna Ahmad[as] ulikuwa mtakatifu na wenye mng'ao sana. Hakuwa na mazoea ya kushughulikia michezo na mzaha usio na maana pamoja na watoto wengine, wala hakuungana na watoto wengine katika utundu na utukutu.[30] Katika utoto wake, safari moja alichunga mbuzi pia kwa muda fulani sawa na suna ya mitume. Ilitokea hivi kwamba safari moja yeye alikaa kwenye kisima nje ya kijiji na akahitaji kuagiza kitu fulani kutoka nyumbani. Akamwambia yule aliyekuwa anachunga mbuzi huko karibu kuwa amletee kitu hicho toka nyumbani. Yeye akasema, Bwana, nani atalinda mbuzi zangu? Akasema, wewe nenda, mimi nitawalinda. Hivyo, akachunga mbuzi zake, na hivyo Mwenyezi Mungu Alimjalia kutimiza suna ya mitume kwa njia hii.[31]

Mwandishi wa maisha yake na mwanahistoria wa Jumuiya, Hadhrat Sheikh Yakub Ali Irfani[ra], ameeleza tukio moja la ajabu la utoto wake kwamba katika umri wake mdogo alikuwa anamwambia mwenzake (ambaye baadaye aliolewa naye) kwamba niombee kwamba Mungu Anijalie sala.[32]

Haya yalikuwa matokeo ya tabia yake safi na mazoea yake mazuri na mienendo mizuri kwamba mtu yeyote aliyemwangalia kwa jicho la busara akawa anampenda.

Mwalimu mmoja wa Kiahmadiya, Mian Muhammad Husain wa Balochistan, anasimulia:

> "Maulawii Burhanud Din[ra] aliniambia kwamba safari moja Hadhrat Masihi Mau'udi[as] katika utoto wake alimwendea Maulawii Ghulam Rasul wa Qila Mian Singh. Katika kikao hicho baadhi ya mambo yalikuwa yanazungumzwa. Maulawii Ghulam Rasul aliyekuwa Walii na mwenye karama akiendelea

[30] Al Hakam, 14 Juni 1936, uk. 10

[31] Siratul Mahdi, sehemu ya kwanza, uk. 250, chapa ya pili.

[32] Hayatun Nabii, J. 1, Na. 2, uk. 158

kuongea akasema, "Kama katika zama hizi angekuwa nabii, basi huyu kijana ana kipawa cha kuwa nabii". Akasema hayo akipitisha mkono wake juu ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as] kwa mahaba. Maulawii Burhanud Din[ra] anasema, mimi mwenyewe nilikuwepo katika kikao hicho."[33]

MASOMO YA SEYYIDNA AHMAD[AS]

Kabla ya serikali ya Kiingereza, ulikuwepo utawala wa Masingasinga katika Panjab, na serikali ya Masingasinga haikujali elimu. Matajiri wa nchi walikuwa wakiajiri waalimu nyumbani mwao kama wakufunzi. Mwanzoni mwa zama za Waingereza pia utaratibu huo uliendelea. Mpango huo huo ulifanyika kwa mafunzo ya Seyyidna Ahmad[as]. Kwa vile Hudhur ameeleza mwenyewe kuhusu mafunzo yake, kwa hiyo inaonekana vizuri kukariri maneno yake mwenyewe. Anasema:

"Nilipokuwa mwenye umri wa miaka 6 au 7, mwalimu mmoja wa lugha ya Kiajemi aliajiriwa kwa ajili yangu aliyenifundisha Kurani Tukufu na vitabu vichache vya Kiajemi. Mzee huyo aliitwa Fadhl Ilahi. Na umri wangu ulipofikia miaka 10 hivi, mwalimu mmoja wa lugha ya Kiarabu aliwekwa kunifunza, ambaye aliitwa Fadhl Ahmad. Nafikiri, kwa vile masomo yangu yalikuwa mwanzo wa kupanda mbegu ya fadhili ya Mwenyezi Mungu, kwa hiyo neno la kwanza la majina ya waalimu hao lilikuwa Fadhl. Maulawii huyo alikuwa mtu wa dini na mwema. Yeye alinifundisha vizuri na kwa bidii sana. Nikajifunza kwake baadhi ya vitabu vya sarufi na baadhi za kanuni za sintaksi. Baadaye nilipokuwa mwenye umri wa miaka 17 au 18, nilipata kusoma kutoka kwa Maulawii mwingine aitwaye Gul Ali Shah. Huyo naye aliajiriwa na babangu hapa Qadian kunifundisha. Nikajifunza kutoka kwa bwana Maulawii wa mwisho sintaksi, mantiki, utabibu na kadhalika nikajifunza elimu za kawaida za zama zile kadri Mungu Alivyotaka. Baadhi ya vitabu vya utabibu nilisoma kwa babangu, yeye alikuwa tabibu mahiri wa fani ya

[33] Masimulizi ya Masahaba yasiyopata kuchapwa, J. 12, uk. 104, 105

utabibu."[34]

Katika dondoo hiyo, waalimu watatu waliotajwa, miongoni mwao wa kwanza alikuwa Maulawii Fadhl Ilahi, mkazi wa Qadian, na alikuwa mfuasi wa dhehebu la Hanafii. Mwalimu wa pili, yaani Maulawii Fadhl Ahmad, alikuwa mkazi wa Ferozwala, wilaya ya Gujranwala, mfuasi wa dhehebu la Ahlul Hadith. Na mwalimu wa tatu alikuwa Maulawii Gul Ali Shah, mkazi wa Batala, na alikuwa Mshia.[35] Ilmuradi, Mwenyezi Mungu Alipanga waalimu kwa mafunzo yake waliohusika na madhehebu maarufu ya Waislamu. Na ikawa hivyo kwa sababu karibuni katika siku zijazo, yeye alikuwa apewe kazi kubwa ya kuwarekebisha Waislamu wote, na kwa mpango huo akajua kiasi fulani itikadi na matendo ya kila dhehebu kwa sababu ya walimu hao.

AKASHIRIKI KATIKA MICHEZO YA KAWAIDA YA ZAMA ZILE

Zama tunazozungumzia, katika zama hizo kikawaida michezo ya mwereka, Kabaddi,[36] Mugdar na Mogri ilikuwepo. Na watu waovu walizoea michezo ya mashindano ya tombo na mashindano ya kuchi. Lakini Seyyidna Ahmad[as] alikuwa akichukia kitabia michezo ya aina ya pili. Lakini kwa kiasi fulani alikuwa akishiriki katika mazoezi na matembezi. Alijifunza kuogelea utotoni na wakati mwingine alikuwa akiogelea katika mabwawa ya Qadian. Kadhalika alijifunza utotoni ubingwa wa kupanda farasi na alikuwa mahiri katika fani hii. Lakini mazoezi yake zaidi yalikuwa matembezi aliyoyadumisha mpaka mwisho wa umri wake. Alikuwa akienda maili nyingi kupunga hewa na alikuwa anatembea kasi sana.[37]

HARUSI YAKE YA KWANZA

Umri wake ulipokuwa miaka 15 au 16, babake alimwoza kwa Bi.

[34] Kitabul Bariyya, uk. 140-150

[35] Hayatun Nabii, J. 1

[36] Kabaddi ni aina fulani ya mwereka, Mugdar na Mogri ni vitu vizito vya mti vinavyotumika katika mchezo wa kuinua vitu vizito.

[37] Sisila Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Bashir Ahmad[ra], uk. 10

Hurmat Bibi binti wa mjomba wake marehemu Mirza Jam'iyyat Beg. Hii ilikuwa harusi yake ya kwanza, matokeo yake alipata wavulana wawili Hadhrat Mirza Sultan Ahmad na Mirza Fadhl Ahmad waliozaliwa mnamo mwaka 1853 na 1855. Mirza Fadhl Ahmad alifariki tangu muda mrefu bila kupata kizazi, lakini Hadhrat Mirza Sultan Ahmad alikuwa na vyeo mbalimbali katika serikali ya Kiingereza, mpaka akawa Naibu Kamishna, na hatimaye akastaafu alipokuwa Mshauri wa Fedha (waziri wa mapato) katika utawala wa Bahawalpur. Na muda mfupi baada ya kupata pensheni alijiunga na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa mkono wa mdogo wake, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, Khalifatul Masihi II.

Hadhrat Mirza Sultan Ahmad alikuwa si tu ofisa mwenye busara, bali alikuwa mwandishi maarufu na aliandika vitabu vingi. Vitabu vyake karibu 50 vikiishachapwa viko mikononi mwa watu. Jambo hili lafaa kutajwa kwamba mwanaye mkubwa Hadhrat Mirza Aziz Ahmad M.A. alifanya baiati katika utoto wake kwa mkono wa babu yake Hadhrat Masihi Mau'udi[as]. Alipata pensheni alipostaafu akiwa ADM, na sasa katika Makao Makuu anatumikia Jumuiya kama Nadhir A'laa. Mwenyezi Mungu Abariki umri wake. Ameishi maisha yake yote kwa ikhlasi na uaminifu, na katika siku za kufanya kazi ameonyesha mfano mzuri wa uaminifu, utekelezaji wa wajibu na uadilifu.

UPWEKE WAKE

Kinyume cha dasturi ya nchi, hata baada ya kuoa pia haikutokea tofauti yoyote katika upweke wake na kujitenga na wengine. Baniani mmoja wa kabila la Jat, mkazi wa vitongojini mwa Qadian alikuwa akieleza kwamba mimi ni mkubwa miaka 20 kuliko Bwana Mirza. Nilikuwa nikimtembelea sana Bwana Mirza mkubwa[38]. Mbele yangu mara nyingi ilitokea hivi kwamba ofisa mkubwa au kiongozi fulani akaja kuonana na Bwana Mirza mkubwa, na katika mazungumzo akamwuliza, "Bwana Mirza, kijana wako mkubwa (yaani Mirza Ghulam Qadir) tunakutana naye mara kwa mara, lakini hatujamwona kijana wako mdogo. Hapo akajibu, "Naam, yupo kijana wangu wa

[38] Yaani Hadhrat Mirza Ghulam Murtadhaa.

pili, mdogo wa Ghulam Qadir, lakini anakaa kando."… Kisha akamtuma mtu kumwita, naye akaja akiinamisha macho na kukaa kidogo mbali na babaye, na alikuwa amezoea kuweka mkono wake wa kushoto usoni mwake; alikuwa hasemi lolote wala kumwona yeyote. Bwana Mirza mkubwa akasema "Sasa umeishamuona 'Bi arusi' huyu". Bwana Mirza mkubwa alikuwa akisema, kijana wangu huyo ni ***masitarh***[39], hapendi kuajiriwa wala hana mapato, kisha alikuwa akisema kwa kutabasamu, njoo nikufanyie mpango uwe sheikh wa msikiti fulani, hivyo ***man***[40] kumi za nafaka zitakuja nyumbani — Kama mzee angekuwa hai leo angeona kwamba mwanaye yu mfalme, na mamia ya watu wanamjia kutoka sehemu za mbali wakiwa watiifu.[41]

KUTALII SANA

Alikuwa akisoma sana Kurani Tukufu hata kwamba baadhi ya watazamaji wanasimulia kwamba katika zama zile wakati wowote tulipomwona tulimkuta akisoma Kurani Tukufu tu.

Mwanaye mkubwa, Hadhrat Mirza Sultan Ahmad, anasimulia kuwa yeye alikuwa na msahafu mmoja aliokuwa akiusoma na kuuwekea alama. Alisema, bila kutia chumvi naweza kusema kwamba pengine aliisoma Kurani nzima mara elfu kumi.[42] Alikuwa anazama sana akitalii vitabu hata kwamba alikuwa hajali mambo yoyote ya dunia. Mwenyewe alisema kwamba

> "Siku zile nilikuwa na mwelekeo wa kusoma vitabu kana kwamba nilikuwa sipo katika dunia. Babangu alikuwa akinisihi mara kwa mara kwamba inapaswa kupunguza kutalii vitabu, kwani kwa kunihurumia alichelea isije afya yangu ikaharibika."[43]

[39] Hili ni neno la Kipanjabi maana yake ni mtu anayekaa msikitini muda mrefu kwa kusali na kusoma Kurani Tukufu.

[40] ***Man*** ni kipimo sawa na karibu frasila 25.

[41] Tadhkiratul Mahdi, sehemu ya pili, uk. 30

[42] Hayatun Nabii, J. 1, uk. 108

[43] Kitabul Bariyya, chapa ya pili, Maelezo ya pembeni, uk. 150

KUFUATILIA MASHTAKA

Babake Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad aliona kwamba yeye anapenda sana kutalii vitabu vya dini na kutekeleza sala, saumu na amri zingine za Mungu, lakini hana habari kabisa za mambo ya kidunia anayokabili yeye katika maisha akiwa mkulima, kwa hiyo kwa kufikiria kwamba mwanangu huyu asiwe anamtegemea maishani kaka yake, alikuwa akimwamrisha kuyafuatilia mashataka.[44] Yeye kwa kumtii babake alikuwa akiyafuatilia mashtaka, lakini kitabia alikuwa akichukia kazi hii. Mwenyewe ameeleza:

> "Baba yangu kwa kujipatia tena vijiji vya baadhi ya mababu zake alikuwa anafungua mashtaka katika mahakama ya Kiingereza. Yeye akaniingiza mimi pia katika huduma hizo na nikashughulikia shughuli hizo kwa muda mrefu. Nasikitika kwamba muda wangu mwingi wa thamani ulipotea bure katika magomvi hayo yasiyo na maana. Na pamoja na haya baba alinipa jukumu la kusimamia mambo ya kilimo pia. Mimi sikuwa mtu mwenye tabia hii na mwelekeo huu, kwa hiyo mara nyingi baba alinikasirikia. Alikuwa na huruma na mahaba sana kwangu, lakini alitaka kwamba sawa na watu wa dunia anifanye niwe mtu wa kuelekea kwenye mahuluku, lakini tabia yangu ilichukia sana njia hiyo. Safari moja Bwana Kamishna alitaka kuja Qadian, babangu aliniambia mara kwa mara kwamba yanipasa kuenda maili tatu au nne ili kumpokea, lakini nilichukia sana, nami nilikuwa mgonjwa pia, kwa hiyo sikuweza kuenda. Basi, jambo hili pia likawa sababu ya yeye kunikasirikia. Yeye alitaka saa zote nishughulikie mambo ya dunia, jambo ambalo sikuliweza kabisa. Hata hivyo, nadhani kwamba kwa nia safi si kwa ajili ya dunia, bali kwa kupata thawabu ya utii nilijishughulisha kumhudumu babangu na nilikuwa nikimwombea pia. Na yeye alikuwa akinitambua kwa yakini kwamba mie ni mwema kwa wazazi na mara nyingi alikuwa akisema kwamba namwelekeza mwanangu huyu kwenye mambo ya dunia kwa kumhurumia tu, waila najua kwamba

[44] Alhakam, Mei, Juni 1943, uk. 5

upande anaoelekea yeye, yaani upande wa dini, hili ni jambo la kweli na sahihi. Sisi tunapoteza tu umri wetu."[45]

Inajulikana wazi kwa kutalii historia ya dini mbalimbali kwamba waja wote ambao Mwenyezi Mungu Anataka kuwatwisha jukumu la kuwarekebisha watu, Anawapitisha kabla ya zama za kutumwa kwao katika hali ambazo zinawasaidia katika kazi ya kuwarekebisha watu. Kwa mfano, angalieni hali za Seyyidna Ahmad[as]. Katika zama zake mahakama ya Kiingereza yalikuwepo ili kupata uadilifu ambapo kikawaida wahusika wa kesi na mawakili walikuwa wakifuata kesi wakiachana na ukweli na uaminifu na unyofu. Yeye kinyume chake aliweka katika kesi mfano usio na kifani kwa watu wa zama zile kiasi hiki kwamba mtu yeyote hawezi kusema kwamba aliacha ukweli hata kidogo katika kesi fulani. Bali, kama itakavyodhihirika katika kurasa zijazo, alionyesha mifano isiyo na kifani hata kwamba mpinzani mkali pia alilazimika kukiri kwamba ameweka mfano mzuri sana.

Kwa sasa naandika mifano michache tu ya kabla ya zama za kutumwa kwake.

Wa kwanza: Alilazimika kwenda Lahore kufuatilia kesi moja. Huko alikaa nyumbani kwa Seyyid Muhammad Ali Shah aliyekuwa tajiri mmoja wa Qadian, lakini kwa sababu ya kuajiriwa na idara ya msitu, alikuwa anakaa Lahore. Kesi ilikuwa katika mahakama kuu, mtumishi wa Bwana Shah alikuwa akipeleka chakula kwake katika mahakama kuu. Siku moja akarudi na chakula, hapo Bwana Shah akamwuliza, je Bwana Mirza hakula chakula? Mtumishi akajibu, Bwana Mirza amesema, nitakula nikirudi nyumbani. Basi, muda si muda, yeye akafika nyumbani kwa Bwana Shah akiwa mchangamfu sana. Bwana Shah akamwuliza kwani leo unachangamka hivyo! Imehukumiwa vipi? Akasema: Kesi imefutwa, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba shughuli hizi zimekwisha.[46] Bwana Shah aliudhika sana na habari hii, lakini yeye hakuhuzunika. Kama angekuwa mtu yeyote wa dunia angehuzunika sana na kuudhika kwa kushindwa katika kesi

[45] Kitabul Bariyya, uk. 150-152, maelezo ya pembeni.

[46] Hayatun Nabii, J. 1, uk. 57

katika mahakama ya mwisho, lakini yeye akafurahi akishukuru kwamba kesi imekwisha na nafasi imepatikana kwa kumwelekea Mwenyezi Mungu.

Wa pili: Anasema:

> "Nilikwenda Batala kufuatilia kesi moja. Saa ya sala ikafika nami nikaanza kusali. Mtumishi wa mahakama aliniita, lakini nilikuwa nikisali. Mdaiwa alihudhuria na akataka kufaidika kwa kupendelewa na akasisitiza sana jambo hili. Lakini mahakama haikujali, na kesi ilihukumiwa dhidi yao nami nikashinda kesi. Nilipomaliza sala, nikaenda, nikafikiri kwamba pengine hakimu amechukulia kisheria kutohudhuria kwangu, kwa hiyo nikasema kwamba nilikuwa nasali. Hapo yeye akasema nimekwishatoa uamuzi, umeshinda kesi."[47]

Wa tatu: Safari moja alipokuwa mwenye umri wa miaka 25 au 30 hivi, babake alikosana na warithi kutoka kwa babake juu ya kukata miti. Babake alikuwa na maoni kwamba kwa sababu ya kuwa mmiliki wa ardhi miti ni yetu, kwa hiyo aliwashtaki warithi hao na akamtuma Hudhur[as] kufuatilia kesi huko Gurdaspur. Mashahidi wawili pia walikuwa pamoja naye. Baada ya kuvuka mfereji alipofika kijijini Pathnanwala akakaa njiani kupumzika kidogo, na akawaambia wenzake, "Baba anasumbuka bure, miti ni kama shamba tu, hao ni watu wenye hali ndogo, haidhuru wakikata kidogo miti. Kwa vyovyote siwezi kusema mahakamani kwamba miti ni yetu tu pekee; naam, twaweza kuwa na sehemu yetu ndani yake." Warithi pia walimwamini sana. Basi, hakimu alipowauliza warithi uhakika ulivyo, mara wakajibu kwamba mwulize Bwana Mirza mwenyewe. Hakimu alipomwuliza, yeye akasema "Nionavyo, miti ni kama shamba kama ambavyo tuna sehemu katika shamba ndivyo ambavyo tunayo sehemu katika miti pia." Kwa kauli yake hii hakimu aliwapa ushindi warithi. Baada ya yeye kurudi, babake alipojua habari hii alimkasirikia.[48]

---

[47] Hayatun Nabii, J. 1, uk. 56

[48] Usimulizi wa Mian Allah Yar kutoka katika Simulizi za Masahaba, sehemu ya

MIFANO MICHACHE YA UNYENYEKEVU WAKE NA KHULKA ZAKE NJEMA

Mwanaye mkubwa, Hadhrat Mirza Sultan Ahmad, alikuwa akisema, "Marehemu baba hakuishi kama Mughali, bali aliishi kama masikini na darweshi."[49]

Sonara wa Qadian, Kanhayya La'l anasimulia kwamba safari moja Bwana Mirza alitakiwa kwenda Batala. Yeye akaniambia kumfanyia mpango wa gari la farasi. Hudhur alipofika kwenye mfereji alikumbuka kwamba amesahau kitu fulani nyumbani. Akamwacha mwenye gari la farasi kusubiri huko, na mwenyewe alirudi kwa miguu. Mwenye gari alipata abiria wengine huko kwenye daraja na akaondoka nao kwenda Batala. Nafikiri, hapo Bwana Mirza alienda Batala kwa miguu. Mimi nilimwita mwenye gari la farasi na nikamchapa na kusema, ole wako! Kama angekuwa Mirza Nidhamuddin, ungesubiri hata kama ungelazimika kukaa huko siku tatu. Lakini kwa kuwa huyo ni mtu mwema na darweshi kwa hiyo ukaondoka kwa kumwacha nyuma. Bwana Mirza alipopata habari hii, akaniita na kusema, "Angeendeleaje kunisubiri, akapata kazi, akaondoka."[50]

Mtumishi wake Bwana Mirza Ismaili Beg marehemu anashuhudia kwamba kabla ya kutumwa kwake, Seyyidna Ahmad[as] kwa amri ya mzee alipokuwa akienda kumwakilisha katika kesi alikuwa na farasi pamoja naye, nami mara nyingi nilikuwa nafuatana naye. Wakati wa kuondoka, mwenyewe alikuwa akitembea na kunipandisha juu ya farasi. Nilikuwa nikiomba radhi na kusema mara kwa mara naona aibu, lakini yeye alikuwa akisema, "Sioni aibu kutembea, mbona unaona aibu kupanda."

Wakati wa kuondoka Qadian, daima alikuwa akinipandisha kwanza, na baada ya kupita karibu nusu ya umbali, nilikuwa nikishuka na yeye alikuwa akipanda. Kadhalika, wakati wa kurudi kutoka mahakamani,

9, uk. 192, 193

[49] Siratul Mahdi, sehemu 1, chapa ya pili, uk. 219

[50] Al Hakam, toleo la sera ya Masihi Mau'udi, Mei, Juni 1943

yeye alikuwa akinipandisha kwanza na baadaye alikuwa akipanda mwenyewe. Alipokuwa akipanda alikuwa akimwacha farasi aende kwa mwendo aendavyo."[51]

Bwana Mirza Din Muhammad anaeleza, "Mwanzoni sikujuana na Hadhrat Masihi Mau'udi[as], yaani sikuzoea kumtembelea. Seyyidna Ahmad[as] mwenyewe alikuwa akiishi upweke, pasipo kujulikana, lakini kwa kuwa yeye alikuwa msimamizi wa sala na saumu na mwenye kupenda sheria, basi shauku hiyo hiyo ilinipeleka kwake na nilianza kukaa naye. Alipokuwa akienda kufuatilia kesi alikuwa akinipandisha juu ya farasi nyuma yake, na baada ya kufika Batala alikuwa akimfunga ndani ya jumba lake. Jumba hili lilikuwa na ghorofa, alikuwa akiishi humo. Mtunzaji wa nyumba hiyo alikuwa mfuma mmoja aliyekuwa mtu maskini. Baada ya kufika huko alikuwa akiagiza chakula cha paisa mbili kwa ajili yake ambamo vipande vya robo ya chapati moja alikuwa akila na maji. Chapati iliyosalia na dengu na kadhalika iliyokuwa pamoja na chapati alikuwa akimpatia yule mfuma. Alikuwa akinipa *Anna*[52] nne kwa chakula. Alikuwa anakula kidogo sana na alikuwa hana uchu wa chakula chochote maalum.[53]

KAMWONA MTUME MTUKUFU[SAW]

Mnamo mwaka 1864 au 1865, wakati umri wake ulipokuwa miaka 30 au 31, yeye alimwona Mtume Mtukufu[saw] katika kashfi. Kwa vile kashfi hii inafafanua upendo na mapenzi yake kwa Mtume Mtukufu[saw], kwa hiyo inaonekana yafaa iandikwe hapa kwa kuwaonyesha wasomaji daraja ya kiroho ya Hudhur[as]. Yeye anaandika:

> "Mwanzoni mwa ujana wangu, usiku mmoja niliota kwamba nipo katika nyumba yenye shani kubwa iliyo takatifu na safi sana, humo ndani anazungumzwa na anatajwa-tajwa Mtume Mtukufu[saw]. Nikawauliza watu kwamba Mtume Mtukufu[saw] amejikalia wapi? Wakaashiria kwenye chumba kimoja. Basi,

[51] Al Hakam 21-28 Mei 1934

[52] *Anna* moja ni sawa na *paisa* nne.

[53] Hayate Ahmad[as], jalada 2 uk. 196

> pamoja na watu wengine nikaingia ndani. Nilipomwasilia Hudhur s.a.w., yeye alifurahi sana na akanirudishia jibu la salamu yangu kwa njia bora sana. Nakumbuka mpaka sasa uzuri wake na sura yake ya kuvutia na mtazamo wake wa upole na upendo, wala siwezi kusahau. Mapenzi yake yakanivutia ajabu, na wajihi wake mzuri ukanifanya nimpende sana. Wakati huo akaniuliza: Ee Ahmad! Kuna kitu gani katika mkono wako wa kulia? Nilipoona kwenye mkono wangu wa kulia, nikaona kuna kitabu mkononi mwangu, na nikafikiria ni kitabu kilicho utungo wangu. Nikasema, Hudhur, hiki ni kitabu kilicho utungo wangu."[54]

Mtume Mtukufu[saw] akiona kitabu hicho akauliza kwa lugha ya Kiarabu, umekiitaje kitabu hiki? Nikajibu, nimekiita kitabu hiki Qutbi… Ilmuradi, Mtume Mtukufu[saw] alichukua kitabu kile kutoka kwangu. Kitabu kile kilipokuja tu mkononi mwa Mtume Mtukufu[saw] mara kwa kuguswa na mkono mtakatifu wake kitabu kile kikawa tunda zuri lenye rangi ya kupendeza lililoshabihiana na pera lakini ukubwa wake ulikuwa kama tikitimaji. Mtume Mtukufu[saw] alipotaka kulikata vipande vipande kwa kuligawa, ilitoka asali kutoka ndani yake kiasi hiki kwamba mkono wake mtukufu ulijaa asali mpaka kiwiko. Hapo mfu mmoja aliyekuwapo nje ya mlango, kwa muujiza wa Mtume Mtukufu[saw] akihuika akaja na kusimama nyuma yangu, nami nilikuwa nimesimama mbele ya Mtume Mtukufu[saw] kama mdai anavyosimama mbele ya hakimu. Na Mtume Mtukufu[saw] alikuwa amejikalia kiti kwa jaha na taadhima na kwa shani ya hakimu kama mshindani mwereka.

Basi, kwa kifupi ni kwamba Mtume Mtukufu[saw] akanipa kipande kimoja ili nimpe mtu aliyehuika upya, na vipande vilivyosalia vyote akatia ndani ya joho langu. Kipande kile kimoja nilimpa mtu aliyehuika hivi punde, yeye akala. Basi, aliyekuwa amehuika alipokwishakula ndipo[55] nikaona kwamba kiti cha Mtume Mtukufu[saw]

[54] Tafsiri kutoka Aina Kamalate Islam, uk. 548-549

[55] Barahine Ahmadiyya, sehemu 3, uk. 248, 249, maelezo ya pembeni kwenye maelezo ya pembeni Na. 1

kiliinuka sana kiasi hiki kwamba kilikaribia dari na nikaona uso wake mtakatifu ulianza kun'gaa kana kwamba miali ya jua na mwezi inauangukia. Nami nilikuwa ninatazama uso wake mtakatifu kwa shauku na mapenzi huku machozi yakinitiririkia. Kisha nikaamka na nilikuwa bado nalia. Na Mwenyezi Mungu Alinitilia moyoni mwangu kwamba mfu yule ni Islam na sasa Mwenyezi Mungu Ataihuisha kwa baraka za kiroho za Mtume Mtukufu[saw] kwa mkono wangu.

اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَّعَلٰى اٰلِ مُحَمَّدٍ وَّبَارِكْ وَسَلِّمْ اِنَّكَ حَمِيْدٌ مَّجِيْدٌ[56]

USHINDANI BAINA YA BABA NA MWANA

Babake alikuwa na hamu sana kwamba mwanaye asishughulikie muda wote kutalii Kurani Tukufu na vitabu vingine vya dini tu, bali aboreshe pia maisha yake ya dunia kwa kupata cheo kikubwa cha heshima. Kwa hiyo, akamwelekeza mara nyingi kupata kazi, lakini kila mara akaacha kwa kuona mwelekeo wake wa dini na chuki kwa shughuli za kidunia. Safari moja aliwasili katika Wilaya ya Gurdaspur ofisa mmoja Mzungu aliyejuana na babake tangu zamani. Kuona nafasi hii nzuri, baba alimtuma Singasinga mmoja, jina lake Jhanda Singh, mkazi wa Kahlwan, aende kumwita Ghulam Ahmad, kwani ofisa mmoja Mzungu ninayemjua amefika Wilayani, kama kijana akipenda anaweza kupatiwa kazi ya cheo kikubwa. Bwana Jhanda Singh anaeleza kwamba:

> "Nikamwendea Bwana Mirza. Nikamwona amezungukwa pande zote nne na rundo la vitabu, na mwenyewe amejikalia ndani akitalii. Nikamfikishia ujumbe wa Bwana Mirza mkubwa. Bwana Mirza akaja na akajibu, "Nimeshaajiriwa tayari pale nilipotaka." Hapo Bwana Mirza mkubwa alisema, 'Kweli umeishapata kazi?' Kasema, "Naam, nimeisha pata'. Hapo Bwana mkubwa akasema, "Haya, kama umeisha pata kazi, ni heri,"[57]

Baba mwenye busara alitambua vizuri madokezo ya mwanaye

[56] Tafsiri kutoka 'Aina Kamalate Islam', uk. 548-549

[57] Siratul Mahdi, sahemu 1, chapa 1, uk. 48

mwema. Wakati aliposema sihitaji kazi yoyote ya dunia bali nimeshapata kazi kwa Mwenyezi Mungu, mara moja babake akaelewa na akasema kama kweli umepata kazi hii, basi ni heri. Lakini hii ilikuwa jadhba ya muda iliyomnyamazisha mzee wake mheshimiwa, waila akapenda kwa moyo kwamba kwa kudumisha heshima ya familia ni lazima apate kazi yoyote kwa kujipatia heshima ya dunia. Hivyo, alitumwa pia aende baadhi ya sehemu kwa kupata kazi, lakini moyo wake haukutulia popote. Naam, kuhusu kazi ile kubwa aliyopangiwa kupewa na Mwenyezi Mungu katika siku zijazo, akapata tajriba nyingi sana.

KAZI MJINI SIALKOT

Mnamo mwaka 1864 hivi huko Sialkot alilazimika kufanya kazi katika serikali kwa karaha kwa miaka michache. Kwa sababu ya kazi hii alikaa mjini Sialkot kwa miaka minne. Kuhusu tajriba aliyopata huko ameeleza akisema:

> "Nikajua kwa tajriba hii kwamba wafanyakazi wengi wanaishi maisha machafu. Miongoni mwao watakuwa wachache sana wanaoshikamana na sala na saumu kikamilifu na wawezao kujilinda na ladha zisizo halali wanaozikabili kama majaribio. Daima nilishangaa kuona hali zao, na niliwakuta wengi wao kwamba matamanio yao yote yanaishia kwa mali na milki tu, ziwe kwa njia ya halali au njia ya haramu. Na nilikuta juhudi za usiku na mchana za wengi wao ni kwa kupata maendeleo ya kidunia tu katika maisha haya mafupi. Niliwakuta wachache sana miongoni mwa kundi la wafanyakazi walio na sifa za khulka bora, upole, ukarimu, utawa unyenyekevu, huruma kwa viumbe, utakaso wa moyo, kula halali, kusema kweli na uchaji kwa kuzingatia adhama ya Mungu tu. Bali niliwakuta wengi wao kuwa ndugu za shetani katika kiburi, maovu, kutojali dini na khulka mbaya za aina aina. Na kwa vile ilikuwa hekima ya Mwenyezi Mungu kwamba nipate tajriba ya watu wa kila aina, kwa hiyo nililazimika kukaa baina yao."[58]

[58] Kitabul Bariyya, uk. 153, 154 chapa ya pili.

KUAJIRIWA NI GEREZA

Katika muda wa kufanya kazi huko Sialkot, safari moja mamake alimtumia jozi nne za nguo kwa mkono wa kinyozi mmoja, jina lake Hayaat. Kwa ukarimu wake, akampa kinyozi jozi mojawapo katika hizo ilihali hizo zilitayarishwa kwa ajili yake hasa. Kinyozi huyo alimwuliza katika mazungumzo kwamba je unaipenda kazi hii? Akasema: "Ni gereza tu."[59]

TUKIO LA KIMWUJIZA LA HIFADHI YA MUNGU

Baada ya kufika Sialkot, kwanza kabisa alilazimika kukaa katika ghorofa moja katika mtaa wa Jhandanwala. Akielezea tukio la ghorofa hiyo kuanguka na kusalimika kimujiza kwa wenzake wote waliokuwamo ndani kwa sababu yake anasema:

> "Usiku mmoja nilikuwa nikilala ghorofani mwa nyumba moja, na katika chumba hicho watu 15 au 16 pia walikuwa pamoja nami. Wakati wa usiku sauti ya "tik-tik" ilisikika boritini, nikawaamsha watu kwamba boriti hii ni hatari, inapaswa tuondoke hapa. Wakasema, labda ni panya tu; hakuna jambo la hofu na wakalala tena. Baada ya muda kidogo tena sauti kama hiyo ikasikika, ndipo nikawaamsha tena lakini hawakujali. Kisha mara ya tatu sauti ikasikika katika boriti hapo nikawaamsha kwa nguvu na kuwatoa wote nje ya nyumba. Na walipokwishatoka wote, nikatoka mwenyewe. Nilipokuwa kwenye kipago cha pili cha ngazi, mara paa likaporomoka, na likaanguka chini pamoja na paa la pili, na wote wakasalimika."[60]

BAADHI YA HABARI ZA MUDA WA KUKAA SIALKOT

Baada ya kuanguka ghorofa, yeye alikaa katika mtaa wa Kashmiri kwa muda fulani, kisha mpaka mwisho akakaa katika sebule moja pamoja na Hakim Mansab Ali, mwandishi wa hati, iliyotazamana na msikiti wa Ijumaa wa Sialkot. Katika mtaa wa Kashmiri alikuwa anakaa katika nyumba ya Umra Mkashmiri, mdogo wa Mian Fadhl Din.

[59] Hayaatun Nabii, J. 1, Na. 2, uk.170

[60] Siratul Mahdi, sehemu ya 1, uk. 236

Mimi mwandishi nilipata fursa ya kuizuru nyumba hiyo, nafikiri, mwaka 1940. Miongoni mwa jamaa wa Mian Fadhl Dini, mmojawapo aliniambia kwamba inasemwa sana kuhusu Seyyidna Ahmad[as] kwamba yeye alipokuwa akirudi kutoka mahakamani, basi baada ya kuingia mlangoni alikuwa hafungi mlango kwa kugeuka nyuma, ili asipate kumwona ghafula mwanamke yeyote mgeni; bali akiingia tu mlangoni alikuwa akinyosha mikono nyuma yake na kurudisha mlango kwanza kisha akigeuka akaufunga. Nyumbani alikuwa hana shughuli nyingine isipokuwa kusoma Kurani Tukufu na kufanya sijida ndefu ndefu ndani ya sala. Alikuwa akiandika baadhi ya aya na kuziangika ukutani na kisha alikuwa akitafakari juu yao. Wakati mwingine baadhi ya wakulima walikuwa wakija nyumbani na kuonana naye, hapo alikuwa anamwambia Mian Fadhl Din, "Waambie, Mian Fadhl Din, nitafanya kazi yao kule kule mahakamani, hakuna haja ya kuja hapa na kunikumbusha."

Alikuwa na jadhba maradufu ya kuwatumikia watu. Baada ya kufanya kazi mwezi mzima, mshahara aliokuwa akileta, baada ya kujiwekea kiasi kidogo kwa chakula chake, alikuwa akiwatengenezea nguo wajane na maskini au alikuwa akigawa fedha taslimu.[61] Alikuwa na ujuzi mwingi wa utabibu pia. Mgonjwa yeyote aliyekuja kwake akamtibu na kumwombea pia ili Mungu Amponye.

NIA IMARA YA KUITANASARISHA INDIA NA MCHANGO WA SIALKOT NDANI YAKE

Baada ya uasi wa mwaka 1857, Waingereza walihisi barabara kwamba tusipowabatiza wananchi wa nchi hii kwa nguvu ya utawala wetu na kwa propaganda, basi haitakuwa vigumu kutokea tena nchini hali ya uasi. Basi, kwa lengo hili mipango mikubwa mikubwa ikaanza kutayarishwa huko London. Mbunge mmoja wa Bunge la Uingereza Bwana Youngles alisema siku hizo katika hotuba yake:

> "Mwenyezi Mungu Ametuonyesha siku hii kwamba nchi ya India iko chini ya utawala wa Uingereza ili bendera ya ushindi wa Bwana Yesu ipepee toka pembe moja hadi pembe ya pili ya

[61] Siratul Mahdi, sehemu 3 uk. 94

> India. Kila mtu anapaswa kutumia nguvu yake yote kwa kazi adhimu ya kuibatiza India na haipaswi kufanya uzembe katika jambo hili."[62]

Katika mwaka 1862, Waziri Mkuu wa Uingereza, Bwana Lord Pamerston na Waziri wa India Bwana Charles Wood walitembelewa na ujumbe mmoja ambamo walikuwepo wanachama wa Halmashauri ya Bunge la Uingereza na Baraza la Malodi na watu wengine wakubwa. Padre Mkuu wa Uingereza Askofu Mkuu wa Canterbury alitambulisha wajumbe. Waziri wa India akiwahutubia wajumbe alisema:

> "Ni imani yangu kwamba kila Mkristo mpya anayekubali Ukristo katika India anakuwa njia mpya ya umoja kwa Uingereza na ndiyo njia mpya ya kuimarisha Ufalme."[63]

Ni dhahiri kutokana na tadbiri za viongozi mashuhuri wa Kikristo kuwa Wakristo walidhani kwamba wakitia bidii yote kwa kueneza Ukristo, tutafaulu katika shabaha yetu katika muda mfupi na kwa kubatiza sehemu kubwa ya nchi tutaimarisha utawala wetu. Kati ya Misheni za Panjab, misheni ya Sialkot ilikuwa na sifa maalum ya pekee, kwani misheni hii ilianzishwa chini ya mpango maalum wa nchi kwa ajili ya utetezi. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Alipanga kumpa Seyida Ahmad[as] kazi ya kuuvunja msalaba, kwa hiyo yeye akaitilia tabia yake ya asili jazba kuu dhidi ya Ukristo, na Akaandaa sababu zake pia toka mwanzo.

JINSI PADRI TAYLOR[64] M.A. ALIVYOATHIRIKA NA SEYYIDNA AHMAD[AS]

Miongoni mwa mapadri waliojadiliana na Hudhur[as], Padri Taylor M.A. alikuwa anajulikana zaidi. Hotuba na hoja za Seyyidna Ahmad[as]

---

[62] Ulamae Hak Aur Unke Mujahidana Karname, utungo wa Maulana Seyid Mian Sahib, Nadhim Jamiatul Ulamaa Hind, uk. 25, 26

[63] 'The Mission', na R. Clork London 1904, uk. 234, kupitia Banie Silsila Ahmadiyya na Angrez, na Maulana Abdur Rahim Dard M.A. Mbashiri wa zamani wa Waislam Waahmadiyya, London.

[64] Katika matini ya Kiurdu, kwa kosa imeandikwa Butler – Mwenezi.

zilimpenya moyoni mwa Bwana Padri kiasi hiki kwamba mara nyingi mwisho wa saa za kazi, alikuwa akimfikia Seyyidna Ahmad[as] ofisini. Na akiongea naye alikuwa akifika mpaka makazi yake, na kwa furaha akaketi naye katika nyumba yake ndogo alimoishi. Baadhi ya Wakristo wenye mawazo finyu walimzuia kwa sababu jambo hili lavunja heshima yake na ya misheni, lakini Bwana Padri akawajibu kwa upole sana kwamba "Huyu ni mtu mwenye shani kubwa sana asiye na mfano wake, nyinyi hammtambui, nami namfahamu sana."[65]

KUZUIA MAFURIKO YA UKRISTO YAENDELEAYO KUZIDI.

Alizuia mafuriko yaliyoendelea kuongezeka ya Ukristo, kwa hoja imara kwa njia bora na makini katika muda aliokaa huko Sialkot hata kwamba wote waliohusiana naye na wasiohusiana walikubali ustadi wake. Hapa chini twaeleza shuhuda mbili kwa urefu za Shamsul Ulamaa marehemu Maulana Seyyid Mir Hasan wa Sialkot zitakazodhihirisha wazi jinsi alivyotimiza wajibu wake kuishi maisha yaliyotakasika na kujibidiisha kuitetea Islam.

USHAHIDI WA KWANZA WA MAULANA SEYYID MIR HASAN KUHUSU SEYYIDNA AHMAD[AS] KUKAA SIALKOT

Shamsul Ulamaa marehemu Maulana Seyyid Mir Hasan aliyekuwa mwalimu wa mshairi maarufu Dkt. Sir Muhammad Iqbal, anasema:

> "Hadhrat Mheshimiwa Mirza alikuja mjini Sialkot kwa ajili ya kufanya kazi na alikaa huko mnamo mwaka 1864. Yeye alikuwa akipenda kukaa peke yake, alikuwa mtawa na alitengana na mambo yasiyo na maana, kwa hiyo alikuwa hapendi kukutana na watu wa kawaida, jambo ambalo mara nyingi linasababisha kupoteza wakati. Bwana Lala Bhim Sain wakili, aliyekuwa babu mzaa mama wa Bwana Mithan Lal ambaye alikuwa ofisa fulani huko Batala, alikuwa rafiki yake sana. Na kwa vile huko Batala, Bwana Mirza na Bwana Lala walijuana, kwa hiyo hata katika Sialkot walifungamana sana. Basi, humo mjini rafiki yake wa karibu sana alikuwa Bwana Lala tu. Kwa kuwa Bwana Lala

[65] Habari kwa kifupi za Masihi Mau'udi zilizomo katika Barahine Ahmadiyya, sehemu 1, chapa ya nne, uk. 66, na Mian Merajuddin Umar.

alikuwa na tabia njema, mjuzi wa lugha ya Kiajemi na mwenye akili nzuri, kwa sababu hii ya yeye kupenda elimu Bwana Mirza alikuwa anampenda sana.

"Watu wa mahakamani hawakujua utaalamu wa Bwana Mirza. Mwaka huo huo kijana mmoja Mwarabu, jina lake Muhammad Salih, aliwasili mjini na akadhaniwa kuwa jasusi. Mkuu wa Polisi aitwaye Bwana Harcison (ambaye baadaye akawa Kamishna wa Rawalpindi) alimwita Muhammad Salih katika ofisi yake kwa upelelezi. Basi, akahitajika mkalimani. Kwa kuwa Bwana Mirza alijua sana Kiarabu na aliweza kuandika na kusema vizuri kwa lugha ya Kiarabu, kwa hiyo yule ofisa akamwita Bwana Mirza na kumwambia amwulize Mwarabu nitakayomwuliza na kuandikisha majibu yake kwa Kiurdu. Bwana Mirza aliifanya kazi hii ipasavyo, na hivyo umahiri wake ukajulikana kwa watu."

"Katika zama hizo, kwa juhudi za Maulawii Ilahi Bakhsh aliyekuwa Mkuu wa Shule (cheo hiki siku hizi kinaitwa Insepekta wa shule za Wilaya), shule moja ilianzishwa kwa makarani wa mahakama kwa kuwafundisha saa za usiku lugha ya Kiingereza. Dkt. Amir Shah aliye siku hizi mpasuaji msaidizi mstaafu, aliwekwa kuwa mwalimu. Bwana Mirza pia alianza kujifunza Kiingereza na kapata kusoma vitabu viwili vya Kiingereza."[66]

"Siku hizo, Bwana Mirza alikuwa na shauku kubwa sana ya kufanya majadiliano ya kidini. Hivyo, mara nyingi alijadiliana na mapadri. Safari moja mjadala ulifanyika na padri Elisha aliyekuwa mwenyeji, aliyekaa katika jumba moja miongoni mwa majumba yale yaliyo upande wa kusini mwa Hajipura. Bwana padri alisema kwamba bila kukubali dini ya Kikristo uokovu hauwezekani. Bwana Mirza akasema: Kifafanuzi cha uokovu ni nini? Unamaanisha nini kwa uokovu? Eleza kwa urefu. Bwana padri hakufafanua na akamaliza mjadala na akasema, "Sikusoma

[66] Katika zama hizo kitabu cha kwanza kilikuwa kutambulisha alfabeti na katika kitabu cha pili kulikuwa na mazoezi ya kuunganisha herufi na kuunda maneno madogo madogo. (Siratul Mahdi, sehemu 1, chapa ya pili, uk.159.)

mantaki ya namna hii."

"Mjadala ulifanyika mara nyingi baina ya Bwana Mirza na Padri Taylor M.A. aliyekuwa mtaalamu na mtafiti. Bwana huyo alikuwa mkazi wa Gohadpur. Safari moja Bwana Padri alisema kwamba siri ya kumwumba Bwana Yesu bila baba ilikuwa hii kwamba alizaliwa kutoka tumboni mwa bikira Mariamu na aliepukana na kushirikishwa na Adamu aliyekuwa mwenye dhambi. Hapo Bwana Mirza alisema kwamba hata Mariamu pia alitokana na kizazi cha Adamu, basi alisalimikaje na kushirikishwa na Adamu? Isitoshe, mwanamke ndiye aliyemshawishi Adamu, basi akala tunda la mti uliokatazwa na akawa mwenye dhambi. Basi ilipasa kwamba Bwana Yesu angeepukana na kushirikishwa na mwanamke pia. Hapo Bwana Padri akanyamaa kimya.

"Padri Taylor alikuwa akimheshimu sana Bwana Mirza na alikuwa akiongea naye kwa adabu sana. Bwana Padri alimpenda sana Bwana Mirza. Bwana Padri alipokaribia kurudi Ulaya, akaja mahakamani kumlaki Bwana Mirza. Naibu wa Kamishna alimwuliza Bwana Padri sababu ya kufika, akajibu kwamba nimekuja kumlaki Bwana Mirza. Kwa kuwa naenda kwetu, kwa hiyo nimekuja kumwaga. Basi akamwendea Bwana Mirza pale alipokaa yeye na akakaa chini na baada ya kumlaki akaenda.

"Kwa vile Bwana Mirza alikuwa akipenda sana kujadiliana na mapadri, kwa hiyo Bwana Murad Beg wa Jalandhar ambaye lakabu yake ya kishairi ilikuwa Mirza Shikasta na baadaye akatumia lakabu Muwahhid, alimwambia Bwana Mirza kwamba yeye aandikiane na Seyyid Ahmad Khan, kwani yeye ameandika maelezo ya Torati na Injili, utapata msaada mwingi kuhusu jambo hili. Hivyo, Bwana Mirza alimwandikia Sir Seyyid barua kwa Kiarabu."

"Alikuwa anampenda sana marehemu Sheikh Ilah Dad miongoni mwa makarani wa mahakama, aliyekuwa mlinzi wa ofisi, na mapenzi yalikuwa imara na ya kweli. Miongoni mwa wazee wa mjini, yeye alimpenda sana Maulawii Mahbub Aalam

aliyependa kukaa peke yake na alikuwa mtu wa ibada sana, mwema na sufii wa Ki-nakshbandi.

"Sebule walimokaa Bwana Mirza na Hakim Mansab Ali aliyekuwa siku hizo mwandishi wa hati, ilikuwa pale madukani, na karibu sana na duka la marehemu Hakim Husamuddin[67] ambamo yeye alikuwa anatayarisha dawa na kuuza, na hiyo ilikuwa kliniki yake pia. Kwa sababu hii, Bwana Hakim na Bwana Mirza walipata kujuana. Bwana Hakim alijifunza kutoka Bwana Mirza ***Kanuncha***[68] na sehemu fulani ya ***Mujiz*** pia.

"Kwa vile Bwana Mirza hakupenda kazi ya kuajiriwa, kwa hiyo alianza kujitayarisha kwa mtihani wa uwakili na akaanza kusoma vitabu vya sheria lakini hakushinda katika mtihani[69]; na angeshindaje kwani hakuumbwa kwa kufanya shughuli za kidunia. Ni kweli, 'kila mtu ameumbwa kwa kazi maalum'.

"Siku hizo Chuo cha Panjab kilianzishwa, humo mwalimu wa Kiarabu alihitajika kwa mshahara wa Rupia 100. Nilimwambia, upeleke ombi la kupatiwa nafasi hii maana ujuzi wako wa lugha ya Kiarabu ni kamili sana, kwa hiyo lazima utapewa kazi hii. Akajibu, sipendi kazi ya ualimu, kwani watu wengi baada ya kusoma wanafanya kazi za ukorofi sana na wanaitumia elimu kuwa njia ya kufanya kazi zisizojuzu. Naogopa sana onyo la aya hii:

اُحْشُرُوا الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا وَ اَزْوَاجَهُمْ [70]

Jibu hili linaonyesha kwamba alikuwa mtu mwema sana.

"Safari moja mtu mmoja alimwuliza kwamba kwa nini manabii

---

[67] Bwana Hakim alikuwa baba mzazi wa Hadhrat Mir Haamid Shah wa Sialkot.

[68] Kanuncha na Mujiz ni vitabu vya elimu ya utabibu. ─ Mwenezi

[69] Sababu moja ya kidhahiri ya kutofaulu katika mtihani ilikuwa ni hii pia kwamba watu 22 walishiriki katika mtihani, mmoja wao alikuwa Narain Singh aliyekamatwa kufanya ukorofi mtihani, basi kwa sababu hiyo wanafunzi wote walifelishwa.

(Siratul Mahdi, sehemu 3, uk. 179, usimulizi wa Pandat Devi Ram.)

[70] Wakusanyeni wale waliodhulumu na wenzao. Assaaffaat 37:23

hawatokwi na shahawa usingizini? Akasema, kwa vile muda wote, wakilala au wakiamka, manabii huwa na fikara takatifu na hawaziruhusu fikara chafu kuingia moyoni, kwa hiyo hata katika ndoto hawapati kutokwa na shahawa.

"Safari moja, ilipokuwa inazungumzwa kuhusu mavazi, mtu mmoja akasema kwamba pajama lenye nafasi pana za kupenyezea miguu huwa bora. Hapo Bwana Mirza alisema kwamba pajama lenye nafasi ndogo ya kupenyezea mguu ni bora na afadhali kwa kujisitiri, na inasitiri vizuri zaidi, kwani kwa kuwa nafasi hiyo ndogo inasitiri hata kwa ardhi pia. Wote wakapenda jibu hili.

"Hatimaye, akivunjika moyo alijiuzulu kazini na akaondoka hapa mwaka 1868. Safari moja akaja hapa mwaka 1877 na alikaa nyumbani mwa Lala Bhiim Sain, na akaja nyumbani kwa Hakiim Mir Husamuddin alipoalikwa.

"Mwaka huo huo, Sir Seyyid Ahmad Khan, Mungu Amsamahe, alianza kuandika maelezo ya Kurani Tukufu. Nilikuwa nimeisha pokea maelezo ya mafungu matatu. Mimi na Sheikh Allah Dad tulipokwenda kumwona Bwana Mirza nyumbani kwa Lala Bhiim Sain, katika mazungumzo Sir Seyyid alitajwa na maelezo yake pia. Mimi mwandishi nilisema kwamba maelezo ya mafungu matatu yameniwasilia ambamo dua na kushuka wahyi vimezungumziwa. Akasema, kesho utakapokuja, uje na maelezo hayo. Keshoye tulipoenda, yeye alisikiliza sehemu zote mbili, lakini hakufurahi wala hakuyapenda maelezo. Mwandishi Mir Hasan"[71]

USHAHIDI WA PILI WA MAULANA SEYYID MIR HASAN KUHUSU SEYYIDNA AHMAD[AS]

"Hadhrat Mirza alikaa nyumbani mwa Umra Mkashmiri akiwa mpangaji karibu sana na nyumba yangu katika mtaa wa Kashmirian. Baada ya kurudi kutoka mahakamani, yeye alikuwa anashughulikia kusoma Kurani Tukufu. Akasoma Kurani

[71] Siratul Mahdi, sehemu 1, uk. 54 chapa ya kwanza.

akikaa, akisimama na akitembea na akalia sana. Akasoma Kurani kwa unyenyekevu na uchungu usio na kifani. Jinsi ambavyo wenye haja sawa na mazoea ya zama wanawaendea maofisa, hivyo ndivyo walivyokuwa wakimfikia yeye pia. Kaka wa Umra aliyeitwa Fadhl Din alikuwa mwenye kuheshimiwa katika mtaa ule, Bwana Mirza alikuwa akimwita na kumwambia, Mian Fadhl Din! Wafahamishe watu hao wasije hapa, wasipoteze wakati wao na wangu, siwezi kufanya chochote, mimi si hakimu. Kazi yote inayohusikana nami namaliza kule kule mahakamani. Bwana Fadhl Din alikuwa akiwafahamisha watu hao na kuwaondoa. Maulawii Abdul Karim[ra] pia alizaliwa katika mtaa huo na kukulia na akawa kijana, na hatimaye akawa miongoni mwa waliomkurubia Bwana Mirza.

"Baadaye yeye alikaa katika sebule moja iliyotazamana na msikiti wa Ijumaa pamoja na Mansab Ali Hakiim aliyekuwa na cheo cha heshima cha kuwa mwandishi wa hati. Karibu na sebule alikuwa mzee moja mwenye duka, jina lake Fadhl Din, aliyekuwa analala usiku dukani tu. Marafiki zake wengi walikuwa wakija kwake baada ya jioni, wote walikuwa watu wema. Wakati mwingine Bwana Mirza pia alikuwa akija huko, na mara moja moja Bwana Nasrullah Mkristo pia akaja aliyekuwa mwalimu mkuu wa shule ya Misheni. Mara nyingi Bwana Mirza na mwalimu mkuu walikuwa wakijadiliana juu ya mambo ya dini. Watu walikuwa wakifaidika na hotuba ya Bwana Mirza.

"Kulikuwa na mzee mmoja mtawa sana, mwema, asiyependa anasa za dunia, jina lake Maulawii Mahbub Aalam, ambaye Bwana Mirza alikuwa akimtembelea na alikuwa akimsisitizia Lala Bhiim Sain pia kuwa awe anamtembelea Bwana Maulawii huyo. Kwa hiyo, yeye pia wakati mwingine alikuwa akimtembelea. Kila ilipotajwa baiati na uongozi na ufuasi. Bwana Mirza alikuwa akisema kwamba inampasa mtu afanye mwenyewe bidii. Kwani Mwenyezi Mungu Anasema:

وَالَّذِيْنَ جَاهَدُوْا فِيْنَا لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا[72]

Hapo Maulawii Mahbub Aalam alikuwa akikasirika na kusema kwamba bila baiati njia haipatikani.

"Ni dhahiri shahiri kuwa Bwana Mirza aliwatangulia wote katika elimu ya dini, lakini katika mbio za kidhahiri pia ushindi wake ulithibitika kwa uwazi juu ya watu wa wakati ule.

"Maelezo yake ni hivi kwamba safari moja baada ya kumalizika saa za kazi za mahakama, wafanyakazi wakaanza kurudi nyumbani, hivi tu ilitajwa kukimbia kwa kasi na shindano la mbio. Kila mmoja alidai anaweza kukimbia sana. Hatimaye, Singasinga mmoja, aitwaye Billa Singh, alisema kwamba ninawashinda wote katika mbio. Hapo Bwana Mirza alimwambia, "Shindana nami katika mbio, basi itathibitika nani anakimbia sana." Hatimaye, Sheikh Allah Dad aliwekwa kuwa mwamuzi, na ilipangwa kwamba wakimbie bila viatu kuanzia hapa mpaka daraja lile linalotenganisha barabara ya mahakama na mji. Mtu mmoja alishika viatu vyao na mtu mmoja alitumwa mapema aende pale darajani ili atoe ushahidi nani ameshinda na ametangulia kufika kwenye daraja. Bwana Mirza na Billa Singh walianza kupiga mbio wakati mmoja. Watu wengine walitembea nyuma yao kwa mwendo wa kawaida. Walipofika kwenye daraja ikathibitika kwamba Bwana Mirza alishinda na Billa Singh alishindwa."[73]

Mimi nasema kwamba Hadhrat Maulawii Ismaili Shahid[rh] pia alikabili jambo la namna hii la ghera ya dini kuhusu shindano la kuogelea na Singasinga mmoja. Yeye alimshinda katika kuogelea.

USHAHIDI WA BWANA MUNSHI SIRAJUDDIN

Maulawii Zafar Ali Khan, mhariri wa gazeti la Zamindar, alikuwa ni kiongozi maarufu Mwislamu ambaye babake mzazi Bwana Munshi

[72] Na wale wanaojitahidi kwa ajili yetu, kwa yakini Tunawaongoza kwenye njia zetu. Sura Al-'Ankabut, 29:70.

[73] Siratul Mahdi, sehemu 1, chapa ya pili, uk. 270-272.

Sirajuddin marehemu alitoa ushahidi kwamba:

> "Bwana Mirza Ghulam Ahmad katika mwaka 1860 au 1861[74] alikuwa karani katika Wilaya ya Sialkot… na sisi twaweza kutoa ushahidi wa kuona kwa macho kwamba katika ujana wake pia yeye alikuwa mtu mwema sana na mchamungu. Baada ya shughuli ya kazini, wakati wake wote ulikuwa unatumika katika kutalii vitabu vya dini tu. Alikuwa akikutana na watu kidogo sana."[75]

AMRI YA BABA KUACHA KAZI NA KURUDI QADIAN

Seyyidna Ahmad[as] akieleza sababu ya kuacha kazi mjini Sialkot anaandika:

> "Kwa vile ilikuwa vigumu sana kwa baba yangu kukaa mbali nami, kwa hiyo kwa amri yake iliyokuwa sawa kabisa na matakwa yangu nilijiuzulu katika kazi iliyokuwa kinyume cha tabia yangu na nikafika kwa baba yangu… Sawa na beti hizi za *Mathnawii* ya Maulana Rum zifuatazo niliishi siku zile zote kwa karaha na uchungu sana:
>
> Sikuridhika na kila jamii; nikachanganyikana na wenye hali njema na wenye hali mbaya.
>
> Kila mmoja wao, katika dhana yake, akawa rafiki yangu, lakini hakuna aliyegundua siri zangu za ndani mwangu.

KIFO CHA MAMA YAKE MZAZI, MWAKA 1868

Baba yake alipomwamuru kurudi baada ya kujiuzulu kazini, wakati huo mama yake alikuwa mgonjwa sana huko Qadian. Inaonekana kwamba pengine hata mama yake pia aliyempenda sana mwanaye alimwomba baba yake katika hali ya kuugua kuwa amwite mwanaye kurejea. Hata baba pia pengine alikuwa mwenye majonzi kukaa mbali na mwanaye mcha Mungu kwa muda mrefu wa miaka minne. Basi, alipofika Amritsar na kuchukua gari la farasi, mtu mwingine pia

[74] Kuhusu mwaka na umri, Bwana Munshi hakukumbuka vizuri. Kwa hakika habari hii inahusikana na muda tangu mwaka 1864 hadi 1868.

[75] Gazeti la Zamindar, Mei 1908.

akawasili Amritsar kutoka Qadian ili kumpokea. Mtu huyo alimwambia mwenye gari la farasi kuendesha haraka, kwani hali ya mama yake haikuwa nzuri. Baada ya muda mfupi tena alisema, "Alikuwa mgonjwa taabani, harakisha isije akafa." Kwa kusikia haya, yeye akawa na yakini kwamba mama yake ameshafariki. Alipofika Qadian akajua kwamba dhana yake ilikuwa sahihi, kweli mama yake alikuwa amekwishafariki. *Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiuun.*

Ingawa kifo cha mama yake kilikuwa chenye uchungu sana mno kwake, lakini akavumilia huzuni hii kubwa kwa subira ya hali ya juu. Imeishaelezwa nyuma kwamba kwa sababu ya kutoshughulikia mambo ya dunia na kushughulikia kutalii vitabu vya dini, baba yake alikuwa akimwita 'Mulla', lakini kinyume chake mama yake alikuwa akimpenda sana sana kwa sababu ya wema na uchamungu wake na kuishi maisha mema. Na alikuwa akimtimizia mahitaji yake ya kila aina. Mapenzi ya Seyyidna Ahmad[as] kwa mama yake yanaweza kujulikana kwa jambo hili kwamba baada ya kifo chake wakati wowote alipomtaja mama, machozi yakamtiririkia machoni mwake. Mwandishi wa sera yake, Hadhrat Sheikh Yakub Ali Irfani[ra], ametoa ushahidi wa kuona kwa macho kwamba safari moja Seyyidna Ahmad[as] alikwenda kwa kupunga hewa na akiacha njia akaelekea upande wa mava ya zamani ya familia yake. Akaja kwa kaburi la mama yake na akaomba dua ndefu pamoja na wenzake, machozi yakijaa machoni mwake.[76]

Tarehe maalum ya kifo cha mamake, Hadhrat Charagh Bibi, haijajulikana hadi sasa, lakini ni jambo la yakini kwamba alifariki mwaka 1868. Kaburi lake lipo katika mava ya zamani ya familia yake yaliyo upande wa Magharibi wa Qadian karibu na uwanja wa kusalia idi.

MWELEKEO WA HADHRAT MIRZA GHULAM MURATADHAA KWENYE MAMBO YA AKHERA

Hadhrat Mirza Ghulam Muratadhaa alipoanza kesi kwa kupata ardhi na majengo ya mababu zake, alikuwa na yakini kamili kupata ushindi,

[76] Hayate Ahmad, J. 1, Na. 2, uk. 143

lakini baada ya kuhangaikia kushughulikia kesi kwa muda mrefu hakupata kushinda na akaona hata milki iliyopo na raslimali pia zinapotea, basi akawa anahuzunika sana. Tena juu yake kulikuwa na huzuni ya kifo cha mkewe.

Seyyidna Ahmad[as] akitaja habari hizo anasema:

> "Niliporejea kwa baba, nikaanza kushughulikia tena kama kawaida mambo ya kilimo, lakini nafasi nyingi ilikuwa ikitumika kusoma na kutafakari Kurani Tukufu, maelezo yake, na Hadithi, na baadhi ya wakati nikamsomea vitabu hivyo baba yangu pia. Na baba alikuwa akihuzunika na kusikitika sana kwa sababu ya kutofaulu kwake. Alitumia karibu Rupia elfu sabini katika kesi zake, matokeo yake akashindwa, kwani tangu muda mrefu vijiji vya mababu zetu vilikuwa vimetoka mkononi mwetu na kuvipata tena kulikuwa ni jambo lisilowezekana. Kwa sababu ya kutofanikiwa huku, baba aliishi maisha ya ghamu nzito na huzuni na mahangaiko, nami nilikuwa napata nafasi ya kujipatia mabadiliko mema kwa kuona mawazo ya aina hii. Kwani hali ya maisha machungu ya baba ilinifundisha somo la kuishi maisha safi yaliyoepukana na machafu ya kidunia. Ingawa vijiji vichache vilikuwa bado mkononi mwa baba na pia alikuwa akipata kila mwaka zawadi kiasi fulani kutoka serikali, na ilikuwa pensheni pia ya kazi aliyofanya zamani, lakini kulinganisha na alichokuwa ameishaona, hayo yote yalikuwa si chochote. Kwa sababu hiyo, daima alikuwa na huzuni, na mara kwa mara alikuwa akisema kwamba kadiri nilivyofanya juhudi kwa ajili ya dunia hii najisi kama ningefanya kwa ajili ya dini ningekuwa leo Qutub[77] au Ghauth[78] wa zama. Na mara nyingi alikuwa akisoma ubeti huu wa Kiajemi:
>
> > Umri umekwisha na siku chache tu zimebaki, ni afadhali nipitishe siku hizi katika kumbukumbu la Dhati Fulani.
>
> Na nilimwona mara kadha akisoma kwa majonzi ubeti wake

[77] '*Qutub*' ni daraja ya juu kabisa ya sufii.

[78] '*Ghauth*' pia ni daraja ya juu ya walii.

mwenyewe wa Kiajemi ambao ndio ufuatao:

> Ewe Msaidizi wa kila asiye na msaidizi, sitazamii nitaondoka kizingitini pako nikikata tamaa.

Na baadhi ya wakati alikuwa akisoma ubeti huu wake mwenyewe wa Kiajemi:

> Kwa machozi ya machoni mwa wapenzi na kwa vumbi la miguuni pa mja fulani, moyo wangu una kiherehere.

KAKATAA KUWA OFISA WA IDARA YA ELIMU KATIKA UTAWALA WA KAPURTHALA

Baada ya kurudi kutoka Sialkot aliambiwa na utawala wa Kapurthala kukubali kuwa ofisa wa Idara ya Elimu. Akakataa na kumwambia baba yake:

> "Sipendi kuajiriwa popote. Tafadhali, uwe unashonesha kwa ajili yangu jozi mbili za nguo, na kuniletea chakula chochote kiwacho."

Baba yake ambaye sasa mabadiliko makubwa yalikuwa yameishatokea katika maisha yake, aliposikia jibu la mwanaye, alimwambia mtu fulani, jina lake Mian Ghulam Nabii, kwa moyo uliolainika, "Mian Ghulam Nabii! furaha yangu imo humo tu, njia ya kweli ni hiyo tu anayofuata huyu."[79]

KAMWOMBA BABA ARUHUSIWE KUKAA MBALI KABISA NA SHUGHULI ZA KIDUNIA

Akiona mabadiliko katika moyo wa baba na kuelekea kwenye dini, alihisi kwamba kama nikimwomba sasa kutengana na shughuli zote za kidunia, inawezekana atakubali. Basi, akamwandikia baba yake barua ifuatayo kwa lugha ya Kiajemi:

> "Mheshimiwa baba! Assalamu alaikum, baada ya adabu zote na utii, ningependa kukuelezea kwamba inashuhudiwa siku hizi na inaonekana kila siku kwamba katika nchi zote na sehemu zote za ardhi maradhi ya kuambukiza yanazuka kila mwaka

[79] Hayatun Nabii, J. 1, Na. 2, uk. 185

yanayowatenganisha marafiki na jamaa na kuleta utengano wa kudumu baina yao. Na hakuna mwaka unaopita bila kudhihiri moto mkubwa na ajali yenye kuhuzunisha au maangamio yasiyoleta makelele makubwa. Kwa kuona hali hizo, moyo wangu hauna raghaba kwa dunia na uso umesawijika. Na mara nyingi napata kusoma mistari hii miwili ya ubeti wa Hadhrat Sheikh Shirazi[rh] na machozi yanatiririka machoni kwa huzuni kubwa: 'Usiutegemee umri huu usio wa kudumu, wala usighafilike na mchezo wa zama'. Vile vile mistari hii miwili pia kutoka katika Diwani ya Farrukh Qadiani[80] inanisumbua sana: 'Usiipende dunia iliyo duni, kwani wakati wa kifo wawadia kwa ghafla'.

"Kwa hiyo, nataka nipitishe maisha yaliyobaki peke yangu na nijitenge na watu na vikao vyao na nijishughulishe katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu ili kulipia yaliyoponyoka:

"Sehemu kubwa ya umri imekwishapita na sasa siku chache zimebakia. Afadhali mausiku machache yaliyobakia niyageuze kuwa asubuhi kwa kumkumbuka Mungu.

"Kwani dunia haina msingi imara, wala maisha hayaaminiwi, na maisha yaliyoazimwa hayategemewi. Mtu anayejichunguza hahusiki na balaa ya mwingine. Wassalam."

Bado haijajulikana kwamba babake aliijibuje barua hii, lakini inakisiwa kwamba bila shaka alithamini jazba zile zidhihirikazo katika barua hii.

UFUNUO WA KWANZA SAWA NA UTAFITI WA HIVI SASA NA BISHARA YA MUSTAKABALI WENYE SHANI

Mnamo mwaka 1868 au 1869, dhehebu la Ahle Hadhith lilipingwa sana katika Panjab. Kama imamu wa msikiti wowote akijua kwamba Ahle Hadithi fulani (kwa kauli yao, Wahabi yeyote) amesali humo ndani, basi baadhi ya wakati yeye alikuwa akivunja sakafu ile au kuiosha kwa maji. Siku hizo Sheikh Muhammad Husain wa Batala

[80] Siku zile Seyyidna Ahmad[as] alikuwa anatumia '*Farrukh'* kama jina lake la kishairi. Mshororo huu ni wake mwenyewe.

alirudi Batala baada ya kuhitimu mafunzo ya dini kutoka kwa Sheikh Seyid Nazir Husain wa Delhi. Waislamu wa kawaida walikuwa wakali sana kumpinga yeye. Seyyidna Ahmad[as] alipofika Batala kwa shughuli fulani, mtu mmoja kwa kung'ang'ania alimchukua mpaka nyumbani kwa Sheikh Muhammad Husain ili kujadili naye. Huko alikuwepo baba yake pia na watu wengi walikuwa na hamu sana ya kusikiliza mjadala. Seyyidna Ahmad[as] akakaa mbele ya Bwana Sheikh na kumwuliza kuhusu madai yake. Bwana Sheikh akasema kwamba imani yangu ni kwamba Kurani Tukufu inatangulizwa juu ya yote, baada yake ni daraja ya kauli za Mtume[saw]. Na kwangu mimi mbele ya Kitabu cha Mungu na Hadithi za Mtume[saw], kauli ya mtu yeyote haina uzito wowote. Akisikia hii, mara Hudhur[as] akasema kwamba imani yako hii inaingia akilini na haipingiki, kwa hiyo sioni haja ya kujadiliana nawe. Hudhur[as] aliposema tu haya, watu walianza kupiga makelele kwamba ameshindwa, ameshindwa. Hata mtu aliyempeleka kule, pia akashikwa na hasira na kasema kwamba umetudhalilisha. Lakini yeye alisimama imara kwa heshima na hakujali kabisa makelele ya watu. Kwa vile aliachana na mjadala kwa ajili ya Mungu, kwa hiyo usiku ule Mwenyezi Mungu akimridhia alimfunulia kwamba "Mungu Amekuridhia kwa kitendo chako hicho, naye Atakubariki sana hata kwamba wafalme watatafuta baraka kutoka katika nguo zako."[81]

Kisha akaonyeshwa pia hao wafalme katika hali ya kashfi wasiopungua sita au saba nao walikuwa wamepanda juu ya mafarasi. Hudhur[as] katika kitabu chake cha lugha ya Kiarabu akitaja kashfi hii anasema:

> "Niliona jumuiya ya waaminio wenye ikhlasi na wafalme waadilifu katika ruya yenye habari njema, ambao miongoni mwao baadhi yao walikuwa wa nchi hii hii (India) na wengine walikuwa wa nchi ya Kiarabu na wengine wa nchi ya Kiajemi na wengine wa Shamu na wengine wa Rumi na wengine wa nchi zingine ambazo sizijui. Baada yake niliambiwa na Mwenyezi Mungu kwamba watu hao watakusadikisha na watakuamini na watakusalia na watakuombea, nami Nitakubariki sana mpaka

[81] Barahine Ahmadiyya, sehemu ya 4, uk. 520, 521. Tanbihi ya tanbihi ya 3.

wafalme watatafuta baraka kutoka katika nguo zako."[82]

Sitaki kueleza maoni yangu kuhusu ufunuo huu. Naona ni lazima niseme kwamba huu ni ufunuo wa zama zile ambapo yeye alikuwa hajulikani kabisa baina ya watu, na hakuna aliyejua mustakabali wake utakuwa wenye shani kiasi gani.

WINGI WA RUYA NA KASHFI, NA ISHARA KWA MABANIANI WA QADIAN

Sasa kwa kuwa zama za kutumwa kwa Hudhur zilikuwa zinakaribia na Mwumba wa mbingu na ardhi alitaka kumtuma kwa kuongoza viumbe waliopotea, kwa hiyo yeye alianza kupata ruya na kashfi kwa wingi, na baadhi ya wakati alibarikiwa kwa kufunuliwa pia. Mabaniani wawili wa Qadian, Lala Sharampat na Lala Malavamal, walikuwa wakimtembelea sana, kuwahusu hao pia ishara kadha zilimdhihirikia.

Katika mwaka 1870, jamaa wa Lala Sharampat aitwaye Lala Bashimbar Das na Baniani mwingine, Khush-hal Chand, walifungwa kutokana na kesi fulani. Hao walikuwa wamekata rufaa. Lala Sharampat alimwomba Hudhur kujua matokeo ya kesi hiyo. Kwa vile Hudhur akapata nafasi nzuri ya kumthibitishia ukweli na ubora wa Islam huyo Baniani, kwa hiyo akamwomba Mungu. Usiku aliambiwa katika kashfi kwamba faili ya kesi hii kutoka mahakama ya juu itarudishwa kwenye mahakama ya chini ambapo muda wa kifungo cha ndugu yake itapunguzwa kuwa nusu, lakini mwenzake atapata adhabu kamili. Habari hii iliyotoka kwa Mungu walipoambiwa Mabaniani wa Qadian, hapo kwa bahati tu, kwa sababu ya kuelewa visivyo ikavuma baada ya siku chache kuwa hao wameshinda katika rufaa na Lala Bashimber Das ameachiliwa. Kwa kusikia hii habari Hudhur[as] alihuzunika sana na Mabaniani wa Qadian waliwasha taa za samli na wakaeneza kwamba utabiri wa Hudhur umebatilika, bali habari hii ilienea sokoni kwamba washitakiwa wameshafika kijijini baada ya kuachiliwa. Wakati habari hii ilipofika, wakati wa sala ya Isha ulikurubia. Hudhur[as] alisema:

"Kwa huzuni hii nikapatwa na hali ambayo Mungu Anaijua.

[82] Lujjatun Nur, uk. 3, 4

> Kwa huzuni hiyo sikuweza kuhisi kwamba mimi niko hai au nimekufa. Basi katika hali hiyo sala ikaanza. Niliposujudu nilifunuliwa:
>
> لَا تَحْزَنْ إِنَّكَ أَنْتَ الْأَعْلَى
>
> Yaani usihuzunike, wewe ndiwe utakayeshinda. Basi nikamjulisha Sharampat na ilijulikana kwamba rufaa ilikubaliwa tu kusikilizwa siyo kwamba Bashimbar Das aliachiliwa."[83]

Baadaye ilitokea vile vile kabisa jinsi ilivyoelezwa katika habari safi ya ghaibu, na Mabaniani wakashangaa na kushikwa na butaa.

Ningependa kueleza hapa ishara moja kuhusu Lala Malava Mal pia ingawaje ilitokea mwaka 1881. Lala Malava Mal toka muda fulani alisumbuliwa na maradhi ya kifua kikuu. Maradhi yalipofikia upeo wake na alama za kukata tamaa zilipodhihiri, hapo siku moja akamjia Hudhur[as] na kwa shida ya maradhi akaanza kulia. Hudhur[as] anasema:

> "Moyo wangu ukalainika kwa hali ya unyonge wake na nikamwombea kwa Mungu. Kwa vile afya yake ilikadiriwa na Mungu, hivyo papo hapo nilifunuliwa:
>
> قُلْنَا يَا نَارُ كُونِي بَرْدًا وَّسَلَامًا
>
> "Yaani, Tuliuambia moto wa homa, uwe baridi na usalama. Basi wakati huo huo Baniani yule na Mabaniani wengine pia, wanaoishi bado katika mji huu huu na ni wakazi wa hapa, walipashwa habari ya ufunuo huu na ilidaiwa kwa kumtegemea Mungu kikamilifu kwamba Baniani huyo lazima atapona na hatafariki kamwe kwa maradhi hayo. Basi baada yake hata wiki moja haikupita, Baniani huyo akapona na maradhi hayo ya kuua, na akapata afya kamili. ***Alhamdulillahi alaa dhalika.***"[84]

Lala Malava Mal alikuwa mtu Mwaria mwungwana wa Qadian. Ingawa yeye na Lala Sharampat walishuhudia mamia ya ishara na hawakusilimu, lakini kidunia waliishi maisha ya uungwana. Lala

[83] Qadian Ke Aria Aur Ham, uk. 28-29

[84] Barahine Ahmadiyya, sehemu 3, uk. 227, 228, Tanbihi ya Tanbihi

Malava Mal, miaka michache baada ya mgawanyiko wa nchi alifariki mjini Qadian katika umri mrefu wa miaka 95, na alisihi watoto wake kwamba sawa na utabiri wa Bwana Mirza, familia yake lazima itarudi Qadian, kwa hiyo msipate kuwapinga Waahmadiyya waliobaki katika Qadian. Mimi mwandishi nasema kwamba Lala Malava Mal alikuwa akikaa dukani mwake katika Soko la Mabaniani la Qadian na alikuwa akitengeneza dawa za baadhi ya maradhi sawa na maagizo ya Seyyidna Ahmad[as] na kuuza. Waahmadiya pia walikuwa wakinunua sana dawa hizo na walikuwa wakisikiliza kutoka kwake habari za siku za ujana wa Seyyidna Ahmad[as].

KAKUTANA NA WATAWA WA ZAMANI KATIKA KASHFI

Mnamo mwaka 1872, katika ndoto alikula chakula pamoja na Hadhrat Masihi[as] katika chombo kimoja na waliongea pasipo kujikalifisha.[85]

Karibu na zama hizo hizo ndani ya ndoto alikutana na Hadhrat Baba Nanak[rh] na yeye alijidhihirisha kuwa yu Mwislamu.[86]

Mnamo mwaka 1875 ndani ya ndoto alikutana na Hadhrat Seyid Abdul Qadir Jilani[rh], na akaambiwa kwamba roho yake na roho ya Seyid Abdul Qadir zinalingana katika tabia ya asili.[87]

SAUMU ZA MIEZI 8 AU 9 NA KUTEREMKA KWA NURU ZA KIMBINGU

Mwishoni mwa mwaka 1875 au mwanzoni mwa 1876, mzee mmoja mtawa alikutana naye ndotoni na "kwa kusema kwamba kufunga saumu kwa kupokea nuru za kimbingu ni suna ya familia wa Mtume[saw] akaashiria nitimiza suna ya Ahle Bait." Kwa hiyo, yeye alifunga saumu za miezi 8 au 9 kwa siri. Akizungumzia habari hii anasema:

> "Basi, niliona yafaa kufunga saumu kwa muda fulani, lakini nikapata wazo kwamba afadhali nilitekeleze hili kwa siri. Basi,

[85] Barahine Ahmadiyya, sehemu 3, uk. 253, Tanbihi ya Tanbihi

[86] Nuzulul Masih, uk. 204

[87] Zamima Barahine Ahmadiyya, sehemu 5, uk. 65, maelezo ya pembeni.

nikafuatilia njia hii kwamba nilikuwa nikiagiza chakula ndani ya sebule yangu kutoka nyumbani, na kwa siri nilikuwa nikiwapa hicho baadhi ya watoto mayatima niliowasisitizia kufika kwa wakati maalum. Na hivyo nilikuwa nikifunga siku nzima, wala hakuna minghairi ya Mwenyezi Mungu aliyejua kuhusu saumu hizo. Kisha baada ya wiki 2, 3 niligundua kwamba kwa saumu kama hizo ambapo ninakula mara moja kwa kushiba sioni shida yoyote, kwa hiyo afadhali nipunguze chakula kiasi fulani. Basi tangu siku ile niliendelea kupunguza chakula hata kwamba nikala chapati moja tu kutwa kucha. Kadhalika nikaendelea kupunguza chakula hata kwamba kwa masaa ishirini na manne chakula changu kikawa *tola*[88] chache tu za chapati. Na nikafanya hivi kwa miezi 8 au 9. Na kwa chakula kidogo sana kiasi hiki ambacho hakiwezi kumtosheleza mtoto wa miezi miwili mitatu, Mungu Alinihifadhi na kila balaa na afa. Na miongoni mwa maajabu ya saumu za aina hii niliyoshuhudia ni kashfi nyepesi nilizoona katika zama hizo. Nikakutana na baadhi ya Manabii wa zamani na Mawalii wa daraja za juu waliopita katika umati huu. Safari moja, katika hali ya kuwa macho nilimwona Mtume Mtukufu[saw] pamoja na Hasan, Husain, Ali na Fatuma, ***Mungu Awe radhi nao wote***. Na hii haikuwa ndoto, bali ilikuwa aina fulani ya hali ya kuamka. Ilmuradi, kwa njia hiyo nilikutana na watakatifu kadha ambao kuwataja ni kurefusha. Na zaidi ya hayo, nuru za kiroho zilionekana kimithali kwa sura ya nguzo za kijani na nyekundu za kuvutia na kupendeza kiasi hiki kwamba hazielezeki. Nguzo zile za nuru zilizoelekea moja kwa moja kwenye mbingu ambazo baadhi yao zilikuwa nyeupe sana, nyingine za kijani na nyingine nyekundu. Hizo zilihusikana sana na moyo kiasi hiki kwamba kwa kuziona moyo ulikuwa unafurahika sana, na haitakuwa duniani ladha yoyote ambayo moyo na roho ilihisi kwa kuziona. Nafikiri nguzo zile zilidhihirishwa kimithali kwa kuchanganyika mapenzi ya Mungu na mja wake. Yaani, hiyo ilikuwa nuru iliyotoka moyoni na ile ya

[88] *Tola* moja ni sawa na uzani wa gramu 12.

pili ilikuwa nuru iliyoteremka kutoka juu na kwa hizo mbili kukutana sura ya nguzo ikazalika. Haya ni mambo ya kiroho, dunia haiyatambui, lakini wapo duniani wanaopata habari za mambo hayo.

Ilmuradi, kwa kufunga saumu kiasi hiki, maajabu yaliyodhihiri kwangu yalikuwa ni kashfi za aina aina."[89]

KAKUTANA NA MAULAWII ABDULLAH GHAZNAWII NA BAADHI YA WATAWA WENGINE

Katika zama zile Seyyidna Ahmad[as] alianza kusafiri kwa kukutana na baadhi ya watawa, na pia akaanza kutembelewa na baadhi ya waja wa Mungu. Kwa ufupi, hapa chini, tunamtaja mzee mmoja tu, naye alikuwa ni Hadhrat Maulawii Abdullah Ghaznawii. Mzee huyo alizaliwa kijijini Geru katika wilaya ya Ghazni (Afghanistan). Yeye alikuwa mtu mwenye ibada na alikuwa anashughulikia kumkumbuka Mungu na alikuwa anampenda sana Mtume[saw]. Katika ndoto yeye aliona Sahihi Bukhari kuwa ni yenye mavumbi, na katika ndoto alianza kuisafisha. Baada ya ndoto hii, yeye alianza kutalii sana Sahihi Bukhari. Masheikh wadhalimu wa Ghazni kwa kuona hali yake hii wakaeneza kuwa yeye ni Wahabi na walimtolea fatuwa ya kufuru. Wakampaka masizi usoni na wakimpandisha juu ya punda wakamfukuza nchini, ndipo yeye akahamia Amritsar.[90] Seyyidna Ahmad[as] alionana naye mjini Amritsar na kitongoji chake Khairdi.

Akieleza habari za kuonana naye, Seyyidna Ahmad[as] anasema:

"Wakati alipokuwa hai, nilipata kuonana naye safari moja katika Khairdi na mara ya pili katika Amritsar. Nikamwambia kwamba wewe unafunuliwa, na kuna utashi wangu mmoja, uombe kuhusu huo, lakini sitakuambia utashi wenyewe ni nini. Akasema, 'Katika kuficha kuna baraka, nami, Mungu Akipenda, nitaomba dua, na kupata ufunuo si katika hiari ya mtu.' Na utashi wangu ulikuwa kwamba dini ya Muhammad[saw] inadhoofika siku hadi siku, Mungu Aisaidie. Baada yake

[89] Kitabul Bariyya, uk. 164-166, Maelezo ya Pembeni.

[90] Sirat Thanai, na Maulawii Abdul Majid Sohdarwii

nilikwenda Qadian. Baada ya siku chache nilipata barua yake kupitia posta ambamo aliandika, "Nilikuombea, nikafunuliwa: وَانْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكٰفِرِيْنَ[91] Ni mara chache kwamba nimejaliwa kufunuliwa haraka hivyo, naona hii ni kwa sababu ya ikhlasi yako."[92]

Hizo zilikuwa funuo za mwanzo, waila baadaye huyo mtawa alimwambia mfuasi wake mmoja mwenye ikhlasi (Bwana Munshi Muhammad Yakub) kwa idhini ya Mungu kiasi hiki kwamba baada yangu Bwana Mirza atatumwa kwa kazi kubwa sana. Vilevile siku chache kabla ya kifo chake (katika Februari 1881) kwa kupata habari kutoka kwa Mwenyezi Mungu alitabiri kwamba:

"Nuru moja imeteremka kutoka mbinguni upande wa Qadian, lakini ni masikitiko kwamba watoto wangu wamenyimwa."[93]

Basi utabiri wa Bwana Maulawii ulitimia, na watoto wake sio tu kuwa hawakumwamini Seyyidna Ahmad[as] bali wakawa katika mstari wa mbele kumpinga. Bwana Maulawii alifariki tarehe 15 Februari 1881 na akazikwa mjini Amritsar nje ya Mlango wa Sultan Wand. *Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiuun.*

KIFO CHA BABA YAKE, JUNI 1876

Mwanzoni mwa Juni 1876, Hudhur alikwenda Lahore kufuatilia kesi fulani. Alipokuwa bado huko Lahore, akaambiwa katika ndoto kwamba wakati wa kifo cha baba yake umekaribia. Anasema:

"Wakati nilipoota ndoto hii, haraka sana nilifika Qadian, na nikamkuta katika maradhi ya kuhara damu, lakini haikutazamiwa kwamba siku ya pili baada ya kufika kwangu atafariki. Kwani shida ya maradhi ilikuwa imepungua na alikuwa akikaa imara. Siku ya pili wakati wa jua kali la utosini, sisi sote tulipokuwa pamoja naye, baba aliniambia kwa huruma, "wakati huu upumzike kidogo", kwani huo ulikuwa mwezi wa Juni, na

[91] Na Utusaidie juu ya watu makafiri.

[92] Hakikatul Wahyi, chapa ya kwanza, uk. 239-240

[93] Hayatun Nabii J. 1, uk. 80-82

joto lilikuwa kali sana. Mimi kwa kupumzika nikaenda ghorofani na mhudumu mmoja alianza kukanda miguu yangu. Katika hali hii nilifunuliwa:

وَالسَّمَآءِ وَالطَّارِقِ

"Yaani, naapa kwa mbingu iliyo chanzo cha kadri, na ninaapa kwa tukio lile litakalotukia baada ya jua kuzama. Nikafahamishwa kwamba ufunuo huu ni salamu za rambirambi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na tukio lenyewe ni kwamba leo hii baba yako baada ya machweo atafariki. ***Subhanallahi***, ni shani kubwa iliyoje ya Mungu Adhimu kwamba mtu aliyefariki kwa masikitiko juu ya kupoteza umri wake, Mungu Anatoa pole kwa kifo chake. Watu wengi watashangaa kwa jambo hili kwamba kutoa pole kwa Mwenyezi Mungu ina maana gani. Lakini ikumbukwe kwamba Mwenyezi Mungu Anapomhurumia mtu basi Anamtendea hivyo kama rafiki. Kucheka pia kwa Mwenyezi Mungu kumetajwa katika Hadithi, hiyo nayo ndiyo katika maana hiyo hiyo.[94]

Basi, baba yake siku hiyo hiyo baada ya machweo alifariki. ***Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiuun.*** Alizikwa katika kona moja ya Masjid Aqsa huko Qadian. Habari hii itaelezwa kirefu baadaye, ***Inshallah***.

MATUNZO YA MUNGU BAADA YA KIFO CHA BABA

Huzuni ya kifo cha baba ilikuwa ni jambo la kawaida, lakini kwa sababu ya kuwa binadamu mara ikapita moyoni mwake kwa kitambo kidogo kwamba kwa kuzikatika njia za mapato zilizohusikana na uhai wa baba, haijulikani matatizo yepi yatanikabili. Wazo hili lilipopita tu moyoni, mara akafunuliwa ufunuo huu wa pili:

أَلَيْسَ اللّٰهُ بِكَافٍ عَبْدَهٗ

Yaani, je Allah Hamtoshei mtumishi Wake? Hudhur anasema:

"Ufunuo huu ulinipa utulivu na raha ya ajabu na uliingia moyoni mwangu kama msumari wa chuma cha pua. Basi, naapa

[94] Kitabul Bariyya, maelezo ya pembeni, uk. 159-161.

> kwa Mungu ambaye uhai wangu umo mkononi mwake kwamba Alitimiza ufunuo wake wenye habari njema namna ambavyo hata sikuwaza wala sikufikiria. Akanikimu namna ambavyo hata baba yeyote hatamkimu mwanaye. Alifululiza kunifanyia hisani ambazo haiwezekani kwangu kuzihesabu.[95]

Kwa vile ufunuo huu ulikuwa na bishara adhimu, kwa hiyo mara akamwambia Lala Malava Mal habari zote na akamtuma aende Amritsar kwa Hakim Muhammad Sharif Kalanori na kupitia kwake achongeshe maneno hayo kwenye kito cha pete na kumletea pete. Basi, Lala Malava Mal alikwenda Amritsar na akaleta pete kwa kutayarisha kwa Rupia 5. Na kwa njia hiyo Baniani mmoja na Mwislamu mmoja wakiwa wajumbe wa mataifa mawili makubwa ya India wakawa mashahidi wa ishara hiyo adhimu.

Mimi naeleza kwamba pete hiyo hivi sasa iko kwa Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad Khalifatul Masihi II a.t.b.a., yaani ikamwangukia yeye kwa kupigwa kura. Zaidi ya pete hiyo, Hudhur[as] alikuwa na pete mbili zingine pia, mojawapo ilitengenezwa mnamo mwaka 1892 ambayo ilichorewa ufunuo huu wa Hudhur[as]:

اُذْكُرْ نِعْمَتِيَ الَّتِيْ اَنْعَمْتُ عَلَيْكَ غَرَسْتُ لَكَ بِيَدِيْ رَحْمَتِيْ وَ قُدْرَتِيْ

Na ya pili ilitengenezwa katika mwaka 1906. Ikawa hivi kwamba familia moja yenye ikhlas ya masonara ya huko Ban Bajwa, Wilaya ya Sialkot, ilimwomba Hudhur[as] kuwa tunataka kukutengenezea pete, basi tuchore nini juu yake. Hudhur[as] kasema: "Mola Bas".[96] Baada ya kifo cha Seyyidna Ahmad[as], Hadhrat Amman Jan, mkewe Seyyidna Ahmad[as], aligawa pete hizo tatu kwa kura. Ni la ajabu kwamba kwa kupiga kura mara kadha, kila mara pete ya kwanza ilimwangukia Hadhrat Khalifatul Masihi II, iliyochorewa: اَلَيْسَ اللّٰهُ بِكَافٍ عَبْدَهٗ na ya pili iliyochorewa: اُذْكُرْ نِعْمَتِيْ... ilimwangukia Hadhrat Mirza Bashir Ahmad, na ya tatu iliyochorewa "Mola Bas" ikawa kwa Hadhrat Mirza Sharif Ahmad.

---

[95] Kitabul Bariyya, uk.162-163.

[96] Yaani: "Mola tu".

MAZISHI YA BABA KATIKA KONA YA MASJID AQSA

Msikiti Aqsa ambao katika kona yake baba yake alizikwa katika sehemu aliyowekea alama baba mwenyewe, yalazimu ielezwe pia historia fupi ya ujenzi wake, kwani masimulizi mengi ya Jumuiya yanahusikana nao. Katika kurasa za nyuma imeshaelezwa kwamba kwa sababu ya kushindwa mfululizo katika kesi za mashamba, baba yake katika umri wake wa mwisho alielekea sana kwenye kutafuta radhi ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, aliamua kwamba kwa ajili ya dunia ametumia mali nyingi lakini hakupata kitu isipokuwa majuto tu, kwa nini sasa kwa kutukuza jina la Mungu usijengwe msikiti, si ajabu hii iwe ni njia ya kusamehewa. Basi, kwa shabaha hii akanunua katikati ya kijiji jumba kubwa lililokuwa limeachwa la Masingasinga kwa kutoa Rupia 700, na kwa ikhlasi kubwa na moyo uliojaa majuto aliweka jiwe la msingi wa msikiti.

Yaonekana ni lazima kueleza hapa mandharinyuma ya msikiti huu aliyoeleza Seyyidna Ahmad[as]. Hudhur anasema:

> "Majuto ya kuhudhuria mbele ya Mungu Mwenye shani kwa mikono mitupu yaliendelea kumshinda baba siku hadi siku katika sehemu ya mwisho ya umri wake. Yeye alikuwa akisema mara nyingi kwamba katika mambo mabovu ya dunia nimepoteza umri wangu bure. Safari moja baba alieleza ndoto yake hii kwamba nilimwona Mtume Mtukufu[saw] akielekea kwenye nyumba yangu kwa shani kubwa kama ajavyo mfalme mkubwa. Nikamwendea mbio ili kumpokea. Nilipofika karibu naye nikafikiri yanipasa nimpe zawadi. Nilipotia mkono wangu mfukoni, humo mlikuwa na Rupia moja tu. Nilipoiangalia kwa makini, nikaikuta ni Rupia bandia. Hapo machozi yalijaa machoni mwangu, nami nikazinduka. Kisha mwenyewe akaiagua kwamba pamoja na mapenzi ya dunia, kumpenda Mungu na Mtume[saw] wake ni kama Rupia bandia. Na alikuwa akisema kwamba sawa sawa nami siku za mwisho za hata baba yangu pia zilipita katika msiba na ghamu na huzuni, na popote alipojaribu, hatimaye akashindwa. Na alikuwa akisoma ubeti wa baba yake, yaani wa babu yangu, ambao mshororo wake mmoja

nimeshasahau, na wa pili ni huu:

'Nifanyapo tadbiri, takdiri inanicheka'.

"Na huzuni yake na uchungu wake huu ulizidi sana katika uzee wake. Kwa kufikiria hayo, takriban miezi sita kabla, baba alijenga katikati ya mji, msikiti uliokuwa msikiti wa Ijumaa wa eneo hilo. Na aliusia kwamba kaburi langu liwe katika kona ya msikiti ili jina la Mungu Mwenye shani liendelee kuingia masikioni mwangu. Si ajabu, hii iwe sababu ya kusamehewa. Basi, siku ambapo msikiti ulikamilika kwa jiha zote, labda matofali machache tu ya sakafu yalibaki kujengwa, baba akafariki kwa maradhi ya kuhara baada ya kuugua siku chache tu, na akazikwa katika kona ile ile ya msikiti huo huo pale alipotia alama hali akisimama. ***Ee Allah mrehemu na mwingize Peponi***. Amin. Alikuwa na umri wa miaka 80 au 85."[97]

Ingawa sawa na mahitaji ya Jumuiya yaendeleayo kuzidi, msikiti huo umepanuliwa sana, lakini sehemu yake ya kwanza imehifadhiwa vilevile ilivyokuwa. Uga mdogo uliojengwa kwa matofali madogo ya aina ya zamani pia umebaki ulivyokuwa. Kwa kuwa kaburi la baba yake limeingia ndani ya uga wa msikiti, kwa hiyo kwa kujenga kuta pande zote nne imetiwa paa ili lihifadhiwe na maji ya mvua. Angalieni bahati njema ya baba yake kwamba yeye, sawa na hali ya wakati ule alitamani kusikia sauti ya adhana tu, lakini Mwenyezi Mungu Akianzisha Jumuiya ya Ahmadiyya kwa mkono wa mwanaye, alizidisha sana kumkumbuka Mungu kiasi hiki kwamba tangu wakati huo mpaka leo Mungu anatajwa humo mfululizo na Mungu Akipenda mpaka siku ya kiama Ataendelea kutajwa. Zaidi ya sala tano, sala za nafali, huo ni msikiti wa Ijumaa pia wa Qadian ambamo zaidi ya kutolewa hotuba za Ijumaa, na kufanywa mikutano, darasa la Kurani Tukufu pia linatolewa kila siku. Na ajabu ni hii kwamba watoaji darasa mara nyingi walikuwa wakisimama karibu na kaburi hilo. Watu wa zamani wanaeleza kuhusu Hadhrat Khalifatul Masihi I[ra] pia kwamba alikuwa akisimama hapo hapo. Nami niliwaona

[97] Kitabul Bariyya, maelezo ya pembeni, uk. 157-159

mwenyewe kwa muda mrefu Hadhrat Hafidh Roshan Ali[ra] na ustadhi Hadhrat Seyid Sarwar Shah[ra] wakitoa darasa hapo. Hadhrat Khalifatul Masihi II[atba] akatoa darasa la Kurani Tukufu nzima akisimama pale karibu na kaburi kwa miaka kadha. Na mara ya pili darasa la Kurani lilikuwa linaendelea bado hata kwamba baada ya miaka michache tukio la 1947 lilitokea.

BAADHI YA RUYA KUHUSU KUDUMU HESHIMA YA UKOO HUU

Habari za ufunuo wenye shani kubwa اَلَيْسَ اللّٰهُ بِكَافٍ عَبْدَهٗ zimeshatajwa juu uliomaanisha kwamba sasa Mungu ndiye Atakayekuwa mkimu wako kikamilifu. Kuhakikisha ufunuo huu alionyeshwa baadhi ya maonyesho pia. Basi, anasema:

> "Baadhi ya wakati katika ndoto au kashfi mambo ya kiroho yakichukua sura ya kimwili yanaonekana mithili ya mwanadamu. Nakumbuka kwamba wakati baba yangu ***Mungu Amsamehe,*** aliyekuwa Chifu mheshimiwa na alijulikana kwa heshima katika maeneo yake, alipofariki, baada ya kifo chake, siku ya pili au ya tatu nilimwona mwanamke mzuri sana katika ndoto ambaye sura yake bado ipo mbele ya macho yangu, yeye akasema, 'Jina langu ni Rani[98],' na akaniambia kwa ishara kwamba 'Mimi ni heshima na jaha ya nyumba hii', na kasema kwamba nilikuwa karibu niende lakini nimebaki kwa ajili yako."[99]

Tena anasema:

> "Katika siku zile zile niliona mtu mmoja mzuri, nami nikamwambia, u mzuri wa ajabu, ndipo kwa ishara akaniambia mimi ni bahati yako njema. Na akijibu swali langu hili kwamba wewe ni mtu mzuri wa ajabu, akasema "Naam, mimi ni mtu nistahiliye kuonwa."[100]

---

[98] '*Rani'* maana yake malkia.

[99] Izala Auham, uk. 213

[100] Izala Auham, uk. 213-214

MWANZO WA MAONGEZI NA MWENYEZI MUNGU KWA WINGI

Baada ya kifo cha baba yake, Seyyidna Ahmad[as] alianza kupokea funuo kwa wingi. Anasema:

> "Upande mmoja baba kafariki dunia na upande mwingine silsila ya maongezi na Mwenyezi Mungu ikaanza sana sana. Siwezi kueleza kwamba nilikuwa na amali gani ambayo kwayo nilifadhiliwa na Mungu. Nahisi tu ndani mwangu kwamba moyo wangu kitabia una mvuto kwa uaminifu wa Mwenyezi Mungu ambao hauwezi kuzuiliwa na kitu kiwacho chochote. Basi, hiyo ni hisani Yake."[101]

ZAMA ZA USIMAMIZI WA KAKA YAKE MIRZA GHULAM QADIR

Baada ya kifo cha baba yake, msimamizi wa mali ya familia akawa kaka yake, Mirza Ghulam Qadir. Kama Hudhur angetaka, angeweza kutengewa sehemu yake kwa kudai ugawanyaji wa mali, lakini hakujali kabisa. Bali, akawa na kawaida yake kwamba chochote alichopata cha kula na kunywa akakipokea na hakulalamika kamwe. Kwa sababu ya kufunga saumu za miezi 8, 9 mfululizo alikuwa amezoea kutosheka kwa chakula kidogo sana, kwa hiyo katika siku zile pia akanufaika kikamilifu na mazoezi hayo. Mara nyingi alikuwa akigawa chakula chake baina ya maskini, na mwenyewe alikuwa akiagiza *chanee* — aina fulani ya choroko nyeusi — za paisa moja na kutafuna, wakati mwingine akashinda na njaa. Maoni ya kaka yake yalikuwa kama maoni ya baba yake, yaani yeye pia alikuwa akimsihi kwa kumwona kwamba hahusiki na mambo ya dunia. Lakini katika zama hizo mbili kulikuwa na tofauti hii wazi kwamba mapenzi ya baba yalikuwa mara nyingi yanataharaki, na wakati mwingine akiona wema wake na ucha Mungu wake alikuwa anajitolea kwake kwa mahaba. Zaidi ya hayo huruma ya mama ilikuwa hisani mojawapo adhimu ya Mwenyezi Mungu. Lakini katika zama za kaka yake matatizo yake yalizidi, kwani kaka yake mwenyewe alikuwa

[101] Kitabul Bariyya, maelezo ya pembeni, uk.163

mkurugenzi katika ofisi ya naibu Kamishna wa Gurdaspur na mara nyingi alikuwa akiishi huko huko, na nidhamu ya nyumbani ilikuwa mkononi mwa mke wa kaka yake aliyekuwa anamtendea kwa ukali. Ilmuradi, zama hizo zilikuwa taabu sana kwake, lakini alifanya subira ya hali ya juu ambayo mfano wake unaweza kupatikana katika maisha matakatifu ya manabii watakatifu tu. Basi, Mwenyezi Mungu Alipomtuma na mamia ya watu walianza kula kwenye meza yake, hapo baadhi ya wakati alikuwa akikumbuka zama zake za nyuma na alikuwa akiitaja pia. Kuhusu jambo hilo amesema katika ubeti huu wa shairi lake.

لُفَاظَاتُ الْمَوَائِدِ كَانَ اُكْلِيْ وَصِرْتُ الْيَوْمَ مِطْعَامَ الْاَهَالِيْ

Yaani, zilikuwepo zama ambapo makombo ya mezani yalikuwa ni chakula changu, na leo Mwenyezi Mungu Amenijalia kwamba mamia ya watu wanakula chakula kwenye meza yangu. ***Alhamdulillahi alaa dhalika.***

Siku hizo zilikuwa zenye taabu sana kwake na kuvunja moyo kiasi hiki kwamba safari moja alimwomba kaka yake fedha kidogo sana kwa kuagiza gazeti fulani kwa haja fulani ya kidini, lakini yeye alikataa akisema, "Huu ndio ubadhirifu".

TAII AMEKUJA

Mnamo mwaka 1900, Seyyidna Ahmad[as] alifunuliwa ***Taii Aii*** ─ maana yake, amekuja ***Taii***. Wakati ule haikueleweka ina muradi gani. Lakini, ni kudra ya Mungu kwamba mke wa kaka ya Seyyidna Ahmad[as], ambaye Seyyidna Ahmad[as] alikuwa ameteseka mkononi mwake, alijiunga na Jumuiya Ahmadiyya kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu kwa mkono wa Khalifatul Masihi II, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad[ra] mnamo mwaka 1921. Basi hapo ikafahamika kwamba ufunuo "Taii Aii" ulimaanisha nini. Mama huyu katika familia yote alitambulika kwa lakabu ya "Taii"[102]. Mwenyezi Mungu Alimzidishia ikhlasi kiasi hiki kwamba hata alifanya wasia pia.

[102] Taii lamaanisha mke wa kaka wa baba. Mama huyo alikuwa mkewe kaka ya baba wa Hadhrat Khalifa II[ra], naye akajiunga katika Ahmadiyya katika zama za ukhalifa wake. ─ Mwenezi.

Akafariki tarehe mosi Desemba 1927 katika umri wa miaka 97 na alizikwa katika Bahisti Makbara Qadian. *Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun.*

Tanbihi: Hapa kulingana na madhumuni ya sehemu hii nimetaja ufunuo wa "Taii Aii" waila mahali pake hasa pa kutajwa ni katika matukio ya mwaka 1900.

MIRZA A'ZAM BEG KASHTAKI ILI KUSHIRIKI KATIKA MILKI YA MABABU YA SEYYIDNA AHMAD[AS]

Mambo ya Mwenyezi Mungu huwa ya ajabu. Mpaka Seyyidna Ahmad[as] alikuwa hajarithi kikamilifu milki yake, heshima na jaha ya nyumba yake iliendelea kupungua sawa na ruya na kashfi zake. Katika zama za Mirza Ghulam Qadir, Mirza A'zam Beg, Naibu Kamishna wa zamani, alishtaki kortini familia yake kwa niaba ya washiriki wasiomiliki, ili kushiriki katika milki yake. Seyyidna Ahmad[as] anasema:

> "Kaka yangu, Mirza Ghulam Qadir marehemu, alifuatilia kesi akiwa na yakini ya kushinda. Nilipofanya maombi, Mungu Mjuzi Alinifunulia kwamba
>
> أُجِيْبُ كُلَّ دُعَائِكَ إِلَّا فِيْ شُرَكَائِكَ[103]
>
> Basi, nikiwakusanya jamaa zangu wote nikawaelezea wazi wazi kwamba Mungu Mjuzi Amenipasha habari kwamba hamtashinda kamwe katika kesi hii, kwa hiyo inapaswa kujitoa katika kesi hii. Lakini, hawakuthamini niliyosema kwa kuangalia sababu za kidhahiri na kwa yakini ya kushinda, na wakaanza kufuatilia kesi na katika mahakama ya mwanzo kaka yangu alifaulu pia. Lakini ingewezekanaje kutendeka kinyume cha wahyi wa Mungu Mjuzi wa ghaibu! Hatimaye, katika mahakama ya juu kaka yangu alishindwa, na hivyo ukweli wa ufunuo uliwadhihirikia wote."[104]

[103] Tafsiri: Nitakubali kila ombi lako, isipokuwa lile linalohusikana na washirika wako.

[104] Nuzulul Masihi, uk. 212, 213

Maelfu ya shukrani ni kwa Mwenyezi Mungu kwamba katika zama za Khalifatul Masihi II Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad[atba] milki ile ilinunuliwa na hivyo milki ya familia yake ilirudi tena.

KESI YA POSTA

Mnamo mwaka 1877, Mkristo mmoja wa Amritsar, Ralia Ram, wakili, alimshtaki Seyyidna Ahmad[as]. Akieleza habari hii anasema Seyyidna Ahmad[as]:

> "Mnamo mwaka 1877 nilituma makala moja iliyoisaidia Islam dhidi ya Waaria kwa kuichapisha katika matbaa ya Mkristo mmoja, jina lake Ralia Ram, ambaye alikuwa wakili pia na aliishi Amritsar, alikuwa anatoa gazeti moja vile vile. Nikatuma makala hiyo katika sura ya kifurushi kilicho wazi pande mbili na nikatia mle ndani ya hicho kifurishi barua moja pia. Kwa kuwa ndani ya barua mlikuwa na maneno ya kuisaidia Islam na ishara ya kubatilisha dini nyinginezo, na ilisisitizwa pia kuchapisha makala, kwa hiyo huyo Mkristo kwa sababu ya hitilafu ya dini akashikwa na hasira. Kwa bahati akapata nafasi ya kushambulia kiuadui, kwani kutia barua ndani ya kifurushi ilikuwa ni hatia[105] kisheria, nami nilikuwa sina habari hii. Adhabu ya hatia hii sawa na sheria za posta ilikuwa faini ya Rupia mia tano au kifungo cha hadi miezi sita. Basi, yeye akiwa mtoa habari akawafanya maofisa wa posta wanishtaki mahakamani.
>
> Kabla ya kupata habari ya kesi hii, Mwenyezi Mungu Alinidhihirishia katika ruya kwamba "Ralia Ram ametuma nyoka kuniuma, nami nikamkaanga kama samaki na kumrudishia."
>
> Najua kwamba hii ilikuwa ishara kwenye jambo hili kwamba jinsi kesi ile ilivyoamuliwa mahakamani, ni mithali inayoweza kuwasaidia mawakili.

[105] Sheria hiyo ya posta haipo siku hizi. Lakini katika zama zile tunazozungumzia ilikuwepo sheria hii. Tazameni Sheria Na. 14 ya 1886 kifungu 12, 56. Vilevile Tangazo la serikali ya India Na. 2424 ya tarehe 7 Desemba 1877, kifungu 43.

Ilmuradi, kwa hatia hii niliitwa kwenye makao makuu ya Wilaya ya Gurdaspur. Mawakili tulioshauriana nao kuhusu kesi walishauri kwamba hakuna njia yoyote isipokuwa kuongopa, na wakashauri kwamba sema tu sikuweka barua katika kifurishi, labda Ralia Ram mwenyewe aliiweka. Na wakasema kwa kutuliza kwamba kwa kusema hivi uamuzi utafanywa juu ya ushahidi, na kwa kuleta mashahidi wachache waongo utaachiliwa, la sivyo, kesi ni ngumu sana na hakuna njia ya kuachiliwa. Lakini nikawajibu hao wote kwamba sitaki kuachana na ukweli katika hali yoyote iwayo, itokee tu itakayotokea. Kisha, siku hiyo hiyo au keshoye nilipelekwa katika mahakama ya Mzungu mmoja, na kunikabili akahudhuria ofisa wa posta kama mdai kwa niaba ya serikali. Wakati ule hakimu wa mahakama kwa mkono wake aliandika kauli yangu. Kwanza kabisa aliniuliza swali hili hili kwamba je wewe uliweka barua katika kifurushi chako? Barua hii na kifurushi hiki ni chako? Hapo mara moja nikajibu kwamba barua hii ni yangu na kifurushi pia ni changu, nami nilituma kifurushi kwa kuweka barua hii ndani yake. Lakini, sikufanya hivi kwa nia mbaya ya kuihasiria serikali gharama ya posta, bali sikuiona barua hii ni tofauti na makala hayo wala haikuelezwa mle habari yoyote ya nyumbani. Kwa kusikia tu jambo hili, Mwenyezi Mungu Akauelekeza moyo wa Mzungu yule upande wangu. Ofisa wa posta alipiga makelele sana dhidi yangu na alitoa hotuba ndefu ndefu katika Kiingereza ambazo sikuzielewa, lakini nilielewa kiasi hiki kwamba baada ya kila hotuba, hakimu yule alikatalia mbali maelezo yake yote kwa kusema 'la, la' kwa lugha ya Kiingereza. Hatimaye, ofisa huyo aliyekuwa mdai alipokuwa ameishamaliza kueleza sababu zake zote na kutoa vikali hoja zake zote, ndipo hakimu alielekea kuandika uamuzi, na baada ya kuandika labda mstari mmoja au mmoja na nusu, aliniambia, "Haya, unayo ruhusa". Nikisikia hayo, nikatoka chumbani mwa mahakama, nikamshukuru Mhisani wangu wa kweli ambaye Alinishindisha dhidi ya ofisa Mzungu. Najua kabisa kwamba wakati ule Mwenyezi Mungu Aliniondolea balaa hiyo kwa

baraka ya ukweli.

Hapo kabla niliota pia kwamba mtu mmoja alijaribu kuniondolea kofia yangu, nikamwuliza, 'Wafanya nini'? Ndipo akaacha kofia kichwani mwangu na kasema 'Ni heri tu, heri tu.'[106]

Tafakarini, katika kesi hiyo yeye alikuwa na mtihani mgumu namna gani. Kama angalikuwa mwingine mahali pake, labda hangaliweza kusimama imara katika mtihani mkali huo, lakini yeye aliye mkweli kabisa alisimama imara juu ya msimamo wake na kwa kukataa ushauri wa mawakili wake, alieleza ukweli mtupu mahakamani.

اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَّعَلٰى اٰلِ مُحَمَّدٍ[107]

AKAPONA KIMUJIZA KATIKA MARADI YA HATARI

Mnamo Mwaka 1880 alipatwa na maradhi ya msokoto wa tumbo. Akahara damu mara kwa mara. Hali hii iliendelea takriban siku kumi na sita. Warithi wake waliishamsomea Sura Yasin mara tatu, na mara ya mwisho walikuwa na yakini kabisa kwamba leo mpaka jioni atakuwa amezikwa. Ilmuradi, hali ya kukata tamaa ilipofikia mwisho na jamaa zake walianza kulia wakisimama nyuma ya kuta, ndipo yeye alifundishwa na Mungu Mponyaji dua hii kwa ufunuo:

سُبْحَانَ اللّٰهِ وَبِحَمْدِهٖ سُبْحَانَ اللّٰهِ الْعَظِيْمِ ۔ اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَّاٰلِ مُحَمَّدٍ[108]

Na mara akatiliwa moyoni mwake kwamba ingiza mkono katika maji ya mto yaliyo na mchanga pia na soma maneno haya matakatifu na uyapake kifuani, mgongoni, mikononi na usoni pako, nawe utapona. Hudhur anasema:

"Haraka sana yaliagizwa maji ya mto pamoja na mchanga, nami nikaanza kufanya vile nilivyofundishwa. Na wakati ule hali yangu ilikuwa kwamba kutoka katika kila unywele moto ulitoka

[106] Aina Kamalaate Islam, uk. 297- 299

[107] Ee Allah, Umtolee baraka Muhammad na ali zake.

[108] Namtukuza Allah na kwa sifa zake njema. Namtukuza Allah Mwenye adhama. Ee Allah, Umtolee baraka Muhammad na ali zake.

na mwili wote ulikuwa unawasha vikali. Na katika hali ya kushindwa, moyo ulielekea kwenye jambo hili kwamba hata mauti ni afadhali ili niokoke na hali hiyo. Lakini nilipoanza kufanya vile, naapa kwa Yule ambaye uhai wangu umo mkononi mwake, kwamba kila mara kwa kusoma maneno hayo na kwa kupaka maji mwilini nikahisi kwamba moto ule unaendelea kutoka na badala yake ubaridi na utulivu unaendelea kupatikana, hata kwamba maji ya bakuli yalikuwa bado hayajaisha, nami nikaona kwamba maradhi yameniacha kikamilifu kabisa, na baada siku kumi na sita nikalala vizuri kwa afya. Ilipopambazuka nikafunuliwa ufunuo huu:

وَإِنْ كُنْتُمْ فِيْ رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلٰى عَبْدِنَا فَأْتُوْا بِشِفَآءٍ مِّنْ مِّثْلِهٖ

Yaani, ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyomteremshia mtumishi wetu, basi leteni ponyo lililo mfano wake."[109]

BISHARA YA KUREJESHWA KAZINI KWA JAJI NAWAB SARDAR MUHAMMAD HAYAT KHAN ALIYEKUWA AMESIMAMISHWA KAZI

Katika siku zile zile kaka ya Hudhur, Bwana Mirza Ghulam Qadir, alimwomba Hudhur kwa ajili ya kumwombea Jaji Nawab Sardar Muhammad Hayat Khan aliyekuwa amesimamishwa kazi na serikali kwa mashtaka fulani, na alikuwa amepatwa na mashaka ya aina aina kwa sababu ya kurefuka zama za kusimamishwa kazi. Yeye alipomwombea akaonyeshwa katika ruya kwamba Bwana Nawab amesimama mbele yake, na yeye anamwambia, "Usiwe na hofu yoyote, Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu, Yeye Atakuokoa."[110]

Ingawaje kulingana na hali ya kidhahiri ilifahamika kuwa kurejeshwa kwake kazini ni muhali, lakini akarejeshwa kazini. *Alhamdulillahi alaa dhalik.*

[109] Tiryaqul Quluub, uk. 37-38

[110] Barahine Ahmadiyya, sehemu ya 3, uk. 252, Tanbihi ya maelezo ya pembeni, Na. 1, na Al Hakam, J. 6, Na. 32 ya tarehe 10 Septemba 1902

USIKU WA MAPINDUZI YA KIROHO YASIYO NA KIFANI

Kifo cha Hadhrat Maulawii Abdullah Ghaznawii kimeshatajwa juu na kwamba alifariki tarehe 15 Februari 1881. Kabla yake kidogo, Hudhur alipokuwa Gurdaspur safarini, usiku moja yeye aliambiwa katika ruya kwamba zama za kifo cha Hadhrat Maulawii Abdullah Ghaznawii zipo karibu. Alipoamka akahisi kwamba mvutano fulani wa kiroho unafanya kazi ndani mwake mpaka akaanza kupata ufunuo. Akitaja mapinduzi ya kiroho ya usiku ule anasema:

> "Huo ulikuwa ni usiku ambamo Mwenyezi Mungu Alinihalisisha kikamilifu, na mabadiliko ya namna fulani yalitokea ndani mwangu ambayo hayangeweza kwa mkono au azma ya binadamu".[111]

[111] Nuzuulul Masihi, uk. 237

MLANGO WA PILI

TANGU KUANDIKA BARAHINE AHMADIYYA MPAKA BAIATI YA KWANZA

MANDHARI NYUMA YA BARAHINE AHMADIYYA

Kabla ya kutaja kitabu chake mashuhuri, Barahine Ahmadiyya, ningependa kuwaelekeza wasomaji waitalii miendeleo ya dini za zama zile. Kuhusu dini ya Kikristo imeshatajwa tayari katika kurasa za nyuma. Zaidi ya hiyo, madhehebu mengine mawili yalikuwa yamezalika pia nchini, Aria Samaj na Barahmu Samaj. Kusudio la dini hizi zote tatu kwa pamoja lilikuwa ni kujibidiisha kuwafutilia mbali Waislamu kidini kwa kufululiza kuishambulia Islam.

Na ilitokea hivi kwamba uasi wa mwaka 1857 ulikuwa umepangwa na Mabaniani kwa kuwatumia Waislamu dhidi ya serikali ya Kiingereza[112], na Waingereza mapema walikuwa na dhana mbaya juu ya Waislamu. Mabaniani walijifaidisha na hali hiyo na kwa njia ya Mwendeleo wao aliouweka msingi wake Swami Dayanand ─ na kuuita Aria Samaj ─ huko Bombay miezi michache kabla, wakapanga kwa kushauriana na viongozi wachache mashuhuri wa Mabaniani kwamba ienezwe chuki dhidi ya Waislamu kwa kushambulia Islam na Mwanzilishi wa Islam s.a.w. kwa mashambulizi ya kuumiza, na Mabaniani wapangiwe nidhamu pana kwa kisingizio cha upendo wa nchi na maendeleo ya taifa. Mushkili mmoja aliokabili Bwana Pandit katika kazi hii ulikuwa kwamba ma-Veda yaliyoweza kuwa msingi wa nidhamu ya Mabaniani, kwanza Mabaniani wengi sana hawakujua lugha yake ya Sanskriti, pili, kwa kupita wakati ma-Veda yalikuwa yamepata kubadilishwa kiasi hiki kwamba hata kama yangefasiriwa pia hayangeweza kufaidisha katika zama hizi za mwanga. Kwa kutatua tatizo hili, Pandit Dayanand aliandika kitabu kipya kiitwacho

[112] Tazameni Tarikh 'Uruje 'Ahde Saltanate Inglishia, uk. 66, chapa cha mwaka 1904, Shamsul Mataabi' Delhi.

Satiarath Parkash na kukiweka mbele ya Mabaniani. Ndani ya kitabu hicho msingi wa nadharia mpya ya Kibaniani uliwekwa kwa kutoa maelezo ya mbali ya mafundisho ya ma-Veda, ambayo walioelimika wa zama hizi wakaanza kuyakubali. Matokeo yakawa kwamba mwendeleo huu ulianza kupanuka polepole. Ingawa ulijulikana katika miji mbalimbali ya India pia, lakini katika baadhi ya miji ya Panjab, kama vile Lahore, Amritsar, na Rawalpindi, matawi yake yaliimarika. Muda mfupi tu ulikuwa umepita baada ya kuanzishwa Mwendeleo mpya, Seyyidna Ahmad[as] alianza kushindana nao na akaanza kuushambulia vikali kiasi hiki kwamba mwanzilishi wa Aria Samaj na wafuasi wake wakafadhaika. Maelezo yake ni kwamba katika gazeti la "Wakile Hindustan" la tarehe 7 Desemba 1877 na magazeti mengineyo, Pandit Dayanand, mwanzilishi wa Aria Samaj, alitangaza itikadi yake kuhusu roho kwamba "Roho hazihesabiki, na ni nyingi sana hata kwamba Parmeshar (Mungu) pia hajui idadi yao, kwa hiyo daima zinapata wokovu na zitaendelea kuupata, lakini hazitakwisha kamwe."

Itikadi hii batili ilipoenezwa tu, haraka sana Seyyidna Ahmad[as] akatoa rundo la hoja kuibatilisha. Kwa niaba ya Waaria, Baba Narain Singh, katibu wa Aria Samaj, na Pandit Kharhak Singh, mwanachama mshupavu wa Aria Samaj ya Amritsar walijitokeza uwanjani, mmoja baada ya mwingine kushindana naye, lakini wote wawili walishindwa vibaya sana hata kwamba hawakujimudu kukabiliana naye mpaka kufa kwao. Pandit Kharhak Singh akawa na dhana mbaya kuhusu ma-Veda kiasi hiki kwamba aliacha Aria Samaj, akawa Mkristo, na akatangaza katika magazeti mbalimbali kwa uwazi kwamba ma-Veda, hayana elimu ya Kiungu wala hayana ukweli, kwa hiyo hayawezi kuwa Neno la Mungu na kadha wa kadha.[113] Na yule wa pili akapigwa na butaa kiasi hiki kwamba hata wataalamu wa Kibaniani wenyewe waliyachukulia majibu yake kuwa upuuzi. Acheni habari za wengine, hata Pandit Dayanand mwenyewe aliathirika na makala za Hudhur na akatatanishwa vibaya sana. Seyyidna Ahmad[as] alimwita mara kwa mara kwenye mashindano. Alipoona kwamba haniachi

[113] Shihnae Haq, uk. 24, chapa ya kwanza.

kabisa, basi aliwatuma kwake Waaria watatu kwa ujumbe huu:

> "Kama roho, kwa hakika, sio nyingi zisizohesabika, lakini *tanasukh* daima inaendelea hivi kwamba wakati roho zote zinapopata uokovu, basi wakati wa haja hizo zinatolewa nje ya nyumba ya uokovu."[114]

Ni dhahiri kwamba huu ulikuwa ni ushinde wa Pandit Dayanand na ushindi dhahiri wa Seyyidna Ahmad[as]. Mashindano hayo yalijulikana sana baina ya watu, Bwana Pandit kwa kujiondolea mbali soni alimwita Hudhur kwenye mjadala ambao yeye akaukubali mara moja, lakini baadaye Bwana Pandit mwenyewe akaukimbia. Akieleza sababu ya kubuniwa ya kukimbia mashindano hayo, Mwaria mmoja Mahasha anaandika:

> "Kwa sababu ya hitilafu za ndani ya Aria Samaj, Mirza Ghulam Ahmad alipata nafasi. Akaanza kuchapisha makala zake mfululizo katika gazeti la "Safire Hind", Amritsar, dhidi ya Aria Samaj na ndani yake alimwita Swami Dayanand pia kwa kushindana naye. Kwa vile Bwana Swami Dayanand alikuwa anatembelea Rajisthan siku zile, kwa hiyo alimwambia Bakhtawar Singh na Munshi Indarman Muradabadi kwamba wakubali mwito wake, lakini ni masikitiko kwamba katika siku hizo hizo Bwana Swami alimfukuza Indarman Muradabadi katika Aria Samaj. Kwa hiyo, mjadala haukufanyika. (Hadhrat) Mirza Ghulam Ahmad alijifaidisha sana na tukio hili na akaandika vitabu vikali dhidi ya Waaria ambavyo vilitia chuki katika mioyo ya Waislam kuhusu dhehebu la Aria."[115]

KUSHINDWA KWA MWENDELEO WA BARHAMU SAMAJ

Mwendeleo wa pili wenye nguvu dhidi ya Islam ulikuwa Barhamu Samaj, lakini hilo nalo Hudhur[as] aliushambulia vikali hata kwamba ulikuwa hauna la kufanya. Kiongozi mmoja wa Barhamu Samaj anaandika:

---

[114] Tablighe Risalat, J. 1, uk. 6-7

[115] Aria Samaj aur Parchar ke Saadhna, uk. 12, cha pandit Devdat.

> "Mtu mmoja hodari, Raja Ram Mohan Rae, alianzisha Barhamu Samaj katika Uingereza na Marikani kama namna ya Kanisa la Unitarian, lakini ni masikitiko kwamba Jumuiya ya Ahmadiyya ilileta athari mbaya juu ya Waislamu wa India, na Waislamu wenye upendo waliojiunga na Barhamu Samaj kwa sababu ya desturi zake, karibu wote walirudi nyuma."[116]

Kiongozi mwingine wa Barhamu Samaj Bwana Devindar Naath Suhae anaandika:

> "Mwendeleo wa Barhamu Samaj ulizuka kama tufani kubwa, na haraka sana matawi yake yakaimarika sio katika India tu bali katika nchi za nje pia. Katika India sio Mabaniani na Masingasinga tu walioathirika, bali sehemu kubwa ya Waislamu pia walijiunga nao. Kila siku maishirini ya Waislamu walijiunga na Barhamu Samaj. Mwanzoni mwake inaonekana kwamba familia kubwa kubwa za Waislamu za Bangal sio waliafikiana tu bali walikuwa wanachama wake hasa. Lakini katika siku hizo hizo, Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, aliyekuwa mtaalamu mkubwa wa Waislamu, aliandika vitabu dhidi ya Mabaniani na Wakristo na aliwaita kwenye mjadala. Ni masikitiko kwamba mtaalamu yeyote wa Barhamu Samaj hakuutikia mwito huo. Athari yake ikawa kwamba Waislamu waliokuwa wameathirika na mafundisho ya Barhamu Samaj sio tu walirudi nyuma bali Waislamu waliojiunga na Barhamu Samaj hao pia waliacha pole pole."[117]

KUANDIKA NA KUCHAPISHA BARAHINE AHMADIYYA

Seyyidna Ahmad[as] alipoona kwamba kuandika makala na kuzichapisha magazetini dhidi ya madhehebu hayo maadui ya Islam hakuwezi kuleta faida ya kudumu, kwani magazeti hayawezi kutunzwa kwa muda mrefu. Kwa muda mfupi watu wanazungumzia makala hizo, kisha habari inasahaulika, basi yeye alianza kuandika kitabu cha kudumu kiitwacho "Barahine Ahmadiyya". Katika kitabu

[116] Hindutu, uk. 982, cha Ramdas Gorh (Tafsiri kutoka Kihindi)

[117] Gazeti "Komdi", la Calcatta, Aug. 1920 (Tafsiri kutoka Kihindi)

hicho aliandika hoja madhubuti za ukweli wa Kurani Tukufu na wa Mtume Mtukufu[saw] zilizoishangaza dunia.

Wa-Aria Samaj hawakuamini ufunuo wa Mungu baada ya ma-Veda, na Wa-Barhamu Samaj walikataa katakata ufunuo wenyewe na waliidhania akili tupu yatosha kwa kupata uokovu. Waislamu nao walioathirika na falsafa ya Kimagharibi wakiona maendeleo ya Ulaya walianza kuelekea kuukana Ufunuo wa Mungu. Maulamaa wa Kiislamu walikuwa wakitoa fatuwa za kukufurishana wao kwa wao kwa mambo madogo madogo, na Islam ilikuwa nyonge, isiyo na msaidizi. Baadhi ya watu walikuwa wakijiunga na Ukristo, na baadhi wakawa windo la Aria Samaj na Barhamu Samaj. Katika hali hizo akajitokeza mja mmoja shujaa wa Mungu kutoka kijiji kisichojulika cha Qadian na akaandika kitabu kisicho na kifani juu ya fadhila za Kurani Tukufu, ukweli wa Mtume[saw], haja ya wahyi na uhakika wake, ambacho upande mmoja kiliwafanya maadui wa Islam wasijue la kufanya, na upande wa pili Waislamu wa India walipata moyo. Sehemu ya kwanza ya kitabu hiki ilichapwa katika mwaka 1880. Katika sehemu hii aliwaita viongozi wa dini zote duniani kwenye mashindano na akasema kwamba kwa kuthibitisha ukweli wa Kurani Tukufu na wa Mtume Mtukufu[saw] hoja tulizoziandika kwa kutoa kutoka katika kitabu chetu kilichofunuliwa, kama yeyote asiyekuwa Mwislamu alete nusu au sehemu ya tatu au ya nne au ya tano kutoka katika kitabu chake cha ufunuo kwa kuthibitisha ukweli wa itikadi za dini yake, au akishindwa kuleta hoja, basi avunje hoja zetu kwa utaratibu, hapo bila kusita nitamkabidhi milki yangu yenye thamani ya rupia elfu kumi, lakini sharti hii itakuwa ya lazima kwamba kamati ya majaji watatu watakaokubaliwa watoe uamuzi kwamba jibu limeshaandikwa sawa na masharti.

Kwa kuitikia mwito huu baadhi ya wapinzani wa Islam walitangaza kwa harara kuwa wataandika jibu la kitabu hicho, hapo mara moja Hudhur akaandika kwamba:

> "Nawaapisha watu wote kwamba msisite hata kidogo kunikabili, muwe kama mwanafalsafa Plato wa Kigiriki, mgeuke kuwa mwanafalsafa Bacon, mlete mtazamo na fikira za

> Asristotle, waombe kwa unyenyekevu msaada kutoka kwa miungu wao wa bandia, kisha waone kwamba Mungu wetu Anashinda au miungu wenu wa bandia."[118]

Katika hali kama hii ilikuwa faradhi ya Wakristo, Wa-Aria Samaj na Wa-Barhamu Samaj kwamba wangechapisha kitabu chochote kwa kukijibu kitabu hiki, lakini Swami Dayanand pia, aliyeishi mpaka miaka mitatu baada ya kuchapwa kwa Barahine Ahmadiyya, akakaa kimya na Wa-Barhamu Samaj pia walinyamaza tu. Naam, mtu mmoja aitwaye pandit Lekhram wa Aria Samaj Peshawar alichapisha kitabu kimoja kiitwacho "Takdhiib Barahine Ahmadiyya"[119] ambaye baadaye alikufa alipomkabili Hudhur[as], akipiga muhuri kwa kudumu juu ya ushinde wa Aria Samaj. Watu ambao wamepata nafasi ya kuona maandishi ya Bwana Pandit huyo, wanajua vizuri kwamba katika maandishi yake hakuna kitu isipokuwa matukano na matusi na upuuzi. Kitabu hicho pia kama inavyodhihirika kwa jina lake kilikuwa mkusanyiko wa mambo yasiyo na maana, hata hivyo hakikuachwa bila kujibiwa. Mfuasi maarufu wa Seyyidna Ahmad[as], Hadhrat Maulana Nurud-Din[ra], ambaye baadaye akawa Khalifa wake wa kwanza, alichapisha jibu lake kwa jina la 'Tasdiik Barahine Ahmadiyya',[120] lipaswalo kusomwa. Minghairi ya huyo baadhi ya watu wengine pia wasiokuwa Waahmadiyya waliandika vitabu kuunga mkono Barahine Ahmadiyya na kupinga 'Takdhiib Barahine Ahmadiyya'.

MAONI JUU YA BARAHINE AHMADIYYA

Tumeshatangulia kuandika kwamba kwa kukiona kitabu hicho cha thamani kubwa, Waislamu walipata moyo na walikithamini sana kama neema isiyotazamiwa kujaliwa. Basi, baadhi ya dondoo kutoka katika maandishi ya baadhi ya wanachuoni Waislamu zinaandikwa hapa chini:

---

[118] Barahine Ahmadiyya, sehemu ya pili, ukurasa wa kwanza wenye jina la kitabu, upande wa ndani.

[119] Yaani, kukadhibisha Barahine Ahmadiyya.

[120] Yaani, kusadikisha Barahine Ahmadiyya.

1. RAI YA KIONGOZI MAARUFU WA AHLE HADITH, MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII

Kiongozi maarufu wa Ahle Hadith Abu Said Maulawii Muhammad Husain Batalawii aliandika:

> "Katika maoni yetu kitabu hiki katika zama hizi, na sawa na hali ya siku hizi, ni kitabu ambacho mfano wake mpaka leo haujaandikwa katika Islam na hatujui habari za baadaye. لَعَلَّ اللّٰهَ يُحْدِثُ بَعْدَ ذٰلِكَ اَمْرًا Na mwandishi wake pia amesimama imara kwa kuisaidia Islam kwa mali, uhai, kalamu, ulimi na kwa hali na kauli kiasi hiki kwamba mfano wake umepatikana kwa nadra katika Waislamu wa awali.
>
> "Kama mtu akifikiria maneno yetu kuwa ni kutia chumvi sawa na tabia ya ki-Asia, basi atuambie angalau kitabu kimoja tu ambamo madhehebu yote ya wapinzani wa Islam, hususan Aria na Barhamu Samaj, yamejadiliwa na kulinganishwa na Islam kwa jazba na harara, na atutajie watu wawili, watatu au wanne walio wasaidizi wa Islam ambao wakachukua jukumu la kuisaidia Islam kwa mali, uhai, kalamu, ulimi, na zaidi ya hayo kwa hali pia, na waliodai kiume kwa kusisitiza kukabiliana na wapinzani wa Islam na waukanao ufunuo kwamba anayekataa ufunuo aje kwetu akafanye tajriba na ashuhudie, na ambaye akawaonjesha pia wasiokuwa Waislamu ladha ya tajriba na ladha ya kushuhudia."[121]

2. MAONI YA SUFII AHMAD JAN WA LUDHIANA

Sufii mashuhuri na maarufu wa Ludhiana, Hadhrat Haji Ahmad Jan, ambaye wafuasi wake walikuwa wameenea katika sehemu za mbali sana, aliandika:

> "Mheshimiwa, mtoaji baraka kwa ulimwengu, mgodi wa ukarimu, hoja ya Islam, mteule baina ya wote, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, zidumu baraka zake, Chifu mkuu wa Qadian, Wilaya ya Gurdaspur Panjab, ameandika kitabu "Barahine

[121] Isha'atus Suna, J. 7, Na. 6, uk. 169-170

Ahmadiyya" katika lugha ya Kiurdu inayofahamika kwa urahisi ambacho ukubwa wake ni juzuu[122] mia tatu, majalada yake manne ya juzuu 35 yameshachapwa tayari kwa maandishi safi sana, na yaliyobaki yataendelea kuchapwa na kuwafikia wanunuzi.

"Kitabu hicho kinathibitisha kwa hoja mia tatu madhubuti za kiakili na za kimaandiko, ukweli wa dini ya Ki-Islamu, Unabii wa Muhammad[saw] na Kurani Tukufu, na kinabatilisha dini zote zilizo dhidi ya Islam, kama Ukristo, Aria, dini za wakanao uwepo wa Mungu, Ubaniani, Barhamu Samaj na nyinginezo kwa kuzichunguza. Mheshimiwa mwandishi ametangaza zawadi ya rupia elfu kumi kwamba kama mpinzani yeyote wa Islam au mkadhibishaji wa Islam akibatilisha hoja zote au nusu yake, hata sehemu yake ya tano, basi mwandishi atamhamishia huyo milki yake ya rupia elfu kumi... Katika zama hizi za karne ya kumi na nne kuna machafuko makubwa ndani ya kila dini. Asemavyo mtu fulani, wapo makafiri wapya na Waislamu wapya. Bila shaka ilisikika haja ya kitabu kimoja na mujadidi mmoja kama Barahine Ahmadiyya na mwandishi wake Bwana wetu Maulana Mirza Ghulam Ahmad ***Mungu Adumishe baraka zake,*** ambaye yupo kwa kuwathibitishia wapinzani madai ya Islam kwa namna zote... Umri wake mtukufu ni miaka arobaini au arobaini na mitano. Watani wa mababu zake unaonekana ni nchi ya Faris ya zamani. Yu mwenye hulka njema, mkarimu, mwenye haya, kijana mzuri, usoni yanaonekana mapenzi ya Mungu. Enyi wasomaji, naomba kwa nia safi na jazba ya kweli kwamba bila shaka Bwana Mirza huyo ni Mujadidi wa zama na ni jua kwa watafutao njia ya kumsogelea Mungu, ni Khidhri kwa wapotofu, upanga mkali kwa waikanao Islam na hoja kamili kwa mahasidi. Muwe na yakini kwamba wakati kama huu hautapatikana tena. Zingatieni kwamba wakati wa mtihani umeshawadia. Hoja ya Mungu imeshaimarika. Na kama mithili ya jua la kuangaza dunia nzima ametumwa mwongozi kamili

[122] Juzuu katika istilahi ya uchapaji wa zama zile ilimaanisha kurasa 16. Mwenezi

kwa hoja madhubuti ili awanurishe wakweli na awatoe kutoka katika giza na upotevu na akamilishe hoja dhidi ya waongo."[123]

Hadhrat Sufii Ahmad Jan ambaye maoni yake yameandikwa hapo juu, alikuwa sufii mkamilifu, maelfu ya watu wampendao walijiunga naye kwa kufanya baiati yake. Lakini alipoona "Barahine Ahmadiyya", basi kwa niaba ya wasomaji wa kitabu hicho akamwambia Seyyidna Ahmad[as]:

Sisi wagonjwa twakuangalia wewe tu,
uwe Masihi kwa ajili ya Allah.

Na alishika njia hii kwamba mtu yeyote akija kwake ili kujiunga naye, alikuwa akimwambia:

"Jua limeshatoka, sasa hakuna haja ya nyota. Nenda ukafanye baiati ya Seyyidna Ahmad[as]."[124]

Ni kauli mashuhuri kwamba yeye alimwomba Seyyidna Ahmad[as] kukubali baiati yake, lakini Hudhur[as] akasema kwamba sipo tayari kuchukua baiati maadamu Mwenyezi Mungu Hajaniamuru.

3. MAONI YA MAULAWII MUHAMMAD SHARIF BENGALORI

Maulana Muhammad Sharif alikuwa mhariri wa gazeti mashahuri la Kiislamu "Manshure Muhammadi" la Bengalore. Aliandika chini ya kichwa cha habari

جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوْقًا

"Nilitamani tangu muda mrefu kwamba mheshimiwa yeyote miongoni mwa wanazuoni wa Islam aliyejaliwa na Mungu uwezo wa kuisaidia na kuihami dini aandike kitabu kilinganacho na hali ya zama hizi, ambacho ndani yake ziwepo dalili za kiakili na hoja kutokana na maandiko, zenye kuthibitisha Kurani Tukufu kuwa Neno la Mungu na kuhakikisha Utume wa Mtume Mtukufu[saw]. Ni shukurani kwa Mungu kwamba

[123] "Ta'athurate Qadian", uk. 64-68, cha Malik Fadhl Husain.

[124] In'amate Khudawande Karim, cha Pir Iftikhar Ahmad.

matamanio hayo pia yametimia."[125]

Baada ya miezi kadha aliandika tena:

"Kusifu kitabu hicho ni nje ya uwezo, na hakika yenyewe ni kwamba jinsi ambavyo kwa utafiti mkubwa hoja ya Islam imetimilizwa juu ya wapinzani wa Islam katika kitabu hiki haihitaji sifa yoyote:

Uso wa mahabubu hauhitaji mrembeshaji.

"Lakini hatuwezi kujizuia kusema kwamba bila shaka kitabu hiki hakina kifani. Na jinsi hoja za kweli zilivyoelezwa kwa msisitizo na nguvu, na mwandishi — ajaliwe umri mrefu — amewadhihirishia wapinzani wa Islam kashfi na funuo zake pia, kama mtu ana shaka, basi ajipatie kashfi za Mungu na nuru zisizo na kikomo ambazo ni zawadi ya Mungu, kwa baraka ya kukaa na mwandishi na kupata jicho la yakini.

Kitabu hiki kisichoweza kujibiwa hakina kifani katika kuthibitisha ukweli wa Islam na kuhakikisha ukweli wa utume na Kurani... Haya ni madhumuni na hoja madhubuti ambazo kwa kuzijibu wapinzani wametamanishwa kupata rupia elfu kumi. Na muda mrefu umeshapisha tangu kutangazwa, lakini mpaka leo hakuna yeyote aliyepata uwezo wa kuandika."[126]

ZAMA ZA UCHAPAJI WA BAADHI YA SEHEMU ZA BARAHI-NE AHMADIYYA

Sehemu mbili za kwanza za Barahine Ahmadiyya zilichapwa mnamo mwaka 1880, sehemu ya tatu mwaka 1882 na ya nne mwaka 1884.

JUHUDI YAKE KWA KUENEZA BARAHINE AHMADIYYA

Kwa kupitia magazeti mashuhuri ya nchi, Barahine Ahmadiyya kilitambulika kote nchini, lakini Waislamu wengi matajiri hawakujali hata kwamba Seyyidna Ahmad[as] alilazimika kuwaandikia barua mfululizo ili wanunue kitabu hiki. Katika zama hizo, yeye alikuwa na

[125] Manshure Muhammadi Bengalore, 25 Rajabu 1300 Hijria.

[126] Manshure Muhammadi Bengalore, 5 Jumada II 1301 Hijria.

shughuli sana hata kwamba mwenyewe alikuwa akitayarisha kifurushi cha vitabu na mwenyewe akakiandikia anwani.

MWENDO WA AJABU WA NAWAB SIDDIK HASAN KHAN

Marehemu Nawab Siddik Hasan Khan alikuwa mwanachuoni maarufu wa kundi la Ahle Hadith, na kwa kumwoa mtawala wa Bhopal, Bi Nawab Shah Jahan Begam, umaarufu wake ukaongezeka. Alifanya juhudi kubwa katika kueneza vitabu vya dini. Kwa hiyo, Seyyidna Ahmad[as] akimfikiria kuwa yu Mwislamu mwenye uchungu wa moyo alimwelekeza kushiriki katika kueneza Barahine Ahmadiyya. Kwa kuhimizwa na Hadhrat Ahmad, yeye mwanzoni alionyesha mwelekeo wa kununua nakala 15, 20 hivi, lakini alipokumbushwa tena akakataa kabisa, kwa kisingizio cha kuihofia serikali ya Kiingereza, na paketi moja ya Barahine Ahmadiyya iliyokuwa imemfikia tayari akarudisha kwa kuichana. Mfuasi mmoja wa Hudhur, Hafidh Haamid Ali, anasimulia kwamba kitabu kiliporudishwa, wakati ule Seyyidna Ahmad[as] alikuwa anarauni nyumbani mwake. Alipokiona kitabu kimechanika na kimeharibiwa vibaya sana, uso wake ukabadilika ukawa mwekundu kwa ghadabu. Katika maisha yake yote hakuonekana katika hali ya hasira kiasi hiki. Kwa kuona uso wake, ilionekana kwamba amekasirika sana mno. Akaendelea kutembea huku na huku na alikuwa kimya, mara moja maneno haya yalitoka ulimini mwake: "Haya, wewe uridhishe serikali yako." Pia akaomba dua kwamba Bwana huyo avunjiwe heshima yake. Baadaye, Hudhur[as] alipoandika sehemu ya nne ya Barahine Ahmadiyya, humo pia aliandika akiashiria kwenye kitendo kibaya cha Bwana Nawab kilicho kinyume cha khulka njema kwamba:

> "Sisi pia hatumtegemei Bwana Nawab, bali tegemeo letu ni Mungu tu, naye ndiye Mtoshelezaji, (Mungu Aijalie serikali ya Kiingereza imridhie Bwana Nawab)"[127]

Miezi michache tu baada ya maandishi haya ya Seyyidna Ahmad[as], serikali ile ile ya Kiingereza, ambayo 'kwa kuipata radhi yake', Bwana Nawab alikataa kununua Barahine Ahmadiyya, ilifungua kesi ya

[127] Tatimma Hakikatul Wahyi, uk. 27

kisiasa dhidi yake na ikamvulia lakabu ya 'Nawab'. Kwa sababu hiyo yeye akawa na mahangaiko sana ─ Mungu Atupe amani na Atuhifadhi. Akajaribu kwa kila njia kujitoa katika matatizo hayo, lakini juhudi yoyote haikufanikiwa. Kuhusu habari hii Seyyidna Ahmad[as] anasema:

> "Jaribio lililompata Nawab Siddik Hasan Khan, hilo pia ni matokeo ya utabiri wangu ulioandikwa katika Barahine Ahmadiyya. Yeye alirudisha kitabu changu akikichana. Mimi nilimwombea kwamba avunjiwe heshima yake, na ndivyo ilivyodhihirika."[128]

Bwana Nawab alipohisi kosa lake, akamwomba Seyyidna Ahmad[as] kwa unyenyekevu sana katika barua yake kwamba aombewe dua. Hudhur[as] anasema:

> "Ndipo nilimwombea kwa kufikiria kuwa anastahili kuhurumiwa, basi Mwenyezi Mungu Akaniambia, "Heshima yake imelindwa na kupondwa kichwa." Hatimaye, baada ya muda fulani kuhusuye hukumu ya serikali ikaja kwamba "Lakabu 'Nawab' ya Siddik Hasan Khan ibaki."[129]

KUAHIRISHWA KWA BARAHINE AHMADIYYA

Sehemu ya nne ya Barahine Ahmadiyya ilichapwa mnamo mwaka 1884. Mwishoni mwa sehemu hiyo alitangaza kwamba:

> "Mwanzoni kilipoandikwa kitabu hiki, wakati huo hali yake ilikuwa tofauti. Kisha baadaye, ghafula Mwenyezi Mungu Alinipasha mimi mtumishi wake mnyenyekevu habari kama Musa kuhusu ulimwengu ambao sikuwa na habari yake hapo kabla. Yaani, mimi pia kama Hadhrat Ibni Imran nilikuwa nikisafiri katika usiku wenye giza wa fikara zangu, mara kutoka ghaibu ikatokea sauti ya إِنِّيْ أَنَا رَبُّكَ na siri zile zikadhihirika ambazo akili na fikara ilikuwa haikuzifikia. Sasa mdhamini na msimamizi wa kidhahiri na kibatini wa kitabu hiki ni Mola wa

[128] Tatimma Hakikatul Wahyi, uk. 27

[129] Tatimma Hakikatul Wahyi, uk. 27

walimwengu.”[130]

Basi, baada ya madai ya kuwa Mujadidi na kutumwa na Mungu, kuchapwa kwa sehemu nyinginezo za Barahine Ahmadiyya kuliahirishwa sawa na matakwa ya Mungu. Hatimaye, mnamo mwaka 1905 sehemu yake ya tano na ya mwisho ilichapwa ambayo ingawa haikufululiza mada ya zamani, lakini katika muda huo mrefu bishara zilizoandikwa katika sehemu nne za awali za Barahine Ahmadiyya ambazo ziliishatimia tayari, Hudhur[as] akizitaja akaiunganisha sehemu hii na sehemu za awali.

UFUNUO WA KWANZA KUHUSU KUWA MUJADIDI NA KU-TUMWA KWAKE

Kwa sababu ya kutaja mahali pamoja sehemu zote nne za Barahine Ahmadiyya tuliacha kutaja matukio ya katikati, kwa hiyo sasa hayo yanatajwa:

Hili ni tukio la mwaka 1882. Hudhur[as] anasema:

> “Safari moja nilifunuliwa ufunuo uliomaanisha kwamba waliopo mbinguni wanajadiliana, yaani azma ya Mungu kuhuisha dini imetaharuki, lakini wakazi wa mbinguni hawajabainikiwa bado mhuishaji”[131]

Anasema kwenye ukurasa ujao:

> “Katika hali hiyo niliona katika ruya kwamba watu wanamtafuta mhuishaji mmoja, na mtu mmoja akaja mbele yangu na kwa kuashiria akasema:
>
> هٰذَا رَجُلٌ يُّحِبُّ رَسُوْلَ اللّٰهِ
>
> Yaani, huyu ndiye mtu anayempenda Mtume[saw] wa Allah. Na kauli hii ilimaanisha kwamba sharti kuu la cheo hiki ni mapenzi ya Mtume[saw], nalo lathibitika katika mtu huyu.”[132]

---

[130] “Sisi na kitabu chetu”, Barahine Ahmadiyya, sehemu ya nne ukurasa wa mwisho.

[131] Barahine Ahmadiyya, sehemu ya nne, uk. 502

[132] Barahine Ahmadiyya, sehemu ya nne, uk. 503

Katika siku hizo hizo Hudhur[as] aliona ruya moja. Anasema:

> "Usiku mmoja nilikuwa nikiandika, katika hali hiyo nilipata usingizi na nikalala. Wakati ule nilimwona Mtume Mtukufu[saw], uso wake ulikuwa unang'ara kama mwezi mpevu. Akanikaribia, nami nikahisi kwamba anataka kunikumbatia. Basi akanikumbatia na nikaona kwamba kutoka uso wake mionzi ya nuru imedhihirika na ikaingia ndani mwangu. Nikaona nuru hizi kama mwangaza kidhahiri na nikafahamu kwa yakini kwamba siioni kwa macho ya kiroho tu bali naona kwa macho ya kidhahiri pia. Na baada ya kukumbatiana huku sikuhisi kwamba ameniacha wala sikufahamu kwamba ameondoka. Baada yake nilifunguliwa milango ya funuo za Mungu. Na Mungu wangu Akaniambia:
>
> يَا اَحْمَدُ بَارَكَ اللّٰهُ فِيْكَ۔ مَا رَمَيْتَ اِذْ رَمَيْتَ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ رَمٰى۔ اَلرَّحْمٰنُ عَلَّمَ الْقُرْاٰنَ۔
>
> لِتُنْذِرَ قَوْمًا مَّا اُنْذِرَ اٰبَاءُهُمْ وَلِتَسْتَبِيْنَ سَبِيْلَ الْمُجْرِمِيْنَ۔ قُلْ اِنِّيْٓ اُمِرْتُ وَاَنَا اَوَّلُ الْمُؤْمِنِيْنَ[133]
>
> Yaani, Ee Ahmad! Mungu Amekubariki. Basi ulipowashambulia wapinzani kwa kutumikia dini, hukuwashambulia wewe, bali ni Mungu Aliyewashambulia. Mungu Amekupa elimu ya Kurani Tukufu ili uwaonye watu ambao mababu zao hawakuonywa na ili njia ya wahalifu ibainike. Waambie watu kwamba nimetumwa na Mungu na mimi ni wa kwanza kuamini."

Kwa funuo na ruya za juu, inabainika wazi kwamba sharti kuu kwa mtu atakayetumwa ni kwamba yeye awe anampenda Mtume Mtukufu[saw] kiasi hiki kwamba mfano wake usiweze kupatikana duniani kote. Na sharti hili lilipopatikana ndani ya Hudhur, basi akachaguliwa. *Allahumma salli alaa Muhammadin wa aali Muhammad[saw].*

Huo ulikuwa ni ufunuo wa kwanza aliofunuliwa kuhusu kutumwa kwake, lakini kwa vile mpaka wakati ule alikuwa hakuamrishwa kupokea baiati, kwa hiyo hakutangaza kuchukua baiati wala hakuweka

[133] Barahine Ahmadiyya, sehemu ya 3, uk. 238, maelezo ya pembeni ya maelezo ya pembeni Na. 1.

msingi wa Jumuiya bali aliendelea kuitumikia Islam kikawaida.

Katika zama hizo hizo alipata baadhi za funuo zilizodhihirisha kwamba wakati ni karibu kuwadia ambapo watu wengi sana watakufikia Qadian kwa kupata baraka zako. Angalia, usipate kuhangaika kwa kifikiwa na watu kwa wingi wajao kwa kuonana nawe.[134] Ilmuradi, pindi alipoanza kuteremshiwa funuo kwa kupashwa habari za ghaibu safi, yeye akaendelea kuzidi katika mapenzi ya Mtume Mtukufu[saw]; kwani alikwishaelewa vizuri hakika hii kwamba anashukiwa nuru hizi za kimbingu kwa kumfuasa Mtume Mtukufu[saw] na baraka zake. Kwa hiyo, alianza kumsalia sana Nabii s.a.w. aliyekuwa amemfuata hata kwamba mnamo mwaka 1883 alidhihirishiwa kwamba yeye na Hadhrat Isa[as] wameumbwa kutoka katika asili moja tu, na nyinyi wawili ni kama kitu kimoja.[135]

Katika siku hizo hizo alihimizwa kumsalia Mtume[saw] na akafunuliwa ufunuo huu:

صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ سَيِّدِ وُلْدِ اٰدَمَ وَخَاتَمِ النَّبِيِّيْنَ[136]

Yaani, Mtume Mtukufu[saw] aliye Seyyidi wa wana wa Adamu na Khatamun Nabiyyina, umsalie yeye na ali zake. Basi, yeye akaanza kumsalia Mtume[saw] kwa wingi kiasi hiki kwamba anasema:

> "Hapa nimekumbuka kwamba usiku fulani nilimsalia Mtume[saw] kwa wingi kiasi hiki kwamba moyo na roho vikanukia kwayo. Usiku huo huo niliona katika ruya kwamba Malaika wanaleta viriba vya nuru kwa sura ya maji safi nyumbani mwangu, na miongoni mwao mmoja akasema, hizi ni baraka zile ulizompelekea Muhammad, baraka za Mungu zimwie yeye."[137]

Katika zama hizo alifunuliwa ufunuo huu pia:

قُلْ اِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّوْنَ اللّٰهَ فَاتَّبِعُوْنِيْ يُحْبِبْكُمُ اللّٰهُ

[134] Tafsiri kutoka katika Barahine Ahmadiyya, sehemu ya 3, uk 242.

[135] Tafsiri kutoka katika Hamamatul Bushra, uk. 42.

[136] Barahine Ahmadiyya, sehemu ya 4, uk. 502-503

[137] Barahine Ahmadiyya, sehemu ya 4, uk. 502.

Yaani, uwaambie watu, ikiwa nyinyi mwataka kumpenda Allah, basi njia yake ni moja tu, nayo ni kwamba nifuateni mimi.

Sub'hanallah; Ni hisani ya ajabu ilioje ya Mungu kwamba Anamwamuru yeye kuwa ikiwa unataka kupata daraja za juu mbele yangu, basi msalie Mtume Mtukufu[saw] sana sana na Anawaamuru watu wa zama zake kwamba katika zama hizi ikiwa mwataka kunipenda, basi mfuateni mtu huyu.

سُبْحَانَ اللّٰهِ وَبِحَمْدِهٖ سُبْحَانَ اللّٰهِ الْعَظِيْمِ ۔ اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَّاٰلِ مُحَمَّدٍ

KIFO CHA BWANA MIRZA GHULAM QADIR, MWAKA 1883

Kaka yake Hudhur, Bwana Mirza Ghulam Qadir, aliugua sana mnamo mwaka 1868 pia, na Mwenyezi Mungu Akamwambia Hudhur ndotoni kwamba mzee wake mmoja marehemu anamwita. Kwa vile uaguzi wa ndoto hii huwa kifo, kwa hiyo akahuzunika sana. Akamwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu sana Ampatie kaka yake afya. Baada ya siku chache alimwona ndotoni kwamba anatembea nyumbani bila kuegemea kitu kama mtu mwenye siha kamili. Basi, Mwenyezi Mungu Akamponya. *Alhamdulillahi.*

Miaka kumi na mitano baada ya tukio hilo, katika mwaka 1883, wakati Hudhur[as] alipokuwa amekaa Amritsar kwa shughuli fulani, alionyeshwa katika ruya kwamba sasa siku za kaka yake zimekwisha na karibuni sana atakufa. Yeye akamwambia Hakim Muhammad Sharif ruya yake huko huko Amritsar, na akamwarifu ndugu yake pia kwa barua kwamba uelekee kwa mambo ya akhera, kwani nimeonyeshwa siku za maisha yako zimebaki kidogo. Bwana Mirza Ghulam Qadir aliwambia watu wote wa nyumbani kuhusu ndoto hiyo. Kisha katika wiki chache tu aliaga dunia.[138] Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.

UFAULU WA BWANA MIRZA SULTAN AHMAD KATIKA MTIHANI WA 'AFISA MAPATO'

Mwanaye mkubwa, Bwana Mirza Sultan Ahmad, alifanya mtihani wa 'Afisa mapato' katika mwaka 1884. Yeye akamwandikia baba barua ili

[138] Tiryakul Kuluub, uk. 39

kuombewa afaulu katika mtihani. Hudhur[as] anasema:

> "Kwa kusoma barua hiyo, badala ya kumhurumia nikakasirika kwamba mtu huyu anahangaikia mambo ya dunia. Basi niliposoma tu barua ile niliichana kwa chuki na karaha, na nikasema moyoni kwamba nimwombeje Mola wangu makusudio ya dunia. Nilipochana tu barua ile nikafunuliwa: 'Atafaulu'. Ufunuo huu wa ajabu pia watu wengi waliambiwa, na kijana yule akafaulu. *Alhamdulillahi*"[139]

HARUSI YAKE YA PILI

Alikuwa akifunuliwa kuhusu harusi yake ya pili tangu mwaka 1881, lakini ikafanyika katika mwaka 1884. Katika mwaka 1881, alipata ufunuo:

اِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلَامٍ حَسِيْنٍ[140]

Yaani, Twakupa habari njema ya mvulana mzuri.

Katika siku hizo hizo alifunuliwa ufunuo huu wa pili:

اُشْكُرْ نِعْمَتِيْ رَاَيْتَ خَدِيْجَتِيْ[141]

Yaani, unishukuru, umepata Hadija wangu.

Kadhalika alifunuliwa ufunuo huu:

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ جَعَلَ لَكُمُ الصِّهْرَ وَالنَّسَبَ[142]

Yaani, sifa zote njema zinamhusu Mungu Ambaye alikufanyia ujamaa wa ndoa wa waungwana na kufanya ukoo wako pia wa waungwana.

Kadhalika, safari moja alipata ufunuo huu:

"Nimenuia nipange harusi yako ya pili. Mahitaji yote Nitatimiza Mimi, na hutapata shida yoyote."

---

[139] Al Hakam, J. 3, Na. 34 la tarehe 23 Septemba 1899.

[140] Tiryakul Kuluub, uk. 34

[141] Nuzuulul Masihi, uk.146-147

[142] Tiryakul Kuluub, uk. 64

Ndani ya funuo hizo kuna maneno haya pia ya Kiajemi:

ہر چہ باید نو عروسے راہماں ساماں کنم و آنچہ مطلوبِ شما باشد عطائے آن کنم[143]

Yaani, vyote vinavyopaswa kuwepo kwa Bi harusi, Mimi Nitavitoa hivyo, na Nitakutimizia mahitaji yako yote.

Hudhur[as] anasema:

> "Bishara hii imeelezwa katika funuo zingine kwa uwazi zaidi hata kwamba jina la mji likatajwa ambao ni Delhi, na bishara hii wakaambiwa watu wengi. Na kama ilivyoandikwa ndivyo ilivyodhihirika, kwani bila mahusiano ya karibu na ujamaa nilioa katika ukoo maarufu wa waungwana wa Masharifu wa Delhi… Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Aliahidi kwamba kutoka katika ukoo wangu Ataweka msingi mkubwa wa kuhami Islam na Ataumba miongoni mwao mtu ambaye atakuwa na roho ya kimbingu ndani yake, kwa hiyo, Alipenda kwamba Aniozeshe binti wa familia ile na kutoka kwake Anipatie watoto ambao waeneze sana duniani nuru zile ambazo mbegu zake zimepandwa kwa mkono wangu. Na hii ni bahati njema ya ajabu kwamba kama bibi ya ukoo wa Masharifu alivyoitwa jina Shehr Bano,[144] ndivyo ambavyo mke wangu huu atakayekuwa katika siku zijazo mama wa ukoo huu, jina lake ni Nusrat Jahan Begam[145]. Hii ikiwa fali njema inaashiria kwenye jambo hili kwamba Mungu kwa kuisaidia dunia nzima Ameweka msingi wa ukoo wangu ujao. Hii ni suna ya Mwenyezi Mungu kwamba baadhi ya wakati ndani ya majina pia bishara yake inafichika."[146]

Maelezo ya tukio lililotajwa juu ni haya kwamba Hadhrat Mir Nasir Nawab[ra] alikuwa mtu wa familia maarufu ya Masharifu wa Delhi. Upande wa kuumeni alihusiana na mheshimiwa Amirul Umaraa,

[143] Shihnae Hak, uk. 57-58

[144] Shehr Bano: Tafsiri yake, mama mwungawana wa mji.

[145] Nusrat Jahan Begum: Tafsiri yake, mama mwungwana aliye msaada kwa dunia nzima.

[146] Tiryakul Kuluub, uk. 64-65

Samsamud Daula, Nawab Khan, Dauran Khana Bahadur,[147] Mir Bakhshi Mansur Jang, Amiri jeshi Mkuu wa Jeshi la Kimughali, na upande wa kuukeni alihusiana na Hadhrat Khwaja Mir Dard[rh] ambaye ukoo wake ni maarufu katika India nzima kwa uchamungu na utawa. Yeye alikuwa anakaa katika Panjab kikazi katika Wilaya ya Gurdaspur, karibu na Qadian, bali hasa katika Qadian pia alipata nafasi ya kukaa nyumbani mwa Hudhur[as] kwa muda. Na alikuwa anafahamu vizuri utawa na uchamungu wa Hudhur[as]. Kwa kupata mahamisho akakaa huko na huko. Alipofika Multan katika mwaka 1884, alihitaji mposa kwa binti yake Hadhrat Nusrat Jahan Begam. Kwa kumtafuta akarejea kwao Delhi likizoni. Aliomba sana kwa kumpata mkwe mwema. Akamwandikia Hudhur[as] pia kwa kuomba dua. Hudhur[as] mwenyewe alikuwa na haja ya kuoa. Hadhrat Mir Nasir Nawab anaeleza kwamba:

> "Kwa kunijibu Bwana Hadhrat Mirza aliniandikia kwamba sina mahusiano na mke wangu (wa kwanza) nami nataka kumwoa mwingine. Mwenyezi Mungu Amenifunulia ufunuo kwamba kama ukoo wako ulivyo bora ndivyo nitakavyokupa mke kutoka kwa ukoo bora wa Masharifu. Na ndani mwa ndoa hii mtakuwa na baraka, nami nitatoa vifaa vyake vyote, hutapata shida yoyote. Huu ni muhtasari wa barua yake. Na akaandika pia kwamba uniozeshe binti yako kwa kunifanyia dhana njema, na mpaka uamuzi wa mwisho, liweke jambo hili katika siri, na usiharakie kukataa"[148]

Hadhrat Bwana Mir anasema:

> "Kwanza nilisita, kwani umri wa Bwana Mirza ulikuwa mkubwa kidogo na alikuwa na mke na watoto, tena hakutokana na kaumu yetu. Lakini, tena kwa kuona uchamungu na wema wa Hadhrat Bwana Mirza niliotaka kwa moyo, niliamua moyoni mwangu kwamba nimwozeshe mtu huyu huyu mwema binti yangu mwenye bahati njema. Pia nilikuwa siwapendi watu wa

[147] Hizi ni lakabu za mzee huyo.

[148] Hayate Nasir, uk. 7

Delhi na tabia na desturi za huku."[149]

Mke wake aliyejulikana kwa Nani Amman — Nyanya — alikuwa na kizingiti hiki kwamba:

"Kwanza moyo haukukubali; pili, kulikuwa na tofauti kubwa ya umri; ya tatu, watu wa Delhi walikuwa wanawachukia sana Wapanjabi."[150]

'Nani Amman' mwenyewe anaeleza:

"Hudhur[as] alipomwandikia Hadhrat Bwana Mir, yeye Bwana Mir hakuniambia akihofia kwamba nitaona vibaya. Katika muda huo maombi kadha ya kuposa kutoka sehemu nyingi pia yaliletwa, lakini sikupata utulivu… Hatimaye, siku moja Bwana Mir alinitajia mkazi mmoja wa Ludhiana kwamba yeye ameleta ombi kwa kusisitiza sana, na yu mtu mwema, mwozeshe binti. Niliuliza ukoo wake na kadha wa kadha, na sikutulia, nikakataa. Hapo Bwana Mir alikasirika kidogo na akasema binti ameshakuwa wa miaka 18, je, atakaa hivi hivi maisha yote. Nikajibu, "Kuliko watu hao, Ghulam Ahmad ni mbora mara elfu." Haraka sana, Bwana Mir akatoa barua moja, akaiweka mbele yangu, kasema barua ya Mirza Ghulam Ahmad pia imeishawasili. Kwa vyovyote, twapaswa sasa kuamua haraka. Nikasema, "Haya, mwandikie, basi, Ghulam Ahmad."[151]

"Hapo, Bwana Mir wakati uo huo akamwandikia barua ya kibali. Siku nane baada ya kuwasili barua ya Bwana Mir, Hudhur[as] alifika Delhi pamoja na hadimu wake Hadhrat Hafiz Haamid Ali, Lala Malawa Mal na mtu mmoja au wawili wengine. Watu wa ukoo wa Hadhrat Mir walipojua, walikasirika sana kwamba binti ameolewa na mzee, tena Mpanjabi. Hudhur[as] hakuenda na mapambo ya dhahabu wala nguo, isipokuwa Rupia 250 taslimu. Hapo pia jamaa walitania kwamba ni nikaha gani

[149] Hayate Nasir, uk. 7-8

[150] Hayate Ahmad, J. 2 na. 3, uk. 77

[151] Siratul Mahdi, sehemu ya 2, uk. 110-111

hii bila mapambo wala nguo."[152]

Ilmuradi, tarehe 17 Novemba 1884, katika msikiti wa Khwaja Mir Dard[rh], Maulawii Seyyid Nazir Husain wa Delhi alitangaza baina ya sala za Magharibi na Isha ndoa hii yenye baraka kwa mahari ya Rupia elfu moja na mia moja. Jamaa wa Hadhrat Mir walikasirika sana lakini hawakuweza kufanya chochote. Hadhrat Mir alimsindikiza binti yake huko huko Delhi aende na mumewe. Kesho yake Hudhur[as] alianza safari yake ya kuelekea Qadian na hivyo harusi hiyo takatifu ikafanyika. *Alhamdulillahi*.

ISHARA YA VITONE VYEKUNDU, 10 JULAI 1885

Mnamo tarehe 10 Julai 1885, ishara ya ajabu ilidhihirika inayoitwa ishara ya vitone vyekundu. Maelezo yake ni haya kwamba tarehe 27 ya mwezi mtukufu wa Ramadhani, siku ya Ijumaa, baada ya sala ya alfajiri, Hudhur akaenda katika chumba kilichoungana na Masjid Mubarak upande wake wa mashariki na akalala kitandani kwa kupumzika kidogo kama kawaida. Hadhrat Maulawii Abdullah Sanauri[ra] anasimulia:

> "Mimi, wakati huo, nilianza kukanda miguu ya Hudhur[as] mpaka jua likachomoza na chumbani mkawa na mwanga. Hudhur[as] alikuwa amelala ubavuni wakati huo na kuweka mkono wake usoni. Wakati huo nikafikiri kwa ladha na furaha kwamba nzuri ilioje bahati yangu! Mungu subhanahu wa taala Amenijalia fursa nzuri, ni mwezi mtukufu wa Ramadhani na tarehe pia iliyo 27 ni yenye baraka, na kumi la mwisho la Ramadhani nalo ni lenye baraka, na siku pia ni ya Ijumaa iliyo yenye baraka sana, na mtu niliyekaa naye pia ni mwenye baraka sana. Allahu Akbar! Baraka nyingi zimejumuika kwangu. Kama saa hizi Mungu Akinionyesha ishara yoyote kumhusu Hudhur[as], sio mbali na uwezekano! Nilikuwa katika furaha hii nikikanda miguu yake karibu na kifundo cha mguu, mara nikahisi mwili wa Hudhur umetetemeka kidogo, na papo hapo yeye akainua mkono wake kutoka usoni na akanitazama. Wakati huo macho yake yalikuwa

[152] Hayate Ahmad, J. 2, Na. 3, uk. 96

yamejaa machozi, labda yalitiririka pia, kisha akaweka tena mkono usoni na akaendelea kulala.

"Nilipoona kifundo chake, huko nikaona kitone kimoja chekundu kilichotungamana, wala hakijaenea. Nilipoweka ncha ya kidole changu cha shahada juu ya kitone kile, kikapanuka na wekundu ule ukakipata kidole changu pia. Wakati huo nikashangaa, na moyoni mwangu ikapitia aya hii: صِبْغَةَ اللّٰهِ وَمَنْ اَحْسَنُ مِنَ اللّٰهِ صِبْغَةً[153]. Ikapita pia moyoni kwamba ikiwa hii ni rangi ya Mungu, labda itanukia pia. Basi, nikakinusa kidole changu, lakini hakikuwa na harufu yoyote. Kisha, nikaanza kukanda mgongo wake, hapo nikaona juu ya shati lake madoa machache mabichi mekundu. Nikashangaa sana, nikainuka na kuchunguza kila sehemu ya chumba, lakini sikuona alama yoyote ya wekundu ndani ya chumba. Hatimaye, nikakaa nikishangaa na nikaendelea kukanda miguu. Hudhur[as] aliendelea kulala akiweka mkono usoni. Baada ya muda kidogo Hudhur[as] alikaa. Kisha akaja katika Masjid Mubarak na kaketi. Mimi nilianza kukanda mgongo wake.

"Wakati ule nilimwuliza Hudhur[as] kuwa wekundu huo umeanguka kutoka wapi? Kwanza alikwepa, na nilipong'ang'nia, basi alinihadithiia tukio lote aliloishaeleza katika vitabu vyake.[154] Lakini kabla alikuwa hajaeleza alinifahamisha vizuri swala la kumwona Mungu na kugeuka mambo ya kikashfi kwa sura ya kiwiliwili kwa kunielezea mambo yaliyotukia katika maisha ya Hadhrat Muhyiddin Ibni Arabi kwamba katika dunia hii wakamilifu wanaonyeshwa kidhahiri baadhi ya sifa za Mungu za kijalali na kijamali. Kisha Hudhur[as] aliniuliza, je kitone kimeziangukia nguo zako pia? Mimi kwa kuzitazama nguo zangu nikasema, Hudhur! Hakikuniangukia kitone chochote. Akasema itazame kofia yako (iliyokuwa nyeupe ya melimeli). Nikavua kofia, nikaona juu yake pia kitone kimoja. Wakati huo

[153] Rangi ya Allah, na ni nani aliye mzuri kwa rangi kuliko Allah? (Sura Al-Baqara 2:139)

[154] Tazameni 'Surma Chashme Aria', uk. 131-132 na kadhalika.

> nilifurahika sana kwamba nimeangukiwa pia kitone kimoja cha wino wa Mungu. Nilichukua kutoka kwa Hudhur kwa kung'ang'nia shati lile lilioangukiwa rangi nyekundu kwa kupata baraka, kwa kuahidi kwamba nitafanya wasia kuzika shati lile pamoja na sanda yangu. Hudhur[as] kwanza alikataa kunipa, kwani baada ya mimi na yeye kufariki ushirikina utaenea na watu watalizuru na wataliabdu. Ilmuradi, baada ya mahojiano akanipa hilo lililopo kwangu mpaka wakati huu na alama za wekundu bado zipo bila kufifia au kuharibika.[155]

Mimi mwandishi nasema kwamba Hadhrat Mian Adullah Sanauri[ra] alifariki tarehe 7 Oktoba 1927. Maiti yake ilipooshwa, shati hilo alivalishwa sawa na wasia wake. Mimi ni miongoni mwa watu wale wenye bahati nzuri waliopata bahati ya kuona shati lile. ***Alhamdulillahi alaa dhalika***.

MWITO KWA KUONYESHA ISHARA, NA TANGAZO LA KUWA MUJADIDI NA KUTUMWA

Mwanzoni mwa mwaka 1885, aliwakaribisha viongozi na wakuu wa dini mbalimbali ili waone baraka na ishara mpya mpya za Islam. Kwa lengo hili alichapisha kipeperushi pia kuhusu madai yake katika lugha mbili za Kiingereza na Kiurdu, ambayo sehemu yake muhimu ni hii:

> "Mwandishi amearifiwa kwamba yu Mujadidi wa zama hizi, na sifa zake kwa kiroho zinafanana na sifa za Masihi mwana wa Mariamu, na kila mmoja anafanana na kulandana sana na mwenzake, naye amejaliwa ubora sawa na sifa za manabii na mitume juu ya mawilii wengi wakubwa waliopita kabla yake kwa baraka ya kumtii Mbora wa watu wote na mbora wa Mitume wote s.a.w., na kufuata nyayo zake inasababisha kupata wokovu, wema na baraka; na kwenda kinyume chake kunasabaisha kutupwa mbali na kukataliwa"[156]

Nakala 20,000 za kipeperushi hiki zlilichapishwa na zikatumwa duniani kote kwa Wafalme, Mawaziri na viongozi wa dini na

[155] Al-Fadhl, tarehe 26 Desemba 1916.

[156] Surma Chashme Aria, Shihnae Haq, Aina Kamalate Islam, Barakatud Dua.

wakakaribishwa kwamba kama wakiwa na shaka yoyote kuhusu ukweli wa Islam au ukweli wa Mtume Mtukufu[saw] au kama kuna shutuma yoyote dhidi ya Ufunuo au uwepo wa Mungu au ipo dukuduku yoyote moyoni kuhusu ubora wa Kurani Tukufu basi wakija kwake au kwa kuandikiana naye wapate kuridhika. Pamoja na tangazo hili alichapisha barua moja pia ikiwa na kichwa cha maneno "Tangazo la Mwito", ambamo walikaribishwa viongozi wa dini mbalimbali wa India na Panjab, na akaandika ndani yake:

> "Kama mkija na msishuhudie ishara yoyote ya Kimbingu kwa kukaa mwaka mmoja, basi mtapewa Rupia 200 kwa kila mwezi kama fidia au faini."[157]

Hudhur[as] anasema:

> "Ingawa tuliwaandikia mapadri na Waaria wa India na Panjab habari hii kwa njia ya barua ya rejista, lakini hakuna yeyote aliyekuja Qadian, bali Munshi Indarman alitumiwa Rupia 2400 taslimu huko Lahore, lakini akihepa alikimbilia Farid Kot. Naam, Bwana mmoja aitwaye Lekhram wa Peshawar kweli alifika Qadian, na akaambiwa mara kwa mara kwamba achukue kutoka kwangu sawa na cheo chake, bali mara mbili kuliko mshahara wake anaopata kazini Peshawar kila mwezi na akae hapa mwaka mmoja. Pia akaambiwa kwamba kama hawezi kukubali kukaa mwaka mzima, basi akae kwa siku arobaini tu, lakini hakukubali njia yoyote kati ya njia hizi mbili."[158]

UTABIRI KUHUSU AHALI NA WATOTO WA BINAMU ZAKE, 5 AGOSTI 1885

Kwa sababu ya binamu zake, Mirza Imamud Din na Nidhamud Din, kuomba na kukazania kuwa waonyeshwe ishara yoyote, Hudhur[as] alitabiri tarehe 5 Agosti 1885 kwamba:

> "Nimefunuliwa kuhusu Mirza Imamud Din na Nidhamud Din kwamba watapata msiba mkubwa katika muda wa miezi 31,

[157] Tablighe Risalat, J. 1, uk. 12, na Hayate Ahmad, J. 2 Na. 3, uk. 116

[158] Ishtihaar Sadakate Anwaar, Tablighe Risalat, J. 1, uk. 77

yaani mwanaume au mwanamke fulani wa familia yao atafariki na kwa hiyo wataudhika na kufarakana. Hiyo itatokea kuanzia tarehe ya leo, 23 Saawan 1942 Bikrami, sawa na 5 Agosti".

Kwenye utabiri huu, Mabaniani wafuatao walitia saini kama mashahidi: Pandit Bharamal mkazi wa Qadian, Pandit Bejnath, Bishandas Brahman, Bishandas Khatri.

Na ndivyo ilivyotokea pia, yaani katikati ya mwezi wa 31 kabisa binti wa Mirza Nidhamud Din, yaani mpwa wa kike wa Mirza Imamud Din, alifariki katika umri wa miaka 15 akiacha nyuma mtoto mchanga.[159]

ISHARA YA VIMONDO

Usiku ulio baina ya 27, 28 Novemba 1885, Mwenyezi Mungu Alionyesha angani ishara isiyo ya kawaida ya vimondo kwa kumsaidia. Hudhur Anasema:

"Usiku wa 28 Novemba 1885, yaani usiku wa kuamkia 28 Novemba 1885, kulikuwa na tamasha kubwa huko angani ambalo sijaona kifani chake katika umri wangu wote. Huko angani zilikuwa zinapitapita ndimi za moto maelfu kwa maelfu ambazo mfano wake haupo duniani ili niweze kufafanua. Nakumbuka, wakati huo nilifunuliwa ufunuo huu kwa wingi sana:

وَمَا رَمَيْتَ اِذْ رَمَيْتَ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ رَمٰى[160]

Na hiyo ilifanana sana na kuvurumizika vimondo.

Tukio hilo la vimondo lililotokea katika eneo kubwa sana usiku wa kuamkia 28 Novemba 1885 hata kwamba lilichapishwa kwa mshangao katika magazeti yote ya Ulaya, Merekani na Asia. Pengine watu wakadhani kwamba hilo lilikuwa bure, lakini Mwenyezi Mungu Anajua kwamba mwenye kuona tamasha hilo

[159] Ishtihar 20 Machi 1885 iliyoandikwa katika Tablighe Risalat, J.1 uk.102

[160] Yaani, hukutupa wewe ulipotupa, walakini Allah ndiye Aliyetupa. Hakikatul Wahyi, uk. 70

kwa makini kuliko wote na mwenye kupata ladha yake nilikuwa mimi tu. Macho yangu yaliendelea kutazama tamasha hilo kwa muda mrefu na tamasha lile la kuvurumizika vimondo lilianzia saa za magharibi ambalo niliendelea kulitazama kwa furaha sana kwa sababu ya bishara za kimbingu, kwani moyoni mwangu mlitiliwa kwa ufunuo kwamba ishara hii imedhihiri kwa ajili yako, kwani katika maandiko ya kiufunuo hii ilihesabiwa kuwa alama kubwa ya kudhihiri kwa Masihi.

ISHARA YA KUTOKEZA KWA NYOTA

Kisha baada yake watu wa Ulaya waliona nyota ile iliyotokeza wakati wa kudhihiri kwa Hadhrat Masihi. Ilitiliwa moyoni mwangu kwamba nyota hii pia ni ishara nyingine ya kwa ukweli wangu.[161]

BAADHI ZA HABARI ZA KUTISHA KUHUSU MAHARAJA DALIP SINGH NA MAREHEMU SIR SEYYID

Katika Novemba 1885, Seyyidna Ahmad[as] aliwaelezea Waislamu na Mabaniani baadhi za habari za kutisha zikiwa kama matabiri kuhusu marehemu Sir Seyyid na Maharaja Dalip Singh. Kisha baadaye alitoa tangazo pia tarehe 20 Februari 1886 ambamo aliandika:

"Nimefunuliwa na Mungu baadhi ya habari za kuogofya kunihusu mimi na baadhi ya jamaa zangu wa karibu, na kuwahusu baadhi ya marafiki zangu na baadhi ya ndugu wanafalsafa wa kaumu yetu ambao kana kwamba ni nyota ya Bara Hindi na kumhusu kiongozi fulani mgeni mwenye asili ya Kipanjabi, zinazodokeza mauti ya jamaa wa mtu fulani, na mauti ya mtu fulani mwenyewe, ambazo habari hizo zitaandikwa baada ya kuidhinishwa."[162]

Muradi wa 'Nyota ya Bara Hindi' ulikuwa Sir Seyyid marehemu, na muradi wa mgeni mwenye asili ya Kipanjabi ulikuwa Maharaja Dalip Singh aliyekuwa mwana wa Maharaja Ranjit Singh. Hudhur[as] anasema

[161] Aina Kamalate Islam, uk.110-111

[162] Ishtihar, 20 Februari 1886.

kwamba niliwaarifu Waislamu na Mabaniani karibu 500 kuhusu habari hizo. Kwa vyovyote, Sir Seyyid alipatwa na msiba mkubwa wa kufiwa katika uzee na mwanaye mmoja aliyekuwa bado kijana. Na pia mjanja mmoja akamwibia Rupia laki moja na nusu kutoka katika mchango aliokusanya kwa juhudi kubwa sana kwa kukamilisha ujenzi wa jengo la Chuo cha Aligarh. Sir Seyyid aliudhika kwa hasara hiyo kiasi hiki kwamba hakula chakula kwa siku tatu kwa huzuni, na baadhi ya wakati alizimia pia. Mwanaye mwingine, Seyyid Mahmud, alisema kwamba, "Wakati wa hasara hiyo kama nisingekuwepo Aligarh, baba yangu lazima angefariki kwa huzuni hii."[163]

MAHARAJA DALIP SINGH

Kwa vile Waingereza walichukua Panjab kutoka kwa Masingasinga kwa kupigana nao vita, hivyo walionelea vyema kwamba Dalip Singh aliye mrithi wa kiti cha kifalme ambaye yu bado mtoto tu, tumtoe katika Panjab. Basi, wakampeleka London. Huko akafanyiwa mpango wa kulelewa na kufundishwa. Pindi alipokuwa kijana, Waingereza walikuwa wameimarika katika Panjab. Masingasinga wakataka kwamba Maharaja Dalip Singh aletwe Panjab. Waingereza wakafikiri kwamba sasa hakuna hatari, kwa hiyo walikubali kumrudisha na wakamsafirisha kwa meli. Habari hii ilipojulikana katika Panjab kwamba Maharaja anarudi, basi Masingasinga wakafurahika sana. Hudhur[as] aliambiwa na Mungu Mjuzi wa mambo ya ghaibu kwamba Maharaja Dalip Singh hataweza kukaa katika Panjab, bali katika safari hii heshima yake, raha au uhai wake uko hatarini. Na ikawa hivyo hivyo. Meli yake ilipofika Eden, Waingereza wakaona ni hatari yeye kuingia Panjab, basi wakarudisha meli yake, na hivyo habari iliyotolewa na Mwenyezi Mungu ilitimia kwa shani kubwa.[164]

SAFARI YA HOSHIARPUR NA BISHARA KUHUSU MUSLIH MAU'UDI

Kwa kweli kila saa ya Hudhur[as] ilikuwa ya thamani sana na akafanya

[163] Ishtihar, 12 Machi 1897.

[164] Tazameni gazeti 'Akhbare Hind', Amritsar, 3 Mei 1886.

kazi kubwa za kutumikia dini. Mwenyezi Mungu pia akimsifu Anasema:

اَنْتَ الشَّيْخُ الْمَسِيْحُ الَّذِيْ لَا يُضَاعُ وَقْتُهٗ

Kwamba wewe ndiwe Masihi Mheshimiwa ambaye wakati wake hautapotezwa. Basi, kazi alizozifanya katika uhai wake, nadhani kama ziandikwe kinaganaga, maelfu ya kurasa zinaweza kuandikwa. Kila tukio la maisha yake lina masomo yenye thamani kwetu. Lakini, mwaka 1886 ulikuwa wa matukio ya maajabu na msaada wa kimbingu. Hapo juu imeshaelezwa kwa kuandika dondoo kutoka katika tangazo moja la Hudhur[as], kwamba mwaka huo yeye alishuhudia maonyesho maalum ya Mwenyezi Mungu. Akapashwa na Mungu habari za mambo yatakayotokea katika siku zijazo. Maelezo yake ni kwamba Hudhur[as] alikuwa na nia tangu muda mrefu kwamba aende mahala ambapo mtu yeyote asimjue, akafanye ibada ya Mungu na kuomba dua kwa siku arobaini mfululizo kama Hadhrat Musa[as]. Basi kwa lengo hilo, awali alinuia katika mwaka 1884 kwenda Sojanpur, Wilaya ya Gurdaspur, lakini kwa utashi wa Mungu safari hiyo iliahirishwa, na Mwenyezi Mungu Akamwambia, "Matatizo yako yatatuliwa katika Hoshiarpur."[165]

Basi, katika Januari 1886 alifunga safari ya kwenda Hoshiarpur. Katika safari hii alikuwa na Hadhrat Maulawii Abdullah Sanauri, Hadhrat Sheikh Haamid Ali na Mian Fatih Khan kama mahadimu. Akifika Hoshiarpur, Hudhur[as] alikaa katika ghorofa ya boma la Bwana Sheikh Mehr Ali.[166] Kwa sababu ya kuenea kwa Barahine Ahmadiyya alipata umaarufu wa kutosha na watu wakawa na shauku ya kuonana naye. Kwa hiyo Hudhur[as] akatangaza kwa vijikaratasi kwamba mpaka siku arobaini mtu yeyote asije kuonana nami. Baada yake kwa siku ishirini nyingine nitakaa hapa, katika siku zile kila mtu

[165] Siratul Mahdi, J. 1, Usimulizi wa 88.

[166] Mimi mwandishi nasema kwamba nyumba ambamo alikaa Hudhur[as], sasa imechukuliwa na Mabaniani. Hao Mabaniani wamegeuza nyumba nzima, lakini chumba alimofanya ibada Hudhur[as] waliacha bila kukibadilisha na wakati mwingine wanafanya ibada ndani yake. (Mimi mfasiri naongeza hapa kwamba sasa Jumuiya imeshanunua nyumba ile.)

atakuwa na ruhusa ya kuonana nami. Hadhrat Maulawii Abdullah Sanauri[ra] anasimulia:

> "Tulipangiwa kukaa sehemu ya chini. Hudhur[as] alituamuru kwa kusisitiza kwamba mtu yeyote asiongee nami mwenyewe, kama nikiuliza jambo, basi swali langu pekee lijibiwe, mazungumzo yasizidishwe, chakula changu kiletwe juu na msingoje kurudisha vyombo, nitasali peke yangu. Lakini kwa sala ya Ijumaa alisema kwamba tafuteni msikiti usioendewa na watu ambamo tuweze kusali peke yetu. Basi nje ya mji, katika bustani fulani, kulikuwepo na msikiti mdogo, tulikuwa tukienda huko kusali sala ya Ijumaa. Hudhur[as] alikuwa akitoa hotuba fupi na kurudi baada ya kusalisha. Hadhrat Maulawii[ra] anasimulia kwamba safari moja nilipoenda juu kupeleka chakula, Hudhur[as] alisema: "Mian Abdullah! Katika siku hizi nimefunguliwa milango ya fadhili kubwa kubwa za Mungu, na baadhi ya wakati Mwenyezi Mungu Anaendelea kuongea nami mambo kwa muda mrefu, ambayo yakiandikwa, kurasa nyingi zitajaa."[167]

Baada ya kupita siku hizo arobaini, tarehe 20 Februari, Hudhur[as] alitoa tangazo moja ambamo aliandika bishara kadha kumhusu yeye mwenyewe, kuhusu watoto wake, kuhusu jamaa zake wa karibu, kuhusu marafiki zake, kumhusu Sir Seyyid na Maharaja Dalip Singh. Bishara kubwa kumhusu Muslih Mau'udi pia aliandika katika tangazo hilo, ambayo maelezo yake yataandikwa sasa hivi, ***Inshaallah***. Baada ya ibada ya siku arobaini, watu kadha wa sehemu mbalimbali pia walihudhuria kwa kuonana naye. Baadhi ya watu walibadilishana mawazo naye pia kuhusu hususan dini, ambayo kati ya hayo mjadala baina yake na Pandit Murlidhar unajulikana sana, ambao taarifa yake imeandikwa katika kitabu cha Hudhur[as] "Surma Chashme Aria".[168] Muda wa miezi miwili ulipotimia, Hudhur[as] alirudi Qadian kwa njia hiyo hiyo aliyopitia alipokwenda. Hadhrat Maulawii Abdullah[ra]

---

[167] Siratul Mahdi, sehemu 1, Riwaya Na. 88 ya Mian Abdullah[ra].

[168] Kitabu hiki kinafaa sana kwa kuwakabili Waaria na Madahria. Katika kitabu hicho Hudhur[as]ameeleza kwa hoja, utaratibu wa ulimwengu, miujiza na uhakika wa Roho. (Mwandishi)

anasema:

"Kutoka Hoshiarpur, kwenye umbali wa maili 5 au 6 kuna kaburi la walii fulani ambapo pana kiunga pia, baada ya kufika hapo Hudhur[as] alishuka kutoka gari la ngo'mbe maksai na akasema kwamba sehemu hii ina kivuli kizuri, tupumzike kidogo hapa. Baada yake Hudhur[as] alikwenda kwenye kaburi, nikamfuata nyuma, Sheikh Haamid Ali na Fateh Khan walibaki kwenye gari la ngo'mbe. Yeye akifikia kaburi akafungua mlango, akaingia ndani akasimama kwenye kaburi upande wa kichwa, akainua mikono na akaomba kwa muda kidogo. Kisha akarudi na akaniambia, 'Nilipoinua mikono kwa kuomba dua, yule mtawa mwenye kaburi akatoka kutoka kaburni na kaketi mbele yangu kwa adabu. Kama usingekuwa pamoja nami, ningeongea naye pia. Macho yake ni makubwa na rangi kidogo nyeusi.'

"Kisha akasema, angalia kama yupo msimamizi yeyote wa kaburi, tumwulize habari zake. Basi, Hudhur[as] akamwuliza msimamizi, naye akasema, "Sikumwona mwenyewe kwani imepita karibu miaka mia moja tangu alipofariki. Naam, nimesikiliza kutoka kwa baba au babu yangu kwamba alikuwa mwenye rangi kidogo nyeusi na macho yalikuwa makubwa na alikuwa na athari kubwa katika maeneo haya."[169]

ISHARA YA REHEMA, YAANI BISHARA KUMHUSU MUSLIH MAU'UDI

Sasa naandika bishara ile mashuhuri na maarufu ya Hudhur[as] kumhusu Muslih Mau'udi, aliyotangaza katika tangazo la 20 Februari 1886. Hudhur[as] anasema:

"Mungu Aliye Rahimu na Karimu, Mtukufu na Mkuu, Aliye Mweza wa kila kitu, Mwenye shani kubwa na jina lake limetukuka, Aliniambia kwa kunifunulia kwamba:

"Mimi Nakupa ishara moja ya rehema kama ulivyoniomba. Nimesikia maombi yako yenye unyenyekevu, na kwa rehema

[169] Siratul Mahdi, sehemu 1, Riwaya Na. 88 ya Mian Abdullah[ra].

yangu Nimepokea dua zako. Na safari yako (iliyo safari ya Hoshiarpur na Ludhiana) Nimeibariki kwa ajili yako. Basi, unapewa ishara ya kudra na rehema na ukaribu. Unajaliwa ishara ya fadhili na hisani, na unapatiwa ufunguo wa ufaulu na ushindi. Ewe mshindi, salamu iwe kwako. Mungu akayasema hayo ili waupendao uzima waokoke katika kucha za mauti, na waliozikwa makaburini watoke nje, na ili heshima ya dini ya Kiislamu na daraja la Neno la Mungu liwadhihirikie watu, na ili haki ije pamoja na baraka zake zote na batili ikimbie pamoja na nuksi zake zote, na ili watu watambue kuwa Mimi ni Mweza, Nafanya Nipendavyo, na ili wayakini kuwa Mimi Nipo pamoja nawe, na ili wasioamini uwepo wa Mungu na wamkanao Mungu na dini ya Mungu na Kitabu Chake na Mtume Wake Mtukufu wapate ishara iliyo wazi, na njia ya wakosefu ibainike. Basi, upate habari njema kwamba utajaliwa mwana mmoja mzuri na mtukufu, utapata ghulamu (mwana) mmoja mnyofu. Mwana huyu atatokana na mbegu yako, dhuria yako na wazao wako. Yuaja mwana mzuri mtukufu, mgeni wako. Jina lake ni Imanueli na Bashiri. Amejaliwa roho takatifu, Ameepukana na uchafu. Yu nuru ya Mungu. Amebarikiwa yule ajaye kutoka mbinguni. Fadhili ipo kwa yule atakayekuja pamoja na kuja kwake. Yeye atakuwa mwenye utukufu, adhama na utajiri. Atakuja duniani na atawaponya wagonjwa wengi kwa pumzi yake ya ki-Masihi na kwa baraka yake ya Roho ya Haki. Yu Neno la Mungu, kwani rehema na ghera ya Mungu imemtuma kwa Neno Takatifu. Yeye atakuwa mwenye akili na fahamu nyingi na mpole wa moyo, na atajazwa elimu za dhahiri na batini, naye atafanya 3 kuwa 4 (maana yake haikuleweka). Ni Jamatatu, Jamatatu iliyobarikiwa. Mwana muhibu, mhashamu, muadhamu, dhihirisho la wa Kwanza na wa Mwisho, dhihirisho la haki na utukufu, kana kwamba Mungu Mwenyewe Ameshuka kutoka mbinguni, yule ambaye ushukaji wake utakuwa wenye kubarikiwa sana na kusababisha jalali ya Mungu kudhihirika. Nuru yuaja Nuru ambaye Mungu Amempaka uturi wa radhi yake. Tutamtilia Roho Yetu, na atakuwa chini ya Kivuli cha

Mungu. Atakua haraka, na atasababisha wafungwa kuachiliwa huru. Naye atapata umashuhuri hadi pembe za ardhi, na mataifa yatajipatia baraka kutoka kwake, ndipo atanyanyuliwa mbinguni kwenye nukta ya nafsi yake. Na hilo ni jambo lililokwisha katwa shauri."

(Tangazo la tarehe 20 Februari 1886, lililoandikwa ndani ya Tablighe Risalat, J. 1)

BISHARA KUMHUSU YEYE MWENYEWE, FAMILIA YAKE NA WAPENZI WAKE

"Kisha Mungu Mkarimu Mwenye shani kubwa Akinipa habari njema Akasema: "Nyumba yako itajaa baraka, nami Nitakutimizia neema zangu, na kutokana na wanawake waliobarikiwa ambao miongoni mwao baadhi yao utawakuta baadaye, wazao wako watakuwa wengi. Na Nitazidisha sana dhuria yako na kuwabariki, lakini baadhi yao watafariki pia katika umri mdogo, na kizazi chako kitaenea sana katika nchi mbalimbali. Na kila tawi la binamu zako litakatwa na litakwisha haraka kwa kukosa kizazi. Wasipotubu, Mungu Atawateremshia balaa juu ya balaa hadi wataangamia. Nyumba zao zitajaa wajane na ghadhabu itazishukia kuta zao. Lakini wakirejea, basi Mungu naye Atarejea kwa rehema. Mungu Ataeneza baraka zako hapa na pale, na Atastawisha kwa njia yako nyumba moja iliyokuwa imeachwa. Na Atajaza kwa baraka nyumba ya kutisha. Dhuria zako hawatakatika na watastawi mpaka siku za mwisho. Mungu Atadumisha jina lako kwa heshima mpaka siku ya mwisho ya dunia, na Atafikisha mwito wako mpaka pembe za dunia. Nitakuinua na kuita kwangu, lakini jina lako halitatoweka kamwe kwenye uso wa ardhi. Na itakuwa hivi kwamba watu wote wanaojaribu kukudhalilisha na kutamani ushindwe na wanafikiria kukuangamiza, wao wenyewe watashindwa na watakufa katika hali ya kushindwa na pasipo kupata shabaha. Lakini, Mungu Atakushindisha kikamilifu na Atakupatia miradi yako yote. Nitaongeza kundi la wapenzi wako waliohalisika na Nitatia baraka katika nafsi zao na mali zao, na nitawazidisha na

watalishinda kundi lingine la Waislamu ambalo ni kundi la mahasidi na maadui mpaka siku ya kiama. Mungu Hatawasahau wala Hatawafutu, nao watapata ujira wao sawa na ikhlasi zao. U kwangu kama mitume wa Waisraeli (yaani unafanana nao kama kivuli). U kwangu kama Umoja wangu. Unahusikana nami na Ninahusikana nawe. Na waja wakati, bali upo karibu kwamba Mungu Atatia mapenzi yako katika mioyo ya wafalme na matajiri hata kwamba watatafuta baraka katika nguo zako. Enyi wakataaji na wapinga haki! Ikiwa mna shaka kuhusu mtumishi wangu, kama mnakana ile fadhili na hisani tuliyomfanyia mtumishi wetu, basi kama m wakweli, leteni nyinyi pia ishara yoyote mfano wa ishara hii ya rehema kuhusu nyinyi. Na msipoweza abadani kuleta ─ na kumbukeni kwamba hamtaweza kuileta kamwe ─ basi uogopeni moto ulioandaliwa kwa waasi, waongo na wapitao mipaka.[170]

Baadaye katika tangazo la tarehe 22 Machi 1886, Hudhur[as] baada ya kuarifiwa na Mungu aliweka muda pia wa miaka tisa kwa kuzaliwa Muslih Mau'udi. Basi, sawa na ahadi ya Mungu tarehe 12 Januari 1889 Muslih Mau'udi alizaliwa. *Alhamdulillahi alaa dhalika.*

Itafaa kueleza kwamba Mwenyezi Mungu, sawa na hekima yake kamilifu baada ya bishara ya Muslih Mau'udi, kwanza Alimpatia Hudhur[as] binti mmoja na kisha akampa mvulana aliyeitwa baadaye Bashir wa Kwanza na akafariki katika umri wa mwaka mmoja na robo. *Inna lillahi wa inna ilaihi rajiun.*

Kwa kuzaliwa watoto hao wawili, wapinzani na wenye imani dhaifu wakapatwa na kikwazo kikubwa nao wakaanza kupinga kwamba Muslih Mau'udi hakuzaliwa sawa na bishara, ilihali katika tangazo la tarehe 22 Machi 1886 Hudhur[as] alieleza waziwazi kwamba kuhusu kuzaliwa kwa Muslih Mau'udi, Mwenyezi Mungu Ameweka muda wa miaka tisa. Na hii haikumaanisha kwamba katika muda wa miaka tisa hatazaliwa kwa Hudhur[as] mtoto yeyote mwingine minghairi ya Muslih

[170] Kutoka katika tangazo la tarehe 20 Februari 1886, lililoandikwa katika Tablighe Risalat, uk. 58-62

Mau'udi, au hatakufa. Kusudio lilikuwa ni hili tu kwamba katika muda wa miaka tisa Muslih Mau'udi atazaliwa, basi na akazaliwa.

WATOTO WA HUDHUR[AS]

Naona yalazimu kutaja hapa mahala pamoja watoto wote wa Seyyidna Ahmad[as]. Mke wake wa kwanza aliyekuwa miongoni mwa jamaa zake, alimzalia wavulana wawili, Hadhrat Mirza Sultan Ahmad na Mirza Fadhl Ahmad. Wa kwanza alizaliwa katika mwaka 1853 na katika sehemu za mwisho wa umri wake alifanya baiati mkononi mwa mdogo wake Hadhrat Mirza Bashirud Din Mahmud Ahmad, Khalifatul Masihi wa Pili, akafariki katika mwaka 1931. Na yule wa pili alizaliwa mnamo mwaka 1855, na alifariki katika mwaka wa 1902. Yeye alikuwa mtiifu sana wa Hudhur[as], lakini katika siku za mwisho aliathirika na jamaa zake wengine.[171]

Mke wake wa pili, Hadhrat Seyyida Nusrat Jahan Begam aliyekuwa binti wa Hadhrat Mir Nasir Nawab wa Delhi, alimzalia watoto kumi, wavulana watano na wasichana watano:

1. Bi 'Ismat: Alizaliwa tarehe 15 Aprili 1886, akafariki katika mwaka 1891.
2. Bashir wa Kwanza: Alizaliwa tarehe 17 Agosti 1887, akafariki tarehe 4 Novemba 1888.
3. Hadhrat Mirza Bashirud Din Mahmud Ahmad, aliyezaliwa tarehe 12 Januari 1889. Yeye akawa Khalifatul Masihi wa Pili katika mwaka 1914.
4. Bi Shaukat: Alizaliwa katika mwaka 1891, akafariki katika mwaka 1892.
5. Hadhrat Mirza Bashir Ahmad M.A.: Alizaliwa tarehe 20 Aprili 1893.
6. Hadhrat Mirza Sharif Ahmad: Alizaliwa tarehe 24 Mei 1895.
7. Hadhrat Bi Nawab Mubaraka Begam: Alizaliwa tarehe 2 Machi 1897.

[171] Siratul Mahdi, sehemu 1, uk. 29, riwaya Na. 37

8. Hadhrat Mirza Mubarak Ahmad: Aliyezaliwa tarehe 14 Juni 1899 na akafariki tarehe 16 Septemba 1907.
9. Bi Amatun Nasiir: Aliyezaliwa tarehe 28 Januari 1903 na katika mwaka huo huo tarehe 3 Desemba akafariki.
10. Hadhrat Bi Amatul Hafiz Begam: Alizaliwa tarehe 25 Juni 1904.

Maelezo ya juu yanadhihirisha kwamba mke wake wa pili alimzalia watoto kumi, miongoni mwao watano walifariki katika umri mdogo na watano kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu bado wako wazima na hao ndio watoto watano, kuhusu hao Hudhur[as] alisema katika ubeti kwamba:

Hao watano ambao ni kizazi cha Seyyida,
hao ndio watano walio msingi.

UTABIRI KUHUSU MIRZA AHMAD BEG NA WENGINEO – Mwaka 1888

Mirza Ahmad Beg wa Hoshiarpur aliyetajwa katika kichwa cha habari alikuwa miongoni mwa jamaa wa Seyyidna Ahmad[as]. Watu hao walikuwa wakimdhihaki Mwenyezi Mungu na mafunzo ya Mtume Mtukufu[saw] na daima wakamwomba Hudhur[as] awaonyeshe ishara. Hudhur[as] alipoelekea kwa Mwenyezi Mungu, aliambiwa kwamba apeleke posa kwa Mirza Ahmad Beg kumwoa bintiye mkubwa Bi Muhammadi Begam. Mirza Ahmad Beg akikubali ndoa hii, basi yeye na familia yake watapata sehemu katika baraka, na kama wakimwozesha mtu mwingine binti yake, basi kwa sababu ya kukadhibisha ishara za Allah na kuzidhihaki, adhabu ya Mwenyezi Mungu itawashukia na Mirza Ahmad Beg na mkwe wake wote wawili watafariki katika muda wa miaka mitatu, na Muhammadi Begam akiwa mjane ataolewa nawe.

Baada ya utabiri huu, Mirza Ahmad Beg hakumwozesha yeyote binti yake kwa miaka mitano na akaendelea kuishi mpaka wakati ule. Baada ya miaka mitano alimwozesha Mirza Sultan Muhammad wa Patti Wilayani Lahore, binti huyo. Ilikuwa haijapita miezi sita baada ya ndoa ya Muhammadi Begam, Mirza Ahmad Beg akishikwa na

homa ya taifodi akafa katika hospitali ya Hoshiarpur.[172] Kifo chake kiliwatisha sana mkewe na jamaa wengine, kwani sawa na utabiri sasa ilikuwa zamu ya kifo cha Mirza Sultan Muhammad. Lakini hao wote wakaelekea kutubu na kuomba msamaha. Wakamwandikia Hudhur[as] pia barua za kuombewa. Basi, kwa hiyo Mwenyezi Mungu Aliepusha kifo kwa mume wa Muhammadi Begam.

Kama mume wa Muhammadi Begam angefariki baada ya kukana na kudhihaki, basi lazima Muhammadi Begam baada ya kuwa mjane angeolewa na Hudhur[as]. Lakini kwa kuwa alisalimika na kifo kwa sababu ya kutubu na kuomba ghofira, hivyo Muhammadi Begam hakuolewa naye. Sharti inapotoweka, jambo lililowekewa sharti nalo latoweka.[173]

[172] Tarehe 30 Septemba 1892

[173] Kwa maelezo zaidi someni "Utabiri Kuhusu Mirza Ahmad Beg" na Kadhi Muhammad Nadhir Lyallpuri.

MLANGO WA TATU

TANGAZO LA BAIATI HADI UPANUZI WA MASJID MUBARAK

TANGAZO LA BAIATI, 1 DESEMBA 1888

Tumeshataja nyuma kwamba kabla ya kuzaliwa Muslih Mau'udi, Seyyidna Ahmad[as] alipata mvulana mmoja anayejulikana kwa jina la Bashir wa Kwanza. Watu walidhani kwamba yeye ametimiza utabiri wa Muslih Mau'udi, lakini alipofariki katika umri wa mwaka mmoja na robo, shutuma zililetwa na wapinzani. Hapo hekima kubwa ya Mwenyezi Mungu ilitaka imfanye Hudhur[as] atoe tangazo la kuchukua baiati. Basi, akachapisha tangazo la kifo cha Bashir wa Kwanza ambalo mwishoni mwake chini ya kichwa cha habari "Tabligh" aliandika:

> "Hapa nawafikishia mahuluku wa Allah kwa jumla, na hususan ndugu zangu Waislamu, ujumbe mwingine pia kwamba nimeamrishwa ya kuwa watu watafutao haki wafanye baiati yangu ili kujifunza imani ya kweli na utakaso wa kweli wa kiimani na njia ya mapenzi ya Mungu, na ili kuachana na maisha machafu na maisha ya uzembe na uasi. Basi wale ambao wanaona uwezo huo kiasi fulani nafsini mwao, hao hawana budi waje kwangu, kwani nitawafariji na nitajaribu kuwapunguzia shida zao, na Mwenyezi Mungu Atawabariki kwa maombi yangu na mwelekeo wangu sharti wawe tayari kwa moyo na roho kufuatilia masharti ya Mungu. Hii ni amri ya Mungu niliyokwishafikisha leo. Kuhusu hiyo, ufunuo wa Kiarabu ni huu:
>
> اِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللّٰهِ ۔ وَاصْنَعِ الْفُلْكَ بِاَعْيُنِنَا وَوَحْيِنَا ۔ اَلَّذِيْنَ يُبَايِعُوْنَكَ اِنَّمَا يُبَايِعُوْنَ اللّٰهَ ۔

يَدُ اللّٰهِ فَوْقَ اَيْدِيْهِمْ ۔ وَالسَّلَامُ عَلٰى مَنِ اتَّبَعَ الْهُدٰى[174]

Mfikishaji,
Mnyenyekevu,
Ghulam Ahmad, *Mungu Amsamehe*
1 Desemba 1888

[174] Tafsiri: Utakapoazimu, basi umtegemee Allah, na kuunda safina mbele ya macho yetu na sawa na wahyi wetu. Watakaofanya baiati yako, watafanya baiati ya Allah, Mkono wa Allah uko juu ya mikono yao.

MASHARTI YA BAIATI

Katika tangazo hilo, masharti ya baiati yaliyotajwa, aliyachapisha katika tangazo la "Takmile Tabligh" la tarehe 12 Januari 1889, ambayo ni haya:

La kwanza ni kwamba mwenye kufanya baiati aahadi kwa moyo wa kweli kwamba tangu sasa mpaka aingie kaburini hatamshirikisha Mungu na chochote.

La pili ni kwamba atajiepusha kabisa na njia za kusema uwongo, uzinzi, kutazama wanawake, ufasiki, uovu, dhuluma, hiana, ufisadi, na uasi. Na hatashindwa na tamaa mbaya za nafsi yake hata akichochewa namna gani na tamaa mbaya.

La tatu ni kwamba atasali sala tano bila kuacha sawa na amri ya Mungu na Mtume wake s.a.w. Na sawa na uwezo wake atadumu kusali sala ya tahajudi na kumsalia Mtukufu Mtume[saw], na kuomba msamaha wa dhambi zake kila siku na kuomba maghufira. Na kwa mahaba ya moyoni atamhimidi na kumsifu Mungu, siku zote akikumbuka hisani za Mwenyezi Mungu.

La nne ni kwamba hatawadhuru, kwa namna yoyote isiyojuzu, viumbe wote wa Mungu kwa jumula na hususa Waislamu, kwa sababu ya harara za nafsi yake, si kwa ulimi wala mkono wala kwa njia yoyote nyingine.

La tano ni kwamba atakuwa mwaminifu kwa Mwenyezi Mungu katika kila hali ya huzuni na raha, dhiki na faraja, neema na msiba, na kwa vyovyote atakuwa radhi juu ya kudra ya Mungu. Na atakuwa tayari kukubali kila fedheha na udhia katika njia yake, naye atakapopata msiba wowote hatarudi nyuma, bali atasonga mbele.

La sita ni kwamba ataacha kabisa kufuata desturi mbaya na kutii tamaa ya nafsi, na atakubali kabisa utawala wa Kurani Tukufu juu yake. Na atachukulia kauli ya Mungu na kauli ya Mtume Mtukufu[saw] kama mwenendo wake siku zote.

La saba ni kwamba ataacha kabisa kufanya kiburi na majivuno na

ataishi kwa upole, unyenyekevu, hulka njema, uvumilivu na umaskini.

La nane ni kwamba atafahamu dini na heshima yake na kuuhurumia Uislamu kuwa ni bora kuliko uhai wake, mali yake, heshima yake na kuliko watoto wake na wapenzi wake wote.

La tisa ni kwamba atashughulikia kuwahurumia daima viumbe vya Mungu kwa ajili ya Mungu tu, naye sawa na uwezo wake atawafaidisha wanadamu kwa nguvu na neema alizopewa yeye na Mungu.

La kumi ni kwamba katika fungamano la udugu atakalofungamana nami kwa ajili ya Mungu, kwa ikrari ya kunitii katika kila amri njema, atakaa imara juu yake mpaka kufariki kwake. Na katika fungamano hili la udugu atakuwa mwenye daraja ya juu sana hata kwamba mfano wake usipatikane katika udugu na mahusiano ya kidunia wala katika hali zote za utumishi.

SABABU YA KUAHIRISHA TANGAZO LA MASHARTI YA BAIATI

Akieleza sababu ya kuahirisha tangazo la masharti ya baiati, Seyyidna Ahmad[as] anasema:

> "Hayo ni masharti ambayo ni lazima wafanyao baiati watimize, ambayo hayakuandikwa katika tangazo la tarehe mosi Desemba 1888. Na iwe wazi kwamba amri ya kutoa mwito wa baiati iliishafika kutoka kwa Mwenyezi Mungu tangu miezi kumi takriban, lakini sababu ya kuahirisha kuichapisha ilikuwa hii kwamba nalichukia kuwa watu wa aina zote, wazuri na wabaya, wajiunge na Jumuiya hii. Na moyo ukataka kwamba katika Jumuiya hii iliyobarikiwa wajiunge watu wale tu waliobarikiwa ambao wawe na asili ya uaminifu na ambao sio wenye imani dhaifu wenye kubadilika haraka na waliotawaliwa na shaka. Kwa sababu hiyo nilikuwa nasubiri kutokea jambo litakalopambanua baina ya wakweli na wabovu, na baina ya wenye ikhlasi na wanafiki. Basi Mungu Mwenye shani kubwa kwa hekima na rehema yake kamili Akakifanya kifo cha Bashir Ahmad kuwa ni

jambo hilo,[175] na Akawatenganisha wenye fikara mbovu, wenye imani ndogo na wenye dhana mbaya. Na wale tu walibaki nasi ambao asili zao zilistahili kuwa nasi; na wale ambao kiasili hawakuwa wenye imani imara na walikuwa wamechoka na kulegea, hao wote wakaangamia na wakaingiwa na shaka. Basi kwa sababu hiyo, ikaonekana yafaa kuchapisha wakati huu tangazo la mwito wa baiati, ili tufaidike na uwanja safi baada ya kufagiliwa mbali takataka, na tusipate kusikia uchungu wa mwisho mbaya wa hao waliodanganyika, na ili wale ambao katika hali ya majaribio haya watakaojiunga na Jumuiya hii iliyobarikiwa kwa kukubali mwito huu wa baiati, hao hao wajulikane kuwa ni Jumuiya yetu na hao hao wawe marafiki zetu halisi nao ndio ambao kuwahusu hao Mwenyezi Mungu Aliniambia kwamba nitawatanguliza juu ya wengine mpaka Kiyama, na rehema na baraka zitakuwa pamoja nao. Na Akaniambia kwamba utayarishe safina kwa idhini yangu na mbele ya macho yangu. Wataofungamana nawe, watafungamana na Mungu, Mkono wa Mungu utakuwa juu ya mikono yao. Na Akasema kwamba mhudhurie mbele ya Mwenyezi Mungu kwa nguvu zenu zote, na msiache Mungu wenu Mkarimu peke yake. Atakayemwacha peke yake, ataachwa peke yake."[176]

ISHARA ILIYOFICHIKA KATIKA KUJUMUIKA PAMOJA KUANZISHWA JUMUIYA NA KUZALIWA MUSLIH MAU'UDI

Hili ni jambo la ajabu, bali ni hekima muhimu miongoni mwa hekima za Mungu kwamba tarehe 12 Januari 1889 Hadhrat Mirza Bashirud Din Mahmud Ahmad, Muslih Mau'udi, alizaliwa na siku hiyo hiyo Seyyidna Ahmad[as] akitangaza masharti ya baiati akaweka msingi wa Jumuiya na akawakaribisha wenye ikhlasi kwa kufanya baiati. Katika kujumuika kwa mambo hayo mawili kwa kweli kulikuwa na ishara iliyofichika kwamba Hadhrat Mirza Bashirud Din

[175] Bashir Ahmad muradi wake ni Bashir wa KWANZA aliyezaliwa baada ya utabiri wa Muslih Mau'udi na akafa tarehe mosi Desemba 1888.

[176] Tangazo la tarehe 12 Januari 1889.

Mahmud Ahmad, ***Mungu amsaidie,*** atakuwa na jukumu muhimu katika kutapakaza Jumuiya hii. Matukio pia yameshashuhudia kwa uwazi kabisa kwamba jambo hilo lilikuwa sahihi, na kwa nini lisingekuwa sahihi wakati Mtume Mtukufu[saw] alipokwishatabiri kumhusu Masihi Mau'udi kwamba يَتَزَوَّجُ وَيُوْلَدُ لَهٗ , yaani "Yeye atamwoa mwanamke wa sifa njema za hali ya juu na wazao wake watafanya kazi muhimu za dini."

Kumbukeni kwamba hapa haikuashiriwa kumwoa mwanamke wa kawaida, wala kuzaliwa kizazi cha kawaida, kwani kwa kukutaja huku hakungeweza kutazamiwa kuleta faida yoyote, hususan wakati ambapo Nabii Mtukufu mweye shani adhimu atabiri na kisha Hudhur[as] pia kabla ya kuzaliwa kila mtoto awatangazie watu wote sifa zake maalum na amsifu mwana mmoja mara kwa mara akimtaja kuwa ni mwenye kutimiza bishara za muhimu.[177] Mambo hayo yote yanaashiria kwamba wazao wa Masihi Mau'udi watapaswa kutekeleza majukumu makubwa katika utangazaji wa dini. Basi, ***Alhamdu lillahi*** wanaendelea kufanya hivyo.

SAFARI YA LUDHIANA NA HOSHIARPUR

Hudhur[as] mwanzoni mwa mwaka 1889 alikwenda Ludhiana na kwa njia ya kipeperushi aliwatangazia jamaa:

> "Kuanzia tarehe 4 Machi 1889 hadi tarehe 25 Machi nipo Ludhiana, katika muda huu mtu yeyote akitaka kuja, basi aje Ludhiana baada ya tarehe 10. Na kama kufika hapa kusababishe hasara na shida, basi ahudhurie[178] Qadian baada ya tarehe 25 Machi wakati wowote kwa kufanya baiati baada ya kuarifu."

Hudhur[as] alipokuwa amefika tu Ludhiana, alikaribishwa kushiriki

[177] Hudhur[as] anasema, "Katika hali ya kashfi nilipewa matunda manne, kati yao matatu yalikuwa maembe, lakini tunda moja la rangi ya kijani lilikuwa kubwa sana, hilo halikufanana na matunda ya dunia hii… Hakuna shaka kwamba muradi wa matunda ni wazao." Barua ya tarehe 8 Juni 1886, kwa Hadhrat Maulana Nurud Din[ra] Khalifatil Masihi wa Kwanza, kutoka katika Maktubati Ahmadiyya, J. 5 , Na. 2, uk. 6

[178] Ishtihar 4 Machi 1889, maelezo ya pembeni.

katika sherehe ya harusi ya mwanaye Sheikh Mehr Ali, chifu wa Hoshiarpur. Familia hii ilikuwa na uhusiano wa zamani na Hudhur[as], katika kipindi cha ibada ya siku arobaini pia Hudhur[as] alikaa katika nyumba moja ya Bwana Sheikh. Basi, kwa sababu ya uhusiano huu wa zamani Hudhur[as] alikwenda Hoshiarpur kushiriki katika sherehe ya harusi.

BAIATI YA KWANZA, 23 MACHI 1889

Katika Ludhiana Hudhur[as] alipenda nyumba ya Hadhrat Munshi Sufii Ahmad Jan[ra] kwa kupokea baiati. Bwana Munshi alikuwa mtu mwenye roho safi sana na mcha Mungu. Pembezoni mwake yeye alikuwa na mamia ya wafuasi waliokuwa na ikhlasi ya hali ya juu. Baada ya kusoma kitabu maarufu cha Hudhur[as], Barahine Ahmadiyya, yeye alikuwa ameishajitolea kwake kwa moyo wake na alitamani kufanya baiati yake akiacha utaratibu wake mwenyewe wa kupokea baiati za watu. Kwa hiyo, alisoma ubeti huu pia kumwambia Hudhur[as]:

Sisi wagonjwa twakutegemea,
uwe Masihi, twakuomba kwa jina la Mungu.

Wakati huo Hudhur[as] alimjibu kwamba bado sijaamrishwa kupokea baiati. Lakini alipotangaza kupokea baiati, yeye alikuwa amekwishafariki, *inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun.*[179] Hudhur[as] alifanya bidii kwa kumfanya Bi Sughra Begam bintiye Hadhrat Sufii Ahmad Jan kuolewa na Hadhrat Maulana Hakim Nurud Din[ra].

DARUL BAIATI

Chumba kile cha nyumba ya marehemu Hadhrat Munshi Sufii Ahmad Jan[ra] ambamo Hudhur[as] alipokea baiati ya kwanza kabisa kinaitwa Darul Baiati. Watoto wote wa marehemu Hadhrat Munshi walijiunga na Ahmadiyya. Hao walitoa wakfu nyumba hiyo kwa Jumuiya, lakini ni masikitiko kwamba katika mapinduzi ya mwaka 1947 ilitoka kutoka mkononi mwa Jumuiya kwa muda lakini

[179] Hudhur[as] alimhesabia miongoni mwa wafanyao baiati, bali miongoni mwa Masahaba 313 pia. Tazameni rejista ya baiati na Anjame Atham.

inshallah, itapatikana tena.[180]

SIKU YA BAIATI

Baiati ilianzia tarehe 23 Machi 1889. Hudhur[as] alitaka kwamba majina ya wafanyao baiati pamoja na anuani zao kamili yahifadhiwe katika rejista moja. Kwa hiyo, Hudhur[as] aliagiza kwamba kila mfanya baiati akiandika jina lake pamoja na anuani kamili juu ya kipande cha karatasi atutolee. Amri ya Hudhur[as] ikatekelezwa. Baada ya siku chache rejista moja ilitayarishwa ambayo iliandikiwa kwenye jalada:

Baiati ya kutubu kwa kupata uchamungu na utakaso

TARATIBU YA WAFANYAO BAIATI

Katika rejista hiyo baadhi ya majina ya mwanzoni aliandika Hudhur[as] mwenyewe, lakini baadaye katika nyakati mbali mbali baadhi ya watu wengine pia walisajili majina wakichukua kutoka katika vipande vile vya karatasi. Kwa sababu ya kuchukua majina kutoka katika vyeti hivyo, taratibu ya wafanyao baiati haikuweza kuhifadhiwa. Kwa hiyo, kulitokea hitilafu kidogo kuwa taratibu sahihi ni ipi? Kwa vyovyote, hakuna shaka kwamba mfanya baiati wa kwanza alikuwa Alhaj Maulana Nurud Din Bherawii[ra] na wa pili alikuwa Mir Abbas Ali Ludhianawii aliyejitenga wakati wa madai ya Hudhur[as] kuwa Masihi Mau'udi. Watu maarufu waliofanya baiati baada yao, majina yao bila taratibu yoyote yanaandikwa chini:

Hadhrat Mian Muhammad Husain Muradabadi[ra] mkaligrafia, Hadhrat Maulawii Abdullah Sanauri[ra], Hadhrat Qadhi Khwaja Ali[ra], Hadhrat Mir Inayat Ali[ra], Hadhrat Chaudhari Rustam Ali[ra], Hadhrat Maulawii Abdullah[ra] mkazi wa Tangi, maeneo ya Charsada, Hadhrat Munshi Zafar Ahmad[ra], Hadhrat Munshi Arurhe Khan[ra], Hadhrat Munshi Muhammad Khan[ra], Hadhrat Munshi Habibur Rahman[ra], Hadhrat Qadhi Dhiaud Din[ra], Hadhrat Sheikh Abdul Aziz[ra] aliye Mwislamu mpya, jina lake la zamani Ram Singh, *Mungu Awe radhi nao wote*.

Kuna hitilafu juu ya Hadhrat Maulawii Abdul Karim[ra] kufanya baiati

[180] Kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu imeshapatikana tayari, sasa ni mali ya Jumuiya na ndugu wanakwenda kuizuru. ─ Mwenezi.

siku ile. Lakini sawa na Hadhrat Sheikh Yakub Ali Turab[ra], Hadhrat Maulawii alifanya baiati siku ya kwanza kabisa. Hadhrat Sheikh anasema kujihusu mwenyewe kwamba ingawa sikufanya baiati siku ya kwanza, lakini nilifanya baiati siku zile zile. Na kusita huku pia kulitokea kwa sababu sikuwa na utulivu wakati huo kuhusu madai ya Hudhur[as] kuwa mithili ya Masihi. Kwa hiyo baada ya kusoma kijitabu "Ushindi wa Islam" nilifanya baiati mara ya pili mjini Lahore.

Ni masikitiko kwamba rejista yenyewe iliyotunzwa na Hadhrat Mirza Bashir Ahmad, ukurasa wake wa kwanza umepotea uliokuwa na orodha ya majina manane ya mwanzo, waila historia kuhusu taratibu ya wafanyao baiati ingekuwa imehifadhiwa vizuri zaidi.

MANENO YA BAIATI

Hadhrat Maulawii Abdullah Sanauri[ra] anasema kwamba siku ya kwanza Hudhur[as] alipopokea baiati, wakati ule maneno ya baiati yalikuwa haya:

> "Leo natubia kwa mkono wa Ahmad dhambi zote na mazoea yote mabaya niliyokuwa nimeyaangukia. Naahidi kwa moyo wa kweli na nia madhubuti kwamba sawa na nguvu na fahamu yangu nitaendelea kuepukana na dhambi zote hadi siku ya mwisho ya umri wangu na nitatanguliza dini juu ya raha za dunia na ladha za nafsi, na nitayafuata sawa na uwezo wangu masharti kumi ya tarehe 12 Januari. Na sasa pia namwomba Mwenyezi Mungu msamaha wa dhambi zangu zilizopita.

اَسْتَغْفِرُ اللّٰهَ رَبِّیْ ۔ اَسْتَغْفِرُ اللّٰهَ رَبِّیْ مِنْ کُلِّ ذَنْبٍ وَّاَتُوْبُ اِلَیْهِ ۔ اَشْهَدُ اَنْ لَّا اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ وَحْدَهٗ لَا شَرِیْكَ لَهٗ وَاَشْهَدُ اَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهٗ وَرَسُوْلُهٗ ۔ رَبِّ اِنِّیْ ظَلَمْتُ نَفْسِیْ وَاعْتَرَفْتُ بِذَنْبِیْ فَاغْفِرْلِیْ ذَنْبِیْ فَاِنَّهٗ لَا یَغْفِرُ الذُّنُوْبَ اِلَّا اَنْتَ" [181]

[181] Siratul Mahdi sehemu ya kwanza, riwaya Na. 98. Tafsiri: Namwomba Allah, Mola wangu, ghofira. Namwomba Allah, Mola wangu, ghofira. Namwomba Allah, Mola wangu, ghofira kwa kila dhambi, na namtubia Yeye. Nashuhudia kuwa hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah, wa pekee, hakuna mshirika wake. Nami nashuhudia kuwa Muhammad ni mtumishi wake na Mjumbe wake. Mola wangu, nimejidhulumu nafsi yangu, na ninakiri dhambi yangu. Basi nighofirie dhambi yangu, kwani hakuna anayesamehe madhambi isipokuwa Wewe.

SAFARI YA ALIGARH

Mpaka mwisho wa Machi, Hudhur[as] alikaa Ludhiana, na mwanzoni mwa Aprili, Hudhur[as] alisafiri kwenda Aligarh kwa kuombwa na Maulawii Seyyid Tafadhul Husain, karani mkuu katika idara ya kutoza ushuru. Huko Aligarh, tukio moja la ajabu lilitokea, nalo ni kwamba Maulawii Muhammad Ismaili alimwomba Hudhur[as] kutoa mawaidha, naye akakubali kwa furaha. Lakini baadaye akazuiliwa na Mwenyezi Mungu kwa njia ya ufunuo. Hapo Maulawii Ismail alipata kisingizio cha kuleta shutuma dhidi ya Hudhur[as], na baada ya sala ya Ijumaa akatoa hotuba kumpinga na akakichapisha kipeperushi na kukieneza. Hudhur[as] akajibu shutuma zake katika kijitabu "Ushindi wa Islam" kinachofaa kusomwa. Kwa vyovyote, mbele ya uzuizi wa Mungu, hakujali dhihaka ya Maulawii Muhammad Ismail na ya watu wengine, na alikataa kabisa kuhututubu. Kwa kuwa Maulawii Muhammad Ismaili alimsingizia Hudhur[as] kutumia elimu ya falaki na akasema kwamba yeye anavyo vifaa vya falaki na kwa njia ya vifaa hivyo anatoa habari za siku zijazo na anaziita kuwa funuo, kwa hiyo, ili kubatilisha shutuma yake, Hudhur[as] alitoa aya ya Mubahala katika kijitabu chake "Ushindi wa Islam". Maulawii huyo akaukubali mwito wa Mubahala ndani ya kitabu chake alichokuwa akiandika siku zile. Lakni kabla hakijakamilika kitabu kile Bwana Maulawii alikufa na akaacha ishara kwa wajao baadaye.[182]

KURUDI LUDHIANA

Baada ya kukaa Aligarh kwa wiki moja, akarudi Ludhiana. Na baada ya kukaa huko siku chache akawasili Qadian mwanzoni mwa wiki ya pili ya Aprili 1889. Tena katika Oktoba 1889, alikwenda Ludhiana kumwona bibi wa mke wake aliyekuwa mgonjwa, kwa vile katika siku zile mkwe wake, Hadhrat Mir Nasir Nawab, alikuwa akiishi Ludhiana kikazi. Kutoka hapo akarudi Qadian tarehe 12 Novemba 1889.

[182] Hayate Ahmad, J. 3, uk. 36

BAIATI YA HADHRAT PIR SIRAJUL HAQ NU'MANI, 23 DESEMBA 1889

Hadhrat Pir Sirajul Haq Nu'mani Jamali aliyekuwa miongoni mwa kizazi cha Hadhrat Chahar Qutub Hansawii na mwenyewe pia alikuwa akipokea baiati na kutoa mawaidha, yeye hata mwanzoni alitambua ukweli wa Hudhur[as], lakini badala ya kufanya baiati huko Ludhiana alitaka kufanya baiati katika Masjid Mubarak ya Qadian. Kwa hiyo, yeye akaja Qadian, na tarehe 23 Desemba 1889 akafanya baiati katika Masjid Mubarak.[183]

BAIATI YA HADHRAT NAWAB MUHAMMAD ALI KHAN, MTAWALA WA MALERKOTLA, 19 NOVEMBA 1890

Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan alikuwa miongoni mwa ukoo wa Nawab wa Malerkotla na Mshia *Tafdhili,* yaani alimwamini Hadhrat Ali[ra] kuwa bora kuliko Makhalifa watatu. Yeye pia alifanya baiati katika siku hizo. Kujiunga na Hudhur[as] kwa kijana aliyelelewa katika ukoo uliotawala waliokuwa na imani ya Kishia, bila kujali lawama ya dunia, ilikuwa ni fadhili mahusus ya Mwenyezi Mungu na ni ushahidi juu ya utakaso wake wa batini na ucha Mungu wake.

Hadhrat Nawab mwanzoni mwa mwaka 1890 alifika Qadian na katika Septemba - Oktoba 1890 alikwenda Ludhiana na kuonana na Hudhur[as]. Kisha tarehe 19 Novemba 1890 alijiunga na Jumuiya akifanya baiati ya Hudhur[as] kwa njia ya barua. *Alamdulillahi alaa Dhalika.* Katika rejista ya baiati namba ya baiati yake ni 210.

MADAI YA KUWA MASIHI MAU'UDI, MWISHONI MWA MWAKA 1890

Mwishoni mwa mwaka 1889, Mwenyezi Mungu Alimfunulia kwamba Masihi mwana wa Mariamu ambaye Mtume Mtukufu[saw] alitabiri ujaji wake ni wewe tu. Masihi wa kwanza hayupo kabisa hai kwa kiwiliwili chake huko mbinguni bali ameshafariki kama manabii wengine. Ingawa kabla yake pia katika funuo na bishara kadha aliitwa kuwa Masihi Mau'udi, lakini mpaka alipokuwa hajadhihirishiwa kinagaubaga, alibaki juu ya itikadi yake ya zamani na kama Waislamu

[183] Hayate Ahmad, J. 3, uk. 41

wengine aliendelea kuelewa na kuamini kwamba Hadhrat Masihi Mnazareti yupo mbinguni na kiwiliwili chake. Lakini uhakika ulipodhihiri kwa uwazi, hakusita hata kidogo katika kuidhihirisha.

UCHAPAJI WA "FAT'HE ISLAM" NA "TAUDHIHE MARAAM"

Kwa kutangaza madai yake ya Umasihi alichapisha kijitabu "Fat'he Islam" ambacho kwenye ukurasa wake wa kwanza wenye jina la kitabu mishororo hii minne ya beti za kiufunuo imeandikwa:

> Mna shaka gani kumwamini Masihi yule ambaye Mungu Ameishajulisha kufanana kwake na Masihi wa kwanza.
>
> Matabibu mahiri nao mwawapa lakabu hiyo. Hata wapenzi pia mnawaita kuwa masiha.

Kijitabu hiki na kadhalika "Taudhihe Maraam" viliandikwa mwishoni mwa mwaka 1890, na vilichapwa katika robo ya kwanza ya mwaka 1891. Vitabu hivyo vilipochapwa tu, moto wa upinzani ulianza kuwaka.

MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII KATIKA KAMBI YA WAPINZANI

Maulawii Muhammad Husain Batalawii aliyekuwa ameishakubali cheo kikubwa cha Hudhur[as] akiandika maoni yake kwa kirefu ndani ya jarida lake maarufu la "Isha'atus Sunna" juu ya kitabu chake mashuhuri, "Barahine Ahmadiyya", yeye naye alianza kuchapisha makala dhidi yake. Maulawii Abdul Aziz wa Ludhiana na Maulawii Muhammad na wengineo waliokuwa wapinzani wa Hudhur[as] tangu muda mrefu na daima walikuwa wakimpinga lakini walikuwa wanakoma kwa sababu ya mashambulizi ya Maulawii Muhammad Husain Batalawii, ya kumtetea Hudhur, sasa hao pia walipata nafasi na wakaanza kupinga waziwazi. Maulawii Muhammad Husain alikwisha jua madai yake ya Umasihi wakati kijitabu "Fat'he Islam" kilipokuwa bado kinachapwa katika matbaa ya Amritsar, Riadhe Hind. Yeye kwa njia fulani aliagiza mswada wa kijitabu na kauona, na haraka akaandika katika gazeti lake "Isha'atus Suna", akimwambia Hudhur:

> "Sasa nakuuliza kwamba je madai haya yanamaanisha kwamba Masihi Mau'udi sio mwana wa Mariamu yule ambaye kuja kwake kumeahidiwa kabla ya Kiama katika Kurani na Hadithi, bali wewe ndiye huyo Masihi? Toa jibu lake kwa 'ndiyo' au 'hapana'.[184]

Kwa kujibu ombi la Bwana Maulawii, Hudhur[as] aliandika; "Kujibu swali lako naona inatosha kusema 'Ndiyo'.[185]

Baada ya jibu hili la Hudhur[as], kuandikiana baina yao kulianzia. Wakati fulani hali ya Bwana Maulawii ilikuwa hii kwamba alikuwa akiona heshima akiwa mhudumu wa Hudhur, na sasa hali yake ikawa kwamba hakuna aliyempita katika upinzani wake katika zama hizo.

MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN KATAKA KUFANYA MJADALA

Mwishoni mwa Februari 1891 au mwanzoni mwa Machi, Hudhur[as] alikwenda Ludhiana na kuandikiana barua kuliendelea na Bwana Maulawii. Bwana Maulawii alitaka kufanya mjadala naye, lakini Hudhur[as] hakuupenda, kwani Hudhur[as] aliona mjadala haukuweza kuleta faida, lakini kwa fikara hii kwamba labda miongoni mwa wasikilizaji, yeyote afaidike alikubali kufanya mjadala kwa sharti hili kwamba mjadala uwe kimaandishi, kwani maneno ya midomoni hatimaye yanasababisha fitina. Sharti moja aliweka hili kwamba:

> "Katika kikao cha mjadala kundi lile la wanaodai kupata funuo pia lazima lishiriki ambao waliniita kuwa mtu wa jahanamu sawa na funuo zao, na pia kafiri ambaye hawezi kuongoka, nao wameomba kufanya mubahala. Kwa funuo zake mwenye kuniita kafiri nisiyemwamini Mungu ni Mian Abdur Rahman wa Lakhoke, na mwenye kuniita mtu wa jahanamu ni Mian Abdul

[184] Isha'atus Suna, J. 12, Na. 12, uk. 354. Tanbihi: Baadhi ya waandishi wa sera wameandika kwamba kabla ya Fat'he Islam, Hudhur[as] alitoa kipeperushi kimoja pia ambamo kulikuwa na tangazo la madai yake. Mungu ndiye Mjuaji wa lililo sahihi.

[185] Kutoka katika barua ya Hudhur[as] kwa Maulawii Muhammad Husain Batalawii iliyoandikwa tarehe 5 Februari 1891, sawa na Hayate Ahmad, J. 3, uk. 61

> Hak Ghaznawii ambaye msadikishaji wa funuo zake na mfuasi wake ni Mian Maulawii Abdul Jabbar. Basi, ni lazima hao watatu wahudhurie katika kikao ili mubahala pia uamuliwe papo hapo."[186]

Kutokana na dondoo ya barua ya Hudhur[as], inaonekana kwamba kundi la Waghaznawii wa Amritsar pia likaanza kupinga vikali na likawa tayari hata kufanya upinzani mkali, na lilikuwa tayari kufanya mubahala. Baadaye kuandikiana barua na Maulawii Muhammad Husain kuliendelea kurefuka, nami naeleza kwa faida ya wasomaji mambo machache kutoka katika kuandikiana huko.

MAMBO MACHACHE KUTOKA KATIKA BARUA

Maulawii Muhammad Husain Batalawii katika barua yake alitoa kama upinzani ibara hii ya Hudhur[as] kutoka katika Barahine Ahmadiyya ambamo yeye aliandika sawa na itikadi maarufu ya Waislamu kwamba Hadhrat Masihi[as] atakapokuja tena duniani, hapo kwa mkono wake Islam itaenea duniani kote. Hudhur[as] akatoa majibu yake kwa ufasaha sana, ambayo muhtasari wake katika maneno ya Hudhur[as] mwenyewe ni huu:

> "Sikutaja chochote katika Barahine Ahmadiyya kwa kupata ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu juu ya mwana wa Mariamu kuwa Mau'udi au asiye Mau'udi, niliitaja kama itikadi maarufu tu. Haitafaa kitu kuitaja hiyo hapa.
>
> Mtume wetu s.a.w. pia alikuwa akifuata suna mashuhuri za manabii wa Bani Israeli katika baadhi ya mambo maadamu alikuwa hajashushiwa wahyi. Na baada ya kuletewa wahyi, akiona jambo fulani limekataliwa, basi alikuwa akiliacha. Hilo hata mtoto anaweza kulifahamu, kwa nini hatalielewa mtaalamu kama wewe."[187]

Maulawii Muhammad Husain alitaka kwamba katika mjadala kwanza

[186] Barua kwa Maulawii Muhammad Husain Batalawii, 8 Machi 1891.

[187] Barua ya Hudhur[as] ya tarehe 14 Machi 1891 kwa Maulawii Muhammad Husain Batalawii.

Hudhur[as] aandike makala kwa uthibitisho wa madai yake na kuhakikisha kifo cha Masihi[as], lakini Hudhur[as] alikuwa na rai hii:

"Nimeshaeleza kwa uwazi madai yangu katika 'Fat'he Islam' na *Taudhihe Maaram* na vilevile katika sehemu ile ya "Izala Auham" iliyochapwa katika "Kaule Fasih."[188] Na madai yale ni haya haya kwamba mimi ni mdai wa kuwa Mithili ya Masihi, nami nasema pia kwamba Hadhrat Masihi, mwana wa Mariamu, kwa kweli ameshafariki.

"Basi uwezekano wa kuwa kwangu Mithili ya Masihi umeshakubali katika "Isha'atus Suna", na sikulazimishi kukubali zaidi ya hayo. Kama mimi ni juu ya haki, basi Mungu Mwenye shani kubwa Mwenyewe Atanisaidia na Atadhihirisha ukweli wangu kwa mashambulio makali.

"Iliyobaki ni kufa kwa mwana wa Mariamu. Basi si wajibu wangu kuandika hoja za kifo, kwani sijadai lolote ambalo ni kinyume cha suna ya kale ya Mwenyezi Mungu, bali imefululiza njia hii tangu mwanzo wa Hadhrat Adamu kwamba aliyezaliwa hatimaye atafariki katika ujana au akiwa mzee kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

وَمِنْكُمْ مَنْ يُتَوَفّٰى وَمِنْكُمْ مَنْ يُرَدُّ اِلٰى اَرْذَلِ الْعُمُرِ لِكَيْلَا يَعْلَمَ مِنْ بَعْدِ عِلْمٍ شَيْئًا[189]

Basi kwa kuwa si faradhi yangu niandike hoja za kifo cha Masihi[as], kwa hiyo hili ni jukumu lako kwamba kwa kubatilisha kauli yangu uchukue kalamu na uthibitishe kwa Aya na Hadithi kwamba watu wote waliendelea kufariki hata Mtume Mtukufu wetu s.a.w. pia alifariki, lakini Masihi hajafa mpaka sasa. Mwulize mjuzi yeyote wa majadiliano kwamba adabu za mjadala ni nini?

---

[188] Jarida hili lilikuwa linatolewa mjini Sialkot, mhariri wake akiwa Munshi Ghulam Qadir Fasih.

[189] Na wapo miongoni mwenu wale ambao hufariki na wapo wengine miongoni mwenu ambao wanarudishwa kwenye umri wa ukongwe hata wanakuwa hawajui kitu baada ya kwishakuwa na elimu. (Sura Al-Hajj, 22:6)

Sasa ukumbuke hii pia kwamba mazungumzo yako yote mengine ni matawi ya Masihi kuinuliwa mbinguni mzima mzima na mwili wake. Kama ukithibitisha kwamba Masihi aliinuliwa mbinguni akiwa hai pamoja na mwili wake, basi umeshathibitisha yote. Ilmuradi, kuandika kwanza ni jukumu lako. Kama hata sasa pia hukubali, basi uweke waumuzi watu wachache wa dini zingine.

"Mwishowe, sikiliza mfano mmoja pia. Zaid amepotea, ambaye miaka mia mbili imeshapita tangu apotee. Khalid na Walid wanahitilafiana juu ya uhai na kifo chake. Khalid aliambiwa na mtu kwamba kwa kweli Zaid ameshafariki, lakini Walid anakanusha habari hii. Sasa una rai gani? Nani anawajibika kuleta ushahidi? Je, Khalid sawa na madai yake, anapaswa kuthibitisha kufariki kwa Zaid au Walid athibitishe uzima wa Zaid hadi muda huu? Kuna fatuwa gani?"[190]

KUANDIKIANA NA MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN KWAKOMA

Hudhur[as] alipoona kwamba Bwana Maulawii haji kwenye habari hasa isipokuwa tu kuandikiana yasiyotakikana, basi mwishoni mwa Aprili 1891 alifunga kuandikiana kwa siku zijazo kwa kumwandikia barua ifuatayo:

Bismillahir Rahmanir Rahim. Nahmaduhu wa Nusalli

Ndugu yangu mpendwa Bwana Maulawii, Mungu Akuweke salama, Assalamu alaikum wa Rahmatullahi wa Barakatuhu.

Barua yako imeshanifikia. Sikukuta jambo lolote jipya ambalo lijibiwe. Dai langu liliutegemea ufunuo. Kama ungalithibitisha kwamba Kurani na Hadithi inapinga dai hilo na kisha nisingaliweza kuvunja hoja hizo kwa maandishi yangu, basi ungalikuwa mkweli mbele ya wahudhuriao wote na sawa na kauli yako ningalitubia ufunuo huo. Kwa vyovyote, sasa anza

[190] Kutoka barua ya Hudhur[as] ya tarehe 20 Aprili 1891, kwa Maulawii Muhammad Husain Batalawii, kupitia Hayate Ahmad, J. 3, uk.78-79.

kuandika kujibu hoja za "Izala Auham", watu wenyewe wataona. Wassalamu, Mimi, Ghulam Ahmad. *Mungu Amsamehe.*"[191]

MBINU NYINGINE YA MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN

Maulawii Muhammad Husain alipoona kwamba Hudhur[as] ameacha kuandikiana naye kwa sababu ya mwenendo wake usio sahihi, basi yeye alimtumia Maulawii Muhammad Hasan, Chifu wa Ludhiana. Yaani sheikh Batalawii mwenyewe alikuwa akiandika barua lakini ili kudhihirisha kuwa Maulawii Muhammad Hasan ndiye aliyeandika alikuwa akimfanya atie saini yake. Ingawa, Hudhur[as] alijua uhakika ulivyo, lakini hakupendelea kutokujibu. Hivyo, kuandikiana barua kulianzia tena kwa njia nyingine, lakini mambo yalikuwa yale yale yaliyoishatajwa mapema, kwa hiyo hakuna haja ya kuyaandika.

TANGAZO MUHIMU

Hudhur[as] alipoona kwamba kina Maulawii wanatupa mwito wa mjadala lakini hawajitokezi, na upande wa pili wanawachochea watu wakieneza propaganda dhidi yake, basi alitoa kipeperushi, kichwa cha habari yake kikiwa "Tangazo Muhimu" kwa kukamilisha hoja juu ya maulamaa na watu wote. Mhutasari wake ni huu:

> "Nasema kwa kupaza sauti kwamba Mwenyezi Mungu Ameniwekea wazi haki kwa kunifunulia na kwa kunitilia moyoni. Na haki niliyofunuliwa ni hii kwamba kwa hakika Masihi mwana wa Mariamu ameshafariki, na roho yake ipo pamoja na roho ya mwana wa mama yake mdogo, Yahya, kwenye mbingu ya pili. Masihi aliyetakiwa kuja kwa njia ya kiroho katika zama hizi ambaye habari zake zipo katika Hadithi sahihi, ndiye mimi. Hiki ni kitendo cha Mwenyezi Mungu kinachoonekana ni ajabu machoni mwa watu na kinadunishwa. Nami naandika wazi wazi kwamba madai yangu hayategemei tu ufunuo, bali Kurani nzima inayasadikisha, Hadithi sahihi zote zinashuhudia usahihi wake, akili timamu pia inayaunga mkono. Kama masheikh wanazo hoja za kisheria dhidi yangu, basi

[191] Hayate Ahmad, J. 3 uk. 79

wakate shauri pamoja nami wakiitisha mkutano kwa njia iliyotajwa juu. Bila shaka haki itashinda. Nasema mara kwa mara kwamba mimi ni juu ya haki. Masheikh wanatoa fursa ya kutolewa makosa ya elimu yao wanaposema kwamba madai hayo ni kinyume cha Kurani na Hadithi.

Enyi mabwana, Mungu Mwenye shani kubwa Anurishe nyoyo zenu kwa mwanga wa mwongozo. Madai hayo si katu kinyume cha kauli ya Allah na kauli ya Mtume[saw], bali huku ni kutofahamu kwenu. Kama hamtajadiliana nami kimaandishi katika mkutano wa hadhara kwa kutaja mahali na tarehe maalumu, basi mtahesabiwa wahalifu mbele ya Mwenyezi Mungu na pia machoni mwa wakweli. Na inafaa kwamba mpaka mjadiliane nami kimaandishi ana kwa ana mfunge midomo yenu msiwapoteze watu wala msidhihirishe rai yenu yenye hitilafu na upinzani, na mwogope aya hii takatifu وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهٖ عِلْمٌ waila mwenendo huu utachukuliwa kuwa kinyume cha haya, imani, ucha Mungu na njia ya uadilifu. Na iwe wazi kwamba tangazo hili linawahusu masheikh wote walioishadhihirisha hitilafu ya rai, na hususan kiongozi wa hao wote yaani Maulawii Abu Said Muhammad Husain Batalawii, Maulawii Rashid Ahmad Gangohi, Maulawii Abdul Jabbar Ghaznawii, Maulawii Abdur Rahman wa Lakhoke, Maulawii Sheikh Ubaidullah Tibeti, Maulawii Abdul Aziz Ludhianawii pamoja na nduguze na Maulawii Ghulam Dastagir Kasuri."[192]

KUKOMA KWA KUANDIKIANA NA MAULAWII MUHAMMAD HASAN PIA

Tumeshataja nyuma kwamba baada ya Maulawii Muhammad Husain, kuandikiana kulianzia na Maulawii Muhammad Hasan, lakini kwa hakika Maulawii Muhammad Husain ndiye aliyekuwa anaandika kwa siri, hivyo kwa kuandikiana huku pia hakukuweza kukatisha shauri. Na kuandikiana huku pia kulifungwa tarehe 14 Juni 1891, lakini watu

[192] Kutoka katika "Tangazo Muhimu", la tarehe 26 Machi 1891, lililomo katika Hayate Ahmad, J. 3, uk. 84-90.

walikuwa na hamu sana ya kusikiliza mjadala, na Hudhur[as] mwenyewe pia alitaka kwamba kwa vyovyote kifo cha Masihi na masiala ya Masihi Mau'udi yajadiliwe.

SAFARI YA AMRITSAR NA KUPATIKANA SABABU ZA MJADALA WA LUDHIANA

Mwenyezi Mungu Alileta sababu zilizomlazimisha Maulawii Muhammad Husain kufanya mjadala. Ikawa hivi kwamba tarehe 13 Juni ilipokoma kuandikiana na Maulawii Muhammad Hasan, basi mwanzoni mwa Julai 1891 Hudhur[as] alikwenda Amritsar kwa kuombwa na baadhi ya machifu wa Amritsar. Huko Ahle Hadith walikuwa wamekwisha gawanyika katika makundi mawili; kundi moja lilikuwa la Maulawii Ahmadullah[193] na la pili la Waghaznawii. Tarehe 7 Juali 1891, Hudhur[as] alimwita Maulawii Ahmadullah kwenye mjadala wa kimaandishi sharti amani iwepo, lakini Bwana Maulawii hakukubali. Matokeo yake, watu wachache wa jumuiya ya Maulawii Ahmadullah walijiunga na Jumuiya Ahmadiyya wakifanya baiati ya Hudhur[as]. Miongoni mwa waliojiunga kati yao wafaao kutajwa hasa ni Hadhrat Maulawii Muhammad Ismail, Hadhrat Mian Nabii Bakhsh mtililia na Hadhrat Maulawii Inayatullah. Hao wazee walipojiunga na Jumuiya, Maulawii Muhammad Husain akalazimika kufanya mjadala.

MJADALA WA LUDHIANA

Hudhur[as] alipowasili Ludhiana, mjadala ulianzia tarehe 20 Julai 1891 kule alikokaa Hudhur[as]. Katika mjadala huo hususan walishiriki Hadhrat Maulawii Abdul Karim[ra], Munshi Ghulam Qadir Fasih[ra] Sialkoti na wanajumuiya wa Kapurthala na Wilaya ya Ludhiana.

MAELEZO YA HADHRAT PIR SIRAJUL HAK NU'MANI

Hadhrat Pir Sirajul Hak Nu'mani[ra] anaeleza:

> "Nilikuwa ninanukuu papo hapo makala ya Hudhur[as]. Maulawii Muhammad Husain Batalawii alipofika nyumbani kwa Hudhur,

[193] Maulawii Ahmadullah alikuwa mwanafunzi wa Maulawii Muhammad Husain Batalawii na mwalimu wa Maulawii Thanaullah Amritsarii.

pamoja na Maulawii Muhammad Hasan, Sa'dullah Mwislamu mpya na watu wengine 5-7, yeye aliandika swali moja na kuweka mbele ya Hudhur[as]. Hudhur[as] aliandika jibu lake na akaniambia kuchonga kalamu kadha na kuziweka kwake. Akasema uendelee kuyanakili nitakayoendelea kuandika. Basi nikaanza kunakili na yeye akaanza kuandika. Maswali na majibu ya siku hiyo yalipokwisha, Maulawii Muhammad Husain, kinyume cha ahadi alianza kutoa mawaidha kwa mdomo na akaeleza kwamba itikadi hii ya Bwana Mirza si sahihi kwamba Kurani Tukufu inaitangulia Hadithi, bali yafaa itikadi iwe kwamba Hadithi inaitangulia Kurani Tukufu, na ndiyo inayofungulia masiala zaidi yaihusuyo Kurani Tukufu, na hiyo ndiyo inayokata shauri. Huo ulikuwa ni mhutasari wa hotuba ya Bwana Maulawii. Hapo Hudhur[as] alisema kwamba kwa kuwa mapema yalikuwa yamefanywa mapatano kwamba mtu yeyote hatatoa hotuba kwa mdomo, lakini kwa kuwa Bwana Maulawii amehutubu kinyume cha mapatano, kwa hiyo ninayo pia haki kwamba nitoe hotuba kidogo kwa mdomo. Kisha Hudhur[as] alisema kwamba itikadi hii ya Bwana Maulawii si sahihi kabisa kwamba Hadithi inaitangulia Kurani Tukufu. Wasomaji, jambo lifaalo kusikiliza ni hili kwamba kwa vile Kurani Tukufu ni wahyi unaosomwa, na Kurani Tukufu nzima ilikusanywa pamoja katika zama za Mtume Mtukufu[saw] na hiyo ilikuwa ni Neno la Mungu, lakini Hadithi takatifu hazikuwa na mpango wa namna hii, wala hazikuandikwa katika zama za Mtume Mtukufu[saw], cheo na daraja iliyonayo Kurani Tukufu, hazinayo hadithi, kwani hizo zilitufikia kwa riwaya baada ya riwaya. Kama mtu akiapa kwamba kila neno la Kurani Tukufu ni Neno la Mungu, kama hilo sio Neno la Mungu basi mke wangu apate talaka, basi kisheria mke wake hawezi kupata talaka. Lakini aapaye kuhusu Hadithi na aseme kwamba kila neno la Hadithi ni lile lile lililotoka mdomoni mwa Mtume wa Mungu[saw], kama sivyo basi mke wangu apate talaka, basi bila shaka mkewe ataachika. Huu ndio mhutasari wa hotuba ya Hudhur[as]. Kwa maelezo hayo na hotuba hiyo na kwa makala iliyoandikwa alipokuwa anasoma,

sauti kubwa za kushangilia na ***subhanallahi, subhanallahi*** zilikuwa zinasikika hata kwamba watu wa upande wa Bwana Maulawii pia hawakuweza kujizuia kutamka ***subhanallahi***, isipokuwa Sa'dullah na Bwana Maulawii huyo. Watu watatu, wanne wakasema kwamba tulikuwa tukidhani kwamba Bwana Mirza hawezi kutoa hotuba kwa vile hajadili kwa mdomo, bali anajadili kimaandishi, lakini leo imetambulika kwamba Bwana Mirza anaweza kutoa hotuba vizuri sana na kipawa chake cha kuhutubia pia ni cha daraja ya juu. Na anapopenda maandishi sio kwa sababu ya kushindwa kuhutubu, bali kwa sababu hii kwamba kwa njia ya maandishi haki na batili ibainike vizuri na kila mmoja apambanue kikamilifu baina ya kuhakikisha haki na kubatilisha batili, na ukweli na uwongo ubainike kikamilifu kwa kila aliyehudhuria na asiyehudhuria. Hapo Bwana Maulawii alikuwa akikasirika na kusema, "Enyi watu, mmekuja hapa kusikiliza au kushangilia na kusema ***subhanallah***? Maandishi ya pande zote mbili yameshachapishwa, hakuna haja ya kuyaandika hapa.[194]

Katika mjadala huo, Hudhur[as] alitoa maelezo toshelevu juu ya Hadithi na Kurani Tukufu na akamaliza mijadala yote kwa siku zijazo. Mjadala huo ulifanyika kwa siku 6-7 katika nyumba ya Hudhur[as]. Sasa Bwana Maulawii alitafuta udhuru na akataka kuepa kwa njia yoyote. Alileta udhuru huu kwamba kwa siku hizi zote mjadala uliendelea nyumbani kwako, sasa inapaswa mjadala ufanyike ninakokaa, yaani nyumbani kwa Maulawii Muhammad Hasan. Hudhur[as] alikubali hii pia na kwa siku zilizobakia mjadala uliendelea nyumbani kwa Maulawii Muhammad Hasan. Hudhur[as] alipokuwa akitoka kwenda huko mimi pia nikahudhuria, waila akaniita, na mpaka nihudhurie, Hudhur[as] alikuwa haendi. Kwa jumla, Maulawii Muhammad Husain alifanya ujanja mwingi lakini ujanja wowote haukufaa. Hata hivyo kaiba makala moja iliyorejeshwa katika mjadala.

Kwenye nyumba ya Maulawii Muhammad Hasan, watu 2-4

[194] Mjadala huu umeshachapishwa kwa jina la "Al Hak Ludhiana". ─ Mwandishi.

walikuwa wakiwepo. Mjadala uliendelea kwa siku 13 na watu wengi walichoka, na toka pande zote nne barua zileanza kufika, hasa watu wa Ludhiana walipiga makelele kwamba mpaka lini mjadala utaendelea juu ya mambo ya kubuniwa. Inapaswa kujadili mada yenyewe iliyopangwa, yaani kifo na uhai wa Masihi. Mungu Avunjilie mbali hayo mambo yaliyozushwa na Bwana Maulawii. Hudhur[as] pia alisema mara kadhaa kwamba ni lazima mjadala uwe kuhusu kifo na uhai wa Masihi ili mambo yote yaamuliwe mara moja tu, lakini Bwana Maulawii hakuelekea kwenye mada hasa yenyewe. Kwa vile Bwana Maulawii hakuwa na hoja za uhai wa Masihi, kwa hiyo aliendelea kuepa mazungumzo hayo … Ilmuradi, ilipofika siku ya 13 ya mjadala, Wakristo, Waislamu, Mabaniani na wengineo wakaja kwa wingi… Hudhur[as], kabla ya kusoma makala, alisema kwa Bwana Maulawii kwamba mjadala umerefuka sana, sasa hakuna haja yake, inapaswa kujadili mada yenyewe, yaani kifo na uhai wa Masihi. Lakini Bwana Maulawii hakukubali. Hakuwa na chochote mkononi kuhakikisha uhai wa Hadhrat Masihi[as]. Hudhur[as] alipoanza kusoma makala, rangi ya uso wa Bwana Maulawii iligeuka, akafadhaika na akahangaika kiasi hiki kwamba aliposhika kalamu kwa kuandika, akaanza kuipiga juu ya ardhi, badala ya kuitia ndani ya kidau cha wino, na kalamu ilivunjika kwa kupiga ardhini mara chache. Na ilipotajwa kwamba imo ndani ya Bukhari Hadithi hii kuwa Mtume wa Mungu alisema kwamba Hadithi yangu iliyo kinyume cha Kurani, hiyo iachwe, bali Kurani ifuatwe, hapo Maulawii Muhammad Husain alikasirika sana na kasema kwamba Hadithi hii haipo katika Bukhari, na kama Hadithi hii ipo katika Bukhari basi wake zangu wote wawili wapewa talaka. Kwa neno la 'talaka' watu wakaangua kicheko na Bwana Maulawii hakujiweza kwa kuona aibu. Na baadaye kwa siku kadhaa aliendelea kuwaambia watu kwamba hapana, hapana hawakutalikiwa wake zangu wote wawili, wala sikutaja neno la talaka. Basi, mwanzoni watu 10-20 au 100-200 walijua, lakini Bwana Maulawii akawapasha habari hiyo maelfu ya watu. Bwana Maulawii

alikuwa ameshikwa na hasira sana, basi aliyoyatamka nini mdomoni Mungu ndiye ayajuaye."[195]

Mjadala huo uliendelea siku kumi na mbili mfululizo, ukaanzia tarehe 20 Julai 1891 na ukaishia tarehe 31 Julai 1891. Seyyidna Ahmad[as] alichapisha maelezo yote ya mjadala huo mwishoni mwa "Izala Auham". Mjadala huo umechapishwa kwa jina la "Al Hak Ludhiana" pia.

GHADHABU YA MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN NA HATUA YA KAMISHNA MDOGO WA LUDHIANA

Maulawii Muhammad Husain asipoweza kufanya chochote katika mjadala, akaanza kuwachochea watu kwa kukasirika, jambo ambalo likasababisha hatari ya kuleta uchafuzi mjini. Kamishna mdogo alipopata taarifa ya vitendo vya Bwana Maulawii, yeye alimwamuru Bwana Maulawii kuondoka mjini, naye akaenda Lahore. Hudhur[as] akafikiria kwamba amri ya kuondoka Ludhiana inahusikana na pande zote mbili. Hudhur[as] akamwandikia Kamishna mdogo barua tarehe 5 Agosti kujua uhakika. Jibu lake lililokuja tarehe 6 Agosti kutoka kwa Kamishna mdogo ni hili:

> Kutoka Mahakama ya Bwana W. Chitose, Kamishna mdogo wa Ludhiana,
>
> Kwa Bwana Mirza Ghulam Ahmad, Chifu wa Qadian, Salam. Barua yako ya jana imewasili. Baada ya kuisoma naandika jawabu kwamba unazo haki zile zile za kukaa Ludhiana kwa kuzifuata na kuzingatia sheria ya Serikali, ambazo raia wengine wanazo ambao wanatii sheria ya Serikali ya Kiingereza.
>
> Iliandikwa tarehe 6 Agosti 1891,
>
> Saini ya Bwana Kamishna mdogo[196]

BAIATI YA MAULAWII NIDHAMUD DIN

Siku ya pili ya mjadala tukio la ajabu lilitokea. Maulawii Nidhamud

[195] Tadhkiratul Mahdi, kilichoandikwa na Hadhrat Pir Sirajul Hak Nu'mani[ra]

[196] Hayate Ahmad, J. 3 uk. 109-110

Din alikuwa Sheikh aliyependa sana Kurani. Yeye pamoja na watu wengine 2-4 walikuwa wamekaa nyumbani kwa Maulawii Muhammad Hasan. Maulawii Nidhamud Din alimwuliza Maulawii Muhammad Husain kwamba je, katika Kurani Tukufu zipo aya zinazoeleza uhai wa Hadhrat Masihi[as]? Bwana Maulawii akajibu: Naam, kuna aya ishirini katika Kurani Tukufu. Baada ya kusikiliza jibu la Maulawii Nidhamud Din akamwendea Hudhur[as] na akauliza, "Bwana Mirza, unayo dalili gani ya kifo cha Masihi?" Akajibu, 'Kurani iko pamoja nami'. Bwana Maulawii akasema, kama nikuletee aya 20 juu ya uzima wa Masihi? Akasema, "Bwana Maulawii, ulete aya moja tu, itanitosha". Maulawii Nidhamud Din akasema, "Angalia, uwe imara, nakuletea aya 20". Akisema hayo akamwendea Mualawii Muhammad Husain Batalawii na akasema, "Bwana Maulawii, nimemkubalisha Bwana Mirza, nikamwambia kwamba nitakuletea aya 20, lakini yeye aliendelea kusema kwamba ulete hata aya moja tu. Sasa nitolee aya chache juu ya uzima wa Masihi, sasa hivi nitampelekea Bwana Mirza hizo na nitamlazimisha kutubia itikadi yake." Wasikilizaji walifurahia ushindi wa Bwana Maulawii, lakini Maulawii Muhammad Husain alighadhibika, akasema, "Hujamshinda Mirza bali umeniangusha mimi na umeniaibisha. Namvuta Mirza tangu zamani kumleta kwenye Hadithi na yeye ananivuta kwenye Kurani Tukufu. Kama ingekuwa aya yoyote katika Kurani Tukufu juu ya uhai wa Masihi[as] ningeileta mapema sana. Kwa sababu hiyo nasisitizia Hadithi, hatuwezi kustawi kwa Kurani Tukufu, Kurani Tukufu inastawisha madai ya Bwana Mirza."

Pir Sirajul Hak N'umani, mwandishi wa "Tadhkiratul Mahdi", anaandika, "Naapa kwa Allah Mwenye shani kubwa kwamba Maulawii Muhammad Husain Batalawii alisema hivyo hivyo, hakuna uongo hata chembe ndani yake. Kwa vyovyote, kwa kusikiliza maneno hayo ya Maulawii Muhammad Husain, Maulawii Nidhamud Din akaelewa hakika yote, akasema:

> "Kama Kurani Tukufu haipo pamoja nawe, kwa nini ulitoa madai hayo, sasa nitamkabilije Bwana Mirza! Kama Kurani Tukufu haipo nawe na haikuungi mkono bali ipo pamoja na

> Bwana Mirza na inamwunga mkono, basi mimi pia siwezi kukuunga mkono, bali katika hali hii nitamwunga mkono Bwana Mirza. Hili sio jambo la dunia bali ni jambo la dini, nipo pale palipo Kurani Tukufu."

Hapo Maulawii Muhammad Husain Batalawii akamwambia Sheikh mwenzake, "Bwana Sheikh, huyu Nidhamud Din hana akili, mwonyeshe aya ile ya Abu Huraira[ra]". Maulawii Nidhamud Din akasema, "Sitaki aya ya Abu Huraira, bali nataka aya halisi ya Mwenyezi Mungu." Masheikh wote wawili wakasema, "Ee mpumbavu, aya ni ya Mwenyezi Mungu, lakini Abu Huraira ameieleza." Maulawii Nidhamud Din akasema, "Hakuna haja ya maelezo yoyote, hayo ni rai tu ya mtu, sihusikani na rai au maoni ya Zaid au Bakari. Bwana Mirza anataka aya ya Kurani tu, nahitaji aya yenyewe ya Kurani juu ya uhai wa Masihi."

Wakati ambapo aya yoyote haikupatikana, Maulawii Muhammad Husain Batalawii akawa na yakini kwamba huyu mtu ametutoka mkononi mwetu. Na akamwambia Maulawii Muhammad Hasan aliyekuwa Wahabi na chifu wa Ludhiana kwamba umkatalie chakula, kwani Maulawii Nidhamud Din alikuwa akila chakula kwa Maulawii Muhammad Hasan, chifu wa Ludhiana. Kwa kusikiliza tisho la Maulawii Muhammad Husain, Maulawii Nidhamud Din kwa kutania akasema akifunga mikono yake miwili "Bwana Sheikh, naiacha Kurani, usiniachishe chakula." Kwa kusikiliza maneno haya Bwana Batalawii akafeheheka sana. Hatimaye, Maulawii Nidhamud Din alihudhuria kwa Hudhur[as]. Kwa kuona haya akakaa mbele yake akiinamisha kichwa. Hudhur[as] akamwuliza, je umeleta aya 20, 19, 10, 5, 2 hata aya moja. Kwanza Bwana Maulawii kakaa kimya, kisha akaeleza habari zote na akasema, "Sasa nipo pale palipo Kurani Tukufu." Akisema hayo akafanya baiati ya Hudhur[as]. Alipofanya baiati, masheikh wakapatwa na msukosuko, na matayarisho ya kufanya mjadala yalianza kufanyika kwa kasi zaidi."[197]

[197] Tadhkiratul Mahdi na Pir Sirajul Hak Nu'mani.

USHAHIDI WA GULAB SHAH DARWESHI

Ujaji wa wanaotumwa na Mwenyezi Mungu unapokaribia, malaika wake wanapewa jukumu la kukusanya wenye roho njema. Miongoni mwa hao wenye roho njema, mmojawapo alikuwa marehemu Mian Karim Bakhsh vile vile. Bwana huyo alikuwa mwema, mcha Mungu, mfuata suna ya Mtume[saw] na mkweli sana. Yeye alipofanya baiati ya Hudhur[as], akaeleza kuwa sababu ya baiati yake ilikuwa ni ushahidi wa Darweshi mmoja, jina lake Mian Gulab Shah. Akitaja bishara kadhaa za huyo Darweshi alisema:

> "Safari moja, miaka thelathini hapo kabla, mtawa huyo aliniambia kwamba sasa Isa ameshakuwa kijana, na atakuja Ludhiana atatoa makosa ya Kurani, na ataamua sawa na Kurani. Na akasema kwamba masheikh watakataa. Kisha akasema kwamba masheikh… watakataa. Ndipo kwa kushangaa nikauliza kwamba je, kuna makosa katika Kurani pia, Kurani ndiyo Neno la Mungu. Yeye akajibu kwamba maelezo juu ya maelezo yameandikwa na lugha ya kishairi imeenea. (Yaani kwa kupiga chuku sana, kweli zimefichwa kama vile mshairi kwa kutia chumvi anaficha hakika yenyewe.) Kisha akasema, atakapokuja Isa, ataamua sawa na Kurani. Kisha akarudia darweshi huyo na akasema hii pia kwamba ataamua kwa Kurani, lakini masheikh watakataa. Na akasema hii pia kwamba masheikh watakanusha. Na Isa atakapokuja Ludhiana njaa itaenea sana. Kisha nikamwuliza "Isa sasa hivi yupo wapi?" Hapo akajibu, "Ndani ya Qadian." Ndipo nikasema kwamba Qadian ipo umbali wa maili sita hivi kutoka Ludhiana, Isa yupo wapi hapo? (Karibu na Ludhiana kuna kijiji pia kinachoitwa Qadian.) Hakulijibu hilo, na mimi sikujua kwamba kuna kijiji katika Wilaya ya Gurdaspur pia kinachoitwa Qadian. Kisha nikamwambia kwamba Isa[as], Nabii wa Mungu, aliinuliwa mbinguni na atashuka juu ya Kaaba. Ndipo akajibu kwamba Isa Nabii wa Mungu, mwana wa Mariamu, ameshafariki hatakuja sasa, nimeshafanya utafiti vizuri sana kwamba ameshakufa. Mimi ni mfalme, sitasema uongo. Na akasema kwamba akaaye mbinguni hamwendei yeyote.

Mtangazaji: Mian Karim Bakhsh wa Ludhiana, mtaa wa Ikbal Ganj.

14 Juni 1891, siku ya Jumamosi."[198]

Baada ya kueleza hayo, Mian Karim Bakhsh akasema tena kwamba nimesahau jambo moja kulitaja, nalo ni hili kwamba Darweshi huyo aliniambia hii pia wazi wazi kwamba jina la Isa huyo ni "Ghulam Ahmad".

Chini ya taarifa hiyo kuna ushahidi wa watu karibu hamsini ambao kwa kiapo walisema kwamba Mian Karim Bakhsh ni mtu msema kweli na mwenye kushikamana na saumu na sala.

KAANDIKA NA KUCHAPISHA IZALA AUHAM

Vitabu viwili Fa'thi Islam na Taudhihe Maram, alikwisha vichapisha kwa kuthibitisha madai yake. Sasa mwishoni mwa mwaka 1891 kitabu kizuri sana "Izala Auham' pia kilichapwa katika sehemu mbili. Katika kitabu hiki cha muhimu ametoa maelezo toshelevu juu ya kifo cha Masihi na madai yake kwa uwazi jinsi wakati wa mchana kila kitu kinavyoonekana wazi pasipo shaka. Kisha akaeleza madhara ya itikadi ya uhai wa Masihi kwa kirefu kwa ufasaha sana. Akieleza manufaa ya kuamini kifo cha Masihi[as], alitoa nasaha ya thamani kwa wafuasi wake inayofaa kuandika kwa herufi za dhahabu. Anasema:

"Enyi marafiki zangu, sasa sikilizeni nasaha yangu ya mwisho. Nasema jambo la siri, likumbukeni vizuri kwamba mbadilishe njia ya mijadala yenu mnayofanya na Wakristo, na wathibitishieni Wakristo kwamba kwa kweli Masihi, mwana wa Mariamu, ameshafariki kwa kudumu. Hilo ni jambo la pekee ambamo kwa kufaulu katika hilo mtaweza kuondolea mbali dini ya Kikristo duniani. Hamna haja ya kupoteza muda wenu wenye thamani katika mabishano marefu marefu. Mkazanie tu kifo cha Masihi, mwana wa Mariam, na wanyamazisheni Wakristo kwa hoja madhubuti. Mtakapothibitisha kuwa Masihi

[198] Izala Auham, sehemu ya 2, uk. 288

yupo miongoni mwa wafu na mtakapotilia hilo nyoyoni mwa Wakristo, basi siku ile mwelewe kwamba leo dini ya Kikristo imeondoka duniani. Fahamuni kwa yakini kwamba maadamu mungu wao hafi, dini yao haiwezi kufa; mabishano mengine yote na hao ni bure tu. Kuna nguzo moja tu ya dini yao, nayo ni hii kwamba mpaka sasa Masihi, mwana wa Mariamu, yu mzima amejikalia mbinguni. Ivunjeni nguzo hii, kisha tazameni mkiinua macho kwamba dini ya Kikristo iko wapi duniani! Kwa vile Mwenyezi Mungu Anataka kuivunja nguzo hiyo vipande vipande na Avumishe upepo wa Tauhidi katika Ulaya na Asia, kwa hiyo Yeye Amenituma na Amenidhihirishia kwa ufunuo wake maalumu kwamba Masihi mwana wa Mariamu ameshafariki. Ufunuo wake ndio huu:

"Masihi mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu, ameshafariki, nawe umekuja kwa sifa zake sawa na ahadi

وَكَانَ وَعْدُ اللّٰهِ مَفْعُوْلًا ۔ اَنْتَ مَعِیَ وَاَنْتَ عَلٰی حَقِّ الْمُبِیْنِ ۔ وَاَنْتَ مُصِیْبٌ وَّمُعِیْنٌ لِّلْحَقِّ ۔ [199]

Laiti masheikh wetu wangeelewa jambo hili la muhimu na kwa kueneza itikadi hii wangewasalimisha maelfu bali malaki ya Waislamu na kuwindwa na Ukristo.

Ee kaumu ya Waislamu, bahati yako mbaya ilioje! Kwani, kati yako Jenerali mmoja wa kiroho alitokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa wakati mwafaka kwa kuvunjilia mbali fitina ya msalaba, alikupatia rundo la hoja madhubuti na imara za kutukuza Islam na kuinamisha Ukristo. Lakini, hata hivyo masheikh wako waling'ang'ania na hawakutangaza waziwazi kifo cha Masihi[as], na kwa njia hii wakasaidia kumwabudu Isa, na wakawa sababu ya kuwatumbukiza Waislamu shimoni mwa Ukristo. ***Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun.***

Ee Mungu, Ee Mwongozi, Ewe Kiongozi, Uwajalie Waislamu

[199] Izala Auham, sehemu ya 2, uk. 232, chapa kubwa, kilichoenezwa na ofisi ya Talifo Tasnif, 20 Desemba 1951. Tafsiri: Na ahadi ya Mwenyezi Mungu haina budi kutimizwa. U pamoja nami, nawe u juu ya haki iliyo wazi. Nawe umepata iliyo sawa, na u msaidizi wa haki. ─ Mwenezi.

fahamu, wajiimarishe na waachane na kuusaidia Ukristo, na wajipanie kuisaidia Islam. *Amin, Allahumma amin.*

Hapa hakuna budi kudhihirisha jambo hili kwamba Hudhur[as] alithibitisha kifo cha Masihi[as] kwa aya thelathini za Kurani Tukufu katika Izala Auham, na alileta Hadithi nyingi na hoja nyingi za kiakili na za kimaandiko, na pia alithibitisha kwa maishirini ya hoja zilizo wazi za Injili na za historia kwamba Masihi mwana wa Mariamu bila shaka ameshaaga dunia hii na anakaa katika Pepo ya juu. Hakwenda mbinguni na kiwiliwili chake cha udongo wala hatarudi, lakini ni masikitiko juu ya masheikh wa Kiislamu kwamba bado wanaendelea tu na dhana yao ya zamani sana.

Kuhusu swala hilo, msingi wa fahari wa masheikh hao, ambao kwao walikuwa wamelitegemeza jengo bovu na dhaifu la uhai wa Masihi[as], ulikuwa na maneno mawili *raf'a* na '*nuzuul*' ambayo hakika yao alieleza Hudhur[as] vizuri na sasa jengo hilo la dhana ya masheikh limeshaanguka kabisa.

CHANGAMOTO KUHUSU MAANA YA NENO TAWAFFI NA ZAWADI YA RUPIA ELFU MOJA

Katika Kurani Tukufu na Hadithi, neno Tawaffi limetumika kwa wenye akili mara maishirini bali mamia. Na kila mahala masheikh wanalifasiri 'kutakabadhi roho na kifo', lakini neno hilo hilo linapotumika kwa Hadhrat Masihi[as], basi wanalifasiri kunyanyua juu mbinguni mzima mzima na kiwiliwili chake. Hudhur[as] akieleza neno hilo kwa ufasaha aliwatupia masheikh changamoto kwamba:

> "Kama mtu yeyote alete uthibitisho kutoka katika Kurani Tukufu au Hadithi yoyote ya Mtume[saw] au beti na kasida, shairi na nathari ya zamani au ya kisasa ya Kiarabu kwamba pahala fulani neno tawaffi limetumika likiwa ni kitendo cha Mwenyezi Mungu kuhusiana na wenye roho na linatoa maana nyingine minghairi ya kutakabadhi roho au mauti, yaani limetumika kwa maana ya kutakabadhi mwili, basi nikiapa kwa jina la Allah Mwenye shani kubwa nakiri ikirari sahihi ya kisheria kwamba nitampa mtu huyo Rupia elfu kumi taslimu kwa kuuza sehemu

fulani ya milki yangu, na nitakiri tangu hapo elimu yake ya hali ya juu ya Hadithi na Kurani.”[200]

Kitabu kizuri “Izala Auham” ambamo Hudhur[as] aliwatupia masheikh mwito huu kiliandikwa katika mwaka 1891. Leo wakati ninapoandika maneno haya ni 22 Mei 1959, yaani, miaka 68 imeshapita, lakini Mwarabu au Mwajemi yeyote wa duniani kote hakujaliwa uwezo wa kukubali mwito huu na kuleta angalao mfano mmoja tu kinyume cha msimamo wa Hudhur[as]. Lakini, masheikh wakihofia tu kwamba wakikiri kifo cha Masihi[as] basi itakuwa rahisi kufahamu madai ya Bwana Mirza kuwa Masihi Mau‘udi, wanaendelea kung'ang'amia uhai wa Masihi[as]. Lakini hata hivyo baada ya kuchapishwa hoja za Hudhur[as] juu ya kifo cha Masihi[as] masheikh wengi wakalazimika kukiri kifo cha Masihi[as] wanaofikiriwa kuwa wenye daraja kubwa kwa umaarufu wao na kwa maarifa yao mapana. Miongoni mwao, majina machache ya baadhi yao ndiyo yafuatayo:

Sheikh Inshallah Khan, marehemu Mhariri wa Watan Lahore, Sheikh Ghulam Ali Kusuri, Sheikh Thanaullah Amritsari, Sheikh Abul Kalaam Aazad, Sheikh Ghulam Murshid, hatibu wa Shahi Masjid Lahore, Allama Muhammad Abduhu wa Misri, Allama Seyyid Rashid Radha wa Misri, Allama Muhmud Shaltut Mkuu wa Jamia Azhar ya Misri na kadhalika.

MADA ZINGINE ZA IZALA AUHAM

Katika Izala Auham, Hudhur[as] ameeleza vya kutosha juu ya Dajali na Yajuja Majuja pia, na kwamba muradi wa Dajali ni fitina ya Ukristo na muradi wa Yajuja Majuja ni Warusi na Waingereza. Amefafanua vizuri kuhusu Mahdi Mau‘udi pia kwamba kama Mahdi angekuwa mtu tofauti, lazima angetajwa katika Sahihi Bukhari na Sahihi Muslim. Lakini Maimamu hao wawili yaani Hadhrat Muhammad Ismaili Bukhari[ra] na Hadhrat Imam Muslim[ra] kutoandika Hadithi kuhusu Imamu Mahdi katika vitabu vyao, kunaonyesha kwamba katika maoni yao Hadithi zile hazikuwa sahihi. Naam, alisadikisha Hadithi hii iliyoandikwa na Ibni Maja na Haakim kwamba لَا مَهْدِيَّ إِلَّا

[200] Izala Auham, uk. 375, saizi kubwa.

عِيْسىٰ yaani hakuna Mahdi ila Isa tu.[201]

TANGAZO LA HADHRAT MIR NASIR NAWAB

Katika faida za mjadala wa Ludhiana, faida moja kubwa ilikuwa ni hii pia kwamba wakajiunga na Jumuiya watu wengi wenye roho njema, ni pia mkwewe Hudhur, Hadhrat Mir Nasir Nawab aliyekuwa na dukuduku kuhusu madai yake ya kuwa Masihi Mau'udi, akalazimika kuacha dhana mbaya naye, na kwa njia ya tangazo akadhihirisha kujuta kwake juu ya vitendo vyake vya zamani na kwa siku zijazo akatubu, na akaandika:

> "Baada ya sasa, kama mtu yeyote achapishe maandishi au hotuba yangu fulani na atake kujifaidisha nayo, basi mbele ya Mungu sina lawama. Na kama nilimlalamikia Bwana Mirza au nilimwambia mtu yeyote jambo lolote kuhusu Bwana Mirza basi namwomba Mwenyezi Mungu msamaha."[202]

BAIATI YA HADHRAT MAULAWII GHULAM NABII KHUSHABI

Hadhrat Maulawii Ghulam Nabii Khushabi aliyekuwa mtu mtawa, mcha Mungu na mwanachuoni mkubwa alikuwa amefika Ludhiana siku hizo hizo. Kwa sababu ya mjadala wa Ludhiana upinzani ulikuwa umechemka sana. Kwa kuona harara ya mashikh wa Ludhiana yeye pia akawa mkali kabisa kumpinga Hudhur[as]. Alikuwa hatibu mwenye kuvutia sana. Tukio lake la kujiunga na Uahmadiyya limeelezwa na Hadhrat Pir Sirajul Hak Nu'mani[ra]. Anaandika:

> "Ilmuradi, mjini Ludhiana Maulawii Ghulam Nabii Khushabi alitambulika vizuri. Hapa na pale watu walianza kuzungumzia elimu na fadhila yake. Maulawii Ghulam Nabii Khushabi naye pia hakuacha nafasi ya kumpinga Hudhur[as]. Akaanza kusoma aya juu ya aya na Hadithi juu ya Hadithi kuhusu Masihi[as]. Nijitolee kwa kudra ya Mungu! Hadhrat Umar[ra] alitoka kumwua Mtume Mtukufu[saw], lakini akauawa mwenyewe, kisha dhati yake

[201] Izala Auham uk. 518-519

[202] Tablighe Risalat, J. 2 uk. 8.

ikawa ishara ya Mungu na akaitwa Faruke A'zam. Hata mpendwa[saw] wa Mungu alisema kwamba shetani anakimbia kivuli cha Umar, na Mungu Mwenyewe Alisema kwamba Mungu Akawa radhi nao na hao wakawa radhi Naye.

"Kwa bahati, siku moja Maulawii Ghulam Nabii Khushabi aliwahutubia watu katika mtaa ule alimokaa Hudhur[as]. Maelfu ya watu walikuwa wamejumuika. Yeye akamaliza elimu yake yote katika hotuba na watu wakamshangilia sana na wakapiga kelele za takbira na marhaba na sala ya Mtume pande zote nne. Katika hotuba hiyo masheikh wote wa Ludhiana walikuwepo na wakamsifu mara kwa mara uzuri wa maelezo na elimu yake. Sheikh Muhammad Hasan, Sheikh Shaahidin, Sheikh Abdul Aziz, Sheikh Muhammad, Sheikh Abdullah na masheikh wengine wachache waliokuja kutoka nje ya mji kwa shauku ya kuona umashuhuri wa kielimu wa Maulawii Ghulam Nabii na ustadi wa ujuzi wake na umahiri aliojaliwa na Mungu, kwani huo ulikuwa ni waadhi maalumu. Sauti za takbira na makelele yote tulikuwa tunayasikia, nasi watu 4-5 tulikaa kimya na moyo ulikuwa unaudhika, nasi tulikuwa hatuna la kufanya. Hudhur[as] alikuwa nyumbani, alikuwa akitayarisha muswada wa Izala Auham. Bwana Maulawii baada ya kutoa waadhi wake na kutumia nguvu yote ya kupinga akaondoka, halaiki ya watu na masheikh walikuwa pamoja naye. Na huko Hudhur[as] akatoka nyumbani akienda kwenye sehemu ya wanaume, mara akamwona Bwana Maulawii. Hudhur[as] mwenyewe akamsalimia na akanyosha mkono. Bwana Maulawii akisema 'wa alaikumus Salaam' akapeana naye mikono. Mungu Anajua kulikuwa na nguvu gani ya umeme na nguvu gani ya kisumaku na mvuto gani wa kiroho kwamba kwa kushika tu mkono wa Hudhur, Bwana Maulawii akashindwa kujitawala na bila kusema neno akaja moja kwa moja na Hudhur[as] nyumbani katika sehemu ya wanaume wakipeana mikono, na akakaa kwa adabu mbele ya Hudhur[as]. Huko nje, masheikh na wasikilizaji waadhi wakasimama wakishangaa. Maongezi yaliyojiri baina yao ni haya: Mmoja: Jamaani imekuwaje, Bwana Maulawii amefanya

ujinga gani kwamba amekwenda na Bwana Mirza? Wa pili: Bwana Mirza ni mchawi, hatujui, pengine kamloga, haikupasa kuenda naye. Wa tatu: Bwana Maulawii hakujiweza, haiba ya Bwana Mirza ni nyingi, akashindwa na haiba. Wa nne: Anayodai Bwana Mirza ni madai makubwa; yeye si mikono mitupu, je madai hayo ni ya mtu tu hivi! Wa tano: Hakika ilivyo ni kwamba Bwana Mirza anazo pesa nyingi na masheikh huwa na tamaa, pengine Mirza amemtamanisha. Wengine: Bwana Maulawii ni mwanachuoni, ameenda kumfahamisha na kumsihi Bwana Mirza. Yeye atamsihi na atarudi baada ya kumfanya atubu. Baadhi ya wengine: Hili ndilo sawa, nafasi kama hii ya kukutana na kusihi haipatikani mara kwa mara, sasa nafasi imepatikana, atamlazimisha Bwana Mirza kutubu. Watu wa kawaida: Bwana Maulawii amenaswa, na amenaswa katika tamaa au katika elimu au kwa njia yoyote. Bwana Mirza ni mwerevu na mtaalamu hashikwi na masheikh. Masheikh kwa sauti moja: Bwana Maulawii ameenda kumkemea Mirza, mtaona Mirza anatwangwa namna gani! Maulawii hana elimu ndogo kuliko Mirza, hana tamaa, ana kazi yake, anamtambua Allah na Mtume[saw], ni mwanachuoni, atamshinda Mirza. Na zaidi ya hayo, kila mtu akasema alivyotaka. Upande wa pili, huko tamasha la kudra ya Mungu na matakwa ya Allah yalikuwa nini? Maulawii Ghulam Nabii alipoenda ndani akakaa kimya, kisha maongezi yakajiri hivi:

Bwana Maulawii: Bwana, ni kutoka wapi ulipochukulia swala la kifo cha Masihi[as]?

Hudhur[as]: Kutoka katika Kurani Tukufu, Hadithi Takatifu na kauli za maulamaa watawa.

Bwana Maulawii: Kama kuna aya ndani ya Kurani Tukufu juu ya kifo cha Masihi[as] basi niambie.

Hudhur[as]: Hii Kurani Tukufu ipo hapa. Hudhur[as] akaifungua Kurani Tukufu sehemu mbili, akaweka alama ya karatasi ndani na akampa mkononi mwa Bwana Maulawii. Sehemu moja ilikuwa ya Sura Aali Imraan, yaani robo tatu ya juzuu ya tatu, na

sehemu ya pili ni fungu la mwisho la Suratul Maaida iliyo katika juzuu ya 7. Ya kwanza ilikuwa aya: يَاعِيْسٰى اِنِّيْ مُتَوَفِّيْكَ , na ya pili: فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِيْ كُنْتَ أَنْتَ الرَّقِيْبَ عَلَيْهِمْ- . Bwana Maulawii akashangaa sana kuona aya zote mbili za sehemu mbili, na akasema: يُوَفِّيْهِمْ اُجُوْرَهُمْ pia imo katika Kurani Tukufu, hii itamaanisha nini?

Hudhur[as]: Aya nilizotoa zina maana nyingine na aya uliyotaja ina maana tofauti. Ukweli wenyewe ni kwamba hii ndiyo ***Baab*** nyingine tofauti na ***Baab*** ile. Tafakari kwa makini na uzingatie.

Bwana Maulawii: Baada ya kutafakari dakika 2-4 akasema, "Samahani, nilikosea, uliyosema ni sahihi. Kurani Tukufu ipo pamoja nawe. Hudhur[as] akasema, "Kama Kurani Tukufu ipo pamoja nami, basi wewe upo pamoja na nani? Bwana Maulawii akaanza kulia, machozi yakatiririka machoni, akashikwa na kwikwi na kasema, mimi mwenye kosa na mwenye dhambi nipo pamoja na Hudhur. Bwana Maulawii akaendelea kulia na kukaa mbele yake kwa adabu…

Bwana Maulawii alipokawia sana ndani, watu walianza kulalamika na kupaza sauti wakisema, 'Bwana Maulawii, tafadhali njoo nje.' Bwana Maulawii hakutikia sauti yao hata kidogo. Ulipopita muda mwingi wakapiga makelele sana, hapo Bwana Maulawii aliwapelekea ujumbe, "Nendeni, nimeshaona haki na nimeipata, sasa sihusikani nanyi. Mkitaka na kupenda kubakiza imani yenu salama, basi njooni na kwa kutubu mpate kufaulu mbele ya Mwenyezi Mungu na mwaminini Imamu huyu. Nawezaje kutengana na huyu Imamu mkweli aliyeahidiwa na Mwenyezi Mungu na pia ameahidiwa na Mtume wake s.a.w. ambaye Mtume[saw] alimtumia salamu. Na Hadithi ile takatifu ndiyo hii: مَنْ اَدْرَكَ مِنْكُمْ عِيْسَى ابْنَ مَرْيَمَ فَلْيُقْرِئْهُ مِنِّيْ السَّلَامَ . Bwana Maulawii akisoma Hadithi hii akamwelekea Hudhur[as] na akasoma Hadithi hiyo hiyo kwa sauti kubwa na akasema kwamba sawa na amri ya Mtume Mtukufu[saw] nakuambia salamu ya Mtume[saw], na kwa upande wangu pia nasema salamu ya daraja ile aliyosema mwenye kusalimu na kwa yule aliyesalimiwa sawa na daraja hiyo. Wakati ule Hudhur[as] kwa tamshi na sauti ya ajabu alisema

wa alaikumus salam hata kwamba nyoyo hazikuweza kuvumilia. Bwana Maulawii akagaagaa kama kuku aliyechinjwa. Wakati huo sura ya uso wa Hudhur[as] pia ilikuwa tofauti ambayo siwezi kueleza katika maandishi. Wahudhuriao na wasikilizaji pia walikuwa wamejaa furaha ya ajabu. Kisha Bwana Maulawii alisema kwamba mawalii na maulamaa walituma salamu na wakimsubiri waliaga dunia. Leo maandiko ya Mungu na ahadi yake imetimia, mimi Ghulam Nabii nimwacheje! Huyu ni Masihi Mau'udi na huyu ndiye Imam Mahdi Mau'udi, ndiye huyu, ndiye huyu. Masihi bin Mariamu wa Musa ameshafariki, ameshafariki, ameshafariki, bila shaka ameshafariki. Yeye hatarudi. Mwenye kuja ameshakuja, ameshakuja, ameshakuja, bila shaka ameshakuja. Ondokeni nyie au kama mimi mwangukie katika miguu yake mitakatifu ili mwokoke, Mwenyezi Mungu Awaridhie na Mtume[saw] afurahi nanyi.

Wenye kusubiri nje walipopata ujumbe huu wa Bwana Maulawii, masheikh na watu wote walipiga makelele ya "kafiri, kafiri, kafiri" na wakatukana na wote wakafumukana. Wakisema maneno mabaya watu wote wakatawanyika mitaani ambao wakasema. "Mirza ni mchawi, yeye ameshinda".[203]

SAFARI YA DELHI, 28 SEPTEMBA 1891

Mnamo 28 Septemba 1891, Hudhur[as] pamoja na mahadimu wachache alifika Delhi, mji mkuu wa India, ulio pia makao makuu ya elimu na ujuzi, na akakaa katika jumba la Nawab Luharu. Lengo la Hudhur[as] lilikuwa kwamba kwa kutangaza madai yake katika Delhi, ujumbe wake utafika katika India nzima. Kwa hiyo, Hudhur[as] alichapisha matangazo matatu mfululizo kwa ajili ya maulamaa wa Delhi na hasa kwa ajili ya Seyyid Nadhir Husain mwenye lakabu ya Sheikhul-kul. Tangazo la kwanza alichapisha tarehe 2 Oktoba 1891 kwa kichwa cha habari "Tangazo la msafiri mnyonge kwa Waislamu wote waadilifu na masheikh mashuhuri kwa kuzingatia." Katika tangazo hili, Hudhur[as] aliandika itikadi zake na aliwakaribisha Sheikh

[203] Tadhkiratul Mahdi sawa na Hayate Ahmad, J. 3 uk. 137-139

Seyyid Nadhir Husain na Sheikh Abu Muhammad Abdul Hak kwa mjadala juu ya uhai na kifo cha Masihi[as]. Akawaandikia kwamba kwa mjadala huu, kushikamana na masharti matatu kutakuwa lazima:

La kwanza: Kwa kudumisha amani mfanye ninyi wenyewe mpango wa serikali, yaani afisa mmoja Mzungu awepo katika kikao cha mjadala.

La pili: Mjadala huu uwe wa kimaandishi, na maswali na majibu yaandikwe katika kikao cha mjadala.

La tatu: Sharti la tatu ni kwamba mjadala uwe juu ya kifo na uhai wa Masihi[as], na mtu yeyote asiende nje ya Kurani na Hadithi.

Na aliandika hii pia kwamba nakiri kwa kuapa kuwa katika mjadala huu kama nikiwa mwenye kosa, basi nitaacha mwenyewe dai la pili (kuwa Masihi Mau'udi). Baada ya kuchapisha tangazo hili nitasubiri jibu sahihi la hao jamaa.

Baada ya kuchapwa kwa tangazo hilo, Sheikh Abu Muhammad Abdul Hak alimfikia Hudhur[as] na akatoa udhuru kwamba mimi ni mtu wa kukaa peke yangu na sipendi kuhudhuria katika mikutano ya aina hiyo. Kwa vile Maulawii Muhammad Husian pia alikuwa ameishi Delhi, yeye alichapisha tangazo kulikabili tangazo la Hudhur[as] na humo aliandika kuhusu Hudhur[as] kwamba "Huyu ni windo langu, kwa bahati yake mbaya limekamatwa na mimi tena katika Delhi, nami nina bahati nzuri kwamba nimepata windo tena aliyekimbia."

Akachokoza sana, kwa hiyo Hudhur[as] alichapisha tarehe 6 Oktoba 1891 tena tangazo moja, kichwa chake cha habari kilikuwa hiki: "Tangazo kumkabili Maulawii Seyyid Nadhir Husain, Mkuu wa Ahle Hadithi." Katika tangazo hili Hudhur[as] aliwaandikia Maulawii Seyyid Nadhir Husain na Maulawii Muhammad Husain Batalawii, wote wawili, kwamba:

> "Kama masheikh wote hao wawili wako juu ya haki katika kusema kuwa Hadhrat Masihi mwana wa Mariamu yu hai, basi wajadiliane nami kwa masharti yaliyoandikwa katika tangazo la 2 Octoba 1891."

Na kwa kukamilisha hoja aliandika hii pia kwamba kama Maulawii Seyyid Nadhir Husain akishindwa kufanya mpango wa kuleta afisa Mzungu yeyote katika kikao cha mjadala, basi akiri kwa kuapa katika tangazo kwamba sisi wenyewe tu wadhamini wa kudumisha amani. Na kama mtu yeyote miongoni mwa wahudhuriao atatamka neno lolote kinyume cha ustaarabu na adabu, basi sisi wenyewe tutamtoa mara moja katika kikao. Katika hali hii pia twaweza kuhudhuria katika msikiti wa Bwana Maulawii kwa mjadala.

Baada ya kuchapishwa tangazo hili la pili, wanafunzi wa Maulawii Seyyid Nadhir Husain wenyewe wakipanga tarehe walichapisha tangazo kwamba tarehe fulani mjadala utafanyika na Bwana Mirza, lakini hawakushauriana na Hudhur[as] kabla ya wakati. Bali, wakati hasa wa mkutano walimtuma mtu mmoja kwa Hudhur[as] kwamba twende kwa kujadiliana, Maulawii Seyyid Nadhir Husain anakusubiri kwa kufanya mjadala. Na papo hapo watu wengi wenye hasira wakazingira nyumba ya Hudhur[as], na Hudhur[as] juu ya kuwa tayari hakuweza kutoka nje kwa mjadala. Hapo watu hao wakaeneza kwamba Bwana Mirza amemwogopa Sheikhulkul. Ndipo tarehe 17 Oktoba 1891 alichapisha tangazo la tatu ambalo lilikuwa na kichwa cha habari:

> "Ombi kwa Maulawii Seyyid Nadhir Husain, kwa kuapisha kwa jina la Allah mwenye shani kubwa, kufanya mjadala juu ya uhai na kifo cha Masihi mwana wa Mariamu".

Katika tangazo hili akitaja mkutano ule ambamo yeye hakuweza kuhuduria alisema:

> "Ijapokuwa kuhudhuria katika mkutano wa upande mmoja tu hakukuwa lazima kwangu kwani mkutano huo haukupangwa kwa rai yangu wala haikuwa ahadi pia kutoka kwangu kuhudhuria katika tarehe maalum, hata hivyo nilijiandaa kwa kuhudhuria lakini mashambulio ya ufisadi ya watu yaliyofanywa ghafla yalinizuia kuhudhuria siku ile. Mamia ya watu ni mashahidi wa jambo hili kwamba katika wakati hasa wa mkutano ule wafisadi walijumuika wengi sana kwenye nyumba yangu, na nikiona hali ya uhuni wao nikaenda ghorofani kwenye

sehemu ya akinamama. Hatimaye hao walikuja pale na wakaanza kuvunja milango ya nyumba hata kwamba baadhi ya watu waliingia katika sehemu ya akinamama. Na watu wengi walisimama chini na mtaani ambao walitusi na kwa harara sana waliendelea kuonyesha ghadhabu yao kwa kutukana. Kwa taabu sana na kwa fadhili na msaada wa Mwenyezi Mungu tulisalimika nao."

Kwa kusonga mbele Hudhur[as] akasema:

"Basi, upande mmoja kwa kuwalaghai watu na kwa kuwatolea hotuba za kuwachemsha waliwaleta watu kuizingira nyumba yangu na upande mwingine waliniita kujadili, kisha kwa kukosa kufika kwa sababu ya mazuio yaliyotajwa, walipiga makelele kuwa niliepa."

Kisha Hudhur[as] akaandika:

"Sasa kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu nimeshafanya mpango wa kujilinda na niko tayari kufanya mjadala. Kwa kuvumilia shida za safari na kustahimili kila siku matusi na laana za Wadelhi nimekaa kwa kujadili tu nawe Ewe Sheikhulkul, njoo, Bwana, kwa kujadili, niko tayari kwa mjadala. Tena nakukaribisha kwa kujadili kwa kuapisha kwa Mungu Mwenye shani kubwa. Popote utakapataka nitahudhuria, lakini mjadala utakuwa kimaandishi."

Hatimaye Hudhur[as] aliandika hii pia:

"Kama hutaki kufanya mjadala kwa vyovyote, basi kwa kusikiliza katika kikao kimoja hoja zangu zote juu ya kifo cha Masihi[as], useme kwa kuapa kwa jina la Mungu Mwenye shani kubwa kwamba hoja hizo si sahihi; jambo lililo sahihi na la yakini ni hili tu kwamba Hadhrat Masihi mwana wa Mariamu amenyanyuliwa mbinguni kwa kiwiliwili chake, na aya za Kurani kwa dalili wazi na Hadithi sahihi *muttasil marfu'* pia zinashuhudia dhahiri shahiri juu yake na itikadi yangu ni hii hii. Hapo kwa sababu ya ujasiri wako na kuficha haki, uhaini na ushahidi wako wa uongo nitamwomba Mwenyezi Mungu sana kwa

unyenyekevu ili kutoa uamuzi. Kwa vile kwa mwelekeo wangu nimeshaambiwa اُدْعُوْنِي اَسْتَجِبْ لَكُمْ na nimehakikishiwa kwamba kama wewe ukiacha njia ya ucha Mungu utakosa adabu namna hii na hutajali aya لَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهٖ عِلْمٌ, basi katika muda wa mwaka mmoja utapata athari yake wazi wazi kwa ujasiri wako, ambayo itakuwa ishara kwa wengine. Kwa hiyo nasema kwamba kama hutaki mjadala basi uamue kwa njia hiyo ili watu ambao wanang'ang'ania kuona ishara, Mwenyezi Mungu Awaonyeshe ishara. Naye Yeye Anao uwezo juu ya kila kitu. Na kauli yetu ya mwisho ni ***Alhamdu lillahi rabbil aalamina.***

ZAWADI KWA KUTHIBITISHA UHAI WA MASIHI KUTOKA KURANI NA HADITHI

Katika tangazo hilo hilo aliandika hii pia:

"Hatimaye, hii pia ibainike kwa Maulawii Seyyid Nadhir Husain kwamba kama alete aya zilizo wazi na Hadithi sahihi ***muttasila marfu'a*** katika kikao cha mjadala kwa kuunga mkono itikadi yake kwamba Hadhrat Masihi mwana wa Mariamu alinyanyuliwa mbinguni na kiwiliwili chake, na kama ilivyo lazima kwa jambo fulani liwe itikadi aeleze kwa ulimi wake uthibitisho wa yakini wa kunyanyuliwa kwa Masihi mwana wa Mariamu pamoja na kiwiliwili, katika mkutano wa hadhara, basi nafanya ikirari sahihi ya kisheria kwa kuapa kwa jina la Mungu Mwenye shani kubwa kwamba nitamkabidhi Rupia 25 kwa kila aya na kila Hadithi."

TAARIFA KWA MUHTASARI YA MKUTANO WA MJADALA WA 20 OKTOBA 1891

Ijapokuwa Hudhur[as] kwa njia ya matangazo alisisitiza sana jambo hili pia kwamba Maulawii Nadhir Husain ajadiliane naye kimaandishi juu ya uhai na kifo cha Masihi[as], na watu wa Delhi nao walitaka hivyo, lakini Maulawii Seyyid Nadhir Husain hakukubali kujadiliana juu ya uhai na kifo cha Masihi[as] wala hakukubali pendekezo lake kwamba Hudhur[as] aeleze hoja za kifo cha Masihi[as] ambazo baada ya kuzisikiliza Bwana Maulawii aseme kwa kiapo kwamba hoja hizo si sahihi sawa na aya za Kurani na Hadithi zilizo sahihi. Hapo Hudhur[as] aliwatuma Hadhrat Munshi Zafar Ahmad Kapurthalwi na Hadhrat

Khan Muhammad Khan Kapurthalwi waende na barua yake kumpelekea Maulawii Nadhir Husain. Hadhrat Munshi Zafar Ahmad anasema:

> "Katika barua hii Hudhur[as] aliandika kwamba kesho tutafika katika Msikiti wa Ijumaa, kama hutafika, itakuwa laana ya Mungu. Tulipoenda na barua hiyo, Maulawii Nadhir Husain alisema kwamba nendeni nje mkakae na Maulawii Muhammad Husain Batalawii, mpeni barua, nami ninakuja. Maulawii Muhammad Husain alifungua barua ile. Kisha Maulawii Nadhir Husain akaja na akamwuliza Maulawii Muhammad Husain kwamba imeandikwa nini katika barua. Maulawii Muhammad Husain kasema siwezi kukusomea; umetukanwa sana. Wakati huo Chifu mmoja wa Delhi pia alikuwepo hapo na yeye pia alikuwa ameisoma barua ile. Yeye alisema hamna matusi katika barua. Maulawii Nadhir Husain akasema, je wewe pia umekuwa Mirzai? Yeye akanyamaa. Nilimwambia Maulawii Nadhir Husain toa jibu utakalo kutoa. Maulawii Nadhir Husain alisema hatutoi jibu, nyinyi mwende tu. M wajumbe, mmeishafikisha barua. Tulisema tutaenda na jibu tu. Kisha watu walisema acheni tu. Ilimuradi, yeye hakujibu. Tukarudi na kumwelezea Hudhur[as] habari yote. Keshoye sisi sote tulikwenda katika Msikiti wa Ijumaa. Pamoja na Hudhur[as] tulikuwa watu 12. [204] Tukiishafika tulikaa kwenye mlango wa kati wa msikiti wa Ijumaa."

Habari za baadaye, sikilizeni kwa mdomo wa Hadhrat Pir Sirajul Hak Nu'mani[ra]. Yeye anasema:

> "Katika muda huo Maulawii Nadhir Husain, na pamoja naye wakaja Maulawii Muhammad Husain na Maulawii Abdul Majid

[204] Miongoni mwao, majina ya wachache ni haya: Bwana Muhammad Khan, Bwana Sheikh Rahmatullah, Bwana Munshi Arurha Khan, Bwana Hafidh Haamid Ali, Bwana Maulawii Abdul Karim, Bwana Muhammad Said aliyekuwa mwana wa dada ya Mir Nasir Nawab na Bwana Munshi Zafar Ahmad, msimulizi wa riwaya hii. Msimulizi anasema: Nafikiri kwamba Bwana Seyyid Amir Ali na Bwana Seyyid Khasilat Ali wa Sialkot pia walikuwepo.

na maulamaa wengine na wakampeleka Maulawii Nadhir Husain katika uga na hawakumleta mbele ya Hudhur[as]... Kisha sala ya alasiri ilisaliwa... Watu walitaka na hao pia washiriki katika sala... Mmoja wao akasema njooni kusali. Maulawii Abdul Karim kasema, tumekuja kwa kujumuisha sala mbili... Baada ya sala tena masheikh wakajumuika kwa Maulawii Nadhir Husain na kumwongoza kwenye uga uliokuwa upande wa kaskazini wa mlango na kumkalisha hapo... Maulawii Abdul Majid na masheikh wengine kadhaa wakaja na walianza kuzungumza na afisa wa polisi. Upande wetu Munshi Ghulam Qadir Fasih alijibu sana maswali na aliongea ilivyokuwa haki ya kuongea. Maulawii Abdul Majid alimwambia afisa wa polisi kwamba mtu huyu anadai kuwa Masihi Mau'udi na anatufikiria, wewe na sisi, kuwa tumepotea. Hadhrat Masihi mwana wa Mariamu ambaye wewe na sisi tuna yakini kwamba yuko hai mbinguni, yeye anamfahamu yu miongoni mwa wafu. Yeye anasema Maulawii Nadhir Husain ajadiliane naye juu ya uhai na kifo cha Masihi[as]. Nasi tunasema kwamba tujadili juu ya madai yake hasa ya kuwa Masihi Mau'udi. Bwana Ghulam Qadir Fasih alimwambia afisa polisi, miongoni mwa mambo mengine, angalia Bwana mkubwa, mtu hawezi kustahili kupewa cheo fulani maadamu nafasi haipo. Kwa hiyo, kwanza habari ya uhai na kifo cha Masihi[as] ijadiliwe, kisha izungumzwe habari ya yeye kuwa Masihi Mau'udi. Bado wanafikiri kwamba Masihi[as] yu mzima. Kama uhai wa Masihi[as] ukithibitika basi itakuwa bure kujadili madai ya Hudhur[as] kuwa Masihi Mau'udi. Madai hayo yenyewe yatabatilika. Na kama kifo cha Masihi[as] kikithibitika, hapo italazimika kujadili kuhusu madai yake ya kuwa Masihi Mau'udi... Afisa Polisi akasema, bila shaka jambo hili ni sahihi. Kwa nini nyinyi hamjadili juu yake. Afisa huyo akashikilia sana jambo hili. Kisha iliongelewa kuhusu kuapa, lakini watu hao wakakataa hii pia. Wakasema, sheikh wetu ni mzee, dhaifu, mwenye umri mkubwa. Hatutaapa wala hatutamhimiza sheikh wetu kuapa. Hudhur[as] anasema kwamba kwa bahati katika kikao hicho alikuwepo pia Khwaja Muhammad Yusuf, Jaji wa

Aligarh. Yeye baada ya kusikiliza udhuru mbovu wa kundi la pili aliniuliza, je ni kweli kwamba kinyume na itikadi za Wasuni unakataa Lailatul Kadri, miujiza, Malaika, na Mi'raji, na unadai unabii? Nikasema, huu ni uwongo walionizulia. Naamini mambo hayo yote. Watu hao hawakuelewa kusudio la vitabu vyangu, na kwa kutoelewa wamenichukulia kuwa nazikana itikadi za Wasuni. Hapo yeye akasema, sawa kabisa; kama ukweli ni huu basi niandikie mambo hayo yote juu ya karatasi moja, sasa hivi nitamsomea hayo Mkuu wa Polisi wa Mji na watu wote, na nitakwenda pia Aligarh na nakala yake moja. Basi, nilimwandikia kwenye karatasi yaliyoandikwa hapa chini kama tanbihi.[205] Na Bwana Khwaja alimsomea kwa sauti kubwa Mkuu wa Polisi wa Mji, na wahudhuriao waliokuwa karibu pia waliisikia.

---

[205] **Maelezo Ya Kimaandishi Ya Hudhur[as]**

"Bismillahir Rahmanir Rahim. Nahmaduhu wa nusalli

Ibainike kwamba swala la hitilafu ambalo ningependa kujadili ni kwamba dai hili kuwa Masihi[as] mwana wa Mariamu amenyanyuliwa mbinguni na kiwiliwili chake, katika rai yangu halithibitiki. Na miongoni mwa Aya za Kurani na Hadithi, hata Aya moja inayohakikisha kwa uwazi au Hadithi sahihi *muttasil marfu'* hata moja haiwezi kupatikana itakayoweza kuthibitisha uhai wa Masihi[as]. Bali, katika mahali mbalimbali aya nyingi wazi za Kurani Tukufu na Hadithi sahihi *muttasil marfu'* zinathibitisha kifo tu. Wakati huu nasema kwa ikrari sahihi ya kisheria kwamba kama Hadhrat Maulawii Seyyid Muhammad Nadhir Husain akithibitisha uhai wa Masihi[as] kwa aya wazi na Hadithi sahihi, basi nitaachana mwenyewe na madai mengine ya kuwa Masihi Mau'udi, na nitatubu mbele ya Bwana Sheikh, bali nitavichoma vitabu vyangu kuhusu somo hilo. Na lawama zingine kwamba mtu huyu anakana lailatul kadri, miujiza na mi'raji na anadai unabii na anakanusha Khatme Nubuwwat, lawama hizo zote ni batili na ni uongo mtupu. Katika mambo hayo yote ninayo imani ile ile iliyo ya Masuni wengine. Na shutuma zilizotolewa kutoka katika vitabu vyangu *'Taudhihi Maram'* na *'Izala Auham'* , ni kosa kabisa la wapinzani. Sasa nakiri waziwazi kwa mambo yafuatayo mbele ya Waislamu katika msikiti, nyumba hii ya Mungu, kwamba naamini Khatme Nubuwwat ya Hadhrat Khatamul Ambiyaa[saw], na mtu anayekana Khatme Nubuwwat namfahamu kuwa hana dini, na yuko nje ya duara la Islam. Kadhalika naamini malaika, miujiza, lailatul kadri na kadhalika."

"Kisha baada yake, Bwana Khwaja alisisitiza kwamba kama hakuna hitilafu ya maana katika itikadi hizo, makundi yote mawili yanaafikiana pamoja, basi yawezaje kuwa mjadala juu yao. Jambo lile lapaswa kujadiliwa ambalo makundi mawili yanahitilafiana ndani yake, yaani swala la uhai na kifo cha Masihi[as]. Hili litakapoamuliwa, yataamuliwa mambo yote. Bali kwa kuthibitika uhai wa Masihi[as], madai ya kuwa Masihi Mau'udi yatabatilika papo hapo. Akasema hii pia akitaja jina langu mara kwa mara kwamba yeye ameahidi mwenyewe kwamba uhai wa Masihi[as] ukithibitika kwa hoja wazi za Kurani na Hadithi, basi nitaacha madai ya kuwa Masihi Mau'udi."

Hudhur[as] anasema:

"Lakini ingawaje Bwana Khwaja alisisitiza kuwa kundi la pili likiacha ukaidi na uadui lianze kujadili juu ya uhai na kifo cha Masihi[as], juhudi hizo zote zikawa bure. Sheikhulkul aliona mauti katika kujadili hilo, kwa hiyo alikataa katakata na wahudhuriao wakavunjika moyo. Nimesikia kwamba mtu mmoja alikuwa akisema kwa uchungu sana kwamba leo Sheikhulkul ameharibu kabisa heshima ya Delhi na ametufedhehesha sana. Baadhi yao wakasema kwamba kama sheikh wetu angekuwa juu ya haki basi lazima angejadiliana na mtu huyu."

Hadhrat Munshi Zafar Ahmad Kapurthalwi anasimulia:

"Upande huu mambo hayo yaliendelea kuzungumzwa, na upande ule watu wakazidi kupandwa na hasira. Katika hali hiyo Kapteni wa polisi aliyekuwa Mwingereza alimwuliza Hudhur[as] kwamba una shabaha gani ya kuja hapa? Sheikh Rahmatullahi alimjibu kwa Kiingereza kwamba Hudhur[as] amekuja ili aeleze hoja za kifo cha Hadhrat Masihi[as], na Maulawii Nadhir Husain aseme kwa kuapa kwamba sawa na rai yangu hata sasa pia inathibitika hii tu sawa na Kurani na Hadithi kwamba Hadhrat Masihi[as] yupo mzima huko mbinguni. Kisha yeye Kapteni alimwendea Maulawii Nadhir Husain na alimwuliza kwamba unakubali kuapa hivyo? Yeye kasema kwamba sitaapa. Yeye akaja kumwambia Hudhur[as] kwamba huyo hayuko tayari kuapa

baada ya kusikiliza hoja zako, kwa hiyo inapasa uende. Akisikia hii Hudhur[as] akasimama ili kuondoka. Mimi (yaani Hadhrat Munshi Zafar Ahmad Kapurthalwi) nikishika mkono wa Hudhur[as] nikamwomba kusubiri kidogo. Nami nikamwambia Sheikh Rahmatullah kwamba amwambie Kapteni wa Polisi kwamba kundi la pili liondoke kwanza, kisha tutakwenda. Hapo yeye aliwaambia lakini wakang'ang'ania kwamba kwanza hao wanapaswa waondoke. Ilmuradi, baada ya kuhojiana kidogo Kapteni wa Polisi alisema kwamba makundi yote mwili yaondoke pamoja. Basi, tukainuka. Sisi watu 12 tulimzingira Hudhur[as] na polisi walituzingira... Tulipotoka kutoka mlango wa upande wa Daribe, gari letu lililotuleta, watu wa Delhi walikuwa wameliondoa. Kapteni wa Polisi akatupatia gari la farasi la magurudumu manne. Inspekta polisi akawa juu ya kiti cha dreva, Ma-inspekta wadogo wawili juu ya mbao mbili za kukanyagia mtu anapoingia garini, na nyuma walikuwa mapolisi ndani ya gari. Ndani ya gari walikuwepo Hudhur[as], Bwana Muhammad Khan, Bwana Munshi Arurhe Khan, mimi na Hafiz Haamid Ali, hata hivyo gari liliendelea kutupiwa changarawe na nawe. Tuliondoka, Maulawii Abdul Karim alibaki nyuma. Bwana Muhammad Khan akashuka haraka. Watu walikuwa wamemzingira Bwana Maulawii. Walipomwona Bwana Muhammad Khan wakamwacha, na Bwana Muhammad Khan akamleta salama Bwana Maulawii."[206]

SILAHA YA MAULAMAA WA DELHI YA KUKUFURISHA NA KUCHOCHEA

Kwa sababu ya uchokozi wa maulamaa wa Delhi, wahuni na watu waovu wa mji walichemka kiasi hiki kwamba mamia ya hao wakajumuika na kushambulia nyumba ya Hudhur[as]. Ilikuwa karibu wavunje mlango wa nyumba ya upande wa wanawake, lakini kwa sababu ya ulinzi wa wafuasi wajitoleao wa Hudhur[as] hawakuweza kufaulu. Wakapiga kelele na kuleta ghasia mitaani mwa mji na kusema maneno ya dhihaka. Wakaeneza vipeperushi vyenye maneno

[206] Kutoka As-habe Ahmad, J. 4, uk. 129-130, kimuhtasari.

ya kishenzi, majivuno na uongo. Fatuwa ya kumkufurisha Hudhur[as] kutoka kwa maulamaa ilisambazwa katika mitaa ya Delhi.

MJADALA NA MAULAWII MUHAMMAD BASHIR BHUPALAWII, 23 OKTOBA 1891

Jinsi alivyoshindwa vibaya Maulawii Seyyid Nadhir Husain wa Delhi katika kukabiliana na Hudhur[as], watu wa Delhi waliona vibaya sana, hasa Ahle Hadithi walijaribu sana kwamba kwa vyovyote lazima mjadala ufanyike juu ya swala la uhai na kifo cha Masihi[as] na Bwana Mirza. Kwa lengo hilo watu wa Alijan waliokuwa wafanya biashara wa kofia, walimchagua Maulawii Muhammad Bashir Bhupalawii. Maulawii Muhammad Bashir alikuwa mkazi wa Sehsawan Wilaya ya Badayun, na alikaa kikazi katika Bhopal akiwa miongoni mwa kundi la masheikh wa Nawab Siddik Hasan Khan. Na hapo Hadhrat Seyyid Muhammad Ahsan Amrohi pia alikuwa anafanya kazi. Hao wote wawili walikuwa na mahusiano makubwa kati yao. Hudhur[as] alipodai, hao wote wawili walianza kujadiliana baina yao. Hadhrat Seyyid Muhammad Ahsan alikuwa akithibitisha madai, na Maulawii Muhammad Bashir alikuwa aliyapinga. Hatimaye wote wawili waliafikiana kwamba Hudhur[as] ndiye mkweli katika madai yake. Hapo Hadhrat Seyyid Muhammad Ahsan Amrohi alijasiri na alifanya baiati ya Hudhur[as], lakini Maulawii Muhammad Bashir akaendelea kufikiri tu. Baada ya kumalizika kazi katika Bhopal, yeye akaja Delhi. Hapo alipata uimamu wa kundi la Ahle Hadith, na ni masikitiko kwamba kitu hiki hiki kikawa kizingiti chake asijiunge katika Jumuiya.

Alipotaka mjadala, Hudhur[as] aliukubali kwa furaha. Hatua hii ya Maulawii Muhammad Bashir kwa kweli yapaswa kusifiwa sana kwamba kinyume cha mwenendo wa Maulawii Muhammad Husain Batalawii na Maulawii Seyyid Nadhir Husain wa Delhi, akiacha mambo yasiyofaa, alikubali kujadili juu ya swala lenyewe la uhai na kifo cha Masihi[as]. Ingawa alikwama katika mzozo wa ***Nuun Thaqila*** lakini kwa vyovyote alisafisha njia ya kutafakari kwa watafutao haki.

Mjadala huu ulianzia tarehe 23 Oktoba 1891 baada ya sala ya Ijumaa. Maulawii Muhammad Bashir aliandika makala tatu na Hudhur[as] pia aliandika tatu tu. Makala hizo za pande zote mbili zimechapishwa

tayari kwa jina la "Mubahatha Al Hak Delhi" na yaweza kuwa mwenge wa njia kwa kuchunguza swala la uhai na kifo cha Masihi Mnazareti.

HOTUBA YA HUDHUR[AS] KWA MAULAWII MUHAMMAD BASHIR

Hadhrat Pir Sirajul Hak Nu'mani[ra] anasimulia kwamba Maulawii Muhammad Bashir, pamoja na marafiki, zake alipofika nyumbani kwa Hudhur[as] kwa lengo la mjadala na wakakaa mbele ya Hudhur[as], hapo Hudhur[as] akizungumza na Bwana Maulawii na wenzake akasema:

> "Bwana Maulawii, naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba madai yangu ya kuwa Masihi Mau'udi ni ya kweli kama yalivyokuwa ya kweli madai ya unabii na utume ya manabii wengine. Msingi wa madai haya ni kwamba kwa miezi kadhaa mfululizo nilifunuliwa kwamba Masihi mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu ameshafariki, na Masihi Mau'udi aliyetabiriwa kuja ndiye wewe. Niliambiwa, nilifahamishwa mfululizo kwa kashfi, kwa ufunuo na kwa ruya, hata hivyo sikuwa na yakini. Lakini, baada ya miezi kadhaa jambo hilo lilipofikia daraja la mfululizo, yakini kamili na yakini ya haki, ndipo nilifungua Kurani Tukufu na nikafikiri kwamba inapaswa nilinganishe ufunuo wangu kwa Kitabu cha Mungu. Kwa kufungua tu Kurani Tukufu, aya ya Suratul Maaida فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي ikatokea. Nilipoitafakari, nilizikuta funuo, kashfi na ruya zangu kuwa sahihi, na ikawa wazi kwangu, na ikathibitika kwamba bila shaka kuwa Masihi mwana wa Mariamu[as] ameshafariki. Kisha nikaisoma Kurani Tukufu kutoka mwanzo mpaka mwisho kwa makini na kutafakari sana, basi ukapatikana uthibitisho wa kifo cha Masihi[as], na haukupatikana uthibitisho wowote wa uhai wa Masihi[as]. Kisha nikafungua Sahihi Bukhari. Ni kudra ya Mungu, nilipofungua tu mara zikatokea aya mbili za Kitabut Tafsir, moja ilikuwa إِنِّي مُتَوَفِّيكَ na ya pili فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي. Tafsiri ya moja مُمِيتُكَ ilikuwa imetolewa na Ibnu Abbas[ra], na tafsiri ya pili ilifanywa na Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe. Kana kwamba Imam Bukhari

> alidhihirisha itikadi yake kwa kujumuisha pamoja aya mbili zilizopo katika sehemu tofauti, kwamba kwa aya hizo mbili kifo cha Masihi[as] tu kinathibitika na hakuna kitu kingine. Kisha nikasoma Sahihi Bukhari nzima neno kwa neno kutoka mwanzo mpaka mwisho, humo pia sikukuta neno lolote la uhai hata kwa ishara au kwa kinaya, isipokuwa kifo tu. Kisha nikasoma neno kwa neno Sahihi Muslim na vitabu vingine vyote vya Hadithi na kwa makini sana nilisoma kila mstari na kila herufi, lakini sikukuta uhai wa Masihi[as] isipokuwa mauti. Naam, Hadithi kuhusu *nuzuul* ─ kushuka ─ zinazotajwa, haimo huko 'kushuka kutoka mbinguni'. Ushukaji na uhai unahusikaje? Wakati ambapo kuwa hai na kunyanyuliwa mbinguni hakuthibitiki, basi kushukuka kuna maana gani? Msafiri pia anaitwa katika Kiarabu naziil ─ mshukaji ─ kama vile nimeshuka sasa katika Delhi."

Ilikuwa bado haijaisha hotuba yake, Maulawii Muhammad Bashir akifadhaika akasema, ukiniruhusu, nikae kule kwenye kona ya mbali ya uga na niandike kitu. Hudhur[as] akajibu, haya, kaa popote utakapo. Basi Bwana Maulawii akaenda kwenye kona ya mbali na akaanza kumwandikisha makala Mujadid Ali Khan. Hudhur[as] alisema kwamba sharti liliwekwa kwamba akikaa karibu ataandika mwenyewe kwa kalamu yake wakati ule ule kwa sura ya maswali na majibu, lakini Bwana Maulawii akikaa mbali anamwandikisha mwingine. Nikasema je, nimwambie hili Bwana Maulawii? Akasema mwache, aandike au aandikishe."[207]

Hadhrat Munshi Zafar Ahmad Kapurthalwi anasimulia:

> "Kisha, Maulawii Muhammad Bashir alipokwishaandikisha makala, tuliyapeleka kwa Hudhur[as], akasema simama hapa hapa, majibu yakiisha andikwa tayari, uyapeleke kwa jamaa kutayarisha nakili yake. Niliona kwamba Hudhur[as] akaitupia jicho makala ile ukurasa baada ya ukurasa, akipitisha kidole kila ukurasa, aliona kila karatasi moja na akaiweka kando. Ilionekana

[207] Hayate Ahmad, J. 3 uk. 182-183

hakuisoma, aliitupia tu jicho na akaanza kuandika jibu. Karatasi mbili zilipokwisha andikwa nilizipeleka chini kutayarisha nakili yake. Karatasi moja alianza kunukuu Maulawii Abdul Karim na nyingine Abdul Quddus. Kadhalika kila mara karatasi mbili zilipokuwa zinaandikwa nilikuwa nikileta chini na hao waliendelea kunakili. Hudhur[as] alikuwa akiandika haraka sana kiasi hiki kwamba karatasi moja au mbili zilikuwa zinabaki kwa wenye kunakili. Bwana Abdul Quddus aliyekuwa mwenye kuandika haraka sana alishangaa na akaona wino kwa kugusa kwa mkono kwamba pengine imeandikwa hapo kabla. Nilisema kwamba kama imeandikwa hivi sasa, basi huu ni mujiza wenye shani kubwa.

Ilmuradi, aliendelea kuandika haraka haraka, na zikanakiliwa pia wakati ule ule. Nikampelekea Maulawii Muhammad Bashir nakili ya jibu la Hudhur[as] na kumwambia kuandika jibu lake. Akajibu, nataka kumwona Hudhur[as]. Sio sisi, lakini mtu mwingine akamwarifu Hudhur[as] kwamba Maulawii Muhammad Bashir anataka kuonana nawe. Hudhur[as] akaja mara moja. Maulawii Muhammad Bashir alisema, ukinipa idhini, nitaleta kesho majibu. Hudhur[as] alimruhusu kwa furaha… Mpaka mwisho wa mjadala Bwana Maulawii alifuatilia mwenendo huo huo. Kamwe hakuandika akikaa mbele yake. Alikuwa akienda kwa kuomba ruhusa."[208]

KUKAA PATIALA WAKATI WA KURUDI

Baada ya mjadala huo, Hudhur[as] alinuia kurudi. Kwa vile Hadhrat Mir Nasir Nawab siku zile alikuwa akikaa Patiala kikazi, kwa hiyo kutoka Delhi Hudhur[as] akaja Patiala na alikaa huko siku chache. Tarehe 30 Oktoba 1891, aliongelea na Sheikh mmoja Muhammad Isihaka wa Patiala juu ya swala la uhai na kifo cha Masihi[as]. Sheikh huyo alisema kwamba imeandikwa katika Hadithi kwamba Hadhrat Masihi mwana wa Mariamu[as] lazima alifariki kwa masaa machache lakini si kwa kudumu, bali akifufuka akaenda mbinguni. Hudhur[as] alimfahamisha

[208] Muhtasari kutoka kijitabu As-habe Ahmad, J. 4 uk. 124-126

kwamba mtu hawezi kupata mauti mawili, wala haithibitiki kuhusu Hadhrat Masihi[as] pia katika Kurani na Hadithi kwamba atapata vifo viwili. Alimfahamisha kwa hoja kadhaa nyingine pia. Lakini alipoenda baina ya watu alianza kutangaza ushindi wake. Hapo Hudhur[as] aliwajulisha watu wa Patiala kwa njia ya tangazo moja kwamba kama Sheikh yu mkweli katika kauli yake, na kauli yetu ni ya uongo, basi ni faradhi juu ya Bwana Sheikh kwamba kwa kuitisha mkutano wa hadhara ajadiliane nami. Hapo Sheikh alinyamaza kabisa na hakuja kumkabili."[209]

MWITO KWA UAMUZI WA KIMBINGUNI

Seyyidna Ahmad[as] alipoona kwamba nimeshakamilisha hoja juu ya Maulamaa wa daraja la juu wa nchi na tena kwa kufika mpaka mji mkuu kama Delhi, lakini Maulamaa wanaepa kujitokeza katika medani ya hoja, na kama mmojawapo akijitokeza kushindana, yeye haonekani tayari kuachana na heshima yake ya kidhahiri, hapo yeye alichagua njia iliyo roho ya dini ambayo bila hiyo mtu yeyote hawezi kudai kuwa na roho ya kimbingu ndani mwake. Yeye aliwakaribisha Maulamaa kwamba kama nyinyi m waaminio kwa hakika mbele ya Mwenyezi Mungu na mna uhusiano wa kirho na mbingu, basi njooni mkashindane nami katika kupata misaada ya kimbingu. Kama nyinyi m waaminio kamili na wacha Mungu, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu Atawasaidieni. Lakini Asipowasaidieni na kuwaacheni, bali nikipewa mimi msaada wa Mungu, basi mnapaswa kuelewa kwamba haki iko kwa nani, na ni nani aliye juu ya batili?

Basi, yeye alieleza alama nne za mwaminio kamili:

Ya kwanza ni kuwa mwaminio kamili mara nyingi anapata bishara kutoka kwa Mwenyezi Mungu, yaani huambiwa habari njema kabla hazijitokea zilizo miradi yake au matakwa ya marafiki zake.

Ya pili, mwaminio mkamilifu hufunuliwa mambo ya ghaibu siyo tu yanayomhusu yeye na jamaa zake, bali mara nyingi mwaminio mteule anapashwa habari ya kadri ya Mungu inayokadiriwa kushuka duniani

[209] Muhtasari kutoka tangazo la 31 Oktoba 1891, lililoandikwa katika Tablighe Risalat, J. 2 uk. 56-57

au mageuko yatakayowapata baadhi ya watu mashuhuri wa dunia.

Ya tatu, maombi mengi ya mwaminio mkamilifu hupokelewa, na mara nyingi yeye huarifiwa pia mapema kuhusu kupokelewa kwa maombi hayo.

Ya nne, mwaminio kamili hufunuliwa zaidi kuliko wote elimu ya ndani na maarifa mapya na maana nyepesi na sifa za ajabu za Kurani Tukufu. Katika alama hizi nne mwaminio mkamilifu kwa kulingana na wengine anawazidi.[210]

Kwa uamuzi huu wa kimbinguni aliwapatia changamoto Maulawii Nadhir Husain, Maulawii Muhammad Husain Batalawii, Sheikh Abdul Jabbar Ghaznawii Amritsarii, Sheikh Abdur Rahman wa Lakhuke, Sheikh Muhammad Bashir Bhopalawii na Sheikh Rashid Ahmad Gangohi hasa kwa kutaja majina yao, na kwa jumla masheikh, Sajjada-nashin, Masufii na Mapirzada, kwamba:

> "Kama nyinyi ni waaminio wakamilifu na, Mungu Apishe mbali, mimi ni kafiri, mkana Mungu, na dajali, basi bila shaka katika misaada ya kimbingu Mwenyezi Mungu Atawasaidieni na hatanisaidia mimi kamwe. Vilevile faida yake kubwa itakuwa hii pia kwamba makelele mnayopiga usiku na mchana kwamba kwanza uthibitishe imani yako kisha utujadili nasi, basi njooni, nathibitisha imani yangu, tena kwa njia ile iliyo sawa kabisa na Kurani na Hadithi lakini kwa kigezo hiki hiki nyinyi pia mtapaswa kuthibitisha imani yenu."

Lakini hakuna yeyote aliyekubali changamoto yake hii.

FATUWA YA UKAFIRI

Maulamaa walipoona kwamba hatuwezi kwa njia yoyote kushindana na mtu huyo, si uwanjani mwa hoja wala katika misaada ya kimbingu, na matokeo yake ni kuwa siku hadi siku watu wanaendelea kufanya baiati yake, basi waliamua kwa pamoja kwamba itayarishwe fatuwa ya kumkufurisha ambayo kuisadikisha ipigishwe mihuru ya masheikh wote wakubwa wa India, kisha hiyo ienezwe sana. Watu

[210] Asmani Faisala, uk. 14, chapa ya pili.

watakapoona kwamba masheikh wote kwa pamoja wamemkufurisha, hakuna yeyote atakayemwelekea. Basi jukumu hilo kapewa Maulawii Muhammad Husain Batalawii. Yeye akisafiri India nzima alipata fatuwa za kukufurisha kutoka kwa masheikh mia mbili. Na halitakuwa tusi lolote chafu sana katika kamusi za Kiurdu na Kiarabu ambalo masheikh hao hawakulitumia kumtukana yeye; bali haitakuwa uongo kama niseme kwamba baadhi ya matusi walibuni wao wenyewe ambayo hayakuwepo hapo kabla katika lugha. Mimi pia nimeziona baadhi ya sehemu za fatuwa hiyo, hakuna mtu mwungwana atakayeweza kuvumilia kuisoma.

Maulawii Muhammad Husain Batalawii alikuwa na dhana hii kwamba Seyyidna Ahmad[as] amepata umashuhuri na utukufu kwa sababu ya yeye Maulawii huyu kuandika maoni yake mazuri juu ya kitabu Barahine Ahmadiyya na kumsifu yeye. Kwa hiyo akajigamba akisema:

> "Mimi ndimi niliyemnyanyua, na mimi ndimi nitakayemwangusha."[211]

Hudhur[as], katika kitabu chake "Nishane Asmani" ametaja fatuwa za maulamaa, na hisani ya Mwenyezi Mungu kwa maneno haya:

> "Mimi siwezi kutoa shukurani kwa hisani za Mwenyezi Mungu kwamba katika wakati huu wa kukufurishwa sauti za Masheikh wa zama hizi zinaposikika toka kila upande kwamba لَسْتَ مُؤْمِنا (wewe si mwaminio), kutoka kwa Mwenyezi Mungu sauti hii inakuja: قُلْ اِنِّيْ اُمِرْتُ وَاَنَا اَوَّلُ الْمُؤْمِنِيْنَ (Yaani, sema, mimi nimetumwa, nami ni wa kwanza wa kuamini kuliko wote). Upande mmoja, Masheikh wanasema kwamba mfuteni kabisa mtu huyu kwa njia yoyote ile, na upande mwingine ufunuo unafunuliwa: يَتَرَبَّصُوْنَ عَلَيْكَ الدَّ وَآئِرَ عَلَيْهِمْ دَآئِرَةُ السَّوْءِ (Yaani, wanangojea misiba ikushukie, msiba mbaya uko juu yao). Na upande mmoja, hao wanajaribu kwamba wamdhalilishe kabisa mtu huyu na kumwondolea heshima, na upande mwingine Mungu Anatoa ahadi: اِنِّيْ مُهِيْنٌ مَّنْ اَرَادَ اِهَانَتَكَ ـ اَللّٰهُ اَجْرُكَ ـ اَللّٰهُ يُعْطِيْكَ جَلَالَكَ - (Mimi Nitamfedhehesha yule atakaye kukufedhehesha. Mungu ndiye ujira wako. Mungu

[211] Jarida '*Nur Ahmad*' uk. 17

Atakujalia utukufu wako). Na upande mmoja Masheikh wanaandika fatuwa juu ya fatuwa kwamba mtu anakuwa kafiri kama akikubali itikadi yake na kumfuata yeye, na upande mwingine Mwenyezi Mungu Anakazania mfululizo kwa nguvu kunifunulia: قُلْ اِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّوْنَ اللهَ فَاتَّبِعُوْنِيْ يُحْبِبْكُمُ اللهُ sema, ikiwa mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni, ndipo Yeye naye Atawapendeni. Ilmuradi, Masheikh wote hao wanapigana na Mwenyezi Mungu, sasa tutazame ushindi anaupata nani."[212]

Hapa jambo hili lapaswa kutajwa kwamba ufunuo: اِنِّيْ مُهِيْنٌ مَّنْ اَرَادَ اِهَانَتَكَ aliofunuliwa Hudhur[as] huko Lahore, ingawa unawahusu wote kwa jumla, lakini wakati ule lengo lake hasa lilikuwa ni Maulawii Muhammad Husain Batalawii. Ufunuo huo jinsi ulivyotimia mara kwa mara kwa njia mbalimbali, maelezo yake yanahitaji maandishi marefu. Habari zake zitatajwa kiasi fulani kwa kifupi katika kurasa zijazo pia.

Kwa kifupi ni kwamba yule Mjumbe ambaye Bwana Batalawii alitaka kuvunja heshima yake, yeye leo duniani kote watu wanamsalia, na jina lake likitajwa watu mashuhuri wa dunia wanainama kwa adabu. Na wakati ule hauko mbali bali upo mlangoni ambapo wafalme wa dunia watatafuta baraka kutoka katika nguo zake. Lakini leo haonekani yeyote anayetaja jina la Bwana Batalawii. Ulikuwa ni wakati ambapo kaumu zote za India zilikuwa zikitaja jina lake kwa heshima na popote alipokuwa akipita watu walikuwa wakisimama kwa kumheshimu, lakini baada ya kujiandaa kwa nia ya kumdhalilisha Hudhur[as], Mungu Apishe mbali, hata katika maisha yake heshima yake ilianzia kupungua. Wazao wake wote wakaangamia na mali zote zilipotea. Na alipofariki katika Batala, Waislamu wa Batala walikataa kumzika katika makaburi yao na alizikwa katika mava fulani ambayo kwa kuyataja ulimi unakwama.

MAONI YA HUDHUR[AS] JUU YA FATUWA YA KUFURU

Fatuwa ya kufuru iliyotajwa juu ilipomfikia Hudhur[as], yeye alichapisha tangazo lake lifautalo:

[212] Nishane Asmani, uk. 38-39

"Nimeiona fatuwa hii toka mwanzo hadi mwisho. Shutuma zilizosababisha fatuwa hii kuandikwa, inshaallah kuhusu shutuma hizi kuwa batili na kinyume cha ukweli nitachapisha kijitabu fulani haraka sana kinachoitwa ***Dafi'ul Wasaawis***. Hata hivyo sisikitiki kwa sababu ya hao watu kunilaani na kunikemea wala sina hofu. Bali nafurahi kwamba Mian Nadhir Husain na Sheikh Batalawii na wafuasi wao wakiniita kafiri, maluuni, dajali, mpotevu nisiye na imani, mtu wa Jahanamu na kafiri mkubwa kabisa, wametoa nyoyoni mwao homa zile ambazo zisingeweza hata kidogo kutoka kwa kushikamana na uadilifu, uaminifu na ucha Mungu. Na kadiri uchungu wa ukamilifu wa hoja zangu na ukweli wangu ulivyokuwa umewajeruhi jamaa hao, kwa ajili ya kuiondoa huzuni ya pigo hilo kubwa kulikuwa hakuna njia nyingine yoyote ile minghairi ya hii kwamba wangetoa laana tu. Mimi pia nimefurahi kuwa kufikiria jambo hili kwamba zawadi yoyote ile ambayo hatimaye Mafakihi na Masheikh wa Kiyahudi walimzawadia Hadhrat Masih[as] nayo pia ilikuwa ni hizi hizi za kumlaani na kumkufurisha kama inavyodhihirika katika historia ya Watu wa Kitabu na katika Injili zote nne. Basi, mimi katika hali ya kuwa mfano wa Masihi, kwa kuzisikia sauti hizi za laana napaswa kufurahi sana. Kwa sababu, kama Mwenyezi Mungu Alivyonijalia uhakika wa ki-Isa kwa ajili ya kuuhilikisha na kuuangamiza uhakika wa kidajali, ndivyo hivyo ambavyo hakuziacha zisitokee zile shida na taabu zihusikanazo na uhakika huu. Lakini kama kuna sikitiko, basi ni hili tu kwamba Sheikh Batalawii, katika kuitayarisha fatuwa hii, alilazimika kufanya hiyana zaidi kuliko ile iliyofanywa na Mafakihi wa Kiyahudi. Na hiyana hiyo ni ya aina tatu:

Kwanza ni hii kwamba baadhi ya watu wasiokuwa masheikh wala wenye madaraka ya kutoa fatuwa, walifanywa kuwa ni Mamufti ili tu kuongeza idadi ya wakufurishao.

Ya pili ni kwamba baadhi ya watu ambao hawana elimu, hao pia walishughulikia ufuska waziwazi, bali walikuwa wanatenda maovu machafu wakachukuliwa kuwa ni wanazuoni wakubwa

wenye kufuata sheria, na kupigishwa mihuri yao.

Ya tatu, wale watu waliokuwa na elimu na uaminifu lakini kwa hakika hawakuweka muhuri juu ya fatuwa hii, bali Sheikh Batalawii mwenyewe akayatia humo majina yao kwa ujanja na ulaghai mtupu.

Tunao uthibitisho wa kimaandishi kuhusiana na watu wa aina hizi tatu. Ikiwa Sheikh Batalawii au mtu mwingine yeyote ana shaka na haya, basi aandae mkutano wa hadhara katika Lahore na atuombe uhakikisho, ili mwongo afedheheke. Kukufurisha sio jambo lolote jipya. Njia ya mababu wa masheikh hao inayoendelea ni kwamba watu hao wasikiapo jambo jepesi mara moja hushikwa na hasira. Na kwa kuwa Mwenyezi Mungu Hakuwapa akili hii ya kufikia kina cha habari na kuweza kugundua uhakika wa ndani wa siri zenye mafumbo, ndiyo sababu katika hali yao ya kutofahamu, hukimbilia kukufurisha. Na miongoni mwa Mawalii watukufu hakuna hata mmoja aliyesalimika na kukufurishwa kwao, hata kwamba wanasema wenyewe kwa vinywa vyao kwamba atakapokuja Mahdi Mau'udi, huyo naye Masheikh watamkufurisha, na vivyo hivyo atakapoteremka Hadhrat Isa[as], yeye pia atakufurishwa. Jibu la mambo haya ni hili tu kwamba Enyi mabwana! Najikinga kwa Mwenyezi Mungu nanyi. Mwenyezi Mungu Mtakatifu Mwenyewe aliendelea kuwaokoa waja Wake watukufu na shari zenu, la sivyo mngalimeza Mawalii wote wa umati wa Muhammad[saw] kama afriti jike. Hamkuwaacha wa kabla wala wa baadaye kuwatukana. Na mnazitimiza kwa mikono yenu wenyewe alama zile mnazozisema. Ni ajabu kwamba watu hao hawana dhana njema hata wenyewe kwa wenyewe. Muda kidogo umepita, iligongwa mihuri karibu mia tatu ndani ya *'Madaarul Haq'* kuhakikisha kuwa *Muwahidiin* hawana dini. Basi, kama kukufurisha ni rahisi hivyo, sasa mtu anawezaje kuogopa kukufurishwa huko. Lakini masikitiko ni haya kwamba katika kukufurisha huku Mian Nazir Husain na Sheikh Batalawii wametumia sana ulaghai na kwa uzushi wa aina mbali mbali

wamefanya mwisho wao kuwa "mwema".[213]

MKUTANO WA KWANZA WA MWAKA, DESEMBA 1891

Siku za baada ya madai ya Umasihi zilikuwa za shughuli nyingi sana kwa Hudhur[as]. Maulamaa wapinzani waliwasha moto wa upinzani pande zote nne, lakini Hudhur[as] kwa heshima kubwa alikuwa ameshughulikia kwa uimara na ushujaa akizima moto huo, na kwa lengo hilo akafanya pia safari ndefu ndefu. Lakini pamoja na kusimama vitani mwa itikadi kwa upanga uliochomolewa, hakughafilika pia na malezi ya watu wapya wafanyao baiati. Basi, kwa agizo la Mungu, Hudhur[as] aliweka msingi wa mkutano wa mwaka katika Qadian, na alipanga tarehe zake 27 hadi 29 Desemba. Hivyo, mkutano wa kwanza uliofanyika katika Desemba 1891, watu sabini na watano walishiriki. Na kwa lengo na makusudio ya mkutano, alitoa tangazo tarehe 30 Desemba 1891 kama ifuatavyo:

> "Ndugu wote wenye ikhlasi waliofanya bai'ati yangu wajue kuwa shabaha ya kufanya bai'ati ni kwamba mapenzi ya dunia yapoe, na mapenzi ya Mola Mtukufu na ya Mtume Mtukufu[saw] yatawale moyoni. Na hali ile ya kutengana na dunia ipatikane ambayo kwayo safari ya Akhera isionekane yenye kuchukiza. Lakini kwa kulipata lengo hili yamlazimu mtu kukaa nami na kutumia muda fulani wa umri wake katika njia hii ili, Mungu Akipenda, kwa kushuhudia dalili yenye yakini, udhaifu na uzembe uondoke, na kwa kuzalika yakini kamili izalike shauku na ladha ya jazba ya upendo mkubwa. Hivyo, kwa ajili ya jambo hili, daima inatakiwa kuwa na hadhari, na yapasa kuomba dua kuwa Mungu Ajaalie uwezo huu. Na mpaka uwezo huo haujapatikana inapasa kuonana nami mara kwa mara, kwani baada ya kuingia katika silsila ya baiati, kisha kutojali kuonana, baiat kama hii haina baraka, itakuwa ni kama kufuata mazoea. Na kwa vile ni vigumu kwa kila mmoja kuja hapa akae nami kutokana na udhaifu wa asili au upungufu wa uwezo au kitalifa kirefu, au kuja mara chache kwa mwaka kuonana nami kwa

[213] Nishane Asmani, uk. 42-44

> kuvumilia shida kubwa, kwani hivi sasa ndani ya mioyo mingi hamna shauku nyingi kiasi kwamba waweze kuvumilia taabu kubwa na madhara mengi, kwa hiyo inaonekana inafaa zipangwe siku tatu kwa mwaka kwa ajili ya mkutano ambamo, Mungu Akipenda, ndugu wote waaminio waweze kuhudhuria katika tarehe zilizopangwa, sharti wakiwa na afya na nafasi na kutokuwa na vikwazo vikubwa. Kwa maoni yangu, ni bora tarehe hizo ziwe 27, 28 na 29 za mwezi Desemba. Yaani baada ya siku ya leo hii iliyo 30 Desemba 1891, kama tarehe 27 Desemba ikifika katika uhai wetu, basi ndugu wote kadri ya wasaa wao wanapaswa wafike kwenye tarehe hiyo kwa ajili ya kusikiliza maneno ya Mwenyezi Mungu tu na kwa ajili ya kushiriki katika maombi. Na katika mkutano huo kutakuwa na shughuli za kuelezea mambo ya ukweli na maarifa ambayo ni ya lazima kwa ajili ya kuzidisha imani na yakini na maarifa. Na vile vile jamaa hao watafanyiwa maombi maalum na mwelekeo mahususi na itafanywa bidii sawa na uwezo mbele ya Mungu Mrehemevu kwamba Mwenyezi Mungu Awavutie kwake na Awakubalie kwake na Awapatie mabadiliko mema..."[214]

Mkutano huo ulifanyika katika Masjid Aqsa ya Qadian. Taarifa yake iliyoandikwa katika kitabu cha Hudhur[as] "*Asmani Faisala*", humo mkusanyiko huo, sawa na hali ya wakati ule, umeitwa "halaiki kubwa". Lakini sasa Mkutano ule ulioanzishwa kwa mikono mitakatifu ya Masihi Mtukufu, unahudhuriwa na watu maelfu wenye huba kutoka duniani kote. Mamia ya wanaojitolea kwa hiari yao wanasimamia shughuli za mkutano. Katika Mkutano uliopita uliofanyika mwaka 1958, watu karibu elfu themanini walijumuika. Na wakati ule hauko mbali ambapo malaki ya wapendao Uahmadiyya kutoka nchi zote za dunia kwa shauku na mapenzi makubwa watashiriki katika Mkutano wa mwaka, Mungu Akipenda.

VITABU VYA 1890-91

Vijitabu *Fat'he Islam* na *Taudhihe Maraam* vilivyoandikwa mwishoni mwa

[214] Tangazo hilo limechapishwa katika kitabu "*Asmani Faisala*".

mwaka 1890, vilichapishwa katika mwaka 1891. Mwaka huu kitabu kizuri sana '*Izala Auhaam*' kilichapwa ambacho kimeshaelezwa kirefu hapo juu. Uandishi na uchapaji wa '*Asmani Faisala*', mada yake pia inadhihirika katika dondoo za juu.

MWINGEREZA KASILIMU, 13 JANUARI 1892

Mnamo 13 Januari 1892, mwandishi mmoja Mwingereza wa eneo la Madras, Bwana Waite John, mwanaye Bwana John Waite alifanya baiati akihudhuria Qadian. Kwa sababu hiyo Hudhur[as] alifurahi sana, kwani kabla ya muda mfupi tu alikuwa ameona katika ruya kuwa:

> "Niliona kwamba nimesimama juu ya mimbari mjini London na ninaeleza kwa dalili madhubuti ukweli wa Islam katika lugha ya Kiingereza. Baada yake nilikamata ndege wengi waliokuwa wametua juu ya miti midogo midogo, nao walikuwa na rangi nyeupe, na walikuwa na mwili labda kama mwili wa kware."
>
> "Basi niliiagua kwamba ingawa si mimi lakini maandishi yangu yataenea katika watu hao na Waingereza wengi wanyofu watakubali ukweli."[215]

Kusilimu kwa Bwana Waite kulikuwa ni uthibitisho kwa kitendo wa uaguzi wa ruya ile, na Hudhur[as] kuifurahia ilikuwa ni sawa kabisa.

SAFARI YA LAHORE, 20 JANUARI 1892

Katika "Asmani Faisala" Hudhur[as] alitangaza kwamba kama miongoni mwa maulamaa, viongozi, madarweshi na wasimamizi wa makaburi, yeyote anataka kushindana nami katika "Misaada ya Kimbingu", basi kwa lengo hilo Lahore itafaa kabisa. Kwa kutimiza ahadi hiyo alifika Lahore katika wiki ya tatu ya Januari na alikaa katika jumba la Munshi Miran Bakhsh lililopo katika Chuna Mandi.

> "Mnamo 31 Januari 1892 alitoa hotuba ya hadhara katika eneo la jumba la Munshi Miran Bakhsh. Bila kutia chumwi, maelfu ya watu walihudhuria, watu wa tabaka zote walikuwepo, wasomi, waheshimiwa wa mji na viongozi. Usimamizi ulikuwa wa polisi.

[215] Izala Auham, uk. 515-516, saizi ndogo

Hudhur[as] alieleza kwa uwazi madai yake na alileta hoja za muhimu juu yake. Na hatimaye katika kujibu shutuma hii kwamba maulamaa mbele yangu wakishindwa katika hoja za Kurani wanatoa fatuwa ya kunikufurisha, akasema ni rahisi kumwita mwaminio kuwa kafiri, lakini kujithibitishia imani si rahisi. Kurani Tukufu imeweka baadhi ya alama kwa mwaminio na asiyekuwa mwaminio. Nawakaribisha wakufurishaji kwamba waamulishe katika mji huu huu wa Lahore kuhusiana na imani yangu na imani yao sawa na uamuzi wa Kurani Tukufu."[216]

HOTUBA YA HADHRAT ALHAJ MAULANA HAFIZ HAKIM NURUD DIN[RA] WA BHERA

Hadhrat Alhaj Maulana Hafiz Hakim Nurud Din[ra] wa Bhera ambaye baadaye akawa Khalifa wa Kwanza wa Seyyidna Ahmad[as] alikuwepo mkutanoni humo. Hudhur[as], baada ya hotuba yake, alimwambia kwamba wewe pia uwahutubie kidogo. Hapo Hadhrat Maulana alisimama na akasema:

"Mmesikiliza madai ya Bwana Mirza na hoja zake kwa ulimi wake, na mmesikiliza pia ahadi na bishara za Mwenyezi Mungu ambazo Mwenyezi Mungu Alimpa katika hali zilizokuwa kinyume cha ahadi hizo. Wanamji wenu wananijua mimi na ukoo wangu, maulamaa pia hawakosi kunijua. Mwenyezi Mungu Amenipa fahamu ya Kurani. Nimechunguza sana madai ya Bwana Mirza, na kumwomba Mwenyezi Mungu. Nilitazama huduma zake za Kiislamu. Na nilitafakari katika hali za wapinzani wake. Basi kwa kuangalia hayo yote Kurani Tukufu iliniongoza. Niliona kwamba jinsi waja wa kabla yake walivyopingwa, hivyo ndivyo inavyofanyika sasa, kana kwamba historia ya zamani inajirudia. Nasema kwa kutamka shahada mbili kwamba Bwana Mirza ni mkweli, na batili itakayogongana na ukweli huu itavunjika tikitiki. Mwaminio anakubali ukweli, nimeukubali kwa kuufahamu kuwa haki. Na sawa na kauli ya Mtume Mtukufu[saw] mwaminio anachopenda kwa ajili yake

[216] Hayate Ahmad, J. 3 uk. 208 na Hadhrat Sheikh Yakub Ali Irfani[ra]

hukipenda kwa ndugu yake. Nawakaribisheni kukubali haki hii. Ni juu yetu kufikisha tu. Assalamu alaikum. Kwa kusema hayo akashuka kutoka mimbari na mkutano ulikwisha."[217]

TUKIO MOJA LA SUBIRA KUBWA YA HUDHUR[AS]

Kwa kuona kupitapita watu wengi na halaiki kubwa, alihama jumba la Munshi Miran Bukhsh kwenye jumba kubwa zaidi la Mahbub Raion[218] Ingawa wakati wa kukaa Lahore pia watu walionyesha upinzani, lakini haukuwa upinzani dhalili jinsi walivyofanya Wadelhi. Naam, likatokea tukio moja lililodhihirisha hali kamili ya subira na uvumilivu wa Hudhur[as]. Hadhrat Sheikh Yakub Ali Turab[ra] anasimulia:

"Hudhur[as] alikuwepo katika kikao na alimpa marehemu Munshi Shamsuddin, katibu mkuu, "Asmani Faisala" ili kuwasomea waliohudhuria. Mandhari kamili ya wakati huo ipo mbele ya macho yangu. Katika kikao hicho alikuwepo Babu Mozamdar aliyekuwa siku hizo kiongozi wa Barhamu Samaj na alikuwa afisa mkubwa katika afisi ya mtihani na alijulikana kwa wema na hulka yake njema na alikuwa katika mstari wa mbele katika kutumikia jamii. Mtu fulani aliyeitwa Mwislamu akaja na akaanza kudhihirisha ghadhabu kwa maneno yasiyostahili na matusi. Hudhur[as] akiweka sehemu ya kilemba chake usoni aliendelea kusikia na akakaa kimya kabisa. Haikudhihirika alama yoyote ya chuki au ghadhabu usoni mwake, ilionekana kana kwamba hasikii chochote. Hatimaye baada ya kuchoka huyo alinyamaza mwenyewe na akaenda. Wengi miongoni mwa wahudhuriao walikasirika, lakini yeyote hakujasiri kumzuia kwa heshima ya Hudhur[as]. Baada ya yeye kuondoka, Babu Mozamdar alisema: "Tumesoma na kusikia mengi kuhusu uvumilivu wa Masihi[as], lakini jambo hili la ajabu tumeliona kwa macho yetu. Alisema mengi kuhusiana na habari hii. Kwa kuwa wanajumuiya wetu wengi walikuwa wanafanya kazi ofisini

[217] Hayate Ahmad, J. 3 uk. 209

[218] Ni jina la kabila la Mabaniani

mwake, na akawaheshimu wote na hasa alikuwa akimstahi sana Hadhrat Munshi Nabii Bakhsh[ra], basi alikuwa akieleza tukio hilo na kusifu uvumilivu wa Hudhur[as].”[219]

BAIATI YA BAADHI YA NDUGU WA LAHORE

Hadhrat Sheikh Yakub Ali Turab[ra] anaeleza pia:

“Katika nyumba ile ndugu wengi wa Lahore walifanya baiati, na mimi pia nilijadidisha baiati yangu. Hadhrat Mirza Yakub Beg[ra], Hadhrat Mirza Ayub Beg[ra], Hadhrat Abdul Aziz Mughal na watu wengi wa familia[220] yake walifanya baiati wakati huo ambao majina yao yamo katika rejista ile ambamo zaidi ameandika Hudhur[as] mwenyewe kwa kalamu yake ambayo nakala yake moja ninayo mimi pia.”[221]

MDAI FULANI WA UMAHDI KAMSHAMBULIA

“Katika siku hizo yeye alikuwa akisali katika msikiti wa Hadhrat Maulawii Rahimullah[ra] (uliokuwepo mbele ya nyumba za Hadhrat Munshi Charagh Din[ra] katika Lange Mandi). Siku moja baada ya kusali sala ya adhuhuri au alasiri yeye alipotoka msikitini kuelekea nyumbani mara mtu mmoja alimshika kiunoni, lakini hakuweza kumwinua wala kumwangusha. (Huyo ndiye aliyekuwa akijiita Mahdi na alikuwa akitoa shahada ya *La ilaha illallahu Mahdi Rasulullahi*). Hadhrat Seyid Amir Ali Shah Sialkoti[ra] akamshika na kumtenganisha na Hudhur. Yeye alitaka kumpiga lakini Hudhur[as] akitabasamu akasema usimpige, anadhani kwamba cheo chake nimejinyakulia, hadi akafika nyumbani akaendelea kutazama nyuma, isije mtu yeyote akamwudhi. Yeye alikuwa akija pamoja naye, na akaanza kutoa hotuba nje ya nyumba. Mtu huyo alikuwa mkazi wa kijiji kimoja cha wilaya ya Gujranwala, na ndugu yake anayejulikana katika Jumuiya

[219] Hayate Ahmad, J. 3 uk. 210

[220] Siku chache kabla ya Hadhrat Abdul Aziz, Hadhrat Mian Mirajud Din Umar alifanya baiati. Hadhrat Mian Charagh Din aliyekuwa baba wa Bwana Mughal na binamu wa Hadhrat Mian Mirajud Din Umar, alifanya baiati pamoja na watu wengi wa familia yake baada ya Bwana Mughal.

[221] Hayate Ahmad, J. 3 uk. 210

yetu kwa jina la Peghambara Singh, hatimaye akajiunga katika Ahmadiyya, na alikuwa mwenye ikhlasi. Huyo ndiye alimrushia Hudhur[as] maua katika kikao kimoja cha Lahore na akaomba radhi kwa kosa la ndugu yake. Peghambara Singh pia wakati fulani alikuwa akidai kwamba yu mfano wa Guru Ram Singh wa Masingasinga, na baadaye Mwenyezi Mungu alimfungulia hakika ya Islam na akawa mcha Mungu na Mwahmadiyya mwenye ikhlasi."[222]

HADHRAT SEYYID MUHAMMAD AHSAN AMROHI AJA KUUNGANA NA JUMUIYA, FEBRUARI 1892

Mjini Lahore mwanzoni mwa Februari 1892, aliwasili Hadhrat Seyyid Muhammad Ahsan Amrohi. Bwana Seyyid, marehemu, ameshatajwa nyuma kwamba yeye alikuwa miongoni mwa waliomkurubia Nawab Siddik Hasan Khan Bhopalawii na alikuwa mtaalamu maarufu wa kundi la Ahle Hadith. Akijiunga na Jumuiya alitoa huduma njema sana katika zama za awali, na kuhusuye Seyyidna Ahmad[as] alifunuliwa:

ازپے آں محمد احسن را[223] تارک روزگارے بینم[224]

MJADALA KWA SHEIKH ABDUL HAKIM KALANORII

Mjadala baina ya Sheikh Abdul Hakim Kalanori na Seyyidna Ahmad[as] juu ya maneno yake aliyoandika katika "*Fat'he Islam*", "*Taudhihe Maram*" na "*Izala Auham*" kwamba "Muhadathi kwa maana moja anakuwa nabii." Bwana Sheikh alikuwa na itikadi hii kwamba kwa maneno hayo madai ya unabii halisi wa asili yanadhihirika. Lakini kwa kauli ya Hudhur[as] kwamba simaanishi hivi kwa maneno hayo wala hayana maana hii kwamba nimedai unabii hasa halisi, mjadala uliishia kwa kutoa kimaandishi maneno yafuatayo:

> "Katika vitabu vyangu *Fat'he Islam*, *Taudhihi Maram* na *Izala Auham* maneno yoyote yaliyopo kwamba Muhadathi kwa maana moja

[222] Hayate Ahmad, J. 3 uk. 210

[223] Katika zama za Ukhalifa wa pili, Maulawii Seyyid Muhammad Ahsan Amrohi, kwa fitina ya ahli zake aliungana na wakanao Ukhalifa lakini baadaye alitubu.

[224] Tafsiri ya ubeti: Muhammad Ahsan ameacha dunia kwa huduma hizo.

anakuwa nabii, au *umuhadathi* ni sehemu ya unabii, au *Umuhadathi* ni unabii usiokamilika, maneno hayo yote hayana maana ya asili, bali umeelezwa muradi wake katika lugha kwa namna itakavyoeleweka kwa urahisi, waila, Mungu Apishe mbali, sidai unabii hasa asilia. Bali, kama nilivyoandika kwenye ukurasa wa 137 wa kitabu cha *Izala Auham,* imani yangu ni kuwa Seyyidna wa Maulana Muhammad Mustafaa[saw] ndiye Khatamul Ambiyaa. Basi ningependa kuwabainishia ndugu wote Waislamu kwamba kama wanakasirika kwa maneno hayo, na kama wakiona shida moyoni mwao kwa maneno hayo, basi wayachukulie hayo kurekebishwa na badala yake wayafahamu hayo kuwa *Muhadathi* kutoka kwangu... na walifahamu neno hilo (yaani neno la nabii) kuwa lililokatwa."[225]

MWANZO WA MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII KUPUNGUKIWA HESHIMA MACHONI MWA WATU

Imeshatajwa juu kwamba Maulawii Muhammad Husain alipoandika kuhusu Hudhur[as] kwamba 'mimi nilimnyanyua na sasa mimi nitamwangusha', ndipo ghera ya Mungu Mwenye kuheshimisha na kudhalilisha ilichemka na Akamwambia Hudhur[as]

اِنِّیْ مُھِیْنٌ مَّنْ اَرَادَ اِھَانَتَکَ وَ اِنِّیْ مُعِیْنٌ مَّنْ اَرَادَ اِعَانَتَکَ۔[226]

Hili lilikuwa tangazo la jambo hili kwamba dhila ya Maulawii Muhammad Husain imeshaanza. Basi dhila ya kwanza alipata katika mjadala wa Ludhiana. Ya pili, alipofika Lahore alitengwa na uimamu wa msikiti wa Chinianwali.[227]

Katika Lahore, Bwana Maulawii hakujitokeza kushindana na Hudhur[as], lakini alifanya mkutano katika Masjid Wazir Khan.

[225] Tangazo la 3 Februari 1892.

[226] Mimi Nitamdhalilisha yule ambaye atanuia tu kukudhalilisha; nami Nitamsaidia atakayenuia tu kukusaidia.

[227] Hayate Ahmad, J. 3 uk. 211. Tanbihi: Wakati ule msimamizi wa msikiti wa Chinianwali alikuwa "Sheikh Ghauth"aliyekuwa baba wa mama wa rafiki yetu Mwahmadiyya mashuhuri marehemu Seyyidi Dilawar Shah. Na ninakisia kwamba Bwana Sheikh huyo pia alifanya baiati katika 1904.

Hadhrat Sheikh Yakub Ali Turab[ra] anasema:

> "Nilikuwepo katika mkutano huo, Wahanafii mapema walimchukia na Ahle Hadith pia hawakuonyesha moyo wa kuupenda."

Kwa hiyo,

> "Katika mkutano huo wa Bwana Maulawii, baadhi ya watu wa Kashmiri Bazar na Chok Wazir Khan walijumuika. Bwana Maulawii akisimama juu ya mimbari alianza kupinga "***Taudhihe Maram***". Watu hawakujali, na wakasema amekuja baada ya kushindwa katika mjadala mjini Ludhiana na sasa anatoa fatuwa ya kukufurisha. Makusanyiko hayo yalibaki kwa nusu saa tu hivi na yakatawanyika."[228]

SAFARI YA SIALKOT

Hudhur[as] bado alipokuwa mjini Lahore, Jumuiya ya Sialkot ilimkaribisha kuja Sialkot na kwa lengo hilo hasa ilimtuma Hadhrat Maulawii Abdul Karim[ra] kama mjumbe wake. Hudhur[as] alikubali mwito wao, na katika wiki ya pili ya Februari 1892, Hudhur[as] alikwenda Sialkot na alikaa katika nyumba ya Hadhrat Hakim Mir Husamud Din. Yeye aliijua vizuri Sialkot, kwani kuanzia mwaka 1864 hadi mwaka 1868 alikaa huko kikazi. Vilevile watu wa Sialkot walikuwa wameyaona maisha yake matakatifu na ghera yake kwa Islam, kwa hiyo hao nao walikuwa wakimheshimu sana. Tumeshaandika katika zama za utoto wa Hudhur[as] kwamba miongoni mwa waalimu wa awali wa Hudhur[as], mwalimu mmoja alikuwa marehemu Maulawii Fadhl Ahmad pia, mwanaye Hadhrat Maulawii Abu Yusufu Mubarak Ali aliyekuwa na sifa bora baina ya Maulamaa wa Sialkot, na alikuwa imamu wa msikiti wa Ijumaa wa Sadr Bazar, alijiunga na Jumuiya kwa kufanya baiati. Hadhrat Maulawii Abdul Karim Sialkoti aliyekuwa hatibu maarufu wa Sialkot na mwenye ghera sana ya Kiislamu, tayari alikwishakubali madai yake. Hadhrat Hakim Mir Husamud Din pia alikuwa maarufu sana. Kwa sababu ya

[228] Hayate Ahmad, J. 3 uk. 211-212

wazee hao watatu pia watu wa Sialkot walipata kuathirika naye sana. Watu wote wa familia ya Hadhrat Hakim walijiunga na Jumuiya na wakapata nafasi nzuri ya kutumikia katika muda wa kukaa kwake huko Sialkot.

Hadhrat Dkt. Mir Muhammad Ismail[ra] anasimulia kwamba Mir Haamid Shah Sialkoti alifanya baiati mwanzoni mwa madai yake ya Umasihi lakini baba yake Hakim Mir Husamud Din aliyekuwa mwenye nguvu, yeye alikuwa na itikadi nzuri lakini hakufanya baiati. Yeye alikuwa mkubwa katika umri kuliko Hadhrat Masihi Mau'udi[as] na alikuwa rafiki yake pia tangu alipokuwa Sialkot. Bwana Mir Haamid Shah daima alikuwa akimhimiza kufanya baiati, lakini kila mara akakwepa. Akajiona mkubwa. Safari moja Bwana Shah alimleta Qadian, na ndugu wote wakamsisitizia kwamba kwa kuwa unajua mambo yote, basi fanya baiati pia. Hatimaye akakubali, lakini alisema kwamba mimi ni mtu wa staili yangu, kwa hiyo sitafanya baiati hadharani, nitafanya baiati faraghani. Mir Haamid Shah aliona hiyo ni afadhali. Alipomwambia Hudhur[as], alikubali na alipokea baiati ya Bwana Hakim marehemu faraghani.[229]

MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII PIA AFIKA SIALKOT

Kwa kutimiza lengo lake bovu, Maulawii Muhammad Husain Batalawii pia alifika Sialkot. Lakini akafika ambapo Hudhur[as] alikwishanuia kurudi. Bwana Maulawii, kwa kuondoa fedheha ya kushindwa huko Ludhiana, alituma baadhi ya watu, Sheikh Ghulam Haidar Tahsildar akiwa mmojawapo, kwa Hudhur[as] pamoja na ujumbe wa kufanya mjadala. Hudhur[as] akiwaelezea habari za mjadala wa Ludhiana na matukio ya Delhi, alisema kwamba sasa Bwana Maulawii ameshanitolea fatuwa ya kufuru pia, kuna faida gani sasa ya mjadala. Sasa anapaswa kwamba sawa na vigezo vilivyopangwa na Kurani Tukufu kwa "Uamuzi wa Kimbingu", ajitokeze uwanjani pamoja na kundi la maulamaa wasaidizi wake na kisha aone kwamba msaada wa Mungu na misaada ya kimbingu inamwunga mkono nani.

[229] Siratul Mahdi, sehemu ya tatu, uk. 257-258

Nikiwa mwongo katika madai yangu, basi Mungu Ataniangamiza Mwenyewe. Lakini nikiwa mkweli, basi maulamaa hao watashindwa katika makusudio yao. Na Mwenyezi Mungu Atanisaidia kwa kila hatua na Ataeneza kupokolewa kwangu duniani kote.

SAFARI YA KAPURTHALA

Watu wa Kapurthala hasa walihusika naye kwa ikhlasi, bali yafaa kusema kwamba walikuwa wamejitolea kwake. Wakati Hudhur[as] alipokuwa Lahore, hao pia walimtuma mjumbe wao na Hudhur[as] akaahidi kuja Kapurthala. Hudhur[as] alikwishatembelea hapo mara mbili hapo kabla pia. Safari hii alipokwenda alipata upinzani kidogo pia kinyume cha hapo kabla. Maulawii Muhammad Husain Batalawii aliwatumia masheikh wa huko kipeperushi chenye kichwa cha habari 'Kumwombea maovu'. Kipeperushi hiki kilipomfikia Hudhur[as], yeye aliona kwamba humo kuna mwito wa mjadala pia. Hudhur[as] alisema kwamba mtu huyo kwa kuondoa fedheha ya mjadala wa Ludhiana anaendelea kufanya hivi. Kwa nini watu hao hawaji kwenye "Uamuzi wa Kimbingu" wa Mwenyezi Mungu?

SIFA ZA JUMUIYA YA KAPURTHALA

Itafaa hapa kutaja baadhi ya sifa kubwa za Jumuiya ya Kapurthala. Jumuiya hii ilizama katika mapenzi ya Hudhur[as] na kujitolea kwake pia kulikuwa hakuna mfano. Ni Jumuiya hii tu ndiyo iliyotolewa habari njema ya Hudhur[as] kimaandishi:

> "Jumuiya ya Kapurthala ipo nami duniani pia na katika akhera pia itakuwa nami."[230]

Napenda kwamba kama si zaidi basi niwaeleza wasomaji angalau tukio moja moja la ikhlasi na upendo wa wazee wawili wa Jumuiya hii, yaani Hadhrat Munshi Zafar Ahmad[ra] na Hadhrat Munshi Arurhe Khan[ra]. Mwanaye Hadhrat Munshi Zafar Ahmad[ra], Sheikh Muhammad Ahmad, wakili na Amiri wa Jumuiya ya Lyallpur, anasimulia kwamba babake alisema:

"Safari moja Hudhur[as] alikuwepo Ludhiana na mimi

[230] Hayate Ahmad, J. 3 uk. 225

nilihudhuria mbele yake. Hudhur[as] akasema, je, Jumuiya yenu itaweza kubeba gharama ya Rupia 60 kwa kuchapisha tangazo moja? Nikajibu, naam. Nikaja Kapurthala na nikauza mkufu wa dhahabu wa mke wangu, na sikumwambia mwanajumuiya yeyote na nikichukua Rupia sitini 'nikaruka'[231] papo hapo, na kwa kufika Ludhiana nikamkabidhi Hudhur[as]. Baada ya siku chache Munshi Muhammad Arurha pia akafika Ludhiana, mimi bado nilikuwepo hapo. Hudhur[as] alimwambia kwamba Jumuiya yenu imesaidia wakati mwafaka sana. Munshi Arurha akajibu kwamba Jumuiya yetu au mimi hatuna habari kabisa. Wakati huo marehemu Bwana Munshi aligundua kwamba mimi (yaani Zafar Ahmad) nimeshatoa Rupia zile kutoka kwangu tu. Hapo marehemu Bwana Munshi alikasirika sana na akamwambia Hudhur[as] kwamba huyu ametufanyia uadui sana kwamba hakutuambia. Hudhur[as] akamwambia Munshi Arurha kwamba Bwana Munshi, nafasi nyingi za kutumikia zitatokea, usione vibaya. Bwana Munshi aliendelea kunikasirikia kwa muda fulani."[232]

Sasa sikilizeni kisa cha mapenzi ya Hadhrat Munshi Arurhe Khan pia. Hadhrat Amirul Muminin Khalifatul Masihi wa Pili a.t.b.a. ameeleza habari hii mara kadhaa katika hotuba zake kwamba Munshi Arurhe Khan alikuwa na hamu sana moyoni mwake kwamba amzawidie Hadhrat Masihi Mau'udi[as] kiasi fulani cha dhahabu. Kwa vile alikuwa na mshahara mdogo, kwa hiyo hakuweza kutimiza hamu yake katika uhai wa Hudhur[as]. Baada ya kifo cha Hudhur[as], yeye akaja kwangu na sarafu kadha za dhahabu na akasema huku machozi yakimlengalenga kwamba nilijaribu maisha yote kwamba nimzawidie Hudhur[as] kiasi fulani cha dhahabu, lakini sikuweza kufaulu. Sasa nimepata sarufi hizi za dhahabu, lakini Hudhur[as] hayupo duniani. Akisema hayo tu akalia, na akalia sana kwa kwikwli. Allah, Allah, mapenzi yalioje haya ya hali ya juu! Laiti katika kizazi cha baadaye pia

[231] Bwana Sheikh Muhammad Ahmad Mazhar anasema kwamba baba alitumia maneno yayo, hayo.

[232] Hayate Ahmad, J. 3, uk. 223

mifano ya aina hii ibaki.

SAFARI YA JALANDHAR

Baada ya kukaa Kapurthala kwa wiki mbili, alikwenda Jalandhar. Katika Jalandhar upinzani ulikuwa wa hali ya juu sana. Kwa hiyo, Hudhur[as] hakutaka kwamba arudi bila kuwafikishia watu wa mji huu ujumbe wa kweli. Basi, baada ya kuwasili Jalandhar alishughulikia kazi yake. Baadhi ya watu walimpelekea Mrakibu wa Polisi aliyekuwa Mwingereza shtaka kwamba mdai mmoja wa Umasihi kutoka Qadian amekuja hapa na anaeneza mawazo yake kwa nguvu sana katika watu, kama hazuiliwi, basi ipo hofu ya kupatikana machafuko mjini. Mwamrishe aondoke mji huu. Kwa kupeleleza shtaka hilo yule afisa Mzungu akaja kwenye makazi ya Hudhur[as] na akamwuliza kwamba umekujaje hapa? Kwa kujibu swali hili Hudhur[as] alitoa hotuba ndefu. Kwa kusikiliza hotuba yake aliathirika sana na aliendelea kumtazama uso wake mtukufu. Hatimaye, baada ya hotuba alikwenda akisema kwamba ukae hapa mpaka upendapo, hakuna mtu yeyote atakayeweza kuleta machafuko.[233]

SAFARI YA LUDHIANA

Katika Jalandhar alikaa kama siku 12,13. Kutoka huko alikwenda Ludhiana, hapo aliandika kijitabu "*Nishane Asmani*" ambacho jina lake la pili ni '*Shahadatul Mulhamin*' pia. Na akaja Qadian, na akachapisha kijitabu hicho tarehe 26 Mei 1892. Alieleza humo kashfi na funuo za mawalii wa umati wa Mtume[saw] kwa kusadikisha na kusaidia madai yake.

FAIDA ZA SAFARI HIZO

Kwa safari hizo, makusudio yake yalipata faida sana. Kwa matokeo ya safari za Ludhiana na Delhi, kwa kuchochewa na Maulawii Muhammad Husain Batalawii na Maulawii Seyyid Nadhir Husain, masheikh 200 walimtolea fatuwa ya kumkufurisha. Kwa kutangazwa kwa fatuwa hiyo na kwa hotuba za upinzani, madai yake yalienea kuanzia kona moja ya nchi hadi kona ya pili.

[233] Muhtasari kutoka Hayate Ahmad, J. 3, uk. 228

2. Sawa na kauli ya Kurani:[234] يٰحَسۡرَةً عَلَى الۡعِبَادِ مَا يَأۡتِيۡهِمۡ مِّنۡ رَّسُوۡلٍ اِلَّا كَانُوۡا بِهٖ يَسۡتَهۡزِءُوۡنَ imethibitika kwa makelele, dhihaka na matusi ya watu kwamba aliyofanyiwa yeye ni sawa na Suna ya Mungu, na ya kwamba yeye kwa hakika ni mkweli katika madai yake ya kutumwa na Mungu.

3. Katika safari hizo, baadhi ya watu wakubwa wa nchi waliokuwa mashuhuri kwa ucha Mungu, utawa, wema na utakaso wao walipata heshima ya kufanya baiati yake. Na hivyo, kwa safari hizo matawi kadhaa ya Jumuiya yalipatikana.

4. Maelfu ya watu walipata heshima ya kumzuru na wakasikiliza hoja za madai yake kwa mdomo wake mtukufu.

MAHUBIRI YA KIROHO KWA WATAFUTAO HAKI

Tumeshaandika juu kwamba kwa kuwaarifu watu kuhusu madai yake, Hudhur[as] alitoa hotuba kwa mdomo, alichapisha matangazo pia, aliwakaribisha watu kwa mijadala na mashindano na aliwaelekeza kwenye uamuzi wa Kimbingu pia. Alileta ushahidi wa mawalii wa umati wa Mtume[saw] na wenye kupata funuo kwa kuthibitisha ukweli wake. Na zaidi ya hayo alieleza njia ya uamuzi ambayo iliweza na inaweza kuwafaidisha zaidi watu ambao ni waungwana, nayo ndiyo kwa njia ya Istikhara kumwuliza Mwenyezi Mungu moja kwa moja kuhusu hali za madai ya Hudhur[as]. Hudhur[as] amesema:

> "Sehemu hii naandika hii pia kwa kuhubiri kwamba wale watafutao haki wanaoogopa kamato la Mungu, wasiwafuate Masheikh wa zama hizi bila ya kufanya utafiti. Na jinsi Mtume wa Mungu s.a.w. alivyowaogopesha kutoka kwa Masheikh wa zama za mwisho, basi hivyo hivyo mwendelee kuogopa. Na msishangae kwa kuziona fatuwa zao, kwa sababu fatuwa hizi sio jambo geni. Na kama kuna shaka juu yangu, na moyoni mna wasiwasi juu ya usahihi wa madai niliyofanya, basi mimi naeleza njia rahisi ya kuondoa shaka, itakayomtuliza anayeutafuta ukweli. Na njia yenyewe ndiyo hii kwamba:

[234] Ni sikitiko kwa watu hao, hawakuwafikia Mtume yeyote ila walikuwa wanamfanyia mzaha. Sura Yaa Siin, 36:31

"Kwanza akifanya toba halisi ya kweli, asali rakaa mbili wakati wa usiku. Katika rakaa ya kwanza asome Sura Yaa Siin na katika rakaa ya pili asome Sura Ikhlaas mara 21, na baada ya hapo asome Sala ya Mtume[saw] mara mia tatu, na aombe ghofira mara mia tatu, halafu amwombe Mwenyezi Mungu dua hii kwamba:

> "Ewe Mweza Mkarimu, Wewe Wazielewa hali zilizofichika, nasi hatujui. Na mwenye kukataliwa na mzushi na mkweli hawezi kufichika machoni mwako. Basi kwa unyenyekevu twakuomba kwamba huyu mtu ambaye anadai kuwa ni Masihi Mau'udi, Mahdi na Mujadidi wa zama, ana hali gani mbele Yako? Je, yu mkweli au mwongo? Ni mwenye kukubalika au mwenye kukatalika? Kwa fadhili zako tudhihirishie hali hii kwa ruya, kashfi au ufunuo ili kama yu mwenye kukataliwa tusipotee kwa kumkubali; na kama ni mwenye kukubalika na ametoka Kwako, tusiangamie kwa kumkataa na kumtweza. Tulinde na kila aina ya fitina, kwani nguvu zote unazo Wewe. Amin.

"Istikhara hii muifanye kwa uchache kwa wiki mbili bila kupendelea upande wowote. Kwani, yule mtu ambaye amejaa bughudha na ametawaliwa na dhana mbaya, kama atataka kuuliza ndani ya ndoto hali ya mtu huyo ambaye anamfahamu kuwa ni mtu mbaya sana, basi shetani huja na kuongeza moyoni mwake mawazo yanayoafikiana na giza lile liliopo moyoni mwake. Basi hali yake inakuwa mbaya zaidi kuliko ile ya awali. Hivyo kama unataka kumwuliza Mwenyezi Mungu habari yoyote basi ukisafishe kifua chako na kuondolea mbali bughudha yote na inadi, na kuifanya nafsi yako isipendelee pande zote mbili za bughudha na mapenzi, umwombe nuru ya mwongozo, hapo hakuna budi kwamba sawa na ahadi Yake Ataterемsha nuru toka Kwake ambayo haitakuwa na moshi wowote wenye mawazo ya kinafsi.

"Hivyo, Enyi mtafutao ukweli! Msijali maneno ya Masheikh hao. Inukeni na mkijitahidi mkamwombe msaada Yule Mwenye

nguvu, Mweza na Mwongozi wa pekee. Na tazameni kuwa sasa nimeishafanya haya mahubiri ya kiroho pia. Sasa tangu hapo mnayo hiyari. Na amani iwe juu ya yule aufuataye mwongozo.

Mhubiri

Ghulam Ahmad, *Mungu Amsamehe*"[235]

UHAMIAJI WA HADHRAT MAULAWII ABDUL KARIM[RA], MWISHONI MWA MWAKA 1892

Japo Hadhrat Maulawii Abdul Karim[ra] Sialkoti alikuwa akimtembelea Hudhur[as] mara kwa mara, lakini mwishoni mwa mwaka 1892 akahama watani wake Sialkot na kuhamia Qadian kwa kudumu. Hadhrat Maulawii[ra] alikuwa na sifa nyingi njema. Alikuwa si tu mjuzi mahiri wa lugha tatu za Kiurdu, Kiajemi na Kiarabu, bali alikuwa na uwezo wa kuhutubia katika lugha hizo tatu kama lugha hizo ni za kwao. Alijua Kiingereza pia vizuri sana. Alikuwa akisoma Kurani Tukufu kwa sauti nzuri kiasi hiki kwamba wapitao njia wasiokuwa Waislamu pia walikuwa wakisimama kusikiliza sauti yake yenye kuvutia na kuathiri. Alikuwa na uwezo kamili wa kueleza Kurani Tukufu. Alikuwa na ghera sana ya dini. Alikuwa bingwa wa kutoa hotuba na kuandika. Alikuwa na sauti nzuri pia na sauti kubwa. Alikuwa anampenda sana mno Masihi Mau'udi[as]. Alipata heshima ya kufasiri baadhi ya vitabu vya Hudhur[as] katika Kiajemi. Tafsiri ya Kiajemi pia ya sehemu ya Kiarabu ya *Aina Kamalate Islam* inayoitwa "Tabligh" alifanya yeye, na pia tafsiri ya Kiajemi ya *Ayyamus Sulhi* cha Kiurdu. Alipata nafasi ya kusoma maandishi ya Hudhur[as] katika mikutano kadha. Hata katika mkutano maarufu wa Dini zote mjini Lahore, makala za Hudhur[as] zilizotoa majibu ya maswali matano, zinazojulikana kwa jina la "Hekima ya mafundisho ya Kislamu" akawasomea yeye. Alikuwa na shani ya ujalali, maisha mazima alikuwa imamu wa sala na hatibu wa Jumuiya. Na Mwenyezi Mungu Alimtaja katika ufunuo kuwa "Kiongozi wa Waislamu". Ee Allah, Umrehemu na Unurishe kaburi lake.

[235] Nishane Asmani, chapa ya Riadh Hind Amritsar, uk. 38-41

VITABU VYA MWAKA 1892

1. Uandikaji na uchapaji wa "*Nishane Asmani*". Madhumuni ya kitabu hiki yadhihirika kwa dondoo la juu.

2. Mwanzo wa kuandika *Aina Kamalate Islam*

MKUTANO WA MWAKA 1892

Katika mwaka 1892 pia upinzani mkali uliendelea katika nchi nzima, lakini idadi ya wafuasi wake, kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu, iliendelea kuzidi. Basi, ulipofika Mkutano wa Mwaka 1892, ndugu 327 walishiriki humo. Katika mkutano, zaidi ya hotuba ya Hudhur[as], Hadhrat Hakim Hafidh Maulana Nuruddin[ra] pia alihutubia. Katika zama zile hazikuwekwa siku maalum kwa shura kama inavyokuwa siku hizi, kwa hiyo kwa kutimiza mahitaji ya dini, namna ya shura pia ilikuwa ikifanyika katika siku za mkutano tu. Basi katika mkutano wa mwaka 1892 mapendekezo yafuatayo yaliletwa:

> Tarehe 28 Desemba 1892, kwa huruma ya kidini ya Ulaya na Marekani iliamuliwa kwamba:
>
> "Kijitabu kimoja kitayarishwe na kichapwe ambacho kikusanye mapasiko muhimu ya Islam na kionyeshe uso mzuri wa itikadi za Islam, na kisha baada ya kukichapisha, zitumwe nakala zake nyingi kule Ulaya na Marekani. Baada yake maoni yaliletwa kuwa tuwe na matbaa yetu katika Qadian. Na orodha ikatengenezwa ya watoa mchango ambao wataendelea kutuma kwa kusaidia matbaa. Hii pia iliamuliwa kwamba Hadhrat Maulawii Seyyid Muhammad Ahsan Amrohi awekwe kuwa Mhubiri wa Jumuiya hii na yeye atembelee Panjab na India. Baadaye maombi yalifanywa."[236]

HADHRAT MIR NASIR NAWAB KASHIRIKI KATIKA MKUTANO WA MWAKA 1892

Hadhrat Mir Nasir Nawab aliyekuwa bado hajajiunga na Jumuiya, bali alikuwa katika shaka shaka, yeye pia alikaribishwa na Hudhur[as] kupitia barua ili kushiriki mkutanoni. Matokeo yake yakawa kwa

[236] Taarifa ya Mkutano wa Mwaka 92, iliyonukuliwa kutoka *Aina Kamalate Islam.*

fadhili ya Mwenyezi Mungu kuwa shaka zake zote ziliondoka na kwa moyo safi alifanya baiati ya Hudhur[as]. *Alhamdu lillahi alaa dhalika*.[237]

UCHAPAJI WA AINA KAMALATE ISLAM, FEBRUARI 1893

Seyyidna Ahmad[as], katika safari zake mbalimbali aliwaahidi kwamba karibuni ataandika kitabu kitakachoitwa "Dafi'ul Wasaawis" na ndani yake shutuma zote zitajibiwa ambazo wajiitao Waislamu wenye fahamu ndogo na mtazamo finyu wananiletea. Kwa kutimiza ahadi hiyo, Hudhur[as] alianzia kuandika kitabu hicho katika nusu ya pili ya mwaka 1892, na akakichapisha mnamo Februari 1893. Kwa vile katika kitabu hicho zilielezwa sifa bora za ukamalifu wa Islam na mazuri ya Kurani Tukufu, kwa hiyo kitabu kikikamilika, Hudhur[as] Mwenyewe alikipa jina "*Aina Kamalate Islam*", ingawa jina lake la pili ni "*Dafi'ul Wasaawis*" pia.

Kwa kutangaza kitabu hicho, Hudhur[as] alichapisha tarehe 10 Agosti 1892 tangazo moja ambamo baada ya kueleza madhumuni ya kitabu akasema:

> "Ilmuradi, kitabu hiki kinajumuisha uchunguzi wa nadra na mwepesi unaofaa sana dhuria za Waislamu na ni sharubati iliyojaribiwa na ya kuponya sana kwa kukinga na kipindupindu cha kiroho cha siku hizi kinachohilikisha dunia kwa sumu yake. Na kwa vile kitabu hicho kinarekebisha ufisadi wa aina zote mbili, wa nje na wa ndani, kwa rai yangu nina yakini kwamba kitabu hicho ni njia bora na yenye baraka kwa kuidhihirishia dunia baraka za Islam, Kurani Tukufu na za Seyyidna wa Maulana Hadhrat Khatamul Ambiyaa[saw]."[238]

ZIARA YA MTUME MTUKUFU[SAW] MARA MBILI WAKATI WA KUANDIKA KITABU HICHO

Kutakuwa na uthibitisho gani mkubwa wa kitabu hicho kuwa chenye baraka na chenye faida kwa watu kuliko huu kwamba Hudhur[as] anasema:

---

[237] Kwa maelezo zaidi someni *Hayate Nasir* na sehemu ya mwisho ya *Aina Kamalate Islam.*

[238] Tablighe Risalat, J. 2 uk. 116

"Wakati wa kuandika kitabu hiki mara mbili nilimwona Mtume wa Mungu s.a.w. naye alidhihirisha furaha kubwa kwa kuandikwa kwa kitabu hiki. Na niliona usiku mmoja kwamba malaika mmoja anawaita watu mioyo yao kwa kupaza sauti na anasema: هٰذَا كِتَابٌ مُبَارَكٌ فَقُوْمُوْا لِلْإِجْلَالِ وَالْإِكْرَامِ , yaani kitabu hiki kimebarikiwa, basi simameni kwa kukitukuza na kukiheshimu."[239]

MAHUBIRI

Pamoja na kitabu hiki, kwa kushauriwa na Hadhrat Maulawii Abdul Karim Sialkoti, Hudhur[as] alichapisha barua moja pia kwa madarweshi na ***Mapirzada*** kwa lengo la kuwahubiri na kukamilisha hoja, ambayo kwanza Hudhur[as] alifikiri iandikwe katika Kiurdu, lakini kwa baadhi ya ishara ya kiufunuo ikafahamika kwamba barua hii iandikwe kwa Kiarabu. Na pia ikafunuliwa kwamba watu hao wataathirika kidogo sana; naam, hoja itakamilika. Hapo Hudhur[as] aliandika barua ile iliyounganishwa na Aina Kamalate Islam kwa jina la "At-Tabligh.' Sehemu hiyo ya kitabu ni maandishi ya kwanza ya Hudhur[as] katika lugha ya Kiarabu yaliyo mkusanyiko wenye maarifa wa ushairi na nathari.

MWITO WA ISLAM KWA MALKIA VICTORIA

Pamoja na kukamilisha hoja juu ya madarwesh na masheikh, Hudhur[as] alimwandikia Malikia Victoria pia barua ya mahubiri kwa lugha ya Kiarabu ambamo alimkaribisha Malkia kusilimu. Malkia aliipokea barua hiyo kwa shukrani nyingi na zaidi ya hayo aliomba vitabu vingine pia vya Hudhur[as].

WASIWASI WA MAPADRI

Siku hizo hizo mapadri wa Uingereza pia kwa kudura ya Mungu walipatwa na wasiwasi kwamba kuna haja ya kutia maanani mwendeleo mpya ulioibuka katika India dhidi ya Ukristo. Kwani, jinsi alivyoeleza, Islam hiyo ni hatari kubwa kwa Ukristo. Basi, katika

[239] Dhamima ya Kamalate Islam, Chapa ya kwanza, uk. 4

mwaka 1894, mapadri waliweka mkutano wa kimataifa katika London ambao Lord Bishop wa Gloucester, Reverend Charles John Ellicott, akidhihirisha wasiwasi sana alisema:

> "Katika Islam, alama za mwamko mpya ziko wazi. Wameniambia watu ambao wanao uzoefu kwamba katika serikali ya Uingereza katika India namna mpya ya Islam inatokeza na katika kisiwa hiki pia huko na huko alama zake zinaonekana... Hiyo inapinga sana bidaa zile ambazo kwazo tunaichukia dini ya Muhammad[saw]. Kwa sababu ya Islam hii mpya, Muhammad[saw] anaendelea kupata tena heshima ile ile ya awali. Mabadiliko hayo mapya yaweza kutambulika kwa urahisi. Tena Islam hiyo mpya ilivyo, si inajitetea tu bali yashambulia pia. Ni masikitiko makubwa kwamba mawazo ya baadhi yetu pia yanaielekea (Islam) hiyo."[240]

Hatari aliyodhihirisha Lord Bishop wa Gloucester katika hotuba yake, yapasa kuzalika moyoni mwa kila Mkristo mwenye akili kwa kusoma vitabu vya Hudhur[as], ***Izala Auham*** na ***Aina Kamalate Islam*** na vile vile "***Jange Mukaddas***" yaani mjadala wa Amritsar uliofanyika katika mwaka 1893 kabla ya Mkutano wa Wakristo utakaotajwa mbele. Kwani katika vitabu hivyo ikitangazwa kifo cha Masihi[as], itikadi za Uungu wa Yesu, Uana wa Yesu, Utatu na Kafara zilibatilishwa kwa nguvu sana. Kisha Islam ilielezwa katika sura yake sahihi hata kwamba haikubaki nafasi kwa wapinzani wasiokuwa Waislamu ya kuipinga kiakili. Bali ukweli ni huu kwamba yeyote miongoni mwa ***Mustashirikina*** akitalii Islam kwa uadilifu, iliyoelezwa na Hudhur[as], haibaki kwa ajili yake njia yoyote isipokuwa kukubali Islam.

KUZALIWA KWA HADHRAT MIRZA BASHIR AHMAD, 20 APRILI 1893

Mnamo 20 Aprili 1893 alizaliwa Hadhrat Mirza Bashir Ahmad, Mungu Amweke salama. Miezi minne kabla ya kuzaliwa kwake Seyyidna Ahmad[as] alipata ufunuo kama bishara:

[240] Taarifa ya Kiserikali ya Mkutano wa Mapadri, 1894. uk. 64

يَاتِيْ قَمَرُ الْاَنْبِيَآءِ وَاَمْرُكَ يَتَاَتّٰى ۔ يَسُرُّ اللّٰهُ وَجْهَكَ وَيُنِيْرُ بُرْهَانَكَ ۔

سَيُوْلَدُ لَكَ الْوَلَدُ وَيُدْنٰى مِنْكَ الْفَضْلُ ۔ اِنَّ نُوْرِيْ قَرِيْبٌ ۔

"Yaani, Mwezi wa Manabii atakuja na kazi yako itafanyika. Mwenyezi Mungu Atakuchangamsha na Atanurisha hoja yako. Karibuni mvulana atazaliwa kwako na fadhili itasogezwa karibu nawe. Bila shaka nuru yangu i karibu."

MWITO MWINGINE KWA MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII KUSHINDANA NAYE KIAMALI NA KIROHO

Imekwisha elezwa juu kuwa Seyyidna Ahmad[as] kwa kukamilisha hoja juu ya madarwesh na *mapirzada* ailichapisha barua moja kwa kichwa cha habari 'At-Tabligh' katika lugha ya Kiarabu. Maulawii Muhammad Husain Batalawii alipoiona barua hii, kwa kuonyesha kiburi cha kielimu aliitaja kama kitu kisicho na maana. Na katika jarida lake *Isha'atus Sunna* akamwita Hudhur kuwa asiyejua elimu ya Kiarabu, asiyejua elimu ya Kurani, na ─ Mungu Apishe mbali ─ mwongo na dajali. Hudhur[as] daima alikuwa akitafuta nafasi ya kufikishia haki. Yeye haraka sana akichapisha tangazo moja alimpa changamoto ya kuandika maelezo ya Kurani katika lugha ya Kiarabu kwa kushindana naye. Na kwa kushindana naye katika ujuzi wa lugha alimwita kuandika kasida fasihi na balighi katika shani ya Mtume Mtukufu[saw]. Na akatangaza kwamba kama Maulawii Muhammad Husain, atanishinda au atakuwa sawasawa nami sawa na waamuzi watakaowekwa, katika kuandika elimu ya ndani na maarifa ya Kurani kwa Kiarabu fasihi na vile vile katika kuandika kasida ya kumsifu Mtume[saw], basi papo hapo nitakiri kosa langu na nitachoma vitabu vyangu. Lakini kama Bwana Maulawii akishindwa mbele yangu basi itakuwa faradhi yake kwamba akichoma vitabu vyake atubu mkononi mwangu.[241]

Ingawa kwa kujibu tangazo hilo la Hudhur[as], Maulawii Muhammad Husain Batalawii kwa kudhihirisha ujuzi wake wa usheikh, aliandika kwamba nipo tayari kushindana nawe katika kila jambo, lakini kwa

[241] Muhtasari wa tangazo la 20 Machi 1893.

kitendo hakuja uwanjani kwa kushindana naye katika jambo lolote, na mpaka Hudhur[as] kufariki aliendelea kuhepa kila shindano la kiroho na kielimu.

MWITO WA MUBAHALA KWA WASIOKUWA WAISLAMU

Ni dhahiri kwamba kazi ya Hudhur[as] haikuwa kushindana na Waislamu tu, bali alitumwa kwa kurekebisha itikadi na mila zao. Lakini pia ilikuwa katika makusudio yake kwamba kwa kudhihirisha sifa za Islam kwa wasiokuwa Waislamu awakaribishe kwenye Islam. Basi pamoja na kuondoa makosa ya masheikh wa Kiislamu, daima akaweka mbele yake kusudio hili pia na kamwe hakulisahau. Tumeshataja mashindano yake na Wakristo na Waaria katika kurasa za nyuma. Kabla ya kuchapwa *Barahine Ahmadiyya* pia maishirini ya makala yenye thamani aliandika ya kupinga dini zingine. Akajadiliana nao, akadhihirisha kuwa yuko tayari kuonyesha ishara, lakini watu hao hawakuchagua njia yoyote ya kufanya uamuzi. Sasa kwa hoja ya mwisho, Hudhur[as] aliwaita pia kwenye mubahala. Akawaambia:

> "Sasa iwe wazi kwamba kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu hali yangu ni hii kwamba naifahamu Islam tu kuwa dini ya kweli, na naziona dini zingine kuwa batili na uongo mtupu. Nami naona kwamba kwa kuiamini Islam, chemchemi za nuru zinapita ndani yangu, na kwa kumpenda tu Mtume[saw] nimepata daraja la juu la kuongea na Mungu na kukubaliwa maombi, ambalo yeyote hataweza kulipata bila kuwa mfuasi wa kweli wa Mtume. Na kama Mabaniani na Wakristo na wengineo hata wakijifia kwa kuiomba miungu yao batili, hata hivyo hawawezi kupata daraja hili. Na Neno la Mungu ambalo wengine wanaliamini kama dhana tu, nalisikia. Nimeonyeshwa na kuambiwa na kufahamishwa kwamba katika dunia Islam pekee ndiyo haki, na nimedhihirishiwa kwamba hayo yote nimepewa kwa baraka ya kumfuasa Hadhrat Khtamul Ambiyaa[saw]. Hakuna mfano wake katika dini zingine, kwani hizo ni batili. Sasa kama yupo yeyote mtafuta ukweli, akiwa Baniani au Mkristo, Aria au Myahudi, Barhamu au yeyote mwingine, yeye mtu huyo ana nafasi nzuri kwamba aje kunikabili. Kama yeye akiweza kushindana nami

katika kudhihirisha mambo ya ghaibu na kukubaliwa maombi, basi nasema kwa kuapa kwamba nitamkabidhi mali yangu yote isiyohamishika iliyo na thamani ya karibu Rupia elfu kumi, au kwa njia yoyote akiridhika kutolewa fidia nitamridhisha.

Akawaambia hasa Wakristo:

"Kama mkisema kwamba hatushindani wala hatuna alama za waaminio, basi mwone kazi za Mungu za upande mmoja tu kwa sharti ya kusilimu. Na inapaswa kwamba miongoni mwenu watu mashuhuri na viongozi na waheshimiwa katika taifa lao, hao wote au mmoja wao aje kushindana nami. Na kama akishindwa kunikabili, basi akiahidi kwamba kama nikiona jambo ambalo haliwezi kufanyika na mwanadamu, nitaamini na nitakubali Islam, aniombe kuonyesha ishara yoyote. Na yapasa achapishe ahadi yake kama tangazo kwa kuapa kwa kuweka ushahidi wa watu 12, Wakristo, Waislamu na Mabaniani, yaani Wakristo wanne, Waislamu wanne na Mabaniani wanne, na nakala moja ya tangazo anitumie pia. Na kama Mwenyezi Mungu Akidhihirisha mwujiza wowote utakaokuwa zaidi ya uwezo wa kibinadamu, basi akubali Islam. Na asipokubali, hapo ishara ya pili ni hii kwamba nitamwomba Mungu wangu kwamba katika mwaka mmoja Amteremshie mtu kama huyo adhabu kali kama vile ukoma, upofu au mauti. Na kama dua hii isikubalike, basi hata hivyo nitalazimika kulipia faini yoyote itakayopendekezwa.

Sharti hilo hilo ni kwa Waaria pia. Kama wakiona Veda yao ni Neno la Mwenyezi Mungu na Kitabu chetu Kitakatifu kilicho Neno la Mungu ni uzushi wa mwanadamu, basi wajitokeze kunikabili. Na wakumbuke kwamba wakati wa kushindana watafedheheka sana. Wanao udaharia na ujanja mwingi kuliko wote usio na mipaka, lakini Mwenyezi Mungu Atawadhihirishia kwamba 'Mimi Nipo'.

Na wasipojitokeza kushindana, basi waone ishara kwangu kwa upande wangu tu bila kuweka sharti lolote bovu. Na yatosha kwa ishara yangu kuwa imetoka kwa Mungu kwamba kama

> Mwaria aliyeona ishara hasilimu bila kusita, nitamwombea dhidi yake. Basi, asiposhikwa katika mwaka moja na balaa ya ukoma au upofu au mauti, niko tayari kupokea adhabu yoyote. Na kwa watu wengine pia masharti ni hayo hayo. Na hata hivyo wasipokuja kunikabili, basi hoja ya Mwenyezi Mungu imekwishatimia juu yao."[242]

Ni masikitiko kwamba hakuna asiyekuwa Mwislamu yeyote aliyekubali kiamali mwito huu wa mubahala.

KUANDIKA KIJITABU BARAKAATUD DUA, 20 APRILI 1893

Kiongozi mkubwa Mwislamu wa India, marehemu Sir Seyyid Ahmad Khan, Mwanzilishi wa Darul 'Ulum Aligarh, alikuwa mwenye huruma kwa Waislamu, mstadi na kiongozi wa kisiasa. Lakini chini ya athari ya Magharibi akawa anafikiri kwamba dua ni ibada tu ambayo haileti matokeo katika dunia; naam, thawabu yake itapatikana huko akhera. Kwani tunaona maombi mengi hayaleti natija sawa na matakwa yetu. Na pia alikuwa anafikiri kwamba wahyi sio kitu cha kuja kutoka nje, bali unaibuka kutoka katika moyo tu. Ni dhahiri kwamba itikadi hizo mbili zilikuwa za hatari sana na kinyume kabisa na mafundisho ya Kiislamu. Kwa hiyo, Hudhur[as] aliandika kijitabu kimoja kiitwacho "Baraka za Dua" dhidi ya mawazo ya marehemu Sir Seyyid. Ndani yake aliandika kwamba itikadi hiyo ya Sir Seyyid ndiyo iliyovunjilia mbali mahusiano baina ya Mwumba na kiumbe. Isitoshe, yeye katika kijitabu hicho aliandika makala na kueleza kinaganaga kuhusu hali ya wahyi sawa na tajriba na ushuhuda wake, na kuhusu kukubaliwa kwa maombi, akatoa mfano wa utabiri wake aliotoa kuhusu kifo cha Lekhram, na akasema, kwa beti za Kiajemi:

> Ewe mtu unayesema kwamba kama dua ingekuwa na athari, basi hiyo iko wapi? Haraka sana njoo kwangu, nitakuonyesha athari ya dua kama jua. Habedari, usikane siri za kudra za Mungu. Katisha maneno, na uone kwangu mfano wa dua ipokelewayo.

[242] Kutoka Tangazo lililoandikwa katika *Aina Kamalate Islam,* chapa 1, uk. 272-278

Makala ambamo aliandika beti hizo, mada yake ilikuwa "Mfano wa dua iliyopokelewa", kwani mpaka wakati huo utabiri wa Lekhram kuuliwa ulikuwa haujatimia.

UTABIRI KUHUSU MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII, 4 MEI 1893

Katika zama zile ambapo Maulawii Muhammad Husain Batalawii alikuwa anampinga Hudhur[as] vikali sana kuliko wapinzani wengine, Hudhur[as] aliona ruya hii kumhusu yeye:

وَإِنِّيْ رَأَيْتُ اَنَّ هٰذَا الرَّجُلَ يُؤْمِنُ بِاِيْمَانِيْ قَبْلَ مَوْتِهٖ وَرَئَيْتُ كَاَنَّهٗ تَرَكَ قَوْلَ التَّكْفِيْرِ وَتَابَ وَهٰذِهٖ رُؤْيَايَ وَاَرْجُوْ اَنْ يَّجْعَلَهَا رَبِّيْ حَقًّا۔

Yaani, niliota kwamba mtu huyu kabla ya kifo chake atakiri kuwa mimi ni muumini. Nami niliona kwamba ameacha fatuwa ya kufuru na ametubu. Hii ni ruya yangu, na nategemea kwamba Mungu wangu Ataitimiza."

Kwa kutimiza ruya hiyo ya Hudhur[as], Mwenyezi Mungu Alizalisha sababu zake kwamba katika mahakama ya hakimu wa daraja la kwanza wa Gujranwala, Bwana Lala Devki Nandan, Maulawii Muhammad Husain Batalawii akiwa shahidi alikiri kwamba:

> "Madhehebu yote haya yanaamini Kurani Tukufu kuwa Neno la Mungu, na makundi haya yanaamini Hadithi pia jinsi yaaminivyo Kurani. Dhehebu moja la Ahmadiyya pia lililopatikana tangu muda mfupi, tangu Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian alipodai kuwa Masihi na Mahdi, dhehebu hili pia linaamini barabara Kurani na Hadithi… Dhehebu lolote lililotajwa juu, kundi letu halililiti kuwa kafiri kamwe."

Ni ya kushangaza kwamba Maulawii Muhammad Husain Batalawii aliyekuwa akimwita Hudhur[as] kafiri na kafiri mkubwa, na kumtaja kwa maneno mengine mengi akakiri kwa uwazi katika mahakama ya Gujranwala kwamba Waahmadiyya ni Waislamu, ambapo mwanamke mmoja alitaka kutengana na mume wake kwani yu Mwahmadiyya.

HABARI ZA MJADALA "VITA TAKATIFU"

Vita Takatifu ni mjadala ule wa Seyyidna Ahmad[as] aliofanya na mapadri huko Amritsar kuanzia tarehe 22 Mei 1893 hadi 5 Juni 1893. Mjadala huo ulisababishwaje? Kuhusu habari hii shahidi mmoja aliyeshuhudia kwa macho mjadala huo, Hadhrat Sheikh Nur Ahmad[ra], mmiliki wa matbaa ya Riadhe Hind Amritsar, anasimulia kwamba siku moja nilikuwa kwa Hudhur[as] katika Qadian takatifu ambapo:

> "Barua kutoka Jandiala, ya Mwislamu mmoja aitwaye Panda ilimwasilia Hadhrat Masihi Mau'udi[as]. Kwa vile katika Jandiala kulikuwa na misheni kubwa ya mapadri na wahubiri wake walikuwa wakihubiri sokoni, Bwana Panda aliwafundisha wanafunzi wake baadhi ya maswali kuhusu Injili. Wanafunzi hao walikuwa wakijadiliana na wahubiri wa Kikristo na kwa kutaja maswali walikuwa wakiomba jibu. Wakristo hao wasipoweza kujibu sawasawa, wakamwambia Dkt. Henry Martin Clark kwamba wanafunzi wa Mwislamu Panda wanatusumbua sana, hao wazuiliwe kwa njia yoyote. Bwana Henry Martin akaja Jandiala na alimwambia Bwana Panda kwamba umewafanya wanafunzi wako wawafuate wahubiri wetu na kuwasumbua, hiyo haina faida yoyote. Afadhali mwitishe mkutano na kuwaleta masheikh wako. Kisha itajulikana dini ipi ni ya haki. Na uwakataze vijana hao wasiwasumbue wahubiri wetu. Hapo Bwana Panda alikubali pendekezo hili na alianza kuwaandikia barua masheikh kwamba waje Jandiala kujadiliana na mapadri juu ya ukweli wa Islam. Akamwandikia barua moja Hadhrat Masihi Mau'udi[as], iliyofika Qadian nilipokuwepo hapo. Kwa kusoma barua hiyo Hudhur[as] alifurahi sana na akaniambia kwamba Mwenyezi Mungu Ametuletea windo moja, twatuma jibu lake leo hii hii. Na akasema kwamba barua moja itaandikwa kwa Bwana Panda na nyingine kwa Bwana Padri. Tumejua kwa tajriba kwamba Bwana Padri atajibu haraka, na hatujui kuhusu Bwana Panda lini atajibu. Keshoye nikaenda Amritsar. Bwana Padri alijibu

kwamba mie niko tayari. Madhumuni ya barua ya Hudhur[as] ilikuwa kwamba kama mkutano utafanyika katika Jandiala au Amritsar au Batala, basi tutakuja kwa matumizi yetu, hatutakuwa sababu ya shida kwa yeyote. Na kama nyinyi mkija Qadian, na mjadala ufanyike, basi gharama yote ya safari na vyakula itakuwa juu yetu. Kwa kujibu, Bwana Henry Martin Clark aliandika kwamba baada ya kushauriana utaarifiwa. Bwana Panda pia aliandikiwa barua ya madhumuni hiyo. Bwana Panda alikuwa akingoja majibu ya masheikh ya kwamba watajibu nini. Katika hali hii wiki mbili zilipita. Masheikh wakijibu walimwuliza Bwana Panda kwamba kuna mpango gani wa kukaa kwetu, matumizi ya safari ya kuenda na kurudi na vyakula? Na baada ya mkutano tutapata zawadi kiasi gani? Bwana Panda alimwandikia Hudhur[as] kwamba masheikh wanaomba zawadi na matumizi ya safari na mie mtu maskini. Kwa vile unafanya kazi kwa kupata ridhaa hasa ya Mungu, kwa hiyo nakuomba wewe tu njoo, nami najitenga na masheikh ambao hawana kitu kwa Mungu. Hadhrat Masihi Mau'udi[as] alipojua jambo hili, alimwandikia barua tena padre Martin Clark kwamba inapaswa kupanga tarehe yoyote ya mjadala, ndugu zetu kadha wanafika kwako, upange nao masharti ya mjadala na tarehe. Vile vile Hudhur[as] alimfikishia Bwana Panda pia barua kwa mkono wa Yusuf Khan ambamo alisisitiza kupanga tarehe ya mjadala, pia alimwuliza kwamba padre gani atajadili kwa niaba ya mapadri? Bwana Yusuf Khan kwanza akaja kwangu, kisha akaenda Jandiala. Alinielezea hali yote. Hapo Mwenyezi Mungu Alinitilia moyoni kwamba nimtafute yule Padre atakayefanya mjadala kwa niaba ya mapadri. Nilikwenda kwenye duka la seremala Qutb Din kwamba aache kazi na aende nami ili tumwulize Padri Imaduddin kwamba padre yupi kwa niaba ya Wakristo atakuja katika mjadala. Bwana seremala akiacha kazi akaja nami. Sisi wawili tulikwenda nyumbani kwa Padre Imaduddin na kumwuliza kwamba ni padre yupi aliyeanza kuandikiana na Hudhur[as] kwa mjadala? … Akasema kwamba nafikiri ni kijana Henry Martin Clark. Kwa kusikia hii nalifika

Mission Hospital, hapo Henry Martin Clark alikuwa amekaa chumbani... Aliuliza, una kazi gani? Nilijibu kwamba nimekuja kuhusu tarehe ya mkutano wa mjadala wa Jandiala. Wafuasi wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wanakuja kupanga tarehe, wakati na masharti. Niwalete kwa nani na wapi? Akasema, sina nafasi, naenda kwa ziara, natengeneza ratiba ya ziara. Nikasema, kwa shauku uende kwa ziara, lakini uamue tarehe kabla ya kuenda … hii ni kazi ya dakika chache tu. Bwana padre kwa udhuru mwingi alisema uwalete watu wako, nitaweza kutoa nafasi ya nusu saa tu, katika muda huo masharti yatapangwa... Nalifika kwenye stesheni na watu ambao walikuja kutoka Qadian niliwaambia wote kusubiri hapo hapo kwenye stesheni. Miongoni mwao walikuwepo Hadhrat Maulawii Abdul Karim Sialkoti, Munshi Ghulam Qadir Fasihi Sialkoti na Munshi Zafar Ahmad Kapurthalawii. Ndugu wote walipojumuika, … sisi kwa kupanda magari 3-4 pamoja na matandiko tulifika moja kwa moja jumbani kwa Bwana padre. Bwana padre alikuwepo nyumbani. Baada ya kufika kwetu yeye alimwamrisha hadimu wake kuweka viti barazani na mwenyewe katoka katika mlango mwingine akaenda nyumani kwa Padre Abdullah Atham. Muda kidogo ulipopita tulimwuliza hadimu kwamba kwa nini Bwana Dkt. haji nje. Akasema, atakuja sasa hivi, ameenda nyumbani kwa Bwana Atham iliyo karibu, kuna barabara tu katikati. Na wakati wa alasiri uliwadia. Katika boma la jumba hilo kulikuwepo mti mkubwa sana wa mbaniani. Sisi sote tulisali pamoja chini yake. Bwana Dkt. alimwambia Bwana Atham kwamba kutoka Qadian watu wachache wamekuja kwa kupanga masharti na tarehe ya mkutano wa mjadala, twende tukapange nao tarehe na masharti. Katika muda huo kutoka Jandiala Bwana Panda pia akafika. Hapo Bwana Atham aliweka mikono kwenye masikio na akasema kwamba Bwana Daktari, kama wangekuwa masheikh wengine hata mia moja haingekuwa shida, mbona umejiletea matata; si rahisi kushindana na Bwana Mirza wa Qadian. Hii ni kazi ngumu sana, wewe umeanzia fitina hii basi nawe ufanye kazi hii mwenyewe, sitaenda kamwe

wala sitashiriki ndani yake. Bwana Dkt. alimwambia kwamba u mpigaji mweleka wa kaumu ya Kikristo na wewe tu unaweza kutekeleza vizuri jukumu hili, kwa kukutegemea wewe nimeanza kazi hii na wewe unaikana. Utalazimika kushiriki. Maongezi yao yakawa marefu. Bwana Dkt. alitaka kumleta pamoja naye, na Bwana Atham akang'ang'ania kukataa. Hatimaye kwa kumbembeleza kwa kumpa moyo, Bwana Dkt. akamleta Bwana Atham. Mazungumzo ya hao wawili yalijulikana baadaye kwa kuelezwa na mpishi Mwislamu wa Abdullah Atham. Walipofika wote wawili na kuketi vitini, mara Bwana Atham akatamka "Hae, nimekufa." Baada yake nilianza kuongea kwamba inapaswa kuamua tarehe na kwamba mjadala utaendelea kwa siku ngapi, na vilevile kwamba mjadala uwe kimaandishi na uandikwe saa ile ile. Basi, baada ya mazungumzo tarehe ilipangwa na siku 15 ziliwekwa kwa kujadili… Masheikh wa Amritsar na Batala walipojua, walimfikia Bwana Atham nyumbani kwake na wakasema kwa nini hukukubali kujadili na masheikh wengine. Kwa nini umeridhika kujadiliana na Bwana Mirza; masheikh wote wanamwita kafiri na fatuwa za kufuru zimeshatolewa dhidi yake na wafuasi wake. Bwana Atham mapema alikuwa na hofu ya Hudhur[as], basi akamwambia Dkt. Henry Martin Clark kwamba nilisema mapema si rahisi kujadilina na Bwana Mirza, "ni kutia mkono katika kiota cha nyigu". Sasa ni nafasi nzuri ya kujisalimisha, afadhali kujiokoa. Mkatae Bwana Mirza, na bila shaka fanyeni mjadala na masheikh hao, hakuna tatizo. Baada ya kushauriana, mapadre walimwandikia Hudhur[as] kwamba sasa masheikh wengine wako tayari kwa mjadala basi usisumbuke kuja kwa kujadili. Kwa kuwa Waislamu wengine wote wanawaiteni makafiri, kwa hiyo huwezi kuwa mwakilishi wa Islam. Kwa hiyo twakusudia kujadilina na masheikh, si wewe. Hudhur[as] aliwajibu kwamba si sahihi kukataa kwenu sasa. Tunayo maandishi yenu, ahadi zenu na masharti yaliyokubaliwa nanyi. Basi mtalazimika kufanya mjadala au mtalazimika kukubali ushinde. Kama mkitangaza jambo hili katika magazeti

na mkikubali kushindwa kwenu, kisha mna hiari ya kujadiliana na sheikh yeyote mnayemtaka. Vilevile alisema kwamba mnatusuta kwa fatuwa za kutukufurisha ilihali fatuwa hizo haziwezi kulingana nasi. Kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu sisi ni Waislamu wa kweli, pamoja nasi kuna Jumuiya ya wacha Mungu, wasomi na wanachuoni. Na zipo fatuwa za kufuru dhidi yenu pia. Waprotestanti wana yakini kwamba Wakatoliki ni makafiri bali wanawajibika kuuawa. Hivyo, nanyi pia hamwezi kuwa wawakilishi wa Ukristo. Basi katika fatuwa za kufuru sisi na nyinyi tupo sawa. Kwa kweli mjadala ni juu ya haki na batili kwamba ukweli upo upande wenu au sisi tupo juu ya haki, hapo hamna swala la fatuwa za kufuru. Sisi tutaiwakilisha Islam na Kurani Tukufu, na nyinyi Injili. Hilo linahusikanaje na fatuwa za kufuru… iliamuliwa kuwa watu hamsini kutoka kwa kila upande kuhudhuria katika mjadala, minghairi ya hao yeyote mwingine hawezi kuenda huko. Siku ya kwanza wakati wa kuenda kwa mjadala Hudhur[as] alimwambia Sheikh Haamid Ali achukue pamoja naye glasi moja na mtungi mmoja. Tulipoingia jumbani mwa Dkt. Martin Clark, tukajua kwamba mjadala umepangwa katika veranda ya jumba ambapo masharti yalipangwa, kwani hiyo ilikuwa yenye wasaa wa kutosha. Dkt. Henry Clark alikuwa ameagiza mitungi mikubwa mipya ya udongo uliookwa na alitia ndani yake barafu na sukari pia, ili kuwakirimu Waislamu na sharubati baridi. Mpishi wa Bwana Dkt. alimletea Hudhur[as] glasi moja ya sharubati baridi, lakini Hudhur[as] alisema tumeshaleta maji ya kunywa kwa ajili yetu; mimi na wenzangu hatutakunywa maji mengine, Waislamu wengine wanayo hiari yao. Hii ni vita ya kidini kati yetu na mapadre, tutakapopatana kisha halitakuwa tatizo lolote katika kunywa maji na kadhalika. Waislamu wengine wasiokuwa Waahmadiyya pia waliathirika na jambo hilo, hao nao hawakunywa maji yale, na mitungi ile yote ilibaki pale ilivyokuwa. Wakristo wenyewe waliendelea kunywa maji hayo. Waislamu waliendelea kupata maji ya kunywa kutoka kisima kingine."

Kisha mjadala ulianza, na makala zilianzia kuandikwa. Baada ya kukamilisha makala ilikuwa inasomwa kwa kusimama. Maulawii Abdul Karim[ra] alipokuwa akisimama kusoma makala ya Hudhur[as], alikuwa akisoma kwanza Suratul Faatiha, kisha akasoma kila neno la maandishi mara mbili tatu. Hapo Dkt. Henry Martin Clark akasema, angalia Bwana, imeandikwa mara moja, kwa nini unarudia kusoma, mara mbili tatu, lakini yeye hakujali na aliendelea kusoma hivyo hivyo. Mwenyezi Mungu Alimjaalia busara ya kiroho. Yeye kwa kila neno alikuwa akipata ladha na raha. Mapadre waliendelea kulalamika, na yeye akaendelea kufanya vivyo hivyo. Niliona kwamba nje mamia ya watu wamesimama. Nikainuka na kusema kwamba watu wengi wana hamu ya kusikiliza mjadala huu na halaiki kubwa imesimama nje, na watu 50-50 tu wanaruhusiwa kuingia ndani ya jumba, na kwa kuingia tiketi inahitajika. Kwa hiyo napenda kwamba makala za pande zote mbili za mjadala niendelee kuchapisha katika matbaa yangu. Hapo Hudhur[as] alisema ipo ruhusa upande wetu, waweza kuchapisha. Kisha kwa kujihadhari niliwauliza mapadre pia kwamba mwasemaje juu ya jambo hilo? Hapo Bwana Atham alisema kwa sauti ndogo, naam, kuna ruhusa upande wetu pia. Basi niliendelea kuchapisha kila siku makala za pande zote mbili na watu wakanunua.

Kwa njia hii mjadala uliendelea siku 15. Katika kupinga uungu wa Masihi, Hudhur[as] alipoandikisha kwamba mnamwita mungu mtu mnyonge na dhaifu aliyekaa miezi 9 katika tumbo la mama akikulia kwa damu ya hedhi, akazaliwa kama watu wengine wa kawaida. Je mtu kama huyo pia aweza kuwa Mungu? Hapo mapadre wakasimama na kusema kwamba hatutaki kusikiliza maneno ya namna hii kuhusu Bwana Yesu Kristo. Bwana Mirza anatupiga visu vifuani mwetu, na anapiga panga shingoni mwetu, na wakawa tayari kuacha mjadala na kuondoka. Kuona hali hii Hudhur[as] alisema kwamba hao sasa lazima watakimbia, andikeni tu ninayoandikisha. Kuona hali hii, padre Martin Clark alisema kwamba nilidhani kwamba Waislamu watapiga makelele, kinyume chake Wakristo wameanza kupiga makelele. Akawaambia Wakristo kwamba kaeni, sasa haitafaa kukimbia kwenu. Huu ni wakati wa bidii, kaeni nyote. Ilmuradi, Hudhur[as] alipinga uungu wa Yesu kwa namna ambavyo

Wakristo wakashindwa kujibu.

Mtu ambaye atakisoma kitabu kiitwacho ***Jange Mukaddas*** kinachoeleza kikamilifu habari za mjadala, mwenyewe atapata kujua hali zote. Bwana Atham akishindwa kujibu alilazimika kuandikisha katika makala yake kwamba kwa miaka thelathini Masihi alikuwa sawa na wanadamu wa kawaida, na Roho Mtakatifu alipomshukia ndipo akaitwa Onyesho la Mungu. Hapo, Hudhur[as] akaandikisha kwamba ndivyo sisi pia tunavyosema kwamba Masihi alikuwa mwanadamu na nabii. Malaika mtakatifu amshukiapo mtu hapo yeye anakuwa Onyesho la Mungu, yaani amekuwa nabii. Kusikia jambo hilo Wakristo wakageuka rangi. Bwana Henry Martin akafadhaika na Bwana Atham naye kafadhaika. Wakristo haraka sana wakamwambia Bwana Atham kwamba hii umeandikisha nini. Bwana Atham akajibu kwamba ningeandikisha nini tena, iliyopaswa kuandikishwa niliandikisha. Mimi ni mgonjwa, niacheni niende andikisheni mnayotaka.

Wasomaji wanaweza kujua hali hiyo yote kwa picha ya Vita Takatifu. Bwana Atham akaathirika na ukweli. Bwana Atham akawa mgonjwa, lakini katika siku za mwisho kwa kuombwa na kusisitizwa na Wakristo alikuwa akija. Katikati Bwana Henry Martin Clark alichaguliwa kwa kujadili; yeye alipitisha siku zote kwa shida kwa mambo ya hapa na pale.[243]

DEPUTY ABDULLAH ATHAM HAKUSHIKAMANA NA MASHARTI YA MJADALA

Kati ya masharti ya mjadala, sharti moja lilikuwa kwamba makundi yote mawili wataleta madai na hoja zao kutoka katika vitabu vyao vilivyofunuliwa, Kurani Tukufu na Biblia. Lakini Bwana padre hakufuata kabisa sharti hilo kiasi hiki kwamba Hudhur[as] alilazimika aandikishe katika maandishi yake ya mwisho:

> "Nasikitika sana kwamba masharti yaliyowekwa kwa mjadala, Bwana Deputy hakujali hata kidogo masharti hayo. Sharti lilikuwa hili kwamba jinsi nilivyoandelea kuleta kila dai langu na

[243] *Nur Ahmad*, uk. 20 hadi 32

kila dalili kutoka katika hoja za kiakili za Kurani Tukufu, Bwana Deputy pia alitakiwa kufanya hivyo, lakini wakati wowote yeye hakuweza kulitimiza sharti hilo."

TUKIO MOJA LA AJABU

"Katika mjadala, siku moja, Wakristo walileta kisirisiri kipofu mmoja, kiziwi mmoja na kiwete mmoja, na wakawakalisha kando katika hafla ya mjadala. Kisha katika hotuba yake, padre alimwambia Hudhur[as] kwamba unadai kuwa Masihi, hawa ndio kipofu, kiziwi na kiwete, uwaponye kama Masihi kwa kugusa na mkono. Bwana Mir[244] anasimulia kwamba sote tulishangaa kwamba tuone sasa Hudhur[as] anajibuje. Kisha Hudhur[as] alianza kuandikisha jibu lake. Akasema kwamba mimi siamini kwamba Masihi alikuwa akiwaponya vipofu, viziwi na viwete kwa kugusa kwa mkono. Kwa hiyo, ombi hilo haliwezi kuwa hoja hata kidogo. Naam, nyinyi mnakubali miujiza kama hiyo ya Masihi, na upande mwingine mnaamini kwamba mtu atakayekuwa na imani sawa na chembe ya haradali pia anaweza kuonyesha yale yote aliyoonyesha Masihi. Basi, ninawashukuruni sana mmenisaidia kutafuta vipofu, viziwi na viwete. Sasa, zawadi yenu mnaletewa; wapo vipofu, viziwi na viwete, kama mna imani sawa na chembe ya haradali, basi sawa na suna ya Masihi mwaponye. Bwana Mir anasimulia kwamba Hudhur[as] aliposema hayo, mapadre wakapigwa na butwaa, nao wakiashiria wakawatorosha."[245]

UTABIRI KUHUSU ABDULLAH ATHAM

Katika maandishi yake ya mwisho, Hudhur[as] alitangaza kwa idhini ya Mungu utabiri pia kuhusu Padre Abdullah Atham, ambao ni huu:

"Leo usiku habari niliyofunuliwa ni hii kwamba wakati nilipomwomba sana Mungu kwa unyenyekevu na vilio kwamba utoe uamuzi katika jambo hili, sisi ni watumishi wako wanyonge, hatuwezi kufanya kitu bila uamuzi wako, basi, Yeye

[244] Muradi wake ni marehemu[ra] Hadhrat Dkt. Mir Muhammad Ismaili aliyekuwa mjomba wa Hadhrat Khalifatul Masihi II[atba].

[245] Usimuliza Na.176 wa Hadhrat Mir Muhammad Ismaili[ra], Siratul Mahdi, sehemu 1 uk.191-192.

> Amenipa ishara hii, ikiwa habari njema, kwamba katika mjadala huu, kati ya makundi mawili, mtu anayefuata uongo kusudi na anamwacha Mungu wa kweli na anamfanya mwanadamu mnyonge kuwa Mungu, kulingana na siku hizi za mjadala — yaani, kila siku ikiwa kama mwezi mmoja — yaani ndani ya miezi 15 atatupwa katika *Hawia* na atapata fedheha kubwa sana, sharti asirejee kwenye haki. Na yule mtu ambaye ni juu ya haki na anamwamini Mungu wa kweli, atapata heshima kwayo, na wakati utabiri huu utakapodhihiri, baadhi ya vipofu watapata kuona na baadhi ya viwete wataanza kutembea na baadhi ya viziwi wataanza kusikia"[246]

Sababu ya utabiri huu, Hudhur[as] alieleza, ni kwamba mjadili Mkristo, Bwana Deputy Abdullah Atham, aliandika kitabu kiitwacho "***Andruna Bible***". Katika kitabu hicho alimwita Mtume Mtukufu[saw] "dajali", Mungu Apishe mbali, na aliidhihaki Islam pia. Hudhur[as] pamoja na utabiri huo alipomkumbusha jambo hilo pia, "mara alitoa ulimi wake na akaweka mikono juu ya masikio, akageuka rangi, macho yakakodoka na akitingisha kichwa alisema sikuandika hivyo."[247]

Kwa hakika aliandika hivyo, lakini kwa hofu ya utabiri akafadhaika sana na katika hali hiyo akasema kwamba sikumwita dajali, "kana kwamba saa ile ile akadhihirisha kurejea kwenye haki, na baada yake mpaka kifo chake hakuandika hata neno moja dhidi ya Islam au Mtume Mtukufu[saw]. Kwa mwisho wa Atham na hali ya utabiri wa ufunuo someni "***Anwarul Islam***" na "***Anjame Atham***".[248]

BAIATI WAKATI WA MJADALA

Katika Amritsar, Hadhrat Sheikh Nur Ahmad[ra] na Hadhrat Qutb Din[ra] seremala tayari walikuwa Waahmadiyya. Sasa katika siku za mjadala, Hadhrat Mian Nabii Bakhsh mtililiaji, Hadhrat Kadhi Amir Husain Bherawii[ra] pia walifanya baiati. Bwana Kadhi alikuwa mtu mwema asiye na 'umimi'. Na alikuwa mwalimu katika Madrasa

[246] Vita Takatifu

[247] Kijitabu *Nur Ahmad*, uk. 32

[248] Kijitabu *Nur Ahmad*, uk. 32

Islamia. Kwa vile alikuwa mwanachuoni mkubwa wa Hadithi, kwa hiyo kwa sababu ya baiati yake masheikh walipiga makelele sana. Katika kila mtaa masheikh walianza kumtusi Hudhur[as] na walianza kusisitiza kwamba mtu yeyote asiende kusikiliza waadhi wa "Mirza", waila "atawindwa" naye, na kadhalika. Na wakaanzia kumtumia Hudhur[as] ujumbe kuwapitia watu wengine kwamba ujadiliane nasi. Hudhur[as] akasema kwamba niacheni nimalize kwanza kujadiliana na Wakristo, kisha, inshallah, tutajadiliana nanyi pia.

MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII KAKIMBIA MUBAHALA, NA SHEIKH ABDUL HAK GAZNAWII KA-ELEKEA

"Mjadala ulipoisha, masheikh walipiga makelele tena kwamba mjadala kwa Wakristo umekwisha, sasa ujadiliane nasi. Maulawii Muhammad Husain Batalawii pia alituma tangazo moja kutoka Lahore kwamba naja Amritsar kwa mubahala na Bwana Mirza, utakuwa mubahala tu, na haitatolewa hotuba yoyote. Kwa kulijibu, Hudhur[as] akatoa tangazo moja kwamba Maulawii Muhammad Husain hatafanya mubahala nami kamwe wala hatakuja hata mbele yangu. Kesho yake ilikuwa siku ya mubahala na Sheikh Abdul Hak Ghaznawii. Maulawii Muhammad Husain pia alifika Amritsar. Katika uwanja wa kusalia Idi, halaiki ya watu walihudhuria, na Maulawii Muhammad Husain pia akisimama mbali na watu, alianza kutoa hotuba. Watu walidhani kwamba baada ya hotuba, Bwana Maulawii atafanya mubahala. Bwana Mirza aliandika kwamba hatakuja mbele yangu kwa mubahala lakini huyu akaja. Katoa hotuba kwa nusu saa au robo tatu, hapo Sheikh Abdul Hak, mwanafunzi wa Maghaznawii, kwa kushauriana na masheikh wa ki-Ghaznawii akaja mbele kwa mubahala.[249]

Katika mubahala huo, Sheikh Abdul Hak hakutamka kwa ulimi hata neno moja kujihusu yeye mwenyewe, lakini hakuacha nafasi yoyote katika kutumia maneno makali sana dhidi ya Hudhur[as] na kuchafua ulimi wake kwa matusi. Kwa kujibu, Hudhur[as] alirudia maneno haya tu:

[249] Kijitabu *Nur Ahmad,* uk. 32-33

> "Nitaomba kwamba katika vitabu vyangu vyote hata kimojawapo hakipo kinyume cha kauli ya Mungu na Mtume[saw], wala mimi si kafiri. Na kama vitabu vyangu viko kinyume cha kauli ya Mungu na Mtume[saw] na vimejaa kufuru tupu, basi Mwenyezi Mungu Aniteremshie laana na adhabu ile ambayo Hajamteremshia kafiri yeyote tangu kuanzia dunia mpaka leo, na nyinyi mseme 'Amin'. Kwani, kama mimi ni kafiri na nimeritadi dini ya Islam wala sina imani, basi ni afadhali nife kwa adhabu mbaya sana, na mimi nachukia maisha ya namna hii sana mno. Na kama sivyo hivyo, basi Mwenyezi Mungu kutoka kwake Ataleta uamuzi wa kweli. Yeye Anaona moyo wangu pia na moyo wa wapinzani pia."

Watazamaji wanasimulia kwamba Hudhur[as] alipokuwa anarudia maneno hayo, hali ilikuwa ya ajabu sana, watu wakalia sana.

BAIATI YA HAFIDH MUHAMMAD YAKUB

Hudhur[as] bado alikuwa hajamaliza dua yake, Hafidh Muhammad Yakub aliyekuwa kaka wa Hafidh Muhammad Yusuf, Mkuu wa Wilaya wa mfereji na alikuwa mfuasi wa Maghaznawii, akilia kwa sauti kubwa akaanguka miguuni pa Hudhur[as] na akaomba, 'ukubali baiati yangu'. Hudhur[as] akasema, ukiisha mubahala, nitapokea baiati. Kuona hali hii masheikh wa Ghaznawii na wafuasi wao wakapigwa na bumbuazi, kwani walihisi kwamba huu ni ushindi wa kwanza wa Hudhur[as]ikiwa ni natija ya mubahala. Maulawii Muhammad Husain Batalawii alipotea wapi, Mungu tu Ajua. Wakati ule watu walipata yakini kwamba aliyosema Hudhur[as] kwamba Maulawii Muhammad Husain hatakuja mbele yangu imethibitika kuwa kweli. Kwa vyovyote mubahala uliishia hivyo, na Hudhur[as] alirudi makazini mwake.

ATHARI YA MUBAHALA

Mubahala huo ulikuwa na athari gani? Hudhur[as] katika kitabu chake *Anjame Atham* ameandika mambo kumi yanayodhihirisha kwamba baada ya mubahala huo Mwenyezi Mungu Alimpa baraka nyingi mno za kiroho na kimwili. Hapa chini twaandika muhtasari wa mambo hayo kumi kwa maneno ya Hudhur[as] mwenyewe:

Mosi: Utabiri uliofanywa kuhusu Atham ulitimia kwa maana yake ya kweli.

La pili lililosababisha heshima yangu baada ya mubahala ni kusanyiko la vitabu vya Kiarabu vilivyoandikwa kwa kudhalilisha masheikh na mapadre wapinzani.

La tatu: Kabla ya mubahala, pengine watu 300-400 hivi walikuwepo, na sasa watu zaidi ya elfu nane ni wale ambao wanajibidiisha katia njia hii.

La nne lililosababisha heshima yangu baada ya mubahala ni kupatwa kwa mwezi na jua katika Ramadhani. Basi, baada ya mubahala, Mungu Amenipa heshima hii pia.

La tano lililosababisha heshima yangu baada ya mubahala ni kukamilisha hoja katika elimu ya Kurani... miongoni mwenu yeyote hawezi kujasiri kwamba aweze kunikabili kueleza kweli na maarifa ya Kurani Tukufu.

La sita lililosababisha heshima yangu, na fedheha ya Abdul Hak baada ya mubahala, ni hili kwamba Abdul Hak alitangaza baada ya mubahala kuwa yeye atajaaliwa mwana, na mimi pia kwa kufunuliwa na Mwenyezi Mungu nilichapisha tangazo katika ***Anwarul Islam*** kwamba Mwenyezi Mugnu Atanijaalia mwana. Basi kwa fadhili na ukarimu wa Mwenyezi Mungu Amenijaalia mwana, jina lake Sharif Ahmad. Sasa Abdul Hak lazima anapaswa kuulizwa kwamba mwana wake yuko wapi?

La saba lililosababisha heshima na kukubaliwa kwangu baada ya mubahala ni jazba ya ikhlasi ya waja wakweli wa Mungu waliyoonyesha kunihudumia. Sitakuwa na uwezo kamwe kwamba niweze kushukuru hisani hizi za Mungu za kiroho na za kimwili nilizozipata baada ya mubahala.

Mfano wa neema za kiroho nimeshaandika, yaani Mwenyezi Mungu Amenijaalia elimu ya Kurani na elimu ya lugha kimwujiza namna ambavyo mbele yake sio Abdul Hak pekee bali wapinzani wote walifedheheka. Na neema za kimwili nilizojaaliwa baada ya mubahala ni baraka za mali Alizofungua Mwenyezi Mungu kwa huyu darweshi

akaaye nyumbani. Kuanzia siku ya mubahala mpaka leo rupia elfu kumi na tano zimeshanifikia kutoka kwa ghaibu zilizotumika katika matumizi ya kidini ya Jumuiya hii.

La nane ni kuandika kitabu 'Sat Bachan'. Kwa kuandika kitabu hiki Mwenyezi Mungu alinijaalia vifaa ambavyo tangu miaka mia tatu mtu yeyote hakuviwaza.

La tisa ni kuwa katika muda huu, watu karibu elfu nane walifanya baiati kwa mkono wangu. Basi, najua kwa yakini kwamba nilipofanywa kuwa njia ya watu wengi hivyo kutubu ni dalili ya kukubaliwa inayopatikana baada ya ridhaa ya Mungu.

La kumi ni Mkutano wa Dini zote wa Lahore. Sina haja ya kuandika zaidi kuhusu mkutano huo. Namna na jinsi ilivyopokelewa nuru kwa kusomwa kwa makala yangu na jinsi watu walivyoniheshimu mimi na makala yangu, haina haja nitoe maelezo yake. Watu wote wakatamka mara moja kwamba kama isingekuwa makala hii, basi leo Islam ingefedheheka kwa sababu ya Muhammad Husain na wengineo.

MASHEIKH WA AMRITSAR KATIKA CHUMBA CHA CHINI CHA MASJID MUHAMMAD JAN

Baada ya mubahala uliotajwa juu, Hudhur[as] alichapisha tangazo moja kuwaambia masheikh ya kwamba:

> "Sasa tumeshamaliza mjadala na Wakristo, na kuanzia leo nitakaa hapa kwa siku tatu. Sheikh yeyote anayetaka kujadiliana nami, ajadiliane nami akipanga sehemu yoyote, isije yakapigwa makelele baadaye kwamba ameshakimbia. Kwa tangazo hilo la Hudhur[as], masheikh wakashikwa na hofu kiasi hiki kwamba yeyote hakujitokeza. Hapo Khwaja Muhammad Yusuf, Chifu wa Amritsar aliwaambia masheikh kwamba "Sasa kwa nini hamjadili ilihali Bwana Mirza ameshakubali kujadili. Ataka-poenda ndipo mtapiga makelele kwamba Bwana Mirza ameshakimbia na hakujadiliana na masheikh wa Amritsar. Masheikh wakajibu kwamba

tutajadiliana, tushauriane kidogo.”[250]

Maulawii Muhammad Husain Batalawii alikuwa amewatisha sana masheikh kwamba kati yenu sheikh yeyote hataweza kujadiliana na Bwana Mirza; yeye atawabaneni katika muda mfupi na atawanyamazisheni katika swali moja mawili tu. Afadhali mhepe mjadala kwa udhuru wowote. Baadaye masheikh wote wa Amritsar, Sheikh Abdul Jabbar Ghazanwii na Ma-Ghaznawii, Sheikh Rusul Baba, Sheikh Ghulamullah Kasuri na wengine waliojulikana na wasiojulikana walijificha ndani ya chumba kimoja chini ya Masjid Jan Muhammad, na wakamwambia mwadhini kutia mlango kufuli na awe na ufunguo. Sheikh Rusul Baba akasema kwamba yeyote akikuuliza juu yetu, basi sema tu kwamba wameenda kwenye karamu ya chakula mahala fulani nao watachelewa kurudi. Khwaja Yusuf Shah akafika msikitini humo akiwatafuta masheikh. Akamwuliza mwadhini kwamba masheikh wako wapi? Akajibu kwamba wameenda kwenye karamu ya chakula. Kisha Bwana Khwaja huyo akafika nyumbani kwa Sheikh Abdul Jabbar, hapo pia alipata jibu lile lile kwamba wameenda kwenye karamu ya chakula. Bwana Khwaja alisema kwa sauti kubwa masheikh wote wameenda kwenye karamu ya chakula, hapa hayupo yeyote, na leo ilikuwa ni siku ya mjadala. Bwana Mirza ataenda, kisha masheikh watapiga makelele. Kwa vyovyote mjadala huu utakuwa lini? Hapo tena Bwana Khwaja akatoka kuwatafuta masheikh na akataka kujua kwamba wamealikwa na nani, na akaja tena kwenye Masjid Muhammad Jan. Hapo mara aliambiwa na mtu fulani kwamba masheikh wote wapo katika chumba fulani chini ya msikiti na nje imetiwa kufuli ili yeyote asijue. Bwana Khwaja akamwuliza tena mwadhini kwamba masheikh wapo wapi? Mwadhini akajibu tena kwamba wameenda kwenye karamu. Bwana Khwaja akauliza wapi na kwa nani? Akihofia akajibu sijui. Hapo Bwana Khwaja akauliza kwamba ufunguo uko wapi wa chumba kilichopo chini ya msikiti? Alisema ninao. Akasema, lete; akampa. Bwana Khwaja akafungua chumba, alipoenda ndani akawakuta masheikh wote humo. Masheikh wakageuka rangi na wakaanza kutetemeka.

[250] Kijitabu *Nur Ahmad,* uk. 33

Bwana Khwaja akasema kwamba leo ni siku ya mjadala na nyinyi mmejificha. Bwana Mirza ataondoka kesho, basi mjadala utakuwa na nani. Masheikh wakaaibika, wakasema bado tunashauriana, baada ya muda kidogo utaarifiwa, wewe tulia tu. Bwana Khwaja akaenda baada ya kusisitiza… lakini alipata yakini kwamba masheikh hawawezi kujadili.

MWENENDO WA MASHEIKH

"Lakini Hudhur[as] alipokuwa tayari kurudi Qadian, masheikh kabla ya yeye kufika stesheni walianza kugawa nyuma ya gari lake kipeperushi walichokuwa wamechapisha mapema, na kupiga makelele, na wakakibandika kwenye kuta pia, ambamo wakaandika "Mirza kakimbia", na kwa mdomo pia wakapiga makelele. Baada ya siku chache tena masheikh walijumuika na wakashauriana. Kwa bahati tu mimi pia nikafika huko. Ilijulikana kwamba kila mmoja anamchagua sheikh fulani kwa rai yake. Mmoja alimtaja Maulawii Muhammad Husain Batalawii kwa kujadiliana na Hudhur[as] na mwingine alimtaja Sheikh Abdul Jabbar Ghaznawii, mwingine alimtaka Sheikh Rusul Baba Amritsari. Hatimaye Sheikh Ghulamullah[251] Kusuri akasema haipaswi kukataa mjadala; naam, andikeni kwamba mjadala unapaswa kufanywa katika Kabul au Makkah au Madina. Yeye hataenda huko wala mjadala hautafanyika."[252]

HALI YA BWANA ATHAM

Sasa twarejea tena kwenye habari za Bwana Atham na kusema kwamba Hadhrat Sheikh Nur Ahmad[ra] amesimulia:

> "Baada ya Hudhur[as] kurudi Qadian, nilikuwa nikienda mahakamani. Nyumba ya Bwana Atham ilikuwa njiani. Niliona kwamba Bwana Atham amesimama juani chini ya mwavuli akiongoza kusafisha bustani ya nyumba yake. Nikamwuliza, Bwana Deputy! unafanya nini saa hizi? Kasema nafyekesha

[251] Pengine muradi wake ni Ghulam Ali, kwa kosa limeandikwa Ghulamullah, au pengine Bwana Sheikh baadaye akaanza kujiita Ghulamullah. Mungu ndiye Ajuaye zaidi.

[252] *Nur Ahmad,* uk. 33 hadi 35.

nyasi na kichaka, isije nyoka akajitokeza na kuniuma, na mkasema kwamba utabiri wa Bwana Mirza umetimia. Nikasema, ujihadhari sana, Mwenyezi Mungu lazima ataonyesha onyesho la kudra yake. Baadaye Bwana Atham alianza kuona ndoto za kuonya na kutisha. Usiku alikuwa akishtuka, na wakati mwingine kuanguka chini ya kitanda na kupiga makelele, 'Hae nafa, nimekamatwa'. Kuona hali hii ya Bwana Atham, mpishi aliyekuwa Mwislamu alifutwa kazi, na Waislamu wakazuiliwa wasije ndani. Baada ya muda fulani wa kufutwa kazi, mpishi yule nilimkuta, naye akanielezea hali yote ya Atham, na akasema kwamba nimeondolewa kazi. Atham aliposema 'Nimekamatwa', 'nimepigwa', nilikuwa nimesimama karibu yake. Niliondolewa kazi ili kama idhihirike hali yoyote, basi siri isifichuliwe. Baada ya kusikiliza hali hiyo kwa mpishi, mimi pia nilikwenda nyumbani kwa Bwana Atham. Nikaona kwamba mlinzi mmoja amesimama aliyekuwa ameagizwa vikali kwamba Mwislamu yeyote asije hapa, na aambiwe kwamba Mwislamu yeyote hana ruhusa ya kumwona Bwana Atham. Kuona hali hii nikarudi na yakasadikika maneno ya mpishi. Waislamu wasiokuwa Waahmadiyya pia wakienda kuonana naye au kwa kazi yoyote hawakupewa nafasi ya kumwona. Bwana Atham alikuwa akishughulishwa katika michezo na kadhalika, alibembelezwa kwa shatranji, lakini hofu ya Bwana Atham siku hadi siku iliendelea kuzidi na hali yake siku hadi siku iliendelea kugeuka. Hakuwa na utulivu na raha wakati wowote. Wakati fulani akasema "hae, hae", na wakati mwingine akasema, 'Nimekamatwa na sitasalimika". Upande mmoja hali ya Bwana Atham ilikuwa hivyo, na upande wa pili mapadre walikuwa na wasiwasi sana moyoni. Mmoja alifariki na mwingine kwa hofu akaacha Amritsar na katika hali ya safari akafariki ndani ya garimoshi. Huzuni juu ya kifo cha padre Wright iliyodhihirishwa kanisani inayodhihirisha hali yao ya kufadhaika na kutishika, yaweza kufahamika vizuri kwa maneno yafuatayo yaliyotoka midomoni mwa baadhi ya mapadre, ambayo ni haya: "Leo usiku fimbo ya ghadhabu ya Mungu ilitupiga bila kutarajia,

na upanga uliofichika ulituua ghafla.”[253] Bwana Padre Wright alikuwa mhubiri wa kujitolea mjini Amritsar, alikubali yote lakini hakukubali haki.

Wakristo walipoona kwamba hali ya Bwana Atham inaendelea kuharibika, walitaka, kwa kushauriana, kwamba apelekwe pahali pengine. Basi alipelekwa Ludhiana. Asipopata utulivu hapo pia, akapelekwa Gujrat, hapo pia hakupata raha na utulivu basi wakaenda naye Ferozpur.

Jumba zuri la Bwana Atham lililokuwa mfano wa pepo sawa na fikara yake alilojengesha kwa shauku sana, ambalo kwa sababu yake hakubahatika kukubali haki, na bustani ndogo aliyotayarisha sawa na matakwa yake, vyote viwili vikaachika. Na akaendelea kuvumilia taabu za safari za huko na huko, na baridi na joto, na hakuweza kupata utulivu popote. Na kalamu ya Atham iliyokuwa ikiandika daima dhidi ya Islam ikakoma mara moja.”[254]

Na jazba ya kuandika kusaidia Ukristo pia ikapoa.

Maelezo yake ni kwamba muda wa Atham uliopangwa ulipoisha, na kwa sababu ya kurejea kwenye haki hakufa katika miezi kumi na mitano, hapo Wakristo walianza kupiga makelele kwamba utabiri umebatilika. Hudhur[as] aliwafahamisha kwamba ilikuwa ndani ya utabiri kwamba Atham akirejea, atasalimika kutupwa katika ***hawiya***, na kama hatarejea, basi ataangushwa ndani ya ***hawiya***. Kwa vile hofu na kurejea kwake imethibitika, yeye katika muda huo wote hakutamka hata neno moja dhidi ya Islam, kwa hiyo Mwenyezi Mungu aliye Ghafuri na Rahimu, Akaahirisha kifo chake, lakini Wakristo hawakuwa wenye kukubali, basi hawakukubali. Kwa kweli kwa mwenendo wao walikuwa wakimwita malaika wa kifo. Kung'ang'ania kwao kulipozidi sana, ghera ya Kiislamu ya Hudhur[as] pia ilichemka na alitangaza kupitia kipeperushi kwamba kama Atham akiapa kwamba hakushikwa na hofu ya utabiri wala hakubadilisha mawazo yake moyoni mwake juu ya Islam na Mwanzilishi Mtukufu[saw]

[253] Maelezo ya pembeni, ***Anwarul Islam,*** uk. 10

[254] Kijitabu ***Nur Ahmad,*** uk.35-37

wa Islam, basi kama hafi katika mwaka mmoja, nitampa zawadi ya rupia elfu moja, lakini Bwana Atham akanyamaa.

Hapo Hudhur[as] alichapisha tangazo la pili na akaahidi kumpa Bwana Atham rupia elfu mbili kama yeye akila kiapo hicho. Hata hivyo, Bwana Atham akanyamaza tu, lakini kwa sauti ndogo alikiri kiasi hiki: "Sikubaliani na itikadi ya Wakristo ya Uana na Uungu wa Yesu wala sikubaliani na Wakristo waliokosana naye (yaani Hudhur[as]).[255]

Kisha Hudhur[as] alichapisha tangazo la tatu na akaahidi kumpa Atham rupia elfu tatu, kama akiapa. Lakini kwa vile hakuwa na nia, kwa hiyo hakujibu. Hatimaye kwa kutimiza hoja akamwita Abdullah Atham kwa kuapa kwa ahadi ya kupewa zawadi ya rupia elfu nne, lakini hata hivyo hakuitika. Katika tangazo hilo Hudhur[as] aliandika:

> "Sasa kama Bwana Atham akiapa (kwamba hakuogopa na Utabiri wala hakurejea kwa jiha yoyote) basi ahadi ya mwaka mmoja ni ya yakini, na kama asiape, basi hata hivyo Mwenyezi Mungu hatamwacha mkosefu kama huyo bila kuadhibu, aliyetaka kudanganya dunia kwa kuficha haki... Na siku zile zi karibu sio mbali. Hata kama Wakristo wamkate Atham vipande vipande na wamchinje, hata hivyo yeye hataapa."[256]

Basi, Atham hakuonyesha nia ya kuapa kwa vyovyote, na akafa kuko Ferozpur ndani ya miezi sita, tarehe 27 Julai 1896, baada ya tangazo hilo la mwisho.[257]

Baada ya kifo cha Atham, Hudhur[as] aliandika kuwaambia wapinzani wote:

> "Kama mtu yeyote anafikiri kwamba Atham hakuogopa adhama ya utabiri, bali kwa kumwua yeye, sisi tuliwatuma watu wenye panga, na wakati fulani tulimtupia nyoka, na wakati mwingine tulimpelekea mbwa waliofundishwa na kadhalika,

[255] Gazeti "*Nur Afshan*", 21 Septemba, 1894.

[256] Tangazo la zawadi ya rupia elfu nne, uk. 11

[257] Kwa maelezo zaidi someni "Anwarul Islam", "Anjame Atham" na "Kitabul Bariyya"

basi mtu kama huyo aape kuhusu hayo mambo, kisha kama akisalimika mpaka mwaka mmoja, basi nitakiri mwenyewe kuwa utabiri wangu umebatilika, na halitakuwa sharti lolote pamoja na kiapo hiki."[258]

Lakini mtu yeyote shujaa hakuja uwanjani si miongoni mwa Wakristo wala miongoni mwa maadui wala masheikh wakufurishaji. Na kwa njia hii alikamilisha hoja juu ya maadui wote.

KAFUNDISHWA MANENO ASILIA ELFU AROBAINI YA LUGHA YA KIARABU KATIKA USIKU MMOJA

Baada ya kumaliza mjadala na mubahala, Hudhur[as] aliporudi Qadian, alishughulikia kama kawaida tena kuandika vitabu na kueneza dini. Changamoto ya kuandika maelezo ya Kurani katika lugha ya Kiarabu na kueleza kweli na maarifa alishawapa tayari Maulawii Muhammad Husain Batalawii na masheikh wengine kama ilivyo dhahiri katika tangazo la "Uamuzi wa Kimbingu". Na hii pia tumeshaandika kwamba Maulawii Muhammad Husain aliposoma tangazo hilo, basi Mungu Apishe mbali, alimwita Hudhur[as] kuwa jahili na asiyejua elimu ya Kiarabu, na alijiita kuwa mwanachuoni asiye na mfano. Ghera ya Mwenyezi Mungu ingewezaje kuvumilia jambo hilo. Yeye Akatilia moyoni mwa Masihi Mtakatifu jazba ya kuomba dua. Hudhur[as] alipoomba dua, Mwenyezi Mungu Alimfundisha maneno asilia elfu arobaini ya lugha ya Kiarabu katika usiku mmoja. Ndipo kwa kukamilisha hoja juu ya Waarabu na Waajemi na kuvunja kiburi cha Maulawii Muhammad Husain Batalawii na masheikh wenye itikadi zake alichapisha vitabu kadhaa kwa lugha ya Kiarabu pamoja na zawadi za rupia maelfu, lakini mtu yeyote hakujasiri kuja kushindana naye kama alivyosema Hudhur[as], (ubeti):

Hakuja mtu yeyote kujaribu
Tulimwita kila mpinzani aje kunikabili.

[258] Anjame Atham uk. 15

KUHAMA KWA HADHRAT ALHAJI MAULANA HAKIM NURUDDIN[RA]

Tukio maalum la mwaka 1893 ni la kuhama kwa Hadhrat Alhaji Maulana Hakim Nuruddin[ra]. Yeye alikuwa tabibu wa kifalme wa Maharaja wa Jammu na Kashmir. Hudhur[as] alipodai kuwa Masihi na Mahdi, Bwana Maulawii[ra] alimwandikia Hudhur[as], "Moyo wangu unatamani sana, Hudhur, kwamba niishi maisha yaliyobaki kukuhudumia. Ukiniruhusu, nije kukaa Qadian nikijiuzulu kazini. Hudhur[as] alimjibu kwamba kuacha kazi ni kutoshukuru neema, usijiuzulu. Baada ya muda fulani, Mwenyezi Mungu Alizalisha sababu hata kwamba Bwana Maulawii alilazimika kuacha kazi na akarudi makwao Bhera, na hapo akaanza kujenga nyumba yake mpya. Nyumba ile bado ilikuwa inajengwa na karibu rupia elfu saba zilikwishatumiwa tayari, Bwana Maulawii[ra] akaja Lahore kwa shughuli fulani . Hapo alifikiri kwamba Qadian ipo karibu, afadhali kwenda kumwona Hudhur[as]. Yeye mwenyewe anasema:

> "Nilipenda nimwone Hudhur[as] pia, kwa hiyo nikaja Qadian. Kwa vile kazi kubwa ya ujenzi iliendelea huko Bhera, kwa hiyo nilikodisha gari la farasi kuja na kurudi. Baada ya kufika hapa nilimwona Hudhur[as], na nilinuia nimwombe ruhusa sasa hivi kurudi. Katika mazungumzo akasema, sasa huna kazi, nilijibu, naam, sasa sina kazi. Nilimwambia mwenye gari la farasi kwamba yeye aende sasa. Si sawa kuomba ruhusa leo, kesho au kesho kutwa nitaomba ruhusa. Kesho yake alisema kwamba utasumbuka kuishi peke yako, umwite hapa mkeo mmoja. Sawa na agizo, nikaandika barua kumwita mke na niliandika hii pia kwamba labda sitaweza kurudi haraka kwa hiyo simamisheni kazi ya ujenzi. Mke wangu alipofika, Hudhur[as] akasema kwamba una shauku kubwa ya vitabu, basi yafaa uagize hapa maktaba yako pia. Baada ya siku chache akasema kwamba mke wako mwingine anajua mazoea yako na ni wa kwanza pia, lazima umwagize aje hapa. Na alimwambia Maulawii Abdul Karim kwamba nimefunuliwa kuhusu Nuruddin, na ubeti huo upo katika Hariri:

لَا تَصْبُوَنَّ اِلَی الْوَطَنِ فِیْہِ تُھَانُ وَتُمْتَحَنْ[259]

Kazi za Mwenyezi Mungu ni za ajabu, hapo tena sikuwaza hata katika ndoto habari za kwetu.’’[260]

Yeye alikuwa mwenye daraja kubwa sana baina ya masahaba wa Hadhrat Masihi Mau‘udi[as]. Jinsi alivyomsaidia Hudhur[as] katika shughuli za Jumuiya, mfano wake haupatikani katika mtu mwingine yeyote awaye. Kutoa darasa la Kurani ilikuwa ni shughuli yake aliyopenda sana. Alikuwa akipenda sana Hadithi za Mtume wa Mungu s.a.w. Alikuwa bingwa sana katika utabibu. Ilmuradi, alikuwa akishughulikia sana viumbe vya Mungu kwa kiroho na kimwili. Hudhur[as] amemsifu sana katika vitabu vyake. Kwa kumsifu ubeti huu wa Hudhur[as] una maneno machache, lakini kuna maana nyingi ndani yake:

چہ خوش بُودے اگر ہر یک زِامت نوردیں بُودے ہمیں بودے اگر ہر دل پُراز نورِ یقین بُودے[261]

VITABU VILIVYOANDIKWA MWAKA 1893

1. ***Aina Kamalate Islam:*** Masomo ya kitabu hiki yametajwa ya kutosha juu.

2. ***Barakaatud Dua:*** (Baraka za Dua) Hudhur[as] aliandika kijitabu hiki kumwambia marehemu Sir Seyyid kuhusu kupokelewa dua. Hicho pia kimetajwa juu.

3. ***Hujjatul Islam:*** (Hoja ya Islam) Katika kijitabu hiki, Hudhur[as] alimwita Dkt. Henry Martin Clark na Wakristo wengine kwamba katika zama hizi dini iliyo hai ni Islam pekee. Sababu na masharti pia yametajwa humo ya mjadala uliofanywa kati ya Hudhur[as] na Wakristo huko Amritsar, unaotambulika kwa jina la Vita Takatifu.

4. ***Sach-chai ka Idh-haar:*** (Dhihirisho la Ukweli) Mjadala uliopangwa

[259] Tafsiri: “Usielekee kamwe makwenu, waila utafedheheka na utaudhika.”

[260] Hayate Nuruddin.

[261] Ingekuwa vizuri ilioje kama kila mmoja wa umati angekuwa Nurudin, na hiyo itakuwa kama kila moyo utajaa mwanga wa yakini.

kufanyika baina ya Hudhur[as] na Wakristo. Mapadre walijuta sana baada ya kuukubali na wakajaribu sana kwamba mjadala ufanyike na masheikh badala ya Hudhur[as]. Kwa hiyo, walitangaza sana fatuwa ya kumkufurisha iliyotayarishwa na Maulawii Muhammad Husain Batalawii, na waliwachochea Waislamu wa Jandiala ambao kwa sababu yao mjadala ulipangwa kwamba mnaomchagua kuwa mjumbe wenu, yaani Hudhur[as], yeye ndiye kafiri sawa na Waislamu wote. Kwa nini hamchagui mwanachuoni mwingine kwa kazi hii, lakini wao wakasema waziwazi kwamba mjumbe wetu atakuwa Hadhrat Mirza tu. Hudhur[as] ametia mwanga juu ya hali hizo katika kijitabu hiki.

5. ***Jange Mukaddas:*** Katika kitabu hiki hali ya mjadala wa Amritsar na maandishi ya pande zote mbili yameandikwa.

6. ***Tuhfa Baghdad:*** Hudhur[as] aliandika kitabu hiki katika lugha ya Kiarabu kwa kujibu kipeperushi na barua ya mtu mmoja Seyyid Abdur Razzak Qadirii Baghdadi. Katika Kitabu hiki, Hudhur[as] ametia mwanga juu ya madai yake kwa urefu sana.

7. ***Karaamaatus Sadikin:*** Katika kitabu hiki Hudhur[as] ameandika kasida nne kwa Kiarabu kwa kumsifu Mtume Mtukufu[saw] na ametoa maelezo ya Suratul Fatihah. Amemwita Maulawii Muhammad Husain Batalawii na masheikh wengine kumkabili yeye katika kuandika maelezo ya Kurani Tukufu na kasida katika Kiarabu.

8. ***Shahadatul Kuran:*** (Ushahidi wa Kurani) Katika kitabu hiki, Hudhur[as] ameeleza hoja za madai yake kuwa Masihi Mau'udi sawa na Kurani Tukufu na Hadithi Sahihi.

KUAHIRISHWA KWA MKUTANO WA MWAKA 1893

Mkutano wa Mwaka 1893, Hudhur[as] aliahirisha kwa sababu mbili.[262]

Ya kwanza ni hii kwamba katika Mkutano wa Mwaka uliopita, kwa sababu ya upungufu wa nafasi, baadhi ya wageni hawakuonyesha mfano mzuri wa kupendana, udugu na ucha Mungu. Jambo hili lilimhuzunisha Hudhur[as].

[262] Someni tangazo lililomo katika *Shahadatul Kuran.*

Ya pili ni hii kwamba bado nafasi ni ndogo sana, na matumizi pia yalifanyika sana kwa sababu ya kuchapisha vitabu vingi vya muhimu.

UJAJI WA MAULANA HASAN ALI KATIKA QADIAN PAMOJA NA HADHRAT SETH ABDUR RAHMAN HAJI ALLAH RAKHA MADRASI

Maulawii Hasan Ali alikuwa mkazi wa Bhagalpur, mkoa wa Bihar, na alikuwa Mwalimu Mkuu wa Patna Sekondari School. Alikuwa mtu mpenda Islam na mwenye ibada, mcha Mungu na mwandishi wa vitabu.[263] Alikuwa mtu mashuhuri sana katika zama zake, mzungumzaji mzuri na hatibu mwenye ufasaha sana. Kwa sifa zake hizo watu walianza kumfikiria kuwa Mujadidi na walikuwa wakimwambia pia kwamba u mjadidi wa karne hii, lakini yeye alikuwa anakataa. Alikuwa akipenda Islam, na shauku na jazba ya mahubiri ilikuwa kiasi hiki kwamba akaacha kazi na akajitolea kwa mahubiri, na akaanza kutoa hotuba za mahubiri katika miji mbali mbali ya India. Mara ya kwanza yeye alipata kusikia jina la Hudhur[as] mjini Amritsar katika mwaka 1887, akatamani kumwona na akaelekea Qadian. Yeye ameeleza maono yake katika kijitabu "Taiide Haq". Anaandika:

> "Nilishangaa kuona ukarimu wa Bwana Mirza. Naandika jambo moja dogo ambalo wasomaji wanaweza kukisia kwalo ukarimu wake. Nilikuwa na tabia mbaya ya kutafuna tambuu. Katika Amritsar nilipata tambuu, lakini katika Batala sikukuta tambuu popote. Katika shida hiyo nikila iliki na kadhalika, nikasubiri. Rafiki yangu wa Amritsar alifanya ajabu, sijui wakati gani alimwelezea Bwana Mirza kuhusu tabia yangu hiyo mbaya. Bwana Mirza alituma mtu aende Gurdaspur kwa kuleta tambuu. Keshoye saa tano nilipoisha kula chakula, nikakuta tambuu ipo. Kutoka maili 32 tambuu ziliagizwa kwa ajili yangu."[264]
>
> Maulana Hasan Ali[ra] baada ya kurudi kutoka Qadian tena alishughulikia kazi yake aliyoipenda ya kueneza Islam, mpaka

[263] Kitabu chake kimoja muhimu ni "*Mi'rajul Muminin*"

[264] Kijitabu *Taiide Haq,* uk. 54

katika mkutano wa mwaka 1893 wa Anjuman Himayate Islam alipata nafasi ya kusikiliza hotuba ya Hadhrat Maulana Hakim Nuruddn[ra] iliyojaa maarifa na mambo ya kweli. Hotuba ile ilimwathiri kiasi hiki kwamba baada ya hotuba akasimama na kusema: "Nina fahari kwamba nimemwona kwa macho yangu mwanachuoni na mfasiri mkubwa sana mno.[265]

Kasema:

"Nilikuwa na hamu ya kuonana na Maulawii Hakim Nuruddin, lakini Bwana Maulawii mwenyewe kwa ukarimu wake akaja kuniona. Nilimwuliza faraghani kwamba umefanya baiati ya Bwana Mirza, uliona faida gani ndani yake? Akajibu, "kulikuwa na dhambi fulani ambayo nilikuwa sikuweza kuiacha. Baada ya kufanya baiati ya Bwana Mirza, sio tu dhambi ile ikaachika, bali naichukia sasa." Jibu hili la Maulawii Hakim Nuruddin liliniathiri sana. Bwana Hakim aliendelea kusisitiza kuenda Qadian lakini sikuenda."[266]

Kisha anasema:

"Nilikuwa nikienda kushiriki katika mkutano wa mwaka wa Anjuman Himayate Islam Madras, sawa na mwaliko wa Anjuman, nikakutana na Bwana Abdur Rahman Haji Allah Rakha mjini Bombay.[267] Nikajua kwamba mkutano wa Anjuman umeahirishwa kwa mwezi mmoja. Bwana Seth alinitaka niitembelee naye miji mashuhuri ya India na niende Qadian pia pamoja naye. Bwana Abdur Rahman Seth alikuwa na nia ya kufanya baiati ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad. Kwanza nilitaka kuepa taabu ya safari hiyo kwa kutoa udhuru, lakini Bwana Seth alinibana vizuri. Bwana Seth alikuwa na

[265] Kijitabu *Taiide Haq,* uk. 64

[266] Kijitabu *Taiide Haq,* uk. 65

[267] Hadhrat Seth Abdur Rahman Madrasi alikuwa mtu mwema sana, alikuwa mpenzi wa Jumuiya na alikuwa na jazba sana kutumikia Islam. Kwa ucha Mungu na ikhlasi yake, Hudhur[as] alimteua kuwa mdhamini wa Sadr Anjuman Ahmadiyya.

dhana nzuri juu yangu. Akaniambia twende ukaone kwamba Bwana Mirza yu mkweli au mwongo. Nikasema, Alhamdulillahi, ni fadhili ya Mwenyezi Mungu juu yangu kiasi hiki kwamba kwa kuona tu uso najua hali ya undani wa mtu. Kumhusu mwanadamu chochote chawezekana; mwema anakuwa mbaya, na mbaya mwema. Kama Bwana Mirza hakubaki yule niliyemwona mwaka 1887 na kama ameingiwa na mambo ya kidunia na ujanja, basi kwa kuona uso tu nitasema. Bwana Seth alisema kwamba kwa sababu hiyo ningependa kukuchukua pamoja nami. Ilmuradi, nilienda Qadian Takatifu pamoja na Abdur Rahman Seth. Njiani niliona tamasha la mkutano wa Aligarh, nilifika Qadian kupitia Amritsar. Naam, katika Amritsar niliota kwamba kuna kitanda maalum cha Bwana Mirza, Hudhur[as] akaniambia nijilaze juu ya kile kitanda. Nikasema nikoseje adabu kwa kulala kitandani mwa Hudhur[as]. Hudhur[as] akitabasamu akasema haidhuri, kwa nini umejikalifisha. Ilmuradi, tarehe 2 Januari 1894 nilifika Qadian. Bwana Mirza Ghulam Ahmad Chifu wa Qadian akaonana nasi kama kawaida, akatupangia makazi mimi na Bwana Seth, akaongea nasi kwa mapenzi na ikhlasi. Katika kulakiana naye huku mara ya kwanza na kwa kumwona tu Hudhur[as] ana kwa ana, rafiki yangu mpendwa Bwana Abdur Rahman Seth akaingiwa na penzi kubwa sana moyoni mwake kwa Imamu wa zama. Bwana seth akaniuliza sema, unamkutaje Bwana Mirza? Ningejibuje, nilikuwa nimeshangaa sana. Yule Bwana Mirza niliyemwona mwaka 1887, huyu hakuwa huyo. Sauti na sura ilikuwa ile ile lakini mambo yote yalikuwa yamebadilika. Allah, Allah! Tangu rasi hadi miguu alionekana ni nuru tupu. Watu wenye ikhlasi, na wanaolia mbele ya Mugu sehemu ya mwisho ya usiku, Mungu Ananurisha nyuso zao pia kwa nuru yake. Na wenye busara hata kiasi kidogo wanaona nuru hiyo. Lakini Mungu kwa mkono wake Mwenyewe Alikuwa Amemvisha mavazi ya mapenzi yake kuanzia rasi hadi miguu. Nilikaa Qadian Takatifu kwa siku 13, kila siku mara mbili niliendelea kumwona Imamu wa zama na mpendwa wa Mungu. Zama hizo

zilikuwa zama nzuri sana za umri wangu. Hapo nilipata nafasi nzuri ya kusoma vitabu vya Hudhur[as] visivyo na mfano. Aina Kamalate Islam, Fat-he Islam, Taudhihe Maraam, Izala Auhaam, Shahadatul Kuran, Barakaatud Dua na vinginevyo nilivisoma kiasi kidogo kidogo. Bwana Abdur Rahman Seth, kwa hisani yake, alininunulia nakala moja moja ya vitabu vya Hudhur[as].

"Sasa swali kubwa likazuka kwamba je, mimi nimfuate Imamu mtukufu na nikufurishwe na kulaumiwa pasipo haki, nitoe dhabihu ya heshima niliyopata katika India nzima nikiwa hatibu mzuri na badala yake niwe mwenye kukataliwa na kulaaniwa, au nishike sera ya Mashia nimwunge mkono nikiwa na Bwana Mirza, na nimpinge — Mungu Apishe mbali — nikiwa kwa wapinzani wake na nipate kusifiwa na watu. Katika hali ya kuchanganyikiwa nilipitisha siku kadha katika Qadian. Kila siku nikilia mbele ya Mwenyezi Mungu nikaomba, Ee Mungu, kama ridhaa yako iko katika kumfuata na kumtii Bwana Mirza basi nifunulie katika ndoto hali halisi kama ulivyofanya mara kadha. Lakini kwa upande wake nikaona kimya. Mungu alitaka kuwa mimi mwenyewe kwa kutumia akili niliyojaaliwa na Mungu nitende jambo kwa kuangalia faida na hasara yake. Safari hii jambo lilikuwa zito kuliko lile la kuacha ualimu mkuu wa shule ya Patna. Safari hii ilipatikana nafasi ya kutoa dhabihu kubwa. Nilikuwa nikichukua hatua moja mbele, mara nikarudi hatua moja nyuma. Shetani akasema, bwana, ukitaka kuepa maangamio na dhila, ondoka Qadian taratibu. Malaika akasema, Ee mwenye bahati ndogo, je, hujasoma Hadithi kwamba asiyemtambua imamu wa zama atakufa kifo cha ujahili. Katika hali ambapo akili uliyojaaliwa na Mungu inakuambia kwamba Bwana Mirza ndiye Imamu wa zama utakwenda wapi kwa kumkimbia. Je kwa ajili ya kazi ya siku chache za maisha ya kidunia na kwa heshima batili utaangamiza manufaa yako ya milele! Ee mwenye fikara finyu, maradhi ya kiroho uliyoshikwa nayo, Mungu Ameshakufikisha kwenye dawa yake. Mwanachuoni mnyofu kama Maulawii Hakim Nurud Din

anakuambia faida ya dawa hiyo akieleza tajriba yake binafsi. Kisha umepatwa na bahati gani mbaya kwamba wataka kuendelea kuzama katika uchafu wa undani na maisha ya unafiki, ukiwa adui wa afya yako ya kiroho! Enyi mabwana, nilimwitikia malaika, na tarehe 11 Januari 1894 usiku wa Ijumaa nilifanya baiati ya Hadhrat Imamu wa zama, mujadidi wa zama, Mirza Ghulam Ahmad, Chifu wa Qadian na kumkubali kuwa Imamu wangu. *Alhamdulillahi* kwa hiyo.

"Baada ya kufanya baiati, nilipata nafasi ya kukaa katika Qadian kwa siku tatu. Katika siku hizi tatu za mwisho nilipokuwa nasali pamoja na jamaa, nikatambua kwamba sasa nasali, yaani nilipata utamu na ladha ya ajabu katika sala. Tarehe 13 Januari baada ya kuomba ruhusa kutoka kwa Imamu wangu nikaja Lahore na nikatoa hotuba katika Kiingereza ambamo nilieleza manufaa ya kiroho niliyopata kutoka kwa Hudhur[as]. Baada ya kumaliza safari ya Panjab nilipofika Madras, nikakabili mambo ambayo wapenzi wa ukweli wanakabili katika kila zama na katika kila nchi. Nikazuiliwa kutoa mawaidha msikitini. Ilitangazwa katika kila msikiti kwamba Hasan Ali siye Msuni, mtu yeyote asisikie mawaidha yake. Polisi iliambiwa kwamba mimi ni mchafuzi wa amani. Mtu ambaye siku chache kabla alikuwa akiitwa ***Shamsul Wa'idhina,*** mheshimiwa Maulana Maulawii Hasan Ali, Hatibu wa Islam, akaanza kuitwa kwa jina la Hatibu Hasan Ali tu. Hapo kabla nilihesabiwa walii kati ya mahatibu, lakini sasa kulikuwa hamna shetani mkubwa mwingine kuliko mimi. Popote niendapo nililaumiwa; nikisalimu sikujibiwa. Watu wanaogopa kuonana nami, nimeshakuwa mnyama hatari."[268]

Mheshimiwa Sheikh Hasan Ali alikuwa mcheshi mchangamfu. Itafaa kunukuu maandishi yake kutoka kitabu chake kwa kutuliza wasomaji. Anasema:

"Baada ya kufanya baiati ya Bwana Mirza, nilipotaka kutoa mawaidha juu ya kumsalia Mtume[saw] katika msikiti Wala Jahi wa

[268] *Taide Hak,* uk. 71-75

Madras, nilikatazwa. Nilipotoka humo, Mwislamu mmoja "mwenye imani" alianza kunitukana kusema, "Yu kafiri, yu kafiri; ni dajali huyu, ni dajali." Nikafikiri moyoni kwamba huyu mtu pia anaunga mkono madai yetu kwani miye sio mwenye chongo wala sikuwa nimepanda punda mwenye urefu wa yadi 70, simfishi aliye hai wala simhuishi mfu. Basi mtu yule kwa nini kaniita kuwa dajali. Kwa sababu hii Akadhani kwamba nimepotea kwani nimemfuata Bwana Mirza mtukufu, na nataka kueneza upotevu. Sasa, kama huyo alifikiri kuwa inajuzu kumwita dajali yule mtu ambaye anatoa shahada mbili, anasali kuelekea Kaaba, aliyetaka kueleza fadhila za kumsalia Mtume mara baada ya sala ya Ijumaa, basi kama sisi tukiiita kaumu inayomwabudu Isa, ambayo haina mfano katika kupoteza watu, kuwa dajali, je tumefanya isiyokuwa sawa?"[269]

ISHARA YA JUA NA MWEZI KUPATWA, APRILI 1894

Miongoni mwa ishara za ujaji wa Hadhrat Imam Mahdi, ishara moja ilikuwa hii pia kwamba katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, mwezi na jua vitapatwa. Na Hadithi ile ni hii:

اِنَّ لِمَهْدِيِّنَا اٰيَتَيْنِ لَمْ تَكُوْنَا مُنْذُ خَلْقِ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ يَنْكَسِفُ الْقَمَرُ لِاَوَّلِ لَيْلَةٍ مِّنْ رَّمَضَانَ وَتَنْكَسِفُ الشَّمْسُ فِي النِّصْفِ مِنْهُ[270]

Yaani, kuna ishara mbili kwa Mahdi wetu, na tangu kuumbwa mbingu na ardhi ishara kama hizi hazijatokea kwa mdai yeyote. Na ishara zenyewe ni hizi kwamba mwezi utapatwa tarehe ya kwanza ya kupatwa mwezi, yaani tarehe 13, na jua litapatwa tarehe ya katikati ya kupatwa jua, yaani tarehe 28.

Ishara hiyo ilidhihirika katika mwaka 1311 Hijriah sawa na mwaka 1894 katika sehemu ya mashariki ya ardhi, yaani katika Ulaya, Asia na Afrika, na mnamo mwaka 1895 katika sehemu ya magharibi ya ardhi, yaani katika Marekani. *Alhamdulillahi*.

Mwenyezi Mungu Akionyesha kupatwa kwa jua na mwezi

[269] *Taide Hak,* uk. 136

[270] Dar Qutni, uk.100

alishuhudia kwamba Imamu huyu ni kutoka Kwake. Ya pili Alidhihirisha hii pia kwamba mwito wake pia ni kwa ulimwengu wote, kama ulivyokuwa wa Mtume[saw] wake ambaye yeye alimfuata na kumtii, yaani Mtume Muhammad[saw]. Ya tatu, kupatwa kwa jua na mwezi katika sehemu ya mashariki kwanza inaashiria kwamba atatokana na sehemu ya mashariki, kisha kutoka kwake sehemu ya magharibi itatolewa mwito kwenye Islam. *Mungu ndiye mjuaji zaidi na elimu yake ni kamili.*

BAIATI YA KHWAJA KAMALUDDIN, MWAKA 1894

Khwaja Kamaluddin alikuwa akisoma katika Foreman Christian College, Lahore. Kwa athari ya mazingira alikuwa ameelekea kwenye Ukristo, lakini Mwenyezi Mungu Alimsaidia hivi kwamba alipata "Barahine Ahmadiyya". Basi ikawa hivi kwamba kiasi alichoendelea kusoma Barahin, athari ya Ukristo ikaendelea kuondoka na akaendelea kupata athari ya Islam. Yeye Akamfikia Hudhur[as] huko Qadian na akafanya baiati. Na kwa kuelekezwa naye, baada ya kutimia bishara kuhusu Lekhram, Maulawii Muhammad Ali pia alifanya baiati katika Machi 1897.

KUTIMIZA HOJA JUU YA MAULAWII RUSUL BABA

Juu ameshatajwa Rusul Baba kati ya masheikh wa Amritsar. Yeye alitokana na ukoo wa Kashmiri, jina lake lilikuwa Ghulam Rasul na aliyejulikana kwa jina Rusul Baba, alikuwa imamu katika msikiti wa marehemu Khan Muhammad Shah. Akalazimishwa na wafuasi Wakashmiri kuandika kitabu juu ya uhai wa Masihi[as]. Kwa hiyo, akaandika kitabu kiitwacho "Uhai wa Masihi". Alidai kwamba kitabu chake hakina jawabu na aliweka zawadi pia ya rupia elfu moja. Kijitabu hiki kilipomfikia Hudhur[as], yeye alitangaza kuandika jibu lake. Na akasema kwamba Rusul Baba anapaswa aweke pesa ya zawadi kwa waheshimiwa wa Amritsar Khan Bahadur Sheikh Ghulam Hasan na Khan Bahadur Khwaja Yusuf Shah na Haji Mir Mahmud mpaka mwisho wa Juni 1894, nao wapewe hiari kwamba wanitumie maandishi yao kwa saini zao kwamba tumeshapokea rupia elfu moja, na twakiri kwamba wakati wa kuthibitika ushindi wa Mirza Ghulam Ahmad tutamkabidhi Bwana Mirza rupia hizo elfu moja bila

kusita na Rusul Baba hatahusika nazo.

Hudhur[as] alisema kwamba namweka Maulawii Muhammad Husain Batalawii kuwa mwaamuzi kwa kutoa uamuzi, lakini kwa sharti hili kwamba Bwana Maulawii aape kwa kuitisha mkutano wa hadhara kwamba:

> "Enyi mliohudhuria, Wallahi, nimesoma vijitabu vyote viwili tangu mwanzo hadi mwisho, nami nasema nikiapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba kijitabu cha Sheikh Rusul Baba kinathibitisha uhai wa Hadhrat Masihi[as] kwa yakini kabisa. Na kijitabu cha mpinzani kilichotoka kukijibu hakibatilishi hoja zake. Na kama nimesema uongo au ninalo jambo moyoni mwangu kinyume chake, basi naomba kwamba katika mwaka mmoja nishikwe na ukoma au niwe kipofu au nife kwa adhabu mbaya yoyote nyingine. Basi. Ndipo wasikilizaji wote waseme kwa sauti kubwa mara tatu Amin, Amin, Amin, hapo mkutano uishie. Kisha mwapaji akisalimika kwa mwaka mmoja, kamati iliyopangwa itamrudishia Rusul Baba rupia zake elfu moja kwa heshima. Hapo sisi pia tutatangaza ikrari yetu kwamba kwa kweli Rusul Baba ameshathibitisha uhai wa Hadhrat Masihi[as]. Lakini kwa mwaka mmoja pesa itabaki kwa kamati iliyopangwa. Na kama Rusul Baba hataiwekea rupia elfu moja kamati katika wiki mbili baada ya kuchapishwa kijitabu hicho, basi utathibitika uongo wake wazi wazi, hapo kila mmoja anapaswa kujikinga kwa Mwenyezi Mungu na shari ya watu waongo kama hao na wajitenge nao."[271]

Kijitabu cha Hudhur[as] kiitwacho "Itmamul Hujjah" kilipochapwa, Hudhur[as] alikituma kwa posta ya rejista kwa Sheikh Rusul Baba, Maulawii Muhammad Husain Batalawii na waheshimiwa wa Amritsar waliotajwa juu. Lakini Maulawii Rusul Baba hakuweza kujipa moyo kutokea uwanjani akikubali masharti hayo. Matokeo yake yakawa kuwa kutoka katika jumuiya yake Hadhrat Mian Jiwan Butt[272], Mian

[271] Kijitabu ***Itmamul Hujjah***, uk. 28

[272] Yeye akawa baadaye mkwe wa Hadhrat Maulana Seyyid Sarwar Shah[ra].

Muhammad Sultan, Mian Ghulam Rasul na baadhi ya watu wema wengine walifanya baiati ya Hudhur[as].

MAULAWII RUSUL BABA KAFA KWA TAUNI, 8 DESEMBA 1902

Baada ya miaka michache ya tukio hilo, Hudhur[as] akipata taarifa kutoka kwa Mwenyezi Mungu alipotangaza kwamba tauni itaenea nchini, hapo Maulawii Rusul Baba alisema kwa fahari sana kwamba kusalimika na tauni hii kali ni dalili ya ukweli wangu. Dalili hii ya ukweli ya Rusul Baba ilipotangazwa vizuri mjini, tarehe 8 Desemba 1902, yeye alikufa kwa tauni na akathibitisha ukweli wa Jumuiya Ahmadiyya kwa kifo chake.

VITABU VYA MWAKA 1894

1. Hamamatul Bushra: Hudhur[as] aliandika kitabu hiki kwa ombi la Mwarabu mmoja mwenye ikhlasi, Muhammad bin Ahmad Makki, kwa watu wa Hijaz. Katika kitabu hiki Hudhur[as] ameeleza itikadi na madai yake.

2. Nurul Hak, sehemu ya kwanza na ya pili: Hiki pia ni kitabu cha Hudhur[as] katika Kiarabu. Sehemu yake ya kwanza ilichapishwa katika Februari 1894 na sehemu ya pili katika Mei 1894. Katika mjadala wa Amritsar, Abdullah Atham alipofedheheka, Padre Imaduddin aliandika kitabu "Tauzinul Akwaal" kwa kulipiza kisasi, ambamo alimtukana sana Mtume Mtukufu[saw] na pia alileta shutuma dhidi ya ufasaha na balagha ya Kurani Tukufu. Vile vile akawachochea Waingereza kwamba mtu huyu anawaiteni dajali. Yeye akipata nguvu ataasi na kadhalika. Kitabu hicho kilipomfikia Hudhur[as], kwa kukijibu Hudhur[as] aliandika ***Nurul Hak*** na aliweka zawadi ya rupia 5000 kwa padre atakayeandika jibu lake.[273]

3. Itmamul Hujjah: Kitabu hiki cha Hudhur[as] ni kwa Kiarabu na Kiurdu. Kitabu hiki kimeishatajwa nyuma.

4. Sirrul Khilafah: Kitabu hiki pia ni katika Kiarabu na Kiurdu. Kilichapwa mnamo Julai 1894. Ndani yake swala la ukhalifa

[273] Tangazo la tarehe 17 Machi 1894, *Tablighe Risalat*, J. 3

limejadiliwa kwa njia nyepesi sana, na hitilafu baina ya Mashia na Masuni imeamuliwa kwa njia bora sana.

5. Nuru za Islam: Kwa vile Abdullah Atham kwa sababu ya kurejea kwake hakufariki katika muda uliopangwa, na watu walipiga makelele sana, basi kwa kujibu makelele yao Hudhur[as] alichapisha kitabu hiki. Hiki ni makusanyiko ya matangazo mbalimabli ya Hudhur[as], ambayo yeye aliyachapisha kwa kumhimiza Atham kuapa pamoja na zawadi za maelfu ya rupia. Kitabu hiki kilichapishwa tarehe 6 Septemba 1894.

MKUTANO WA MWAKA 1894

Ingawa Hudhur[as] aliahirisha mkutano wa mwaka 1893 kwa baadhi ya sababu, lakini mkutano wa mwaka 1894 ulifanyika katika tarehe maalum zilizopangwa. Kwa kuhudhuria katika mkutano huo, Hudhur[as] aliwaalika kwa barua pia baadhi ya watu, kwa sababu hiyo katika mkutano huo watu wengi walishiriki kuliko mikutano iliyopita.

KUZALIWA KWA HADHRAT MIRZA SHARIF AHMAD, 24 MEI 1895

Mnamo 24 Mei 1895 alizaliwa Hadhrat Mirza Sharif Ahmad. Kumhusu yeye, Hudhur[as] alifunuliwa na Mungu mara mbili [274]مُعَمَّرُ اللهِ yaani mwenye kujaaliwa umri kutoka kwa Mungu. Kwa ufunuo huu tuna yakini kwamba Mwenyezi Mungu Atampa umri mrefu kinyume cha kawaida. Safari moja Hudhur[as] aliota kwamba Mirza Sharif Ahmad amevaa kilemba na watu wawili wamesimama karibu naye, mmoja wao akiashiria kwenye Sharif Ahmad alisema kwamba "Amekuja huyu mfalme." Wa pili akasema kwamba kwanza atakuwa kadhi. Hudhur akasema: Hakam pia anaitwa kadhi. Kadhi ni yule anayesaidia haki na kubatilisha batili."[275]

Safari moja, mwana huyo alipounga, Hudhur[as] alifunuliwa kumhusu yeye funuo zifuatazo:

1۔ عَمَّرَهُ اللهُ عَلٰی خِلَافِ التَّوَقُّعِ 2۔ اَمَّرَهُ اللهُ عَلٰی خِلَافِ التَّوَقُّعِ 3۔ اَءَنْتِ لَا تَعْرِفِیْنَ الْقَدِیْرَ

[274] Al Hakam, J. 11 Na.1, Badr, J. 6 Na.1

[275] Badr, 10 Januari 1907.

4۔ مُرَادُكَ حَاصِلٌ 5۔ اَللّٰهُ خَيْرٌ حَافِظًا وَّهُوَ اَرْحَمُ الرَّاحِمِيْنَ

Tafsiri ya funuo hizi ni hii:

1. Mwenyezi Mungu Atamjaalia umri zaidi ya matarajio.

2. Mwenyezi Mungu Atamjaalia kuwa amiri zaidi ya matarajio.

3. Je, humtambui Mweza (ufunuo huu ni kumhusu mama yake).

4. Mradi wako utapatikana.

5. Mungu ndiye Mlinzi bora kuliko wote, Naye ndiye Mrehemevu kuliko warehemevu wote.

KATUMA UJUMBE KWENDA SRINAGAR KWA KUTAFITI KABURI LA MASIHI[AS]

Katika mwaka huo kwa kuthibitisha kaburi la Hadhrat Masihi Mnazareti katika mtaa wa Khanyar, mjini Srinagar, alifanya uvumbuzi mpya wa kihistoria kwa ulimwengu wa Kikristo na Kiislamu. Ameeleza vya kutosha uchunguzi huu katika "*Nurul Kurani*" sehemu ya pili, na amethibitisha kwamba Wakashmiri wote ni Waisraeli waliohamia Afghanistan na Kashmir katika zama za Nebuchadnezzar. Kwa utafiti zaidi alituma pia ujumbe wa wanajumuiya wake, uliomletea taarifa baada ya utafiti kamili. Kwa kunufaika na taarifa hiyo, yeye aliandika kitabu cha kihistoria "Yesu katika India". Lengo muhimu la kutumwa kwa Hadhrat Masihi Mau'udi[as] lilikuwa "kuvunja msalaba", basi kwa uchunguzi huo aliweka msingi madhubuti wa lengo hilo. Baadaye Mwenyezi Mungu Akazalisha sababu hata kwamba watafiti wa Kikristo wenyewe wakaleta mambo ya kutosha kuhusu habari hiyo:

La kwanza: Katika Encyclopaedia Britannica, J. 14, zimechapishwa baadhi ya picha za Hadhrat Masihi Mnazareti[276] zinazodhihirisha kwamba Hadhrat Masihi Mnazareti[as], kwa yakini alipata umri zaidi ya

[276] Baadhi ya wazee wa Kikristo wa karne ya kwanza pia waliamini umri mrefu wa Hadhrat Masihi[as]. Irenaeus aliandika katika karne ya pili, kwamba Hadhrat Masihi[as] Mnazareti ni mfano kamili kwa dunia, maana amepita katika zama za utoto, ujana na uzee. (Someni: Kitabu cha Bishop Irenaeus 'The Works Against Heresies')

miaka 100. Picha hizo zimetunzwa kama "Amana Takatifu" katika Roma kwa Papa. Na imeandikwa katika Encyclopaedia kwamba Wakristo wa karne ya pili, tatu walitayarisha picha hizo.

La pili: Injili tulizonazo, ndani yake imeelezwa wazi kwamba Hadhrat Masihi[as], baada ya tukio la msalaba, alinyanyuliwa mbinguni. Katika sehemu ya mwisho ya Marko, mwisho wa Luka na katika Yuhana 3:13 imetajwa kuenda mbinguni kwa Masihi. Lakini, watafiti wa Kikristo wa zama hizi wakijipatia Injili za zamani na nakala zinazotegemewa kutoka akiolojia wakathibitisha kwamba mambo hayo yaliongezwa baadaye. Katika ***Authorised Version*** ya mwaka 1611 maoni hayo yote yamo, lakini katika ***Revised Version*** ya mwaka 1881, kwenye maelezo ya pembeni imeandikwa kwamba katika nakala zilizo bora na kutegemewa maneno haya kwamba Hadhrat Masihi[as] alienda mbinguni na wanafunzi walimwona Masihi akipanda mbinguni, hayamo. Ni dhahiri kwamba huo ulikuwa wakati ambapo Hadhrat Masihi Mau'udi[as] alikuwa akiandika kitabu chake maarufu "Barahine Ahmadiyya". Kwa hiyo inajulikana kwamba Mwenyezi Mungu Alianza kutayarisha njia kwa kazi yake kwa kupitia malaika.

Kisha kutoka Revised Standared Version ya mwaka 1946, aya hizo zote zikaondolewa katika matini na katika maelezo ya pembeni imeandikwa kwamba katika baadhi ya nakala aya hizi pia zimo. Na sasa katika maelezo ya pembeni ya Injili ya Kiurdu pia imeandikwa kwamba aya 12 za mwisho za Marko, zinazoeleza kwenda mbinguni kwa Hadhrat Masihi[as] hazimo katika nakala za zamani, bali badala ya aya hizo imetajwa kufika ujumbe wa Masihi[as] katika mashariki na magharibi.[277]

Tafsiri ya ibara hiyo ya C. R. Gregory inadhihirisha wazi kwamba baada ya tukio la msalaba, Hadhrat Masihi alidhihiri katika mashariki, na kwa kupitia wanafunzi wake dini ilihubiriwa mpaka magharibi. Ndiyo kusema kwamba katika nakala za zamani, badala ya kwenda mbinguni, ibara hii ilikuwepo kwamba baada ya tukio la msalaba

[277] Someni kijitabu: "Injili Markas ka Akhri Warak", utungo wa Sheikh Abdul Qadir Lyallpuri.

Hadhrat Masihi[as] alidhihiri katika mashariki.[278] Je, mabadiliko hayo hayathibitishi kwamba sawa na waandishi wa Injili zote nne, Hadhrat Masihi Mnazareti[as] hakuenda mbinguni bali alihamia nchi za mashariki na kutoka hapo mpaka magharibi alihubiri dini yake kupitia wanafunzi wake. Kama tukio la kwenda mbinguni lingekuwa sahihi, ingeyumkinikaje kwamba katika Injili zote nne habari hii isingetajwa.

La tatu: Hivi karibuni, Sanda ya Masihi[as] imepatikana ambamo mwili wake mtukufu ulifunikwa baada ya tukio la msalaba. Kuhusu sanda hiyo wanasayansi Wajerumani walifanya utafiti mpya uliochapwa katika gazeti moja[279] la Scandinavia kwa kichwa cha habari "Je, Masihi alifia msalabani?". Mhariri wa gazeti hilo aliandika:

> "Kundi moja la wanasayansi Wajerumani walikuwa wakifanya utafiti kuhusu sanda ya Yesu tangu miaka minane, ambao natija yake siku hizi imejulishwa kwa vyombo vya habari kwamba sanda ya Yesu ya miaka elfu mbili iliyopita imepatikana katika mji wa Turin wa Italia, juu yake zipo alama za mwili wa Yesu.
>
> Wanasayansi wameshamwarifu Bwana Papa pia kuhusu utafiti wao, lakini Bwana Papa amenyamaza mpaka sasa. Kwani, kwa matokeo ya utafiti huo, siri ya muhimu ya historia ya kidini ya kanisa la Katoliki imefichuliwa. Kwa msaada wa sanaa ya fotografia, wanasayansi wamejaribu kuthibitisha kwamba jambo walilodhania watu kuwa mwujiza miaka elfu mbili hapo kabla, kwa hakika ni tukio la kawaida kabisa, na wakathibitisha kinagaubaga kwamba Yesu kamwe hakufia msalabani."

Kuhusu habari hiyo, mbele imeandikwa:

> "Alama maradufu juu ya kitambaa cha sanda zinadhihirisha kwamba katika nusu ya kitambaa mwili wa Masihi[as] ulifunikwa, na katika nusu kilifunikwa kichwa. Kisha joto la mwili wa Yesu

[278] Someni kitabu cha C. R. Gregory, "The Canon and Text of the New Testament".

[279] Jina la gazeti hilo ni ***Stock Holm Zidiningen***, ndani yake makala hii ilichapwa katika toleo la 2 Aprili 1957.

na athari za dawa zilitia alama za mwili juu ya kitambaa, na damu ya Yesu iliyopenyea kitambaani ikatia alama. Alama za kuvishwa taji la miba, mikwaruzo ya paji la uso na kisogo, uvimbe wa shavu la kuume la Yesu, alama ya mkuki kwenye ubavu wa kulia na alama ya kukwaruzwa na msalaba mgongoni, hivyo vyote vinaweza kuonwa pichani. Lakini la kushangaza sana ni uhakika huu kwamba picha ya negativu inayadhihirisha macho yaliyofungwa ya Masihi kuwa macho mawili yaliyo wazi.

"Picha inaonyesha pia kwamba misumari haikupigiliwa viganjani bali ilipigiliwa katika viungu imara vya kiwiko, na hii pia inaonekana kwamba mkuki haukugusa kamwe moyo wa Yesu. Biblia inasema kwamba Yesu alikata roho, lakini wanasayansi wanang'ang'ania kwamba moyo haukuacha kufanya kazi.

"Hii pia inasemwa kwamba kwa sababu ya Yesu kutundikwa akiwa mfu, kwa saa nzima, ilipaswa damu ikauke, na kuisha, na katika hali hiyo damu isingepenya kwenye kitambaa. Lakini damu kupenyea ndani ya kitambaa yaonyesha kwamba Yesu alipoteremshwa kutoka msalabani alikuwa mzima."[280]

La nne: Chini ya Idara ya Arkiolojia ya India ilichimbwa ardhi hivi karibuni kandokando ya Srinagar, matokeo yake ni kuwa eneo kubwa la makaburi ya zamani ya Wakristo limegunduliwa. Hii pia inadhihirisha kwamba katika zama fulani Wakristo walikuwa wengi sana hapo.

La tano: Siku hizi upande wa mashariki ya Palestina na kaskazini mwa bahari ya chumvi katika mapango ya bonde la Qumran vijitabu kadha vilivyoandikwa na Bwana Yesu Mnazareti vimepatikana sawa na utafiti wa Kikristo. Katika vijitabu hivyo imetajwa kwamba maadui walijaribu kuniua, lakini Mwenyezi Mungu Aliniokoa na mauti, na akanileta juu ya uso wa ardhi kutoka ndani ya kaburi au pango ili niweze kutalii sehemu nyingi sana. Na katika vijitabu hivyo amedhihirisha itikadi zile zile

[280] Stock Holm Zidiningen, la tarehe 2 Aprili 1957

ambazo Kurani Tukufu imezieleza za Bwana Yesu.[281]

TANBIHI KWA WAARIA NA WAKRISTO KWA KUREKEBISHA MIJADALA YA KIDINI NA UKUMBUSHO KWA SERIKALI, 22 SEPTEMBA 1895

Kwa vile Hudhur[as] alikuwa amekabiliana na dini mbili za India katika mijadala, zilizojulikana kwa maneno yao makali, yaani Waaria na Wakristo, kwa hiyo, tarehe 22 Septemba 1895, Hudhur[as] alizipelekea dini hizo mbili tanbihi, na humo aliielekeza serikali ya India pia kwamba yapasa kubadilisha kabisa mtindo wa siku hizi wa mijadala, na badala yake yapasa kuizingatia haya:

La kwanza: Kundi moja lisilipinge kundi jingine kwa jambo lililopo pia katika kitabu cha ufunuo cha kundi hilo lenyewe.

La pili: Kila kundi lichapishe orodha ya vitabu vyake linavyoamini na kuvikubali, na mpinzani yeyote hatakuwa na haki ya kuleta shutuma kutoka katika vitabu visivyo katika orodha hiyo.

Orodha aliyochapisha Hudhur[as], ya vitabu vya kuaminika na kukubalika ni hii: Cha kwanza: Kurani Tukufu. Cha pili: Sahihi Bukhari, kwa sharti kwamba Hadithi yenyewe isipingane na Kurani Tukufu. Cha tatu: Sahihi Muslim, kwa sharti kwamba Hadithi yenyewe isipingane na Kurani Tukufu na Hadithi ya Bukhari. Cha nne: Sahihi Tirmidhii, Ibni Majah, Muwatta, Nasai, Abu Dawud na Dar Qutni, kwa sharti kwamba Hadithi yenyewe isipingane na Kurani Tukufu na vitabu viwili Sahihi, yaani Bukhari na Muslim.

Aliwaandikia Waaria na Wakristo pia kwamba nyinyi vilevile mchapishe vitabu vyenu mnavyoamini na kuvikubali. Na makundi yote mawili yashikamane na jambo hili kwamba kundi moja lisilipinge jambo lisiloweza kulithibitisha kutoka katika vitabu hivyo.

Ni dhahiri kwamba kwa kuzuia machafuko ya kidini, hilo lilikuwa ni pendekezo linaloingia akilini. Aliutuma ukumbusho pia kwa serikali ya India kwa saini za maelfu ya Waislamu. Lakini ni masikitiko

[281] Kwa vijitabu hivyo someni kitabu: *The Riddle of the Scrolls,* na H. E. Del Medico.

kwamba wakati ule serikali haikulifikiria. Naam, baada miaka kadha kanuni hii ilipitishwa kwamba kumtusi au kumvunjilia heshima mwanzilishi wa dini yoyote ni hatia kisheria.

SAFARI YA KWENDA DERA BABA NANAK, 30 SEPTEMBA 1895

Ni habari ya karibu mwaka 1872 kwamba Hudhur[as] alimwona Baba Guru Nanak[rha] katika ruya mara mbili, aliongea pia naye, na yeye alikiri kwamba mimi ni Mwislamu na ninakunywa maji kutoka chemchemi ile ile ambamo mnakunywa. Hudhur[as] anasema kwamba mimi binafsi nilikuwa na yakini kwamba Baba Nanak[rha] ni Mwislamu, lakini kwa kuwa sikuwa na uthibitisho kuwahakikishia watu, kwa hiyo nikakaa kimya.

Lakini baada ya muda mrefu Mwenyezi Mungu Alileta mathibitisho ambayo kwayo ikathibitika kwa yakini kwamba yeye alikuwa Mwislamu. Hapa chini mathibitisho mawili tu yanatajwa:

Kwanza: Jambo hili lilijulikana sana kwamba Hadhrat Baba Nanak[rh] alikuwa na kanzu moja aliyopewa kutoka mbinguni. Kanzu ile ilimilikiwa na wazao wa Kabli Mal katika Dera Baba Nanak, Wilayani Gurdaspur, na kwa kuizuru Masingasinga walikuwa wakija kutoka mbali sana. Na Masingasinga walipokuwa wakipata shida yoyote, wakaiweka kanzu hiyo kichwani na kuomba dua na hiyo shida ikaondoka. Hudhur[as] akisikia sifa hii ya kanzu, akafikiria moyoni kwamba hakuna budi kuiona kanzu hiyo. Basi baada ya kufanya istikhara sawa na suna, akafunga safari ya kwenda Dera Baba Nanak tarehe 30 Septemba 1895, siku ya Jumatatu asubuhi, pamoja na wafuasi wake wachache ambao majina yao ndiyo yafuatayo:

دیکھو اپنے دیں کو کس کس صدق سے دکھلا گیا ؛ وہ بہادر تھا نہ رکھتا تھا کسی دشمن سے ڈر

1. Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin[ra]
2. Hadhrat Maulawii Seyyid Muhammad Ahsan[ra]
3. Hadhrat Maulawii Abdul Karim Sialkoti[ra]
4. Bwana Munshi Ghulam Qadir Fasih[ra]
5. Hadhrat Sheikh Abdur Rahim (Bhai Jì).
6. Sheikh Rahmatullah Gujrati.
7. Bwana Mirza Ayub Beg[ra]
8. Hadhrat Mir Nasir Nawab[ra]
9. Hadhrat Mir Muhammad Ismail[ra]
10. Hadhrat Sheikh Haamid Ali[ra]

Karibu saa nne kabla ya adhuhuri alifika Dera Baba Nanak. Saa tano, kwa juhudi ya rafiki mmoja, ilipatikana nafasi ya kuona kanzu. Kanzu hiyo ilifunikwa katika mamia ya leso. Kila mtu mkubwa aliyekuja aliongeza leso ya thamani kama sadaka, lakini yeyote hakujua kwamba juu ya kanzu imeandikwa nini. Hudhur[as] na wenzake walimpa fedha ya kutosha yule mtu aliyekuwa anaonyesha kanzu, ili kuiona kanzu. Hudhur[as] aliwapa watu mbali mbali jukumu kwamba mtu fulani aandike ibara iliyoandikwa kwenye mkono wa kulia, na mtu fulani, maandishi ya mkono wa kushoto, na fulani yale ya kifuani na kadhalika. Basi kila ndugu alitimiza jukumu lake. Ikajulikana juu ya kanzu hiyo imeandikwa: لَا اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ ۔ اِنَّ الدِّيْنَ عِنْدَ اللّٰهِ الْاِسْلَامُ ۔ اَشْهَدُ اَنْ لَّا اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ وَ اَشْهَدُ اَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهٗ وَ رَسُوْلُهٗ ۔ , Suratul Fatihah, Ayatul Kursi, Suratul Ikhlas na kadhalika. Baada ya kurudi Qadian, Hudhur[as] aliandika mambo ya safari hiyo katika kitabu kimoja kiitwacho 'Sat Bachan' ambamo zaidi ya kutia picha ya kanzu, akatia marejeo kadha pia ya *'Janam Sakhi'* ili kuhakikisha kuwa Baba Nanak alikuwa Mwislamu.

Pili: *Pothi Sahib:* Kuna uthibitisho muhimu wa pili kwa kuhakikisha kwamba Hadhrat Baba Nanak[rh] alikuwa Mwislamu. Ingawa uthibitisho huu ulipatikana baada miaka kadha mnamo Aprili 1908, lakini kwa kusudio la kuyataja mathibitisho yote pamoja, huu umetajwa hapa, na uthibitisho huu ni *Pothi Sahib* ya Baba Nanak.

Hiyo pia ni ukumbusho wa Hadhrat Baba Sahib waliohifadhi masingasinga kwa uangalifu sana katika Guru Hars-hae, Wilaya ya Gurdaspur. *Pothi Sahib* imemilikiwa na wazao wa Guru wa nne wa Masingasinga Bwana Ramdas. Kuhusu *Pothi* hiyo Masingasinga wanasimulia kwamba Hadhrat Baba Sahib alikuwa anaining'iniza shingoni mwake saa zote, na nyakati nyingi alikuwa akiisoma hiyo. Kuizuru *Pothi* hiyo watu huja kutoka sehemu za mbali na wanatolea pale maelfu ya rupia. *Pothi* hiyo pia imefunikwa katika maishirini ya leso kama vile kanzu, na inaonyeshwa kwa nadra tu ikifunguliwa. Na sababu yake ni kwamba atakaye kuiona analazimika kutoa sadaka ya rupia mia moja na moja, na msimamizi wake anaionyesha baada ya kuoga mara mia moja na moja. Hudhur[as] alipopata habari kuhusu *Pothi* hiyo, basi kwa kuizuru alituma ujumbe mmoja wa wafuasi wake walioenda na wakazuru *Pothi* hiyo. *Pothi* hiyo ilipofunguliwa, kumbe hiyo ilikuwa ni Kurani Tukufu nzima katika saizi ndogo, kuanzia Bismillahi hadi Wannas. Ni dhahiri kwamba huo ni uthibitisho muhimu wa pili wa jambo hili kwamba Hadhrat Baba Nanak[rh] alikuwa Mwislamu.

VITABU VYA MWAKA 1895

Mnamo mwaka 1895, Hudhur[as] aliandika vitabu vifuatavyo:

1. Minanur Rahman: Kwa kuhakiki lugha ipi ni mama wa lugha zote, kitabu hiki hakina mfano. Ndani yake, yeye amethibitisha kwa hoja madhubuti kwamba Kiarabu ni mama wa lugha zote. Kitabu hicho kwa kutokamilika hakikuweza kuchapwa katika uhai wa Hudhur[as], bali hata baadaye kilichapwa katika hali ile ile aliyokuwa amekiacha.

2. Nurul Kurani, sehemu ya kwanza na ya pili: Tarehe 15 Juni na 20 Desemba 1895, Hudhur[as] alikuwa na nia kwamba kwa kudhihirisha sifa kamilifu za kiroho za Kurani Tukufu, lianzishwe jarida la kila mwezi. Basi, kwa jina la "Nurul Kurani" alianzisha jarida moja, lakini ni masikitiko kwamba kwa shughuli nyingi matoleo yake mawili tu yaliweza kutolewa.

3. Sat Bachan: Katika kitabu hiki, Hudhur[as] ameeleza kwa urefu sana habari za safari yake ya Dera Baba Nanak. Vilevile ameeleza itikadi ya

Hadhrat Baba Nanak sawa na *Guru Garanth* na *ma-Janam Sakhi*.

4. Aria Dharm: Kitabu hiki kilichapwa 22 Septemba 1895. Ndani yake, Hudhur[as] ameeleza vizuri kuhusu mitala, talaka, na pia imani ya Waaria ya *Neyoga*.

PENDEKEZO LA KUTOA RUHUSA SIKU YA IJUMAA, 1 JANUARI 1896

Tarehe mosi Januari 1896 Hudhur[as] alimwandikia *Viceroy* wa India kwa saini za Waislamu wengi kuiomba serikali kwamba kusali sala ya Ijumaa ni faradhi ya kidini kwa Waislamu, kwa hiyo Waislamu wapewe ruhusa siku ya Ijumaa. Lakini ni masikitiko kwamba baadhi ya masheikh na Waislamu waliokuwa chini ya athari yao waliupinga kwa sababu hii tu kwamba ukumbusho huo umeandikwa kwa kalamu ya Hudhur[as]. *Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun.* Hudhur[as] alipojua jambo hili, yeye alimwandikia Maulawii Muhammad Husain Batalawii kwamba kama wataka kujaribu kuhusu jambo hili, nipo tayari kukukabidhi mambo yote niliyofanya tayari kuhusu jambo hilo, lakini Bwana Sheikh mwenyewe pia hakufanya kitu wala hakumwacha Hudhur[as] kufanya. Matokeo yake ni kwamba kwa sababu ya upinzani wa masheikh jambo hilo lilishindikana wakati huo, lakini baada ya Hudhur[as] kufariki, katika zama za Khalifatul Masihi[ra] I, jambo hilo likaanzishwa tena. Safari hii kwa kuwa Waislamu wote walilipeleka kwa pamoja, kwa hiyo serikali ilikubali. Lakini ni masikitiko kwamba Waislamu hawakujifaidisha sana na ruhusa hiyo, ni Waislamu wachache sana wanaosali kila sala ya Ijumaa.

MWITO KWA WAKRISTO KWENYE UAMUZI KWA NJIA BORA, 14 DESEMBA 1896

Utabiri kuhusu Deputy Abdullah Atham na mwisho wake umeshaandikwa kwenye kurasa za nyuma. Baada ya kifo chake, mapadre walipopiga makelele sana, Hudhur[as] akawaambia njooni ili kwa kumaliza ugomvi wa kila siku niwaambieni njia bora ya uamuzi, nayo ndiyo hii kwamba "Hitilafu hii iliyozidi sana, tupate uamuzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu."

Basi, akasema:

"Kama uamuzi wa Mungu si kunisaidia, nitawapa Wakristo mali yangu yote inayohamishika na isiyohamishika ambayo haipungui rupia elfu kumi. Pia naweza kuwawekea hadi rupia elfu tatu mapema. Kutoka mali kiasi hiki mkononi mwangu itakuwa adhabu ya kutosha kwangu. Zaidi ya hayo, nakiri hii pia kwamba nitachapisha tangazo kwa saini yangu kwamba Wakristo wameshinda na mimi nimeshindwa, nami nakiri hii pia kwamba katika tangazo hili halitakuwa sharti lolote pia, si kwa maneno wala si kwa maana.

Na kwa uamuzi wa Mungu taratibu yake itakuwa hii kwamba kwa kunikabili padre mmoja mheshimiwa achaguliwe kwa ridhaa ya pande mbili, miongoni mwa mapadre wafuatao ambaye awe amekubali kuingia katika medani ya mashindano. Kisha sisi wawili pamoja na makundi yetu tuhudhurie katika medani iliyopangwa, na tumwombe Mwenyezi Mungu uamuzi huu kwamba kati yetu wawili yule mtu ambaye kwa kweli ni mwongo na mwenye kughadhabikiwa machoni mwa Mwenyezi Mungu, katika mwaka mmoja Mwenyezi Mungu Amteremshie mwongo huyo adhabu ambayo kwa sababu ya ghera yake Aliwateremshia Firauni, Nimrodi, kaumu ya Nuhu[as] na Wayahudi. Waheshimiwa mapadre wakumbuke kwamba katika kuombeana hivi, hamna laana wala dua mbaya dhidi ya kundi lolote maalum, bali lengo lake ni kumwadhibisha mwongo ambaye hataki kuacha uongo wake. Afadhali afe mmoja kwa kuhuika dunia nzima."

Katika tangazo hilo hilo, mbele anasema Hudhur[as]:

"Enyi mapadre! Angalieni, nimesimama kwa kazi hii. Mkitaka kwamba kwa hukumu na uamuzi wa Mungu ibainike tofauti kati ya mkweli na mwongo, basi njooni tushindane uwanjani kwa maombi ili mwongo aaibike. Jueni kwa yakini kwamba Mungu Yupo, na bila shaka Yule Mweza Yupo, na daima Anawahami wakweli. Basi kati yetu sisi wawili atakayekuwa mkweli, lazima Mwenyezi Mungu Atamsaidia. Kumbukeni jambo hili kwamba mtu aliye dhalili machoni mwa Mungu

atapata dhila baada ya mashindano haya, na aliye mheshimiwa machoni mwake atapata heshima."

Kisha akasema:

"Sisi wawili tutaomba hivi: Ee Mungu Mweza, wakati huu twashindana makundi mawili. Kundi moja lamwita Yesu mwana wa Mariamu kuwa Mungu na halimtambui Mtume wa Islam kuwa Nabii mkweli, na kundi la pili lamwamini Isa mwana wa Mariamu kuwa Mtume na binadamu tu, na kumtambua Mtume wa Islam kuwa mkweli kabisa na mwamuzi baina ya Wayahudi na Wakristo. Basi kati ya makundi haya mawili, kundi lililo lenye imani ya uwongo machoni mwako uliangumize katika mwaka mmoja. Na inapaswa kwamba kundi moja litakapoomba, kundi la pili liseme Amin; na litakapoomba kundi lile, kundi hili liseme Amin.

"Hamu yangu ni kwamba kwa shindano hili achaguliwe Dkt. Martin Clark kwani yu mnene, kijana, mwenye afya nzuri sana, tena ni daktari. Yeye atafanya mpango kamili wa kuzidisha umri wake. Kwa yakini Martin Clark lazima atakubali ombi letu… Na akikimbia, basi Padre Imaduddin anafaa kwa shindano hili aliyetumia kila ujanja wa kibinadamu kwa kumfanya mwana wa Mariamu kuwa Mungu na akamvunjia heshima Jua (Mtume s.a.w.). Kama yeye pia akikimbia kwa hofu kwamba adhabu ya Mungu lazima itamwangamiza, basi Husamuddin au Safdar Ali au Thakar Das au Thomas Houle na hatimaye Fat-he Masih aje uwanjani au padre yeyote mwingine aje uwanjani. Kama baada ya kuchapishwa kijitabu hiki mpaka miezi miwili hakuja uwanjani yeyote na kuleta udhuru tu wa kishetani, basi itapigika muhuri juu ya mapadre wote wa Panjab na India kuwa waongo. Kisha Mungu mwenyewe Ataung'olea mbali mzizi wa uongo. Kumbukeni kwamba lazima Ataung'oa, kwani wakati wenyewe umewadia."[282]

[282] Kutoka katika Tangazo la 14 Desemba 1896, lililomo katika Anjame Atham, uk. 34 hadi 44.

Ni dhahiri kwamba kwa kupima ukweli wa Islam na Ukristo, njia hii ya uamuzi ilikuwa ya kiadilifu, lakini miongoni mwa mapadre hata mmoja hakuikubali.

TAARIFA YA MKUTANO WA DINI ZOTE, DESEMBA 1896

Kazi moja ya Hudhur[as] ilikuwa kuishindisha Islam juu ya dini zote za duniani. Kwa ajili yake, Mwenyezi Mungu Alimjaalia nafasi nyingi, lakini nafasi ninayotaja labda ilikuwa ya muhimu kuliko zote. Yeye alikuwa na hamu tangu zamani kwamba mkutano mmoja ufanyike ambamo viongozi wa dini zote wa dunia wakaribishwe kuthibitisha uzuri wa vitabu vyao vya ufunuo. Basi kwa ajili yake Mwenyezi Mungu Alimpatia nafasi nzuri sana.

Katika mwaka 1896, baadhi ya waheshimiwa Mabaniani walipendekeza kufanya mkutano wa dini ambamo ilipendekezwa kuwa hotuba zitolewe kwa kujibu maswali matano yafuatayo:

1. Hali za binadamu za maumbile, khulka na roho.

2. Nini hali ya mtu baada ya kufa?

3. Nini shabaha ya maisha ya binadamu katika dunia, na ni njia gani ya kuipata?

4. Nini athari ya vitendo katika dunia na akhera?

5. Ni zipi njia za kupata elimu ya kiroho?

Inaonekana kwamba kwa kutimiza makusudio yake, Mwenyezi Mungu Aliwafanya waitishe mkutano huo. Mpendekezaji wa mkutano huo Swami Shivgun Chandar alipomwendea Seyyidna Ahmad[as], yeye mara moja alikubali kuandika makala, bali tangazo lake la kwanza alichapisha katika Qadian na alimteua mfuasi wake mmoja kuwasaidia kwa njia zote. Waaria, Wakristo, Wasanatan Dharm, Wabarhamu Samaj, Masingasinga, Wateosofia, Free Thinker, ilmuradi viongozi wa kila dini walikaribishwa kuandika majibu ya maswali hayo. Miongoni mwa Waislamu, zaidi ya Hudhur[as], Maulawii Muhammad Husain Batalawii, Maulawii Thanaullah Amritsari na Maulawii Abu Yusuf Muhammad Mubarak Ali Sialkoti walikaribishwa.

Mkutano ulipangwa kufanyika tarehe 26, 27 na 28 Desemba 1896, na ilipendekezwa kufanyika katika ukumbi wa Islamia College.[283] Hudhur[as] alipokuwa bado akiandika makala, alifunuliwa kwamba makala yako itashinda makala zote. Hapo kwa kutangaza ufunuo huo, Hudhur[as] alichapisha tangazo moja tarehe 21 Desemba 1896, yaani siku 5, 6 kabla ya mkutano, ambalo ni hili:

> "Katika Mkutano Mkuu wa Dini utakaofanyika katika Ukumbi wa Mji wa Lahore,[284] tarehe 26, 27 na 28 Desemba 1896, makala yangu kuhusu ubora na miujiza ya Kurani Tukufu itasomwa. Makala hii inazidi uwezo wa kibinadamu na ni ishara mojawapo katika ishara za Mungu na imeandikwa kwa msaada Wake maalum. Ndani yake kweli na maarifa ya Kurani Tukufu vimeandikwa vitakavyohakikisha kama jua ling'aavyo kwamba kwa kweli Kurani Tukufu ndiyo Neno la Mungu na Kitabu cha Mola wa walimwengu. Na mtu yeyote atakayesikiliza kwa makini majibu ya maswali yote matano yaliyoelezwa ndani ya makala hii, tangu mwanzo hadi mwisho, nina yakini kwamba ndani ya mtu huyo imani mpya itazalika na nuru moja mpya itang'aa nafsini mwake, na atapata mkononi mwake maelezo makamilifu ya Neno Takatifu la Mwenyezi Mungu.
>
> "Hotuba yangu imeepukana na upuuzi wa kibinadamu wala haina doa la majivuno. Huruma ya binadamu imenilazimisha wakati huu kutoa tangazo hili, ili wakashuhudie uzuri na jamali ya Kurani Tukufu na wazingatie kwamba wapinzani wetu wanadhulumu namna gani kwa kulipenda giza na kuuchukia mwanga. Mungu Aliye Mjuzi wa mambo ya ghaibu Amenijulisha kwa ufunuo kwamba makala hii itazishinda makala zote zingine. Na ndani yake kuna nuru ya ukweli,

[283] Katika zama zile haikuwepo Islamia College ya sasa, mkutano ulifanyika katika jengo la Anjuman Himayate Islam Lahore iliyopo katika Lango la Sheranwala katika sehemu ya ndani. (Mwandishi)

[284] Inaonekana kwamba mkutano huo mwanzoni ulipangwa kufanyika katika Ukumbi wa Mji wa Lahore, lakini baadaye kwa kitendo ulifanyika katika Ukumbi wa Islamia College Lahore. (Mwandishi)

hekima na maarifa ambayo watu wa mataifa mengine, wawe Wakristo au Wasanatan Dharm au wowote wengine, wakihudhuria na kusikiliza kwa makini tangu mwanzo hadi mwisho, wataona haya, wasiweze kuonyesha ubora huo kutoka katika vitabu vyao vya dini. Kwani, Mwenyezi Mungu Amekusudia kudhihirisha shani ya Kitabu chake Kitukufu siku ile. Kuihusu hiyo niliona katika kashfi kwamba Mkono mmoja kutoka kwa ghaibu ulipigwa juu ya jumba langu, na kwa sababu ya Mkono huo kuligusa jumba hilo nuru moja ing'aayo ikatoka kutoka katika jumba na kuenea pembezoni mwake; mwanga wake ukaangukia hata mkono wangu pia. Hapo mtu mmoja aliyekuwa amesimama karibu nami akapaza sauti akisema: *Allahu Akbar, Kharibat Khaibar* (Mungu ni Mkuu, Khaibar imeanguka). Uaguzi wake ni kwamba 'jumba' linamaanisha moyo wangu panaposhukia nuru ambayo nuru hiyo ni maarifa ya Kurani; na Khaibar ni zile dini mbovu ambamo ushirikina na bidaa vimechanganyikana na mtu amepewa cheo cha Mungu; au sifa za Mungu zimeshushwa hadhi. Basi nimehakikishiwa kwamba kwa njia ya makala hii kuenea sana, uwongo wa dini za batili utadhihirika na ukweli wa Kurani utazidi kutapakaa siku hadi siku mpaka utimize duara lake. Kisha nikahamishwa kutoka katika hali hiyo ya kashfi kwenye hali ya kupokea ufunuo, nami nikafunuliwa: *Innallaha Ma'aka. Innallaha Yakuumu Ainamaa Kumta*. Yaani, Mungu Yupo pamoja nawe. Mungu Anasimama pale usimamapo. Hiyo ni istiara inayomaanisha Msaada wa Mungu. Sipendi kuendelea kuandika zaidi. Nampasha habari kila mmoja ili kuhudhuria Lahore katika tarehe za Mkutano hata kwa kuacha shughuli zingine za muhimu kwa kusikiliza mambo hayo yenye maarifa, kwani kwa kuyasikiliza hayo akili zao na imani zao zitanufaika wasivyotazamia."[285]

Tangazo hili lililokuwa na bishara kubwa lilifikishwa kila sehemu ya nchi. Lilibandikwa kwenye kuta za Lahore na liligawanywa kwa watu

[285] Tablighe Risalat, Tangazo la 21 Desemba 1896.

pia. Kisha ilipofika tarehe ya mkutano, wajumbe wa dini zote walikuwepo. Wakati kwa hotuba ya Hudhur[as] ulikuwa tangu saa 7:30 hadi saa 9:30.[286] Hadhrat Maulawii Abdul Karim Sialkoti[ra] alipoanza kusoma hotuba hiyo, watu walitawaliwa na hali ya ajabu, kutoka pande zote sauti zilipazwa za kusifu. Masaa mawili, yaliyokuwa yamewekwa kwa hotuba hiyo yalipoisha, na hata sehemu moja ya makala hiyo haikumalizika, watu wakasema kwa sauti moja kwamba lazima tutasikiliza hotuba hii. Hata kama siku moja nyingine itengwe. Hapo, wasimamizi wakawa hawana la kufanya na wakaongeza siku ya 29 Desemba kwa hotuba hiyo. Hotuba hiyo ilipomalizika, mheshimiwa Baniani mmoja aliyekuwa mwenyekiti wa mkutano mara alitamka "makala hii imezishinda makala zote." Na Gazeti maarufu la Lahore la Kizungu 'Civil and Military Gazette' likaandika:

> "Mkutano Mkuu wa dini zote wa Lahore uliofanyika tarehe 26, 27, 28 Desemba 1896 katika Ukumbi wa Islamia College Lahore, humo wajumbe wa dini mbalimabli walijibu maswali matano yafuatayo: (Mbele maswali matano yaliandikwa). Lakini wasikilizaji walivutika kwa moyo wote kwa hotuba ya Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, ambaye ni mahiri kabisa kuihami na kuitetea Islam. Kwa kusikiliza hotuba hiyo, khalaiki ya wafuasi wa madhehebu mbalimbali walimiminika kutoka mbali na karibu. Kwa kuwa Mirza Sahib hakuweza kuhudhuria binafsi, hivyo hotuba yake aliisoma mwanafunzi wake hodari, Maulawii Abdul Karim Sialkoti. Tarehe 27, hotuba hiyo ilisomwa kwa masaa matatu. Watu waliisikiliza kwa furaha na makini kabisa, lakini bado jawabu la swali moja pekee lilimalizika. Maulawi Abdul Karim aliahidi kusoma sehemu iliyobakia ikiwa atapewa nafasi zaidi. Kwa hiyo, wasimamizi na mwenyekiti walikubali pendekezo la kuongeza siku ya tarehe 29 Desemba."

Kuhusu hotuba hiyo, taarifa iliyoandikwa na Mabaniani, maneno yake ni haya:

[286] Baadaye Maulawii Abu Yusufu Mubarak Ali Sialkoti pia akatoa wakati wake kwa kusoma makala hiyo.

"Baada ya hotuba ya Pandit Gurdhan Das, kulikuwa na nafasi ya nusu saa ya kupumzika, lakini kwa kuwa baadaye ilikuwa imepangwa hotuba ya mwakilishi maarufu wa Islam, hivyo washabiki wengi hawakuinuka kabisa. Muda mwingi ulibaki kutimia saa 7:30, lakini uwanja wenye wasaa mkubwa wa Chuo cha Islamia ulijaa kabisa katika dakika chache. Ilikuwa ni hafla ya watu wapatao elfu saba hadi elfu nane. Wataalamu wengi wa dini, madhehebu na vyama mbalimbali walikuwepo. Ijapokuwa viti, meza na matandiko vililetwa kwa wingi, lakini mamia ya watu hawakuwa na budi kusimama. Miongoni mwa hao waliolazimika kusimama walikuwepo matajiri wakubwa, viongozi wa Panjab, wataalamu, mawakili, maprofesa, madaktari na kadhalika wakuu wa idara mbalimbali. Kukusanyika kwa watu hao hivyo, na kusikililza kwa masaa manne au matano kwa shauku na jazba kwa kusimama, kunadhihirisha jinsi walivyopenda Mwendeleo huu mtukufu. Mwandishi wa hotuba hakuweza kuhudhuria binafsi mkutanoni, lakini alikwishamtuma mwanafunzi wake maalum, Maulawii Abdul Karim Sialkoti, ili kusoma makala yake. Ingawaje masaa mawili tu yaliwekwa na kamati kwa makala hiyo kusomwa, lakini wasimamizi wa mkutano walipoona shauku na kiherehere cha wasikilizaji wa makala hiyo, wakaruhusu kwa furaha kwamba mkutano utaendelea hadi makala hiyo ipate kusomwa kikamilifu. Uamuzi huo uliafikiana na maoni ya wasikilizaji, kwani nafasi iliyokuwa imewekwa kwa makala hiyo ilipokwisha, mara Sheikh Abu Yusuf Mubarak alitoa nafasi ya hotuba yake ili makala hiyo ipate kumalizika, na hapo wasikilizaji na wasimamizi wakamtolea shukurani Sheikh huyo kwa kupaaza sauti kwa furaha. Mkutano ungemalizika saa 10:30 sawa na ratiba, lakini kwa kuangalia shauku ya watu wote mkutano uliruhusiwa kuendelea hadi saa 11:00. Kwani makala hiyo ilichukuwa masaa manne takriban, na ilisikilizwa tangu mwanzo hadi mwisho kwa uchangamfu na upendo wa namna moja."[287]

[287] Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Dini, kurasa. 79-80.

Wasomaji wakitaka kukisia thamani ya makala hiyo, basi wasome taarifa ya mkutano huo iliyochapwa na wasimamizi wa mkutano. Ndani yake imeandikwa hotuba kamili ya mjumbe wa kila dini. Ama tafsiri ya hotuba ya Hudhur[as], hiyo imeshachapwa katika lugha nyingi za dunia. Katika Kiurdu inaitwa "Islami Usul ki Falasafi", katika Kiarabu "Alkhitabul Jalil" na katika Kizungu "Teachings of Islam".

Hapa chini yandikwa maoni ya baadhi ya wanachuoni kuhusu makala hiyo.

1. Theosophical Book Notes likaeleza: "Kitabu hiki ni picha nzuri sana ivutiayo mno ya dini ya Muhammad[saw]."

2. 'Indian Review' likaandika: "Kitabu hiki ni cha kuvutia na cha kufurahisha. Mawazo yake ni yenye kung'aa, yaelezayo yote yaliyotakikana na yaliyojaa hekima, na msomaji hulazimika kukisifu. Kitabu hiki kinapaswa kiwe mkononi mwa kila mtu atakaye kusoma dini ya Muhammad[(saw)]."

3. 'Bristal Times and Mirror' likaandika: "Kwa yakini, mtu azihutubiaye Ulaya na Amerika hivyo, hawezi kuwa mtu wa kawaida."

4. Mwandishi mmoja asiyekuwa Mwahmadiyya aliandika akitoa maoni juu ya hotuba ya Hudhur[as]:

> "Katika hotuba zote, hotuba iliyo nzuri zaidi iliyokuwa roho ya Mkutano ilikuwa ya Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian ambayo ilisomwa na mwenye ufasaha Maulawii Abdul Karim wa Sialkot kwa njia nzuri sana. Hotuba hiyo ilimalizika katika siku mbili: ilisomwa kwa masaa manne tarehe 27 Desemba, na kwa masaa mawili tarehe 29 Desemba. Ikamalizika kwa masaa sita kwa jumla, ambayo inaelekea kujaza kurasa kubwa 100 hivi.
>
> "Ilmuradi, Maulawii Abdul Karim alianza kusoma hotuba hiyo; lo, ni vizuri sana alivyoanza kuisoma! Wasikilizaji wakajazwa na upendo ajabu. Sauti za furaha na sifa zikasikika kila fungu la maneno liliposomwa; bali wakati mwingine wasikilizaji wakaomba maneno fulani yarudiwe kusomwa. Maisha mazima, masikio hayajawahi kusikia hotuba nzuri ya

kupendeza kiasi hiki.

"Hotuba zilizotolewa na wataalamu wa dini zingine, kwa kweli hazikuweza kujibu hata maswali yaliyoulizwa. Wasemaji wengi walizungumzia swali la nne tu na waliyagusia kidogo sana maswali mengine. Wasemaji wengi walikuwa na maneno mengi lakini bila kiini, isipokuwa hotuba ya Bwana Mirza Sahib aliyetoa majibu makamilifu ya maswali yote mbalimbali ambayo wahudhuriao waliyasikiliza kwa makini na shauku sana na wakayathamini na kuyatukuza.

"Sisi sio wafuasi wa Bwana Mirza Sahib, wala hatuhusikani naye hata kidogo; lakini hatuwezi kusema kinyume cha adili, wala hakuna mwenye dhamiri safi awezaye kuihalalisha. Bwana Mirza Sahib alitoa majibu ya maswali yote kutoka katika Kurani Tukufu ilivyopaswa, na akapamba mafunzo ya kimsingi na mafunzo mengine ya Kiislamu kwa hoja za kiakili na dalili za kifalsafa. Ilionyesha shani ya ajabu kuhakikisha kwanza kiakili masaala ya kiungu na kisha kusoma Neno la Mungu kama marejeo.

"Bwana Mirza Sahib hakueleza tu hekima za masaala ya Kurani, bali pia akafafanua hekima za maneno ya Kurani na falsafa yake papo hapo. Gharadhi, hotuba ya Bwana Mirza Sahib kwa jumla ilikuwa kamilifu timilifu ambamo lulu zisizohesabika zilikuwa ziking'aa za maarifa na kweli na hekima na siri; na falsafa ya kiungu ilielezwa namna ambavyo wafuasi wa dini zote wakashikwa na butaa. Watu wengi hivyo hawakuhudhuria katika hotuba ya mtu yeyote mwingine jinsi walivyohudhuria kwa wingi wakati wa hotuba ya Bwana Mirza Sahib. Ili kupambanua baina ya hotuba ya Mirza Sahib na hotuba za wasemaji wengine, yatosha kusema kwamba wakati wa hotuba ya Mirza Sahib watu walipakimbilia hapo jinsi nyuki waikimbiliavyo asali. Bali katika hotuba ya wengine wasikilizaji wakaanza kuondoka kwa kuchoka na kutokuvutika. Hotuba ya Sheikh Muhammad Husain wa Batala ilikuwa hivi tu ya kawaida; yale yale mawazo ya

kisheikh tunayosikia kila siku yakaelezwa. Haikuwa na jambo lolote jipya. Katika wakati wa hotuba ya sheikh huyo watu kadha wakaondoka; tena sheikh hakuruhusiwa hata dakika chache zaidi ili amalize hotuba yake."[288]

Kwa vyovyote, katika kitabu hicho imeonyeshwa taswira kamili ya Islam. Mtu yeyote atakayeona bishara ya Hudhur[as] iliyochapwa kabla ya wakati na kisha makala hiyo, lazima hataweza kujizuia kueleza kwamba kweli makala hiyo iliandikwa kwa msaada wa Mungu.

VITABU VYA MWAKA 1896

Katika mwaka 1896, vitabu vifuatavyo vilichapwa:

1. Anjame Atham: Kitabu hiki kilianzia kuandikwa katika mwaka 1896, na mwanzoni mwa mwaka 1897 kilichapwa. Ndani yake kuna tukio la Atham, na kisha shutuma za Masheikh wa Islam, Wakristo na Waaria zimejibiwa.

2. Hekima ya mafundisho ya Kiislamu: Hii ni hotuba ile iliyosomwa kwa niaba ya Hudhur[as] katika mkutano wa dini zote mjini Lahore.

ZAWADI YA RUPIA ELFU MOJA, 28 JANUARI 1897

Mtu yeyote miongoni mwa Wakristo asipofika kwa shindano hilo ambalo kwalo Hudhur[as] aliwaita katika tangazo la 14 Desemba 1896, basi kwa kutimiza zaidi hoja juu yao, Hudhur[as] alichapisha tangazo la zawadi ya rupia elfu moja, ambamo aliandika:

"Wakati huu nachapisha tangazo hili kwa ahadi madhubuti kwamba kama mtu yeyote miongoni mwa Wakristo akiweza kuthibitisha ishara za Yesu zinazochukuliwa kuwa dalili ya uungu wake, kuwa zinazidi kuliko ishara na miujiza yangu katika nguvu ya uthibitisho na wingi wa idadi, basi nitatoa rupia elfu moja kama zawadi. Nasema kwa kweli kabisa na kwa kuapa kwamba haitafanywa kinyume na ahadi. Naweza kuwekeza rupia hizo kwa mwamuzi ambaye anaaminiwa na

[288] Gazeti la 'Chaudawin Sadii', Rawalpindi, la 1 Feb. 1897. Tanbihi: Nakala ya Gazeti ipo katika Maktaba ya Ukhalifa, Rabwah.

kundi la pili.”[289]

Nakala elfu sita za tangazo hilo zilichapwa, walipelekewa Mapadre wote mashuhuri kwa njia ya rejista, lakini hata mmoja hakujibu. Naam, Mkristo mmoja asiyejulikana ingawa hakukubali mwito wa kushindana, lakini alichapisha shutuma chache katika “Christian Advocate Lucknow”. Hudhur[as] alizijibu katika magazeti ya tarehe 28 Februari 1897, na tarehe 11 Machi 1897. Na “Mukhbir Dakkan Madras” lilichapa kama nyogeza. Nani angaliweza kuyabatilisha majibu ya Hudhur[as]. Naam, jazba mpya dhidi ya Ukristo ikazalika moyoni mwa Hudhur[as].

KUVUNJA MSALABA NA LAANA, 6 MACHI 1897

Tarehe 6 Machi 1897 Hudhur[as] aliandika chini ya kichwa cha habari “Laana ya Mungu na Kuvunja Msalaba:

> “Kwa vile Wakristo wanaafikiana katika itikadi kwamba Yesu akifa msalabani alilaaniwa kwa siku tatu, na msingi wote wa wokovu sawa na imani yao ni juu ya laana hiyo. Kuhusu maana ya laana hiyo kuna ukinzani mkali ambao kwao inathibitika waziwazi kuwa batili itikadi ya utatu na kafara na swala la kusamehewa dhambi. Kama mtu yeyote anataka kuihami dini hiyo, basi ajibu haraka, waila angalieni jengo hilo zima limeshaanguka, na limeanguka vibaya sana hata kwamba itikadi zote za Kikristo zimepondeka chini yake, haukubaki utatu wala kafara wala msamaha wa dhambi. Angalieni kudra ya Mungu, umevunjilikaje mbali msalaba!!
>
> “Baadaye alieleza maana za laana kutoka ndani ya kamusi “Aqrabul Mawarid” ambazo ni hizi:
>
> اَللَّعْنُ اَلْاِبْعَادُ وَالطَّرْدُ مِنَ الْخَيْرِ وَمِنَ اللّٰهِ وَمِنَ الْخَلْقِ وَمَنْ اَبْعَدَهُ اللّٰهُ لَمْ تَلْحَقْهُ رَحْمَتُهٗ وَخَلَدَ فِي الْعَذَابِ وَاللَّعِيْنُ الشَّيْطَانُ وَالْمَمْسُوخُ وَقَالَ الشَّمَّاخُ اَلذِّئْبُ كَالرَّجُلِ اللَّعِيْنِ
>
> Yaani, muradi wa laana ni huu kwamba mlaaniwa ni yule akosaye kabisa kila aina ya heri na kipawa na rehema ya Mungu

[289] Tangazo la tarehe 28 Januari 1897

na maarifa ya Mungu, na aingiaye katika adhabu ya kudumu. Yaani, moyo wake uwe mweusi kabisa na isibaki nafsini mwake heri yoyote kutokea wema wowote mkubwa hadi wema mdogo, na ageuke kuwa shetani, na undani wake uharibike. Shammakh anamwita mtu mlaaniwa kuwa mbwamwitu katika ubeti wake, kwa sababu ya mlingano huu kwamba undani wa maluuni huharibika." Maneno yao yamekwisha.

"Sasa ukinzani ni huu kwamba kama hakika ya laana ni hii kwamba mahusiano yote ya maluuni yanakatika na Mungu, na haibaki tofauti kabisa kati yake na shetani, basi twawauliza mapadre kwa adabu sana kwamba je, hii ni kweli kwamba laana hiyo pamoja na mapasiko yote jinsi ilivyotajwa ilimwangukia Yesu kutoka kwa Mwenyezi Mungu? Naye kwa kupatwa na laana na ghadhabu ya Mungu akawa mwenye moyo mweusi na mbali na Mungu? Kwangu mimi, mtu yule mwenyewe ni mlaaniwa anayemwita mtu mwema kuwa mlaaniwa, kwa maneno mengine anapaswa kuitwa mwenye moyo mweusi, mbali na Mungu, na mwenye sifa ya shetani. Je, yeyote aweza kusema kwamba mtu mpendwa kama huyo kweli alikuja chini ya laana ambayo haiwezi kupatikana pasipokuwa na uadui mkamilifu wa Mungu...

Mwishowe akasema:

"Kama hiyo haijuzu, basi angalieni kwamba jengo zima la kafara limeporomoka na dini ya utatu imeangamia na msalaba umevunjika. Je, yupo yeyote duniani aijibuye?"[290]

MWITO WA HUDHUR[AS] WA MUBAHALA KWA WANAZUONI WAPINZANI KWA KUTAJA MAJINA, KUHUSU KUFUNULIWA KWAKE NA KUONGOLEWA NA MUNGU

Masheikh wapinzani wa Hudhur[as] walikuwa wakimtolea mwito wa mubahala tangu mwanzo wa madai yake, lakini yeye kwa kufikiria kwamba si sawa kufanyika Mubahala kati ya makundi mawili ya Waislamu, aliendelea kukataa. Lakini masheikh walipochapisha

[290] Tangazo la tarehe 6 Machi 1897.

fatuwa ya kufuru dhidi yake, ndipo yeye pia aliruhusiwa na Mwenyezi Mungu kufanya mubahala. Basi, katika mwaka 1892 aliwaambia masheikh wakufurishaji na wakadhibishaji kwamba sasa mtu yeyote miongoni mwa masheikh hao wapinzani anayetaka kufanya naye mubahala, anaruhusiwa kabisa; lakini wakati ule sheikh yeyote hakujitokeza.

Sasa alipotabiri kuhusu padre Abdullah Atham, ndipo masheikh wapinzani waliwaunga mkono waziwazi Wakristo sawa na mwenendo wao. Hapo, yeye aliwaandikia masheikh hao "Tangazo la Mubahala" ambamo alieleza kwanza kuwa yu Masihi Mau'udi na kasema kwamba kazi ya Masihi Mau'udi ndiyo kuvunja msalaba. Na njia yake kubwa ni kuthibitisha kifo cha Masihi[as] Mnazareti. Kisha alionyesha masikitiko juu ya mwenendo wa masheikh kwamba bila kujali aya za Kurani na Hadithi juu ya swala hilo wanawaunga mkono wazi wazi mapadre. Baada yake aliandika:

> "Kama bado masheikh wananidhania kuwa mzushi, basi kuna njia bora ya uamuzi, nayo ni hii kwamba kwa kushika mkononi funuo nilizoishachapisha nifanye mubahala na masheikh. Kwa njia hii kwamba nieleza kwa kula kiapo cha Mwenyezi Mungu kwamba kwa kweli nimebarikiwa na kuongea naye, na kwa kweli Yeye Amenituma mwanzoni mwa karne ya 14 ili niondoe fitina ile iliyo fitina kubwa mno dhidi ya Islam, na Yeye ndiye Aliyenipa jina la Isa na Amenituma kwa kuvunjilia mbali msalaba."

Baada yake, Hudhur[as] aliandika funuo zake zilizo kuanzia يَاعِيْسٰى اِنِّيْ لَا يُضَاعُ وَقْتُهٗ hadi "Lakini Mungu Atamkubali na Atadhihirisha ukweli wake kwa mashambulio makali".

Mbele kidogo, Hudhur[as] anaandika:

> "Je, jambo hili halistaajabishi kwamba mwongo, dajali na mzushi anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo mfululizo tangu muda wa miaka ishirini, hajafa mpaka sasa kwa dhila… Torati na Kurani Tukufu zote mbili zinashuhudia kwamba anayemzulia Mungu uwongo anaangamia haraka, hata habaki

yeyote kutaja jina lake. Na imeandikwa katika Injili pia kwamba kama hii ni kazi ya mwanadamu basi haraka itabatilika; lakini kama ni ya Mungu, isije mkawa wahalifu kwa kushindana naye. Mungu Mwenye shani kubwa Anasema katika Kurani Tukufu

اِنۡ يَّكُ كَاذِبًا فَعَلَيۡهِ كَذِبُهٗ ۚ وَاِنۡ يَّكُ صَادِقًا يُّصِبۡكُمۡ بَعۡضُ الَّذِىۡ يَعِدُكُمۡ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَهۡدِىۡ مَنۡ هُوَ مُسۡرِفٌ كَذَّابٌ[291]

Yaani, huyu akiwa mwongo, basi uongo wake ni juu yake, na kama akiwa mkweli, basi hamtaweza kuepuka na baadhi ya matabiri anayowaahidini. Mwenyezi Mungu Hamwongozi yule apitaye kiasi, mwongo mkubwa."

Baada yake aliandika kuwaambia Masheikh na ***ma-Sajjada Nashin*** kwamba:

"Sasa, Enyi Masheikh wapinzani na ***ma-Sajjada Nashin***, hitilafu hii imezidi sana baina yetu, na ingawa Jumuiya hii ni ndogo kuliko Jumuiya zenu na ni kundi dogo na labda mpaka sasa idadi yake haizidi elfu nne, tano,[292] hata hivyo mfahamu kwa yakini kwamba huu ni mmea uliopandwa na Mkono wa Mungu, Mungu hataipoteza kamwe. Hataridhika mpaka Aufikishe kwenye ukamilifu wake. Yeye Ataumwagilia maji na Ataulinda na Ataupa maendeleo ya ajabu. Je, mliacha kasoro yoyote kutumia nguvu? Kama ingekuwa kazi ya mwanadamu, basi ungekuwa umekatwa mapema sana mti huu na haingebaki hata alama yake.

"Yeye ndiye Ameniamuru kwamba nilete ombi la mubahala mbele yenu ili aliye adui wa ukweli aangamie na anayependa giza aingie katika giza la adhabu. Sikunuia kamwe hapo kabla mubahala wa namna hii, wala sikutaka kumwapiza mtu yeyote. Abdul Hak Ghaznawii, tena Amritsari, alinitaka nifanye mubahala, lakini niliendelea kukataa kwa muda mrefu.

[291] Sura Al Mumin, 40:29

[292] Kwa fadhili ya Mungu, leo idadi ya Jumuiya hii inafikia malaki. Je, hii si miongoni mwa bishara kubwa ambayo haiwezi kukanwa na mtu wa dini na dhehebu lolote. (Mwandishi)

Hatimaye kwa sababu ya kung'ang'ania kwake mubahala ulifanyika, lakini sikumwapiza. Lakini sasa nimesumbuliwa sana na kuudhiwa, nimekufurishwa, na nimeitwa dajali, nimeitwa jina shetani, nilichukuliwa kama mwongo na mzushi. Nikalaaniwa katika matangazo yao, nikatajwa kwa chuki katika vikao vyao, kwa kunikufurisha mlifanya bidii sana kana kwamba hamkuwa na shaka hata kidogo katika kufuru yangu.

"Sasa, inukeni, na muwe tayari kwa mubahala. Mmeishasikia kwamba madai yangu ni juu ya msingi wa mambo mawili. Kwanza juu ya aya za Kurani na Hadithi, pili juu ya funuo za Mungu. Lakini hamkukubali aya za Kurani wala Hadithi na mlikwepa Neno la Mungu kama mtu atupavyo kijiti akikivunja. Sasa imebakia sehemu ya pili ya msingi wa madai yangu. Nawaapisheni kwa jina la Mungu Mweza Mwenye ghera Ambaye kiapo chake hawezi kukikataa yeyote mwenye imani, kwamba njooni kwa kufanya mubahala nami kwa kuamua juu ya msingi wa pili.

"Itakuwa hivi kwamba baada ya kupangwa tarehe na mahali pa mubahala nitahudhuria uwanjani mwa mubahala nikishika mkononi mwangu karatasi ya funuo zote nilizoandika na nitaomba kwamba: Ee Mungu wangu, kama funuo hizi zilizomo mkononi mwangu ni uzushi wangu na wajua kwamba nimezitunga mwenyewe, au kama hizi ni wasiwasi wa kishetani na sio funuo zako, basi kuanzia tarehe ya leo, nifishe kabla ya kupita mwaka mmoja, au nitie katika adhabu itakayokuwa mbaya zaidi kuliko mauti, na usiniokoe katika hiyo mpaka mauti yanijie, ili dhila yangu idhihirike na watu wasalimike na fitina yangu, kwani sitaki kwamba kwa sababu yangu watu wako waingie katika fitina na upotofu, na ni bora mzushi wa aina hii afe. Lakini, Ee Mungu Mjuzi na Mwenye habari, kama Unajua kwamba funuo hizi zote zilizomo mkononi mwangu ni funuo zako na ni maneno kutoka kinywani mwako, basi uwatie wapinzani waliohudhuria wakati huu katika udhia mkali katika muda wa mwaka mmoja. Mmoja wao umpofushe, mwingine

umfanye kuwa mwenye ukoma, mwingine apatwe na faliji na mwingine awe mwendawazimu na mwingine ashikwe na kifafa, na mwingine aumwe na nyoka au mbwa mwenye kichaa, na mwingine umtermshie balaa mali yake, uhai wake na heshima yake. Nikishamaliza dua yangu, makundi yote mawili yaseme Amin. Kadhalika, kila mtu miongoni mwa kundi la pili aliyehudhuria mubahalani amwombe Mungu kwamba: Ee Mungu Mjuzi na Mwenye habari, kwa kweli twamfahamu mtu huyu aitwaye Ghulam Ahmad kuwa mwongo, mzushi na kafiri. Basi kama mtu huyu kwa kweli ni mwongo, mzushi, kafiri na asiye na dini, na funuo zake hizo si kutoka kwako bali ni uzushi wake, basi Uufanyie hisani umati huu wenye kuhurumiwa kwamba Umhilikishe mzushi huyu katika mwaka mmoja ili watu wasalimike na fitina yake. Na kama huyu si mzushi, bali ni kutoka kwako, na funuo hizo zote ni maneno kutoka kinywani mwako, basi Ututeremshie sisi tunaomfahamu kuwa kafiri na mwongo adhabu yenye dhila katika mwaka mmoja. Mmoja wao Umpofushe, mwingine Umfanye mwenye ukoma, mwingine apatwe na faliji, mwingine awe mwendawazimu na mwingine ashikwe na kifafa, na mwingine aumwe na nyoka au mbwa mwenye kichaa, mwingine Umteremshie balaa mali yake, uhai wake na heshima yake.

"Kundi la pili litakapomaliza dua hii, basi makundi yote mawili yaseme Amin.

"Baada ya mubahala huu nikifa katika mwaka mmoja au nikishikwa na adhabu ambamo alama za kupona hamna, basi watu watasalimika na fitina yangu na nitatajwa kwa laana ya kudumu… Lakini kama katika mwaka mmoja Mungu Akinilinda na mauti na adhabu za kimwili, na kwa wapinzani wangu zikadhihirika athari za adhabu na ghadhabu ya Mungu, na kila mmoja wao akishikwa na balaa yoyote na dua yangu dhidi yao ikidhihirika wazi wazi sana, basi ukweli utadhihirika kwa dunia na mabishano hayo ya kila siku yatakwisha. Nasema mara ya pili kwamba hapo kabla sikuapiza mtoaji shahada mbili

yeyote na nikaendelea kuvumilia. Lakini siku ile nitamwomba Mungu uamuzi, na nitashikamana na Utukufu Wake na Heshima Yake, ili Akiangamiza kundi dhalimu na mwongo kati yetu Aisalimishe dini yake hii imara na fitina ya wakorofi... Naweka sharti hili pia kwamba athari ya dua yangu ifahamike hapo tu ambapo watu wote ambao watakuja katika uwanja wa mubahala watashikwa na balaa yoyote kati ya balaa hizo. Na kama akisalimika hata mmoja, basi nitajiona mwongo, ingawa wawe elfu moja au elfu mbili… Uwe shahidi, Ee ardhi na Ee mbingu, kwamba laana ya Mungu iwe juu ya mtu ambaye baada ya kumfikia kijitabu hiki asihudhurie mubahalani wala asiache kunikufurisha na kufedhehesha wala asijitenge na kundi la wafanyao mzaha. Na enyi waaminio, kwa ajili ya Mungu nyote mseme Amin."[293]

Baada yake Hudhur[as] aliandika majina ya masheikh na ***Ma-Sajjada Nashin*** ambao aliwaita kwa mubahala. Miongoni mwao, majina ya masheikh na masufii mashuhuri ni haya:

MAJINA YA MASHEIKH

1. Maulawii Seyyid Nadhir Husain lakabu yake Sheikhulkul, Surajgarhi kisha Delhawii, 2. Sheikh Rashid Ahmad Gangohi, 3. Maulawii Abu Said Muhammad Husain Batalawii, 4. Maulawii Abul Wafaa Thanaullah Amritsari.

MAJINA YA MASUFII

1. Ghulam Nidhamuddin makamu wa Seyyid Niaz Ahmad Barelwii, 2. Mian Allah Bakhsh, Sajjada Nashin, Taunswi, 3. Hadhrat Mian Ghulam Farid wa Chacharan Sharif.

USADIKISHO WA HADHRAT MIAN GHULAM FARID WA CHACHRAN SHARIF

Kwa kujibu mwito wa mubahala huo, mwanachuoni au Sajjada Nashin yeyote hakujasiri kusadikisha au kukadhibisha, lakini kiongozi wa Nawab wa Bahawalpur, Hadhrat Khwaja Ghulam Farid wa Chacharan Sharif alimwandikia Hudhur[as] barua kwa lugha ya Kiarabu

[293] Tablighe Risalat, J. 5, uk. 54-55

ambayo tafsiri ya sehemu yake ndiyo ifuatayo:

> "Ibainike kwamba kitabu chako kimenifikia ambamo kuhusu mubahala jawabu limeombwa. Ingawa nilikuwa sina fursa, hata hivyo nimesoma sehemu moja ya kitabu hicho iliyojumuisha msemo mwema na njia ya kuatibu. Basi, Ewe mpendwa kuliko wapendwa wote, ujue kwamba tangu mwanzo nimesimama mahali pa kukuheshimu ili nipate thawabu, sijatamka neno lolote kuhusu wewe isipokuwa maneno ya taadhima, heshima na kudhihirisha adabu. Na sasa nakuarifu kwamba bila shaka nakiri hali yako njema, nami nina yakini kwamba u miongoni mwa waja wema wa Mungu, na juhudi yako mbele ya Mungu inastahili kushukuriwa utakayopata ujira wake, na fadhili ya Mungu Mfalme Mpaji iko juu yako. Niombee mwisho mwema, nami nakuombea mwisho mwema."[294]

Kwa kuona barua hiyo ya Hadhrat Mian Ghulam Farid, Hudhur[as] alifurahi sana na akaitia ndani ya Dhamima ya Anjame Atham, na akawasihi ma-Sajjada Nashin wengine pia kwamba waufuate mfano wa Mian Ghulam Farid.

Usadikisho wa Seyyid Rashiduddin, Kiongozi Sahibul 'Alam:

Sajjada Nashin wa pili alikuwa Seyyid Rashiduddin Kiongozi Sahibul 'Alam wa Sind aliyemsadikisha.[295] Huyu pia alimwandikia Hudhur[as] barua katika lugha ya Kiarabu ambayo tafsiri yake ndiyo ifuatayo:

> "Nilimwona Mtume Mtukufu[saw] katika hali ya kashfi. Nikamwuliza, Ee Mtume wa Allah, mtu huyu anayedai kuwa Masihi Mau'udi, je yu mwongo na mzushi au mkweli? Mtume wa Allah s.a.w. akajibu, yu mkweli na ndiye kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hapo nikaelewa kwamba u mkweli. Sasa baada yake hatutashuku katika mambo yako, na hatutakuwa na shaka yoyote katika shani yako. Na utakachosema nitakifuata. Basi kama ukisema uende Marekani, nitaenda huko.

[294] Dhamima Anjame Atham, uk. 36

[295] Baadhi ya wafuasi wa kiongozi huyu alimwomba kuomba kwa kujua ukweli wa Hudhur[as].

Nimejisalimisha kwako na utanikuta mwaminifu, inshallah.

"Khalifa wake marehemu Abdul Latif na Sheikh Abdullah Mwarabu waliniambia mambo hayo kwa mdomo. Hata sasa rafiki yangu mpendwa Seth Saleh Muhammad Haji Allah Rakha alimwendea kutoka Madras na akamkuta msadikishaji tu, bali akisimama katika kikao akishika fimbo mkononi akawaambia wahudhuriao wote kwa sauti kubwa kwamba namfahamu kuwa mkweli katika madai yake, na hivyo ndivyo nilivyofahamu kutoka katika kashfi. Na mwanaye alisema kwamba baba yangu anaposadikisha, basi mimi pia sikani."[296]

LAANA YA SHEIKH GHULAM DASTGIR KUSURI NA ATHARI YAKE, MWAKA 1897

Maulawii Ghulam Dastgir Kusuri alimwita Hudhur[as] kwa mubahala, lakini akaweka sharti hili kwamba kama Bwana Mirza yu mkweli basi inapaswa nishukiwe na adhabu papo hapo katika uwanja wa mubahala. Kwa kumjibu, Hudhur[as] alichapisha tarehe 15 Januari 1897 tangazo moja ambamo aliandika kwamba njia ya suna ya mubahala ni ile aliyoishika Mtume Mtukufu[saw] wakati wa kufanya mubahala na Wakristo wa Najran. Nayo ilikuwa ni hii kwamba wakija kwa mubahala wangeangamia katika mwaka mmoja. Ni dhahiri kwamba hii ilikuwa ni njia ya suna ya mubahala, ambayo Ghulam Dastgir Kusuri alilazimika kuifuata, lakini akiepa njia ya suna, alijichagulia njia nyingine ya kuangamia. Nayo ilikuwa ni hii kwamba katika mwaka 1315 Hijria aliandika kitabu "Fat-he Rabbani" ambamo aliandika: Ewe Mungu, Ee Mwenye utukufu na heshima, jinsi Ulivyokuwa Umemwangamiza Mahdi mzushi na Masihi wa bandia kwa dua na juhudi ya mwanachuoni mcha Mungu, Hadhrat Muhammad Tahir, mwandishi wa Majma'ul Bihari (aliyezaliwa katika zama zake), ndivyo ilivyo dua na ombi la Fakiri Kusuri — Mungu Awe naye — anayefanya juhudi sawa na uwezo wake kwa moyo wa kweli kusaidia dini yako imara kwamba umjaalie Mirza wa Qadian na wafuasi wake kufanya toba halisi; na kama hiyo haikukadiriwa, basi uwakamate

[296] Dhamima Anjame Atham, uk. 20 hadi 35

sawa na aya hii:

فَقُطِعَ دَابِرُ الْقَوْمِ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعَالَمِيْنَ۔ اِنَّكَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ وَبِالْاِجَابَةِ جَدِيْرٌ۔ اٰمِيْنُ-

Yaani, waliodhulumu watakatwa mizizi yao, na sifa zote njema zamhusu Allah, nawe ndiwe Mwenye uwezo juu ya kila kitu na Mwenye kupokea dua."[297]

Maulawii Ghulam Dastgir Kusuri aliandika hii pia katika kitabu chake kuhusu Hudhur[as] kwamba تَبًّا لَّهُ وَلِاَتْبَاعِهٖ , yaani, yeye na wafuasi wake waangamie." Ni kudra ya Mungu kwamba njia ya uamuzi Maulawii Ghulam Dastgir Kusuri aliyotaka, baada ya dua hiyo, sawa nayo katika siku chache tu akawa windo la tauni. Sasa je, kumbukumbu lolote la maana la Maulawii Ghulam Dastgir Kusuri limebaki? Hasha! Basi, jipatieni ibra, enyi wenye busara.

Maulawii Ghulam Dastgir Kusuri alipata shauku hii kwamba kama Imam Muhammad Tahir alivyomwombea dhidi ya Masihi mwongo, na Mwenyezi Mungu Akamwangamiza, ndivyo hivyo kwa maombi yangu Mwenyezi Mungu Atakavyomwangamiza mdai wa Umahdi wa zama zangu. Lakini ikawa hivi kwamba katika siku chache baada ya dua hiyo mwenyewe akaangamia.

MWITO KWA MASHEIKH WAPINZANI KUSHINDANA KATIKA ISHARA

Hudhur[as] alipoona kwamba masheikh wapinzani hawapo tayari kufanya nami mubahala kuhusu "funuo", basi kwa kutimiliza hoja zaidi aliwakaribisha kushindana naye katika ishara. Akasema kwamba ishara za Mwenyezi Mungu ninazo za aina sita. Muhtasari wake kwa maneno ya Hudhur[as] mwenyewe unaandikwa hapa chini:

Ya kwanza: Kama Sheikh yeyote akitaka kushindana na kitabu changu (Anjame Atham) katika ufasaha wa Kiarabu, huyo atafedheheka.

Ya pili: Na kama ishara hiyo isikubalike, basi wapinzani wangu wanikabili katika kuandika maelezo ya Sura yoyote ya Kurani kunikabili.

[297] Fa'the Rahmani, uk. 26-27

Ya tatu: Na kama ishara hiyo pia isikubalike, basi sheikh yeyote maarufu miongoni mwa wapinzani akae kwangu kwa mwaka mmoja. Katika muda huo, kama ishara yoyote iliyo nje ya uwezo wa mwanadamu isidhihirike nami, basi hata hivyo pia mimi ni mwongo.

Ya nne: Na kama hiyo pia isikubalike, basi kuna mapendekezo kuwa baadhi ya wapinzani mashuhuri watangaze kwamba baada ya tarehe hii, katika mwaka mmoja ishara yoyote ikidhihiri, tutatubu na tutakuwa wasadikishaji.

Ya tano: Na kama hiyo pia isikubalike, basi Sheikh Muhammad Husain Batalawii na wapinzani wengine maarufu wafanye mubahala nami. Kama baada ya mubahala akisalimika hata mmoja wao na athari ya dua yangu, basi nitakiri kwamba mimi ni mwongo.

Ya sita: Na wasipofanya lolote kati ya mambo hayo, basi wafanye suluhu nami na Jumuiya yangu kwa miaka saba hivi kwamba wasikufurishe wala kukadhibisha na kutusi, na wakutane na kila mmoja kwa mapenzi na huluka njema... Basi, katika miaka hiyo saba, kama isidhihirike athari kubwa ya kutumikia kwangu Islam kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, na kama vile ni lazima dini batili ziangamie kwa mkono wa Masihi, na ikiwa maangamio hayo ya dini batili yasidhihirike kwa njia yangu, yaani Mwenyezi Mungu Asidhihirishe ishara kwa mkono wangu zitakazosababisha ushindi wa Islam, ambao uwafanye watu waanze kujiunga na Islam kutoka kila upande na mungu batili wa Wakristo aangamie, na dunia igeuke kuwa nyingine kabisa, basi nasema kwa kula kiapo cha Mwenyezi Mungu kwamba nitajitambua kuwa mwongo. Hii miaka saba sio mingi, na kupatikana mapinduzi kiasi hiki katika muda mfupi siyo katika hiari ya mwanadamu. Basi ninapokiri kwa moyo wa kweli na kukiri kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu, na kuwaiteni kwenye suluhu kwa jina la Mungu, sasa Mwogopeni Mungu. Kama mimi si kutoka kwa Mwenyezi Mungu, nitaangamia, waila hakuna yeyote awezaye kumwangamiza aliyetumwa na Mungu.”[298]

Hudhur[as] aliwakaribisha Waislamu wasiokuwa Waahmadiyya kwa

[298] Dhamima Anjame Atham, uk. 20 hadi 35

sababu hii kwamba kazi ya kutangaza Islam aliyokuwa anafanya Hudhur[as], masheikh walikuwa wakiizuia na kupiga makelele kwamba watu hao wasio Waislamu na kadhalika. Kama Waislamu wote wangejumuika na kwa umoja wakiwakabili wengine, bila shaka hali ya India ingebadilika, lakini ni masikitiko kwamba shughuli ya Waislamu kukufurishana iliidhuru sana dini. Baada ya miaka 4-5, katika mwaka 1901, Hudhur[as] akaleta pendekezo hili na akipunguza muda wa suluhu akaufanya kuwa miaka mitatu, lakini ni masikitiko kwamba masheikh walikataa pendekezo hilo pia."[299]

UTABIRI KUHUSU KIFO CHA PANDIT LEKHRAM

Pandit Lekhram alikuwa Mwaria mwenye mdomo mchafu na mkali. Hadhrat Masihi Mau'udi[as] alipowakaribisha wasiokuwa Waislamu kuonyesha ishara katika mwaka 1885, yeye pia akaja Qadian kwa kushindana, lakini baada ya kukaa siku chache kwa wapinzani akarudi. Yeye alimwomba Hudhur[as] ishara mara kwa mara na akasema kwamba kuna ruhusa kutoka kwangu kuchapisha utabiri wowote kunihusu mimi.[300] Hudhur[as] alipoomba kumhusu yeye, akafunuliwa:

عِجْلٌ جَسَدٌ لَّهُ خُوَارٌ لَهُ نَصَبٌ وَّعَذَابٌ

Yaani, yu ndama tu asiye na uhai ambaye sauti ya kuchukiza inatoka kutoka ndani yake, na kwa sababu ya kukosa adabu na matusi imekadiriwa adhabu na huzuni na ikabu ambazo hana budi kuzipata.[301]

Baada ya ufunuo huo, tarehe 20 Februari 1893 alipoomba kwa kujua wakati wa adhabu yake, Mwenyezi Mungu Alimdhihirishia:

> "Kuanzia tarehe ya leo iliyo 20 Februari 1893, katika muda wa miaka sita, mtu huyo atashikwa na adhabu kali, kwa sababu ya mdomo wake mchafu, yaani ataadhibiwa kwa sababu ya utovu

[299] Someni Tangazo "*As-Sulhu Khair*" la tarehe 5 Machi 1901, lililoandikwa katika *Tablighe Risalat*, J. 10, uk. 6

[300] Tangazo la 20 Februari 1893

[301] Tangazo la 20 Februari 1893 lililoandikwa katika *Tablighe Risalat*, J. 3

wa adabu aliotenda dhidi ya Mtume wa Allah s.a.w.”[302]

Kuhusuye, Hudhur[as] alifunuliwa يُقْطٰى اَمْرُهٗ فِيْ سِتٍّ[303] , yaani habari za Pandit Lekhram zitakwisha katika ‘sita’.

Mwanzoni mwa tangazo la 20 Februari 1893, Hudhur[as] aliandika beti kwa Kiajemi kuhusu Pandit Lekhram ambazo tafsiri yake ni:

> Habedari! Ewe adui mjinga wa Islam uliyepotea, uuogope upanga wa Muhammad[saw] unaokata.
>
> Njia ya Mungu ambayo watu wameipoteza, njoo ukaitafute katika wana wa Kiroho na wasaidizi wa dini yake aliyoleta.
>
> Ewe mtu unayekana shani ya Muhammad[saw] na nuru yake iliyo wazi, ingawa karama haipatikani siku hizi, lakini njoo ukaishuhudie katika watumisi wa Muhammad[saw].

Kisha, tarehe 2 Aprili 1893, Hudhur[as] alitangaza kwa njia ya kipeperushi:

> “Leo, 2 Aprili 1893, sawa na 14 Ramadhan 1310 Hijria, wakati wa asubuhi katika lepe la usingizi kidogo nilijiona nimekaa katika nyumba yenye wasaa na pamoja nami wapo marafiki wachache pia. Mara akaja mtu mmoja na kusimama mbele yangu aliyekuwa pande la mtu, mwenye kutisha sura yake kana kwamba damu inatiririka usoni mwake. Nilipomwona nikafahmau kwamba yu mtu wa umbo na sura tofauti, kana kwamba si mwanadamu bali ni miongoni mwa malaika wagumu wakali, na hofu yake iliingia mioyoni. Na nilipomwona tu akaniuliza, “Lekhram yupo wapi?” na alitaja jina la mtu mwingine kwamba yu wapi? Ndipo nikaelewa wakati ule kwamba huyu ametumwa kumwadhibu Lekhram na yule mtu wa pili, lakini sikumbuki kwamba huyo mtu wa pili ni nani?”[304]

Kisha, katika huo mwaka 1893, Hudhur[as] aliandika kumwambia

---

[302] Tangazo la 20 Februari 1893 lililoandikwa katika ***Tablighe Risalat***, J. 3

[303] ***Istiftaa***, Kiurdu, maelezo ya pembeni, uk. 17

[304] Aina Kamalate Islam

marehemu Sir Seyyid Ahmad Khan katika kitabu chake "*Barakaatud Duaa'*" kwamba

ایکہ گوئی دعا ہا را اثر بودے کجاست　　سُوئے من بشتاب بنمائم تراچوں آفتاب

ہاں مکن انکار زیں اَسرارِ قدرتہائے حق　　قصہ کوتاہ کن بَبیں از ما دعائے مستجاب

Yaani, ewe usemaye kwamba kama dua ina athari, basi hiyo athari iko wapi, njoo kwangu haraka nikakuonyeshe athari ya dua kama jua. Usikatae kudra nyepesi sana za Mungu. Ukipenda kuona athari ya dua, njoo ukajionee natija ya dua yangu ambayo kuhusu hiyo Mungu Ameniambia kwamba imekubalika, yaani dua yangu kumhusu Lekhram.

Kisha aliandika katika kitabu chake Karamatus Sadikin kilichoandikwa katika mwaka 1893:

وَ بَشَّرَنِیْ رَبِّیْ وَ قَالَ مُبَشِّرًا　　سَتَعْرِفُ یَوْمَ الْعِیْدِ وَالْعِیْدُ اَقْرَبُ

Yaani, Mungu Amenibashiria kuhusu kifo cha Lekhram na Akasema kwamba karibuni utatambua siku ile ya idi, na siku yenyewe ya idi pia itakuwa karibu na idi hiyo.

Kwa sababu ya Pandit Lekhram kuomba ishara mara kwa mara, ile ishara ambayo Hudhur[as] alitaka kumwonyesha, kuhusu hiyo tumeshaandika utabiri kwa uwazi wa kutosha. Sasa tazameni upande wa pili wa picha.

Kwa kuwa pandit Lekhram hakujali kabisa utabiri wa Hudhur[as], kwa hiyo, kadri alivyozidi kueleza utabiri, ndivyo Bwana Pandit alivyoendelea kuzidi katika ujasiri na shari. Aliingiwa na dhana hii kwamba utabiri wa Hudhur[as] utabatilika — Mungu Apishe mbali — jinsi utabiri wake mwenyewe ulivyobatilika ambao yeye miaka michache hapo kabla alitoa kuhusu Hudhur[as] kwamba "Mtu huyu (yaani Hudhur[as]) atafariki katika miaka mitatu kwa kipindupindu, kwani (Mungu Apishe mbali) yu mwongo." Kisha aliandika, "Ataangamia katika miaka mitatu na hatabaki yeyote kati ya kizazi chake".[305]

[305] Someni *Takdhib Barahine Ahmadiyya*, na Pandit Lekhram, uk. 311

Lakini, angalieni uamuzi wa Mungu Jalia kwamba katika mwaka wa tano kutokea utabiri wake, ilivyoambiwa katika ufunuo يُقْطٰى اَمْرُهٗ فِيْ سِتٍّ , yaani habari za Pandit Lekhram zitakwisha katika miaka sita, Bwana Pandit siku ya pili ya Idilfitr, 6 Machi 1897, saa mbili jioni sawa na utabiri aliuawa. Na hivyo ikathibitika kwamba utabiri wa Hadhrat Masihi Mau'udi[as] haukuwa kutoka kwake mwenyewe, bali ulikuwa kutoka kwa Mjuzi wa ghaibu.

MATUKIO BAADA YA KUUAWA

Pandit Lekhram alikuwa kiongozi maarufu wa Waaria, na utabiri wa Hudhur[as] pia ulijulikana katika kila mahala. Hivyo, Bwana Pandit alipouawa, habari hiyo ikatapakaa katika nchi nzima. Katika magazeti ya Kibaniani, tukio hili la kuuawa lilichukuliwa kuwa ni njama ya Hudhur[as]. Aliandikiwa bila jina la mwandishi barua za kumtishia kumwua yeye. Katika vikao vya siri, zawadi kubwa kubwa ziliwekwa kwa kumwainisha mwuaji na kwa mwenye kumwua Hudhur[as], lakini haikugunduliwa nani amemwua. Mwenyezi Mungu Mwenyewe Alikwishachukua jukumu la ulinzi wa Hudhur[as] kama ilivyo dhahiri kutoka katika ufunuo wake: وَاللّٰهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ yaani Mungu Atakulinda na mashambulizi ya watu.

UPEKUZI WA NYUMBA YA HUDHUR[AS]

Hila yoyote ya Mabaniani isipofua dafu, walisisitiza kwamba serikali ifungue kesi ya jaribio la mauaji dhidi ya Hudhur[as]. Wapelelezi maarufu wa serikali walipewa jukumu la kuchunguza tukio hilo. Waislamu waheshimiwa wa Lahore na Amritsar walifanyiwa upekuzi. Tarehe 8 Aprili 1897, Le Marchand S.P. Gurdaspur na Mian Muhammad Bakhsh Deputy Inspector wa Batala pamoja na kundi la polisi wakapekua nyumba ya Hudhur[as] pia, lakini matokeo yake yakawa kwamba Hudhur[as] na Jumuiya yake hawahusiki na tukio hilo.

SHAURI JEMA KWA ANAYEMDHANIA HUDHUR[AS] KUWA MSHIRIKI KATIKA NJAMA YA UUAJI

Kwa vile magazeti ya Kiaria na viongozi wa Waaria walikuwa wakimwona Hudhur[as] kuwa amehusikana na uujai huo, kwa hiyo yeye alichapisha tangazo moja kwa kichwa cha habari "Mawazo ya

Waaria kuhusu kifo cha Lekhram", ambamo aliandika:

> "Kama hata sasa haiondoki shaka ya mwenye kushuku na ananifahamu kuwa mshiriki katika njama ya uuaji huo kama magazeti ya Mabaniani yalivyodhihirisha, basi nawapa shauri jema ambalo kwalo jambo hilo litakatwa hukumu. Nalo ni hili kwamba mtu kama huyo aape mbele yangu. Maneno ya kiapo yawe haya: "Najua kwa yakini kwamba mtu huyu (yaani Hudhur[as]) ni mshiriki katika njama ya uuaji, au kwa amri yake tukio la uuaji limetokea. Kama hiyo si sahihi, basi Ewe Mungu Mweza, katika mwaka moja uniteremshie adhabu ambayo iwe ya kutisha, lakini si kwa mikono ya mwanadamu, wala isiweze kufikiriwa humo njama ya mwanadamu. Basi kama mtu huyo (yaani mwapaji) katika mwaka mmoja alisalimika na dua yangu, hapo mimi ni mhalifu na ninastahili kupewa adhabu ile inayopaswa kwa mwuaji. Je, kama yupo sasa Mwaria yeyote shujaa, mjasiri ambaye aondoe shaka za dunia nzima, basi na afuate njia hii."[306]

UJASIRI WA GANGA BISHAN

Katika kukabili mwito wa Hudhur[as] wa kiapo hakuna aliyejasiri kuapa kiapo cha namna hii, lakini mtu mmoja miongoni mwa Waaria, Ganga Bishan, alimwandikia Hudhur[as] kwamba "Nipo tayari kuapa" kwa masharti matatu: La kwanza: Kama utabiri usitimie basi (Mungu Apishe mbali) Hudhur[as] apewe adhabu ya kunyongwa. La pili: Kwa ajili yake (yaani kwa Lala Ganga Bishan) rupia elfu kumi ziwekwe serikalini au katika banki ile atakayoiridhia na asipofariki kwa dua apewe rupia zile. La tatu: Wakati atakapofika Qadian kwa kiapo, itolewe dhamana kwamba asiuawe kama Lekhram.

Hudhur[as] akikubali masharti ya Lala Ganga Bishan aliandika kwamba Lala Ganga Bishan anapaswa aape kwa maneno yafuatayo:

> "Mimi fulani bin fulani, wa kabila fulani, mkazi wa mji fulani, wilaya fulani naapa kwa Mungu Mwenye shani au *Parmeshar*

[306] Tangazo la tarehe 15 Machi 1897

kwamba Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian ndiye muuaji wa Pandit Lekhram nami najua kwa yakini kamili kwamba lazima Lekhram aliuawa kwa njama na ushirikiano wa Ghulam Ahmad. Na kadhalika najua kwa yakini kamili kwamba utabiri ule haukuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, bali ilikuwa njama ya mwanadamu iliyotendeka kwa kisingizo cha utabiri. Kama kauli yangu hii si sahihi, basi Ee Mungu Mweza, kwa kudhihirisha ukweli wa mtu huyo Uonyeshe ishara yako hii kwamba katika mwaka mmoja unifishe kwa njia isiyokuwa njama ya mtu. Na kama nikifa katika mwaka mmoja, basi dunia nzima ikumbuke kwamba kifo changu kitakuwa ushahidi wa jambo hili kwamba kwa kweli hilo lilikuwa Neno la Mungu sio njama ya kibinadamu, na hii pia kwamba kwa hakika dini ya kweli ni Islam tu, na dini zingine zote kama vile dini ya Aria, Sanatan Dharm, Ukristo na kadhalika ni itikadi zilizoharibika."

Ilmuradi, kiapo cha madhumuni hiyo kichapishwe katika gazeti maarufu linaloaminika, na kiapo hicho hicho kitaapwa katika mkutano wa hadhara akija Qadian. Sasa kama mimi nikirudi nyuma kutimiza ahadi hiyo, basi laana ya Mungu iwe juu yangu, waila juu yako.

Sawa na ombi lako itakuwa ni wajibu juu yangu nikuwekee rupia elfu kumi, na sawa na ombi langu itakuwa ni wajibu juu yako kuchapisha ikrari kama hiyo bila kupunguza wala kuongeza kwa kiapo katika gazeti maarufu linaloaminika kama vile Akhbare Aam. Na kama nilivyokwisha kubali, nitakuwekea Rupia elfu kumi katika miezi miwili baada ya kuniwasilia ikrari yako hiyo iliyochapishwa. Kama nisiweke, nitahesabiwa kuwa mwongo.[307]

Hudhur[as] alipokubali masharti yote matatu ya Lala Ganga Bishan, na aliandika maneno ya kiapo pia, Lala Ganga Bishan aliongeza sharti moja lingine katika "Hamdarde Hind" la tarehe 12 Aprili. Nalo ni hili kwamba Hudhur[as] akionekana mwongo (Mungu Apishe mbali),

[307] Tangazo la 16 Aprili 1897 lililomo ndani ya ***Tablighe Risalat***, J. 6, kurasa 87,88

anyongwapo, mwili wake nipewe mimi (Lala Ganga Bishan). Kisha yeye afanye apendavyo na mwili huo: auchome, autupe mtoni au aufanyie chochote.

Kwa kujibu Hudhur[as] alisema:

> "Sharti hili pia nalikubali, na nionavyo mimi pia, mwili wa mwongo unapaswa kila aina ya dhila. Na kwa kweli sharti hilo lilikuwa muhimu sana alilokumbuka Lala Ganga Bishan kwa wakati mwafaka. Lakini sisi nasi tuna haki kwamba tuweke sharti hilo kwa ajili yetu pia… Nalo ni hili kwamba Ganga Bishan atakapofariki sawa na utabiri, mwili wake pia tupewe sisi ili mwili ule ubaki kwetu kama alama ya ushindi. Hatutapoteza mwili huo, bali tutauhifadhi kwa madawa, tutauweka hadharani kama alama ya ushindi au katika jumba la makumbusho la Lahore. Lakini kwa kupokea mwili, inapaswa kuwa na mpango mzuri tangu sasa. Basi hauonekani mpango bora zaidi kuliko huu kwamba rupia elfu hamsini au elfu sitini zilizokusanywa kwa kumbukumbu ya Pandit Lekhram, katika hizo, rupia elfu kumi ziwekwe katika banki ya serikali kama dhamana ya mwili, na katika hati za serikali iandikishwe kwamba Ganga Bishan akifa katika mwaka mmoja na tusipopewa mwili wake, basi badala yake kama bei ya mwili au faini ya kutokabidhi mwili, rupia elfu kumi tutapewa sisi, na nakala ya kibali cha namna hii kwa saini ya afisa wa hazina inapaswa nipewe mimi pia."[308]

Kwa kujibu sharti hili la Hudhur[as] Lala Ganga Bishan aliandika:

> "Mimi si mwanachama wa Aria Samaj, ili wanihurumie kiasi hiki na waniwekee rupia elfu kumi."[309]

Kwa kujibu Hudhur[as] aliandika:

> "Kumbukeni kwamba Ganga Bishan hana tatizo kabisa kuweka rupia elfu kumi, kwani kama hata Waaria pia wana maoni hayo

[308] Kutoka Tangazo la 16 Aprili 1897 lililoandikwa katika *Tablighe Risalat*, J. 6 uk. 91-92

[309] Kutoka tangazo la 27 Aprili 1897, *Tablighe Risalat*, J. 6

tu kwamba muuaji wa Lekhram kwa kweli ni mimi tu, na wana yakini kwamba ufunuo na maongezi na Mungu ni mambo ya uongo, bali kwa njama yangu uuaji ulitendeka, basi kwa shauku sana watamsaidia Lala Ganga Bishan, na sio tu elfu kumi, bali waweza kuweka hata elfu hamsini. Na waweza kupanga kwamba rupia elfu kumi zitakazochukuliwa kutoka kwangu zitumike katika kazi nzuri za Aria Samaj. Sasa Waaria wana shida gani kuweka rupia elfu kumi kama dhamana, bali hiyo ni biashara ya bure ambamo hakuna wasiwasi wa aina yoyote. Ndani yake kuna faida hii pia kwamba serikali itajua kwamba jambo hili limepangwa kwa ridhaa ya Waaria, na vile vile kwa ishara hii nzuri magomvi ya kila siku yatakwisha.

"Na kama ni hali hii kwamba waheshimiwa wa Waaria wanamwona Lala Ganga Bishan kuwa mwongo katika maoni haya kwamba mimi ndimi muuaji wa Lekhram,… basi nina haja gani nishindane na mtu ambaye kaumu yake mapema imeshamtambua kuwa mwongo."

Mwishowe Hudhur[as] aliandika:

"Kama Lala Ganga Bishan hakubali sharti letu hili, basi hatajibiwa tena kamwe, na kuhusu kumkabili yeye, tangazo letu hili ni la mwisho."[310]

Baada ya tangazo hili la Hudhur[as], Lala Ganga Bishan alinyamaza kabisa.

MWITO WA KIAPO KWA MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII

Waheshimiwa wasomaji watashangaa wakisikia kwamba Maulawii Muhammad Husain Batalawii wakati huu pia hakukosa kumpinga Hudhur[as]. Akaanza kutangaza kimaandishi na kwa mdomo kwamba utabiri haukutimia. Hapo Hudhur[as] akaandika:

"Kama Maulawii Muhammad Husain ana yakini kwa moyo wa

[310] Kutoka Tangazo la 27 Aprili 1897 lililoandikwa katika *Tablighe Risalat*, J. 6, uk. 101-102

kweli kwamba utabiri huu kuhusu Lekhram umebatilika, basi hahitaji kutaabika kuandika maneno ya upinzani. Nasema kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba kama yeye katika mkutano wa hadhara aape mbele yangu kwamba "utabiri huo haukuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu wala haukutimia, na kama ulikuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kwa kweli ulitimia, basi Ee Mungu Mweza, katika mwaka mmoja uniteremshie adhabu kali". Kisha kama Bwana Maulawii akisalimika na adhabu kali katika mwaka mmoja, mimi nitajiona mwongo na nitatubu kwa mkono wa Bwana Maulawii na vitabu nilivyo navyo kuhusu habari hii nitavichoma. Na kama aepe hata sasa, basi Waislamu waelewe wenyewe kwamba hali yake ni ya namna gani na imeishafika wapi."[311]

USHAHIDI MMOJA KUHUSU UUAJI WA LEKHRAM

Leo, siku ya Ijumaa, tarehe 12 Februari 1960, baada ya sala ya Alasiri katika Masjid Ahmadiyya nje ya 'Lango la Delhi', Lahore, Mheshimiwa Maulawii Muhibbur Rahman, mwana wa Hadhrat Munshi Mian Habibur Rahman Kapurthalwi, aliandika maneno haya kwa kalamu yake mbele ya ndugu wachache:

"Mimi Muhibbur Rahman naeleza kwamba karibu na mwaka 1909 mtu mmoja Pandit Gokul Chand, mwalimu mkuu wa Nadalon, Wilaya Hoshiarpur, aliniambia kwamba kabla hajauawa Pandit Lekhram, yeye alikuwa akisoma kwake Sanskriti. Katika siku zile Mwislamu mmoja akamjia aliyedhihirisha shauku ya kusoma Sanskriti na akaendelea kusoma kwa siku chache. Siku ya kuuawa, yeye Gokul Chand alikuwepo, na wakati wa kuuawa Lekhram alipochomwa kisu, akatamka "mama". Mama yake akaja haraka na kuona kwamba mwuaji akitembea pole pole kwa utulivu akaenda katika chumba kimoja. Mama wa Lekhram akasonga mbele na akafunga toka nje mlango wa chumba kile, na akamwambia

[311] Kutoka Tangazo la 11 Aprili 1897 lililoandikwa katika *Tablighe Risalat*, J. 6, uk. 81, maelezo ya pembeni.

polisi kwamba muuaji yupo katika chumba hiki. Wakati huo Mkuu wa polisi Mzungu alikuwepo. Polisi yeyote asipokuwa tayari kuenda chumbani, hapo Mkuu wa polisi mwenyewe aliingia ndani akishika bastola katika mkono mmoja na taa katika mkono mwingine. (kwani mlikuwa na giza chumbani) Alichunguza chumba kizima kwa taa na kasema hayumo yeyote humu. Mama yake Lekhram alisisitiza kwamba muuaji yumo mumu humu. Hapo Mkuu wa Polisi akasema kwamba kama ametoka akigeuka kuwa nzi, yawezekana, waila hakuna nafasi kwa mwanadamu kutoka humu. Tukio hili Pandit Gokul Chand alieleza kwa kiapo na mimi pia naeleza kwa kiapo."

Mwandishi: Muhibbur Rahman 12.02.1960

Shahidi: Dkt. Ubaidullah Khan Batalawii.

Shahidi: Master Muhammad Ibrahim, Mwenyekiti wa Jumuiya ya 'Lango la Delhi.'

Tanbihi: Kuhusu tukio hilo kauli zilizoenea, Bwana Maulawii alieleza kuhusu hizo kwamba Pandit Gokul Chand alikuwa akisema kwamba Waaria walitayarisha kauli zile kwa msaada wa mawakili wao, waila ukweli ni ule tu nilioeleza. *Mungu Ajuaye yaliyo sahihi*. Mimi Abdul Qadir 12. 2. 1960

FAIDA MOJA YA KISIASA YA UUAJI HUO

Waislamu walipata faida hii ya kisiasa kwa uuaji huo kwamba katika zama hizo maduka ya maziwa, mtindi na tamutamu yalikuwa ya Mabaniani tu. Kwa sababu ya tukio hilo Mabaniani wenye maduka waliwapa baadhi ya watoto Waislamu tamutamu kwa kutia sumu ndani yake, hapo Waislamu wakazinduka na wakaanza kufungua maduka yao ya maziwa, mtindi na tamutamu.

TUKIO LA GHERA YA DINI YA HUDHUR[AS]

Habari za Pandit Lekhram zaendelea kutajwa. Hapa lapaswa tukio moja kuhusu Pandit Lekhram liandikwe linalodhihirisha ghera ya dini ya Hudhur[as]. Hadhrat Sheikh Yakub Ali Irfani[ra] anaandika:

"Safari moja, Hudhur[as] alikuwa akija Qadian kutoka Ferozpur...

Nilikuwa naye mpaka Raewind. Hapo aliniambia kwa hisani yake kwamba wewe si mtu wa kuajiriwa, kwa hiyo endelea mpaka Lahore. Ulikuwa ni wakati wa sala ya alasiri, Hudhur[as] alijiandaa kusali. Siku hizo kule kulikuwepo na jukwaa lakini siku hizi kuna platfomu pale. Nilikwenda kwenye platfomu, huko Pandit Lekhram Aria Musafir, aliyekuwa akiandika siku zile maisha ya Pandit Dayanand, alikuwa tayari aondoke kwenda Jalandhar, kwani alikuwa pengine akifanya kazi pale. Akaniuliza, umetokea wapi? Nilipomjulisha kuhusu ujaji wa Hudhur[as], sielewi akafikiri nini akapakimbilia pale Hudhur[as] alipokuwa kitawadha (kana kwamba hata hivi sasa mandhari ile naiona. — Irfani). Yeye alimsalimia Hudhur[as] kwa mtindo wa Waaria kwa adabu. Hudhur[as] akiinua kichwa kaona kidogo, akaendelea kutawadha. Yeye alidhani kwamba labda Hudhur[as] hajasikia, kwa hiyo akamsalimia tena, lakini Hudhur[as] akaendelea kushughulikia kutawadha. Yeye alisubiri kidogo na akaondoka. Mtu fulani baadaye alimwambia Hudhur[as] kwamba Lekhram alikusalimia. Akasema kwamba yeye amemfedhehesha sana Mtume Mtukufu[saw], ni kinyume cha imani yangu kwamba nipokee salamu yake. Anamshambulia Mtume[saw] na amekuja kunisalimia."

Allah, Allah! Hudhur[as] alikuwa na ghera kiasi gani kwa ajili ya Mtume Mtukufu[saw]. Kiongozi mheshimiwa wa dini nyingine ambaye alikuwa anamfedhehesha Mtume[saw], Hudhur[as] hakupenda kupokea salamu yake. *Allahumma Salli alaa Muhammadin wa aali Muhammad wa Khulafaai Muhammad wa barik wa sallim.*

KUZALIWA KWA HADHRAT MUBARAKA BEGAM, 2 MACHI 1897, SAWA NA 27 RAMADHAN 1314 HIJRIA

Tarehe 2 Machi 1897, sawa na bishara ya Mungu, alizaliwa kwake Hadhrat Mubaraka Begam. Kabla ya kuzaliwa kwake Hudhur[as] alifunuliwa: [312]تُنَشَّأُ فِي الْحِلْيَةِ yaani atakulia katika mapambo. Ilimaanisha kwamba hataona zama za dhiki wala hatafariki katika umri mdogo.

[312] Haqiqatul Wahyi, uk. 217

Basi, matukio ya baadaye yalionyesha kwamba utabiri wa Hudhur[as] ulitimia neno kwa neno. Yeye aliolewa na Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan aliyekuwa na mali nyingi zisizohamishika na alikuwa mheshimiwa Chifu aliyehusikana na familia ya kifalme ya jimbo la Maler Kotla.

UJAJI WA HUSAIN KAMI, BALOZI WA UTURUKI, KATIKA QADIAN, 10-11 MEI 1897

Mwanzoni mwa Mei 1897, balozi wa Uturuki, Husain Bik Kami, aliyewekwa Karachi, akaja Lahore, na alimwandikia Hudhur[as] kwa adabu sana akiomba nafasi ya kumwona. Hudhur[as] hakutaka kumpa nafasi ya kuonana naye, kwani Mwenyezi Mungu Alikwishamwambia mapema kwamba "mtu huyu ana tabia ya unafiki",[313] lakini kwa kufikiria kwamba balozi asivunjike moyo akamruhusu. Tarehe 10 au 11 Mei 1897, balozi alifika Qadian na aliomba kumwona Hudhur[as] faraghani. Hudhur[as] hakutaka kumpa nafasi hiyo, kwani alikuwa na alama za kupenda dunia tu, lakini kwa sababu ya huluka njema alimruhusu. Katika kikao hicho yeye "aliomba kwamba Sultan wa Roma aombewe dua maalumu. Na pia alitaka kujua yatakayotokea kwake toka kwa kudra za kimbingu."

Hudhur[as] alimwambia waziwazi kwamba "hali ya ufalme wa Sultan si nzuri, na kwa njia ya kashfi sioni hali ya mawaziri wake kuwa njema. Nionavyo mimi, mwisho pamoja na hali hizo si mwema."

Balozi aliona vibaya sana maneno hayo ya Hudhur[as]. Yeye aliporudi Lahore alimwandikia barua mhariri wa *Nadhimul Hind* ambamo alipayuka sana dhidi ya Hudhur[as]. Mhariri alichapa barua ile. Hapo Hudhur[as] aliwaelezea watu habari sahihi kupitia kipeperushi.[314]

KUFICHULIWA AIBU YA BALOZI WA UTURUKI

Baada ya tukio hilo, hali fulani zilizuka, na mwaka huo huo, yaani mwaka 1897, vita ikaanza baina ya Ugiriki na Uturuki. Waislamu wa India wakachanga fedha kwa kuwasaidia Waturuki na kumkabidhi

[313] Tangazo la 24 Mei 1897

[314] Kwa maelezo zaidi someni *Tiryaqul Qulub* uk. 121.

balozi wa Uturuki, Husain Kami, ambazo yeye hakuzitia katika hazina ya serikali ya Uturuki. Hapo jinsi alivyofedheheka inadhihirika katika muhtasari wa barua ya Constantinople (Istanbul) ya kwamba habari hii ilipomfikia Bwana Salim Pasha Malhama, mwanakamati wa mchango, yeye kwa juhudi kubwa alijaribu kufanya atoe rupia hizo. Yeye aliuza ardhi yake kwa mnada wa hadhara na akapata fedha hizo, na akafikisha habari za wizi wa amana kwa korti ya Khalifa wa Uturuki na akafukuzwa kazini.[315]

TOBA YA MZEE WA GAZETI CHAUDAWIN SADII

Balozi wa Uturuki, Husain Bik Kami, ameshatajwa juu. Yeye aliporudi Lahore kutoka Qadian akishindwa, akamwandikia mhariri wa gazeti la "Nadhimul Hind", Lahore, barua chafu yenye maneno kinyume cha ustaarabu na utu, iliyochapwa katika gazeti hilo katika toleo la 15 Mei 1897. Kwa sababu ya balozi Mwislamu mgeni, magazeti yaliitilia umuhimu sana barua ile. Katika zama hizo lilikuwa linatolewa gazeti moja liitwalo "Chaudawin Sadii" mjini Rawalpindi, gazeti hilo liliandika katika toleo moja kwamba mzee fulani aliposoma barua hiyo mara alitamka ubeti huu:

Mungu Anapotaka kufichua siri za mtu,
Anamwelekeza kuwapinga watu wema.

Toleo hilo la gazeti "Chaudawin Sadii" liliposomwa mbele ya Hudhur[as] katika Qadian, roho ya Hudhur[as] ilipata msisimko fulani kuhusu mzee yule. Alijaribu sana kuuondolea mbali kutoka rohoni mwake, lakini ikashindikana. Hapo, yeye alimwomba Mwenyezi Mungu kuhusu mzee yule kwamba Ee Mungu wangu, kama Ukijua kwamba nimetumwa na wewe, na ni Masihi Mau'udi, Utoboe siri za yule aliyetajwa kwa jina la 'mzee' katika gazeti hili. Lakini kama akija Qadian katika muda huo na kutubu hadharani, basi Umsamehe, kwani U Rahimu na Mkarimu. Na kwa ajili ya yeye kuomba msamaha aliweka muda wa mwaka mmoja kuanzia 25 Juni 1897 mpaka tarehe mosi Julai 1898, na akachapisha habari hizi zote katika tangazo la 25 Juni 1897. Tangazo hilo la Hudhur[as] lilipomfikia mzee yule, yeye

[315] Gazeti "Nayyire Aasfi", Madras, la 12 Oktoba 1899.

akahangaika sana, na baadhi ya alama pia zilitokea ambazo kwa sababu ya hizo ikaelekea kuwa siri zake zitatobolewa sana. Kwa kuangalia mambo hayo yote aliandika barua ya kuomba msamaha. Na pia akaandika kuwa anastahiki kusamehewa kuhudhuria wakati huu kwa baadhi ya sababu. Labda nitahudhuria kabla ya Julai 1898.

Hudhur[as] aliandika kujibu barua hiyo:

"Mwenyezi Mungu Asamehe kosa la mzee huyo na Awe radhi naye, nimemridhia na ninamsamehe."[316]

MAHUBIRI KWA MFALME WA AFGHANISTAN:

Katika mwaka huo, Hudhur[as] alimtumia barua ya mahubiri Mfalme wa Afghanistan, Amir Abdur Rahman Khan, pia kumpitia mfuasi wake, jina lake pia Abdur Rahman. Kwa vile masheikh walikuwa na nguvu katika nchi ile, kwa hiyo pengine barua ile haikuweza kumfikia Amir Abdur Rahman, na sawa na fatuwa ya masheikh mjumbe wa Hudhur[as], Abdur Rahman Khan, aliuawa. *Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun.*

AMIN YA MAHMUD, 7 JUNI 1897

Kwa vile Hudhur[as] alikuwa na mapenzi sana ya Kurani Tukufu, na alikuwa na shauku sana ya kuifundisha na kuitangaza, kwa hiyo Hadhrat Mirza Bashirud Din Mahmud Ahmad *(Imam Jamaat Ahmadiyya, Mungu Atufaidishe na urefu wa umri wake)* alipohitimu Kurani Tukufu, Hudhur[as] alifurahi sana, na akataka kufanya kikao kuhusu jambo hili: Akawaalika wafuasi wa nje ya Qadian pia. Akaandika shairi moja pia kwa ajili ya hafla hiyo inayojulikana kwa jina la "Amin ya Mahmud" na imo katika Durre Thamin ya Kiurdu. Beti nne tu za shairi hilo zinaandikwa hapa chini:

> Ee Mola, ni hisani Yako, nijitolee kizingitini pako, Umetupatia imani. U Mlinzi wakati wote.
>
> Ukarimu wako twaupata kila saa, U Mwingi wa rehema na Mwengi wa ukarimu, Ubariki siku hii. Namtukuza Yule

[316] Kutoka katika Tangazo la 20 Novemba 1897, lililoandikwa katika *Tablighe Risalat*, J. 6 uk. 178-179.

Anayeniona.

Wewe umetuonyesha siku hii ambapo Mahmud amekuja akiishahitimu. Kwa kuona hisani hii, moyo ukaimba kwa kukusifu:

Nakushukuru mara mia Ee Mungu, nakushukuru mara mia Ee Mungu. Ubariki siku hii. Namtukuza Yule Anayeniona.

SHEREHE YA JUBILII YA MIAKA SITINI YA MALKIA VICTORIA, 19 JUNI 1897

Mnamo 19 Juni 1897, ilisherehekewa katika Uingereza na India Jubilii ya miaka sitini ya Muadhama Malkia Victoria. Wakati ule Hudhur[as] aliandika kijitabu kiitwacho *Tuhfa Kaisaria* ambamo alieleza kuwa Hadhrat Masihi[as] alikuwa mja wa Mwenyezi Mungu na mtume mkweli. Na akabainisha kuwa dini ya Kikristo ya siku hizi ni batili, na Islam ndiyo dini sahihi, na akamkaribisha Muadhamu Malkia kwenye Islam. Nakala nyingi za kitabu hicho ziligawanywa bure, na zilitumwa pia kwa Muadhamu Malkia, Viceroy wa India na Luteni Govana wa Panjab.

OMBI KWA MASHEIKH NA WATU WEMA KWA KUAPISHA KIAPO CHA MUNGU MWENYE SHANI, 15 JULAI 1897

Mtukufu Hudhur[as] alitoa pendekezo moja kwa kuwatimizia hoja masheikh, watu wema na waja wa Mungu, ambalo ni hili:

"Nawaapisha masheikh, madarweshi na watu wema wote wa Panjab na India, kiapo cha Allah Mwenye shani, Ambaye kujitoa muhanga kwa jina lake ni kazi ya wakweli wenye dini, kwamba wamuombe Allah kuhusiana nami kwa uchache kwa siku 21, yaani kama isijulikane kabla ya siku 21, na wautake uhakika huu kutoka kwa Mungu kwamba mimi ni nani? Ni mwongo au nimetoka kwa Mungu? Nawaomba tena na tena wazee wa dini kwa kuwaapisha kwa kiapo cha Allah Mwenye shani, kwamba lazima waendelee kuomba kwa siku 21 kama haibainiki mapema, kwa ajili ya kuondoa mifarakano hii. Najua kwa yakini kwamba baada ya kusikiliza kiapo hicho cha Mwenyezi Mungu kisha kutojali si kazi ya wakweli. Na ninajua

kwamba baada ya kusikiliza kiapo hicho, kila mwenye moyo safi, aichaye adhama ya Mwenyezi Mungu, ni lazima ataelekea. Kisha baada ya kukusanywa mashuhuda kama hayo ya kiufunuo, ule upande utakaokuwa na mashuhuda mengi, utafahamika kuwa ndio kutoka kwa Mungu.

"Kwa pendekezo hili watu wa Mungu watafaidika sana, inshallah, na mioyo ya Waislamu, kwa sababu ya mashuhuda mengi, ikipata kutulia kwa upande mmoja, watasalimika na fitina. Na katika Hadithi za Mtume[saw] pia inaonekana hivi kwamba kwanza Mahdi wa zama za mwisho atakufurishwa na watu watakuwa maadui zake na watamtusi sana, na hatimaye waja wa Mwenyezi Mungu wataambiwa kwa ruya na ufunuo na kadhalika kuhusu ukweli wake. Na ishara zingine za kimbingu pia zitadhihiri. Ndipo masheikh wa wakati ule watamkubali watake wasitake. Basi, Enyi wapendwa na wazee, elekeeni kwa Mungu Aliye Mjuzi wa ghaibu. Nawaapisheni kwa Allah Mwenye shani kwamba itikieni ombi langu. Nawaapisheni kwa Mweza Mwenye ujalali kwamba msilikatae ombi langu hili."

(Kutoka katika Tangazo la 29 Julai 1897)

UPANUZI WA MASJID MUBARAK

Msikiti Mubarak ulikuwa mdogo sana. Katika safu yake moja kwa shida watu 6 tu waliweza kusimama, na watu 30-32 katika sehemu nzima kwa jumla. Kwa sababu ya watu kuwa wengi, baadhi ya wakati "Baitul Fikr" pia ilitumika kama msikiti. Uga wa Masharaki pia baadhi ya wakati ulikuwa ukitumika. Hapo Hudhur[as] alipata fikara ya kupanua msikiti. Basi, Hudhur[as] kupitia tangazo aliwaelekeza ndugu kutoa mchango. Wenye ikhlasi walichanga kwa moyo mkunjufu na baadaye msikiti ukapanuliwa mnamo mwaka 1907.

(Someni Tangazo la 29 Julai 1897)

MLANGO WA NNE

KUANZIA KESI YA KUJARIBU KUUA HADI KUDHIHIRIKA TAUNI

PADRE DKT. HENRY MARTIN CLARK KAMSHTAKI HUDHUR KWA KUJARIBU KUMWUA, 1 AGOSTI 1897.

Kusudio moja muhimu kati ya makusudio ya kutumwa kwa Hudhur[as] lilikuwa kuvunja msalaba, na alikuwa hakosi nafasi yoyote ya kulitekeleza. Katika mwaka 1893, huko Amritsar alifanya mjadala maarufu na Deputy Abdullah Atham, unaojulikana kwa jina la Vita Takatifu. Katika mjadala huo Dkt. Henry Martin Clark pia alishiriki. Baada ya mjadala huo alipofariki Abdullah Atham baada ya kujifaidisha na sharti ya kurejea, ndipo mapadre waliudhika sana, na hususan Dkt. Henry Martin Clark alihuzunika na kughadhibika zaidi kuliko wote. Yeye alikuwa anatafuta nafasi yoyote ili Hudhur[as] apate kudhurika. Basi alipouawa kiongozi maarufu wa Waaria Pandit Lekhram, hao walichemka sana. Vilevile Dkt. Clark pia alipata nafasi, na hao wote wakajumuika kumdhuru Hudhur[as].

FITINA YA ABDUL HAMID

Hadhrat Maulawii Ghazi Burhanud Din Jhelumii alikuwa na mpwa mmoja mzururaji aitwaye Abdul Hamid. Hakuhusika na dini lakini kwa kujifaidisha alikuwa akibadilisha badilisha dini yake. Kwa bahati tu katika mwaka 1897 alifika Qadian. Alijaribu kufanya baiati, lakini hakuweza kufanikiwa. Hudhur[as] hakupenda, kwa sababu ya nuru ya busara yake, kwamba yeye akae Qadian, kwa hiyo alifukuzwa katika Qadian. Basi, kutoka Qadian alienda moja kwa moja Amritsar. Kwanza alimfikia padre H.G. Gray, lakini yeye akimwona ni mzururaji, hakumpokea. Kisha akamwenda Dkt. Henry Martin Clark. Bwana Dkt. kwa kujua kwamba amekuja moja kwa moja Amritsar kutoka Qadian, aliona ni afadhali amekuja, na aliongea na mapadre wazalendo waliokuwa chini yake kwa kutekeleza njama aliyofikiria

moyoni mwake. Na akamtayarisha Abdul Hamid kwa kumpa tamaa na kumtisha kwamba aende naye mahakamani na kutoa taarifa kwamba (Hadhrat) Mirza Ghulam Ahmad Qadiani amenituma niende Amritsar ili nimwue Dkt. Martin Clark kwa kumpiga jiwe. Abdul Hamid akawa tayari. Bwana padre alienda naye katika mahakama ya Disii wa Amritsar, Bwana A. E. Martino. Abdul Hamid aliandikiksha taarifa yake sawa na matakwa ya Dkt. Henry Martin Clark, na baada yake Bwana Dkt. aliandikisha taarifa yake mwenyewe. Baada ya kupata taarifa za wote wawili, Disii wa Amritsar alituma tarehe mosi Agosti 1897 waranti ya kumkamata Hudhur[as], pamoja na amri ya kutoa dhamana ya rupia 40,000 na bondi ya rupia 20,000. Lakini ni kudra ya Mwenyezi Mungu ya kwamba hata kwa kupita siku kadha waranti ile haikuweza kufika Gurdaspur, isijulikane ikapotea wapi. Upande wa pili, Wakristo na Masheikh wapinzani kila siku walikuwa wakija kwenye stesheni ya garimoshi ya Amritsar kwa kumwona Bwana Mirza akitiwa pingu ya mkono atashuka kutoka gari katika ulinzi wa polisi.

Baada ya wiki moja, yaani tarehe 7 Agosti 1897, Hakimu wa Wilaya aligundua kosa lake kwamba yeye hana madaraka ya kutuma waranti ya kumkamata mkazi wa wilaya nyingine. Hapo alimtumia telegramu Hakimu wa Wilaya ya Gurdaspur kwamba asifuatilie waranti ile niliyotuma tarehe mosi Agosti 1897. Hapo, Hakimu wa Wilaya ya Gurdaspur na maafisa wengine wa Wilaya walishangaa sana kwamba lini waranti ile ilifika ambayo isifuatiliwe. Hatimaye telegramu hiyo ikatiwa tu katika faili. Baadaye faili ya kesi hiyo ilifika kwa Disii wa Gurdaspur. Mwenyezi Mungu Alitia moyoni mwa Disii wa Gurdaspur kwamba kesi hiyo ina mashaka. Hapo juu ya kung'ang'ania na kutia juhudi ya Dkt. Henry Martin Clark na wakili wake, Disii badala ya kutuma waranti ya kumkamata, alimtumia samansi ambamo alisisitiza kufika Batala tarehe 10 Agosti 1897. Hudhur[as] alienda Batala tarehe iliyowekwa, na mbele yake Dkt. Martin Clark alitoa taarifa yake. Katika taarifa yake hakusema jambo lolote jipya, bali alirudia taarifa ile ile aliyotoa mbele ya Disii wa

Amritsar. Tarehe 12 na 13 Agosti pia Bwana Dkt. Akatoa maelezo.[317]

MAELEZO YA ABDUL HAMID

Siku hiyo hiyo Abdul Hamid pia alieleza taarifa yake. Yeye pia alirudia kauli yake ile ile ya Amritsar, lakini safari hii katika taarifa yake kulikuwa na maelezo zaidi. Baada ya kutoa maelezo yake alisema, akiongozwa na Wakristo, kwamba nahofia kuhusu uhai wangu, kwa hiyo niruhusiwe kukaa na Dkt. Henry Clark.

USHAHIDI WA MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN BATALA-WII

Katika kesi hiyo Maulawii Muhammad Husain Batalawii alikuwa shahidi kutoka kwa upande wa Wakristo. Alipokuja kwa kutoa ushahidi katika mahakama ya Disii, yeye alikuwa anafikiria moyoni mwake kwamba atakapofika mahakamani atamwona Hudhur[as] katika hali ya kukamatwa, lakini alipofika mahakamani akamwona Hudhur[as] amekaa kitini. Hapo, yeye alimwomba Disii kuwa yeye naye apatiwe kiti. Bwana Mkubwa alisema kwamba huwezi kupata kiti mahakamani. Lakini Bwana Maulawii akang'ang'ania na akasema kwamba mie pia napewa kiti mahakamani na baba yangu pia. Kwa kusikia hayo, Bwana Mkubwa akakasirika na kasema, 'U mwongo, hupati kiti, wala baba yako Rahim Bakhsh alikuwa hapati.' Hapo, Maulawii Muhammad Husain alisema kwamba ninazo barua kwamba Gavana ananipa kiti. Kusikia hayo Disii akaghadhibika sana na akasema, "Usipayuke, rudi nyuma na simama wima."[318] Ushahidi ulimalizika. Maulawii Muhammad Husain alimsuta Hudhur kadri alivyoweza. Lakini kwa kumjibu, njia ya Hudhur[as] ilikuwa hivi kwamba wakili wake Maulawii Fadhl Din alipotaka kumwuliza Maulawii Muhammad Husain swali ambalo lingetia doa katika nasaba yake na mienendo yake, mara Hudhur[as] akainuka kitini mwake na

[317] Maelezo hayo yote yapo katika "*Kitabul Bariyya*", cha Hudhur[as].

[318] Bwana mkubwa alimwambia Maualwii kusimama wima kwa sababu kati yake na kati ya Bwana Maulawii ilikuwepo feni inayovutwa kwa mkono na kwa sababau hiyo Bwana Maulawii akalazimika kuinama kwa kuona uso wa Bwana mkubwa. (Mwandishi)

akinyosha mkono wake kwenye mdomo wa Maulawii Fadhl Din, akasema kwamba sikuruhusu kuuliza swali kama hili... Akiona hulka duni ya Maulawii Muhammad Husain na hulka bora na moyo mkubwa wa Hudhur[as], Disii aligundua kwamba Bwana Maulawii ni adui wa Bwana Mirza. Kwa hiyo, maneno yake ni mabovu na hayaaminiki. Hivyo, yeye katika uamuzi wake hata hakutaja maelezo ya Bwana Maulawii.

Baada ya kutoa ushahidi Bwana Maulawii alipotoka nje ya chumba cha mahakama, kwa kuficha alivyotendewa ndani aliketi juu ya kiti kilichokuwepo katika chumba cha nje. Kwa kuwa watumishi wa mahakama walishajua kwamba mtu huyu hakupewa kiti ndani, kwa hiyo walimwondoa Bwana Maulawii kitini. Kisha Bwana Maulawii alienda kwenye chumba cha polisi, kwa bahati kulikuwepo na kiti katika chumba cha nje, yeye akajikalia juu yake. Alipokaa tu, mkuu wa polisi akapata kumwona. Yeye papo hapo akamtuma polisi na kumwondoa Bwana Maulawii kitini. Mamia ya watu walishuhudia fedheha ya Bw. Maulawii na wakapata yakini kwamba sababu ya feheha hiyo ni ushahidi ule aliotoa Bw. Maulawii kwa kumsaidia padre katika kesi ya uogno. Baada yake, Bwana Maulawii akaja nje katika kiwanja cha mahakama, kachukua shuka ya mtu, kaitandika na kujikalia juu yake. Yule mwenye shuka alivuta shuka kutoka chini ya Bwana Maulwii akisema, "Ukiwa Mwislamu, tena kuitwa kiongozi, kisha kusema uongo hivyo!!"[319]

UWAKILI WA WAKILI MWARIA PANDIT RAM BHAJDAT

Tumeshataja juu kwamba katika kesi hiyo Waaria pia waliwasaidia Wakristo kwa sababu ya Lekhram kuuawa. Basi, katika kesi hiyo kutoka kwa Wakristo, Pandit Ram Bhajdat, wakili wa Kiaria, pia alifuatilia. Alipoulizwa umekujaje, akasema wazi wazi, "Sikuchukua malipo yoyote, nimeshiriki tu, huenda nikapata dokezo kuhusu uuaji wa Pandit Lekhram pia.[320]

[319] Kwa maelezo yote someni *Kitabul Bariyya*.

[320] *Hayate Ahmad,* J. 4, uk. 602

MUNGU KATAWALA MOYO WA KAPTENI DOUGLAS

Raja Ghulam Haidar, karani wa Kapteni Douglas Disii, anasimulia kwamba tarehe 13 Agosti katika Batala zilipoisha shughuli za siku hiyo za kesi na tulipofika kwenye stesheni ya Batala ili kwenda Gurdaspur, gari likachelewa. Bwana Disii akawa akitembea kwenye platfomu kutoka kona moja hadi kona ya pili katika hali ya kutotulia. Kwa kuona hali yake hiyo nikajasiri kumwuliza kwamba unaonekana na wasiwasi wakati huu. Kuna sababu gani? Bwana mkubwa akajibu kwamba "Ninahangaika sana kwa kesi hiyo. Popote niangaliapo namwona Bwana Mirza Sahib, naye anasema usiachane na uadilifu ulio sifa ya taifa lenu." Isitoshe, naona alama za uadui na uhasama katika shtaka hilo. Siwezi kufahamu nifanyeje, hata kwamba udhihirike wazi uhakika ulivyo." Nikamshauri kwamba ukimtenganisha Abdul Hamid na Wakristo, na kumkabidhi polisi, hapo uhakika unaweza kujulikana. Bwana Mkubwa mara moja kaenda katika afisi ya reli, akamwandikia mkuu wa polisi baadhi ya maagizo, kisha tukaenda Gurdaspur.

Baada siku chache, yaani asubuhi ya tarehe ishirini, mfanyakazi wa mahakama alifika kuniita. Nilipoenda, nikajua kwamba Bwana Lee Marchand, Kapteni wa polisi, ameleta kwa kuandika maelezo kwa kirefu ya Abdul Hamid, na Disii alitakiwa kuyasadikisha. Mbele ya Kapteni wa polisi, kwanza Abdul Hamid alirudia kisa kile kile cha uongo alichoeleza awali. Lakini Bwana Kapteni alipomwambia, usipoteze wakati wetu, twataka kujua uhakika tu ulivyo, ndipo yeye akamwangukia miguuni pa Bwana Kapteni na akaanza kulia sana na kasema kwamba kauli yangu ya awali ilikuwa ya uongo mtupu, na Dkt. Martin Clark na mapadre wenzake wakinitisha na kunipa tamaa walinifanya kutoa kauli ile. Niliposahau jambo fulani wakaliandika juu ya mkono wangu kwa penseli, ili kuweza kueleza nikiona wakati ule. Ilmuradi, ukweli ni huu kwamba Bwana Mirza hakunituma kamwe kumwua Bwana daktari. Kisa chenyewe hiki ni cha uongo, na nilieleza mambo hayo yote kwa hofu na tamaa. Baada yake alieleza kauli yake sahihi ambayo Bwana Kapteni wa polisi mbele yake akamwambia Disii kuyasadikisha.

Jambo hili hasa lapaswa kutajwa kwamba Wakristo walipojua kwamba Abdul Hamid amekiacha kisa chake cha zamani cha uongo na ameshatoa kauli sahihi, walipata wasiwasi sana. Wakamtuma kwake mtu mmoja, Abdul Ghani, aliyemwambia, "Andikisha kauli yako sawa na kauli yako ya awali, waila utafungwa." Abdul Hamid alimwambia Kapteni wa polisi jambo hili pia.[321]

UAMUZI WA KESI, 23 AGOSTI 1897

Bwana Disii alipanga 23 Agosti 1897 kutoa uamuzi wa kesi. Masheikh wapinzani, mapandit na mapadre walikuwa na yakini kwamba kwa kuwa kesi hiyo inahusikana na padre mkubwa Dkt. Henry Martin Clark, kwa hiyo Bwana Mirza atapewa adhabu kali. Lakini walipoona kwamba Bwana Disii amemwachilia Hudhur[as] moja kwa moja, wakageuka rangi nyuso zao, na hawakuweza kukawia mahakamani.

UJASIRI WA KIHULKA WA KAPTENI DOUGLAS

Wasomaji hawapaswi kusahau kamwe kwamba Masihi[as] wa kwanza pia alishtakiwa kwa njama ya Wayahudi, lakini hakimu aliyekuwa wakati wa Masihi wa kwanza, yaani Pilato, ingawa alijua kwamba Hadhrat Masihi hana kosa, lakini aliwaogopa Wayahudi na kinyume cha dhamira yake alihukumu kumtundika Hadhrat Masihi msalabani. Lakini hakimu huyu ameonyesha ujasiri wa kihulka kiasi hiki kwamba akaangalia uadilifu na hakumpendelea padre wa dini yake, Dkt. Henry Martin Clark, wala hakuwajali masheikh wa Kiislamu na Waaria, bali akifuatilia matakwa ya uadilifu alimwachilia Hudhur[as] kwamba hana hatia. Na hivyo akawa mtu mwenye heshima wa kihistoria katika ulimwengu wa Kiahmadiyya. Naam, hakimu wa wilaya alisema hii pia kwamba "Waweza kuwashtaki hao Wakristo." Jawabu Hudhur[as] alilomtolea hakimu wa wilaya linapaswa kuandikwa kwa herufi kubwa, yaani akasema, "Kesi yetu dhidi ya Wakristo yaendelea huko mbinguni. Yatutosha mahakama ya kimbingu, hatutaki kuendesha kesi yoyote katika mahakama za dunia."

[321] Someni kauli ya mkuu wa polisi iliyoandikwa katika *Kitabul Bariyya,* uk. 238-239

KAULI YA FADHLUDDIN WAKILI WA MAHAKAMA KUU YA PANJAB, KUHUSU HULKA YA HALI YA JUU YA HUDHUR[AS]

Madhumuni yanaendelea kurefuka, nahofia isije yakawachosha wasomaji, lakini nalazimika kwa tabia yangu ya asili kwamba matukio yanayodhihirisha hulka ya hali ya juu na shani kubwa ya Hudhur[as], lazima niyaweke mbele ya wasomaji.

Lala Dina Nath, mhariri wa gazeti la "Hindustan Wadesh", alimwelezea Hadhrat Sheikh Yakub Ali Turab, mhariri wa gazeti la Al-Hakam, kwamba:

> "Namtambua Bwana Mirza kuwa mtu mkubwa, mja wa kiroho wa daraja kubwa... Nikawa na itikadi hii kwa sababu ya tukio moja. Watu wengi walikuwa wakijumuika jioni kwenye nyumba ya Hakim Ghulam Nabii, ***zubdatul hukamaa*** ─ hii ni hati ya uganga mkubwa ─ mimi pia nilikuwa nikienda huko. Siku moja watu kadha walipokuwa wamejumuika huko, Bwana Mirza akapata kutajwa. Mtu mmoja alianza kumpinga lakini kwa njia iliyokuwa kinyume cha uungwana na hulka njema. Kusikia hayo, marehemu Fadhulddin akashikwa na harara na akasema kwa jazba kubwa kwamba mimi si mfuasi wa Bwana Mirza wala siamini madai yake, achilia mbali sababu yake, lakini naamini kwamba Bwana Mirza ni mtu mwenye shani kubwa na mwenye khulka kamilifu. Mimi ni wakili, na watu wa kila tabaka wananifikia kwa kesi zao. Watu wema sana ambao hawawezi kudhaniwa kwamba watajionyesha visivyo kwa njia yoyote, hao katika kesi waliposhauriwa kubadilisha kauli zao, walibadilisha bila kusita. Lakini katika maisha yangu yote nimemwona Bwana Mirza pekee asiyeachana na kusema ukweli hata kidogo. Mimi nilikuwa wakili wake katika kesi moja. Katika kesi hiyo niliandika kwa ajili yake taarifa ya kisheria na kuweka mbele yake. Baada ya kuisoma akasema kwamba ndani yake kuna uongo. Nikasema kwamba mshtakiwa hatoi kauli yake kwa kuapa, na kisheria anayo ruhusa ya kueleza atakavyo. Hapo, yeye akasema, "Sheria imemruhusu kwamba aeleze atakavyo, lakini Mwenyezi Mungu hakuruhusu kwamba aseme uongo,

wala sheria haimaanishi hivyo. Basi sipo tayari kutoa kauli iliyo kinyume cha matukio, nitaeleza ukweli mtupu." Bwana Maulawii wakili akasema, "Unajiingiza mwenyewe katika balaa." Hudhur[as] akajibu, "Kujiingiza katika balaa ni kwamba kwa kutoa kauli ya kisheria kwa kujifaidisha nimkasirishe Mungu wangu; siwezi kufanya hivyo hata itokee nini". Bwana Fadhluddin anasema kwamba Bwana Mirza alieleza mambo hayo kwa jazba kubwa hata kwamba ulionekana usoni mwake utukufu na jazba ya aina maalumu. Baada ya kusikia hayo nikamwambia kwamba basi huwezi kufaidika na uwakili wangu hata kidogo. Hapo yeye akasema: Mimi sikuwaza kamwe kwamba uwakili wako utanifaa nitanufaika na juhudi ya mtu mwingine yeyote awaye, wala sifahamu kwamba upinzani wa mtu yeyote unaweza kuniangamiza. Tegemeo langu ni Mungu tu Anayeona moyo wangu. Nimekuchukua kama wakili, kwa sababu kutumia njia za dhahiri ni njia ya adabu. Kwa kuwa najua kwamba u mwaminifu katika kazi yako, hivyo nimekuchukua kuwa wakili.

"Bwana Fadhluddin alisema kwamba nilimwambia tena kuwa nakushauri kutoa kauli hii hii. Bwana Mirza akasema "Hapana, maelezo ninayoandika mimi mwenyewe, ingiza yale bila kujali matokeo yake, humo lisibadilishwe hata neno moja. Nami nasema kwa yakini kabisa kwamba haya yataathari zaidi kuliko kauli yako ya kisheria, na yale matokeo unayoyahofia hayatadhihirika, bali, Mungu Akipenda, mwisho utakuwa mwema. Na kama katika mtazamo wa dunia mwisho usiwe mwema, yaani nipewe adhabu, basi sijali hiyo, kwani wakati ule nitafurahi kwa sababu sikumwasi Mola wangu."... Ilmuradi, Maulawii Fadhluddin alimtetea Bwana Mirza kwa jazba kubwa na ikhlasi, na akasema kwamba kisha Bwana Mirza aliandika haraka sana maelezo yake kwa kalamu. Na ni kudra ya Mungu kwamba jinsi alivyosema aliachiliwa kwa maelezo yayo hayo. Maulawii Fadhluddin akitaja ujasiri na ushujaa wake kwa kukubali msiba wa kila aina kwa kusema ukweli aliwaathiri sana wahudhuriao wa kikao. Hapo, baadhi yao walisema kwa nini,

> basi, huwi mfuasi wake. Akasema kwamba hiyo ni amali yangu binafsi, nanyi hamna haki ya kuniuliza. Nina yakini kwamba yu mkweli barabara, nami namheshima sana kwa moyo!![322]

Enyi wasomaji, tafakarini, huo ni mfano wa hali ya juu ambao Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian[as] amewawekea mawakili wa zama hizi na makundi mawili ya kesi. Mshitaki ni mzungu tena padre, na Hakimu naye ni Mzungu, na ipo hali ya hatari sana, lakini katika hali hiyo ya kutisha pia hakupenda kusema hata neno moja kinyume cha ukweli.

KAPTENI DOUGLAS KAATHIRIKA MNO NA DHATI TUKUFU YA HUDHUR[AS]

Baada ya kustaafu, Kapteni Douglas alienda Uingereza, na aliishi muda mrefu. Maishirini ya Waahmadiyya walikutana naye katika London na wakasikiliza kutoka kwake maelezo ya kesi hiyo. Yeye daima alikuwa akisema kwamba upande mmoja alikuwa mheshimiwa padre na upande wa pili Bwana Mirza. Kwangu ilikuwa vigumu kumkadhibisha Bwana Padre, lakini nilikuwa nimeathirika na dhati adhimu ya Bwana Mirza na ukweli na umaasumu wake kiasi hiki kwamba ilikuwa haiwezekani kwangu kuwa na yakini kwamba Bwana Mirza anaweza kumtuma Abdul Hamid kumwua Bwana padre. Hapo nilipotaka kupata kauli ya Abdul Hamid kupitia polisi, yeye alianguka kwenye miguu ya Kapteni wa polisi, na akasema akilia kuwa nililazimishwa kusema uongo, waila Bwana Mirza hana hatia kabisa.

Bwana Kapteni alikuwa akisema hii pia kwamba watu wanaofanya kazi katika nchi za nje, wanaporudi, watu wa hapa wanawaomba kueleza matukio maalum ya huko. Mtu yeyote aliponiomba kueleza tukio lolote, nilieleza tukio hili hili tu.

Miaka michache imepita tangu Bwana Kapteni afariki,[323] yeye alikuwa akisema kwa kushangaa kwamba nilitambua adhama ya Bwana Mirza, lakini sikufikiria kwamba siku moja Bwana Mirza atapata adhama

[322] Al Hakam, 14 Novemba 1934

[323] Kapteni Douglas (ambaye baadaye akawa Kanali) alifariki katika umri wa miaka 93, tarehe 25 Februari 1957, huko London.

kubwa kiasi hiki kwamba Jumuiya yake itaenea duniani kote.

KUANZISHA SHULE TA'LIMUL ISLAM, QADIAN

Idadi ya wanajumuiya katika Qadian ilikuwa inaongezeka siku hadi siku, lakini haikuwepo shule yoyote kwa watoto wa Jumuiya. Hivyo, wanajumuiya walilazimika kupeleka watoto wao katika shule ya Waaria. Hudhur[as] alipata taarifa kwamba katika shule ya Kiaria, Islam inapingwa, na hivyo wanajaribu kuwapoteza watoto wetu. Hapo moyo wa Hudhur[as] uliudhika sana na akaamua kuanzisha shule yetu mara moja. Basi, Hudhur[as], aliwaomba Waahmadiyya kutoa mchango, kupitia tangazo moja, tarehe 15 Septemba 1897. Kisha katika Mkutano wa Mwaka 1897 pia aliwakumbusha. Matokeo yake ni kuwa mwanzoni mwa mwaka 1898, kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu, shule Ta'limul Islam ilianzia, na Hadhrat Sheikh Ya'kub Ali Turab akawa Mwalimu wake Mkuu wa kwanza.

SAFARI YA MULTAN, MWANZONI MWA OKTOBA 1897

Mwanzoni mwa Oktoba 1897, kwa kutoa ushahidi fulani, Hudhur[as] alitakiwa kwenda Multan. Wakati wa kurudi kutoka huko, alikaa katika Lahore pia nyumbani mwa Sheikh Rahmatullah Gujrati. Siku zile nyumba ya Bwana Sheikh ilikuwepo nyuma ya duka lake "Bombay House", na duka lilikuwa katika Anarkali mbele ya Panjab Religious Book Socity. Katika nyumba hiyo watu wa kila dini na mila waliendelea kufika kwa kumwuliza maswali na kujipatia elimu ya dini. Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, Imamu wa Jumuiya Ahmadiyya, anasimulia kwamba:

> "Hapa (yaani katika Lahore) katika mitaa yote alipopita Hudhur, watu wa huko walimtusi na kwa kupaza sauti wakasema maneno mabaya. Wakati ule umri wangu ulikuwa miaka minane, nami nilikuwa naye katika safari hiyo. Sikuweza kuelewa sababu ya upinzani wao huo, kwa hiyo nilishangaa sana kuona kwamba popote alipokuwa akipita, kwa nini watu walikuwa wakimpigia makofi na mbinja? Nakumbuka kwamba alikuwepo kati yao mtu mmoja aliyekuwa amekatika mkono wake, na mkono uliobakia ulikuwa umefungwa na kitambaa,

sikujua kwamba jeraha lilikuwa kwa sababu ya kukatika kigasha au lilikuwa jeraha jipya. Yeye pia pamoja na watu wengine alikuwa akipiga makofi akikaa kwenye ngazi ya Masjid Wazir Khan, na kupiga mkono uliokatwa juu ya mkono mwingine na kupiga makelele, "Hae, hae, Mirza amekimbia". Nilishangaa sana kuona hayo na hasa kwa mtu huyo, na kwa muda mrefu niliendelea kumtazama mtu yule nikitoa kichwa nje ya gari."[324]

KUANZISHA GAZETI LA 'AL-HAKAM' KUTOKA QADIAN

Kesi ya kujaribu kuua iliyotajwa juu, habari zake alikuwa akiandika Hadhrat Sheikh Yakub Ali alikuwa akiandika, lakini magazeti yalikuwa yakiepa kuchapa habari hizo. Bwana Sheikh alipata jazba moyoni mwake ya kuanzisha gazeti lake. Hivyo, katika mwaka 1897 alianzisha gazeti liitwalo 'Al-Hakam' kutoka Amritsar na mnamo mwaka 1898, sawa na mahitaji ya Jumuiya, akalihamisha Qadian kutoka Amritsar. Gazeti hilo limetoa huduma maalum ya Jumuiya. Mwenyezi Mungu Amjaalie malipo bora mwanzilishi wake na Ampe mahali pema huko peponi. Amin thumma Amin.

HATI YA MAOMBI KWA VICEROY WA INDIA ILI KUREKEBISHA HITILAFU ZA DINI, SEPTEMBA 1897

Hudhur[as] alikuwa akiona kwamba Waaria na Wakristo siku hadi siku wanaendelea kuzidi katika ukali na matusi dhidi ya Islam na Mwanzilishi wa Islam. Kwa hiyo, Hudhur[as], katika mwezi wa Septemba 1897, alitayarisha hati ya maombi iliyotiliwa saini za Waislamu wengi na kumpelekea Lord Elgin, Viceroy wa India. Katika kumbukumbu hilo alieleza kwamba sababu kubwa ya machafuko katika India ni magomvi ya kidini. Kwa hiyo katika kanuni kuhusu kuchochea kuasi iliyopitishwa mwaka huu tu, inapaswa kuingiza humo kutumia maneno makali dhidi ya dini pia. Alitoa mapendekezo matatu yafuatayo:

1. Inapaswa kuunda kanuni kwamba wafuasi wa kila dini bila shaka waeleze mazuri ya dini zao, lakini hawataruhusiwa

[324] Sirat Masihi Mau'udi[as], mwandishi Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, Imamu wa Jumuiya Ahmadiyya, uk. 41.

kuishambulia dini nyingine. Kwa kanuni hiyo uhuru wa kidini hautaathirika wala dini yoyote maalum haitapendelewa. Na hakuna sababu kwa wafuasi wa dini yoyote kutofurahi kwamba kwa nini hawaruhusiwi kushambulia dini nyingine.

2. Kama njia hiyo isikubaliwe, basi kwa uchache watu wakatazwe kushambulia dini nyingine kuhusiana na mambo ambayo kwa sababu yake hata dini yao inaweza kushambuliwa. Yaani wasitaje mambo dhidi ya mpinzani wake ambayo yamo ndani ya dini yao wenyewe pia.
3. Kama hiyo pia isipendeze, basi serikali kwa kuwauliza wawakilishi wa kila dini itayarishe orodha ya vitabu vya dini vinavyoaminika kwao, ipitishe kanuni kwamba dini yoyote isikosolewe kwa mambo yasiyokuwemo katika vitabu vinavyoaminika katika dini hiyo. Kwani, kama msingi wa ukinzani uwe juu ya dhana tu au masimulizi ya uongo ambayo hayakubaliwi na wafuasi wa dini ile, basi matokeo ya shutuma za aina hii yaweza kuwa nini ila kuzidi katika bughudha na uadui kati yao.

Hudhur alipeleka, kumbukumbu hilo, kwani aliona kwamba kwa kuacha waislamu, wafuasi wa dini yoyote hawana kitabu kinachoweza kukubaliwa duniani kwa mazuri yake binafsi na kwa kuvutia. Nao hawana chochote isipokuwa shutuma mbovu za hovyo dhidi ya dini zingine. Hao walikuwa hawawezi kuonyesha mazuri katika kitabu chao cha kukubalika yawavutiayo waadilifu. Na kama kumbukumbu hilo likipitishwa, basi Wakristo na Waaria hawataweza kusonga mbele hata hatua moja.

Kuhusu hiyo ninayo tajriba yangu binafsi pia. Muda mfupi umepita, nilikwenda "Masihi Darut Tabligh" huko Anarkali kwa kusikiliza hotuba ya padre fulani. Huko vilikuwepo baadhi ya vitabu pia kwa kuuza vilivyowekwa na misheni juu ya meza moja. Msimamizi wa vitabu alikuwa mtu mtulivu, aliponiona nikisimama karibu na meza, alifikiri kwamba mtu huyu anaonekana mpenda elimu, labda atanunua kitabu chochote. Basi aliuliza, "Je, utanunua kitabu chochote? Nikasema, naam, nipe kitabu ambamo mazuri ya dini ya

Kikristo yameelezwa, lakini dini nyingine yoyote haikupingwa humo. Kusikia hii alishtuka, na baada ya kufikiri kidogo akasema hatuna kitabu cha aina hiyo. Nikasema, "Basi, mnaipa nini dunia? Kwa kupinga Islam au dini nyingine yoyote, dini yenu haitathibitika kuwa kweli. Akasema, "Hili ni jambo la kweli." Nikasema, "Basi, jaribuni kusisitiza kujenga mkiyaacha yanayoharibu." Akasema, "Sawa kabisa, nitapeleka maoni haya mbele ya kamati yetu."

Ukweli ni huu kwamba hao watu wanalitegemea jambo hili kwamba wanaweka rundo la shutuma mbele ya Waislamu wanyonge wasio na elimu, ambao hawawezi kujibu, wakiathirika wanasarenda mbele yao. Lakini kama kumbukumbu la Hudhur[as] lingekubaliwa, basi njia ya kueneza Islam ingefunguka na dini za uongo zingejifia zenyewe. Lakini serikali ilikuwa ya Wakristo, ilijua vizuri kwamba kama yakikubaliwa mapendekezo hayo, basi mapadre hawatakuwa na la kufanya, na Islam itaenea. Lakini serikali haikujua kwamba kwa kuenezia Islam njia za kimbingu zimeshazalika. Basi hata kama njia za kiardhi zishindikane, hata hivyo Islam itasonga mbele na itastawi, na nguvu yoyote ya dunia haitaweza kujitia kati.

VITABU VYA MWAKA 1897

1. Uchapaji wa ***Anjame Atham*** (Mwisho wa Atham): Madhumuni ya kitabu hiki yanadhihirika kutokana na jina lake.
2. Uandishi na uchapaji wa ***Istiftaa*** (Toeni Fatwa): Katika kitabu hiki Hudhur[as] ameeleza habari zote kuanzia mwanzo hadi mwisho za utabiri kuhusu Pandit Lekhram, na akakituma kwa njia ya posta kwa wenye fahamu na wenye akili nzuri na kuwauliza kwamba sasa semeni kwamba utabiri umeshatimia kinagaubaga au la? Juu yake karibu watu elfu nne walitia saini kwa kusadikisha, katika hizo, saini chache zimenukuliwa katika *Tiryakul Kulub*.
3. ***Siraje Munir*** (Siraji Imulikayo): Katika kitabu hiki, Hudhur[as] ameandika ishara zake 37 zilizokwishatimia. Na ametoa maelezo zaidi ya utabari kuhusu Abdullah Atham na Pandit Lekhram pia. Vilevile amenukuu barua tatu za Khwaja Ghulam Farid, *Sajjada Nashin* wa Chachran Sharif.

4. ***Tuhfa Kaisariyya*** (Zawadi kwa Malkia): Madhumuni ya kitabu hiki yanadhihirika kutokana na jina lake. Ndani yake Malkia wa India amehubiriwa Islam.

5. ***Hujjatullah***: Hiki ni kitabu cha Hudhur[as] kwa lugha ya Kiarabu kilichotangazwa na Hudhur[as] tarehe 17 Machi 1997 kwamba ataandika, kisha katika siku 41 alikiandika, na kukichapisha tarehe 26 Mei 1897. Katika kitabu hiki masheikh wote, hususan Sheikh Abdul Hak Ghaznawii na Sheikh Najfi waliitwa, walipewa changamoto kwamba kama mna ghera na haya hata sawa na chembe, basi nyinyi pia andikeni na chapisheni kijitabu kama hiki kwa Kiarabu katika siku arobaini na moja. Kisha Sheikh Abdullah Tonki au mwanachuoni mwingine yeyote wa lugha ya Kiarabu apewe vijitabu vyote viwili kuvichunguza. Kama akisema kwa kuapa — kwa kusisitizwa kuwa aadhibiwe kama akiongopa — kwamba kulingana na "fasaha, balagha na maarifa za ndani, madhumuni yenu ni bora au sawasawa na yangu, hapo mwapaji baada ya dua yangu asiposhikwa na adhabu ya Mungu katika siku 41, basi nitachoma vitabu vyangu nitakavyokuwa navyo, na nitatubu kwa mkono wao.

6. ***Sirajuddin I'sai ke char sawalon ka jawab*** **(**Majibu ya Maswali Manne ya Mkristo Sirajuddin**):** Kijitabu hiki cha kurasa 48 kilichapwa 22 Juni 1897. Ndani yake majibu ya maswali manne ya Sirajuddin aliye Mkristo, Profesa wa Mission College Lahore, yametolewa.

MKUTANO WA MWAKA 1897

Mkutano huo ulifanyika katika likizo za Krismasi. Humo Hudhur[as] akatoa hotuba tatu, Hadhrat Hakim Alahaji Maulana Nuruddin hotuba moja na Hadhrat Maulana Abdul Karim hotuba mbili. Hotuba hizo zilichapwa na ndani ya hizo kuna bahari iliyojaa elimu.

TANGAZO LA KUMTOLEA FIDIA YA RUPIA 20,000 ATAKAYE-LETA HADITHI YA KUPAA NA KUSHUKA KWA HADHRAT MASIHI[AS]

Ni jambo la ajabu kwamba masheikh walikuwa wakimtolea Hudhur[as] fatuwa ya kumkufurisha, na Hudhur[as] alikuwa akiwakaribisha kwenye utafiti wa kielimu kwa njia mbalimbali. Kwa mwenendo huu wa Hudhur[as] badala ya kufuata njia inayokubaliwa na akili, walikuwa wakizidi katika hasira na ghadhabu.

Tarehe 24 Januari 1898 kilichapishwa "*Kitabul Bariyya*". Ndani yake akiwaambia masheikh akatangaza kwamba:

> "Kisha wakiulizwa kwamba kuna uthibitisho upi wa kupaa Hadhrat Masihi[as] mbinguni na kiwiliwili chake, hawawezi kuleta aya yoyote wala hawawezi kuonyesha Hadithi yoyote. Wakiongeza wenyewe neno 'mbingu' pamoja na neno ***Nuzul*** wanawadanganya watu wa kawaida. Lakini iwe wazi kwamba katika Hadithi yoyote ***Muttasil Marfu'*** neno 'mbingu' halipatikani. Neno ***Nuzul*** katika lugha ya Kiarabu latumika kwa msafiri, na msafiri huitwa ***Naziil***. Hata katika nchi yetu pia, mgeni huulizwa kwa heshima tu kwamba umeshukia wapi. Katika mazungumzo, mtu yeyote hafikiri kwamba mtu huyo ameshuka kutoka mbinguni. Mkitafuta katika vitabu vya Hadithi vya madhehebu yote ya Islam, achilia mbali Hadithi sahihi, hata Hadithi ya kutungwa pia hamtapata ambamo imeandikwa kwamba Hadhrat Masihi[as] alipaa mbinguni na kiwiliwili chake, na katika zama fulani atarudi ardhini. Kama mtu akileta Hadithi ya aina hii, twaweza kumpa mtu kama huyo faini ya rupia 20,000, na kutubu kwetu na kuchoma vitabu vyetu vyote itakuwa zaidi ya hiyo."[325]

Muda zaidi ya miaka sitini umepita tangu ulipotolewa mwito huo wa Hudhur[as]. Masheikh baada ya kusoma maelfu ya vitabu wameandika mamia ya vitabu juu ya swala la "Uhai wa Masihi[as]", lakini mpaka leo mtu yeyote hajaweza kujaaliwa kukubali changamoto hiyo ya

[325] *Kitabul Bariyya,* uk.192, Maelezo ya pembeni.

Hudhur[as] na kuleta Hadithi yoyote ambamo imetajwa kupaa mbinguni kwa Hadhrat Masihi[as] pamoja na kiwiliwili chake na kushuka kwake.

UTABIRI WA KUENEA TAUNI KATIKA PANJAB

Tarehe 6 Februari 1898 aliona katika ruya:

> "Malaika wa Mwenyezi Mungu wanapanda mimea ya rangi nyeusi katika sehemu mbalimbali za Panjab, na miti hiyo ni ya sura mbaya sana, ya rangi nyeusi, ya kutisha na ni mifupi. Niliwauliza wapandaji kwamba hii ni miti ya aina gani. Wakajibu kwamba hii ni miti ya tauni, itakayoenena baada ya muda mfupi nchini."

Kwa kueneza utabiri huo, siku ile ile alichapisha tangazo moja. Na kinyume cha fatuwa za masheikh, aliwashauri watu kwamba si mwiko kukaa uwanjani nje ya kijiji katika siku za tauni sawa na mafundisho ya Islam, bali yafaa sawa na kanuni ya kutunza afya. Lakini imekataliwa kuhamia kijiji kingine kutoka katika kijiji kilichoshikwa na tauni, kwani jambo hili linahatarisha kuenea tauni katika vijiji vingine.

Tangazo hilo lilipotolewa tu wakadhibishao na wakufurishao walipata nafasi ya kufanya mzaha, kwani Hudhur[as] alipotoa tangazo hilo wakati huo katika Panjab haikuwa hata alama ya tauni. Magazeti pia yalifanya dhihaka. "*Pesa Akhbar*" lililokuwa miongoni mwa magazeti yenye kusifiwa zaidi ya Lahore liliandika kwamba:

> "Mirza huwa anawaogofya watu kwa njia kama hii, mtaona yeye mwenyewe atashikwa na tauni."

Hatimaye, sawa na utabiri wake katika msimu wa baridi ujao, katika Wilaya ya Jalandhar na Hoshiarpur maradhi ya tauni yalizuka na yalienea kiasi hiki kwamba ikawa vigumu kwa serikali kuyazuia. Katika Qadian pia mkutano ulifanywa kuhusu kuzuia tauni ambamo mipango ya serikali ya kujitahadhari ilisifiwa. Kwa wagonjwa walioshikwa na tauni, Hudhur[as] alitayarisha dawa moja aliyoita "*Tiryake Ilahi*". Dawa nyingine alitayarisha kwa tezi ya tauni. Na akatayarisha dawa nyingine kwa kupaka kwenye tezi ya tauni na

jeraha lake na akaiita "*Marhame Isa*". Maelezo ya kutengeneza dawa ya pili yanapatikana katika vitabu vya utibabu na imeandikwa kwamba dawa hii ni ile waliyotayarisha wanafunzi wa Yesu kwa kupaka kwenye majeraha ya Hadhrat Masihi[as]. Kwa sababu hiyo zaidi ya majina mengine, jina moja la dawa hiyo ni 'Marhame Hawariyyina'. Yaani, malhamu yaliyotengenezwa na wanafunzi wa Yesu.

KUMBUKUMBU KUHUSU KITABU CHA "UMMAHATUL MUMININ", 4 MEI 1898

Ahmad Shah aliye Mkristo alichapisha kitabu kimoja kichafu cha kuudhi sana kiitwacho "Ummahatul Muminin", ambamo alitumia maneno ya kukosa adabu sana kuhusu Mtume Mtukufu[saw] na wakeze watakatifu. Mtu huyu mwenye mdomo mchafu alipokwisha wagawia Waislamu vitabu elfu moja bure, Anjuman Himayate Islam Lahore iliipelekea serikali ya Panjab kumbukumbu moja ambamo iliomba kwamba kitabu hicho kipigwe marufuku. Hudhur[as] alipopata habari ya kumbukumbu hiyo, hakuipenda, na mwenyewe akatayarisha kumbukumbu moja na kuipelekea serikali. Na aliwaambia Waislamu pia kwamba nakala elfu moja za kitabu hicho zimeshagawanywa bure kwa Waislamu, sasa itafaa nini kupigwa marufuku kitabu hicho. Bali, sasa yapasa kuandika jibu lake na kugawa kwa Waislamu ili liwe ni malhamu kwa majeraha yao. Hudhur[as] alisema hii pia kwamba mapadre wamechapisha mamia ya vitabu vya aina hii kwa kuudhi mioyo ya Waislamu na kujeruhi maono yao. Dawa yake ni kuwatendea walivyotutendea. Na kama serikali haipendi njia hii, basi yafaa itoe amri ya kakataza tangu sasa kutumia katika mijadala ya Kidini, maneno ya kuudhi na machafu na kadhalika.[326]

Ni masikitiko kwamba serikali ya Panjab haikujali kumbukumbu la Anjuman Himayate Islam, wala sawa na kumbukumbu la Hudhur[as] haikuelekea kukataza kutumia maneno makali na yenye kuudhi. Na sababu yake kwa yakini ilikuwa hiyo tu tuliyoeleza juu kwamba mapadre wenye dini ya serikali wasingeweza kamwe kuhubiri dini yao bila kuzishambulia dini zingine. Lakini mambo yalipopita mipaka,

[326] Tangazo la 4 Mei 1898

baada ya muda mrefu, iliwekwa kuwa ni hatia kisheria kuwavunjia heshima waanzilishi wa dini sawa na kifungu cha 153 B.

MWONGOZO KWA JUMUIYA KUHUSU KUOANA, 7 JUNI 1898

Mpaka sasa kulikuwa hamna kizuizi kuoana na wasiokuwa Waahmadiyya, lakini Hudhur[as] alipoona kwamba watoto wetu kwa kukosa kidini mazingira mwafaka hawawezi kuendelea na wengine, aliitolea Jumuiya agizo muhimu. Yafaa kuliandika hapa kwa maneo matakatifu ya Hudhur[as] mwenyewe. Anasema:

> "Kwa vile kwa fadhili na ukarimu na hisani ya Mwenyezi Mungu idadi ya Jumuiya yetu inaendelea kuongezeka, na sasa imeshafikia maelfu, na kwa fadhili yake katika muda si mrefu itafikia malaki, kwa hiyo inafaa kwamba kwa kuimarisha umoja wao na vilevile kwa kuwasalimisha na athari mbaya na matokeo mabaya ya jamaa zao, upangwe mpango mzuri kuhusu ndoa za wasichana na wavulana. Hii ni dhahiri kwamba watu waliofikia mwisho wa chuki, inadi, ubahili na uadui chini ya athari ya masheikh wapinzani, imekuwa haiwezekani kwa Jumuiya yetu kuoana nao tena mpaka wakitubu wajiunge na Jumuiya. Na sasa, Jumuiya hii haiwategemei katika jambo lolote. Wako wengi katika Jumuiya hii wanaowashinda katika mali, fedha, elimu, fadhila, ukoo na uchamungu na watu wa kila kaumu ya Kiislamu wapo katika Jumuiya hii. Basi, katika hali hii haina haja yoyote kwamba Jumuiya yetu ianzishe uhusiano mpya na watu wa aina hii wanaotuita makafiri na madajali, au wenyewe hawatuiti hivyo, lakini wanawasifu na ni wafuasi wa watu wa aina hiyo.
>
> Iwe wazi kwamba mtu ambaye hawezi kuwaacha watu wa aina hiyo, huyo hapaswi kujiunga na Jumuiya yetu. Maadamu kwa ajili ya kupata utakaso na ukweli, ndugu hataachana na nduguye na baba hatatengana na mwanaye, huyo hayumo miongoni mwetu. Basi Jumuiya yote isikilize kwa makini kwamba ni lazima kwa mkweli kufuatilia masharti hayo."[327]

[327] Tangazi la 7 Juni 1898

KESI YA KODI YA MAPATO 1898

Maadui na wapinzani wa Hudhur[as] walipoona kwamba yeye hakupata madhara yoyote katika kesi ile ya kuua kwa kusudi iliyofunguliwa dhidi yake, basi wakafungulisha kesi ya kodi ya mapato dhidi yake kwa kumpatia hasara ya mali, ambayo ilifunguliwa katika mahakama ya Hakimu wa Tarafa aliye Baniani. Hudhur alitaka kutoa vipingamizi lakini kwa ajili yake huwa lazima kuleta rejista ya hesabu ya kila siku. Mahadimu walipokuwa wameanza kutayarisha hesabu, Hudhur[as] akajawa na hali ya kashfi, na kajua kuwa hakimu wa Tarafa aliye Baniani amehamishwa na mahala pake amekuja hakimu Mwislamu wa Tarafa, na Mungu Akipenda kesi itaishia kwa heri. Basi, ikawa hivyo hivyo. Huyo hakimu Baniani wa Tarafa alipata uhamisho na mahala pake akaja hakimu Mwislamu wa Tarafa, jina lake Tajuddin. Baada ya utafiti kamili akapeleka taarifa kwa Disii kwamba fedha zinazomfikia kwa sura ya mchango, zote hizo zinatumika kwa shughuli za kijamii, na mapato yake mwenyewe hayaingii katika eneo la kutozwa kodi kisheria. Tarehe 31 Agosti 1898, Bwana Hakimu wa Tarafa alituma ripoti na tarehe 17 Septemba 1898 Disii wa Gurdspur, Bwana T. Dixon alitoa uamuzi wake ambamo aliandika:

> "Hatuna sababu yoyote ya kumtilia shaka mtu huyu nia yake safi. Mapato yake ya mchango anayoeleza ni kiasi cha rupia 5,200, tunasamehe kodi yake kwani sawa na kifungu cha (5) (E) yanatumika kwa mahitaji ya kidini tu."[328]

MWITO WA MUBAHALA KWA MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII

Uadui wa Maulawii Muhammad Husain Batalawii haufichiki kwa mtu mjuzi. Yeye ndiye aliyechukua fatuwa ya kufuru dhidi ya Hudhur[as] kutoka kwa masheikh 200 akisafiri India nzima. Naye ndiye aliyesema maneno haya kwamba:

> "Mimi ndimi niliyemnyanyua Mirza, nami ndimi nitakayemwangusha chini."

[328] Nuzulul Masihi, uk. 229, na Dharuratul Imam, uk. 35

Na yeye ndiye alijishughulishia usiku na mchana kufanya njama ya kumdhuru Hudhur[as]. Kwa kuona mwenendo wa uadui wake huo haupungui, baadhi ya wafuasi wa Hudhur[as] walichapisha tangazo kwa ajili ya Waislamu wote, katika Oktoba 1898, ambamo waliwaambia wapinzani kwamba kama mkijiona m wakweli katika itikadi zenu, basi mwambieni Maulawii Muhammad Husain Batalawii ajiweke tayari kufanya mubahala na Hudhur[as]. Kama akifanya mubahala na haikudhihirika athari wazi wazi ya mubahala katika mwaka mmoja, basi Maulawii Muhammad Husain atapewa zawadi ya rupia 2,525 na Anna 8 taslimu. Bwana Maulawii akitaka, tutaweka fedha hiyo kwa kumwondolea mashaka, kwenye Anjuman Himayate Islam Lahore au katika Bangal Bank, katika wiki tatu baada ya yeye kukubali mubahala.[329]

MATANGAZO YA MAULAWII ABUL HASAN TIBETI NA JA'FAR ZATALLI

Kwa kujibu tangazo hilo, wanafunzi wawili wa Maulawii Muhammad Husain Batalawii, yaani Maulawii Abul Hasan Tibeti na Maulawii Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli walichapisha tarehe 31 Oktoba 1898 na 10 Novemba 1898 matangazo mawili dhidi ya Hudhur[as] ambamo halikukuwa jambo la maana isipokuwa maneno ya ovyo tu.

DUA YA HUDHUR[AS], 21 NOVEMBA 1898

Hudhur[as]akisoma hayo matangazo mawili, alimwomba Mwenyezi Mungu tarehe 21 Novemba 1898 dua hii:

> "Ee Mola wangu Jalali, kama mimi ni dhalili, mwongo na mzushi machoni mwako kama Maulawii Muhammad Husain Batalawii alivyonitaja mara kwa mara katika gazeti lake ***Isha'atus Sunna***, kuwa mimi ni mwongo sana, dajali na mzushi, na kama ambavyo yeye na Muhammad Bakhsh Ja'far Zatalli na Abul Hasan Tibeti hawakuacha kasoro yoyote kwa kunifedhehesha katika tangazo lile lililochapwa tarehe 10 Novemba 1898, basi Ee Mola wangu, kama mimi ni dhalili hivyo machoni mwako, basi nifedheheshe katika miezi 13, yaani kuanzia 15 Desemba

[329] Dhamima Tablighe Risalat, J. 7, uk. 79-80

1898 hadi 15 Januari 1900, na Udhihirishe heshima na utukufu wa hao watu na Utoe uamuzi wa hitilafu hii ya kila siku. Lakini, Ee Bwana wangu, Ee Mola wangu, Mwenye kunineemesha, Mtoaji wa neema kwangu unazozijua nami pia nazijua, kama kuna heshima yangu mbele yako, basi naomba kwa unyenyekevu kwamba katika miezi hii 13 itakayohesabiwa kuanzia 15 Desemba 1898 hadi 15 Januari 1900, uwafedheheshe duniani kwa dhila Maulawii Muhammad Husain, Ja'far Zatalli na Tibeti ambao wameandika tangazo kwa kunifedhehesha."

Katika tangazo hilo hilo, Hudhur[as] aliandika mbele kidogo:

"Hiyo ilikuwa dua niliyoomba. Kwa kuijibu, nilipata ufunuo huu kwamba Nitamdhalilisha na kumfedhehesha mdhalimu, naye atakata mikono yake."[330]

Kisha aliandika baadhi ya funuo pia za Kiarabu katika tangazo lile ambazo baadhi yake ni hizi:

أَتَعْجَبُ لِأَمْرِيْ. جَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ بِمِثْلِهَا وَتَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ مَّا لَهُمْ مِّنَ اللهِ مِنْ عَاصِمٍ

Yaani, je mnastaajabia amri yangu. Malipo ya ubaya yatakuwa sawa nao, na watu hao watafedheheka sana. Yeyote hataweza kuwalinda na adhabu ya Allah.[331]

UAMUZI WA MUNGU KADHIHIRI

Dua hiyo ilikubaliwa na Mungu, na Yeye Akaleta sababu zifuatazo za kumdhalilisha Maulawii Muhammad Husain:

Kabla ya tangazo la Hudhur[as], tarehe 14 Oktoba 1898, Maulawii Muhammad Husain alitoa kisirisiri toleo moja la Gazeti lake *Isha'atus Sunna* kwa Kiingereza ambamo akiiarifu serikali kumhusu Hudhur[as], aliandika kwamba mtu huyo anayedai kuwa Mahdi ni hatari zaidi kuliko hata Mahdi wa Sudani. Na uaminifu anaodhihiri anafanya kwa

[330] Maana ya kukata mikono ni hii kwamba mdhalimu asiye juu ya haki ameandika maandishi yasiyojuzu kwa mikono, basi mikono hiyo itasababisha yeye kujuta, na atasikitika kwamba kwa nini mikono hiyo ilifanya kazi kama hii.

[331] Tangazo la 21 Novemba 1898, lililoandikwa katika *Tablighe Risalat,* J. 7, uk.55

kupitisha wakati tu, atakapopata nguvu basi atagongana na serikali vikali hata kwamba serikali itamsahau Mahdi wa Sudani. Serikali inapaswa kumkamata haraka mtu huyo. Na kujihusu mwenyewe aliandika kwamba kwa vile mimi siamini ujaji wa Mahdi yeyote wa aina hii nami naona Hadithi zote za aina hii hazikukubaliwa ambamo ujaji wa Mahdi umetajwa, kwa hiyo mimi huwa nazipinga.

Katika tangazo hilo aliandika hii pia kuhusu Hudhur[as] kwamba yeye anao uhusiano na Amir Abdur Rahman Khan, mtawala wa Afghanistan, na anaandikiana naye akipitia wafuasi wake walio Patan.

Kwa taarifa hiyo ya siri na ya uongo, serikali ilimpa, kama zawadi, eka kadha za ardhi katika Chak 23, tarafa ya Jaranwala, Wilaya ya Lyallpur; na kuhusu Hudhur[as] ikaagiza kisiri kuchunguza habari zake.

UPEKUZI WA POLISI

Mwishoni mwa Oktoba 1898, wafuasi wa Hudhur[as] walikuwa wakijumuika kwenye paa la Masjid Mubarak kwa kusali sala ya magharibi, jioni ya siku ile Msimamizi wa polisi pamoja na Rana Jalaluddin Khan Inspekta wa polisi, wakiwa na kundi la polisi, walifika kwenye paa la Masjid Mubarak. Maulawii Abdul Karim Sialkoti alikuwepo msikitini, alipoona hiyo alishtuka. Akapeleka habari kwa Hudhur[as]. Hudhur akatoka nje kwa utulivu sana. Msimamizi alisema kwamba tumekuja kupekua nyumba yako, kwani tumepata taarifa kwamba una mahusiano na mtawala wa Kabul, nawe unanuia kugongana na serikali ukipata nguvu. Hudhur[as] alisema kwamba jambo hilo si sawa kabisa. Twaiheshimu sana serikali ya Kiingereza. Uhuru wa kidini na uadilifu uliopo katika serikali hii pahali pengine hauonekani kabisa. Twafahamu kuwa haijuzu sawa na mafundisho ya Islam kueneza Islam kutumia upanga. Twaona kuwa Islam haihitaji upanga kwa kuenea kwa sababu ya mazuri yake. Lakini hii haimaanishi kwamba hatutaki upekuzi. Lakini wakati wa sala yetu umewadia, kwa hisani yako usubiri kidogo, kwanza tumalize sala. Msimamizi wa polisi alikuwa mtu mwungwana, alikaa katika kona moja ya msikiti na akaanza kushuhudia sala.

Maulawii Abdul Karim Sialkoti[ra] aliongoza sala, yeye alikuwa na sauti

nzuri sana, tena alikuwa na athari pia ya ujaji wa polisi. Alisoma Kurani kwa sauti nzuri na kwa uchungu na unyenyekevu hata kwamba wenye kusali walilia sana. Msimamizi wa polisi aliathirika sana na sala hiyo kiasi hiki kwamba Hadhrat Maulawii Sahib alipotoa salamu, yeye akasimama na akamwambia Hudhur[as] kwamba Bwana Mirza, nimeshapata yakini kwamba u mtu mkweli na mcha Mungu. Uliyosema yote ni ukweli mtupu, hii ilikuwa ni propaganda ya uongo ya wapinzani dhidi yako. Kwa hiyo, sioni haja ya kupekua nyumba yako. Akisema hayo, Bwana Kapteni akaondoka na polisi, lakini Hudhur[as] alishangaa kwamba kundi lipi lilisababisha upekuzi huo wa nyumba? Hatimaye katika Desemba 1898, Hudhur[as] alipata gazeti lile la Maulawii Muhammad Husain Batalawii kumpitia mtu fulani, ambalo baada ya kusomewa alipata uhakika kamili. Kwa kulijibu, Hudhur[as] aliandika tarehe 27 Desemba 1898 kijitabu kimoja kiitwacho "***Kashful Ghitaa***" kwa ajili ya Serikali ya Kiingereza, ambamo baada ya kueleza habari za ukoo wake alifichua hila ya Maulawii Muhammad Husain aliyofanya kwa kupata eka kadha za ardhi kutoka kwa serikali.

OMBI LA KUTOA FATUWA

Maulawii Muhammad Husain Batalawii kwa kusema katika gazeti lake la Kiingereza kwamba siamini ujio wa Mahdi yeyote, na Hadithi zinazotaja ujio wa Mahdi naziona si za kukubalika, aliongopa waziwazi ili kupata eka zile. Hapo, sababu ilipatikana, kutoka kwa kudra ya Mungu, ya kumdhalilisha yeye kwamba Mwenyezi Mungu Alimtilia moyoni mwa mfuasi mwenye ikhlasi wa Hudhur[as], Dkt. Muhammad Ismaili Khan Goryanawii kwamba wakati huu inapaswa nitoe huduma ya dini. Basi, yeye akahudhuria Qadian katika siku za Krismasi mwaka 1898. Mkutano haukuweza kufanyika katika siku za Krismasi kwa baadhi ya sababu. Lakini yeye akisoma gazeti la Kiingereza la Maulawii Muhammad Husain Batalawii alimwomba Hudhur[as] kwamba niandikishe ombi la fatuwa. Mimi nitapata saini ya masheikh juu yake. Ombi la fatuwa aliloandikisha Hudhur ndilo lifuatalo:

KUOMBA FATUWA

> "Wasemaje Maulamaa wa dini na Mamufti wa sheria imara kumhusu mtu ambaye anakataa katakata kabisa ujio wa Mahdi atakayekuja katika zama za mwisho na atakuwa khalifa wa haki kidhahiri na kibatini na atakuwa miongoni mwa kizazi cha Bi Fatima kama ilivyotabiriwa katika Hadithi, na anaona ni upuuzi itikadi hii wanayoamini Masuni wote, na anafikiri kwamba kuwa na itikadi ya namna hiyo ni aina ya upotevu na ukafiri, je, twaweza kumfahamu kuwa miongoni mwa Ahle Sunna na kwenye njia iliyo sawa. Au yu mwongo na mwenye kutengana na ijmaa, mshirikina na dajali. Elezeni waziwazi mkapewe ujira.

Imeandikwa tarehe 29 Desemba 1898 sawa na 15 Shaabani takatifu 1316.

Mwombaji aliyeshikamana na Mungu Mmoja, Mirza Ghulam Ahmad, *Mungu Amsamehe na Amsaidie*."[332]

Bwana Dkt. Muhammad Ismaili Khan akichukua maandishi haya ya kuomba fatuwa aliwafikia baadhi ya masheikh maarufu ambao Maulawii Muhammad Husain alikuwa amechukua fatuwa zao, lakini akiwa mwangalifu akaondoa jina la Hudhur[as] mwishoni mwake. Masheikh hao hawakuwa na habari ya gazeti la Kiingereza la mheshimiwa wao Maulawii Muhammad Husain Batalawii. Hao kwa kudhania kwamba fatuwa hiyo inamhusu Mirza Ghulam Ahmad, waliandika fatuwa kwa moyo mkunjufu kwamba mtu wa aina hii ni mpotevu, dajali na yuko nje ya duara la Islam. Kwa mfano someni fatuwa chache.

[332] Tablighe Risalat, J. 8 uk.6

FATUWA ZA MAULAMAA

FATUWA YA MAULAWII ABDUL HAK GHAZNAWII[333] ALIYE MWANAFUNZI WA HADHRAT MAULAWII ABDULLAH GHAZNAWII

Mtu atendaye kinyume cha itikadi thabiti iliyokubaliwa na Masuni, yeye bila shaka anastahiki kupata onyo la aya hii takatifu:

قال عز من قائل ۔ وَمَنْ يُّشَاقِقِ الرَّسُوْلَ مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدٰى وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيْلِ الْمُؤْمِنِيْنَ نُوَلِّهٖ مَا تَوَلّٰى وَنُصْلِهٖ جَهَنَّمَ وَسَآءَتْ مَصِيْرًا[334]

قَالَ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مَنْ فَارَقَ الْجَمَاعَةَ قَيْدَ شِبْرٍ فَقَدْ خَلَعَ رِبْقَةَ الْاِسْلَامِ عَنْ عُنُقِهٖ رَوَاهُ اَحْمَدُ وَاَبُوْ دَاوٗدَ ۔ قَالَ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَجْمَعُ اُمَّتِيْ عَلٰى ضَلَالَةٍ وَيَدُ اللّٰهِ عَلَى الْجَمَاعَةِ وَمَنْ شَذَّ شُذَّ فِي النَّارِ ۔ رواه الترمذی ۔[335]

Na Masuni wanaafikiana kwamba Mahdi[as] atakuja katika zama za mwisho na atatokana na kizazi cha Bi Fatima[ra] na dini itapata ushindi itashinda kwa mkono wake.

وَمَنْ خَالَفَ عَنْ ذٰلِكَ فَقَدْ ضَلَّ وَاَضَلَّ وَمَنْ يُّضْلِلِ اللّٰهُ فَمَا لَهٗ مِنْ سَبِيْلٍ

FATUWA YA SHEIKH ABDUL JABBAR BIN ADULLAH GHAZNAWII

Hadithi *mutawatira* zipo kuhusu Imam Mahdi na kushuka Isa bin Mariamu Mtume wa Allah na kutoka dajal, na juu yake kuna Ijmaa ya Masuni. Mkanaji wa Hadithi *mutawatira* ni kafiri, mpinga Masuni, mwenye bidaa, mpotevu na anayewapoteza wengine. Mwisho.

---

[333] Maulawii Abdul Hak Ghaznawii alikuwa mwanafunzi wa Hadhrat Maulawii Abdullah Ghaznawii sio mwanaye. (Mwandishi)

[334] Na anayemwasi Mtume baada ya kumdhihirikia mwongozo, na kufuata njia isiyo ya waaminio, Tutamgeuza alikogeukia mwenyewe na Tutamwingiza katika Jahanamu; nayo ni mahali pabaya pa kurudia. (Sura An-Nisaa 4:116.)

[335] Mtume[saw] alisema kwamba anayetengana na Jama'at hata sawa na kiwango cha shibri, yeye anatengana na Islam. Hiyo imesimuliwa na Ahmad na Abu Daudi. Na alisema Mtume[saw] kwamba bila shaka Mungu hatajumuisha umati wangu kwenye upotevu. Na mkono wa Mungu upo juu ya Jamaat, na atakayekwenda kombo atatupwa motoni.

FATUWA YA SHEIKH GHULAM MUHAMMAD BUGWI, IMAMU WA SHAHI MASJID LAHORE

Jibu la Maulamaa wakubwa ni sahihi. Bila shaka, mtu aliyetajwa katika swali ni mpotevu na mwenye kupoteza na yuko nje ya Ahle Suna.

FATUWA YA MUFTI MUHAMMAD ABDULLAH, PROFESA WA ORIENTAL COLLEGE LAHORE, MWENYEKITI WA ANJUMAN HIMAYATE ISLAM LAHORE NA KATIBU WA ANJUMAN MUSTASHARUL ULAMAA

Ujio wa Imam Mahdi, amani iwe juu yake na juu ya mababu zake, karibu na Kiama na kujaza dunia kwa uadilifu unathibitika katika Hadithi zilizo maarufu, na Umati kwa jumla umezikubali. Kukana ujio wa Imamu huyo ni upotevu dhahiri na ni kuachana na itikadi ya Masuni.

FATUWA YA SHEIKH ABDUL AZIZ LUDHIANAWII

Nasema, kwa kujaaliwa uwezo na Mungu, kwamba kukana ujaji wa Imam Mahdi kama ulivyoelezwa ndani ya Hadithi na Waislamu wa zamani na wa baadaye wanavyoamini, ni dhalala na upotevu na ukanaji huo ni kazi ya dajali tu. Mwisho

SHEIKH AHMADULLAH AMRITSARI

Aliyoandika Sheikh Abdul Hak katika kujibu, naafikiana nayo. Yafaa kujitenga na wakaao na mtu kama huyo, na inapaswa kuachana na kukaa nao. Muhuri[336]

Zaidi ya masheikh hao, Sheikh Rashid Ahmad Gangohi, Sheikh Muhammad Yakub wa Delhi, Sheikh Abu Muhammad Zubair Ghulam Rasul Al-Hanafi Al-Kasimi, Maulana Muhammad Wasiyyat Ali mwalimu wa Madrasa Husain Bakhsh, Maulana Muhammad Shah, Maulana Muhammad Yunus mwalimu wa Madrasa Sheikh Abdul Wahid, Maulana Fat'he Muhammad mwalimu wa Madrasa Fathepuri Delhi, Maulana Abdul Ghafur mwalimu wa Madrasa

[336] Muhuri huu ni wa Anjuman Taiidul Islam Amritsar, ambayo wanachama wake ni masheikh na matajiri na kadhalika wapatao mia tatu.

Husain Bakhsh, Maulana Muhammad Abdul Ghani, Maulana Muhammad Hidayatullah, Maulana Abdullah Khan, Maulana Muhammad Abdur Razzak na kadhalika masheikh wengi walitoa fatuwa ya kufuru.

FATUWA YA SHEIKH SEYYID NADHIR HUSAIN DELHAWII:

Bwana Dkt. hakuishia hapo, bali alimfikia pia Maulawii Seyyid Nadhir Husain Delhawii, mwalimu wa Maulawii Muhammad Husain. Alipoombwa fatuwa, yeye aliandika kwamba:

"Mtu huyu aliyetajwa katika swali (anayekataa ujio wa Mahdi) ni mzushi, mwongo, amepotea na anawapoteza wengine, naye ametoka katika Ahle Suna."

Chini ya fatuwa hii baadhi ya Maulamaa pia walitia saini zao.

Fatuwa hizo za masheikh zilipomfikia Hudhur[as], yeye alichapisha fatuwa hizo zote kwa njia ya tangazo.[337]

Kuona tangazo hilo la Hudhur[as], Maulawii Muhammad Husain akapigwa na bumbuazi. Masheikh waliokuwa wametoa fatuwa wakapatwa na msukosuko. Baadhi yao waliandika kwamba hatukutoa fatuwa hiyo kwa Maulawii Muhammad Husain, bali tumeitoa dhidi ya Mirza Ghulam Ahmad.[338]

Miongoni mwa masheikh, wengine wawili waliandika kwamba hatukutoa fatuwa dhidi ya mtu maalum, bali tulitoa sawa na ombi la fatuwa.[339]

Hudhur[as] akitaja ufunuo wake جَزَآءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ بِمِثْلِهَا وَتَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ katika tangazo

[337] Someni *Tablighe Risalat,* J. 8 uk. 6-9

[338] Someni matangazo ya 20 , 21 Januari 1899 yaliyomo katika *Tablighe Risalat* J. 8, uk. 38-39. Sheikh Abdul Hak na Sheikh Abdul Jabbar Ghaznawii walijuta juu ya fatuwa zao, hao walichukia maandishi yao kupitia tangazo. Someni marejeo yaliyotajwa.

[339] Hao masheikh wawili walikuwa Mufti Muhammad Abdullah Tonki, profesa wa Oriental college Lahore na katibu wa Anjuman Mustasharul Ulamaa na Sheikh Ghulam Muhammad Al Bagwi Imam wa Shahi Masjid Lahore. Someni Tangazo la 20 Januari 1899 lililopo katika *Tablighe Risalat,* J. 8, uk.40-41

lake lililotajwa juu, aliandika kwamba utabiri niliochapisha tarehe 21 Novemba 1898 umeshatimia, na akaandika kwamba Maulawii Muhammad Husain akinilaumu kwa mambo ya uongo na itikadi zisizo sahihi alipata fatuwa ya kufuru dhidi yangu kutoka masheikh, lakini mwenyewe kweli kweli akiachana na itikadi za Masuni kwa kuwafurahisha Wazungu ili kupata eka kadha za ardhi alishikwa na fatuwa hizo. Je, hii sio pahala pa ibra kwake, alitaka kunifedhehesha lakini mwenyewe akafedheheka!!

Ikifikiriwa, Hudhur[as] asingeweza kuathirika hata kidogo na fatuwa za masheikh. Kwani, Hudhur[as] alikuwa mdai wa Umahdi. Kama hangetolewa fatuwa, ukweli wake ungeweza kuwa na shaka. Tena watoaji fatuwa dhidi ya Hudhur[as] walikuwa wenye hatia ya kumkadhibisha na kumkufurisha mdai mkweli aliyetumwa na Allah. Lakini masheikh waliomtolea fatuwa Maulawii Muhammad Husain walikuwa wakimkubali kiongozi wao. Je, kwa kiongozi wa dini yaweza kuwa dhila zaidi ya hiyo? Jifunzeni enyi wenye akili.

KUFICHUKA AIBU YA KIELIMU YA MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN

Tumeshaandika juu kwamba tangazo alilochapisha Hudhur[as] tarehe 21 Novemba 1898, ndani yake ulikuwepo ufunuo wake mmoja huu pia kwamba "اَتَعْجَبُ لِاَمْرِیْ". Hapo Maulawii Muhammad Husain alipinga kwamba ibara hii si sahihi kwani kihusishi cha عجب ni "*min*" sio "*lam*". Yaani sawa na mawazo yake ibara sahihi inapaswa kuwa hivi "اَ تَعْجَبُ مِنْ اَمْرِیْ" . Jibu la upinzani huu alilotoa Hudhur[as] katika maelezo ya pembeni ya ukurasa wa kwanza wa tangazo la 30 Novemba 1898 na tangazo la 17 Desemba 1898, kwalo heshima iliyobaki ya Bwana Maulawii pia ilipotea kabisa. Hudhur[as] alitoa beti tano za Diwani ya Hamasa ambamo kihusishi cha *lam* kilitumika kwa *ajab*, sio *min*. ubeti mmojawapo ni huu:

عَجِبْتُ لِمَسْرَاهَا وَاَنّٰی تَخَلَّصَتْ اِلَیَّ وَبَابُ السِّجْنِ دُوْنِیْ مُغْلَقُ

Yaani, mpenzi aliyenijia katika mawazo, nilishangaa kwamba alifikaje, kwani nimefungwa katika jela ambayo milango yake pia imefungwa.

Sasa tazameni hapa kihusishi cha *ajab* ni *lam* sio *min*.

KESI YA KULINDA AMANI NA DHAMANA

Tumeshaandika juu kwamba katika tangazo la 21 Novemba 1898 Hudhur[as] alitabiri kudhalilika kwa Maulawii Muhammad Husain. Maulawii Muhammad Husain alijifaidisha pasipo haki kwa maneno haya ya utabiri wa ufunuo:تَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ . Yeye kwa kupitia rafiki yake Muhammad Bakhsh, Deputy Inspekta wa polisi wa Batala, alipeleka taarifa kwa maafisa wa juu kwamba Mirza Ghulam Ahmad amefanya kinyume na amri ya Disii wa Gurdaspur, Bwana Douglas, aliyotoa katika kesi ya Dkt. Henry Martin Clark kwamba asichapishe katika siku zijazo utabiri wa hilaki au mauti ya mtu yeyote, lakini ametoa utabiri wa mauti ya Maulawii Muhammad Husain. Kwa hiyo serikali inapaswa kupata dhamana ya amani chini ya kifungu cha 107 kutoka kwa Bwana Mirza. Ripoti hiyo ilipelekwa tarehe mosi Desemba 1898. Kupata ripoti hiyo Disii wa Gurdaspur Bwana Dixon, chini ya kifungu cha 107, alimshtaki Hudhur[as] kwa kesi ya jinai. Lakini hali zilivyokuwa, zikasababisha hata Maulawii Muhammad Husain pia akashtakiwa chini ya kifungu hicho hicho kwa kesi ya jinai.

Kwa ajili yake, Hudhur[as] pamoja na mahadimu walitakiwa kuenda Pathankot na Dhariwal kwa kufuatilia kesi. Lakini kwa sababu ya uhamisho wa Disii hakuna kilichofanyika katika Pathankot. Katika Dhariwal wakili wa Maulawii Muhammad Husain, Bwana Herbert, alileta udhuru mbele ya Disii mpya Bwana Dowie, kwamba sawa na kanuni mpya kesi haiwezi kuendeshwa dhidi ya Maulawii Muhammad Husain na Bwana Mirza wakati mmoja. Disii akakubali jambo hili la kisheria na aliweka tarehe 14 Februari 1899 kwa kesi. Kwa kujitetea, jibu alilotayarisha Hudhur[as] katika kesi hiyo lilikuwa hili kwamba alitaja hitilafu zote zilizokuwa na Maulawii Muhammad Husain, kisha aliieleza mahakama kwamba sikutabiri kabisa mauti au hilaki ya Bwana Maulawii bali nilitabiri dhila tu ifananayo na alivyotenda. Bwana Dowie, Hakimu wa Wilaya, aliposoma kwa makini jibu la Hudhur[as], alishangaa kuona kwamba maneno makali na machafu waliyoandika wapinzani wa Hudhur, kuyajibu hayo Hudhur[as] hakuandika hata sehemu yake ya mia. Basi alifuta kesi na akamwambia Hudhur[as] kwamba badala ya kujibu matangazo yao machafu ungepaswa kuwashtaki mahakamani.

Maulawii Muhammad Husain pia alikuwa amekuja mahakamani kusikiliza kesi. Hakimu alimwita pia kwa kufupisha mambo na akiandika maandishi fulani akapata saini juu yake, za wote wawili, Hudhur[as] na Maulawii Muhammad Husain. Notisi yenyewe ilikuwa hii:

"Tangu sasa mtu yeyote asitabiri kuhusu kifo cha mpinzani wake. Mtu yeyote asimwite mwingine kafir, dajali, mzushi na mwongo. Mtu yeyote asimwite mwingine kwa mubahala. Na Qadian lisiandikwe kwa ك wala Batala kwa ط. Na tumianeni maneo laini nyinyi kwa nyinyi, mjiepushe na maneno mabaya na matusi. Na kila upande uwaagize marafiki zake na wafuasi wake kushikamana na agizo hili. Na si tu Waislamu kwa Waislamu, bali njia hii ifuatwe na Wakristo pia."

DHILA YA MAULAWII MUHAMMAD HUSAIN ILIKAMILIKA KWA KILA JIHA

Maulawii Muhammad Husain alipeleka kesi hiyo ili Hudhur[as] afedheheke, Mungu Apishe mbali. Lakini matokeo yakawa kwamba Hudhur[as] hakupata madhara yoyote lakini dhila ya Bwana Maulawii ilikamilika kwa kila jiha. Ni hivi kwamba fatuwa alizopata Bwana Maulawii dhidi ya Hadhur[as] kutoka kwa masheikh akitembelea India nzima, na akamwita kafiri, dajali, mzushi na mwongo na kadhalika, Mungu Apishe mbali, akabatilisha hizo zote akisaini juu ya maandishi ya mahakama kwa kalamu yake mwenyewe na akafutilia mbali yote aliyofanya kwa mkono wake. Kama fatuwa zile zilikuwa sahihi sawa na Bwana Maulawii, basi mahakamani Bwana Maulawii alitakiwa kusema kwamba sawa nami mtu huyu kwa kweli ni kafiri na mwongo, siwezi kuacha kuandika maneno ya aina hii, lakini Bwana Maulawii akaogopa. Hudhur[as] pia akasema kwamba Maulawii Muhammad Husain Batalawii "atapata dhila gani zaidi ya hii kwamba mtu huyo amebomoa jengo lake kwa mikono yake."[340]

Ama swali la Hudhur[as] kutia sahihi, kwa hakika yeye hakutangulia

[340] Kutoka katika tangazo lilioandikwa katika *Tablighe Risalat*, J. 8, uk. 109

kamwe kumwita yeyote kafiri, mwongo na kadhalika. Hudhur[as] alipotumia neno kali kwa yeyote, lilikuwa kwa kujitetea, nalo pia lilikuwa laini kuliko maneno yao. Sasa mshambulizi alipokoma, mwenye kujitetea alikuwa na haja gani ya kutumia maneno makali. Naam, kama swali lizuke kwamba yeye pia amezuiliwa kutabiri kifo na dhila ya mtu kwa siku zijazo, basi jibu lake kwa ulimi mtakatifu wa Hudhur[as] ni hili:

> "Kazi yetu hii iliishia mapema kabla ya wakati huo ilipoandikwa hivyo katika notisi ya Bwana Dowie. Bali katika kitabu chetu, 'Anjame Atham' niliishaandika waziwazi kwamba sitaki tangu sasa hata kusema nao mpaka hao wasemezane nami. Sisi kwa moyo tumechoka na twachukia hata kutaja jina la watu hao, licha ya kuwatolea utabiri na kuwapatia heshima hata kusema nao kiasi hicho. Lengo letu lilikuwa matabiri matatu kuhusu makundi matatu. Basi tumeshakamilisha shabaha yetu. Sasa hatuna haja ya kutoa utabiri kuhusu kifo na dhila ya watu hao. Na swali hili kwamba nimezuiliwa kwa jumla kutangaza funuo zangu na matabiri ya aina zote, hayo ni maneno ya wale walio chini ya onyo la ***laanatullahi alalkadhibin*** yaani laana ya Mungu iwe juu ya waongo. Hata sasa pia baada ya kesi hii tumeshatangaza bishara nyingi. Basi, huu ni uongo mchafu namna gani ambao watu hao wanawaeleza wale wasio na habari. Na swali hili kwamba Muhammad Husain amepata ardhi kiasi fulani, yaani badala ya dhila amepata heshima, hayo ni mawazo mabovu. Swali hilo lingetajwa wakati Muhammad Husain angeishapata manufaa kidogo katika ardhi hiyo. Hivi sasa yeye yupo katika mtihani fulani, haijulikani hatimaye ardhi hiyo itamhasiri au italeta manufaa kidogo. Isitoshe, katika ***Kanzul Ummal, kitabu Muzara'a,*** kwenye ukurasa wa 73, kuna Hadithi hii ya Mtume wa Mungu s.a.w.: لَا تَدْخُلُ سِكَّةُ الْحَرْثِ عَلٰى قَوْمٍ اِلَّا اَذَلَّهُمُ اللهُ (Tabarani, msimulizi Abi Yamama). Yaani, ulimi wa plau hauingii katika kaumu isipokuwa unawadhalilisha watu wake... Ama jambo hili kwamba Muhammad Husain amepangiwa mshahara na utawala fulani, basi jambo hili halichukuliwi kuwa heshima na yeyote mwenye akili. Katika tawala hizo watu wa

kila aina wanapangiwa mishahara, ambao hata kutaja pia vitendo vya baadhi yao ni aibu. Basi, kama Muhammad Husain pia amepangiwa mshahara, jambo hili limeleta heshima gani? Bali hapa nakumbuka sentensi hii: [341] بِئْسَ الْفَقِيْرُ عَلٰى بَابِ الْاَمِيْرِ — Mbaya alioje fukara mlangoni pa amiri.

Sasa waliobaki ni Abul Hasan Tibeti na Jafar Zatalli, wanafunzi wa Maulawii Muhammad Husain Batalawii. Hao nao walizuiliwa wasiandike maandishi machafu na mapujufu sawa na utabiri huu wa Hudhur[as]: [342] يَعَّضُ الظَّالِمُ عَلٰى يَدَيْهِ وَيُوْثَقُ yaani "Mdhalimu atakata mikono yake na atazuiliwa."

VITABU VYA MWAKA 1898

1. Kitabul Bariyya: Kitabu hiki kilichochapwa 24 Januari 1898, ndani yake maelezo yote ya kesi ya kunuia kumwua Dkt. Henry Martin Clark yameandikwa, na kwa mfano matusi yale pia yametajwa ambayo mapadre walimtolea Mtume Mtukufu[saw]. Na serikali imearifiwa kwamba kwa kujibu matusi hayo katika maandishi yetu ukali kiasi ukipatikana, basi ni uchungu wa moyo ulioudhika.

Katika kitabu hiki, swali hili pia limejibiwa kikamilifu kwamba kwa nini nilishtakiwa katika kesi hiyo? Habari za ukoo wake na habari zake binafsi pia zimeelezwa humo, na madai yake na hoja zake pia. Kwa kubatilisha Ukristo, kitabu hiki hakina mfano, hakiyumkiniki kujibiwa.

2. Albalagh: Jina lake la pili ni Faryade Dard. Kitabu hiki kinahusu zaidi kitabu cha Wakristo chenye kuudhi. Ndani yake Hudhur[as] ametaja kumbukumbu la Anjuman Himayate Islam lililopelekwa serikalini kwa kupiga marufuku kitabu hicho kinachochokoza na kuudhi moyo sana. Na akaeleza kwamba njia ya kuondoa athari yenye hatari na yenye sumu ya vitabu vya aina hii vya kuudhi sio kwamba serikali itumiwe kumbukumbu la kuvipiga marufuku. Kwani, kitabu kikienezwa nchini kimeshaingiza athari yake mbaya

[341] Kutoka Tangazo la tarehe 17 Desemba lilioandikwa katika *Tablighe Risalat*, J. 8

[342] Kutoka katika Tangazo la 21 Februari 1899

mioyoni mwa wasomaji wake, basi kuna faida gani sasa ya kukipiga marufuku? Sasa inapaswa kuandika kwa upole na adabu sana jibu lake la kufumba midomo. Katika kitabu hicho Hudhur[as] aliandika masharti kumi pia yaliyo muhimu kupatikana katika mwandishi wa anayejibu. Chapa ya Kiingereza ya kitabu hicho mara moja kilitolewa lakini chapa ya Kiurdu kilitolewa baada ya kufariki kwake.

3. Dharuratul Imam (Haja ya Imamu): Katika kitabu hiki, swali hili limejibiwa kwamba nani anaitwa Imamu wa zama na alama zake ni zipi? Ana ubora gani kuliko wengine wenye kupokea funuo, waotaji ndoto na wenye kupata kashfi? Kadhalika imefafanuliwa alama za ufunuo wa kweli na hakika ya baiati. Maelezo ya kesi ya kodi ya mapatao pia yameandikwa.

4. Najmul Hudaa: Kitabu hiki kilichapwa 20 Novemba 1898. Kina safu nne: Kiarabu, Kiurdu, Kiajemi na Kiingereza. Kana kwamba ilinuiliwa kueleza madhumuni yale yale katika lugha nne. Katika lugha tatu madhumuni haya yalichapwa, lakini haikupatikana nafasi ya kuchapa kwa lugha ya Kiingereza. Baadaye madhumuni haya kwa Kiingereza pia yalichapwa yaliyofasiriwa na Khan Bahadur Abul Hashim Khan.

Katika kitabu hicho hakika ya majina ya Mtume Mtukufu[saw], Muhammad na Ahmad, imeelezwa kinagaubaga.

5. Raze Hakikat (Siri ya Uhakika): Kitabu hiki kilichapwa 30 Novemba 1898. Humo habari za maisha ya Hadhrat Isa[as] zimeelezwa, hususan imetajwa safari yake ya Kashmir na kaburi lake lililomo katika Srinagar, mtaa wa Khanyar. Mwishoni mwa kitabu kuna tangazo moja pia ambamo mambo ya Maulawii Muhammad Husain Batalawii yametajwa.

6. Kashful Ghitaa: Kitabu hiki kilichapwa 27 Desemba 1898. Ndani yake akitaja habari za ukoo wake na uaminifu wa Jumuiya yake, amebatilisha propaganda ya uongo ya wapinzani waliyofanya dhidi yake, hasa alibatilisha kabisa shutuma za Maulawii Muhammad Husain.

KUZALIWA KWA MUBARAK AHMAD, 14 JUNI 1899

Tarehe 14 Juni 1899 alizaliwa kwake mwana wa nne aliyeitwa Mubarak Ahmad. Miezi miwili kabla ya kuzaliwa kwa mwana huyo roho yake ikasema kiufunuo maneno haya:

اِنِّیْ اَسْقُطُ مِنَ اللّٰہِ وَ اُصِیْبُہٗ

Yaani, "Sasa wakati wangu umewadia, nami kutoka kwa Mungu na kwa mikono ya Mungu nitaanguka ardhini, na kisha nitarejea kwake."

Akaagua ufunuo huu kwa ijtihadi yake kwamba:

> "Kijana huyo atakuwa mwema sana na ataelekea kwa Mungu au atafariki haraka."[343]

Basi sawa na sehemu ya pili ya uaguzi, tarehe 16 Septemba 1907 katika uhai wa Hudhur[as], Mubarak Ahmad alifariki. *Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun*. Kwa sababu ya kuwa mtoto mdogo, Hudhur[as] alimpenda sana. Yeye alipougua, Hudhur[as] alimshughulikia sana usiku na mchana kwa kumtibu, lakini alipofariki, akaonyesha mfano wa subira na ridhaa kiasi hiki kwamba watu walishangaa. Aliandika beti chache pia kwa jiwe la kaburi la Mubarak Ahmad zinazoleta machoni taswira sahihi ya hali ya moyo wake. Katika beti hizo, beti mbili zaandikwa chini:

> Mwanagu mpendwa, Mubarak Ahmad, aliyekuwa na sura nzuri na tabia njema, leo ametuaga akihuzunisha mioyo yetu.
>
> Alikuwa na umri wa miaka minane na miezi michache ambapo Mungu Alimwita. Mwitaji ni mpendwa kuliko wote, Ee moyo, ujitolee kwake uhai wako.[344]

KWA NJIA YA KUMBUKUMBU, SERIKALI ILIOMBWA KUITISHA MKUTANO WA DINI ZOTE, 27 SEPTEMBA 1899

Tarehe 27 Septemba 1899, aliiomba serikali kwa kuipelekea kumbukumbu moja kwamba siku hizi ambapo wafuasi wa dini zote wanapigana kwa kuishindisha dini yao, yafaa serikali iitishe mkutano

[343] Tiryaqul Qulub, uk. 40

[344] Shairi kamili litaandikwa mbele pahali pake, inshallah. Mwandishi

kwa kuchunguza dini ipi ni ya kweli duniani, ambamo viongozi wa dini zote waeleza mafundisho mazuri ya vitabu vyao. Kisha kwa nguvu yao ya kiroho walete uthibitisho kuhakikisha kwamba kwa kufuata dini yao mtu anaweza kupata ukamilifu wa kiroho. Hudhur[as] alisema:

> "Serikali yetu tukufu ikitangaza mkutano wa dini iweke tarehe ya mkutano huo ndani ya muda usiozidi miaka miwili. Na waitwe maulamaa maarufu, madaruweshi na wapokeaji ufunuo wa kaumu zote kwa shabaha kwamba wakihudhuria tarehe ya mkutano walete uthibitisho wa aina mbili wa ukweli wa dini yao.
>
> "Wa kwanza: Walete mafundisho ambayo yawe bora kuliko mafundisho mengine, ambayo yaweze kustawisha vipawa vyote wa mwanadamu. 2. Wa pili, walete uthibitisho huu kwamba katika dini yao mambo ya roho na nguvu tukufu zipo kama ilivyokuwa imedaiwa mwanzoni. Na iagizwe kwa uwazi kwamba viongozi wa kaumu zote wakijiandaa kwa kutoa mathibitisho hayo mawili wajitokeze uwanjani mwa mkutano. Na baada ya kueleza mazuri ya mafundisho, watoe bishara za hali ya juu ambazo zihusike na elimu ya Mungu tu, na zitimie katika muda wa mwaka mmoja pia."

Kisha anasema:

> "Na dini ya kweli ni ile ambayo inao mfano hai pamoja nayo. Je, moyo wowote na dhamira ya mtu yaweza kukubali kwamba dini fulani ni ya kweli, lakini mwanga wa ukweli wake na alama za ukweli wake hazipo sasa, bali zimebaki nyuma, na mpelekaji wa miongozo amenyamaa kwa kudumu? Najua kwamba kila mtu ambaye anayo njaa na kiu ya kweli kumpata Mwenyezi Mungu, hatafikiria hivyo. Kwa ajili yake ni lazima kwamba alama ya dini ya kweli iwe hii kwamba mifano iliyo hai ya Mungu Aliye Hai na nuru za kumetameta za ishara zake zipatikane mpya mpya katika dini ile. Kama serikali yetu ikipanga mkutano wa aina hii, basi hili litakuwa kusudio lenye baraka na kwalo litathibitika kwamba serikali hii inausaidia

ukweli. Na kama mkutano kama huo ukifanyika, basi kila mtu anaweza kuhudhuria mkutanoni humo kwa hiari na kuchangamka. Viongozi wa kaumu mbalimbali ambao wakijiita watakatifu walikula malaki ya rupia ya kaumu, hakuna njia bora zaidi kwa kujaribu utukufu wao kuliko hii kwamba waombwe uthibitisho ulio hai wa uhusuano wao au wa dini yao na Mungu."

UJUMBE KWA NASIBIN

Hudhur[as] alipoishajua kwamba Hadhrat Masihi Mnazareti alikuja Kashmir baada ya tukio la msalaba, na alifariki huko baada ya kupata umri mrefu wa miaka mia moja na ishirini, basi alijaribu kwamba kuhusu habari hii uthibitisho mpya mpya uletwe. Kwa kusoma kitabu "Raudhatus Safaa" aligundua kwamba wakati wa fitina ya msalaba, mfalme wa Nasibin alimkaribisha Hadhrat Masihi[as] kwake. Na umepatikana ushahidi pia wa Mwingereza mmoja kwamba lazima Hadhrat Masihi[as] alipokea barua ya mfalme huyu, bali barua ile pia ameiandika Mwingereza huyo katika kitabu chake, hapo Hudhur[as] alipata mawazo moyoni mwake kwamba si ajabu kwamba kwa kupata maelezo zaidi juu ya suala hilo, baadhi ya mbao za mawe zipatikane katika Nasibin zenye miandiko au yajulikane makaburi ya baadhi ya wanafunzi wa Hadhrat Masihi[as]. Kwa hiyo, aliamua kwamba watu watatu wenye busara na nia ya azimio watumwe kwenda Nasibin kwa lengo hili. Basi tarehe 10 Oktoba 1899, alichapisha tangazo moja lenye kichwa cha habari "Mkutano wa kusindikiza", ambamo aliandika kwamba tarehe 12 Novemba 1899 ndugu wajumuike na wausindikize ujumbe wa Mirza Khuda Bakhsh na wenzake wawili baada ya kuomba dua.[345] Lakini ni masikitiko kwamba kwa baadhi ya matatizo ya safari, ujumbe huo haukuweza kuenda.

MAHUBIRI KWA MABANIANI KWA NJIA YA FONOGARAFU

Hudhur[as] alikuwa na shauku sana kwamba njia mpya mpya zitafutwe za kuhubiri Islam. Katika siku hizo tunazozungumzia, Hadhrat

[345] *Tablighe Risalat,* J. 8, uk. 76-77

Nawab Muhammad Ali Khan wa Maler Kotla akinunua fonografu (ni kama santuri) aliileta Qadian. Pamoja nayo vilikuwa vifaa kwa kujaza sauti pia. Fungu la mwiso la Suratul Ambiyaa likisomwa na Hadhrat Maulawii Abdul Karim likajazwa ndani na likasikilizishwa kwa Hudhur[as]. Hudhur[as] alifurahi sana. Waaria wa Qadian walipojua kwamba Bwana Nawab ameleta fonografu, wakiona ni kitu cha ajabu wakamwomba Hudhur[as] kwamba sisi pia twataka kusikiliza fonografu. Hudhur[as] akasema, vyema, nyinyi pia mje wakati fulani. Akawaambia hayo, na akamwambia Hadhrat Maulawii Abdul Karim kwamba "Twaona kusikiliza na kusikilizisha fonografu ni kupoteza wakati isipokuwa itumike kwa shabaha ifaayo. Kwa nini wasihubiriwe hao Waaria kwa njia ya fonografu." Basi Hudhur[as] aliandika beti chache na akamwambia Maulawii Abdul Karim azisome kwa sauti nzuri kuzijaza ndani yake. Amri yake ikafuatwa. Waaria walipofika walisikilizishwa beti zile ambazo ubeti wake wa kwanza ulikuwa huu:

Sauti hii inatoka kutoka katika fonografu,

Mtafuteni Mungu kwa moyo, si kwa majisifu.

Hivyo, ombi la Waaria pia likakubaliwa, na shauku ya mahubiri ya Hudhur[as] pia ikatimia.

MFULULIZO WA MASOMO YA KUFUNDISHA KIARABU

Hudhur[as] alizingatia sana jambo hili kwamba Jumuiya ihimizwe kujifunza Kiarabu. Kwa ajili yake alitayarisha baadhi ya masomo pia. Lakini kwa sababu ya shughuli zingine, kazi hiyo haikuendelea kwa muda mrefu. Lakini, Hudhur[as] alianzisha fikara ya kujifunza Kiarabu katika Jumuiya.

VITABU VYA MWAKA 1899

1. ***Ayyamus Sulh:*** Kitabu hiki kilichapwa katika lugha mbili, Kiajemi na Kiurdu. Chapa ya Kiajemi ilitoka 1 Agosti 1898, lakini chapa ya Kiurdu kwa sababu ya baadhi ya maongezo ilitolewa baada muda, yaani 1 Januari 1899. Kitabu hicho kiliitwa Ayyamus Sulh kwa sababu mbili:

Ya kwanza ni hii kwamba siku hizi Islam inashambuliwa na kalamu na hoja badala ya upanga, kwa hiyo ni jukumu letu pia kwamba kwa

kuihifadhi Islam tuitumie njia ya upole na suluhu tutumie kalamu na hoja tu.

Ya pili: Dunia imeshikwa na maovu na madhambi. Mwanadamu anapaswa kujiletea mabadiliko mema na kufanya suluhu, na Mwumba na Mmiliki wake kwa toba na kuomba ghofira.

2. *Hakikatul Mahdi:* Hudhur[as] alichapisha kitabu hiki 21 Februari 1899. Humo, Hudhur[as] akielezea serikali alifichua uhakika wa kijitabu cha siri cha Maulawii Muhammad Husain Batalawii, alichoandika kuichochea serikali dhidi ya Hudhur[as]. Hudhur[as] alisema kwamba aliyoandika Maulawii Muhammad Husain katika kijitabu chake ni uongo mtupu. Hatuna nia kabisa ya kuasi serikali wala hatumwamini Mahdi yeyote mmwagaji damu. Lakini Maulawii Muhammad Husain amehini kabisa katika kueleza itikadi yake. Kama yu mkweli katika kauli yake, basi yampasa serikali kumwambia kwamba atangaze itikadi yake hiyo baina ya masheikh wenzake na watu wa kawaida. Lakini tunaihakikishia serikali kwamba hatafanya hivyo kamwe.

3. *Masih Hindustan Mein:* Hudhur[as] alikuwa na jukumu muhimu hili pia kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwamba afutilie mbali fitina ya kimsalaba. Basi, alitimiza kazi hiyo kwa njia bora kiasi hiki kwamba sasa watafiti wengi pia wa ulimwengu wa Kikristo wakimwunga mkono wanasema kwamba Hadhrat Masihi[as] hakufia msalabani wala hakunyanyuliwa mbinguni mzima mzima pamoja na kiwiliwili chake. Ni dhahiri kuwa haya yalikuwa ni mambo mawili ya kimsingi ambayo juu yake jengo zima la Ukristo limejengwa. Katika kitabu hicho ameleta hoja madhubuti zisizoweza kupingika juu ya kutokufia kwake msalabani na kusafiri kwenye Kashmir na hatimaye kufariki huko huko na kuzikwa katika Srinagar, mtaa wa Khanyar. Na dunia inaelekea upande huu. Hata watafiti Mabaniani na Wakristo pia wanakiri kwamba Hadhrat Masihi[as] akisalimika na kifo cha msalaba alikuja Kashmir, hata kwamba Mustashrikina maarufu pia wamelazimika kukiri kwamba katika aya za Injili habari za kunyanyuliwa mbinguni kwa Hadhrat Masihi[as] kwa yakini ni nyongeza ya baadaye.

4. *Sitara Kaisariyya* (Nyota ya Kaisari): Kijitabu hiki kilichapwa 24 Agosti 1899. Jinsi alivyofanya katika Tuhfa Kaisariyya, katika kijitabu hiki pia Hudhur[as] alipinga itikadi za Kikristo na alimhubiria Islam Malkia Muadhamu Victoria.

5. *Tiryaqul Qulub:* Kitabu hiki kiliandikwa katika mwaka 1899. Na tarehe 28 Oktoba 1902 zikiongezwa kurasa chache kilichapishwa. Mwanzoni mwa kitabu hicho kuna kasida maarufu ya Kiajemi ambamo ameeleza sifa za mwaminio mkamilifu. Baada yake ameeleza alama maalum ya Nabii aliye hai, na kisha ameeleza ishara zake.

MIRZA IMAMUDDIN NA NIDHAMUDDIN WAKAJENGA UKUTA MBELE YA MASJID MUBARAK, 7 JANUARY 1900

Hudhur[as] alikuwa anashirikiana kwa usawa na binamu zake Mirza Imamuddin na Mirza Nidhamuddin katika miliki ya Qadian. Kwa hiyo, alikuwa na haki ya kufaidika na ardhi ya pamoja ya kijiji, lakini kwa sababu ya upole wake wadhalimu hao walimwudhi sana yeye na Jumuiya yake. Walizuia kuchukua udongo kutoka katika ziwa la maji ya mvua, na kupata maji kutoka katika kisima. Safari moja wakati hao wasipokuwepo, baadhi ya ndugu walileta udongo kutoka ziwa la maji ya mvua, basi hao waliporudi walikasirika sana hata walitusi. Na wakamwita topasi aliyejenga ukuta mbele ya Masjid Mubark. Hudhur[as] aliudhika sana, kwani watu walikuwa wanaingia msikitini kwa njia hii hii, na Hudhur[as] pia mara nyingi kwa njia hiyo alikuwa akienda nje kwa kupunga hewa. Magari ya farasi pia ya Waahmadiyya wageni yalikuwa yakifika pale pale. Sasa wenye kusali walilazimika kuzunguka sana ili kufika msikitini kwa kupitia soko la Mabaniani. Kwanza Hudhur[as] alituma watu wachache waende kwa Imamuddin, na akawasihi kuongea naye kwa upole; lakini pale hali ilikuwa tofauti sana. Baada ya kusikiliza ombi la ujumbe, Mirza Imamuddin alighadhabika sana na kasema kwamba kwa nini yeye mwenyewe hakuja? Kisha Hudhur[as] alituma ujumbe mmoja kwa Disii. Disii na Kapteni wa polisi walikuwa wamekuja katika kijiji fulani kutafiti kesi moja. Ujumbe ulipohudhuria mbele ya Disii, yeye naye akawa mkali. Akasema:

"Nyinyi watu wengi kwa kujumuika mnataka kuniogofya.

> Nawajueni vizuri na ninaelewa vyema kwamba kwa shabaha gani Jumuiya hii imeanzishwa, sijaghafilika na mambo yenu. Nami haraka sana nitawajua na mtaelewa namna inavyoundwa Jumuiya kama hii, na kadha wa kadha."[346]

Ilmuradi, ujumbe ulirudi bila kufanikiwa. Hudhur[as] aliposikia habari zote aliudhika sana. Maulawii Muhammad Husain Batalawii na baadhi ya wapinzani wengine walikuwa wameishaifanya serikali imdhanie viovu. Kwa kuona mwenendo huu wa serikali, Mirza Imamuddin na Nidhamuddin pia waliharakisha upinzani wao. Polisi tayari walikuwa dhidi yake. Kwa hali hiyo, alijumuisha wanajumuiya na kushauriana nao kwamba kuhama ni katika suna ya manabii, kwa nini tusihamie mahali ambapo tuweze kufanya kazi yetu kwa urahisi zaidi. Hadhrat Hakim Maulana Hafidh Nuruddin[ra] alishauri kuhamia Bhera, Hadhrat Maulawii Abdul Karim alimkaribisha kuenda Sialkot, Sheikh Rahmatullah aliomba kwenda Lahore. Chaudhary Hakim Ali anasimulia kwamba niliomba kwenda kijiji chetu Panyar. Baada ya kusikiliza maombi ya wote, Hudhur[as] alisema, "Vyema, wakati utakapowadia tutaona. Popote Mungu Atakapopeleka tutakwenda pale.

Hudhur[as] alipoona kwamba Mirza Imamuddin hakubali wala Disii hasikii, sasa hakuna njia nyingine isipokuwa kupeleka kesi mahakamani. Basi kwa kushauriana na ndugu, alimshtaki Mirza Imamuddin katika mahakama ya sheikh Khuda Bakhsh, Hakimu wa wilaya ya Gurdaspur. Kwa kesi hiyo safari moja alilazimika kuenda Gurdaspur pia. Hapo kwa sababu ya shughuli nyingi alipata homa na kuhara damu. Usiku aliwaagiza ndugu kulala, basi sawa na agizo watu wakalala. Kwa vile Hudhur[as] alikuwa na shida, kwa hiyo sahaba mmoja mwenye kujitolea kwake, Hadhrat Munshi Abdul Aziz Aujlawii na ndugu wengine wawili, watatu walikesha. Wakati wowote Hudhur[as] alipoinuka kwenda kujisaidia, Hadhrat Munshi akahudhuria na birika la maji. Bwana Munshi alikesha mausiku mawili matatu mfululizo. Hudhur[as] akafurahi sana kuona ikhlasi yake hiyo, na

[346] Usimulizi wa Chaudhari Hakim Ali ulioandikwa katika ***Siratul Mahdi,*** sehemu ya kwanza, usimulizi Na. 135, uk. 138-140

kasema kwa kweli kuwa na adabu na kumhudumia mwongozi ni kitu ambacho kwa kumwunganisha mfuasi na mwongozi sana kinaleta natija ya kumfikisha kwa Mungu na kupata lengo.

Tarehe 16 Julai 1901, alikuwa ahudhurie mahakamani. Kwa sababu ya umaarufu wake, Makomishna wasaidizi watatu wa Gurdaspur pia wakiacha mahakama zao wakaja kuhudhuria katika mahakama ile kusikiliza kauli yake. Hudhur[as] alitoa kauli yake kwa uwazi sana, kisha akatoka nje akichangamka.

Baadaye, tarehe 10 Agosti 1901, Hudhur alitakiwa kuhudhuria. Siku ile mashahidi wa waliodaiwa wakahudhuria na majadiliano ya mawakili pia yaliisha. Tarehe 12 Agosti 1901 uamuzi ulitolewa. Uamuzi ulikuwa kama radi iliyomwangukia Mirza Imamuddin. Hakimu wa wilaya aliamuru kwamba aliyedaiwa mara moja abomoe ukuta, na tangu sasa jengo lolote lisijengwe kamwe katika kiwanja cha wazi. Na mdaiwa zaidi ya kutoa matumizi ya kesi, amtolee mdai (Hudhur[as]) rupia mia moja kama faini. Siku ile Hudhur[as] hakwenda Gurdaspur. Jioni, Hudhur[as] alipopata habari hiyo alisema, "Kana kwamba ilikuwa Ramadhani ya mwaka moja na miezi minane, ambayo Idi yake ni leo."[347]

Saa kumi jioni ya 20 Agosti, topasi yule yule aliyejenga ukuta kwa amri ya Mirza Imamuddin alilazimika kuubomoa.

Sasa ilibaki utoaji wa faini na matumizi ya kesi. Mirza Imamuddin alijua kwamba Hudhur[as] ni mtu mwenye huruma na mkarimu, hivyo hamna swala la kutoa matumizi. Basi, akamletea Hudhur[as] ombi la kusamehewa faini, amablo lilikubaliwa kwa moyo mkunjufu.

IKADHIHIRI ISHARA YA KIMWUJIZA KATIKA KESI HIYO

Katika kesi hiyo ishara ya kimwujiza iliyodhihiri, Hudhur[as] ameitaja katika kitabu chake kisicho na mfano, Hakikatul Wahyi. Anasema:

> "Siku zile zilikuwa za wasiwasi sana kiasi hiki kwamba tukawa sawa na aya ضَاقَتْ عَلَيْهِمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ . Ikaja shida bila sababu. Kwa hiyo dua iliombwa kwa Mungu na msaada ukaombwa Kwake.

[347] Al Hakam, 17 Agosti 1901

Ndipo baada ya dua ulifunuliwa ufunuo ufuatao:

اَلرَّحٰی تَدُوْرُ وَیَنْزِلُ الْقَضَآءُ۔ اِنَّ فَضْلَ اللّٰہِ لَاٰتٍ وَّلَیْسَ لِاَحَدٍ اَنْ یَّرُدَّ مَا اَتٰی۔ قُلْ اِیْ وَ رَبِّیْٓ اِنَّہٗ لَحَقٌّ۔ لَّا یَتَبَدَّلُ وَلَا یَخْفٰی۔ وَیَنْزِلُ مَا تَعْجَبُ مِنْہُ۔ وَحْیٌ مِّنْ رَّبِّ السَّمٰوٰتِ الْعُلٰی۔ اِنَّ رَبِّیْ لَا یَضِلُّ وَلَا یَنْسٰی۔ ظَفَرٌ مُّبِیْنٌ۔ وَّاِنَّمَا یُؤَخِّرُھُمْ اِلٰٓی اَجَلٍ مُّسَمًّی [348]

Tafsiri: "Kinu kitazunguka, na kadiri itateremka, yaani sura ya kesi itageuka, kama vile kinu kinapozunguka sehemu ya mbele inaenda nyuma na kwa sababu ya mzunguko inafichika, na ile sehemu iliyofichika inakuja mbele. Muradi wake ni huu kwamba hali ya hivi sasa ya kesi iliyopo mbele ya Hakimu ambayo ni yenye kutudhuru, hali hiyo haitabaki na hali nyingine itazalika itakayotufaa... Vile vile mambo yaliyofichika yatakuja mbele na yatadhihirika, na yaliyo dhahiri hayatajaliwa bali yatafichika. Kisha akasema kwamba hii ni fadhili ya Mungu iliyoahidiwa, hiyo lazima itatimia, mtu yeyote hana uwezo wa kuibatilisha... Kisha akasema 'Naapa kwa Mungu wangu kwamba hilo ni jambo la kweli. Hakuna hitilafu itakayotokea katika jambo hilo, wala halitabaki katika uficho. Na jambo fulani litatokea litakalokustaajabisha. Huu ni wahyi wa Mungu Aliye Mungu wa mbingu za juu. Mungu wangu Haiachi njia hii iliyonyoka. Ni Yule ambaye anao uhusiano na watumishi wake walioteuliwa; na Hasahau watumishi wake wanaostahiki kusaidiwa. Basi, utapata ushindi ulio wazi katika kesi hii, lakini kuna taahira katika uamuzi huo hadi wakati Aliouweka Mungu."

Baada ya kuandika ufunuo wote, Hudhur[as] anasema:

"Utabiri huo ulifanyika wakati ambapo wapinzani walisema kwamba kwa yakini kesi itafutwa. Na wakasema juu yangu kwamba kwa kujenga ukuta mbele ya milango yote ya nyumba yake tutamwudhi kiasi hiki kana kwamba atafungwa katika jela. Na kama nilivyoandika sasa hivi, Mungu Amebashiri katika utabiri huo kwamba nitadhihirisha jambo fulani ambalo kwa sababu yake ashindwaye atashinda, na ashindaye atashindwa...

[348] Haki katul Wahyi, uk. 268

Kisha ikajia siku ya hukumu. Siku hiyo wapinzani wetu walikuwa na furaha kwamba leo hukumu itatolewa ya kufuta kesi. Na wakasema kwamba tangu leo tutapata nafasi ya kumpatia udhia wa kila aina. Ilikuwa ni siku hiyo hiyo ya kueleweka maana ya maneno ya bishara ile kwamba kuna jambo fulani la siri litakalopindua kesi, nalo litadhihirishwa mwishoni. Basi, kwa bahati tu siku ile wakili wetu Khwaja Kamaluddin alipata wazo kwamba yapasa kuona faharisi ya faili ya zamani, yaani nyongeza ambamo mnakuwa na muhtasari wa amri za muhimu. Alipoiona, lilipatikana jambo ambalo halikutarajiwa, yaani ilipatikana amri hii iliyosadikishwa na Hakimu kwamba ardhi hiyo sio imemilikiwa na Imamuddin pekee bali na Mirza Ghulam Murtadhaa (yaani baba yangu) pia. Ndipo, kwa kuona hiyo wakili wangu alielewa kwamba tumeshinda kesi. Hakimu alipopata taarifa hiyo, mara moja aliagiza faharisi ile na kwa kuiona tu alipata uhakika ulivyo. Kwa hiyo bila kusita alitoa hukumu dhidi ya Imamuddin kuhusu ardhi pamoja na kutoa matumizi ya kesi."[349]

SHULE YA TA'LIMUL ISLAM ILIYOKUWA MPAKA DARASA LA NANE IKAFANYWA KUWA MPAKA DARASA LA KUMI, 1 FEBRUARI 1900

Tarehe 1 Februari 1900, shule ya Ta'limul Islam, iliyokuwa mpaka darasa la nane sasa ikafanywa mpaka darasa la kumi. Kisha katika Machi 1900 ilipendekezwa kuanzisha katika shule hiyo tawi la kufundisha dini pia.

HOTUBA YA KI-UFUNUO SIKU YA IDUL ADH-HA, 11 APRILI 1900, SAWA NA MWAKA 1317 HIJRIA

Siku ya Arafa, asubuhi na mapema, Hudhur[as] alimjulisha Maulana Hakim Haji Nuruddin kimaandishi kwamba nataka kutumia siku ya leo na sehemu kidogo ya usiku kwa kuomba dua. Majina na anuani za watu waliopo hivi sasa niletee ili wakati wa kuomba dua niwakumbuke. Amri hii ya Hudhur[as] ikatekelezwa, na orodha kubwa ya majina na anuani ilipelekwa kwa Hudhur[as]. Keshoye ilikuwa Idi.

[349] Hakikatul Wahyi, uk.269-272

Hadhrat Maulawii Abdul Karim Sialkoti wakati wa asubuhi alihudhuria mbele ya Hudhur[as] na akasema "Nimekuja hasa kwa kukuomba Hudhur, kwamba utoe hotuba ingawa ziwe sentensi chache." Akajibu kwamba "Mungu pia ametoa amri hii hii." Leo asubuhi nilifunuliwa, 'Toa hotuba katika mkusanyiko kwa Kiarabu, umepewa uwezo." Nilidhani mkusanyiko mwingine, labda ni mkusanykio huu. Vilevile nilifunuliwa: كَلَامٌ اُفْصِحَتْ مِنْ لَّدُنْ رَّبٍّ كَرِيْمٍ , Yaani, katika maneno haya mmejaaliwa ufasaha kutoka kwa Mungu."[350]

Hudhur[as] aliagiza kujumuika katika Masjid Aksa kwa sala ya Idi. Mpaka saa mbili asubuhi, sehemu ya ndani ya msikiti na uwanja wake ulijaa. Watu wapatao mia mbili walihudhuria. Hudhur[as] alikuja saa mbili u nusu. Hadhrat Maulana Abdul Karim alisalisha sala. Kwa kutoa hotuba Hudhur[as] alisimama katika mlango wa katikati wa msikiti. Alianza kutoa hotuba kwa lugha ya Kiurdu kwanza ambamo alieleza vizuri juu ya Islam kuwa ni dini iliyo hai. Hotuba ilikuwa bado haijaisha, Hadhrat Maulawii Abdul Karim akamwomba Hudhur kusema juu ya umoja wa Jumuiya pia. Basi, Hudhur[as] alitoa baadhi ya nasaha juu yake pia. Baada yake Hudhur[as] alisema kwamba sasa nataka kuzungumza katika lugha ya Kiarabu sawa na ufunuo wa Mungu. Maulawii Nuruddin na Maulawii Abdul Karim wakae karibu nami na waendelee kuandika maneno ya hotuba. Akitaja hotuba hiyo, Hudhur[as] anasema:

> "Kisha baada ya sala ya Idi nilisimama kutoa hotuba katika lugha ya Kiarabu. Na Mwenyezi Mungu Anajua kwamba nilipewa uwezo kutoka kwa ghaibu, na hotuba ile yenye ufasaha iliendelea kutoka mdomoni mwangu bila kujiandaa mapema katika Kiarabu iliyokuwa nje kabisa ya uwezo wangu. Na siwezi kufikiria kwamba hotuba ya aina hiyo kubwa mpaka ***juzu***[351] kadha kwa fasaha na balagha ya aina hii bila kuandika mapema kwenye karatasi, mtu yeyote duniani aweza kutoa bila ufunuo wa Mungu. Hotuba hiyo ya Kiarabu, iliyoitwa "Khutba Ilhamiah" (Hotuba ya Ki-ufunuo) ilipotolewa mbele ya watu,

[350] Al Hakam, 7 Aprili 1900

[351] *Juzu*: Sawa na istilahi ya zama zile, maana yake kurasa 16.

wakati ule watu walikuwepo pengine karibu mia mbili. *Subhanallahi*! Wakati huo chemchemi ya ghaibu ilikuwa inabubujika. Sijui kwamba mimi nilikuwa nasema au malaika alikuwa anasema kwa ulimi wangu, kwani nilijua kwamba sikuhusikana na maneno hayo. Sentensi zilizoundwa tayari zilikuwa zinatoka zenyewe ulimini mwangu, na kila sentensi ilikuwa ishara kwangu... Huu ni mwujiza wa kielimu Alioonyesha Mungu, hakuna yeyote awezaye kuleta mfano wake."[352]

Kurasa 38 za mwanzo za kitabu hicho kuanzia يَاعِبَادَاللّٰهِ فَكِّرُوْا hadi وَسَوْفَ يُنَبِّئُهُمْ خَبِيْرٌ ni za hotuba yenyewe. Na sehemu iliyobaki, Hudhur[as] aliiandika baadaye. Hudhur[as] alipomaliza hotuba, Hadhrat Maulawii Abdul Karim alisimama kuifasiri. Alipokuwa akifasiri, Hudhur[as] akaanguka katika sijida kwa jazba. Pamoja naye wahudhuriao wote walifanya sijida ya shukurani. Baada ya kuinua kichwa katika sijida, Hudhur[as] alisema:

"Sasa hivi nimeona neno 'Mubarak' lililoandikwa kwa herufu nyekundu, kana kwamba hii ni alama ya kukubalika."[353]

UCHAPAJI WA KHUTBA ILHAMIAH, 17 OKTOBA 1902

Kitabu hiki kina kurasa 204 kwa ujumla: kurasa 28 ni za hotuba yenyewe na ndio mlango wa kwanza. Baadaye Hudhur[as] aliongeza mlango wa pili na wa tatu. Katika hotuba yenyewe hekima ya dhabihu imeelezwa, na baadaye Hudhur[as] ametia mwangu juu ya madai yake.

CHANGAMOTO KWA ASKOFU WA LAHORE

Padre mmoja aitwaye Lefroy akipewa cheo cha Askofu aliwasili Lahore kutoka Ulaya. Mara baada ya kufika Lahore, alitangaza kutoa hotuba juu ya mada za "Nabii aliye maasumu" na "Nabii aliye hai", na akajasiri sana kuwapa Waislamu changamoto ya kushindana naye. Akatoa hotuba ya kwanza, tarehe 18 Mei 1900, juu ya "Nabii

[352] Hakikatul Wahyi, uk.362-363

[353] Al Hakam, J. 4, Na. 16, ya tarehe 1 Mei 1900

maasumu" katika Foreman Chapel, Anarkali, Lahore. Katika hotuba hiyo kwa msingi wa Hadithi na tafsiri zisizotegemewa alijaribu kuthibitisha kwamba manabii wote walikuwa wenye dhambi isipokuwa Bwana Yesu. Akawaita Waislamu kwamba kama yupo mtu yeyote mshupavu, basi ajitokeze. Maulamaa waliokuwepo mkutanoni walitoka mkutanoni wakisoma la haula! Kwa bahati mkutanoni humo alikuwepo mpenzi wa Uahmadiyya, Hadhrat Mufti Muhammad Sadik. Ghera yake ingewezaje kuvumilia kwamba Bwana Askofu awaite Waislamu kushindana naye, kisha aondoke mkutanoni kwa shamrashmra za ushindi wake. Mara moja yeye akasimama na akasema kwa sauti kubwa, "Bwana padre, hoja ulizotoa kutoka Injili kwa kuthibitisha kwamba Bwana Yesu hana dhambi haziwezi kukubaliwa na mtafiti yeyote, kwani Injili hizi ni maandishi ya wafuasi wake, na wafuasi daima husifu tu. Lakini, kama ipo kauli ya Bwana Yesu mwenyewe kwa kuthibitisha umaasumu wake, hiyo kweli itakubaliwa. Basi, tunapoona Injili, Bwana Yesu anasema kwa kujibu kauli ya mfuasi wake mmoja kwamba "Mbona unaniita mwema? Hakuna aliye mwema ila baba Aliye mbinguni." Imejulikana kwamba hakujiona bila dhambi. Lakini Mtume wetu s.a.w. lazima hana dhambi, kwani Mwenyezi Mungu Alimwambia: وَاللّٰهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ yaani miongoni mwa watu wewe ndiwe tu uliye maasumu." Bwana padre alifadhaika kwa kusikiliza dalili ya Bwana Mufti na kaondoka penye mkutano na kaenda zake.

Hudhur[as] alipojua habari za hotuba hiyo ya Bwana askofu, kwa kuijibu alichapisha tangazo moja[354] ambamo alimwita Bwana askofu kwa kujadili juu ya mada ya "Nabii maasumu". Na kaandika kwamba kuthibitisha kwamba nabii fulani hana dhambi hakuwezi kuleta matokeo mazuri, kwani katika ufafanuzi wa wema, dini kadha wanayo hitilafu kubwa kati yao. Kwa mfano:

> "Baadhi ya madhehebu yanaona kunywa pombe ni dhambi kubwa. Na sawa na itikadi ya wengine mpaka kipande cha mkate kiwekwe pombeni, na mfuasi mpya pamoja na wazee wa

[354] Someni tangazi "Ombi la uamuzi wa kweli kwa Bwana askofu wa Lahore," lililoandikwa tarehe 25 Mei 1900, uk. 18-19

dini ale huo mkate na anywe pombe ile, yeye hawezi kupata uthibitisho kamili kwamba amekuwa mtu wa dini... Naam, njia hii ni bora sana kwamba Hadhrat Isa[as] na Mtume Muhammad[saw] walinganishwe katika elimu, vitendo, hulka, utukufu, baraka, athari, imani, maarifa, kutoa heri, njia ya kuishi na mengineyo, na kuonyesha kuwa katika mambo hayo nani anathibitika kuwa mwenye fadhila na anamshinda mwenzake, na nani hathibitiki... Hata kama tukubali pia kwamba mataifa yote yanaeleza kwa usawa muradi wa umaasumu ─ ingawa haiwezekani kufikiri hiyo ─ hata hivyo, kwa sababu ya kuchunguza tu kwamba mtu fulani hanywi pombe, haibi, hanyanganyi, haui wala hatoi ushuhuda wa uongo, mtu kama huyo kwa kutokuwa na hatia za namna hii hawezi kuwa mtu mkamilifu wala hawezi kuwa mwenye wema wa kweli wa hali ya juu... Kuwasifu manabi kwa njia hii na kueleza mara kwa mara kuwa walikuwa maasumu na kuonyesha kwamba hawakutenda dhambi ni mbaya sana na kukosa adabu. Naam, pamoja na maelfu ya sifa njema kama zitajwe hizo pia, basi si vibaya... Kwa kumtambua mtu mkamilifu inapasa kuona kwa jiha ya heri, yaani alidhihirisha mema gani ya kweli na alikuwa na ukamilifu upi wa kweli moyoni, ubongoni na dhamirini mwake, na anazo sifa gani ndani mwake. Basi hili ni jambo ambalo kwa kuliweka katika mtazamo, yapasa kuchunguza sifa kamilifu na aina mbalimbali za heri za Bwana Yesu[as] na sifa kamilifu na mambo ya heri ya Mtume wetu s.a.w....”

Tangazo hilo la Hudhur[as] lilisambazwa katika Lahore na miji mingine na Bwana askofu pia alipelekewa tafsiri yake ya Kiingereza, na aliombwa kwa jina la Bwana Yesu[as] kwamba lazima akubali mjadala huo. Lakini, Bwana askofu alifadhaika kiasi hiki kwamba hata hakujibu kabisa, ilihali mwanzoni yeye ndiye aliyetoa changamoto. Kwa sababu mbili Bwana askofu aliogopa:

Ya kwanza ni kwamba katika tangazo hilo hoja madhubuti za fadhila za Mtume Mtukufu[saw] zilitolewa na umaasumu wa kiinjili wa Bwana Yesu ulibatilishwa.

Ya pili, siku ile Bwana padre alipopata changamoto hii ya Hudhur[as], yaani tarehe 25 Mei 1900, Bwana padre alikwishatangaza kutoa hotuba yake juu ya "Nabii aliye hai", na kama kawaida yake, aliwakaribisha Waislamu pia kushindana naye. Miongoni mwa masheikh wa Lahore, hakupatikana yeyote kwa kushindana na Dk. Lefroy. Waipendao Islam walimleta Maulawii Thanaullah kutoka Amritsar. Lakini badala ya kushindana naye, bwana Maulawii aliwakataza Waislamu wasiende kusikiliza hotuba ya padre. Waislamu waliona aibu sana kushindwa kwa masheikh wao na wakamwelekea Hudhur[as]. Hudhur kwa msaada wa Ruhul Qudus alikuwa ameishaandika makala moja mapema juu ya "Mtume aliye hai", kabla ya madhumuni yaliyotarajiwa ya Dkt. Lefroy. Na ni jambo la ajabu kwamba hotuba aliyotaka Bwana padre kutoa, jibu kamili la hoja zake lilikuwapo ndani ya madhumuni ya Hudhur. Basi Bwana padre alipomaliza hotuba yake, na Hadhrat Mufti Muhammad Sadik alipoanza kusoma makala ya Hudhur[as], wasikilizaji walishangaa kuona kwamba Bwana Mirza alijuaje hoja za Bwana padre mapema, ambazo alizivunja moja baada ya nyingine kwa taratibu. Bwana askofu na wenzake pia wakashikwa na butaa, kwani makala hiyo ilikuwa jibu kamili la hotuba yake.

Ilmuradi, kwa kupata changamoto ya Hudhur[as], Bwana askofu akatatanishwa sana, na akakataa kabisa kufanya mjadala. Hudhur[as] alipotangaza masharti ya mjadala ule, magazeti maarufu ya Kiingereza ya wakati ule ambayo wahariri wake pia walikuwa Waingereza, yalidhihirisha maoni ya kuvutia.

Pioneer liliandika:

> "Kama Dkt. Lefroy akikubali kushindana, bila shaka mjadala huu utapendeza sana."

1. Indian Spectator, gazeti maarufu la Kiingereza, liliandika:

> "Inaonekana kwamba Bwana askofu wa Lahore akiacha umakini, kwa haraka amekwepa changamoto ambayo yeye mwenyewe alitangulia kuitoa."

2. Indian Daily Graph pia katika maoni yake marefu liliandika:

> "Ni rai yetu kwamba Bwana askofu akikubali changamoto hiyo, itakuwa vizuri sana."

Vilevile likaandika:

> "Hatuwezi kuelewa pia kwamba Bwana askofu awezaje kuleta udhuru huu kwamba katika mjadala huu mzuri sehemu kubwa ya wakati wake itatumika. Anapaswa asikose nafasi hii ya kujibu wapinzani wake wa aina hii na kuwaridhisha. Hususan alipoombwa kuthibitisha kwamba kati ya dini mbili, Ukristo na Islam, dini ipi yaweza kuitwa dini iliyo hai. Na kati ya mafundisho ya Kurani Tukufu na Biblia, mafundisho ya kitabu gani ni bora zaidi na yanalingana na tabia ya asili ya binadamu. Tutapenda ikubalike changamoto hii, kwani taonavyo, mjadala huo utathibitika wa kuvutia sana."[355]

Ubovu wa sababu zote za kukimbia na kukataa kwa Bwana askofu Lefroy ulichapishwa baadaye kwa kirefu katika *Review of Religions* pia. Na wakati ule pia ilitiwa bidii kumhamasisha kukubali changamoto hiyo lakini kwa kuwa hakutaka kukubali, basi hakukubali.

TANGAZO LA KUTOA MCHANGO WA MANARATUL MASIHI, 28 MEI 1900

Tarehe 28 Mei 1900, kwa kutimiza kusudio la Hadithi za Mtume[saw], Hudhur[as] alipanga kujenga mnara upande wa mashariki wa Masjid Aqsa na akaeleza makusudio yake matatu:

La kwanza ni kwamba mwadhini akipanda juu yake atoe adhana mara tano kwa sala, na ili jina takatifu la Mungu litangazwe kwa sauti ya juu mara tano katika usiku na mchana, na ili kwa maneno machache mara tano tuwatangazie watu kwamba Mungu wa tangu azali na wa kudumu ambaye wanadamu wote wanapaswa kumwabudu ni Mungu yule tu ambaye Mtume Mteule na Mtakatifu Muhammad Mustafaa[saw] anaongoza kwake. Pasipo yeye hakuna Mungu yeyote ardhini wala mbinguni.

La pili: Kusudio la pili la mnara huu litakuwa kwamba kwenye

[355] Toleo la 19 Juni 1900

sehemu ya juu sana ya ukuta wa mnara huu, taa kubwa sana itawekwa… Mwanga huu utaenda mpaka mbali sana kwa kunurisha macho ya wanadamu.

La tatu: Kusudio la tatu la mnara huu litakuwa kwamba kwenye sehemu ya juu ya ukuta wa mnara huu, saa kubwa itawekwa, ili wanadamu wathamini nyakati zao na wanadamu waelekee kuzingatia wakati.

Kazi hizo tatu zitakazofanyika kwa mnara huu, ndani yake zimefichika hakika tatu:

Ya kwanza ni kwamba adhana itakayotolewa kwa sauti kubwa mara tano, ndani yake ukweli huu umefichika kwamba sasa kwa kweli wakati umewadia kuwa sauti ya لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ ifikie kila sikio. Yaani, sasa wakati wenyewe unasema kwamba Mungu wa azali na wa kudumu Aliye hai Ambaye kwake Mtume Mtukufu Muhammad[saw] ameongoza, minghairi yake miungu wote waliobuniwa ni batili. Kwa nini ni batili? Kwa sababu wanaowaamini hawawezi kupata baraka yoyote kwao wala hawawezi kuonyesha ishara yoyote.

Ya pili: Taa ile itakayowekwa kwenye ukuta wa mnara huu, ndani yake kuna ukweli huu kwamba watu watambue kuwa zama za mwanga wa kimbingu zimefika. Na kama vile ardhi ilivyosonga mbele katika uvumbuzi wake, ndivyo mbingu pia ulivyotaka kwamba udhihirishe nuru zake wazi wazi sana, ili kwa watafutao ukweli zije tena siku za kustawi, na kila jicho liwezalo kuona na lione mwanga wa kimbingu, na kwa mwanga huo asalimike na makosa.

Ya tatu: Saa ile itakayowekwa kwenye sehemu fulani ya ukuta wa mnara huu, ndani yake ukweli huu umefichika kwamba ili watu watambue wakati wao. Yaani waelewe kwamba wakati wa kufunguliwa milango ya mbingu umewadia. Tangu sasa jihadi ya kiardhi imefungwa na vita vimekwisha.[356]

[356] *Tablighe Risalat,* J. 9, uk. 35-36, Tangazo la 28 Mei 1900

KUWEKA JIWE LA MSINGI WA MANARATUL MASIHI, MWAKA 1903

Mchango kiasi fulani kwa ajili ya Manaratul Masihi ulikusanyika, lakini kwa shughuli zingine ujenzi wake ulichelewa, mpaka katika mwaka 1903 Hudhur[as] aliweka jiwe la msingi wake. Kuta zake zilipoanza kuinuka kidogo, wapinzani walianza kupeleka malalamiko kwa maafisa kwamba faragha yetu ya nyumbani itaathirika, kwa hiyo inapaswa ujenzi wake ukomeshwe. Disii wa Gurdaspur alimwagiza Mkuu wa tarafa ya Batala kufanya utafiti.

Mkuu wa tarafa akaja kumwona Hudhur[as], na wenye kushtaki pia waliitwa. Lakini, kwa sababu ya hisani za Hudhur[as] juu yao hata mtu mmoja hakuweza kusema wazi wazi kwamba wakati fulani nilisumbuliwa na Hudhur[as]. Lakini juu ya hayo kwa sababu ya uadui wa Islam, Mkuu wa tarafa alituma taarifa iliyo kinyume cha uhakika. Kwa kuijibu ikaandikwa tena kwamba juu ya mnara huu adhana pekee itatolewa na hautakuwa mahali pa kutembelewa na watu. Hapo, Bwana Disii akaruhusu ujenzi. Lakini ujenzi wake haukuweza kukamilika katika uhai wa Hudhur[as], bali katika zama za Hadhrat Khalifatul Masihi wa pili *Mungu Amsaidie,* kazi hiyo ilikamilika. *Alhamdulillahi.*

FATUWA YA KUKATAZA JIHADI YA UPANGA, 7 JUNI 1900

Kwa kuwa katika zama hizo masharti ya jihadi ya upanga hayakuwepo, kwa hiyo Hudhur[as] alichapisha katika shairi lake la Kiurdu fatuwa ya kuahirisha jihadi ya upanga sawa na Hadithi ya Mtume[saw]. Beti chache za fatuwa hiyo ndizo zifuatazo:

> Enyi marafiki, sasa acheni mawazo ya jihadi, sasa kwa ajili ya dini vita na mapigano ni haramu.
>
> Kwa nini mnasahau habari ya يضع الحرب . Je, hiyo haimo katika Bukhari, tazameni kwa kukifungua.
>
> Kiongozi wa dunia na akhera, Muhammad Mustafaa[saw] ameshasema kwamba Isa Masihi ataahirisha vita.[357]

[357] Kutoka tangazo la 5 Juni 1900

Pahali pengine Hudhur[as] ameandika wazi wazi kwamba

لَا شَكَّ اَنَّ وُجُوْهَ الْجِهَادِ مَعْدُوْمَةٌ فِيْ هٰذَا الزَّمَنِ وَفِيْ هٰذِهِ الْبِلَادِ[358]

"Yaani, hakuna shaka kwamba katika zama hizi na katika nchi hii masharti ya jihadi yameadimika."

Kwa vile baadhi ya watu wakieleza visivyo fatuwa hiyo walipiga makelele sana kwamba Hudhur[as] ameharamisha jihadi kwa kudumu, kwa hiyo Hudhur[as] na mahadimu wake walilazimika kujibu mara kwa mara kwa kirefu.

CHANGAMOTO KWA PIR MEHR ALI SHAH GOLARAWII KWA KUMKABILI HUDHUR[AS] ILI KUANDIKA MAELEZO YA KURANI, 20 JULAI 1900

Golra ni mji ulio mbali maili chache kutoka Rawalpindi ambapo Sajjada Nashiin Pir Mehr Ali Shah Golarawii alikuwa akiishi. Katika maeneo ya mipakani. Pir huyo alikuwa maarufu sana. Yeye aliandika kitabu "Shamsul Hidaya" kupinga madai ya Hudhur[as] ambamo alijaribu kutoa hoja nyingi ya kuthibitisha "uhai wa Masihi" na kupinga "kifo cha Masihi". Kitabu hicho kwa njia fulani kilimfikia Hudhur[as] pia. Kwa vile katika kitabu hicho haikuwa dalili yoyote mpya, hoja zilikuwa zile zile ambazo alizijibu mara kwa mara katika vitabu vyake, kwa hiyo Hudhur[as] alimwita Bwana Pir kwenye uamuzi rahisi sana, nao ndio huu:

"Inathibitika kutoka katika Kurani Tukufu kwamba watu ambao kwa kweli ni watumishi wakweli wa Mwenyezi Mungu, hao wanapata msaada wa Mungu kwa njia tatu:

1. Kati ya hao na wengine huwekwa tofauti fulani, yaani upambanuzi. Kwa hiyo wakati wa mashindano baadhi ya mambo yasiyo ya kawaida yanadhihirika ambayo hayawezi kudhihirika na kundi la pili, kama aya hii ilivyo shahidi: وَيَجْعَلْ لَّكُمْ فُرْقَانًا
2. Wanajaaliwa elimu na maarifa ya Kurani, na wengine

[358] Tuhfa Golarwiyya, uk. 43

hawajaaliwi, kama aya hii ilivyo shahidi: لَا يَمَسُّهٗۤ اِلَّا الۡمُطَهَّرُوۡنَ

3. Maombi yao mengi yanakubaliwa, na ya wengine hayakubaliwi kiasi hicho, kama aya hii ilivyo shahidi wake: اُدۡعُوۡنِیۡۤ اَسۡتَجِبۡ لَکُمۡ

"Basi yafaa kwamba katika Lahore, ambayo ni makao makuu ya Panjab, mkutano ufanyike kwa kupambanua mkweli na mwongo. Na wafanye mjadala nami hivi kwamba tuchague kwa kupiga kura Sura yoyote ya Kurani Tukufu na kisha kuteua aya zake arobaini au Sura nzima (ikiwa haina aya zaidi ya arobaini). Kisha makundi yote mawili, yaani mimi na Bwana Mehr Ali Shah kwanza tuombe kwamba Ewe Mungu wangu, miongoni mwetu wawili yule aliye na ukweli, mjaalie uwezo wa kiroho kutoka Kwako kwa kuandika mkutanoni humu maelezo ya Sura hiyo, yenye maarifa ya ndani katika Kiarabu kwa fasaha na balagha, na msaidie kwa roho mtakatifu. Na kati yetu wawili yule mtu aliye kinyume na ridhaa yako na si mkweli mbele yako umnyanganye uwezo huo, na uzuie ulimi wake kutoa Kiarabu cha fasaha na yenye maarifa ya ndani, maelezo ya Kurani, ili watu watambue kwamba U pamoja na nani, na nani amekosa fadhili yako na usaidizi wako wa roho mtakatifu.

Kisha baada ya dua hiyo wote wawili waanze kuandika maelezo yake kwa lugha ya Kiarabu. Na sharti ya lazima litakuwa kwamba yeyote asiwe na kitabu chochote wala msaidizi yeyote. Na itakuwa lazima kwamba kila mmoja aandike kwa mkono wake akiwa kimya bila kutoa ili mwenzake asiweze kunukuu au kuiba maneno yake kwa kusikiliza maandishi ya fasaha na maelezo yake ya maarifa. Na kwa kuandika maelezo hayo, kila mmoja atapewa muda wa masaa saba kamili, na italazimika kuandika kukaa ana kwa ana pasipo pazia katikati... Wote wawili watakapomaliza kuandika, basi maelezo hayo ya pande zote mbili baada ya kutiwa saini ya wanachuoni watatu ambao kuwachagua na kuwaleta kutakuwa ni jukumu la Bwana Mehr Ali Shah, yatasomwa. Na itakuwa kazi ya hao masheikh watatu kwamba watoe maoni yao kwa kuapa kwamba kati ya maelezo

haya na maandishi haya mawili ya Kiarabu, maelezo gani na maandishi yapi yameandikwa kwa usaidizi wa roho mtakatifu. Na itakuwa lazima kwamba kati ya hao mashikh watatu, yeyote asiwe mwanajumuiya wangu wala mfuasi wa Bwana Mehr Ali Shah. Nami nakubali kwamba kwa ushahidi huo Pir Meh Ali Shah achague Maulawii Muhammad Husain Batalawii, Sheikh Abdul Jabbar Gaznawii na Sheih Abdullah Profesa Lahori, au masheih wengine watatu ambao wasiwe wafuasi wake, lakini itakuwa lazima kwamba masheikh hao watatu watoe maoni yao kwa kuapa kwamba maelezo na ibara ya Kiarabu ya nani ni ya hali ya juu na imeandikwa kwa usaidizi wa Mungu… Basi kwa mjadala wa aina hiyo na kwa ushahidi wa masheikh watatu na aina hiyo ikithibitika kwamba kwa kweli Bwana Mehr Ali Shah katika kuandika maelezo ya Kurani na kuandika Kiarabu yu kama watu waliosaidiwa na Mungu, nami sikuweza kufanya kazi hiyo, au mimi pia niliweza lakini yeye pia alifanya kunikabili, basi dunia yote iwe shahidi kwamba nitakiri kwamba ukweli upo kwa Bwana Pir Mehr Ali Shah. Na katika hali hiyo, nakiri pia kwamba nitachoma vitabu vyangu vyote vinavyohusikana na madai hao, na nitajitambua sikusaidiwa na Mungu na nimekataliwa... Lakini, kama Mungu wangu Alinishindisha katika mjadala huo na mdomo wa Bwana Mehr Ali Shah ulifumbwa, hakuweza kuandika Kiarabu cha fasaha wala hakuweza kuandika maelezo ya maarifa ya ndani ya Sura ya Kurani, au akikataa kukubali kufanya mjadala huo, basi katika hali hizo zote atawajibika kwamba akitubu afanye baiati yangu. Na itakuwa lazima kwamba achapishe ikrari yake kwa maneno wazi kwa njia ya tangazo katika muda wa siku kumi.” [359-360]

JIBU LA BWANA PIR MEHR ALI SHAH

Bwana Pir Mehr Ali Shah aliposoma tangazo hilo, alipata wasiwasi

[359] Baadaye Hudhur[as]aliongeza muda huo na kufanya mwezi mmoja. Someni Dhamima ya tangazo la mwito kwa Pir Mehr Ali Shah Golarawii ndani ya *Tablighe Risalat*, J. 9

[360] Kutoka tangazo la 20 Julai 1900

sana, kwani alikuwa hana elimu kiasi cha kuwa tayari kushindana, wala hakuwa na mategemeo ya kukubalika kwa Mungu kwamba kwa msingi huo angejasiri kushindana. Lakini alikuwa akiitwa ***sajjada nashin,*** Sufii mkubwa na walii, kwa hiyo kukana wazi wazi kungetia doa baya katika Usufii wake na elimu yake. Kwa hiyo, alifanya hila fulani ambayo kwa njia yake bila kushindana afanikiwe. Na hila ile ilikuwa hii kwamba alimwandikia Hudhur[as] kwamba nakubali masharti yako, lakini kwanza inapaswa tujadili itikadi zako sawa na Kurani na Hadithi. Kisha kama Maulawii Muhammad Husain Batalawii na wenzake masheikh wawili wakitoa rai kwamba katika majadiliano hayo wewe si juu ya haki, basi utalazimika kufanya baiati yangu. Kisha baada yake ushindane pia katika kuandika maelezo ya Kurani pia.[361]

Ni dhahiri kwamba hiyo ilikuwa hila moja ya kuepa shindano la kuandika maelezo ya Kurani, aliyotumia Bwana Pir kwa kuwapumbaza wafuasi wake. Waila kila mtu anaweza kuelewa kwamba kuhusu itikadi ingekuwa maana gani Hudhur[as] kukubali Maulawii Muhammad Huasain na masheikh wenzake kuwa waamuzi. Kuhusu itikadi, watu hao wakamkufurisha mapema sana wakaishatoa uamuzi wao; sasa wangewezaje kusema kinyume cha itikadi zao! Lakini katika shindano la kuandika maelezo ya Kurani lilikuwa ni sura tofauti sana. Waliweza kuapa juu ya itikadi zao mbovu bila kusita walizodhania kuwa sahihi, lakini kati ya maelezo mawili, maelezo yale yanayoshinda, kuficha ushindi wake na kudhihirisha rai tofauti, kulikuwa ni jambo la kuaibika kielimu machoni mwa wenye elimu wengine, kwa hiyo hawangeweza kutoa rai isiyo sahihi kuhusu maelezo hayo. Zaidi ya hayo, Bwana Pir alijua hii pia kwamba Hudhur[as] alikwishaahidi katika kitabu chake "Anjame Atham" kwamba tangu sasa hatajadiliana na masheikh wa wakati ule, basi angewejaze kuvunja ahadi yake hiyo!

Kisha jambo hili kiakili ni mbali kiasi gani alilosema Bwana Pir kwamba baada ya mjadala juu ya itikadi waombe masheikh wapinzani watoe uamuzi. Kisha wakiamua dhidi yako, basi tubu na fanya baiati

[361] Kutoka tangazo la 25 Agosti 1900 yaliyomo katika *Tablighe Risalat*, J. 2

yangu na baada yake ushindane nami katika maelezo ya Kurani. Katika hali hii kwamba baada ya masheikh wapinzani kudhihirisha rai dhidi ya Hudhur[as], yeye atakapochoma vitabu vyake vyote na kufanya baiati, nafasi gani na wakati gani unabaki wa kushindana katika kuandika maelezo ya Kurani. Na shindano la kuandika maelezo huwa kwa shabaha gani? Je mtu akiwa mfuasi aweza kufanya mjadala na kiongozi wake? Bwana Pir amefahamu kwamba ameishajitafutia udhuru mzuri wa kuhepa kuandika maelezo ya Kurani, lakini wenye kufahamu, hata wakihuzunika namna gani kuhusu "pendekezo" lake hili, ni kidogo tu.

UJANJA MWINGINE WA BWANA PIR

Bwana Pir alipoona kwamba haiyumkiniki kushindana katika kuandika maelezo ya Kurani na ni lazima kutunza heshima na umaarufu wake pia katika wafuasi wake, hasa wafuasi wa mipakani, kwa hiyo katika Lahore akaeneza kwamba tumeshakubali masharti yote ya Bwana Mirza na tutakuja Lahore kwa kujadili naye lakini si kimaandishi, ilihali miaka minne kabla katika "Anjame Atham" Hudhur[as] aliahidi kwamba sasa hatafanya mijadala kwa mdomo kwani ni bure tu. Lakini Bwana Pir alihitaji umaarufu usio na thamani. Wafuasi wake walitangaza tangaza katika mitaa ya Lahore ujio wa Bwana Pir. Na walipiga makelele kuwachochea watu dhidi ya Hudhur[as] na Jumuiya yake, na wakawachochea watu kuwapinga Waahmadiyya. Kama moyoni mwa Bwana Pir na wafuasi wake ingekuwa hofu ya Mwenyezi Mungu hata kidogo, wasingetangaza uongo kama huu kwamba Hudhur[as] amekubali mjadala kwa mdomo. Hudhur[as] alimkaribisha kwa kushindana katika kuandika maelezo ya Kurani, lakini wafuasi wake hawaitaji hata kidogo habari hii.

UJIO WA BWANA PIR KATIKA LAHORE, 24 AGOSTI 1900

Bwana Pir alijua vizuri kwamba Hudhur[as] amemwita kwa kushindana katika kuandika maelezo ya Kurani, na hii pia alijua vyema kwamba kwa kuacha kutaja shindano la kuandika maelezo ya Kurani, amenasibisha kwa Hudhur[as] kwamba yeye amekubali kufanya mjadala kuhusu itikadi, jambo ambalo ni kinyume cha hakika kabisa. Akajua pia kuwa Hudhur[as] hatakubali kujadili juu ya itikadi kwa

sababu zilizoandikwa juu, na badala ya kushindana katika kuandika maelezo ya Kurani, kwa kufanya mjadala juu ya itikadi, ambao ameishauacha kabisa, hatakuja katu Lahore. Kwa hiyo, pamoja na wafuasi wake wengi yeye alifika Lahore tarehe 24 Agosti 1900, na alianza kumtupia Hudhur[as] mwito kwamba njoo ujadili nami juu ya itikadi, ilihali Hudhur[as] alitoa changamoto ya kumkabili kuandika maelezo ya Kurani, na hakutaja mjadala kwa mdomo. Waahmadiyya wa Lahore walipoona kwamba watu hao wakifanya propaganda ya uongo wanawachochea watu kwa kuwadanganya, basi walichapisha tangazo moja tarhe 24 Agosti 1900, kwa kueleza ukweli ambamo kwa kuweka wazi ukweli wakaandika:

> "Kama Bwana Pir amekubali mwito wa shindano la Bwana Mirza na masharti yake, basi kwa nini wafuasi wake hawamfanyi Bwana Pir atoe mwenyewe tangazo lake kwa maneno waziwazi kwamba nakubali kushindana katika kuandika maelezo ya Kurani sawa na tangazo la Bwana Mirza bila kupunguza au kuzidisha chochote."

BARUA KWA BWANA PIR

Bwana Pir na wafuasi wake wasipotoa jibu lolote la tangazo hilo pia, keshoye, 25 Agosti 1900, Hadhrat Hakim Fadhl Ilahi na Hadhrat Mian Merajuddin Umar walimwandikia Bwana Pir barua ambayo madhumuni yake ilikuwa kwamba uandike kwa maneno waziwazi kwamba Hadhrat Mirza katika tangazo la tarehe 20 Februari 1900 alitoa changamoto kwa kushindana katika kuandika maelezo ya Kurani, nami nipo tayari kwa shindano hilo. Na twakuomba kwa kukuapisha mara elfu kwa adabu sana kwamba sawa na changamoto aliyokutolea Hudhur[as] kwa kushindana katika kuandika maelezo ya Kurani, ushindane na Hudhur[as] ili uamuzi kati ya haki na batili upatikane. Kama ukitoa udhuru wowote au ukifuatilia mambo mengine ukiacha habari za shindano la kuandika maelezo ya Kurani au hukujibu ombi letu, basi itadhihirika kwamba hutaki kubatilisha batili na kuhakikisha haki, bali unataka kudanganya watu na kukataa katakata ukweli.

KIMYA CHA BWANA PIR

Bwana mmoja asiyekuwa Mwahmadiyya, Mian Abdur Rahim, msimamizi wa Soko, alimpelekea Bwana Pir barua hiyo. Ulikuwa ni wakati wa adhuhuri. Bwana Pir alisema atajibu baada ya Alasiri. Bwana msimamizi alipokwenda baada ya Alasiri, wafuasi wake hawakumruhusu kumwona Bwana Pir. Tarehe 26 Agosti 1900, wanajumuiya walimtumia Bwana Pir barua ya rejista iliyo na madhumuni hiyo, lakini Bwana Pir alikataa kuipokea. Hapo tangazo lilitolewa na Jumuiya kuhusu madhumuni hii hii kwamba Bwana Pir hajakubali mpaka sasa masharti ya Bwana Mirza wala hajamtumia Bwana Mirza telegramu yoyote wala hajamfikishia tangazo lolote la kibali chake. Yanayotangazwa ni uongo mtupu. Lakini ni masikitiko kwamba Bwana Pir hakujibu hata tangazo hilo pia. Katika muda huo tangazo la Hudhur[as], la 25 Agosti 1900, pia likafikia Lahore lililochapishwa mara moja. Hata hivyo Bwana Pir hakuwa tayari kwa kuandika maelezo ya Kurani, lakini wafuasi wake waliendelea kushughulika katika kueneza uchochezi na kuwadanganya wasiojua.

KUTIMILIZA HOJA YA MWISHO JUU YA BWANA PIR

Kutimiliza hoja ya mwisho, tarehe 28 Agosti 1900, Hudhur[as] alichapisha tangazo lingine ambamo aliandika kwamba kwanza Bwana Pir anapaswa kukubali shindano la kuandika maelezo ya Kurani, lakini kama hawezi kujipa moyo kwa shindano kama hilo, hapo namwita kwenye njia nyingine ya uamuzi kwa kutimiliza hoja ya mwisho, nayo ndiyo:

> "Niruhusiwe kwamba katika hadhara … kwa masaa matatu nieleze madai yangu na hoja zake mbele ya watu. Bwana Pir Mehr Ali Shah hataingilia kati. Nitakapomaliza hotuba yangu, Bwana Mehr Ali Shah ainuke na yeye pia kwa masaa matatu, awahutubie watu na kuthibitisha kwamba kwa kweli sawa na Kurani na Hadithi inathibitika hii tu kwamba Masihi atakuja kutoka mbinguni. Kisha, baada yake watu watalinganisha wenyewe hotuba zote mbili."

BWANA PIR KAREJEA GOLRA

Kuhusu Bwana Pir Golarawii ilijulikana kwamba atakaa Lahore mpaka Ijumaa, kwa hiyo wasomi wa Lahore walisisitiza kwamba Bwana Pir asalishe sala ya Ijumaa katika Shahi Masjid, na hapo awahutubie watu wote. Ombi hilo lilipozidi, Bwana Pir aliyejua elimu yake, akaona afadhali arudi Golra siku moja kabla ya Ijumaa. Ukweli wenyewe ni kwamba yeye aliweza kutoa hotuba baina ya watu wa kawaida, lakini hakuweza kuwahutubia walioelimika na waheshimiwa. Kwa sababu ya kuondoka kwake siku moja mapema, hata tangazo la Hudhur[as] pia halikuweza kufikishwa kwake, kwa hiyo nakala tatu za tangazo akapelekewa Golrha kwa njia ya posta kwa rejista. Na pia ikaandikwa kwamba kama akija Lahore kwa shindano la aina hiyo, basi atapewa nauli ya garimoshi, ya daraja ya pili, na mahadimu wake wawili nauli ya daraja ya kati, lakini hakujibu kabisa. Na akajivunia na kufurahia uwongo na uchochezi aliokwisha eneza.

UANDISHI WA IJAZUL MASIHI

Pir Mehr Ali Shah Golarawii asipokuwa tayari kwa njia yoyote kwa kushindana katika kuandika maelezo ya Kurani, basi kwa kutimiza hoja juu yake, Hudhur[as] alimtolea pendekezo lingine ambalo ni hili:

"Leo hii limetiliwa na Mwenyezi Mungu moyoni mwangu pendekezo ninalotoa kwa kutimiza hoja. Nami nina yakini kwamba kwa njia hii uhakika wa Pir Mehr Ali Shah utadhihirika, kwani watu wote sio vipofu. Miongoni mwao wako watu ambao wanao uadilifu. Na njia yenyewe ni hii kwamba matangazo yote yanayotolewa mfululizo kwa kumwunga mkono Pir Mehr Ali Shah, leo nayajibu hayo yote kwamba kama kwa kweli Pir Mehr Ali Shah ni mtaalamu asiye na kifani katika elimu ya maarifa ya Kurani, fasaha na balagha ya Kiarabu, basi ni yakini kwamba mpaka sasa uwezo wote huu bado anao, kwani tangu alipofika Lahore muda mrefu haujapita. Kwa hiyo, napendekeza kwamba mimi mwenyewe nikiandika maelezo ya Suratul Fatiha katika Kiarabu chenye ufasaha nithibitishe madai yangu, na nieleze maarifa na elimu ya ndani ya Sura hiyo pia. Na Bwana Pir athibitishe kinyume changu kutoka katika sura hiyo ujaji wa Masihi atakayekuja kutoka mbinguni na Mahdi mmwagaji damu.

Na kwa njia yoyote akitaka atoe kutoka katika Suratul Fatiha kinyume changu dalili madhubuti na maarifa yang'aayo, katika Kiarabu chenye ufasaha na balagha. Vitabu hivyo viwili vichapishwe katika siku 70 kuanzia tarehe 15 Desemba 1900. Ndipo wenye elimu wenyewe watavilinganisha. Na kama miongoni mwa wataalamu, watu watatu walio waandishi na ambao lugha yao ni Kiarabu wasiohusika na pande zote mbili, wakisema kwa kuapa kwamba kitabu cha Bwana Pir kinashinda katika fasaha na balagha na kwa elimu ya ndani ya Kurani, basi nafanya ahadi sahihi kisheria kwamba nitamkabidhi Bwana Pir bila kusita rupia mia tano taslimu. Na kwa njia hii, ule usumbufu utaondolewa wanaolalamikia kila siku wafuasi wa Bwana Pir kwamba Bwana Pir alisumbuliwa bila sababu kufika Lahore."[362]

Katika tangazo hilo, mbele Hudhur[as] anaandika:

> "Twamruhusu kwamba awaite Maulawii Muhammad Husain Batalawii, Sheikh Abdul Jabbar Ghaznawii, Muhammad Hasan Bhiin na kadhalika. Bali ana hiari ya kuwakaribisha waandishi wachache Waarabu kwa kuwatamanisha kidogo. Maelezo ya Kurani ya pande zote mbili yasipungue ***juzu***[363] nne. Na kama katika muda uliopangwa, yaani kuanzia 15 Desemba 1900 hadi 25 Februari 1900, ambao ni siku 70, yeyote kati ya wawili hachapishi maelezo ya Suratul Fatiha na siku hizi zenyewe zipite, basi huyo ataonekana mwongo, na haitahitajika dalili nyingine yoyote kuhakikisha kuwa yu mwongo."

UCHAPAJI WA IJAZUL MASIHI, 20 FEBRUARI 1901

Sawa na tangazo hilo, Hudhur[as] alichapisha kitabu chake maarufu Ijazul Masihi tarehe 20 Februari 1901 katika muda uliokuwa umewekwa. Ndani yake alitoa maelezo yaliyojaa maarifa ya ndani ya Suratul Fatiha kiasi hiki kwamba wanachuoni wakubwa wakikisoma wanapata ladha ya kiroho na wanastaajabika. Wasomaji wa kitabu hicho wanajua kwamba kwa yakini kitabu hicho kimeandikwa kwa msaada wa Mungu. Ni la ajabu kwamba kwenye ukurasa wa nje wa

[362] Kutoka katika tangazo la 15 Desemba 1900

[363] *Juzu* moja yamaanisha kurasa 16, sawa na istilahi ya zama zile.

kitabu hicho, yeye aliishaandika kwa yakini kwamba:

فَإِنَّهٗ كِتَابٌ لَيْسَ لَهٗ جَوَابٌ فَمَنْ قَامَ لِلْجَوَابِ وَتَنَمَّرَ فَسَوْفَ يَرٰى اَنَّهٗ تَنَدَّمَ وَتَذَمَّرَ

Yaani, Hiki ni kitabu ambacho mtu yeyote hataweza kuandika jibu lake. Na mtu yeyote atakayanuia kukijibu na kujitayarisha, atajuta na atadhalilika.

Na kwenye kurasa 66, 67 za kitabu hicho imeandikwa dua yake moja ifuatayo:

"Nilimwomba Mwenyezi Mungu kwamba Akifanye kitabu hiki (Ijazul Masihi) kuwa mwujiza kwa maulamaa, na kwamba mwandishi yeyote asiweze kuleta mfano wake wala hao wasipate uwezo wa kuuandika. Na dua yangu ilikubaliwa na Mwenyezi Mungu usiku uo huo. Nami nikaona ruya ya habari njema, na Mungu wangu Akanipa bishara na Akasema kwamba مَنَعَهٗ مَانِعٌ مِّنَ السَّمَآءِ , yaani atakayejitokeza kushindana, atazuiliwa kwa vizuizi vya kimbingu asiweze kushindana. Hapo, nikaelewa kwamba hiyo ni ishara kwenye jambo hili kwamba maadui hawataweza kuleta mithili yake, wala hawataweza kuonyesha mfano wa balagha, fasaha, hakika halisi na maarifa ya aina hiyo. Na bishara hiyo nilipewa katika kumi la mwisho la Ramadhani Tukufu."[364]

Baada ya kuchapishwa kitabu hicho, Pir Mehr Ali Shah akichagua sentensi chache za kitabu akaleta shutuma kwamba hizo zimeibiwa kutoka "*Makamate Hariri*", lakini mwenyewe hakuweza kuchapisha kitabu chochote kabisa. Naam, mfuasi wake mmoja, Sheikh Muhammad Hasan, mkazi wa Bhiin wilaya ya Jhelum, alianza kuandika jibu la "Ijazul Masihi". Lakini sawa na utabiri wa ukurasa wa nje wa "Ijazul Masihi", kabla ya kuandika kurasa chache katika kujibu maelezo ya Kurani, aliaga dunia. Kwa kuandika jawabu la kitabu cha Hudhur[as] "Ijazul Masihi", yeye alikuwa ameandika kumbukumbu zake pembeni mwa "Ijazul Masihi" na "Shamse Bazigha" cha Hadhrat Maulawii Muhammad Ahsan Amrohi. Na kwa

[364] *Ijazul Masihi,* uk. 66-67, tafsiri kutoka Kiarabu.

kukadhibisha mambo ya kweli aliyoeleza Hudhur[as], alikuwa ameandika لعنة الله على الكاذبين . Lakini bado ilikuwa haijapita hata wiki moja tangu kutuma laana, mwenyewe alishikwa na kifo cha laana.[365]

Pir Mehr Ali Shah alijua kumbukumbu za mfuasi wake alizoandika kwa kujibu "Ijazul Masihi". Kwa hiyo, aliagiza kwa kumtuma mfuasi wake fulani vitabu vyote viwili vilivyotajwa hapo juu ambamo aliandika kumbukumbu zake pembeni mwa kurasa zake. Na kwa kuzijumuisha alichapisha kitabu kiitwacho "Saife Chishtiyai", lakini katika kitabu chake hicho hakumtaja marehemu Sheikh Muhammad Hasan. Bwana Pir alimtumia Hudhur[as] kitabu hicho kwa posta ya rejista. Hudhur[as] akikitaja hicho alisema:

> "Kitabu hiki (Saife Chishtiai) nimepata 1 Julai 1902 kupitia posta, ambacho Pir Mehr Ali Shah Golarwii amenitumia labda kwa lengo la kunijulisha kwamba ameshaandika jibu la kitabu changu *Ijazul Masihi* na la *Shamse Bazigha*. Na kabla ya kufika kitabu hicho nilipata habari kwamba yeye anaandika kitabu kwa kushindana na Ijazul Masihi… Lakini ni masikitiko kwamba dhana yangu haikuwa sahihi. Nilipopata kitabu chake Saife Chishtiyai, kwanza nilifurahi kwa kukishika mkononi kwamba sasa tutaona maelezo yake kwa Kiarabu, na mbele yake heshima ya maelezo yetu itabainika zaidi kwa watu. Lakini nilipoona kitabu na nilikikuta kimeandikwa katika Kiurdu, na hayakuwepo maelezo yoyote ya Kurani, ndipo mara nikalia juu ya hali yake.[366]

BWANA PIR KAKIKOSOA *"IJAZUL MASIHI"*

Badala ya kuandika maelezo ya Suratul Fatiha katika Kiarabu fasihi kushindana na Hudhur[as], Bwana Pir alianza kuleta vipinzani vya aina hii kwamba katika kitabu hicho sentensi fulani zimeibiwa kutoka katika *Makamate Hariri* na kwamba wahyi wake ni aina ya ndoto zilizovurugika na ni kusema na nafsi. Hudhur[as] katika kitabu chake "*Nuzulul Masihi*" amejibu kwa urefu sana vipinzani hivyo viwili. Kwa

[365] Nuzulul Masihi, uk. 194

[366] Kwa maelezo zaidi someni *Nuzulul Masih*.

ufupi ni kwamba katika kitabu cha kurasa 200, kama sentensi 2-4 zilingane kwa bahati tu na zilizomo katika kitabu kingine pia kuna ubaya gani ndani yake. Mtu anayeweza kuandika maelfu ya kurasa katika Kiarabu fasihi ana haja gani anukuu sentensi chache kutoka katika kitabu kingine. Hii ni bahati inayopatikana mara nyingi katika vitabu fasihi vya waandishi wakubwa. Akatoa mifano kadha ya bahati ya aina hiyo.

Katika kujibu upinzani wa pili, ameandika madhumuni yenye maarifa ya hali ya juu, ya kurasa nyingi kwa kutofautisha "Neno la Mungu" na kusema na nafsi au ufunuo wa kishetani, yanayofaa kusomwa. Ni masikitiko kwamba kwa kufikiria kurefuka sana maandishi hatuwezi kuyaandika madhumuni yale hapa. Wasomaji waweza kuyasoma kuanzia ukurasa 85 wa "Nuzulul Masihi".

WIZI WA KIMAANDISHI WA BWANA PIR

Bwana Pir alimlaumu Hudhur[as] kwa wizi wa sentensi 2-4 katika kitabu chenye kurasa 200, ambao Hudhur[as] alijibu kwa fasaha sana. Lakini kuhusu Bwana Pir ilithibitika kwamba aliiba kitabu kizima na akakinasabisha kwake mwenyewe. Maelezo yake ni haya kwamba Hudhur[as] alikuwa ameshughulikia kuandika jibu la kitabu cha Bwana Pir, "Saife Chishtiyai" katika "Nuzulul Masihi", mara tarehe 26 Julai 1902 mtu mmoja Mian Shihabuddin wa Bhiin, wilaya ya Jhelum, alimwandikia barua kwamba nilikuwa nikiona kitabu cha Bwana Pir, kwa bahati mtu mmoja alionana nami, aliyekuwa na vitabu vichache na akauliza nyumba ya Sheikh Muhammad Hasan iko wapi? Na kwa kuulizwa sababu yake, alisema kwamba Bwana Pir alikuwa ameagiza vitabu vya Muhammad Hasan, nami sasa nimekuja kuvirudisha. Nilipoona vitabu hivyo, nikakuta kimoja kilikuwa ***Ijazul Masihi***, na cha pili ***Shamse Bazigha***, ambavyo marehemu Muhammad Hasan aliandika kumbukumbu zake juu ya hivyo kwa mkono wake. Na kwa bahati, wakati ule, nilikuwa nacho kitabu 'Saife Chishtiyai' pia. Nilipolinganisha kumbukumbu zile na kitabu kile, nilikuta kwamba aliyoandika Muhammad hasan, yote hayo neno kwa neno katika kitabu chake amenukuu Pir Mehr Ali kiwizi bila kubadilisha chochote. Bali, kwa maneno mengine inapaswa kusema kwamba

kitabu cha Pir Mehr Ali Shah ni zile zile kumbukumbu za kuibiwa, hamna mle zaidi ya hizo. Basi, nilishangaa sana kwa wizi huu na hiana hii kwamba alijasirije kunasibisha kwake kumbukumbu zile zote. Jambo hilo lilikuwa la aina hii kwamba kama Mehr Ali angekuwa na haya kidogo angejifia kwa kufichuliwa siri ya wizi kama huo badala ya kujasiri na kukosa haya, na kuyanasibisha kwake mpaka sasa maandishi ya mtu mwingine aliyekufa kwa sababu hiyo, asiashirie hata kidogo kwenye maandishi ya yule mfile mwenye bahati mbaya.[367]

Baada yake Hudhur[as] ameandika kwamba

> "Kisha, baada yake, Mian Shihabuddin anaandika kwamba kila mtu anayetaka kuona hiana hiyo ya Mehr Ali naweza kumwonyesha wizi huo wa aibu, bali ameleta barua moja iliyotiliwa sahihi ya Pir Mehr Ali Shah mwenyewe ambamo anakiri wizi huo. Lakini baada yake anatoa jibu hili bovu kwamba marehemu aliniruhusu katika uhai wake kwamba nichapishe kitabu kile kwa jina langu. Lakini udhuru huo ni mbaya zaidi kuliko kosa lenyewe. Kwani, kama yeye aliruhusu kwamba baada ya kifo chake, Mehr Ali ajidhihirishe kuwa mwandishi wa kitabu kile, basi kwa nini Mehr Ali hakutaja ruhusa ile katika kitabu hicho, na kwa nini alidai kwamba mimi ndimi niliyeandika kitabu hicho. Ni dhahiri shahiri kwamba hii ni njia ya hiana kuwa amekinasibisha kwake kitabu kizima cha mtu aliyefariki na hakutaja hata jina lake. Kama ambavyo Muhammad Hasan akishindana na Mwenyezi Mungu, sawa na utabiri ulioandikwa kwenye ukurasa wa nje wa ***Ijazul Masih*** اَنَّهٗ تَتَدَّمَ وَ تَذَمَّرَ alishindwa kiasi hiki kwamba alikufa, na kisha akiwa windo la dua ya mubahala ya ukurasa wa 199 wa ***Ijazul Masihi*** alijitia katika maangamio, basi kutaja hisani ya windo la shindano la aina hiyo ilikuwa lazima. Na uaminifu ulimlazimisha Pir Mehr Ali Shah kuandika kwa maneno wazi kwamba kitabu hiki si maandishi yangu bali ni maandishi ya Muhammad Hasan na mimi ni mwizi tu, badala ya kukinasibisha kwake kitabu

[367] Nuzulul Masihi, uk. 67

hicho kwa njia ya uongo katika dibaji ya kitabu. Bali ilipaswa kuweka sehemu fulani ya mapato ya kitabu hicho kwa kujikimu kwa mjane wa marehemu yule mwenye bahati mbaya… Na kama angefuata njia kama hii na akipokea *Anna* 4 kwa kila nakala angempa mjane mwenye msiba, angeepuka hivyo kidogo kudhalilika. Lakini ilikuwa lazima kwamba angefanya wizi huo wa aibu ili Neno la Mwenyezi Mungu lingetimia lililonishukia miaka kadha kabla ya leo, nalo ni hili: اِنِّیْ مُھِیْنٌ مَّنْ اَرَادَ اِھَانَتَکَ , yaani nitamdhalilisha atakayenuia kukudhalilisha. Mtu huyo alinilaumu kwa wizi, katika kitabu chake "Saife Chishtiyai", na wizi wenyewe ulikuwa huu kwamba kati ya sentensi karibu elfu ishirini za kitabu *Ijazul Masihi* kuna setensi 2-4 zilizo baadhi ya methali mashuhuri za Kiarabu au sentensi chache za *Makamate Hariri*, zilizolingana na ufunuo. Na sasa tendo lake bovu limethibitika kwamba muswada mzima wa Muhammad Hasan aliyekufa ameunasibisha kwake mwenyewe... Tazameni, athari ya kuwashambulia wakweli inakuwa hii kwamba kwa kuniita mwizi wa sentensi chache, yeye mwenyewe akathibitika mwizi wa kitabu kizima, na sio mwizi tu bali mwongo mkubwa pia kwani uongo mchafu alichapisha katika kitabu chake, na akaandika katika kitabu kwamba hiki kitabu nimeandika ilihali hakukiandika."[368]

Baada yake, Hudhur[as] alinukuu barua mbili za Mian Shihabuddin ambazo katika hizo moja aliandikiwa Hudhur[as] na ya pili[369] Hadhrat Maulawii Abdul Karim. Katika barua hizo mbili, yeye aliandika mambo yote aliyotaja Hudhur[as] hapo juu. Hudhur[as] na Hadhrat Maulawii Abdul Karim, wote wawili, walimwandikia Mian Shihabuddin kwamba avinunue na kuvileta vitabu hivyo viwili, yaani Ijazul Masihi na Shamse Bazigha, ambamo marehemu Sheikh Muhammad Hasan aliandika kumbukumbu zake pamoja na saini yake. Kwa kujibu, Mian Shihabuddin aliandika kwamba:

[368] Nuzulul Masihi, uk. 68-70

[369] Someni *Nuzulul Masihi*, uk. 72 hadi 74, maelezo ya pembeni.

"Nakubali amri yako, lakini baba wa Muhammad Hasan hatoi vitabu na anasema kwamba bila shaka uvione mbele yangu, lakini havitoi nichukue kwa muda. Naomba radhi, nifanye nini. Tena nimekosea kwamba nimemwandikia Bwana Golarawii barua kwamba wewe hukuandika kitu, umenukuu tu kumbukumbu alizoandika Muhammad Hasan. Kwa hiyo, Golarawii amemwandikia baba yake Muhammad Hasan kwamba usimwonyeshe vitabu, kwani mtu huyo ni adui yetu. Sasa mushkili ni huu kwamba baba yake Muhammad Hasan ni mfuasi wa Galarawii na anafuata kauli yake. Nasikitika kwa nini nilimwandikia barua Galarawii, ambayo kwa sababu yake wote wamekuwa maadui zangu. Tafadhali unisamehe, kuja kwangu bila vitabu ni gharama ya bure, kwani hawatoi vitabu. Basi

Ni mimi Shihabuddin, kutoka Bhiin, Tarafa ya Chakwal."[370]

Barua ambayo Hadhrat Maulawii Abdul Karim alimwandikia Mian Shihabuddin, yeye alimwonyesha Maulawii Karmdin barua ile. Maulawii Karmdin, mkazi wa Bhiin, ambaye baadaye akawa mpinzani mkali wa Hudhur[as], lakini wakati ule alikuwa na dhana njema kwa Hudhur[as]. Yeye pia alimwandikia Hudhur[as] barua[371] ambamo baada ya kudhihirisha maono ya kumtukuza akaandika:

"Jana, nilipokea barua ya rejista ya Maulawii Abdul Karim kupitia rafiki yangu mpendwa Mian Shihabuddin mwanafunzi, ambamo kilitajwa kitabu Saife Chishtiyai cha Bwana Pir Galarawii. Ni mimi niliyemwarifu kwamba katika kitabu cha Bwana Pir sehemu kubwa ni ya kumbukumbu zile za marehemu Maulawii Muhammad Hasan alizoandika katika maelezo ya pembeni ya kitabu "Ijazul Masihi" na "Shamse Bazigha". Vitabu hivyo viwili, Bwana Pir aliagiza kutoka kwangu na sasa vimesharudishwa. Kwa kulinganisha, kumbukumbu zile zile zimekutwa kuandikwa kitabuni. Hii ni

[370] Barua aliyoandikiwa Hudhur[as] ipo kwenye maelezo ya pembeni ya ***Nuzulul Masih***, kurasa 73,74

[371] ***Nuzulul Masihi***, uk. 75 hadi 77, maelezo ya pembeni.

kazi ya wizi kabisa kwamba akiandika maoni ya mtu aliyefariki, akayanasibisha kwake mwenyewe na hakutaja hata jina lake. Na ni la ajabu kwamba baadhi ya aibu anazoeleza katika maandisho yako mifano yake imo katika kitabu cha Bwana Pir. Vitabu hivyo viwili, kwa vile viko kwa baba wa Maulawii Muhammad Hasan, kwa hiyo ni vigumu kuvituma kwako vitabu vile, kwani yu mpinzani wako na hawezi kamwe kuruhusu jambo hilo. Naam, hii itawezekana kwamba kumbukumbu zile zikinukuliwa zitumwe kwako. Na hii pia inawezekana kwamba mtu yeyote maalum wa Jumuiya yako aje hapa kuziona, lakini itawezekana kuziona mtu akifika haraka. Postikadi moja ya Bwana Pir iliyoniwasilia juzi tu nakutumia hiyo yenyewe ili uione ambamo yeye mwenyewe amekiri kwamba akiiba kumbukumbu za Maulawii Muhammad Hasan akakipamba ***Saife Chishtiyai***. Lakini kudhihirisha kuwa mimi nimetoa habari hizi ni kinyume na hekima. Naam, haidhuru kama jina la Mian Shihabuddin lidhihirishwe. Kwani sitaki kwamba Jumuiya ya Bwana Pir inichukie sana. Niombee wewe kwamba itikadi yangu ipate kutakatika kukuhusu wewe, na nifahamu kwamba kwa kweli u mwenye kupokea ufunuo na umetumwa na Mungu."[372]

Hadhrat Hakiim Fadhl Din pia alikuwa na uhusiano mzuri na Maulawii Karmdin mkazi wa Bhiin.Yeye pia alimwandikia Maulawii Karmuddin barua moja ambamo ilisisitizwa sana kupata vitabu. Sasa ilitokea hivi kwamba mwanaye marehemu Maulawii Muhammad Hasan aliyekuwa ameajiriwa pahali fulani alifika kwao kwa likizo ya mwezi mmoja. Maulawii Karmuddin kwa kumpa rupia 6 alichukua kitabu cha Hudhur[as], "***Ijazul Masihi***", ambamo kwenye maelezo ya pembeni Maulawii Muhammad Hasan aliandika kumbukumbu kwa mkono wake. Akitaja habari hii yote, Maulawii Karmuddin ameandika:

"Mhshimiwa Muadhamu Bwana Hakim ─ ajaaliwe umri mrefu.

[372] Barua ya Maulawii Karmuddin aliyomwandikia Hudhur[as], maelezo ya pembeni katika ***Nuzulul Masihi,*** uk. 76-77

Assalamu alaikum wa rahmatullahi wa barakatuhu! Tarehe 31 Julai kijana[373] alifika nyumbani. Nilijaribu kumshughulikia yeye kuhusu kazi ile maalum tangu wakati ule. Mwanzoni alikataa vikali kutoa vitabu na akasema kwamba vitabu hivyo ni vya Ja'far Zatalli na yeye anatambua maandishi ya marehemu Maulawii Muhammad Hasan, na yeye ameniambia kwa kusisitiza kwamba mara moja nifikishe vitabu Lahore kwa Zatalli. Lakini baada ya kutumia hekima nyingi na kumpa tamaa akakubali. Hatimaye aliridhia na malipo ya rupia 6. Baada ya kuandika kumbukumbu zote za kitabu cha ***Ijazul Masihi*** kwenye nakala ya pili, kitabu chenyewe ambamo marehemu Maulawii aliandika kumbukumbu kwa kalamu yake, nakutumia kwa mkono wa anayekuletea barua. Ukipokea kitabu mpe risiti mletaji barua na mpe rupia 6 pia kama zipo ili apewe kijana, na ili isiwe taabu kwa kupata kitabu Shamse Bazigha. Utakapoleta nakala ya kitabu Shamse Bazigha bila jalada, mara moja nakala yenyewe ambamo kuna kumbukumbu utatumiwa kwa njia hiyo. Utulie tu, Mungu Akipenda, ahadi haitavunjwa… Nategemea kwamba huduma yangu hii wakikubali Hudhur[as] na Jumuiya yake wataniombea. Lakini, naomba kwamba jina langu lisidhihirishwe kabisa."[374]

Baadaaye kwa kutoa rupia 6 tena, Hadhrat Hakim Fadhl Din alipata kitabu cha pili pia. Vitu vyote hivyo vilipomfikia Hudhur[as], basi kwa sababu ishara yenye shani kubwa ya Mwenyezi Mungu ilidhihirika kwayo, yaani aibu ya kielimu ya Pir Mehr Ali Shah ilifichuka, kwa hiyo Hudhur[as] alizichapisha habari hizo na hakujali kwamba wafuasi wa Bwana Pir watampinga Maulawii Karamdin. Hudhur[as] ameandika:

"Maulawii Karmuddin kwa kusahau hakufikiria kwamba kuficha ushuhuda ni dhambi kubwa ambayo kuhusu hiyo Kurani Tukufu inaonya kwa maneno haya: اٰثِمٌ قَلۡبُهٗ . Kwa hiyo, uchamungu ni huu kwamba tusijali lawama ya mwenye kulaumu

[373] Mwanaye marehemu Maulawii Muhammad Hasan.

[374] Nakala ya barua ya Maulawii Karmuddin kwa marehemu, Hadhrat Hakim Fadhl Din, ***Nuzulul Masihi***, maelezo ya pembeni, uk. 78-79

> na tutoe ushuhuda tulionao. Basi hatuwezi kuwa wasaidizi katika hatia ya kuficha. Na kuficha huku kwa Maulawii Karmuddin si kwa amri ya Mungu, ni udhaifu wa moyo tu. Mungu Ampe nguvu."[375]

Mambo hayo yote yalipodhihirika wazi, uhakika wa umaarufu wake wa kielimu na wa vitendo wa Bwana Pir ukadhihirika wazi na akaanza kupitia wafuasi wake kupinga Maulawii Karmuddin. Maulawii Karmuddin aliyekuwa mtu dhaifu wa hali, aliona afadhali akane barua zake hizo. Basi, alitangaza katika ***Sirajul Akhbar***, Jhelum, la tarehe 6 Oktoba 1902 na 13 Oktoba 1902, kwamba barua hizo ni za bandia na za kubuniwa. Kama itakavyodhihirika mbele, barua hizo zilisababisha kesi iliyoendelea kwa muda mrefu.

SENSA YA MWAKA 1901, NA JUMUIYA KUPEWA JINA 'MUSALMAN FIRKA AHMADIYYA' – WAISLAMU WA DHEHEBU LA AHMADIYYA

Serikali ilikuwa imetangaza kwamba mwakani, yaani mwaka 1901, katika India nzima sensa itafanyika. Na mpaka wakati huo Hudhur[as] alikuwa hajaipa Jumuiya yake jina lolote. Watu walikuwa wakiwaita wanajumuiya wake "Mirzai" na "Qadiani". Kwa hiyo, Hudhur[as] aliona hakuna budi Jumuiya kupewa jina mwafaka. Basi, akaipa Jumuiya yake jina 'Musalman Firika Ahmadiyya' – yaani, Waislamu wa dhehebu la Ahmadiyya". Katika tangazo[376] moja, Hudhur[as] akieleza sababu ya jina hili, anasema:

> "Jumuiya hii imeitwa "Waislamu wa dhehebu la Ahmadiyya" kwa sababu hii kwamba Mtume wetu[saw] alikuwa na majina mawili: moja Muhammad[saw] na la pili Ahmad[saw]. Jina la Muhammad[saw] ni jina la ***kijalali*** na humo mlifichika utabiri huu kwamba Mtume Mtukufu[saw] atawaadhibu kwa upanga maadui ambao waliishambulia Islam kwa upanga na wakaua mamia ya Waislamu. Lakini Ahmad ni jina la ***kijamali***, linalomaanisha

[375] Nuzulul Masih, uk. 77, maelezo ya pembeni.

[376] Someni tangazo la 4 Novemba1900 lililoandikwa katika ***Tablighe Risalat,*** J. 9 uk. 91

kwamba Mtume Mtukufu[saw] ataeneza duniani amani na suluhu. Basi Mungu aligawa hivi majina hayo mawili kwamba kwanza katika maisha ya Mtume[saw] katika Makka lilidhihirika jina la Ahmad, na kwa kila hali fundisho lilikuwa la subira na uvumilivu. Kisha katika maisha ya Madina lilidhihirika jina la Muhammad, na hekima ya Mungu iliona lazima kuponda vichwa vya wapinzani. Lakini ilitabiriwa kwamba katika zama za mwisho tena jina la Ahmad[saw] litadhihirika. Na mja mmoja ambaye atadhihirika, kwa njia zake sifa za Ki-Ahmad yaani sifa za *Ki-jamali* zitadhihiri na vita zote zitakwisha. Basi, kwa sababu hiyo ilionekana sawa kwamba dhehebu hili liitwe 'Firka Ahmadiyya'."[377]

VITABU VYA MWAKA 1900

1. *Tuhfa Ghaznawiyya:* Maulawii Abdul Hak alitoa tangazo dhidi ya Hudhur[as], ambamo kwanza alipinga baadhi ya bishara za Hudhur[as], pili, pendekezo alilotoa Hudhur[as] mbele ya maulamaa na masheikh kwa kupambanua kati ya haki na batili kuwa mshindane nami katika kupokelewa dua kwa kuwaponya wagonjwa, basi itajulikana wazi kwamba nani anakaribiana na Mungu, Sheikh Abdul Hak alilipinga pendekezo hili akisema kwamba masheikh wa nchi nzima wawezaje kujumuika, na tena nani atalipia matumizi yao. Kwa kujibu tangazo hilo Hudhur[as] aliandika kijitabu hiki. Ingawa kiliandikwa kijitabu hicho katika mwaka 1900, lakini kilichapwa tarehe 3 Oktoba 1902.

2. *Risala Jihad:* Katika kijitabu hiki alieleza hakika na hekima sahihi ya jihadi. Wasioelewa maana sahihi ya jihadi waliiita jihadi kuwa ni kunyang'aya na kuua. Fikara hii alisahihisha.

3. *Lujjatun Nur:* Hudhur[as] aliandika kitabu hiki kuwahubiri maulamaa na masheikh wa nchi za Kiarabu. Katika kitabu hicho yamethibitishwa kwa njia nzuri sana madai ya Umahdi na Umasihi wake. Ingawa kiliandikwa kitabu hicho katika mwaka 1900, lakini kilichapwa baada ya kifo chake katika mwaka 1910, kwa sababu ya kushughulikia vitabu vingine.

[377] Tablighe Risalat, J. 9, uk. 91

4. *Mwanzo wa Uandishi wa Tuhfa Galarawiya:* Pir Mehr Ali Shah aliandika kitabu kiitwacho "Shamsul Hidaya". Ingawa Maulana Muhammad Ahsan Amrohi alishaandika jibu lake katika kitabu "*Shamse Bazigha*" kilichoishachapwa tayari, hata hivyo Hudhur[as] mwenyewe aliona afadhali yeye aandike jibu lake. Basi, alianza kuandika kitabu hicho mwishoni mwa mwaka 1900, akamaliza mnamo mwaka 1901 na akachapisha tarehe 1 Septemba 1902. Katika kitabu hicho alieleza vizuri sana madai yake, kisha hoja zake. Tukio maalum lifaalo kutajwa lililoandikwa ndani yake ni ushuhuda wa walii mtukufu wa Mungu, Hadhrat Seyyid Amir, Pir wa Kotewala, alioeleza mbele ya wafuasi wake kuhusu Imam Mahdi wa zama za mwisho. Mtukufu huyo mkamilifu alikuwa akiishi katika kijiji cha Kota katika maeneo ya Yusufzei na alijulikana kwa jina la Pir Kotewala. Alifariki katika mwaka 1877 sawa na mwaka 1264 Hijria.[378] Kabla ya kufariki kwake ushuhuda aliotoa kuhusu ujaji wa Hadhrat Imam Mahdi[as], sikilizeni alivyoeleza Sheikh Hakiim Muhammad Yahya Dipgarani. Bwana Hakiim mwenyewe alienda 'Kota' . Akaenda na shuhuda alizopata kutoka kwa wafuasi wa Bwana Pir Kotewala, katika hizo alimweleza mbili Hudhur[as] kwa barua, nazo ni hizi:

> 1. "Mtu mmoja hafidh wa Kurani aitwaye Nur Muhammad, mwenyeji wa Garhi Amazei kiasili, siku hizi yu mkazi wa Kota, anasimulia kwamba Hadhrat (Kotewale) siku moja alipokuwa akitawadha, nami nilikaa mbele yake, akasema "Sasa tupo katika zama za mwingine". Sikuelewa maneno haya, na kuuliza, 'Je Hadhrat, umekuwa mzee kiasi hiki kwamba zama zako zimekwisha? Bado wapo wengi wa rika yako wenye afya sana na wanafanya shughuli zao za dunia. Akasema, "Hujaelewa maneno yangu, muradi wangu ni mwingine kabisa." Kisha akasema, "Mtu ambaye huinuliwa kwa kujadidisha ameshazaliwa, kwa hiyo awamu yetu imekwisha, kwa sababu hiyo nasema kwamba tupo katika zama za mwingine." Kisha

[378] Nadhmuddurri fi Silkissiyar, na Mulla Safii.

akasema, ninahusika na mahuluku pia kidogo, lakini yeye hatahusika na yeyote. Atafikiwa na taabu na misiba mingi kiasi hiki hata kwamba mfano wake hautapatikana katika zama zilizopita, lakini hatajali katu''... Kisha nikauliza, 'Niambie jina, alama na mahali pake.'' Akajibu sitasema.''[379]

2. ''Mtu wa pili aitwaye Gulzar Khan, mkazi wa Budabir, Peshawar, na siku hizi anaishi karibu na Kota Sharif, kijiji chake kinaitwa Topi, mzee huyo kwa muda mrefu alikaa na Hadhrat (Pir Kotewala). Kwa kuapa yeye alieleza kwamba siku moja Hadhrat alikaa katika kikao cha kawaida na alikuwa mchangamfu sana. Akasema ''Baadhi ya marafiki zangu watamwona kwa macho yao Mahdi wa zama za mwisho.'' (Aliashiria kwamba Mahdi atakuwa karibu na nchi hii, ambaye watamwona). Kisha akasema, ''Watasikiliza kwa masikio yao maneno yake.''[380]

Kadhalika mtu mwingine, Mirza Muhammad Ismaili Qandhari,[381] aliyekuwa inspekta wa shule, alimwelezea Hadhrat Maulawii Seyyid Sarwar Shah kwamba yeye alikaa kwa muda mrefu pamoja na Hadhrat Pir Kotewala. Yeye alikuwa akisema kwamba Mahdi wa zama za mwisho ameshazaliwa, bado hajadhihiri. Na alipoulizwa jina, akasema sitawaambia jina, lakini nawaambia kiasi hiki kwamba lugha yake ni Kipanjabi.''[382]

Hadhrat Seyyid Amir Kotewala ni yule yule ambaye mtawa Hadhrat Maulawii Abdullah Ghaznawii alifanya baiati yake akihudhuria kwake.[383]

Katika Dhamima ya Tuhfa Golarawiya, Hudhur[as] ameeleza kwa kirefu sana aya لَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا. Na alitoa muhula wa siku 15 na kuweka

[379] Tuhfa Golarwiya, uk. 57, maelezo ya pembeni.

[380] Tuhfa Golarwiya, uk. 57, maelezo ya pembeni.

[381] Mtu huyo alikuwa mjomba wa mke wa Hadhrat maulana Ghulam Hasan Khan Peshawarii na miongoni mwa wasadikishaji wa Hudhur[as].

[382] Tuhfa Golarwiya, uk. 55-56, maelezo ya pembeni.

[383] Sera ya Hadhrat Maulawii Abdullah Ghaznawii, uk. 28

zawadi ya rupia 500 kwa mletaji wa mfano wa mzushi aliyepata muda wa miaka 23. Kwenye jalada la nje la kitabu hicho Hudhur[as] aliandika hii pia kuhusu Pir Mehr Ali Shah kwamba:

> "Kama kwa kukipinga hiki, yeye akiandika kijitabu avunje hoja zangu zote kutoka mwanzo mpaka mwisho, kisha Maulawii Abu Said Muhammad Husain Batalawii akiweka mkutano katika Batala wakati sisi wawili tuwepo awaelezee wasikiliza hoja zangu zote, moja baada ya nyingine, kisha kwa kila dalili atakayowasomea wasikilizaji bila kupunguza chochote wala kuzidisha, asome majibu ya Bwana Pir, na kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu aseme kwamba majibu haya ni sahihi na yanavunja hoja zilizoletwa, basi baada ya kushinda kwake nitamkabidhi Bwana Pir zawadi ya rupia 50 katika kikao kile kile."

5. Arbain: Katika zama zile, kwa kuwa upinzani ulikuwa na nguvu sana, kwa hiyo yeye alinuia kwamba kwa kutimiza hoja juu ya wapinzani achapishe mfululizo matangazo arobaini juu ya madai yake. Kwa nia hiyo aliyaita matangazo hayo jina Arbain. Miongoni mwa hayo, tangazo la kwanza lilitoka kwa sura ya tangazo hasa, lakini matangazo ya baadaye yalikuwa na kurasa kadha, kwa hiyo yalianzia kutoka kwa sura ya vijitabu. Baada ya kutoka vijitabu vinne, ukubwa wake ukawa sawa na kitabu cha wastani. Hapo, akitosheka na hivyo, na akachapisha vijitabu hivyo vinne kwa sura ya kitabu kimoja, lakini alibakiza jina "Arbain".

KWA NINI ILIKATAZWA KUSALI NYUMA YA IMAMU ASIYE MWAHMADIYYA

Mpaka sasa Hudhur[as] alikuwa hajakataza Jumuiya yake kusali nyuma ya wasiokuwa Waahmadiyya, lakini sasa upinzani ulishapita mipaka kiasi hiki kwamba Waahmadiyya walipoenda kusali katika misikiti ya wasiokuwa Waahmadiyya, walichokozwa sana. Mabirika ya udongo uliookwa waliyotumia kutawadha yalikuwa yanavunjwa; mikeka waliyotumia kusalia waliichoma moto. Sakafu waliposimama Waahmadiyya, hiyo ilioshwa, bali baadhi ya masheikh wakaamuru na sakafu ile ilivunjwa, na Waahmadiyya walikuwa wakiteswa kadri

ilivyowezekana. Fatuwa ilitolewa kwamba Mwahmadiyya akisimama katika safu, ni kama nguruwe; katika hali hiyo, wasimamao karibu naye, sala yao haisihi na kadhalika. Mungu wa ardhi na mbingu Alikuwa Anaona hali hizo zote, kwa hiyo Akamfanya mtumishi wake atangaze kwamba:

> "Kumbukeni, kama Mungu Alivyoniambia, ni haramu juu yenu na ni haramu kabisa, kwamba msali nyuma ya mkufurishaji na mkadhibishaji au mwenye kusita-sita. Bali yapasa kwamba imamu wenu awe aliye miongoni mwenu. Kwenye habari hiyo kwa namna moja Hadithi hii ya Bukhari inaashiria: إِمَامُكُمْ مِنْكُمْ, yaani Masihi atakapokuja, hapo mtalazimika kuacha kabisa madhehemu mengine yanayodai Uislamu, na imamu wenu atakuwa kutoka miongoni mwenu. Basi mfanye hivyo. Je, mwataka mlaumiwe na Mungu na amali zenu zipotee na msijue. Mtu anayenikubali kwa moyo, huyo anatii pia kwa moyo, na katika kila hali ananifanya kuwa mwamuzi, na anataka kupata uamuzi kutoka kwangu kwa kila hitilafu. Lakini yule mtu ambaye hanikubali kwa moyo, mtakuta ndani yake kiburi, majivuno na ukinaifu. Basi jueni kwamba huyo hahusiki na mimi, kwani haheshimu mambo yangu niliyopata kutoka kwa Mungu, kwa hiyo hana heshima mbinguni."[384]

Tangazo hilo halikuwaathiri wakati huo masheikh wasiokuwa Waahmadiyya, bali waliliona jambo hilo kuwa ushindi wao kwamba wameshafaulu kuwafukuza Waahmadiyya kutoka misikiti yao. Lakini, sasa, kinyume chake, wanawalaumu Waahmadiyya kwamba hao hawasali nyuma yetu.

PENDELEZO LA KUANZISHA JARIDA 'REVIEW OF RELIGIONS'

Kwa vile kazi yake moja muhimu ilikuwa "kuvunja msalaba" pia, na ingawa alikwishafanya kazi hii kwa njia bora sana kihoja, lakini kwa kuwa wasimamizi wa msalaba, wengi wao, walikuwa wakiishi katika nchi za magharibi, na lugha yao ilikuwa Kiingereza, kwa hiyo alitaka

[384] Arbain, Na. 3, uk. 34, maelezo ya pembeni.

kwamba wafikishiwe, kwa dalili za kutuliza na hotuba zinazoathiri, wale walioelimika wa nchi hii na Waulaya watafutao haki, kweli zote na maarifa matakatifu na hoja imara za kuihami dini ya Kiislamu na mambo yatulizayo roho ya binadamu ambayo yalimdhihirikia na bado yanaendelea kudhihiri. Basi kwa hiyo, yeye alichapisha tarehe 15 Januari 1901 tangazo moja lenye kichwa cha habari "Pendekezo la Muhimu", ambamo alidhihirisha hamu na jazba na uchungu wa moyo wake na alipendekeza kwamba kwa kutimiza makusudio hayo, jarida moja lianzishwe kwa lugha ya Kiingereza na kwa kulishughulikia njia iliyo bora ifuatawe. Na akatangaza kwamba kwa kutafakari juu ya pendekezo hili ndugu wajumuike Qadian siku ya Idi kubwa na kutoa shauri kuhusu habari hii kwamba tupangaje ili jarida hili liweze kuanzishwa. Basi, tarehe 31 Machi 1901, kwa kushauriana na ndugu wote iliamuliwa kwamba usimamizi wa jarida hili upewe kwa kamati moja itakayoitwa "Anjuman Isha'ate Islam", na jarida liliitwa "Review of Religions". Maulawii Muhammad Ali M.A. na Khwaja Kamaluddin waliwekwa kuwa wahariri. Na ikaamuliwa kwamba jarida lianze kutolewa tarehe mosi Oktoba 1901. Maulawii Muhammad Ali atayarishe makala mwenyewe pia akipata mwongozo kutoka kwa Hudhur[as], na aendelee kuyafasiri kwa Kiingereza makala atakayoandika Hudhur[as]. Lakini kwa sababu fulani jarida halikuweza kutolewa tarehe iliyowekwa. Tarehe 24 Novemba, ilifanyika kikao cha Bodi ya Wakurugenzi na iliamuliwa kwamba jarida la Kiingereza lazima lianzishwe kutoka Januari 1902. Na kama wanunuzi 300 walete maombi kwa kununua jarida la Kiurdu pia, basi tolea la Kiurdu pia litolewe.[385] Basi jarida likaanza kutolewa.

DHIHIRISHO LA TAUNI, MACHI 1901

Wasomaji wanakumbuka kwamba Hudhur[as] alitangaza utabiri tarehe 26 Februari 1898 kuhusu kuenea tauni nchini. Akaandika kwamba nilionyeshwa kuwa katika sehemu mbalimbali ya nchi hii mimea myeusi imepandwa nayo ndiyo mimea ya tauni. Na Hudhur[as] akatoa

[385] Haitakuwa bure kutaja kwamba katika majarida mawili ya Kiingereza na Kiurdu makala nyingi ziliandikwa na Hudhur[as], lakini jina lake halikuandikwa. Lakini wasomaji wa maandishi ya Hudhur[as] mara moja wanatambua. Mwandishi

habari hii pia kwamba mimea ile inaweza kutilifika kwa toba na kuomba ghofira, lakini tangazo hilo likasomwa siku hizo kwa masihara na dhihaka tu badala ya kutubu na kuomba ghofira. Sasa, tauni ilipoenea nchini, na hapa na pale vifo vikaanzia kutokea, tena Hudhur[as] kwa sababu ya huruma akachapisha tangazo moja chini ya kichwa cha habari "Tauni", ambamo baada ya kukumbusha utabiri wa tarehe 26 Februari 1898 akaandika:

> "Enyi wapendwa, nachapisha tangazo hili tena kwamba mjitahadhari na kumcha Mungu na onyesheni mabadiliko mema ili Mungu Awarehemuni na balaa ile iliyokaribia sana Mungu Aitoweshe. Enyi mlioghafilika, huu sio wakati wa kucheka na kudhihaki. Hii ni balaa inayokuja kutoka mbinguni na inaondoka kwa amri ya Mungu wa mbingu tu."

Katika tangazo hilo akaandika hii pia:

Nasema kweli kabisa kwamba kama katika mji fulani wenye wakazi laki kumi kuna mtu mmoja tu mkweli mkamilifu, hata hivyo balaa hii itaondolewa katika mji huo. Basi, kama mkiona kwamba balaa hii inaendelea kuumeza mji na inauangamiza, basi mjue kwa yakini kwamba mjini humo hamna hata mkweli mmoja mkamilifu. Kutokea tauni ya daraja ya kawaida au ugonjwa mwingine wa kuambukiza ni jambo dogo la kawaida, lakini balaa hii inapoendelea kumeza mji kama moto wa kuteketeza kila kitu, basi muwe na yakini kwamba mjini humo hamna wakweli kabisa. Hapo haraka sana ondokeni mji huo au tubuni kikamilifu. Kuondoka mji kama huo jinsi inavyofaa sawa na kanuni ya utabibu ndivyo ifaavyo sawa na kanuni za kiroho pia. Lakini yule aliye na sumu ya dhambi ndani yake, huyo yupo katika hali ya hatari. Kaeni na watu wema, maana kukaa na watu wema na dua ya waliotakasika ni tiba ya sumu hiyo. Dunia inaelekea kwenye njia za kiardhi, lakini mzizi wa maradhi hayo ni sumu ya dhambi, na inafaidisha kukaa karibu na mtu aliye na sifa ya kiuasumu."[386]

[386] Tangazo la 17 Machi 1901

PENDEKEZO LA KUWATAHINI WENYE BUSARA WA JUMUIYA

Mnamo Septemba 1901, Hudhur[as]alichapisha tangazo moja chini ya kichwa cha habari "Ishtihaar Mufidul Akhyar", ambamo aliilazimisha Jumuiya yake kwamba:

> "Katika Jumuiya yetu hii kwa akali watu mia moja wawepo wenye fadhila na ukamilifu ambao wawe na elimu ya Jumuiya hii na ya ishara na hoja na dalili imara kuhusu madai haya, ambazo Mwenyezi Mungu amedhihirisha, na waweze kutimiza hoja kwa njia bora juu ya wapinzani katika kikao, na waweze kujibu upinzani wao wa uzushi, na waweze kumwokoa kila mtafuta haki katika wasiwasi walioeneza Wakristo na Waaria na waweze kuwafahamisha kikamilifu kitimilifu ukweli wa dini ya Islam. Basi, kwa mambo hayo yote imeamuliwa kwamba wasomi hodari na wenye akili na busara wote wa Jumuiya yetu waelekezwe kwamba wajiweke tayari kwa mtihani baada ya kusoma vitabu mpaka tarehe 24 Desemba 1901, na katika likizo za mwezi Desemba ujao wakifika Qadian wafanye mtihani kimaandishi kuhusu mambo yaliyotajwa juu. Hapa hapa kwa lengo hilo, katika likizo hizo, patakuwa na mkutano na maswali yataulizwa juu ya mada hizo. Watakaoshinda kujibu maswali watachaguliwa kwa huduma hizi, nao watafaa watumwe kwenda sehemu mwafaka kwa kuwaita watu kwenye ukweli. Na kwa lengo hilo hilo, kila mwaka mkutano utafanyika katika Qadian, Mungu Akipenda, mpaka idadi kubwa ya wenye kujadiliana na watu ipatikane."[387]

[387] "Tangazo la Mufidul Akhyar", 9 Septemba 1901, lililoandikwa katika *Tablighe Risalat*, J.10, uk. 12

MLANGO WA TANO

UANDISHI WA "KUONDOA KOSA MOJA", SAFARI YA KWENDA DELHI NA KURUDI

Sasa twataka kueleza maoni ya Hudhur[as] juu ya swala hili ambalo kwa sababu yake sehemu ndogo sana ya Jumuiya Ahmadiyya ikihitilafiana na walio wengi ikajitenga tangu muda mrefu katika mwaka 1914 wakati wa uchaguzi wa Khalifa wa Pili. Swala lenyewe ni hili kwamba daraja na cheo cha Hudhur[as] ni nini, na kwamba je, kutoka mwanzo wa madai yake mpaka mwisho aliendelea kukiita cheo chake kwa jina lile lile moja au baada ya muda fulani akabadilisha jina la daraja yake na cheo chake. Basi itikadi ya wanajumuiya wengi sawa na maandishi ya Hudhur[as] ni hii kwamba bila shaka katika funuo zake kutoka mwanzo aliendelea kuitwa nabii na mtume, lakini sawa na kifafanuzi maarufu cha nabii na mtume, kwa muda fulani akafasiri maneno hayo na kuendelea kujiita *Muhaddath*. Lakini Mwenyezi Mungu Alipomwambia waziwazi kwamba maana ya nabii iliyo maarufu katika Umati wa Muhammad[saw] sio sahihi, sio sawa, hapo akibadilisha itikadi yake ya zamani akasema yu katika kundi la manabii.

Lakini waliojitenga na Jumuiya katika mwaka 1914, wakati wa uchaguzi wa Khalifa wa pili, wana imani hii kwamba Hudhur[as] kamwe hakudai unabii wala utume bali daima aliikana na aliiona ni kufuru. Kutoka mwanzo alidai Umuhaddath tu na mpaka mwisho madai hayo yaliendelea na kamwe hakuyaacha.

Maelezo yake ni haya kwamba hakuna shaka ndani yake kwamba kabla alikuwa hajafunuliwa maana ya kweli ya utume, akafasiri maneno ya ufunuo 'nabii' na 'mtume' na akajiita *Muhaddath,* na hiyo ilikuwa sahihi kwani wakati huo maana ya nabii ilifahamika kwamba:

> "Katika istilahi ya Islam, maana na nabii na mtume ni hii kwamba hao wanaleta sheria kamili au wanatangua baadhi ya amri za sheria ya zamani au hawaitwi umati wa nabii wa zamani, na huwa na uhusiano na Mwenyezi Mungu moja kwa moja bila

kufaidika na nabii yeyote."[388]

Sawa na ufafanuzi huo, yeye hakuwa nabii kwani hakuleta sheria mpya yoyote, bali alikuwa chini ya sheria ya Muhammad[saw]. Hakuwa mwenye kubadilisha baadhi ya sheria ya Muhammad[saw], bali alitumwa kuilinda na kuitangaza na kuieneza, na yote aliyopata katika daraja za kiroho hakupata moja kwa moja bali alipata kumpitia Hadhrat Khatamun Nabiyyin[saw]. Naye hakuwa nje ya utii wa Mtume[saw] wala nje ya umati wake, bali alikuwa mtiifu wa Bwana wake na Nabii wake na alikuwa katika umati wake Hadhrat Muhammad Mteule[saw]. Kwa hiyo alikana kuwa nabii na mtume sawa na ufafanuzi uliokubalika hapo kabla, na akafasiri maneno ya ufunuo wake na akajiita ***Muhaddath,*** na njia yake hiyo ilikuwa sahihi, na uaminifu ulitaka hivyo alivyofanya. Lakini hekima ya Mungu ilipotimia iliyosababisha mwenendo huo, na Mwenyezi Mungu Akamfunulia kwamba ufafanuzi wa nabii sio ule ulioafikiana nao na kukana kuwa nabii na mtume na kujiita ***Muhaddath,*** bali ufafanuzi wa neno nabii ni huu kwamba:

> "Mwenye kuwafikishia watu maneno anayopokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu, yaliyo na habari za gahaibu na matabiri makubwa, huitwa nabii katika istilahi ya Kiislamu."[389]

Kisha Hudhur[as] anasema:

> "Nionavyo mimi, Nabii anaitwa yule anayeshukiwa maneno ya Mungu kwa yakini na kwa wingi yaliyo na mambo ya ghaibu ndani yake. Kwa hiyo Mungu Ameniita Nabii, lakini bila kuleta sheria."[390]

Vilevile anasema:

> Maongezi hayo yanapofikia daraja ya ukamilifu katika ubora na wingi, na kusiwe na kitu kingine kilichochanganyika ndani yake, wala yasiwe na upungufu wowote, na yawe na mambo ya

[388] Barua ya Hudhur[as] iliyopo katika gazeti Al Hakam, 17 Agosti 1899

[389] Hujjatullah, uk. 6

[390] Tajalliyate Ilahiya, uk. 20

> ghaibu waziwazi, basi hayo kwa maneno mengine yaitwa unabii, na juu yake manabii wote waafikiana."[391]

Kisha anasema:

> "Haikuzingatiwa maana ya kweli ya 'nabii'. Maana ya 'nabii' ni mpokeaji wa habari kutoka kwa Mungu kwa njia ya wahyi na mwenye kujaaliwa maongezi na Mungu. Kuleta sheria si lazima kwake, wala si lazima kuwa asiwe mtii wa mtume mwenye sheria. Basi yule aliye katika umati wa Mtume[saw] akiitwa nabii wa namna hii hamna shida, hususan katika hali ambapo huyo anapata baraka kutoka kwa nabii wake anayemtii."[392]

Maandishi hayo yanadhihirisha kwamba ufafanuzi wa unabii aliokuwa anafahamu Hudhur[as] na ambao sawa nao alikuwa anasema kuwa yeye si nabii, ufafanuzi huo haukuwa sahihi. Ufafanuzi wa kweli ni ule aliodhihirishiwa kwa kufahamishwa na Mungu, yaani 'nabii' ni yule ambaye Mwenyezi Mungu Aongee naye kwa wingi, na maongezi yale yajumuishe mambo muhimu ya ghaibu, na Mwenyezi Mungu Amwite kuwa nabii na amtume kuwaongoza watu. Kuleta sheria mpya au kutokuwa mtiifu wa nabii wa zamani hamna katika ufafanuzi wa nabii.

Kwa kuwa ufafanuzi huu uliafikiana kabisa na Hudhur[as], kwa hiyo Hudhur[as] alisema kwamba mimi ni nabii na mtume. Na kauli hii ya Hudhur[as] pia ilikuwa sawa kabisa na uaminifu wake. Maadamu alikuwa hajafunuliwa uhakika, Hudhur[as] aliendelea kudhihirisha waziwazi kwamba mimi si nabii wala mtume bali ni Muhaddath; lakini alipofunuliwa uhakika, hapo alisema waziwazi kwamba mimi ni nabii na mtume, sio muhaddath pekee.

Uhakika huo waliendelea kukiri katika uhai wa Hudhur[as] wale waliojitenga na Jumuiya, yaani wasiofanya baiati ya Khalifa. Amiri wao wa kwanza marehemu Maulana Muhammad Ali, katika uhai wa Hudhur[as] alikuwa mhariri wa jarida *Review of Religions*. Sio safari moja

[391] Al Wasiyyat, uk. 12

[392] Dhamima Barahine Ahmadiyya, sehemu ya 5, uk. 138

bali mara maishirini akimhesabu Hudhur[as] kuwa katika kundi la manabii akaandika makala kadha dhidi ya wapinzani. Katika mjadala mmoja wa kimaandishi aliofanya na Khwaja Ghulamuth Thakalain, aliandika:

> "Khwaja Ghulamuth Thakalain ameeleza mambo manne katika kupinga maelezo yangu ya aya إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَوٰةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ : 1. Shetani aliapa kwa Mungu kwamba atawapoteza wote… Shetani akawa mkweli katika mawazo yake. 2. Watu wa Firauni walikuwa wakiwaua watoto wao wachanga (wa wana wa Israeli). 3. Masihi alisulubiwa. 4. Miongoni mwa makhalifa wanne na wajukuu wawili wa Mtume[saw] ambao ni watu sita kwa jumla, kati yao watu watano waliuawa na maadui.
>
> Mada yenyewe ilikuwa kwamba Kurani Tukufu imeweka alama ipi ya kupambanua kati ya mdai mkweli na mwongo wa utume. Sasa Khwaja Ghulamuth Thakalain aseme mwenyewe kwamba kati ya waliotajwa ni nani mdai wa unabii mingahiri ya aliyetajwa katika namba ya tatu, yaani Hadhrat Isa[as]? Je, shetani ndiye mdai wa unabii? Je, watoto wachanga wa wana wa Israeli walidai unabii? Je, makhalifa wanne na wajukuu wawili wa Mtume[saw] walidai unabii? Kama hapana, basi mambo hayo yahusikanaje na mada yenyewe"[393]

Katika ibara hiyo, kati ya mambo yaliyotajwa na Khwaja Ghulamuth Thakalain, Bwana Maulawii huyo amemwita aliyetajwa katika jambo la tatu, yaani Hadhrat Isa[as], kuwa mdai wa unabii. Au anataka kuthibitisha unabii wa Hudhur[as] akijadili madai yake ya unabii, kwa hiyo habari za wengine walitajwa na Bwana Khwaja, yeye Bwana Maulawii akasema hazihusikani na mada, kwa sababu miongoni mwao yeyote hakudai unabii.

Kadhalika mnamo mwaka 1904, katika kesi ya Sheikh Karmuddin wa Bhiin, Maulawii huyo alipohudhuria kama shahidi wa aliyeshtakiwa, akaeleza kwa tamko dhati mahakamani kwamba:

> "Mkadhibishaji wa mdai wa unabii huwa mwongo, Bwana

[393] Review of Religions, J. 5, uk. 432

Mirza aliyeshtakiwa ndiye mdai wa unabii."

Basi, katika uhai wa Hudhur[as], Bwana Maulawii na wenzake wote waliendelea kumwita Hudhur[as] na kuandika kuwa nabii. Bali katika zama za Ukhalifa wa Hadhrat Maulana Nuruddin, Khaliftul Masihi I[ra], pia wakafahamu cheo na daraja yake kuwa hiyo hiyo. Naam, katika miaka ya mwisho ya ukhalifa wake, watu hao wakifikiri jambo fulani, ndani kwa ndani wakaanza kuhitilafiana juu ya swala hilo, lakini walikuwa na hofu pia ya Hadhrat Khaliftul Masihi I[ra]. Wakati fulani katika Jumuiya ulipoanzia mnong'ono juu ya itikadi za watu hao, basi hao wenyewe walitoa tangazo hili katika gazeti lao: "*Paighame Sulha*" kwamba:

> "Ijulikane kwamba baadhi ya watu wameeleweshwa visivyo kwamba wahusika wa gazeti hili au mmoja wao anamwona Seyyidna Mwongozi wetu, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Mau'udi na Mahdi[as], kuwa mdogo kuliko daraja yake kubwa au anashusha hadhi yake. Sisi sote Waahmadiyya, wahusikao kwa njia yoyote na gazeti *Paighame Sulha,* twatangaza kwa kumtambua Mungu kuwa Yupo kila mahala na Anatuona kwamba kusambaza habari ya namna hii kutuhusu sisi ni kutusingizia tu. Sisi twamwamini Hadhrat Masihi Mau'udi na Mahdi wa zama kuwa Nabii wa zama hizi, Mtume na Mwokoaji, na daraja yake aliyoeleza Hadhrat Masihi Mau'udi[as] kuipunguza au kuizidhisha twaona ni sababu ya kukosa imani. Ni imani yetu kwamba wokovu wa dunia hauwezi kupatikana bila kumwamini Hadhrat Mtume Mtukufu[saw] na mtumishi wake Hadhrat Masihi Mau'udi. Baada yake tunamfahamu Khalifa wake wa haki Seyyidna Kiongozi wetu, Maulana Hadhrat Maulawii Nuruddin, Khalifatul Masihi, pia kuwa mwongozi wa kweli. Baada ya tangazo hili, kama mtu yeyote haachi kusambaza dhana mbaya juu yetu, basi twamwachia Mungu habari hii yetu."[394]

Hizo zilikuwa ni itikadi zao katika zama za Hudhur[as] na Khalifatul Masihi I[ra]. Lakini baada ya kutengana na Jumuiya, Maulawii

[394] Paighame Sulha, 16 Oktoba 1913

Muhammad Ali alitangaza kwamba:

> "Naona kumwita Bwana Mirza kuwa nabii si tu kuing'olea mbali Islam, bali kwangu mimi Bwana Mirza pia ataathirika vibaya sana."[395]

Vilevile akaliandika:

> "Ni kazi ya mwongo sana kudai unabii hata akiwa ndani ya umati wa Mtume[saw]."[396]

Matokeo ya lazima yanayotokea na maandishi hayo ni wazi.

Baada ya kufafanua swala la unabii kwa wasomaji, sasa tunataja sababu ya kuandika kipeperushi "Kuondoa Kosa Moja". Basi, kama ilivyoishaelezwa, sawa na ufafanuzi wa nabii uliokubaliwa na wengi, kwa muda fulani Hudhur[as] alijiita muhaddath badala ya kujiita nabii, na huo ni zama za kabla ya mwaka 1900. Mnamo mwaka 1901, Hudhur[as] alifunuliwa vizuri sana kwamba ufafanuzi wa unabii ambao kwa sababu yake alikuwa anakana unabii wake, si sahihi kabisa bali ni kinyume cha Islam. Kwa hiyo, yeye alianza kubainisha habari hiyo kwa wafuasi wake. Zikisomwa hotuba za Ijumaa za zama hizo, za Hadhrat Maulawii Abdul Karim Sialkoti, inaweza kusadikika vizuri kwamba Bwana Maulawii huyo alikuwa amemtaja Hudhur kuwa nabii na mtume. Katika zama ambapo Hudhur[as] alikuwa ameishaelewa vizuri cheo na daraja yake, Mwahmadiyya mmoja, asiye msomi, aliulizwa huko Amritsar na mpinzani mmoja kwamba "Yule uliyefanya baiati yake anadai kuwa nabii na mtume?" Mtu huyo alimjibu kwa maneno ya kukana tu, ilihali jibu kama hilo halikuwa sahihi. Hudhur[as] akitaja huyo Mwahmadiyya alisema:

> "Baadhi ya watu miongoni mwa Jumuiya yetu ambao wanayo elimu kidogo kuhusu madai yetu na hoja zetu, ambao hawakuwahi kusoma vitabu kwa makini wala hawakuweza kukamilisha elimu zao wakikaa nami muda wa kutosha, hao baadhi ya wakati wanatoa jawabu la shutuma ya wapinzani

[395] Paighame Sulha, J. 2 uk. 119, la 16 Aprili 1915

[396] An-Nubuwwatu Fil-Islam, uk.115

linalokuwa kinyume kabisa na uhakika. Kwa hiyo, juu ya kuwa wenye haki wanapata kujuta. Siku chache zimepita mtu mmoja aliletewa shutuma na mpinzani kwamba yule uliyefanya baiati yake anadai kuwa nabii na mtume, na hiyo ikajibiwa kwa maneno ya kukataa tu, ilihali jibu kama hilo si sahihi."

Imebainika kutokana na ibara hiyo kwamba katika tangazo maalum aliloona Hudhur lazima alitoe, mwanzoni mwake tu aliwajulisha wanajumuiya kuhushu madhara na hasara ya, na kuwalinda na, jambo ambalo akaliona ni kinyume cha uhakika na ni sababu ya wenye haki kujuta. Na jambo lenyewe hilo lilikuwa ni jibu la Mwahmadiyya asiyeelimika alilotoa kumjibu mpinzani shutuma yake kwamba Hudhur[as] hakudai unabii wala utume.

Baada ya maandishi hayo ya Hudhur[as], sawa na itikadi maarufu ya Waislamu swali hili lingeweza kuzuka kwamba baada ya Khatamun Nabiyyin, mtume atakujaje? Basi, Hudhur[as]mwenyewe akitaja swali hilo akalijibu. Hudhur[as] amesema:

"Basi, kama ikisemwa kuwa Mtume[saw] ni Khatamun Nabiyyin, awezaje, mtume mwingine kufika baada yake, basi jibu lake ni hili ya kwamba bila shaka hawezi kufika mtume yeyote mpya – au hata wa kale kama nyinyi mumteremshavyo Hadhrat Isa[as] katika zama za mwisho, nanyi mna itikadi kuwa wahyi wa utume utaendelea kumshukia kwa miaka 40 kwa kupita zama za Mtume[saw]. Bila shaka itikadi kama hii ni kosa. Na aya hii:

وَلٰكِنْ رَّسُوْلَ اللّٰهِ وَخَاتَمَ النَّبِيّٖنَ

na Hadithi:

لَا نَبِيَّ بَعْدِيْ

hutoa ushahidi juu ya itikadi hii kuwa uongo mtupu. Lakini sisi tu wapinzani wakali wa itikadi za namna hii, nasi tuna imani ya kweli iliyokamilika juu ya Aliyosema Mwenyezi Mungu kwamba:

وَلٰكِنْ رَّسُوْلَ اللّٰهِ وَخَاتَمَ النَّبِيّٖنَ

Katika aya hii kuna bishara wasiyoitambua wapinzani wetu, nayo ni hii ya kwamba baada ya Mtume[saw] milango ya bishara imekwisha fungwa. Haiwezekani, sasa, kuwa yeyote yule – Baniani au Myahudi au Mkristo au Mwislamu wa jina tu – aweze kuthibitisha neno Nabii kwa dhati yake. Madirisha yote ya utume yamekwisha fungwa, lakini dirisha la ***Sirati Siddiqi*** liko wazi – yaani kupata utume kwa kujipoteza ndani ya mapenzi ya Mtume[saw]. Basi yule amjiaye Mwenyezi Mungu kwa njia ya dirisha hili huvishwa shuka la utume, kwa hiyo kuwa kwake nabii si mahali pa ghera, kwani hupata siyo kutoka dhati yake bali kutoka katika chemchem ya Mtume wake…

Basi muradi wa aya:

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ اَبَآ اَحَدٍ مِّنْ رِّجَالِكُمْ وَلٰكِنْ رَّسُوْلَ اللّٰهِ وَخَاتَمَ النَّبِيّٖنَ [397]

ndio huu kwamba Muhammad[saw] si baba wa yeyote katika wanaume wa kidunia lakini ni baba wa wanaume wa Akhera kwa kuwa yu Khatamun Nabiyyin, wala hakuna njia yoyote ya kupata fadhili ya Mungu minghairi ya njia yake Mtukufu Muhammad[saw].... Hivyo basi, haikuingia tofauti katika maana ya Khatamun Nabiyyin, lakini kwa kushuka kwa Isa, maana ya Khatamun Nabiyyin lazima itatanguka kabisa. Ikumbukwe pia kwamba maana ya nabii kwa njia ya lugha ni 'Mwenye kutoa habari za ghaibu akizipata kutoka kwa Mwenyezi Mungu'. Basi popote itakapoingia maana hii, humo humo neno 'Nabii' pia litathibitika. Na ni sharti kwa nabii kwamba awe Rasul (mtume) vilevile, maana ikiwa yeye hawi mtume tena hawezi kupata habari safi za ghaibu kwa sababu aya hii inakataza:

لَا يُظْهِرُ عَلٰى غَيْبِهٖٓ اَحَدًا ۙ اِلَّا مَنِ ارْتَضٰى مِنْ رَّسُوْلٍ [398]

Basi kama akikataliwa nabii baada ya Mtume[saw], italazimu tena kuchukua itikadi ya kwamba umati huu wa Mtume[saw] hauna

[397] Al Ahzab, 33:41

[398] Hamdhihirishii yeyote habari za ghaibu isipokuwa Aliyemridhia yaani mtume. (Al Jinn, 72:27-28)

sehemu katika kuzungumza na kufunuliwa na Mwenyezi Mungu, kwa kuwa yeyote ambaye mkononi mwake habari za ghaibu zitadhihirika kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hapo lazima kabisa maana ya nabii itathibitika kwa dhati yake kwa mujibu wa aya:

لَا يُظْهِرُ عَلٰى غَيْبِهٖٓ

Na atakayetumwa na Mwenyezi Mungu tutamwita mtume, ila tofauti ni hii kwamba baada ya Mtume wetu[saw] mpaka siku ya Kiyama, hakuna nabii yeyote yule itakayemshukia sheria mpya au atakayepewa lakabu ya utume hivi tu bila njia ya Mtume[saw] na bila kujipoteza ndani ya mapenzi ya Mtume[saw] hivi kwamba apewe jina Muhammad na Ahmad huko mbinguni. Na yule anayedai hivyo amekufuru basi."[399]

Sasa angalieni katika ibara hiyo yote ***Umuhaddathi*** haukutajwa kabisa hata kwa njia ya ishara au kinaya, ilihali katika hali ya dai la Hudhur[as] la ***Umuhaddathi*** ingepasa kutajwa hapa ***Umuhaddathi***, sio unabii, lakini katika ibara iliyoandikwa juu umetajwa unabii; haukutajwa kabisa ***Umuhaddathi***. Kama Hudhur[as] angedai umuhaddathi tu, basi ilivyodhihirishwa juu, swali hilo halingeweza kuzuka alilotaja Hudhur[as]. Lakini kama lilikuwa limeletwa, basi jibu lake hili fupi lilitosha kwamba kinyume cha aya ya Khatamun Nabiyyin ni ujio wa nabii sio wa muhaddathi, na dai langu ni la umuhaddathi sio la unabii. Lakini Hudhur[as] hakujibu hilo, kwani Hudhur[as] alikuwa na dai la unabii na aliita daraja yake kuwa unabii sio umuhaddathi pekee. Mbele kidogo Hudhur[as] amesema:

"Ikiwa apokeaye habari za ghaibu kutoka kwa Mwenyezi Mungu hapati jina nabii, niambieni basi, anaitwa jina gani? Kama mkisema, inapasa kumpa jina 'Muhaddathi; basi nasema kwamba katika kamusi yoyote maana ya neno Tahdith haikuandikwa kuwa ni 'kudhihirisha habari za ghaibu'. Lakini

[399] Ek Ghalati Ka Izala ─ Kuondoa Kosa Moja, uk. 9-12

'Utume', maana yake ndiyo 'kudhihirisha mambo ya ghaibu.''[400]

Katika maandishi hayo ya Hudhur[as] habari za Umuhaddathi zimeamuliwa kwa shani kubwa hata kwamba yeyote miongini mwa wanasibishao kwa Hudhur[as] dai la Umuhaddathi hana la kusema. Mkononi mwa wakanaji baada ya kukubali dai la Hudhur[as] la unabii na utume kulikuwa na mambo mawili tu makubwa miongoni mwa mambo mengine machache. Moja ni hili kwamba kila nabii analeta sheria, ni lazima kwa nabii kuleta sheria. La pili ni kwamba asiyeleta sheria aweza kuwa muhaddathi tu, hawezi kuwa nabii. Mambo hayo mawili yamebatilishwa tayari katika "Kuondoa Kosa Moja". Hudhur[as] anasema:

> "Na baada ya Mtume wetu s.a.w. mpaka Kiyama, hakuna nabii yeyote yule atakayeshukiwa na sheria mpya."

Ni dhahiri kutokana na kauli hii kwamba baada ya Mtume Mtukufu[saw], sawa na kauli ya Masihi Mau'udi[as] nabii aweza kuja (hapa, kulingana na madhumuni, muradi wa neno nabii ni dhati ya Hudhur[as] mwenyewe), lakini mpaka Kiyama hawezi kuja nabii ashukiwaye sheria mpya. Hudhur[as] anasema:

> "Si lazima kwa nabii kuleta sheria."

Baada ya maandishi wazi na bayana ya Hudhur[as], kusema kwamba wakati wa kuandika "Kuondoa Kosa Moja", muradi wa Hudhur[as] kwa maneno ya 'nabii' na 'mtume' ulikuwa ni muhaddathi tu, na Hudhur[as] alikuwa na yakini kwamba yeye si nabii wala mtume, bali ni muhaddathi tu, ni upuuzi na batili kabisa na ni sawa na msemo تَفْسِيْرُ الْقَوْلِ مَالَا يَرْضٰى بِهٖ قَائِلُهٗ[401], bali mbovu zaidi.

Katika madondoo ya Hudhur[as] yaliyo juu, ulitajwa unabii na utume wake na maelezo yake, na ilielezwa kuwa siyo sahihi jina muhaddath kwa ajili yake, na jina la nabii na mtume ni sahihi. Sasa katika dondoo lijalo imeelezwa kwamba kwa nini Hudhur[as] alikanusha mwanzoni madai ya unabii na utume na kwa nini

[400] Ek Ghalati Ka Izala ─ Kuondoa Kosa Moja, uk. 13

[401] Tafsiri ya kauli ambayo msemaji wake haridhiki nayo.

baadaye alikiri. Hudhur[as] anasema:

> "Nami popote nilipokana Unabii au Utume wangu, ni katika maana hii tu ya kwamba mimi sikuleta sheria yoyote mpya wala mimi siye nabii kwa kujitegemea. Lakini kwa njia hii ya kuwa nimepata habari za ghaibu kutoka kwa Mungu nikijipatia fadhili za kiroho kutoka kwa Mtume wangu nimfuataye – Muhammad[saw] – na kwa kupata jina lake na kwa sababu ya ***wasila*** wake, mimi ni Mtume na Nabii, lakini bila sheria yoyote mpya. Nami sikukana kamwe kuitwa nabii wa namna hii, bali katika maana hiyo hiyo Mungu Ameniita nabii na mtume; wala sikatai hata sasa kuwa kwangu nabii na mtume katika maana hii. Na usemi wangu huu:
>
> من نیستم رسول ونیاوردہ ام کتاب
>
> "Mimi siye mtume wala sikuleta kitabu, una maana hii tu ya kuwa mimi siye mwenye kuleta sheria mpya. Naam, inawapaseni kukumbuka jambo moja, wala msilisahau, ya kwamba juu ya mimi kuitwa kwa neno nabii na mtume nimeambiwa na Mwenyezi Mungu kuwa fadhili zote hizi hazikunifikia moja kwa moja bila wasila wowote, bali kuna dhati tukufu huko mbinguni ambaye baraka zake za kiroho nazipokea – yaani Muhammad Mteule[saw]."[402]

Ibara hiyo inadhihirisha waziwazi kwamba alivyojua Hudhur[as], yeye alikuwa na daraja ya unabi usio na sheria mpya ukiwa ni kivuli cha Mtume Muhammad[saw], bila kuzidi wala kupungua. Unabii aliopewa Hudhur[as] si kitu kingine kabisa isipokuwa unabii tu; huo bila shaka sio unabii wenye sheria mpya wala wa kujitegemea, lakini lazima ni unabii bila sheria mpya ukiwa kivuli cha Mtume Muhammad[saw]. Na huu hauwezi kuitwa kwa jina lolote lingine isipokuwa unabii tu, na Hudhur[as] alipata unabii huo kwa kupitia, na kwa baraka ya, Bwana wake amtiiye, Seyyidna Hadhrat Khatamun Nabiyyin[saw]. Kwa kufahamisha barabara unabii na utume wake, Hudhur[as] alikuwa

[402] Ek Ghalati Ka Izala ─ Kuondoa Kosa Moja, uk.15

mwangalifu kiasi hiki kwamba alipoona katika jambo lolote kuna nafasi ya kupatikana shaka, basi akalibainisha waziwazi, kama ilivyo dhahiri kutokana na maelezo yake ya mshororo huu:

”من نیستم رسول و نیاوردہ ام کتاب“

Kwa mshororo huo, ingeweza kuzuka shaka au ingeweza kuzushwa shaka kwamba Hudhur[as] anakanusha kuwa mtume, ilihali hakanushi kabisa kuwa kwake mtume; amekanusha kuleta sheria tu. Basi kwa kauli hii “Maana yake ni hii tu kwamba mimi si mwenye kuleta sheria”, Hudhur ameeleza uhakika waziwazi na amebainisha kama jua la utosini kwamba bila shaka Hudhur[as] ndiye mtume lakini si wa kuleta sheria mpya.

Ilmuradi, “Kuondoa Kosa Moja” ni kauli ya kwanza kimaandishi aliyotoa Hudhur[as] kwa kueleza daraja ya unabii wake, na baada yake katika kila kitabu alijiita kama nabii na mtume; hakujiita kamwe kuwa muhaddathi.

AMIN YA BASHIR AHMAD, SHARIF AHMAD NA MUBARAKA BEGAM, 30 NOVEMBA 1901

Kwa vile Hudhur[as] alikuja kwa kuimarisha Islam na kuhuisha sheria ya Kiislamu, kwa hiyo alizingatia mafundisho ya kidini ya watoto wake, na alifurahi sana kwa watoto wake kuhitimu Kurani Tukufu. Mwanaye Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad alipokuwa amehitimu Kurani Tukufu, alipanga sherehe kwa furaha kubwa iliyotajwa nyuma. Na sasa mwanaye Mirza Bashir Ahmad, mwanaye Mirza Sharif Ahmad na bintiye Nawab Mubaraka Begam walipohitimu Kurani Tukufu, basi kwa furaha hiyo pia akaitisha mkutano, tarehe 30 Novemba 1901, ambamo watu wengi kutoka nje pia walishiriki. Siku hiyo wenye hali ndogo na maskini walilishwa pia. Hudhur[as] aliandika shairi moja pia. Kwa vile shairi lile lina bishara adhimu, kwa hiyo kuandika hapa beti zake chache bila shaka zitafaa kuongeza imani ya ndugu. Hudhur[as] anasema:

> Ee Mungu, Mungu wangu Mpendwa, zipo tunu zako nyingi namna gani ulizonipatia.

Maana umenionyesha tena siku hii kwamba mwanangu wa pili pia ameshahitimu Kurani.

Bashir Ahmad Uliyemfundisha, Ukaliponya jicho lake, Ukamfanya aweze kuona.[403]

Sharif Ahmad pia Umemlisha tunda hili: Wewe Mwenyewe Umemfundisha Furkani.

Ni hisani zako, Ewe Mola wa viumbe, Umemhuisha[404] tena Mubarak pia.

Ulipomwita kwako kijana[405] mmoja, haraka sana Ukatufurahisha kwa kutujaalia wanne.

Ya huzuni ni siku moja, na ya furaha siku nne. Basi namtukuza Yule Aliyewafedhehesha maadui.

Na yupo binti[406] mmoja pamoja nao, huyu mwenye bahati njema umri wake ni chini kidogo ya miaka mitano.

Anasoma bila shida Neno la Mungu, ni fadhili ya Mungu na rehema tupu.

Katika ruya moja nimedhihirishiwa kwamba huyu naye atajaaliwa bahati bora sana.

Atapata lakabu ya heshima aliyowekewa, hiyo imekadiriwa tangu azali.

Mungu Amenijaalia wavulana wanne na binti huyu, basi hiyo ni hisani Yake tupu.

---

[403] Hadhrat Mirza Bashir Ahmad, ***Rahmani Amweke salama,*** alikuwa na matatizo machoni. Alitibiwa vya kutosha lakini hakupata nafuu. Hapo Hudhur[as] alimwomba Mwenyezi Mungu dua iliyokubaliwa na macho ya mwanaye yalipona kabisa. ***Alhamdulillahi.***

[404] Mwanaye Hadhrat Mubarak Ahmad pia safari moja aliugua sana, na Mwenyezi Mungu alimponya kwa dua ya Hudhur[as]. Kwa maelezo zaidi someni Hakikatul Wahyi, uk. 253

[405] Bashir wa kwanza

[406] Mubaraka Begam

Kama kila unywele wangu uwe wenye kunena, hata hivyo haiwezekani kutolewa shukurani barabara.

Ee Mungu Karimu, waondolee kila shari, Ee Rahimu, wajaalie kuwa wema na wajaalie umri mrefu.

Umkirimu pia yule aliyefundisha,[407] mpatie malipo bora katika dini na dunia.

Njia moja ya kufundisha[408] Umetuambia. Basi, namtukuza Yule Aliyewafedhehesha maadui.

Ee Mola wangu, ninalo ombi moja hili, najinyenyekeza na kulia kizingitini pako:

Watoto wangu Ulionijaalia, nipate kumwona kila mmoja wao kuwa yu mcha Mungu.

Hakuna uzio mbele ya kudra yako, uwape yote uliyonipa mimi.

U Mhisani wa ajabu, Ewe Bahari ya neema. Basi namtukuzu Yule Aliyewafedhehesha maadui.

Ee Mola, nakumbuka fadhili zako, Ulitoa bishara na kisha Ukanijaalia watoto hawa.

Ukasema, hawataangamia hao kamwe, watakua kama miboksi,[409] katika bustani.

Habari hiyo Umenipasha mara nyingi. Basi namtukuza Yule Aliyewafedhehesha maadui.

Ingawaje kwa furaha ya kuhitimu Kurani Tukufu kwa mwanaye, Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, Hudhur[as] alifanya sherehe pia na akawakaribisha wanajumuiya wa hapo na wa nje, na akaandika shairi moja lenye kichwa cha habari ***Mahmud ki Amin,*** na habari hii imeishatajwa katika matukio ya mwaka 1897, lakini jambo hili lina ladha ya ajabu kwamba alipoandika shairi la ***Amin*** wakati

[407] Hadhrat Pir Manzur Muhamad ndiye aliyewafundisha Kurani.

[408] 'Njia ya kufundisha' ni 'Yassarnal Kuran' iliyovumbuliwa na Hadhrat Pir Manzur Muhammad.

[409] Mboksi ni aina ya mti unaoitwa kwa Kiarabu Baqs na kwa Kiingereza Box tree.

walipohitimu Kurani Tukufu vijana wapendwa na binti mwenye bahati njema, humo pia aliona kuwa lazima amtaje mwanaye mwenye shani, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad. Ndani yake kuna sababu kubwa ya furaha na kuzidisha imani kwa wenye kutafakari. Hudhur[as] katika shairi hili hili tunalozungumzia sasa amesema:

> Ulitoa bishara kwamba yupo mwanao mmoja, atakayekuwa siku moja mpendwa wangu.
>
> Nitaondolea giza kwa njia ya 'mwezi' huo; Nitauzungusha ulimwengu.
>
> Bishara hiyo ni nini? Ni mlo wa moyo. Basi namtukuza Yule Aliyewafedhehesha maadui.

Hapa itafaa kutaja kwamba safari moja Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan, Chifu wa Maler Kotla, alimwandikia Hudhur[as] kuhusu sherehe ya ***Amin*** ya watoto wake kwamba hafla hiyo ya ***Amin*** ni mila au ni nini? Hudhur[as] alijibu kwa kirefu, muhtasari wake katika maneno ya Hudhur[as] ni huu:

> "Ninapofanya jambo lolote, lengo na nia yangu huwa kudhihirisha shani ya Mwenyezi Mungu, ndivyo hivyo ilivyotokea wakati wa sherehe hiyo ya ***Amin*** pia. Kwa vile wanangu hao ni ishara moja ya Mwenyezi Mungu, na kila mmoja wao ni mfano hai wa bishara za Mwenyezi Mungu, kwa hiyo naona faradhi kuthamini ishara hizi za Mwenyezi Mungu. Kwani, hao ni uthibitisho wa unabii wa Mtume wa Mungu s.a.w. na ukweli wa Kurani Tukufu na uwepo wa Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Wakati walipohitimu Neno la Mungu, niliambiwa kwamba kuhusu sherehe hiyo niandike beti chache za maombi ambamo ielezwe shukrani pia ya fadhili na rehema ya Mwenyezi Mungu. Kama nilivyosema sasa hivi, mimi hufikiria kuleta rekebisho. Nikaiona sherehe hiyo kuwa yenye baraka sana."[410]

[410] Al Hakam, 10 Aprili 1903

'AL MANAR'

Zama ambazo tunaandika habari zake, katika zama hizo gazeti moja lilikuwa likitoka liitwalo "Al Manar" kutoka Cairo. Hudhur[as] alipoandika kijitabu "Ijazul Masihi" kwa kuwafanya Pir Golarawii na masheikh wengine washindwe, alizipeleka nakala chache kwenye nchi za Kiarabu pia. Kwa kuwa katika kijitabu hicho Hudhur[as] alikuwa amesahihisha mawazo potofu ya Waislamu kuhusu swala la jihadi pia, kwa hiyo mhariri wa gazeti "Al Manar" kwa sababu ya uadui alipinga madhumuni ya Hudhur katika gazeti lake. Kwa njia fulani toleo lile lilifika katika Panjab pia. Mtu mmoja alichapisha makala hiyo katika gazeti "Chaudhawin Sadii" kwa kutia chumvi. Toleo hilo lilipotoka tu majahili walipata nafasi ya kudhihaki na wakaanza kupiga makelele kwamba tazameni mwenye lugha asili ya Kiarabu amekosoaje Kiarabu cha Bwana Mirza, ilihali makala yake haikuhusu Kiarabu, yeye alipinga mada ya makala, "jihadi". Naam, alisema kwamba "Tukitaka twaweza kuandika mithili yake." Kana kwamba alirudia usemi uliopo katika Kurani Tukufu: لَوْ نَشَاءُ لَقُلْنَا مِثْلَ هٰذَا . Lakini hata yeye pia hakuweza kuandika mithili yake wala asingeweza."[411]

Hudhur[as] alipojua madhumuni ya toleo hilo, alichapisha tangazo moja kwa kichwa cha habari "Al Manar", ambamo aliandika:

> "Wajinga hawakujua kwamba ukali wote huo ulitolewa ni kwa kusoma makala kuhusu kupinga itikadi ya jihadi. Katika Cairo hiyo hiyo, mhariri wa gazeti "Munadhir" aliye mhariri mwenye jina ambaye hata "Manar" pia linamsifu, anakiri wazi wazi katika jarida lake kwamba kitabu ***Ijazul Masihi*** bila shaka hakina mfano wake katika fasaha na balagha, na ametoa ushahidi waziwazi kwamba masheikh wengine hawataweza kabisa kuleta mfano wake. Wapinzani hao wapaswa wakiagiza jarida 'Munadhir' walisome kwa kufumbua macho na watuambie

[411] Katika mwaka huo, kwa kuunganisha madhumuni iliyobaki pamoja na hotuba alikamilisha uandishi wa kitabu.

kwamba kama mhariri wa "Manar" ndiye Mwarabu, je, na mhariri wa "Munadhir" si Mwarabu.? Bali "Munadhir" limeeleza waziwazi kwamba fasaha na balagha ya *Ijazul Masihi* kwa hakika ni ya kimwujiza. Na kisha mhariri wa "Hilal" pia lililo jarida la Wakristo, amesifu fasaha na balagha ya *Ijazul Masihi*, na jarida hilo pia latoka kutoka Cario. Sasa upande mmoja wako mashahidi wawili na upande wa pili kuna maskini 'Manar' peke yake."

VITABU VYA MWAKA 1901

Sehemu iliyokuwa imebaki ya Tuhfa Golarawiyya, 2. Khutba Ilhamiyya, 3. Ijazul Masihi,[412] 4. Ek Ghalati ka Izalah.

Vitabu hivyo vitatu na kipeperushi 'Ek Ghalati ka Izalah' vimeshatajwa kwa kirefu hapo juu.

NIDHAMU YA MICHANGO YA JUMUIYA, 5 MACHI 1902

Mpaka wakati huo hakukuwa na nidhamu maalumu ya michango ya Jumuiya. Wanajumuiya kwa ikhlasi yao walikuwa wakimpelekea Hudhur[as] mchango kiasi chochote walichopenda. Au kama yalizuka mahitaji maalum, Hudhur[as] alikuwa akieleza na wanajumuiya wakashiriki katika kuchanga sawa na ikhlasi yao. Lakini sasa idadi ya wanajumuiya ilikuwa inazidi siku hadi siku, na wageni pia walianza kufika kwa wingi, kwa hiyo matumizi ya Nyumba ya Wageni yalizidi sana. Vilevile kazi zingine pia zilianzia katika makao makuu zilizohitaji matumizi ya kudumu kila mwezi, kama vile Madrasa Ta'limul Islam, kuanzisha gazeti 'Review of Religions' na kadhalika. Kwa hiyo, ilisikika haja ya kuwa lazima kila mwanajumuiya ahimizwe kujilazimisha kutoa kiasi chochote cha mchango hata kama ni kidogo sana, kisha autoe kila mwezi mfululizo. Kwa lengo hili, tarehe 5 Machi 1902, Hudhur[as] alitoa tangazo moja ambamo akaandika:

"Sasa yapasa kwamba kila mtu baada ya kutafakari, aahidi kutoa mchango kila mwezi kiasi anachoweza, hata kama ni Paisa tu

[412] Kwa maelezo zaidi someni Dibaji ya Ijazul Masihi iliyochapwa huko Palestina na Maulana Abul Ataa Jalandharii, mbashiri wa zamani katika ncha za Kiarabu.

moja kila mwezi, lakini asiropoke wala kuongopa mbele ya Mungu. Kila mtu aliye mfuasi anapaswa ajilazimisha kutoa chochote kila mwezi hata kama ni Paisa moja au nusu yake. Na yule ambaye hajilazimishi kutoa chochote wala haisaidii Jumuiya hii kwa mwili, ni mnafiki. Sasa baada yake hataweza kubaki katika Jumuiya hii. Baada ya kutoa tangazo hili, hadi miezi mitatu litangojewa jibu la kila mfanya baiati kwamba anakubali kutoa mchango kiasi gani kila mwezi kwa kuisaidia Jumuiya hii. Na kama mpaka miezi mitatu jibu la mtu fulani halitafika, basi jina lake litafutwa katika wafanyao baiati na kutangazwa. Na kama mtu baada ya kuahidi kutoa mchango wa kila mwezi hakujali kuleta mchango kwa miezi mitatu, jina lake pia litafutwa. Na baada yake kila mwenye kiburi na kutojali ambaye hayumo miongoni mwa wasaidizi, hatabaki katika Jumuiya hii."[413]

ISHARA YA TAUNI NA MAENDELEO MAKUBWA YA JUMUIYA

Tumeshaandika juu kwamba kwanza kabisa tarehe 26 Februari 1898, kupitia tangazo moja, Hudhur[as] akataja ruya yake moja na akawaarifu watu kwamba tauni itaenea nchini, na tiba yake hakuna isipokuwa kutubu na kuomba ghofira. Kisha, tarehe 17 Machi 1901, vifo vilipoanzia kutokea nchini hapa na pale, ndipo aliwasihi watu kujiepusha na kufanya masihara na kujifanya huru na kutenda maovu, na kuleta mabadiliko mema ndani mwao. Lakini, ni masikitiko kwamba watu hawakujifaidisha na onyo hilo lililotolewa kwa wakati mwafaka, bali wakazidi katika kufanya dhihaka na masihara. Matokeo yake, Mungu Mwenye jalali akaighadhabikia ardhi, na mnamo mwaka 1902 tauni ilienea kwa nguvu kiasi hiki kwamba watu walianza kufa kama mbwa. Wakati mwingine watu wote katika baadhi ya nyumba walikutwa kushikwa na tanuni na hawakuwapo hata mtu wa kuwasaidia maji. Maiti zilioza nyumbani na hakuna aliyekuwa na moyo na uwezo wa kuzizika. Sababu ya kwanza ilikuwa kwamba watu waliosalimika na tauni hawakukaribia watu

[413] Kutoka katika tangazo la 5 Machi 1902 lililoandikwa katika Tablighe Risalat, J. 10

walioshikwa na tauni wakiogopa isije sisi pia tukashikwa na maradhi haya mabaya. Pili, kwa sababu ya maradhi kuenea kwa wingi na kwa nguvu, kama mtu mmoja akisalimika kwa nadra, basi alikuwa sawa na msemo wa Kiurdu "*Komamanga moja na wagonjwa mia.*" Yule maskini mmoja angaliweza kujaribu kuwahudumia wangapi na kuwaokoa! Matokeo yakawa kwamba watu walishikwa na msiba mkali na wa kutisha. Kwa sababu ya hali hizo, kwa mwongozo wa Mungu, Hudhur[as] alichapisha kijitabu kiitwacho "*Dafi'ul Balaa wa Mi'yaru Ahlil Istifaa*"[414]. Ndani yake, yeye kwanza aliwasisitizia watu usafi wa kidhahiri, tena aliwaelekeza kwenye tiba asilia na ya kweli iliyokuwa hii kwamba kwa kutubu madhambi na ukorofi wao wafanye suluhu ya kweli na Mwumba na Mmiliki wao, na waelekee kwa mtu aliyetumwa na Mwenyezi Mungu katika zama hizi. Katika kitabu hicho aliwakumbusha watu ufunuo ule aliouchapisha tarehe 26 Mei 1898 katika tangazo kwamba اِنَّ اللّٰهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتّٰى يُغَيِّرُوْا مَا بِاَنْفُسِهِمْ اِنَّهٗ اٰوَى الْقَرْيَةَ Yaani, Mungu amenuia kwamba Hataliondoa kamwe balaa hili la tauni mpaka watu waondolee mbali fikira zile zilizomo mioyoni mwao, yaani hadi wamkubali Mjumbe na Mtume wa Mungu, tauni haitaondoka. Na Mungu Mweza Huyu Atalinda Qadian na maangamizo ya tauni, ili mfahamu kuwa Qadian imehifadhiwa kwa sababu huyo mtume wa Mungu aliyetumwa naye alikuwa ndani ya Qadian.[415] Akieleza neno اٰوَى , alisema kwamba maana ya اٰوَى ni 'akilinda na maangamio na kusambaratika kuchukua katika ulinzi wake.' Kana kwamba maana ya اِنَّهٗ اٰوَى الْقَرْيَةَ ni hii kwamba Qadian itasalimika na tauni kali yenye kuangamiza inayoitwa kwa Kiarabu طَاعُوْنٌ جَارِفٌ yaani yenye kufagilia mbali, ambayo watu wanaikimbia kwenda huko na huko na wanakufa kama mbwa, na hakuna mwenye kuwajulia hali; aina hiyo ya hali haitatokea kamwe katika Qadian. Kwa kueleza ufunuo huo wa juu kuhusu Qadian akaeleza ufunuo wa pili pia kwamba: لَوْلَا الْاِكْرَامُ لَهَلَكَ الْمُقَامُ Yaani, "kama nisingejali heshima ya Jumuiya hii, ningehilikisha Qadian pia."

Kwa ufunuo huo mambo mawili yanaeleweka. (1) La kwanza,

[414] Kilichochapwa 23 Aprili 1902

[415] Dafi'ul Balaa, uk. 17

haidhuru kama tukio lolote litukie kwa nadra katika Qadian pia kiasi cha kuvumiliwa na binadamu ambalo lisiwe la kuangamiza na kuwakimbiza watu na kuwasambaratisha, kwani kitu cha nadra ni kama kisichokuwepo. (2) La pili ni kwamba katika vijiji na miji ambamo, kulingana na Qadian, wakaidi wakali, wakorofi, wadhalimu, waovu, wafisadi na maadui wakali wa Jumuiya hii wanaishi, hakuna budi tauni ya kuangamiza itazuka katika miji na vijiji vyao hata kwamba watu watakimbilia kila upande kwa kupotewa na fahamu. Tumekwisha eleza maana hizo za *Aawaa* sawa na upana wake. Nasi twaandika kwa uthabiti kwamba katika Qadian tauni iangamizayo haitaenea kamwe. Lakini kinyume chake katika miji na vijiji vingine vilivyo na dhuluma na ufisadi, lazima zitatokea hali za kuogofya. Katika dunia nzima ni Qadian pekee iliyotolewa ahadi hiyo, kwa hiyo, basi, twamhimidi Mungu."[416]

Katika kitabu hicho hicho mbele Hudhur[as] anasema:

"Nasema kweli kabisa kwamba waja wakati, bali upo karibu, ambapo watu watanikimbilia wakisema: "*Ya Masihal-khalki 'Adwana*." Hayo niliyotaja ni maneno ya Mungu, yanayomaanisha kwamba Ewe uliyetumwa ukiwa Masihi kwa viumbe, tufanyie maombezi kuondoa ugonjwa huu wa kuangamiza. Mwelewe kwa yakini kwamba leo hamna mwombezi yeyote minghairi ya Masihi huyu isipokuwa Mtume Mtukufu[swa]; na mwombezi huyu si mbali na Mtume Mtukufu[saw], bali maombezi yake kwa hakika ndiyo maombezi ya Mtume Mtukufu[saw]."[417]

Kadhalika Hudhur[as] aliandika akiwatolea changamoto wapinzani na wakadhibishao wote:

"Mimi nami nasema kwa kuapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba mimi ni Masihi Mau'udi na ndimi yule ambaye manabii waliahidi ujaji wake, na kunihusu mimi na zama zangu utabiri

[416] Dafi'ul Balaa, maelezo ya pembeni, uk. 18

[417] Dafi'ul Balaa, uk. 28

umo katika Torati, Injili na Kurani Tukufu kwamba wakati ule mbinguni jua na mwezi vitapatwa, na ardhini tauni kali itaenea. Na ishara yangu ndiyo hii kwamba kila mpinzani hata akikaa huko Amroha au Amritsar au Delhi au Calcutta au Lahore au Golra au Batala, kama atasema kwa kuapa kwamba mahali pake fulani patasalimika na tauni, basi lazima kabisa mahali hapo patashikwa na tauni, kwani amekosa adabu mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hilo halimhusu Sheikh Ahmad Hasan pekee, bali sasa wakati wa kushindana na watu wote kutoka mbinguni umekwishafika tayari. Watu wote wanaonifikiria kuwa mwongo, kama vile Sheikh Muhammad Husain wa Batala ambaye anajulikana kama Maulawii, na Pir Mehr Ali Shah wa Golra ambaye amewazuia wengi wasifuate njia ya Mungu, na Abdul Jabbar na Abdul Haki na Abdul Wahid wa Ghazni ambaye katika kundi la Maulawii Abdullah anaitwa mwenye kufunuliwa funuo, na Munshi Ilahi Bakhsh mhasibu ambaye dhidi yangu akidai kupata ufunuo amemfanya Maulawii Abdullah kuwa 'Sharifu' na hakuchukia kusema uwongo mtupu kabisa, na kadhalika Nadhir Husain wa Delhi ambaye ni dhalimu kitabia na ndiye wa kwanza kunikufurisha, hao wote wanapaswa kwamba katika hali kama hii walinde heshima ya funuo zao na imani yao, na watangaze kuhusu makazi yao kwamba yatalindwa katika tauni. Ndani yake imo heri tupu kwa watu na huruma kwa serikali, tena utukufu wa hao watu utathibitika na watahesabiwa mawalii; la sivyo, watapiga muhuri juu ya kuwa kwao waongo na wazushi."[418]

Tafakarini kwamba mtu ambaye watu walikuwa wanamwita mwongo na dajali (Mungu Apishe mbali) anapasha habari ya tauni kwanza miaka minne kabla ya ujio wa tauni, wakati ambapo haikuwepo alama yoyote pia ya maradhi hayo yenye kuudhi kisha wakati maradhi hayo yalipoenea nchini kwa nguvu yote na watu walianza kufa kama mbwa, anatoa habari ya kusalimika kwake na kwa maskani yake, na anawatolea changamoto wapinzani na wakadhibishao kwamba kama

[418] Dafi'ul Balaa, uk. 37-38

wao pia wanao uhusiano wowote na Mwenyezi Mungu, basi hao pia wachapishe madai yao ya aina hii. Kama maskani zao pia zikisalimika na tauni, basi nitawatambua miongoni mwa mawalii wa Mungu, lakini yeyote hakujipa moyo kujitokeza katika medani ya shindano.

AHADI YA KULINDA AD-DAR

Katika zama hizo, Hudhur[as] alifunuliwa ufunuo huu pia kwamba

اِنِّیْ اُحَافِظُ کُلَّ مَنْ فِی الدَّارِ اِلَّا الَّذِیْنَ عَلَوْا مِنِ اسْتِکْبَارٍ وَاُحَافِظُکَ خَاصَّةً ۔ سَلَامٌ قَوْلًا مِّنْ رَّبٍّ رَّحِیْمٍ

Yaani, nitamlinda na mauti ya tauni kila mtu atakayekuwa nyumbani mwako, isipokuwa watu ambao watajikuza kwa kiburi. Nawe nitakulinda hasa. Salamu kwako kutoka kwa Mungu."[419]

Kwa vile inadhihirika kutokana na ufunuo huo kwamba nyumba ya Hudhur[as] katika hali yoyote itasalimika kabisa na tauni, kwa hiyo aliwakaribisha ndugu wengi waje kukaa nyumbani mwake. Hadhrat Maulawii Abdul Karim pamoja na mkewe alikuwa tayari anaishi nyumbani mwa Hudhur[as]. Hudhur[as] aliwapatia nafasi nyumbani mwake Hadhrat Hafidh Hakim Nuruddin, Hadhrat Maulawii Muhammad Ahsan Amrohi na Maulawii Muhammad Ali pia. Zaidi ya hao baadhi ya familia zingine pia zilianza kuishi nyumbani mwa Hudhur[as]. Lakini juu ya kujumuika kwa watu wengi hivyo, mtu yeyote hakusumbuka hata kidogo. Na Mwenyezi Mungu akalinda kiasi hiki kwamba achilia mbali mwanadamu hata panya pia hakufa wakati wowote nyumbani mwa Hudhur[as].

TUKIO KUMHUSU LA MAULAWII MUHAMMAD ALI

Hudhur anasema:

> "Safari moja, katika siku za kuenea tauni kwa nguvu ambapo katika Qadian pia tauni ilikuwepo, Bwana Maulawii Muhammad Ali M.A. alishikwa na homa kali na akawa na dhana sana kwamba hiyo ni tauni. Yeye akaandika wasia wake kama watu wanaokufa, na akamfahamisha Mufti Muhammad Sadik mambo yote.Yeye alikuwa akiishi katika sehemu moja ya nyumba yangu,

[419] Nuzulul Masihi, uk. 23

ambayo kuihusu nyumba hiyo kuna ufunuo huu wa Mwenyezi Mungu: اِنِّیْ اُحَافِظُ کُلَّ مَنْ فِی الدَّارِ. Mimi nilienda kumjulia hali, nikamkuta katika wasiwasi na fadhaa. Nikamwambia kwamba kama ukishikwa na tauni, basi mimi ni mwongo na madai yangu kuwa napata ufunuo ni batili. Nikisema hayo, nikaweka mkono wangu juu ya mshipa wake wa damu, nikaona mfano wa kudra ya Mungu kwamba kwa kumgusa tu kwa mkono nikakuta mwili wake baridi, kulikuwa hamna alama ya homa kabisa."[420]

Ndiyo kusema kuwa Hudhur[as] alikuwa na yakini kabisa juu ya ufunuo wake kiasi hiki kwamba hakuweza hata kuwaza kwamba mtu yeyote anaweza kushikwa na tauni nyumbani mwake pia.

KASHTI-E-NUH, 5 OKTOBA 1902

Katika zama zile aliandika kitabu 'Kashti-e-Nuh' (Safina ya Nuhu), ambamo aliitolea shukrani serikali kwamba imepanga kudunga sindano kwa kulinda uhai wa raia. Lakini kujihusu yeye mwenyewe aliandika kwamba tunacho kizuizi cha kimbingu. Kama kisingekuwepo hicho basi tungepata sindano kabla ya wote, na kizuizi chenyewe ni hiki kifuatacho:

MFUASI KAMILI HANA HAJA YA KUDUNGWA SINDANO

"Mwenyezi Mungu Ametaka kuwaonyesha watu wa zama hizi ishara moja ya rehema ya kimbingu. Basi, Yeye Aliniambia kwamba wewe na yule atakayekuwa nyumbani mwako na Yule mwenye kukufuata kikamilifu na kukutii na kujipoteza ndani yako kwa uchamungu wa kweli, hao wote wataepushwa na ugonjwa wa tauni. Na hii itakuwa ishara ya Mwenyezi Mungu siku hizi za mwisho ili Apambanue baina ya kaumu mbalimbali. Lakini, asiyekufuata barabara, huyo hatokani nawe; usimhuzunikie. Hii ni amri ya Mwenyezi Mungu, ambayo kwa sababu yake sisi hatuna haja, wala wale wote wanaokaa nyumbani mwetu hawana haja yoyote ya sindano… sharti aache kila nia ya ukinzani na aingie katika silsila ya bai'ati kwa ikhlasi kamili, utii na unyenyekevu. Na mbele ya amri za Mwenyezi

[420] Hakikatul Wahyi, uk. 253, na Al Badr, J. 3 Na. 18, ya tarehe 8-16 Mei 1904

> Mungu na yule aliyetumwa naye asiwe mwenye kiburi na mwasi na mwenye majivuno na mwenye kughafilika, mkaidi na mwenye majisifu, bali matendo yake yalingane na mafundisho. Na pia aliniambia kwamba haitatokea katika mji wa Qadian tauni yenye nguvu ya kusababisha maangamio ambayo kwayo watu wafe kama mbwa, na wapotewe na fahamu kwa huzuni na mahangaiko.[421]

Mbele kidogo Hudhur[as] amesema:

> "Nasema kweli kabisa kwamba kama haikutokea ishara hii sawa na utabiri unaoendelea kutangazwa tangu miaka 20-22, basi sitakuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Alama ya kutoka kwangu kwa Mungu itakuwa ni kwamba watu waliohalisika wakaao katika nyumba yangu watalindwa na kufa kwa ugonjwa huu. Na Jumuiya yangu yote itahifadhiwa katika shambulio la tauni kuliko wengine, na usalama utakaokuwa ndani yao hautaonekana mfano wake katika kundi lolote lingine. Na katika Qadian haitatokea tauni kwa shida ya kutisha yenye kuangamiza isipokuwa kidogo tu na kwa nadra."[422]

KIFO KWA NADRA HAKIWEZI KUPUNGUZA HADHI YA ISHARA

Kisha akasema:

> "Asidhani mtu yeyote kuwa kama mmojawapo katika Jumuiya yetu akifa kwa tauni, thamani na hadhi ya ishara hii itapungua. Kwani, zamani Nabii Musa na Yesu na mwishoni Mtume wetu s.a.w. waliamrishwa ya kwamba wale waliokuwa wameinua upanga na kuwaua mamia ya watu, hao wauawe kwa upanga tu. Na hii ilikuwa ishara iliyoonyeshwa na manabii, ambayo baada yake ukapatikana ufaulu mkuu. Lakini katika mapigano na wakosefu, waaminio wenye haki nao pia walikuwa wanauawa kwa upanga wao, lakini wachache sana, na hasara hiyo kidogo ilikuwa haikupunguza thamani ya ishara ya Mungu. Basi,

[421] Kashti-e-Nuh, uk. 2

[422] Kashti-e-Nuh, uk. 4-5

> wakipata tauni watu wachache kabisa katika Jumuiya yetu kwa sababu zile tulizotaja juu, basi tauni kama hiyo haitashusha hadhi ya ishara ya Mungu. Je! hii si ishara kubwa kuwa mimi nakariri kusema kwamba Mwenyezi Mungu Atadhihirisha bishara hii kwa njia ambayo kwayo kila mtafuta haki hatakuwa na shaka yoyote, na atafahamu ya kuwa Mungu Ameitendea Jumuiya hii kwa njia ya kimwujiza. Bali ikiwa ishara ya Mungu, matokeo yatakuwa haya kwamba Jumuiya hii itazidi sana kwa njia ya tauni, na itapata maendeleo kimwujiza, na maendeleo yao haya yatatazamwa kwa mtazamo wa kustaajabia"[423]

Sawa na maelezo haya ya Hudhur[as], katika siku za tauni Mwenyezi Mungu Alionyesha ishara kubwa ya kuihifadhi Jumuiya ya Aahmadiyya kwamba juu ya kutodungwa sindano, kati ya Jumuiya ya watu maelfu, kesi kwa nadra tu ilitokea katika Jumuiya. Ni dhahiri kwamba huo ulikuwa mwujiza waziwazi ulioshuhudiwa na malaki ya mahuluku wa Mungu. Athari yake ilikuwa kubwa kiasi hiki kwamba vijiji kwa vijiji vikajiunga na Uahmadiyya. Wakati mwingine kila siku barua za baiati zilifika kutoka kwa watu mia kadha. Na katika siku zile mafundisho yake aliyoandika katika Safina ya Nuhu yalithibitika sindano la kimbingu ambayo kwayo Jumuiya yake ilisalimika na adhabu ya tauni.

HILAKI YA CHARAGH DIN JAMMUNI

Ni habari ya Aprili 1902, mtu mmoja aitwaye Charagh Din Jammuni aliyekuwa miongoni mwa wafuasi wa Hudhur[as], alishikwa na dhana kwamba yu mtume wa Isa, na ametumwa na Mungu ili awapatanishe Waislamu na Wakristo, na aondoe hitilafu ya Kurani na Injili. Hudhur[as] alipojua habari hii, alielekea kwa Mungu. Hapo alifunuliwa kumhusu yeye:

نَزَلَ بِهٖ جَبِيْزٌ

> Yaani, ***jabiz*** ilimshukia, na akaidhania kuwa ufunuo au ruya. ***Jabiz*** kwa hakika ni chapati iliyokauka isiyo na ladha ambayo

[423] Kashti-e-Nuh, uk. 12-13

haina utamu wowote, inayoweza kumezwa kwa shida tu. Na mtu bahili na mwenye kulaumiwa pia anaitwa ***Jabiz***, ambaye kitabia ana sehemu kubwa ya uchoyo, uduni na ubahili. Na hapa neno ***Jabiz*** lamaanisha mazungumzo na nafsi, na ndoto zilizovurugika ambazo hazina nuru ya kimbingu, na zipo alama za ubahili. Na fikira kama hizo huwa matokeo ya jitihada kavu, wakati wa tamaa na uchu au shetani anatilia moyoni fikara kama hizo; au kwa sababu ya ukavu na kwa majimaji yale ya nyongo wakati wa kutamani, fikira kama hizo zaingia moyoni. Na kwa kukosekana hali ya kiroho ndani yake, fikira za aina hiyo zinaitwa ***Jabiz*** katika istilahi ya Mungu. Na tiba yake ni toba, kuomba ghofira na kujiepusha kabisa na fikira za aina hiyo. La sivyo wingi wa ***Jabiz*** huhatarisha kuleta wazimu. Mungu Amlinde kila mmoja na balaa hii."[424]

Tena usiku fulani, mwezi ulikuwa unapatwa, Hudhur[as] alifunuliwa kumhusu yeye:

اِنِّیْ اُذِیْبُ مَنْ یُّرِیْبُ

Mimi Nitamwangamiza, Nitamhilikisha, Nitamteremshia ghadhabu ikiwa atashuku na hataamini; wala hatatubia madai ya ujumbe na utume."[425]

Mtu huyo alikuwa rafiki wa Maulawii Muhammad Ahsan Amrohi, yeye alipomsisitizia, akaleta kwanza barua ya toba yake tarehe 27 Aprili 1902 iliyochapishwa katika Al-Hakam,[426] lakini baada ya muda fulani akatawaliwa tena na umajinuni ule ule na safari hii alianza kwa jazba kubwa sana kutangaza madai yake. Bali kwa kumpinga Hudhur[as] akaandika kitabu pia alichokiita '***Manartul Masihi***', na — Mungu Apishe mbali — akamwita Hudhur[as] dajali aliyeahidiwa. Kwa kuchapwa kitabu hicho, ulipopita mwaka mmoja, akaandika kitabu kingine dhidi ya Hudhur[as] na humo kwa kukaribisha hilaki yake akaandika dua ya mubahala pia. Angalieni kudra ya Mungu,

[424] Dafi'ul Balaa, uk. 46, maelezo ya pembeni Na. 1

[425] Dafi'ul Balaa, uk. 47 maelezo ya pembeni Na. 2

[426] Al Hakam, 30 Aprili 1902

alipomkabidhi madhumuni ya mubahala yule fundi wa kaligarafia, naye alikuwa bado hajayapanga juu ya mbao za mawe, wanawe wote wawili wakafa wakishikwa na tauni. Na hatimaye tarehe 4 Aprili 1906, siku mbili tatu baada ya kifo cha wanawe, mwenyewe pia kafa kwa kupatwa na tauni. Na hivyo alidhihirisha kwa watu kwamba nani ni mkweli na nani mwongo. Jifunzeni, enyi wenye macho.

NDOA YA HADHRAT MIRZA BASHIRUDDIN MAHMUD AHMAD, OKTOBA 1902

Ndoa ya Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad (ambaye baadaye akawa Khalifatul Masihi II) ilikuwa imepangwa kufungwa na Hadhrat Mahmuda Begam, binti mwenye bahati njema wa Hadhrat Dkt. Khalifa Rashiduddin. Kwa kuwa Bwana Dkt. katika zama hizo aliajiriwa huko Rurki (U.P.), kwa hiyo mwanzoni mwa Oktoba 1902, katika uongozi wa Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin watu wachache walienda Rurki na kushiriki katika sherehe ya ndoa, na tarehe 5 Oktoba 1902 wakarudi Qadian. Ndoa ilitangazwa na Hadhrat Maulana kwa mahari ya rupia elfu moja. Binti alisindikizwa mwaka ujao mnamo Oktoba 1903, ambapo Bwana Dkt. alikuwa profesa katika Medical College Agra. Kwa kuchukua mke, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad pamoja na Hadhrat Mir Nasir Nawab wakaendea Agra kutoka Qadian, na wakarudi Darul Amaan tarehe 11 Oktoba 1903. Twamshukuru Mungu juu yake.[427]

KUANZISHA GAZETI AL-BADR

Bwana Babu Muhammad Afzal alikuwa mfanyakazi katika idara ya reli katika Afrika Mashariki. Mnamo mwaka 1902 baada ya kustaafu akarudi Qadian na akaanza kuishi katika Qadian Darul Aman. Kwa vile alikuwa mwenye akili na mwandishi, kwa hiyo alianzisha kutoka Qadian gazeti moja "Al-Qadian" katika Septemba 1902, lakini mwezi ujao tu, yaani katika Oktoba 1902, alibadilisha jina la gazeti hilo na akaliita "Al-Badr". Mheshimiwa Babu alifariki katika Machi 1905. Katika uhai wake gazeti hilo liliendelea vizuri, Bwana Babu alikuwa akichapisha kumbukumbu za kila siku za Hudhur[as] katika gazeti lake

[427] Al Hakam, 12 Oktoba 1903

kwa uangalifu sana. Baada ya kifo chake kwa muda fulani gazeti lilifungwa. Kisha tarehe 30 Machi, Hadhrat Mufti Muhammad Sadik alishikilia jukumu hilo. Bwana Babu alikuwa mmiliki kamili wa gazeti, sasa katika kipindi kipya mmiliki wa gazeti alikuwa Hadhrat Mian Merajuddin Umar[ra], na mhariri, Hadhrat Mufti. Sawa na mwongozo wa Hadhrat Maulawii Abdul Karim, jina la gazeti likabadilishwa likawa 'Badar' badala ya "Al-Badr". Hadhrat Mufti pia alifanya bidii sana kuboresha gazeti katika uhai wa Hudhur[as]. Yeye pia aliendelea kuchapisha kumbukumbu za kila siku za Hudhur[as] na funuo zake mfululizo. Kwa kweli magazeti hayo mawili, Al-Hakam na Al-Badr, au Badr yalikuwa mikono miwili ya Hudhur[as], yaliyoshiriki barabara katika kutangaza Jumuiya ya haki. Mwenyezi Mungu Awape malipo bora wahariri hao. Walifanya kazi kubwa sana.

MJADALA WA MUDD, WILAYA YA AMRITSAR, 29-30 OKTOBA 1902

Munshi Muhammad Yusuf na Muhammad Yakub walikuwa ndugu wawili, wakazi wa kijiji Mudd, wilaya ya Amritsar. Kwanza Bwana Munshi alifanya baiati. Kwa vile alikuwa akiishi Mardan, wilaya ya Peshawar, kikazi, kwa hiyo kijijini hakikutokea chochote, lakini alipofanya baiati ndugu yake Muhammad Yakub, kwa vile alikuwa akiishi kijijini, kwa hiyo upinzani mkali ulianzia kiasi hiki kwamba hata wanakijiji walimtenga. Yeye alimwandikia ndugu yake Muhammad Yusuf, naye akaja kijijini kwa kuchukua ruhusa. Akawafahamisha sana watu, lakini wakaendelea na upinzani wao. Hatimaye, iliamuliwa kwamba mjadala ufanyike juu ya masiala ya kuhitilafiana. Yeye akafika Qadian, akamwarifu Hudhur[as] kuhusu uamuzi huo. Hudhur[as] hakupenda mijadala, hasa mijadala ya kutoleana hotuba, lakini kwa sababu ya yeye kusisitiza, Hudhur[as] akakubali, na akamtuma Hadhrat Maulawii Seyyid Muhammad Sarwar Shah kwa kufanya mjadala. Upande wa pili alikuwa Maulawii Thanaullah Amritsari. Mjadala ulifanyika tarehe 29, 30 Oktoba 1902. Kwa hotuba za pande zote mbili dakika 20-20 ziliwekwa. Mjadala ulianzia juu ya uhai na kifo cha Masihi Mnazareti na ushukaji wa Masihi. Maulawii Thanaullah alipoona kwamba katika medani ya hoja hana chochote mkononi mwake, akaanza kushambulia dhati ya

Hudhur[as] na aliwachochea sana watu kiasi hiki kwamba hatari ya fujo ilitokea. Kuona hali hizo, watu wenye busara wakasimamisha mjadala. Hadhrat Maulawii Seyyid Muhammad Sarwar Shah alipohudhuria mbele ya Hudhur[as], akamwelezea yote yaliyotukia. Baada ya kusikiliza habari kamili, Hudhur[as] aliona kwamba mambo matatu ya Maulawii Thanaullah yajibiwe, yaani:

> La kwanza ni hili kwamba sawa na usemi wa Maulawii Thanaullah bishara zote za Hudhur[as] zilitokea batili.
>
> La pili, mimi niko tayari kufanya mubahala na Bwana Mirza.
>
> La tatu ni kwamba Hadhrat Maulawii Seyyid Muhammad Sarwar Shah alitaja "Ijazul Masihi" na akasema kwamba kama u mkweli kwa nini hukuandika jibu la "Ijazul Masihi", hapo Maulawii Thanaullah akasema kwamba nikitaka naweza kuandika jibu kwa urahisi sana.

UANDISHI WA 'IJAZE AHMADI'

Kwa kujibu mambo hayo matatu ya juu, Hudhur[as] aliandika kitabu "Ijaze Ahmadi" alichokianzia 8 Novemba 1902 na akamaliza 12 Novemba 1902; yaani, siku tano tu zilitumika kuandika kitabu hicho. Hudhur[as] aliandika katika kitabu hicho kuhusu Maulawii Thanaullah:

> "Maulawii Thanaullah, wakati wa mjadala wa Mudd, alisema hii pia kwamba bishara zote zikawa batili. Kwa hiyo, twamkaribisha kwamba kwa utafiti huu aje Qadian na azichunguze bishara zote. Na twaahidi kwa kuapa kwamba kwa kila utabiri utakaothibitika uongo kwa njia ya unabii tutampa rupia mia moja, waila 'medali' ya laana itabaki shingoni mwake. Tutatoa nauli pia ya kuja na kurudi. Bishara zote zitachunguzwa ili ugomwi usibaki kwa siku zijazo, na kwa sharti hiyo fedha itatolewa, na uthibitisho utakuwa juu yetu."

Maulawii Thanaullah alisema hii pia kwamba nipo tayari kufanya mubahala na Bwana Mirza. Hudhur[as] aliijibu hivi:

> "Basi kama Maulawii Thanaullah awe tayari kupokea changamoto kama hii, basi barua ya maandishi pekee

haitatosha. Bali yampasa achapishe tangazo la madhumuni haya kwamba: 'Namwona mtu huyu (hapa ataje jina langu waziwazi) kuwa mwongo, dajali na kafiri. Na mtu huyo anayedai kuwa Masihi Mau'udi na mwenye kupokea ufunuo na wahyi, nina yakini kwamba madai yake hayo ni ya uongo. Na Ee Mungu, nakuomba kwamba kama itikadi yangu hii si sahihi, bali mtu huyo kwa kweli ni Masihi Mau'udi, na kwa hakika Isa[as] ameshafariki, basi nifishe kabla ya kifo chake. Na kama mimi ni mkweli katika imani hiyo, na mtu huyo kwa kweli ni dajali, asiye imani, kafiri na muritadi, na Hadhrat Masihi[as] yuko hai mbinguni atakayerudi tena katika wakati usiojulikana, basi mhilikishe mtu huyo ili fitina na mafarakano yaondoke na Islam isipate kudhurika na dajali aongozaye vibaya na mwenye kupoteza. Amin tena Amin... Na kisha inapaswa kwamba juu ya tangazo kama hili la mubahala waheshimiwa angalao 50 watie saini. Na nakala kwa uchache 700 za madhumuni hayo yapaswa kuchapishwa nchini, na nakala 20 unitumie mimi pia kwa posta ya rejista. Sina haja ya kuwaita kwenye mubahala au nifanye mubahala dhidi yao. Mubahala wao wenyewe waliodhihirisha kufanya unatosha kwa ukweli wangu."

Jambo la tatu alilosema Maulawii Thanaullah ni kwamba nikitaka naweza kuandika kitabu mithili ya "Ijazul Masihi" katika lugha ya Kiarabu. Kwa kulijibu, Hudhur[as] alichapisha makala moja kwa Kiurdu na kasida moja kwa Kiarabu pamoja na tafsiri yake ya Kiurdu kwa jina la ***Ijaze Ahmadi***. Na sio Maulawii Thanaullah tu bali aliwakaribisha pia Pir Mehr Ali Shah Golarawii, Sheikh Asghar Ali Ruhi, profesa wa Kiarabu wa Islamia College Lahore, Sheikh Ali Hairii Mshia Mujtahid wa Lahore, Sheikh Muhammad Hasain Batalawii na Kadhi Zafruddin, profesa Oriental college Lahore, kwamba wachapishe makala ya Kiurdu katika kujibu makala ya Kiurdu, na kasida ya Kiarabu pamoja na tafsiri katika kujibu kasida ya Kiarabu, katika muda uliopangwa, hapo watapewa zawadi ya rupia elfu kumi. Akaandika hii pia kwamba watakuwa na haki ya

kupata zawadi yao kupitia mahakama pia."[428]

Baada ya kukamilika "Ijaze Ahmadi", Hudhur[as] aliwatuma, tarehe 16 Novemba 1902, Hadhrat Maulana Seyyid Muhammad Sarwar Shah na Hadhrat Sheikh Yakub Ali Mhariri wa Al-Hakam huko Amritsar kwa nakala yake moja ili kumfikishia Maulawii Thanaullah. Na siku hiyo hiyo aliwatumia nakala moja moja wapinzani wengine pia kwa rejista na akaeneza kitabu hicho kwa watu wote kwa jumla.

KALAMU ZA WAPINZANI ZIKAVUNJIKA

Muda uliowekwa ulikwisha, lakini mpinzani yeyote hakuweza kuleta mfano wa 'Ijaze Ahmadi'. Kalamu za wote zikavunjika. Naam, Kadhi Zafruddin, profesa Oriental College Lahore, alianza kuandika jibu la kasida. Bado alikuwa ameandika beti chache tu akaugua ghafula na akafa. Maulawii Thanaullah hakuandika jibu la kitabu Ijaze Ahmadi wala hakuwa tayari kufanya mubahala.

MAONI JUU YA MJADALA BAINA YA BATALAWII NA CHAKRALAWII

Mtu mmoja, aliyeitwa jina Maulawii Abdullah, alikuwa mkazi wa Chakrala, wilaya ya Mianwali. Mwanzoni, yeye alikuwa Ahle Hadith, kisha alikana kabisa Hadithi za Mtume wa Mungu s.a.w. na akaacha hata kusoma ***Attahiyyat*** au sala ya Mtume[saw] au maombi mengine yanayosomwa katika sala; na badala yake alitaka watu wasome aya za Kurani Tukufu tu. Hudhur[as] alipojua jambo hilo, akasikitika sana juu ya hali yake hiyo. Katika siku hizo hizo huyo mtu alifanya mjadala na Sheikh Muhammad Husain Batalawii. Kwa vile Hudhur[as] alikuwa Mwamuzi na Mwadilifu, kwa hiyo aliona lazima adhihirishe maoni sahihi kuhusu mjadala huo. Basi tarehe 27 Novemba 1902 alitoa maoni ya muhimu sana kimaandishi juu ya mjadala huo wa masheikh wawili ambamo aliandika:

> "Uhakika ni huu kuwa kundi moja kati ya mawili limeshika njia ya kuzidisha kupita kiasi, na la pili, njia ya kupunguza kupita kiasi. Kundi la kwanza, yaani la Sheikh Muhammad Husain, lina

[428] Kwa maelezo zaidi someni kitabu cha Hudhur[as] ***Ijaze Ahmadi***.

ukweli ndani ya jambo hili kuwa Hadithi za Mtume[saw] zilizo *mar'fu'a, muttasila* haziwezi kuhesabiwa kuwa ni kitu bure, kisicho na maana. Lakini asipojali kanuni ya kuhifadhi heshima ya kitu, anazidisha sana daraja ya Hadithi kiasi cha kuivunjia heshima Kurani Tukufu hata inalazimika kukataliwa. Hili ni kosa kubwa lililo wazi na ni kuachana na njia ya uadilifu. Mungu Mtukufu Anasema ndani ya Kurani Tukufu: فَبِاَيِّ حَدِيْثٍ بَعْدَ اللّٰهِ وَاٰيٰتِهٖ يُؤْمِنُوْنَ . Yaani, ni hadithi gani watakayoamini baada ya Mungu na aya Zake … Na mpinzani wake, Sheikh Abdullah, amechukua njia ya kupunguza kupita kiasi kwamba alizikataa Hadithi kabisa. Na kuzikataa Hadithi kwa maana nyingine ni kuikataa Kurani Tukufu pia kwani Mwenyezi Mungu asema ndani ya Kurani Tukufu: قُلْ اِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّوْنَ اللّٰهَ فَاتَّبِعُوْنِيْ يُحْبِبْكُمُ اللّٰهُ . Hivyo basi, maadamu kupata mapenzi ya Mwenyezi Mungu kunategemea kumfuata Mtume[saw], na ili kujua mifano ya matendo yake ambayo kumfuata yeye kunaitegemea, Hadithi pia ni njia mojawapo, basi yule anayeacha Hadithi, huacha pia njia ya kumfuata."

Mbele kidogo Hudhur[as] aliandika:

"Na njia iliyoonyoka ambayo kwa kuidhihirisha nimeandika makala hii ndiyo kwamba Waislamu wanavyo vitu vitatu mkononi mwao kwa kuimarika juu ya miongozo ya Kiislamu:

(1) Kurani Tukufu, iliyo Kitabu cha Mungu, ambayo hakuna maneno yoyote yawayo ya kweli kabisa na ya yakini zaidi kuliko hiyo, ni Neno la Mungu. Hamna shaka yoyote iwayo ndani yake.

(2) Cha pili ni Suna. Hapa tunazungumzia bila kujali istilahi za Ahli Hadithi, yaani sisi hatuchukulii Suna na Hadithi kuwa kitu kimoja kama ilivyo dasturi ya Muhadithina (wataalamu wa Hadithi) wa kawaida; bali Hadithi ni kitu kimoja na Suna kitu kingine. Kwa Suna tunamaanisha mazoea ya matendo ya Mtume s.a.w yanayofululiza, yaliyokuwepo pamoja na Kurani Tukufu tangu mwanzo na yatadumu kuwa pamoja nayo. Au kwa maneno mengine twaweza kusema kwamba Kurani Tukufu

ni kauli ya Mwenyezi Mungu, na Suna, matendo ya Mtume wa Mungu[saw]. Ni kawaida ya Mungu tangu kale kuwa manabii huleta kauli ya Mungu kwa kuwaongoza watu, nao hufafanua kauli hiyo kwa matendo yao ili watu wasiwe na shaka kufahamu kauli hiyo; wenyewe hutenda sawa na kauli hiyo na huitendesha kwa wengine pia.

(3) Njia ya tatu ya mwongozo ni Hadithi. Na kwa Hadithi tunamaanisha masimulizi yale yaliyokusanywa kwa njia ya wasimulizi mbalimbali kwa sura ya visa, miaka mia na hamsini takriban baada ya Mtume[saw].”[429]

VITABU VYA MWAKA 1902

1. ***Dafi'ul Balaa*:** (Kinga ya Balaa) Uandishi na uchapaji wa kitabu hicho kimeshatajwa nyuma.

2. ***Nuzulul Masih*:** Kitabu hiki kiliendelea kuandikwa na Hudhur[as] katika Julai, Agosti 1902, na kiliendelea kuchapwa pia papo hapo. Tumeshatangulia kuandika kwamba wakati wa kuandika kitabu hicho barua za Mian Shihabuddin na Maulawii Karmuddin, mkazi wa Bhiin, kuhusu wizi wa Mehr Ali Shah Golarawii zilifika, na Hudhur[as] aliziingiza katika “Nuzulul Masih”. Kitabu cha Hudhur[as] kilikuwa bado hakijachapwa, lakini Hadhrat Sheikh Yakub Ali Turab, mhariri wa Al-Hakam akatangulia na kuzichapisha barua hizo katika gazeti lake Al-Hakam. Hapo Maulawii Karmuddin alichukia na aliwaambia Waahmadiyya kwamba sasa nitawaoneni. Basi alichapisha barua katika gazeti la “*Sirajul Akhbar*” la Jhelum, la tarehe 6 Oktoba 1902, na kasida moja tarehe 13 Oktoba 1902 ambamo aliandika kwamba barua hizo ni za bandia na za uongo na kamwe hazikuandikwa nami. Kwa kujaribu tu kwamba anafunuliwa Bwana Mirza au hapana, nikimfanya mtoto fulani kuandika barua hizo nikamdanganya Bwana Mirza. Kwa kuona alivyotenda, Hudhur[as] aliahirisha uchapishaji wa Nuzulul Masih kwa muda usioelezwa. Katika muda huo, Maulawii Karmuddin aliwashtaki mahakamani Hudhur[as], Hadhrat Sheikh

[429] Kutoka kijitabu “Review Bar Mubahatha Batalawii wa Chakralawii” — Maoni juu ya Mjadala Baina ya Masheikh Wawili.

Yakub Ali Turab, Mhariri wa Al Hakam, na Hadhrat Maulawii Fadhl Din Bherawii kwa sababu ya barua hizo. Kesi iliendelea kwa miaka miwili au miwili na nusu. Kitabu hicho kilibaki hivi hivi bila kukamilika na katika hali hiyo baada ya kifo cha Hudhur[as], tarehe 25 Agosti 1909 kilichapwa.

3. **Uchapaji wa Tuhfa Golarawiyya:** Kitabu hiki kimeshatajwa hapo juu kwamba kilianzia kuandikwa mnamo mwaka 1900 na kilikamilika mwaka 1901, lakini kilichapwa katika mwaka 1902.

4. **Uchapaji wa Tuhfa Ghaznawiyya:** Kitabu hiki pia kiliandikwa katika mwaka 1900, lakini kilichapwa katika mwaka 1902.

5. **Khutba Ilhamiyya:** Sehemu ya mwanzo ya kitabu hiki ni ile hotuba ya Idi aliyotoa Hudhur[as] kwa amri ya Mwenyezi Mungu siku ya Idul Adh'ha ya mwaka 1900. Lakini sehemu iliyobaki ni ya mwaka 1901, lakini hicho pia kilichapwa katika mwaka 1902.

6. **Tiryakul Kuluub:** Maelezo yake yameshaandikwa katika matukio ya 1899 kwamba kitabu hiki kiliandikwa katika mwaka 1899, lakini kilichapwa mnamo mwaka 1902.

7. **Kashti-e-Nuh:** Kimeshatajwa mapema.

8. **Tuhfatun Nadwa:** Kitabu hiki kiliandikwa kwa kujibu kijitabu: Qat'ul Watiin, cha Abu Is'hak Muhammad Din. Katika kitabu hicho Hudhur[as] amefafanua kirefu aya لَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا... .

9. **Ijaz Ahmadi**: Kitabu hiki pia kimeshaelezwa mapema.

10. **Review Bar Mubahatha Batalawii Wa Chakralawii:** Kijitabu hiki pia kimeshaelezwa juu.

UJAJI WA MAULAWII THANAULLAH AMRITSARI KATIKA QADIAN, 10 JANUARI 1903

Hapo juu imeshaelezwa chini ya kichwa cha habari 'Uandishi wa Ijaze Ahmadi' kwamba Maulawii Thanaullah Amritsari alisema pia katika mjadala wa Mudd kwamba utabiri wowote wa Bwana Mirza haukuthibitika kuwa kweli, na katika kuijibu Hudhur[as] alisema kwamba "Twamkaribisha (Maulawii Thanaullah) kwamba aje Qadian kwa kufanya utafiti na azichunguze bishara zote." Kwa hiyo Bwana

Maulawii alifika Qadian tarehe 10 Januari 1903. Na badala ya kukaa kwa Hudhur[as] alikaa katika Mandir ya Waaria walio wapinzani wakali wa Islam na Uahmadiyya. Na siku ya pili alimwandikia Hudhur[as], "Nimeshafika Qadian sawa na mwito wa Ijaze Ahmadi. Nategemea utafanya kila linalowezekana kunifahamisha, na sawa na ahadi utaniruhusu kwamba katika hafla nieleze mawazo yangu juu ya bishara zako." Hudhur[as] alimkaribisha Maulawii Thanaullah kwa kuchunguza bishara sio kufanya mjadala. Kwani baada ya kufanyika mijadala mingi, kwa sababu watu hawaachi ujeuri wao, alishatangaza kwa kuapa katika kitabu chake "Anjame Atham" kwamba tangu sasa mjadala hautafanyika na watu hao. Lakini Maulawii Thanaullah alitaka kuanzisha mjadala ili kama Hudhur[as] akikubali, Bwana Maulawii apate nafasi ya kusema kwamba amevunja kiapo chake. Na asipokubali, basi Bwana Maulawii aseme kwamba ingawaje aliniita lakini amekataa kuiondolea shaka. Basi, Hudhur[as] alimwandikia kwamba kwa kutafiti utabiri njia hii inatosha kwamba utabiri ambao unayo shaka nao niandikie katika mistari miwili hivi, nami nitakujibu. Kama ikizuka shaka nyingine, hiyo nayo waweza kuniandikia tena pia. Usipokubali hii, basi sawa tu. Nami kutofanya mijadala nimeshatangaza katika "Anjame Atham". Lakini kwa vile lengo la Maulawii Thanaullah halikuwa kuondoa shaka kuhusu bishara, bali akaja Qadian kwa lengo la kupanga mjadala kwa njia yoyote, kwa hiyo hakuridhia na maoni ya Hudhur[as], na akarudi Amritsar, na kwa njia hii utabiri wa Hudhur[as] alitimia kwamba Maulawii Thanaullah hatakuja kamwe kwangu Qadian kwa kuchunguza bishara zote."[430]

SAFARI YA KWENDA JHELUM KWA KESI YA MAULAWII KARMUDDIN, 15 JANUARI 1903

Sababu ya kesi hiyo imeshaelezwa hapo juu kwamba Pir Mehr Ali Shah Golarawii aliandika kitabu chake "Saife Chishtiyai" kwa kuiba kumbukumbu za Maulawii Muhammad Hasan, mkazi wa Bhiin, na hakutaja hata jina lake huyo maskini katika kitabu chake. Barua ambazo Hudhur[as] na Hadhrat Maulawii Abdul Karim Sialkoti na Hadhrat Maulawii Fadhl Din Bherawii waliandikiana na Mian

[430] Kwa maelezo someni Al Hakam, 7 Februari 1903

Shihabuddin na Maulawii Karmuddin mkazi wa Bhiin, hizo Hadhrat Sheikh Yakub Ali, Mhariri wa Al-Hakam, alizichapisha. Maulawii Karmuddin akakasirika sana kwa uchapaji wake, na akaandika katika "Sirajul Akhbar" la Jhelum kwa kuwafurahisha wafuasi wa Pir Mehr Ali Shah kwamba sikumwandikia kamwe Bwana Mirza barua yoyote, bali nilimtahini tu Bwana Mirza kuwa kweli anafunuliwa kwa kumfanya mtoto fulani aziandike, na kadhalika. Baadaye, katika mahakama ya Lala Sansaar Chand katika Jhelum akawashtaki watu hao watatu kwa kumkashifu, chini ya vifungu vya 500-501 na 502 vya kanuni ya India kuhusu adhabu. Kwa ajili ya yake Hudhur[as] alilazimika kwenda Jhelum.

UTABIRI WA KUONDOLEWA KWA KESI NA UENEZAJI WA UTABIRI

Mwaka mmoja kabla ya kesi hii, Mwenyezi Mungu Alimwonyesha ruya hii mara kwa mara kwamba mtu mmoja duni atataka kuvunja heshima yako lakini atashindwa kabisa katika matamanio yake.

Siku hizo, yeye alikuwa akiandika kitabu chake cha Kiarabu "Mawahibur Rahmani". Kabla ya kwenda safari ya Jhelum, alitaka kuandika humo ruya hiyo kama utabiri na kuchapwa pia kabla ya kwenda Jhelum. Basi, alichapisha ruya hiyo katika Mawahibur Rahmani.

Tarehe ya kesi ilikwishawekwa kuwa 17 Januari 1903. Kwa hiyo, Hudhur[as] akaondoka Qadian tarehe 15 Januari. Njiani, tarehe 16 Januari, huko Lahore Hudhur[as] alifunuliwa: أُرِيْكَ بَرَكَاتٍ مِّنْ كُلِّ طَرَفٍ , yaani nitakuonyesha baraka kutoka kila upande. Wakati uo huo Hudhur[as] aliwaambia ndugu wote ufunuo huu. Alikaa usiku huko Lahore. Tarehe 16 Januari 1903, alielekea Jhelum kwa garimoshi. Kuanzia Lahore mpaka Jhelum, kwenye stesheni zote, yaani Lahore, Gujaranwala, Wazirabad, Gujrat, Lala Musa na Jhelum, walijazana wenye shauku ya kumwona. Kwa sababu ya kumalizika tiketi za kuingilia stesheni watu wengi wakivunja vizuizi wakaingia stesheni. Kila mtu alikuwa na kiherehere sana kwa kutazama uso wake mtukufu. Wafanyakazi wa reli pia waliwatendea watu kwa upole. Katika baadhi ya sehemu garimoshi halikuondoka kwa wakati wake,

gari lilipokuwa linaondoka ilikuwa vigumu kuwatenganisha watu na gari, kwa muda fulani watu walikuwa wakikimbia na gari. Njiani mtu mmoja Mwingereza mwanaume na mama mmoja Mwingereza walijaribu kupiga picha ya Hudhur[as] kwenye kila stesheni lakini hawakuweza kufanikiwa. Kwenye stesheni ya Gujrat, Chaudhari Nawab Khan, Mkuu wa tarafa ya Gujrat, alimkaribisha yeye na wenzake kwenye chai na chakula. Kwa shida sana garimoshi lilipofika stesheni ya Jhelum, watu walikuwa wamejazana kiasi hiki kwamba popote ulipoona, halaiki ya watu walionekana. Hudhur[as] alipangiwa behewa la daraja ya pili. Sawa na desturi ya zama zile, ilikuwa lazima kwamba kwenye stesheni ya Jhelum behewa lile lingetangwa na gari, lakini halaiki wengi walijumuika huko kiasi hiki kwamba haikuwa nafasi kwa injini kutenganisha behewa. Kwa shida sana Hudhur[as] alitoka stesheni na kapanda gari la mafarasi wawili. Raja Ghulam Haidar, ambaye wakati wa kesi ya Dkt. Henry Martin Clark alikuwa karani wa Disii wa Gurdaspur, alikuwa Mkuu wa Tarafa huko, yeye aliendelea kuzuia watu na kusawazisha njia kwa gari la mafarasi la Hudhur[as]. Hali ya mji wa Jhelum ilikuwa kwamba kwa kujua ujio wa Hudhur[as], watu wengi walijumuika barabarani, juu ya mapaa ya nyumba na mitini. Siku ile, Hudhur[as] alikuwa na nguvu ya kuvutia na usoni mwake nuru ilimetameta kiasi hiki kwamba mtu yeyote aliyemwona, hakutaka kutengana naye. Moyo wa kila mtu ulitaka kwamba aendelee kumwona yeye tu kwa masaa. Kwa ajili ya Hudhur[as] kukaa, Sardar Hari Singh, Chifu Mkuu wa Jhelum alitoa nyumba yake iliyokuwa kando ya mto Jhelum. Hudhur[as] aliingia nyumbani humo, lakini halaiki ya watu kwa kumwona kwa shauku walikuwepo nje ya nyumba walitaka Hudhur[as] kwa vyovyote. Kwa kuona hali hii kwamba watu hawaendi nyumbani kwao, Raja Ghulam Haidar Khan alimwendea, Hudhur[as], akamtajia kuwepo kwa halaiki kubwa na akimwelezea matakwa yao akamwomba Hudhur[as] kwamba kama Hudhur[as] apande juu ya nyumba na akae hapo kwa muda mfupi, basi matakwa ya wenye shauku ya kumwona yatimie na kisha waende kwao. Hudhur[as] akakubali ombi la Bwana Raja. Kiti kiliwekwa juu ya nyumba ambapo Hudhur[as] alikaa kwa muda kidogo, kisha akateremka chini, na watu walienda nyumbani kwao. Jumuiya

ya Jhelum ilitimiza wajibu wa ukaramu vizuri sana na waliendelea kuwalisha mamia ya watu kwa siku tatu, asubuhi na jioni, kwa mpango mzuri. Mungu Awajaalie malipo bora.

Siku ya pili, yaani 17 Januari 1903, ilikuwa kesi mahakamani. Hudhur[as] alikaa kitini nje ya mahakama chini ya mti mkubwa na kwa watu pia viti vingi vilikuwepo. Hadhrat Seyyid Abdul Latif pia alikuwa pamoja na Hudhur[as] katika safari hiyo, na Khan Ajab Khan wa Zedah pia alikuwapo. Maelfu ya watu walijumuika huko. Kwa kuona mvuto huo na uwezo wa kiroho, Khan Ajab Khan alimwomba Hudhur, "Ningependa kubusu mkono wa Hudhur". Mara Hudhur[as] akatoa mkono wake na Bwana Khan akaubusu kwa jazba ya mapenzi. Baada yake, Hudhur[as] alitoa hotuba yenye maarifa iliyosikilizwa kwa makini sana. Kesi ilipotajwa mahakamani, Bwana Lala Sansar, Hakimu wa daraja ya kwanza, kwa kumwona tu Hudhur akasimama kwa heshima. Halaiki ya watu walijumuika mahakamani pia. Kesi ilitajwa. Maulawii Karmuddin alikuwa amewashtaki Hudhur[as], Hadhrat Shiekh Yakub Ali Turab na Hadhrat Hakim Maulawii Fadhl Din Bherawii. Dhidi ya Hudhur[as] shtaka lilikuwa kwamba ametumia maneno katika kitabu chake Nuzulul Masih yanayovunja heshima ya Muhammad Hasan Bhiin. Ikumbukwe kwamba "Nuzulul Masihi" kilikuwa bado hakijachapwa, Maulawii Karmuddin akiiba kwa njia ya mtu fulani kurasa chache zilizochapwa aliziunganisha na kesi. Dhidi ya Hadhrat Sheikh, lawama ilikuwa hii kwamba amechapisha barua za Maulawii Karmuddin katika gazeti lake, na aliandika pia kidogo juu ya Muhammad Hasan Faidhi. Dhidi ya Hadhrat Sheikh Fadhl Din lawama ilikuwa hii kwamba yu mmiliki wa kiwanda cha uchapaji. Karmuddin aliyekuwa mshtaki, akasisitiza haki ya kuwashtaki kwamba mimi ni ndugu wa mke wa marehemu na ni msimamizi wa watoto wake, kwa hiyo nimehuzunika kwa maneno hayo ya kuvunja heshima, na yafaa nipewe haki ya kupokea faini mahakamani kutoka kwa walioshtakiwa. Wakili wa Hudhur[as] alikuwa Khwaja Kamaluddin na wasaidizi wake walikuwa Maulawii Muhammad Ali M.A., Sheikh Nur Ahmad na Mian Azizullahi. Mawakili walileta swali kwamba je, sawa na sheria, Maulawii Karmuddin anaweza kuwa mrithi wa halali wa marehemu hata

kwamba awe na haki ya kuwashtaki ambao wametuhumiwa kutumia maneno ya kuvunja heshima ya marehemu? Jambo hilo lilijadiliwa sana. Baada ya kusikiliza majadiliano, hakimu aliamua kwamba wakati baba, mjane na wanawe wapo, Karmuddin hana haki kwamba amshtaki yeyote. Na haitoshi kusema kwake kwamba nimehuzunika kwa kusikiliza maneno ya kuvunja heshima ya marehemu. Hiyo ni dhana tu ambayo haina uthibitisho. Basi katika hali hiyo mshtaki hawezi kupewa haki ya kufungua kesi kuhusu faini, kwa hiyo kesi inafutwa.

Baada ya kuondoka mahakama, Hudhur[as] alirudi kwenye makazi yake. Nasaha na mawaidha yalikuwa yanaendelea muda wote. Watu kutoka sehemu zote za Panjab walijumuika kwa wengi kumwona Hudhur[as]. Baiati ilipoanzia, wanaume 1100 na wanawake 200 walifanya baiati. Watu walitoa zawadi kwa mapenzi na unyenyekevu sana, na Hudhur akarudi kwa baraka za aina zote. Itakuwa vizuri ikinukuliwa hapa maneno ya gazeti moja lisilo la Waahmadiyya la "*Panjae Faulad*" la Lahore. Gazeti hilo liliandika:

> "Wakati wa kurudi kutoka Jhelum, Mirza Ghulam Ahmad Qadiani alifika Wazirabad. Ingawaje alikuwa hana mpango wa kuja mjini wala hakutoa taarifa ya kuja kwake, na mpango ulikuwa kukaa stesheni tu kwa dakika chache, hata hivyo halaiki kubwa ya watu walijazana kwenye platfomu ya stesheni hata kwamba haikubaki hapo nafasi yoyote. Kama mkuu wa stesheni aliye mwenye hulka njema na ni mchangamfu asingepanga mpango mzuri, bila shaka ilikuwa hatari ya watu wengi kukanyagwa na kwa yakini wengi kujeruhika. Kwa kumwona Bwana Mirza, Mabaniani na Waislamu walikuwepo kwa shauku sana."

Tarehe 18 Januari Hudhur[as] akawasili Lahore kutoka Jhelum, na tarhe 19 Januari 1903 akafika Qadian, Darul Amaan.

UAMUZI WA OMBI LA UANGALIZI LA MAULAWII KARMUDDIN

Baada ya Hudhur[as] kurudi, Maulawii Karmuddin alipeleka ombi la

uangalizi katika Mahakama ya Jinai ya Jaji wa Jhelum dhidi ya uamuzi wa Lala Sansaar, Hakimu wa daraja ya kwanza. Tarehe 15 Mei 1903 ilipangwa kusikilizwa kesi hiyo. Hadhrat Shiekh Yakub Ali Turab na Hadhrat Hakim Maulawii Fadhl Din Bherawii pamoja na mawakili walifika tarehe iliyopangwa. Kesi ilianza, baada ya kusikiliza hoja za pande mbili, Jaji alipanga tarehe 29 kwa kutoa uamuzi. Tarehe hiyo Jaji alifuta uangalizi huo. *Alhamdulillahi.*

KESI TATU DHIDI YA MAULAWII KARMUDDIN

Kwa vile kesi za Maulawii Karmuddin zinazungumzwa, hivyo inaonekana yafaa kesi za baadaye pia zitajwe hapa hapa.

Maulawii Karmuddin alikuwa ameandika baadhi ya makala kinyume cha heshima ya Hudhur[as] katika "Sirajul Akhbar" la Jhelum, la tarehe 6 na 13 Oktoba 1902, na aliandika hii pia kwamba sikuandikiana kamwe na Bwana Mirza. Barua zilizochapishwa katika "Al Hakam" kwa jina langu, sikuziandika. Kwa hiyo, Hudhur[as] alitaka iamuliwe kupitia mahakama kwamba kumbukumbu zile alizoandika marehemu Muhammad Hasan Faidhi kwenye *Ijazul Masihi* na *Shamse Bazigha*, ambazo Pir Mehr Ali Shah Golarawii aliziingiza katika kitabu chake *Saife Chishtiyai* kwa kuziiba, ziliandikwa kwa mkono wake mwenyewe au hapana? Na je, barua alizoziandika Maulawii Karmuddin kupeleka Qadian ni za kibandia au za kweli? Basi tarehe 14 Novemba 1903, mashtaka matatu yalifunguliwa dhidi ya Maulawii Karmuddin katika mahakama ya Lala Ganga Ram, Hakimu wa daraja ya kwanza wa Gurdaspur.

1. Kesi moja ya kudanganya ilikuwa kutoka kwa Maulawii Hakim Fadhl Din Bherawii dhidi ya Sheikh Karmuddin kwamba kama kauli yake hii ni sahihi aliyochapisha katika "Sirajul Akhbar", basi ametudanganya.

2. Kesi ya pili pia ilikuwa kutoka kwake kwamba kuchukua kutoka kiwanda changu cha uchapaji, kurasa za kitabu ambacho kilikuwa hakijatolewa, ni wizi dhahiri.

3. Kesi ya tatu ilikuwa ya kuvunja heshima, kutoka kwa Hadhrat Sheikh Yakub Ali, mhariri wa Al-Hakam. Kwani Maulawii

Karmuddin aliandika baadhi ya mambo katika "Sirajul Akhbar" dhidi ya Bwana Sheikh yaliyokuwa kinyume cha heshima yake binafsi. Katika kesi hiyo pamoja na Maulawii Karmuddin alishtakiwa pia Fakir Muhammad, mhariri wa "Sirajul Akhbar" la Jhelum.

KESI YA MAULAWII KARMUDDIN

Maulawii Karmuddin akaona kwamba kesi ya heshima binafsi aliyofungua katika mahakama ya Lala Sansaar Chand, Hakimu wa daraja ya kwanza wa Jhelum, dhidi ya Bwana Mirza imeshafutwa, na uangalizi alioomba katika mahakama ya Jinai ya Jaji pia umeshafutwa, basi, alifungua kesi dhidi yake katika Jhelum ya kuvunjiwa heshima yake binafsi kwa sababu ya utabiri ulioandikwa katika kitabu cha Hudhur[as] "Mawahibur Rahmani". Ndani yake madhumuni ilikuwa hii kwamba Mwenyezi Mungu Amenipasha habari kwamba atanisingizia mtu mmoja aliye ***kadh-dhab*** (mwongo sana) na ***laimu*** (duni) na atajaribu kuvunja heshima yangu, lakini hataweza kunidhuru. Maulawii Karmuddin aliandika katika kushtaki kwamba katika ibara hiyo ameniita ***kadh-dhab*** na ***laimu***, na maana ya ***kadh-dhab*** ni mwongo na mwongo sana pia, na maana ya ***laimu*** ni 'duni', lakini wakati mwingine mwanaharamu pia anaitwa ***laimu***. Kwa hiyo, kwa kutumia maneno makali ya namna hii, Bwana Mirza amevunja heshima yangu. Papo hapo akamshtaki Hadhrat Hakim Maulawii Fadhl Din pia kwamba kitabu ***Mwahibur Rahmani*** kilichapwa katika matbaa yake. Ilmuradi, kesi zilianzia kutoka pande zote mbili.

MAOMBI YA UHAMISHO WA KESI

Maulawii Karmuddin alitaka kwamba kesi hizo zisikilizwe Jhelum, na Hudhur[as] alitaka kesi hizo zisikilizwe Gurdaspur. Maulawii Karmuddin alipopeleka ombi lake kwenye mahakama kuu kwa kuhamisha kesi huko Jhelum, Hadhrat Shiekh Yakub Ali Turab na Hadhrat hakim Maulawii Fadhl Din pia walitumia ombi kwenye mahakama kuu kwamba kesi ya Jhelum ihamishwe Gurdaspur. Hapo ombi la Maulawii Karmuddin lilikataliwa, na la Bwana Sheikh lilikubaliwa. Na tarehe ya kwanza kwa kusikiliza kesi hizo ikawa 15 Mei 1903 katika Gurdaspur.

Lala Ganga Ram, Hakimu, ameshatajwa juu kwamba katika mahakama yake kesi za kuvunja heshima zililetwa, lakini katika hali hiyo, yeye alipata uhamisho na badala yake akaja Mwaria mmoja, adui mkali, Lala Chandu La'l.

Kesi ya kwanza: Kesi ya kudanganya iliyosajiliwa na Hadhrat Hakim Maulawii Fadhl Din dhidi ya Maulawii Karmuddin, ilikuwa kwamba kwanza Maulawii Karmuddin alisema kuwa kumbukumbu zilizoandikwa kwenye 'Ijazul Masihi' na 'Shamse Bazigha' ni za marehemu Maulawii Muhammad Hasan na baadaye aliandika katika 'Sirajul Akhbar' la Jhelum kwamba hizo hakuziandika yeye. Katika kesi hiyo jambo hili lingebainika na vilevile ingesadikika kwamba barua ambayo Pir Mehr Ali Shah Golarawii alimwandikia Maulawii Karmuddin ambamo alikuwa amekiri kwamba alinukuu kumbukumbu za marehemu Muhammad Hasan katika 'Saife Chishtiyai', barua hiyo ilikuwa yake au ya mtu mwingine. Bwana Pir Golarawii aliitwa mahakamani tarehe 22 Juni 1903, lakini kwa vile alijua uhakika wenyewe, kwa hiyo aliepa kwa kutuma cheti cha daktari. Baadaye pia aliitwa mara kadha mahakamani, lakini kila mara alituma cheti cha daktari, na hiyo akaja chini ya athari ya fatuwa ya Kurani Tukufu kwamba مَنْ يَكْتُمْهَا فَإِنَّهُ اٰثِمٌ قَلْبُهُ, yaani anayeficha ushahidi, basi moyo wake una dhambi.

Kwa kujikinga na mashtaka ya udanganyifu, Maulawii Karmuddin alikanusha makala zile alizozichapisha katika 'Sirajul Akhbar' la Jehlum.

Kesi hiyo ilikuwa wazi sana, lakini kwa vile hakimu alikuwa Mwaria mpinzani, kwa hiyo alichelewesha sana kesi hiyo mpaka miezi minane ikapita. Katika muda huo, kwa kuona upendeleo wake wa upande mmoja, Khwaja Kamaluddin alipeleka, tarehe 14 Januari 1904, ombi kwa kuhamisha kesi hizo katika mahakama nyingine, na tarehe hiyo hiyo alipeleka ombi katika mahakama ya Lala Chandu La'l kwamba iahirishwe kusikilizwa kwa kesi hizo. Lala Chandu La'l, siku hiyo hiyo alitangaza uamuzi wa kesi ya udanganyifu, na kwa kesi zingine alipanga tarehe ya 16 Februari 1904. Uamuzi aliotoa ni kwamba barua ambazo Maulawii Karmuddin aliandikia kwa Bwana

Mirza na Waahmadiyya wa Qadian, aliziandika yeye mwenyewe. Na makala zilizochapwa katika 'Sirajul Akhbar' pia ni zake, na haya aliyoandika baadaye kwamba makala za Sirajul Akhbar si zangu, ni uongo. Hata hivyo yeye hakumdaganya Hakim Maulawii Fadhl Din. Kwa hiyo kesi ya kudanganya inafutwa.

Kesi hiyo, iliyofutwa kidhahiri, mahakama pasipo shaka ilitoa uamuzi kwamba barua za Mian Shihabuddin na Maulawii Karmuddin ni za kweli na barua ya Pir Golarawii pia ni ya kweli. Na kwa uamuzi huo, masingizio yalibatilika ambayo kwayo yeye alimsingizia Hudhur[as] na Bwana Pir hakuweza kuiepa athari ya لَا تَكْتُمُوا الشَّهَادَةَ.

Kesi ya pili: Kesi ya pili ilikuwa kutoka kwa Hadhrat Hakim Maulawii Fadhl Din kwamba Maulawii Karmuddin, kabla ya uchapaji wa kitabu "Nuzulul Masihi", kinyume cha ridhaa ya mwandishi wake na mmiliki wa kiwanda cha uchapaji, alichukua kurasa zake, jambo ambalo ni wizi waziwazi. Lakini Lala Chandu Lal, Hakimu, kwa vile alikuwa mpinzani wa Hudhur[as] na Jumuiya yake, kwa hiyo baada ya miezi kumi, tarehe 16 Machi 1904, alifuta kesi hiyo pia.

Kesi ya tatu na ya nne: Sasa zilibaki kesi mbili tu. Kesi ya tatu, ndani yake Hadhrat Sheikh Yakub Ali Turab alimshtaki Maulawii Karmuddin na mhariri wa Sirajul Akhbar kwa kuvunja heshima, na kesi ya nne, ndani yake Karmuddin alimshtaki Hudhur[as] kwa kuvunja heshima. Kwa vile kesi ya nne ilikuwa muhimu sana na Hakimu aliitia maanani sana, kwa hiyo twaieleza kwa urefu. Kesi ya tatu itatajwa mumu humu.

Ibainike kwamba Maulawii Karmuddin alisisitaza kwamba maneno haya matatu yaliyotumika katika Mawahibur Rahman, ***Buhtan, Kadhdhab*** na ***Laimu*** siwezi kuyavumilia kabisa na kwayo nimedhalilika sana. Lakini ikifikiriwa, maneno hayo yanaafikiana barabara na hali yake. Kwani Lala Chandu La'l mwenyewe alitoa uamuzi kwamba barua ambazo Karmuddin aliandika kwa Hudhur[as] na masahaba zake zilikuwa zake tu, na katika "Sirajul Akhbar" makala zilizoandikwa, hizo nazo pia zilikuwa zake, lakini mahakamani alisema uongo kabisa kwamba barua na makala hizo si zangu. Basi, katika hali hiyo kuna shaka gani katika kuwa kwake

mwongo, na yule anayesema uongo na kusingizia kiasi hiki ana kasoro gani ya kuwa duni pia. Lakini chuki ni kitu kibovu. Lala Chandu La'l akarefusha kesi hiyo sana, na akarefusha hata kwamba Disii aliyekuwa Mwingereza pia alistaajabia. Kwa vile mara nyingi wakati wa kwenda mahakamani, yeye alikuwa akiwaona Hudhur[as] na masahaba zake wakikaa katika maeneo ya mahakama, kwa hiyo safari moja akastaajabu sana alisema kwamba kama kesi hiyo ingekuwa kwangu ningetoa uamuzi katika siku moja tu. Katika kesi hiyo, hakimu aliyekuwa Mwaria, alikuwa mpinzani; lakini hata baadhi ya mahakimu Waislamu pia wakampendelea Maulawii Karmuddin. 'Paisa Akhbar' la Lahore pia lilikuwa likiandika makala kwa kumpinga Hudhur[as] na kumwunga mkono Maulawii Karmuddin na akaomba watu watoe mchango kwa ajili yake. Juu ya mambo hayo yote, Hudhur[as] kwa utulivu sana alikuwa anashughulikia kutoa mawaidha na nasaha na kuhudumia dini na kukutana na ndugu kwa utulivu sana kana kwamba hana kesi yoyote. Khwaja Kamaluddin alikuwa wakili wake. Kila mara baada ya kusikilizwa kesi, yeye alipokuwa anakuja Qadian na kumwelezea Hudhur[as] chuki ya hakimu na shari za watu na kusema kwamba hakuna njia ya kusalimika katika kesi hii, hapo Hudhur[as] alikuwa akimtuliza na kusema akitabasamu:

> "Bwana Khwaja, Mwachie Mungu pia sehemu moja. Kama hali zote zikiafiana nasi, hapo watu waweza kusema kwamba hali ziliafikiana naye na wafuasi wake walikuwa wanasheria wakubwa, kwa hiyo wameshinda kesi. Ajabu itakuwa hapo tu iwapo hali zote ziwe kinyume, na Mungu Alete fadhili zake kutoka kwake, ndipo jambo hilo lasababisha kuongeza imani."

Tuseme, Bwana Khwaja alikuwa akija akilia, na kuondoka akitabasamu.

UTABIRI KUHUSU HATIMA YA KESI, 29 JUNI 1903

Waheshimiwa wasomaji tafakarini, Hakimu ana chuki sana, watu wote ni wapinzani, zaidi ya Waislamu, hata Mabaniani pia wanamwunga mkono Maulawii Karmuddin, bali wakili wake aliye mfuasi wake pia anafadhaika sana kwa kuona mambo yaliyo kinyume, lakini yeye anaendelea na shughuli zake kwa utulivu sana,

na ana yakini kamili juu ya Mwumba na Mmiliki wake kiasi hiki kwamba hana hata alama yoyote ya wasiwasi usoni. Na katika hali kama hizo, tarehe 29 Juni 1903 alichapisha tangazo moja kwa kichwa cha habari "Utabiri kuhusu hatima ya kesi", kwamba:

> "Wakati wa usiku uliokuwa baada ya mchana wa 28 Juni 1903… kwa nguvu fikara yangu ilivutika kwenye jambo hili kwamba mashtaka aliyofungua Karmuddin dhidi yangu, au yaliyofunguliwa na wanajumuiya wangu dhidi ya Karmuddin, mwisho wao utakuwaje? Wakati wa kutawaliwa na mvuto huo, hali yangu ikasogea kwenye wahyi wa Mungu na maneno haya ya Mungu yaliniteremkia: اِنَّ اللّٰهَ مَعَ الَّذِيْنَ اتَّقَوْا وَّالَّذِيْنَ هُمْ مُّحْسِنُوْنَ ۔ فِيْهِ اٰيٰتٌ لِّلسَّائِلِيْنَ . Nilifahamishwa maana yake ni hii kuwa kati ya makundi haya mawili Mungu Atakuwa pamoja na wale na kuwapa ushindi na msaada walio wachamungu, yaani ambao hawasemi uongo, hawadhulumu, hawasingizii hawawaudhi waja wa Mungu bila haki kwa udanganyifu na ulaghai na uhaini, nao wanajiepusha na kila uovu na wanashikilia ukweli na uadilifu; na kwa kumcha Mungu wanawatendea waja wake kwa huruma na kuwatakia heri na wema, na ndio wawatakiao watu heri kwa kweli, na hawana unyama, dhuluma na jazba ya uovu, bali wapo tayari kumtendea wema kila mmoja. Basi hatima ni hii kwamba hao ndio watakaoshinda kesi. Ndipo watu ambao wanauliza-uliza kwamba ni nani aliye juu ya haki kati ya makundi hayo mawili, kwa ajili yao si moja bali ishara nyingi zitadhihiri."[431]

Hapo kabla kuhusu kesi hiyo alipata ufunuo huu pia:

يَوْمُ الِاثْنَيْنِ وَفَتْحُ الْحُنَيْنِ[432]

Yaani, katika kesi hii utapata ushindi kama ushindi wa Hunain, yaani kama katika vita ya Hunain walivyosukumwa kwanza masahaba kidhahiri, ndivyo itakavyokuwa katika kesi hii, lakini kisha haraka sana ushindi adhimu utapatikana.

[431] Tadhkirah, uk. 86

[432] Tadhkirah, uk. 476

Kadhalika, ufunuo mwingine aliopata mara kwa mara wakati wa kesi hiyo ulikuwa huu:

سَأُكْرِمُكَ إِكْرَاماً عَجَبًا[433]

Yaani, Nitakupa heshima ya ajabu sana. Vilevile alifunuliwa ufunuo huu:

سَأُكْرِمُكَ إِكْرَاماً حَسَنًا[434]

Yaani nitakuheshimu kwa heshima bora sana. Funuo hizo zote ziliashiria kwa hatima nzuri ya kesi hiyo.

OMBI LA KUHAMISHA KESI LILIKATALIWA

Imeshaelezwa nyuma kwamba tarehe 14 Januari 1904 Khwaja Kamaluddin alimwomba Hakimu wa Wilaya ya Gurdaspur kuhamisha kesi kutoka mahakama ya Lala Chandu La'l, lakini hakimu wa Wilaya alikatalia ombi hilo tarehe 12 Februari 1904. Baadaye, Bwana Khwaja alipeleka ombi lake katika mahakama kuu ambako tarehe 22 Februari 1904 ilipangwa, lakini katika mahakama ya Lala Chandu La'l, tarehe 16 Februari 1904 ilikuwa imekwishapangwa. Siku ile hakimu alikuwa na nia mbaya na alikwishaamua kwamba atamfedehesha Hudhur[as], lakini Mwenyezi Mungu Hakumpatia nafasi. Hadhrat Maulana Seyyid Sarwar Shah alieleza kwamba:

> "Siku hizo, Waariya walifanya mkutano ambamo Lala Chandu La'l pia alishiriki. Katika mkutano huo, Waaria walimwambia Chandu La'l kwamba wajua, Bwana Mirza ni adui wetu mkali, na ni mwuaji wa kiongozi wetu Lekhram, na sasa yu windo mkononi mwako. Ukiacha windo hili, basi utakuwa adui wa kaumu. Hapo, Hakimu akasema, mapema ninayo nia kwamba ikiwezekana, si Mirza tu bali wenzake wote katika kesi hii na mashahidi wake niwafikishe jahanamu. Lakini nifanyaje, kesi inaendeshwa kwa akili sana kiasi hiki kwamba haibaki nafasi ya kuwakamata, hata hivyo nimeshakusudia kwamba kwa vyovyote

[433] Tadhkirah, uk. 472, 474 na 489

[434] Tadhkirah, uk. 489

katika mahudhurio ya kwanza tu nitachukua hatua ya kimahakama.”

Hadhrat Maulana Seyyid Sarwar Shah alisema kwamba:

“Tukio hilo lote, marehemu Dkt. Muhammad Ismaili Khan alinihadithia na akasema kwamba katika mkutano huo Munshi Muhammad Husain, karani wa Hakimu wa Wilaya, alikwepo ambaye akaja kwangu na akanielezea tukio hilo lote. Na alisema hii pia kwamba aliyosema Hakimu kuwa ‘Nitachukua hatua ya kimahakama’, maana yake ni kwamba hakimu akitaka, mwanzoni mwa kesi au kati ya kesi, anaweza kumfunga mshtakiwa bila kukubali dhamana. Muhammad Husain akasema kwamba ingawaje mimi ni mpinzani mkali wa Jumuiya yenu, lakini siwezi kuvumilia kwamba familia iliyoheshimika sana katika Wilaya nzima ipate kufedheheka hivyo mkononi mwa Baniani mmoja. Basi, nimekufikishia habari hii, mpange mpango wowote kuhusu hii.

Hapo Bwana Maulawii aliamua kwamba haraka iwezekanavyo kwa kuchukua gari la farasi yapasa kumjulisha Hudhur[as] kuhusu habari hiyo. Lakini kwa sababu ya upinzani mkali mjini, yeyote mwenye gari la farasi hakukubali. Ndipo yeye akawatuma Sheikh Hamid Ali, mpishi Abdur Rahim na mtu mwingine wa tatu waende Qadian kwa miguu. Hao wakafika Qadian wakati wa sala ya alfajiri na kumweleza Hudhur[as] habari zote. Hudhur[as] alisema, haya, twende Batala, huko Bwana Khwaja na Maulawii Muhammad Ali wakija toka Lahore watakutana nasi. Tutawaelezea, na pale itajulikana kwamba ni nini matokeo ya juhudi yao kuhusu kuhamisha kesi. Basi, siku hiyo Hudhur[as] alifika Batala. Garini, Maulawii Muhammad Ali na Bwana Khwaja pia walikuwepo, walitoa habari kwamba haikufanikiwa juhudi ya kuhamisha kesi. Kisha Hudhur[as] alikwenda Gurdaspur na njiani hakuwaarifu Bwana Khwaja na Bwana Maulawii juu ya habari hiyo. Alipofika nyumbani Gurdaspur, kama kawaida yake alienda kulala kitandani katika chumba peke yake. Lakini wakati huo sisi tulikuwa na hofu sana kwamba sasa itakuwaje!

Hadhrat Maulawii anasema kwamba

> "Baada muda mfupi, Hudhur[as] aliniita, nikaenda. Wakati huo Hudhur[as] akiunganisha mikono yake miwili alikuwa ameweka chini ya kichwa chake na kulala chali. Nilipofika akalala ubavuni akiweka kichwa chake juu ya mkono wake ulioegemea kikoni mwake na akasema kwamba nimekuita ili nisikilize tukio lile lote kwamba ni nini. Wakati huo hakuwepo mtu yeyote mle chumbani, mlangoni tu alikuwa amesimama Mian Shadi Khan. Nilimwelezea tukio zima… Hudhur[as] aliendelea kusikiliza akiwa kimya. Nilipofika kwenye neno la "windo", mara akakaa na macho yake yakang'ara na uso ukawa mwekundu na akasema: "Mimi ni windo lake? Mimi si windo, mimi ni simba, tena simba wa Mungu. Anawezaje kumkamata simba wa Mungu. Basi na aone akijaribu kufanya hivyo."

Hadhrat Maulawii alisema kwamba akitamka Hudhur[as] maneno hayo, sauti yake ilipaa sana hata watu wote waliokuwa nje ya chumba nao pia wakashtuka na wakaelekea huko kwa kushangaa, lakini yeyote hakuingia chumbani. Hudhur[as] alirudia neno 'simba wa Mungu' mara kadha, na wakati huo macho yake, yaliyokuwa yanainama sikuzote na huwa yamefumbika nusu, yakafumbuka kweli kweli kama macho ya simba na yakaanza kung'ara kama mwako. Na uso ukawa mwekundu kiasi hiki kwamba ilikuwa shida kuuangalia. Kisha akasema:

> "Nifanyeje? Nimejitolea mbele ya Mungu kwamba nipo tayari kuvaa chuma mkononi na miguuni mwangu kwa ajili ya dini yako, lakini Yuasema, hapana, Nitakulinda na kila dhila na Nitakuachilia kwa heshima."

Kisha akaanza kutoa hotuba kuhusu mapenzi ya Mungu, na karibu nusu saa aliendelea kuzungumza kwa jazba. Kisha mara akakokomoa na papo hapo akatapika damu halisi ambamo ilikuwa damu kidogo iliyoganda na nyingine ya kutiririka. Baada ya kutapika Hudhur[as] akainua kichwa na akapangusa midomo na pia macho yaliyopata maji kwa kutapika. Lakini hakujua katika matapishi imetoka nini, kwani akatapika mara moja kisha akainua kichwa. Lakini nilipoinama kuyatazama, akaniuliza ni nini? Nikajibu, kuna damu katika matapishi. Hapo akayatazama. Kisha Bwana Khwaja, Maulawii

Muhammad Ali na watu wengine wakaja chumbani, na daktari aliitwa. Dakrati alikuwa Mzungu. Yeye akaja na akiona matapishi, na akaendelea kuongea na Bwana Khwaja kwa Kiingereza. Maongezi yalimaanisha kwamba katika uzee matapishi ya damu ni hatari. Kisha akasema, kwa nini hapumziki? Bwana Khwaja akasema apumzikeje, Hakimu anasumbua kwa kupanga tarehe za kuhudhuria karibu karibu, ilihali kesi ni ya kawaida inayoweza kuamuliwa mara moja. Yeye alisema kwamba wakati huu kupumzika ni lazima, naandika hati. Niandike kwa muda gani? Kisha mwenyewe akasema, nionavyo mimi yapasa kupumzika kwa miezi miwili. Bwana Khwaja akasema, kwa muda huu, mwezi mmoja utatosha. Yeye mara moja kaandika hati kwa mwezi mmoja, na kaandika kwamba katika muda huu wote namwona hawezi kuhudhuria mahakamani. Baada yake, Hudhur[as] aliamuru kurudi, lakini tuliogopa isije ikaanza sasa kesi nyingine mpya, kwani keshoye yalikuwa mahudhurio, na Hudhur[as] baada ya kuja Gurdaspur alipanga kurudi bila idhini ya mahakama. Lakini Hudhur[as] alikuwa na utulivu kabisa usoni mwake. Basi tulirejea Qadian."[435]

Keshoye, tarehe 16 Februari, Hudhur[as] alitakiwa kuhudhuria mahakamani. Hati ya maradhi ya daktari iliwekwa mbele ya Hakim, ambayo akiiona tu alikasirika sana, lakini alikuwa hana la kufanya chochote. Ombi lililokuwa limepelekwa la kuhamisha kesi katika mahakama kuu, hilo nalo lilikataliwa tarehe 22 Februari 1904, na tarehe 23 Februari kesi ilitajwa tena katika mahakama ya Lala Chandu La'l. Siku hiyo, kwa niaba ya Hudhur[as], walihudhuria Bwana O'Gorman mwanasheria, Khwaja Kamaluddin na Maulawii Muhammad Ali kama wakili.

KASHTAKIWA RASMI

Ingawaje Khwaja Kamaluddin alieleza tarehe 9 Machi 1904 jambo hili kwa masaa manne kwamba kesi hiyo haiwezi kufunguliwa dhidi yetu, lakini kwa vile Hakimu alikwishaamua kabisa kushtaki rasmi, kwa hiyo tarhe 10 Machi akawashtaki rasmi Hudhur[as] na Hakim

[435] Siratul Mahdi, sehemu ya kwanza, kimuhtasari.

Maulawii Fadhluddin. Muda wa hati ya daktari ilikuwa iishe 13 Machi, Hudhur[as] bado alikuwa hajapata afia barabara. Kwa hiyo, tena daktari aliitwa aje Qadian kutoka Gurdaspur. Baada ya kuchunguza, alisema kwamba bado yahitajika kupumzika zaidi. Basi akatoa hati nyingine kwa mwezi mmoja. Tarehe 14 Machi 1904, lilipopelekwa hati hiyo, Hakimu Chandu Lala alikasirika sana, na siku ijayo tarehe 15 akamwita daktari mahakamani kutoa maelezo kwa kuapa, ilihali katika mahakama hiyo hiyo hati ya daktari iliendelea kuletwa na Pir Mehr Ali Shah Golarawii kila tarehe ya mahudhurio, lakini hakimu huyo huyo hakumwita daktari hata safari mmoja kwa kutoa maelezo kwa kuapa. Sawa na amri ya mahakama, Bwana daktari akaja kwa kutoa ushahdi kwa kuapa. Hapo tarhe 11 Aprili ilipangwa.

LALA CHANDU LA'L KASHUSHWA CHEO

Jinsi Lala Chandu La'l alivyomtendea Hudhur[as] ilitaharakisha ghera ya Mwenyezi Mungu dhidi yake. Sasa ikawa hivi kwamba katika jela ya Gurdaspur mhalifu mmoja alitakiwa kunyongwa. Sawa na sheria Disii anampanga Hakimu mmojawapo ambaye mbele yake mhalifu ananyongwa. Siku hiyo, Disii akamwamuru Lala Chandu La'l kuhudhuria wakati wa kunyongwa mhalifu. Lakini Bwana Lala kwa kuwa alikuwa mpole wa moyo akaomba radhi na akasema kwamba siwezi kumwona mhalifu yeyote kunyongwa, kwa hiyo Hakimu mwingine apewe jukumu hili. Disii alimwandikia kwamba u Hakimu wa kesi za jinai, kesho ukipandishwa cheo na kuwa Jaji wa mahakama ya jinai, utafanyaje? Je hutatoa hukumu ya kuwanyoga wahalifu? Kwa hiyo wewe walazimika kutekeleza wajibu huu. Bwana Chandu La'l akaung'an'ania usemi wake, basi Hakimu wa Wilaya alipeleka taarifa serikalini kwamba hafai Hakimu mwenye moyo dhaifu kiasi hiki kwa kuamua kesi za jinai. Matokeo yake yakawa kwamba tarhe 11 Aprili kabla ya tarehe ya mahudhurio, Bwana Chandu La'l alishushwa cheo na kufanywa hakimu wa kawaida na akahamishwa na kupelekwa Multan. Na hivyo ufunuo wa Hudhur[as] [436] اِنِّیْ مُھِیْنٌ مَّنْ اَرَادَ اِھَانَتَکَ ukatimia waziwazi mara nyingine.

[436] Nitamdhalilisha atakayenuia kukufedhehesha.

HAKIMU MPYA LALA ATMARAM ALIVYOMTENDEA HUDHUR[AS]

Mahali pa Lala Chandu La'l, akaja hakimu mpya Bwana Lala Atmaram. Yeye pia alikuwa Mwaria mwenye chuki. Yeye akashika njia iliyokuwa kali zaidi hata kuliko Lala Chandu La'l. Kabla yake, kila mara Hudhur[as] alikuwa akipewa kiti mahakamani, lakini yeye si tu alikataa kumpa kiti bali wakati mwingine hakuruhusu hata kunywa maji katika hali ya kusikia kiu sana. Na akaanza kupanga tarehe za kuhuduria zilizo karibu karibu, ili Hudhur[as] asiweze kwenda Qadian kwa kupumzika. Kwa hiyo, kuanzia 13 Agosti 1904, Hudhur[as] alipanga nyumba moja na kuishi Gurdaspur pamoja na familia.

USHAHIDI WA MAULAWII THANAULLAH

Katika kesi hiyo maneno *Kadhdhab* na *Laim* yalikuwa yanajadiliwa zaidi. Masheikh wakubwa wakubwa walikuwa wakihudhuria pamoja na kamusi na vitabu vya Kiarabu. Ingawa hakika ya elimu na uaminifu wa masheikh wote ilifichulika, lakini Maulawii Thanaullah alipata kudhalilika zaidi kuliko wote. Ikawa hivi kwamba katika ushahidi wake, Maulawii Thanaullah, kwa kuthibitisha uchamungu wa Sheikh Karmuddin, alisema kwamba si lazima kwa mchamungu kwamba asiongope. Akasema hayo kwa sababu Lala Chandu La'l alikwishatoa uamuzi wake kwamba Sheikh Karmuddin ndiye mwongo. Maulawii Thanaullah kwa kuipa nguvu usemi wake, alitoa aya za mwanzo za Sura Al Bakarah ambamo alama za imani zimetajwa, lakini hakuna humo maelezo ya matendo. Kwa kuhoji dalili ya Maulawii Thanaullah, Khwaja Kamaluddin alipouliza, 'Maulana, hapo kuiba, kuzini na kunywa pombe pia havikuelezwa, basi je, kwa mchamungu matendo hayo pia yanajuzu?' Bwana Maulawii kwa vile kwa vyovyote alinuia kuthibitisha uchamungu wa Maulawii, kwa hiyo akajibu, 'Naam!' Hapo wote wakaangua kicheko mahakamani na Bwana Maulawii alipata aibu.

JUHUDI YA SULUHU

Kesi ziliendelea kwa muda mrefu, kwa hiyo kwa kudokezwa na mahakama, baadhi ya Waislamu wenye moyo wa huruma walitaka kuingilia kati na kupatanisha, lakini juhudi yao ikashindikana. Hapo,

kesi zikaanza kuendelea tena. Shtaka rasmi aliloandika Hakimu Lala Chandu La'l alilibakisha Lala Atmaram vile vile. Miongoni mwa mashahidi wa kutetea alikuwa Pir Mehr Ali Shah pia. Kwani ilikuwa lazima kusadikisha barua zilizoandikwa kwa mkono wake. Lakini mahakama haikuona haja ya kumwita, ilihali alikuwa shahidi muhimu zaidi kuliko wote, lakini kama nia yenyewe ya Hakimu iwe mbaya, yaweza kufanywa nini!

UAMUZI WA KESI, 18 OKTOBA 1904

Baada ya kwisha ushahidi wa kutetea, Lala Atmaram aliweka tarehe mosi Oktoba 1904 kwa kutoa uamuzi wa kesi. Hapo kabla, yeye alipoanza kumsumbua Hudhur[as], mwanaye alishikwa na maradhi. Na mke wake aliambiwa ndotoni kumhusu Hudhur[as] kwamba kama mumeo akimwadhibu huyo mkweli, basi mtapata adhabu. Yeye akamwambia Bwana Lala ndoto hiyo, lakini ni masikitiko kwamba moyo wa Bwana Lala ulikuwa mgumu zaidi kuliko Pilato aliyeletewa kesi ya Hadhrat Masihi Mnazareti[as]. Yeye kwa kuathirika na ndoto ya mkewe akaagiza maji mahakamani, akaosha mikono yake, na akasema kwamba sioni kosa lolote katika mtu huyo. Lakini Wayahudi wakipiga makelele walisema, asulubiwe. Ndipo akasema, "adhabu ya kumwaga damu hii itakuwa juu ya nani? Wayahudi wakajibu, 'juu yetu na juu ya kizazi chetu.' Lakini ni masikitiko kwamba Hakimu huyo (Lala Atmaram) akawa mwenye moyo mgumu kuliko Pilato, na adhabu yote alibeba mwenyewe. Matokeo yake yakawa kwamba baada ya uamuzi wake kijana wake aliyekuwa mgonjwa akafa. Kisha baada ya siku 20-25 mwanaye wa pili pia alikufa na sawa na kashfi moja ya Hudhur[as], yeye alishikwa na huzuni ya kizazi."[437]

Imeshatajwa juu kwamba kwa kutoa uamuzi, Lala Atmaram alipanga tarehe mosi Oktoba 1904. Siku hiyo halaiki kubwa ya wasiokuwa Waahmadiyya walikuwepo mahakamani, na Waahmadiyya pia karibu 250-300 walifika kutoka sehemu za Karachi, Haidarabad Sindh, Peshawar, Wazirabad, Kapurthala, Qadian, Lahore, Amritsar, Narowal, Dina Nagar na kadhalika. Pengine kwa kuona halaiki

[437] Hakikatul Wahyi, uk. 121

kubwa ya watu au kwa sababu nyingine, Hakimu hakutangaza uamuzi siku ile, bali akaweka tarehe 8 Oktoba 1904 kwa kutoa uamuzi. Kwa vile alikuwa na nia mbaya kuhusu Hudhur[as], kwa hiyo alichagua njia hii kwamba uamuzi wa kesi ya Hudhur[as] utangazwe wakati ambapo saa za mahakama ziwe zinakwisha na isiweze faini kutolewa mara moja. Pili, kwa ujanja alipanga siku ya Jumamosi kwa kutoa uamuzi. Hadhrat Mian Abdul Aziz Mughal alikuwa akisema kwamba Hakimu alikuwa na nia hii ya kwamba nitapitisha saa za mahakama katika kuendelea kutoa uamuzi. Kisha wakati wa kutoa faini nitasema kwamba saa za mahakama zimekwisha, kwa hiyo faini itapokelewa keshokutwa, siku ya Jumatatu, na hivyo Bwana Mirza atalazimika kukaa gerezani angalau kwa siku mbili.

Mimi, mwandishi wa maneno haya, nilipomtaka Hadhrat Mirza Bashir Ahmad asadikishe habari hii, akasadikisha.[438]

Kesi aliyofungua Hadhrat Sheikh Yakub Ali Turab dhidi ya Maulawii Karmuddin na Mhariri wa Sirajul Akhbar, uamuzi wake Hakimu alitoa kwanza ambao ulikuwa kwamba washtakiwa waliambiwa ya kuwa kosa lenu limethibitika na udhuru wenu ni batili. Kwa kusema hayo Maulawii Karmuddin alifainiwa Rupia 50 na asipoweza kutoa, afungwe jela miezi miwili. Na Fakir Muhammad, Mhariri wa Sirajul Akhbar, alifainiwa Rupia 40 na asipoweza kutotoa faini atiwe katika jela kwa mwezi mmoja na nusu.

Baada yake, aliwaita ndani Hudhur[as] na Hadhrat Hakim Maulawii Fadhluddin. Polisi walisisitizwa kwamba minghairi ya washtakiwa, mwingine yeyote asiingie ndani. Kama ilivyoelezwa juu, walidhani kwamba kwa kulipa faini kwa vyovyote muda kidogo utahitajika, nami nitaendelea kutoa uamuzi mpaka saa za mahakama ziishe, na baada yake muda usibaki kwa kulipa faini. Na kwa uchache, mpaka siku ya tatu lazima kwa siku mbili watakaa jela. Basi, akaanza kusoma uamuzi saa kumi kasa robo. Wakili wake Khwaja Kamaluddin alikuwa ameenda kujisaidia. Alirudi saa ile ile walipokuwa wanaingia

[438] Baadaye nilipoona kalenda kwa kuhakikisha siku basi ilijulikana kwamba kweli tarehe 8 Oktoba 1904 ilikuwa siku ya Jumamosi.

Hudhur[as] na Hadhrat Hakim katika chumba cha mahakama. Alikimbilia chumba cha mahakama. Alipofika mlangoni maaskari wawili walijaribu kumzuia asiingie ndani. Bwana Khwaja akawasukuma maaskari wote wawili na akaingia ndani akisema kwamba itakuwaje nisiende ndani, mie ndiye wakili wa washtakiwa. Alipoingia chumbani Hakimu alikuwa akitangaza uamuzi, na sawa na ujanja wake alikwishaandika uamuzi mrefu sana. Kwani, alidhani kwamba uamuzi utakapomalizika kusomwa, muda wa mahakama utakuwa umekwisha. Kisha hata kama faini ikilipwa, sitakubali, na nitasema kwamba lipeni keshokutwa. Ni kudra ya Mungu kuwa Hakimu alipotamka tu, "Mirza Ghulam Ahmad anafainiwa Rupia 500 na Hakim Fadhluddin Rupia 200, na wasipolipa basi kifungo cha miezi sita kila mmoja, papo hapo Khwaja Kamaluddin aliweka noti za Rupia elfu moja juu ya meza ya Hakimu,[439] na kasema, 'Bwana, hizi ni noti za Rupia 1000, chukua Rupia 700 ya faini katika hizi, isije ukasema baadaye kwamba sasa muda umekwisha. Kwa kusikia hayo Hakimu akafadhaika kwani aliona kwamba hila yake yote ikatilifika, alikuwa hawezi kufanya chochote. Kwa vyovyote akazitazama noti. Alipoona kwamba juu ya noti haikuandikwa Lahore au Calcutta, bali imeandikwa Karachi na Madras, akachangamka kidogo na alitumia ujanja mwingine huu kwamba katika zama zile kikawaida katika Panjab noti zile zilikubaliwa ambazo ziliandikiwa Lahore au Calcutta; noti za Karachi na Madras hazikupokelewa; lakini katika hazina za serikali noti za aina zote zilikuwa zikitolewa. Hakimu alidhani labda Bwana Khwaja hajui jambo hilo, kwa hiyo akasema kwamba Bwana Khwaja, juu ya noti zako haijaandikwa Lahore au Calcutta, kwa hiyo hatukubali hizo. Bwana Khwaja mara moja akasema, "Uniandikie

[439] Kwa vile ilitarajiwa kwamba Hudhur[as] na Hadhrat Hakim watatozwa faini kubwa, kwa hiyo Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan alimtumia Rupia 900 Hudhur[as] siku moja kabla ya uamuzi. Zikiongezewa Rupia 100, Bwana Khwaja alikabidhiwa Rupia 1000, kwani ilidhaniwa kwamba faini itakuwa rupia 500 kila mmoja. Hadhrat Sheikh Yakub Ali Turab anaeleza kwamba Rupia 100 nyingine pia ziliwekwa kama akiba, kwani Hakimu alikuwa adui mkali, kwa hiyo ilihofiwa kwamba anaweza kutoza Rupia 1000 kila mmoja. Someni As-habe Ahmad, J. 2, uk. 462-463

kuwa noti za Rupia 700 zilitolewa, lakini kwa kuwa zilikuwa za Madras na Karachi, kwa hiyo mahakama haikuzikubali." Sasa angewezaje kukataa. Basi, akakubali shingo upande noti zile, na kwa majuto sana akawaruhusu Hudhur[as] na Hadhrat Hakim kuondoka mahakamani.

Baada yake, kwa kupata nakala za uamuzi na kukusanya vifaa na kadhalika Hudhur alikaa Gurdaspur kwa siku mbili. Kisha siku ya tatu tarehe 11 Oktoba alirudi Qadian.

KUREKEBISHA KOSA MOJA LA KIHISTORIA

Katika kesi hiyo inayotajwa, safari moja katika Gurdaspur wakili wa kundi la pili alimwuliza Hudhur[as] kwamba je, shani na daraja yako ni ile ile jinsi ilivyoandikwa katika Tuhfa Golarawiyya?[440] Hudhur[as] alilijibu, 'Naam'. Hudhur[as] amelitaja tukio hilo katika Hakikatul Wahyi,[441] lakini kwa kusahau ikaandikwa 'Tiryakul Kulub' badala ya 'Tuhfa Golarawiyya'. 'Tiryakul Kulub' ni kitabu cha kabla ya mwaka 1901, na Hudhur[as] alijiita humo nabii wa namna fulani, kwa hiyo Waahmadiyya wa kundi la Lahore wanataja mara kwa mara rejeo hilo, ilihali Hudhur[as] aliulizwa swali kuhusu 'Tuhufa Golarawiyya' si juu ya Tiryakul Kulub.[442]

KUKATA RUFAA DHIDI YA UAMUZI HUO

Kwa vile Hudhur[as] alikwishaambiwa na Mwenyezi Mungu kwamba ataachiliwa na mahakama kuu, kwa hiyo alimwambia Bwana Khwaja, "Bwana Khwaja, kata rufaa haraka sana. Bwana Khwaja, akatekeleza amri, na dhidi ya uamuzi wa Lala Atmaram akakataa rufaa mahakamani mwa Bwana Hery, Jaji wa kesi za jinai, Amritsar. Tarehe 26 Novemba 1904 ilipangwa kwa mahudhurio ya kwanza. Akichunguza sababu za rufaa, Jaji alipanga tarehe 6 Januari 1905, na akatoa notisi kwa kundi la pili. Ni kudra ya Mungu, katika mahudhurio ya kwanza tu aliwaachilia Hudhur[as] na Hadhrat Hakim, na akaamuru kurudisha fedha ya faini. Kwa kuona faili ya kesi,

[440] Tuhfa Golarawiyya, chapa ya kwanza, uk. 48-50, Ruhani Khazain, J. 17, uk. 167

[441] Hakikatul Wahyi, chapa ya kwanza, uk. 266. Ruhani Khazain, J 22, uk. 278

[442] Kwa maelezo zaidi someni *Siratul Mahdi,* sehemu ya pili, uk. 67

alisema hii pia kwamba ni masikitiko ya kuwa kesi hii mbovu ilirefushwa sana hivyo. Kama kesi hii ingekuwa kwangu, ningeiamua katika siku moja tu. Na tarehe 7 Januari 1905 aliandika katika uamuzi wake kiasi hiki kwamba kama yangeandikwa maneno makali zaidi kuliko hayo dhidi ya Karmuddin, angestahiki hayo.

Akitaja kesi hiyo Hudhur[as] aliandika:

> "Kisha ikawa hivi kwamba katika siku takriban 20-25 wanawe wawili (wa Hakimu Lala Atmaram) walikufa. Na hatimaye ikatokea hivi kwamba Atmaram hakuweza kunipa adhabu ya kifungo ingawa katika kuandika uamuzi aliweka msingi wa kufunga pia, lakini hatimaye Mungu Alimzuia kutenda hivyo. Akatoza faini ya Rupia 700. Kisha katika mahakama ya ***divisional Jaji*** niliachiliwa kwa heshima. Na adhabu ya Karmuddin ilibaki, na faini yangu ilirudishwa, lakini wavulana wawili wa Atmaram hawakurudi."[443]

Kwa ajili ya urahisi wa wasomaji watukufu tumetaja pamoja kesi zinazomhusu Maulawii Karmuddin. Sasa twaanza tena kueleza matukio ya mwanzoni mwa 1903.

KUZALIWA KWA AMATUN NASIIR, 28 JANUARI 1903

Usiku wa katikati ya 27-28 Januari, saa sita za usiku, Hudhur[as] alifunuliwa: "غَاسِقُ اللهِ" yaani, Mwenyezi Mungu Atateremsha giza. Akaamka saa hiyo hiyo na akaanza kuomba dua. Mwenyezi Mungu kwa fadhili Yake Alimhifadhi Hadhrat Amman Jan ─ mkewe Hudhur[as] ─ lakini binti aliyezaliwa alifariki baada miezi michache, tarehe 3 Desemba 1903, sawa na ufunuo غَاسِقُ اللهِ. ***Innaa lillahi wa innaa ilaihi rajiun.***

UJENZI WA BAITUD-DU'AA

Tangu muda mrefu, Hudhur[as] alitaka kwamba pamoja na Baitul Fikr kijengwe chumba kidogo kama Baitud Du'aa ambamo shughuli yoyote isifanywe isipokuwa dua. Hivyo, katika Machi 1903 chumba

[443] Hakikatul Wahyi, uk. 122

kile kilijengwa.[444]

HADHRAT SAHIBZADA ABDUL LATIF SHAHID[RA]

Sahibzada Seyyid Abdul Latif[ra] alikuwa mkazi wa maeneo ya Khost, Afghanistan, mtawa mwenye kupokea ufunuo, kashfi na alikuwa mwenye karama. Utawa wake uliaminiwa nchini kote. Alikuwa na maelfu ya wafuasi katika Afghanistan. Uchamungu, utakaso, elimu na fadhila zake zilikuwa za hali hii kwamba wakati wa kutawazwa kwa Habibullah, Amiri wa Kabul, yeye mtawa huyo kwa mikono yake alimvika kilemba cha ufalme. Alikuwa na uchungu sana kwa Uislamu na alikuwa akiomba sana kwamba kwa kuhifadhi Uislamu, Mwenyezi Mungu Amtume haraka Mujadidi mwenye shani kubwa. Katika hali hiyo, alipata baadhi ya vitabu vya Hudhur[as]. Basi kwa kuviona tu mara moja alikuwa akajitolea kwake kwa moyo wote. Alipata shauku sana ya kukutana naye, lakini haikuonekana njia yoyote. Hatimaye, Mungu Alimtilia moyoni mwelekeo kwenda kuhiji. Hapo, akafikiri kwamba njiani atapitia Qadian pia. Yeye alimweleza Amiri wa kabul pia kuhusu nia yake ya kuhiji. Yeye si tu alimruhusu, bali alimzawadia pia fedha kiasi fulani kwa matumizi katika safari. Kutoka nchini mwake nafikiri alifika Qadian mnamo Oktoba 1902, na kwa kumwona Hudhur[as], alizama katika mapenzi yake kiasi hiki kwamba wakati wa hija ulipita. Alikaa Qadian kwa miezi kadha. Imeshatajwa nyuma kwamba kwa kesi ya Maulawii Karmuddin katika safari ya Jhelum Hadhrat Sahibzada Seyyid Abdul Latif pia alikuwa pamoja na Hudhur[as].

BWANA SAHIBZADA AREJEA NCHINI MWAKE NA NJIANI KAKAA KATIKA LAHORE

Sahibu yake mmoja, Mian Ahmad Nur, anasimulia kwamba Sahibzada Sahib alipokuwa Qadian alipata ufunuo huu mara kwa mara:

> "Toa uhai wako katika njia hii, na usijali, kwani Mungu Ametaka hivyo kwa heri ya Kabul."

Safari moja alisema:

[444] Al Hakam, 31 Machi 1903

> "Nafunuliwa kwamba mbingu inapiga kelele, na ardhi inatetemeka kama mtu ambaye amepatwa na malaria kali. Dunia haijui; jambo hili litatokea."

Alipoondoka kutoka Qadian kwa idhini ya Hudhur[as], Hudhur[as] alienda naye mbali sana ili kumsindikiza. Wakati wa kuagana na Hadhrat, Hadhrat Sahibzada alijawa na jazba kubwa na kwa mapenzi makubwa alianguka miguuni pa Hudhur[as]. Wazee watazamaji wanasimulia kwamba kwa kuona hali yake hiyo machozi yakamlengalenga Hudhur[as] pia, na kwa shida akajituliza. Hata hivyo alikuwa hapendi kwamba mtu yeyote amwangukie miguuni mwake au aguse magoti yake kwa heshima. Akamwambia Bwana Sahibzada kuinuka, lakini yeye akabaki pale pale. Hapo Hudhur[as] akasema: اَلْاَمْرُ فَوْقَ الْاَدَبِ . Kwa kusikiliza kauli hii haraka akasimama na kasema, "Hudhur, sababu ya mahangaiko yangu na kutotulia kwangu ni kwamba moyo wangu unayo yakini kuwa katika uhai wangu huu sitaweza kukuona tena. Hii ndiyo mara yangu ya mwisho kukuona." Akisema hayo, akaagana naye kwa moyo mzito na macho yatiririshayo machozi. Alikuwa na mpango wa kununua vitabu kadha kutoka Lahore. Hadhrat Mian Abdul Aziz Mughal[ra] ambaye kwa sababu ya kuwa na hazina kubwa ya masimulizi, huwa namwita Abu Huraira[ra] wa Uahmadiyya, nafikiri kuwa, mnamo mwaka 1939 nilipokuwa nikitembelea miji na vijiji mbalimbali kwa kuagizwa na Nadharat Talif-o-Isha'at kwa ajili ya kukusanya masimulizi ya msahaba, yeye alinihadithia mara kadha kwamba Hadhrat Sahibzada alikuwa akiviringisha shuka juu ya kilemba chake na alikuwa akivaa juba kubwa. Alipokuwa amekaa Lahore, bwana fulani aliwaalika ndugu kadha kwenye karamu ya chakula. Humo Hadhrat Sahibzada pia alifika. Bwana Mughal alikuwa akisema kwamba katika karamu ile mimi pia nilienda pamoja na Hadhrat Sahibzada. Alipofika kwenye chumba cha karamu, vyakula vya aina aina vilipangwa mezani kwa njia nzuri sana. Hadhrat Sahibzada alipoketi tu alipata hali ya kuona kashfi, akaniambia kwa lugha ya Kiajemi, 'Nyinyi mmenileta hapa kwa kunilisha kinyesi. Akisema hayo akainuka, akaondoka akitembea

haraka haraka hata kwamba juba lake lilikuwa linapepea katika upepo. Njiani alinipa Anna nne na kasema nunua ***Naan*** (aina ya chapati) na kababu, nikafuata amri. ***Naan*** na kababu zile zilizokuwa nyingi, tukala tukikaa katika msikiti wa Gumtiwali uliokuwa siku hizo chini ya usimamizi wa Jumuiya Ahmadiyya. Mwenyeji alipomwona Hadhrat Sahibzada akaondoka hivyo, aliathirika sana na mtazamo wake wa kashfi, kwani alijua kwamba karamu hiyo ilikuwa kutokana na fedha ya riba.

Akiondoka Lahore, akaenda kwao Khost. Njiani aliwaambia wanafunzi wake mara kwa mara kwamba ardhi ya Kabul inahitaji damu yangu kwa kujirekebisha. Kwa vile hali za baadaye Hudhur[as] mwenyewe ameandika katika kitabu chake Tadhkiratush Shahadatain, kwa hiyo zile zinaelezwa kimuhtasari kwa maneno ya Hudhur[as] mwenyewe.

KIFO CHA KISHAHIDI CHA HADHRAT SAHIBZADA ABDUL LATIF, 14 JULAI 1903

> Bwana Maulawii alipofika karibu na maeneo ya utawala wa Kabul, akakaa katika maeneo ya serikali ya Kiingereza na kumwandikia barua Brigedia Muhammad Husain, mkuu wa polisi, aliyekuwa mwanafunzi wake, kwamba niombee Amiri ruhusa kufika kwangu, kisha niarifu ili nimwendee Bwana Amiri huko Kabul. Hakuenda bila kuomba ruhusa kwa sababu wakati wa kwenda safarini alimwambia Amiri kwamba anakwenda kuhiji, lakini hakuweza kutimiza nia ile kwa sababu ya kukaa muda mrefu katika Qadian na wakati wa kuhiji ukapita... Basi, akaona afadhali amwandikie Brigedia Muhammad Husain ili kwa wakati mwafaka amweleze Amiri hakika yenyewe kwa maneno yafaayo. Na akamwandikia katika barua hiyo kwamba ingawa nilitoka kwa nia ya kuhiji, lakini nilipata kuonana na Masihi Mau'udi. Na kwa vile kwa kuonana na Masihi na kutanguliza utii wake kuna amri ya Allah na Mtume[saw], kwa hiyo nililazimika kukaa Qadian. Na sikufanya hivi kwa hiari yangu, bali sawa na Kurani na Hadithi nikaona jambo hilo kuwa la lazima. Barua hiyo ilipomfikia Brigedia Muhammad Husain,

yeye aliiweka chini ya goti lake na hakupeleka wakati huo. Lakini makamu wake, aliyekuwa mpinzani na mwenye shari, akajua kwa njia fulani kwamba hiyo ni barua ya Sahibzada Abdul Latif, naye alikaa katika Qadian. Basi, akachukua barua ile kwa njia fulani na akaiweka mbele ya Amiri... Kwa vile kifo cha kishahidi cha Bwana Sahibzada kilikuwa kimepangwa kwa kadri ya Mungu na huko mbinguni alikwishaingia katika kundi la mashahidi walioteuliwa, kwa hiyo, Bwana Amiri alitumia ujanja kwa kumwita, na akamwandikia njoo tu bila wasiwasi wowote, kama madai hayo yatakuwa kweli, hata mimi pia nitakuwa mfuasi… Wasimulizi wamesimulia kwamba marehemu shahidi alipopita penye maduka mjini Kabul, alikuwa amepanda farasi na nyuma yake walikuwepo wapandaji wanane wa farasi wa serikali … Na walisimulia hii pia kwamba hao wapandaji wanane wa farasi wa serikali walimfuatilia kutoka Khost, kwani kabla ya kufika kwake Khost, amri ya serikali kwa kumkamata ilikuwa imekwishamfikia Hakimu wa Khost. Ilmuradi, alipoletwa mbele ya Amiri, wapinzani walikuwa wameishamkasirisha sana tayari. Kwa hiyo alimpokea kwa njia ya dhuluma sana na akaamuru kwamba msimamisheni mbali kidogo kwani ananuka. Kisha baada ya muda kidogo akaamuru kwamba mfungeni katika ngome ile anamoishi Amiri mwenyewe na afungwe mnyororo ya ***Gharagharab***. Mnyororo huu una uzito wa karibu kilo 64 ya Kiingereza, unaozunguka kuanzia shingo mpaka kiuno na kuna pingu pia ndani yake. Vilevile akaamuru atiwe pingu ya miguuni yenye uzito wa karibu kilo nane za Kiingereza. Katika hali hiyo marehemu Sahibzada alibaki gerezani kwa miezi minne. Katika muda huo, mara kadha akaambiwa na Amir kwamba kama ukitubu na kuachana na itikadi hii kwamba Bwana Qadiani ni Masihi Mau'udi, basi utaachiliwa. Lakini kila mara yeye akamjibu kwamba mimi ninayo elimu, na Mungu Amenijaalia uwezo wa kutambua haki na batili, nimeshagundua kwa utafiti kamili kwamba kwa kweli mtu huyo ni Masihi Mau'udi. Ingawaje najua kwamba kwa kuchagua njia hii uhai wangu hauna usalama na familia yangu

itaangamia, lakini wakati huu natanguliza imani yangu juu ya uhai wangu na juu ya kila raha ya dunia… Miezi minne ya kifungo ikapita. Hapo Amri akimwita barazani marehemu shahidi alimsihi kutubu. Akamhimiza sana kwamba hata sasa pia ukikataa mbele yangu kumsadikisha Bwana Qadiani na kusadikisha mafundisho yake, basi utasamehewa na utaachiliwa kwa heshima. Marehemu shahidi akajibu kwamba hii haiyumkiniki kwamba niachane na ukweli. Adhabu ya watawala wa dunia hii itakwisha pamoja na mauti, lakini namwogopa Yule ambaye adhabu yake haiwezi kuisha kamwe. Naam, kwa vile mimi ni juu ya ukweli, kwa hiyo nataka upangwe mjadala wangu na masheikh walio wapinzani wa itikadi yangu. Nikikutwa mwongo kwa hoja, basi niadhibiwe... Amiri alipenda jambo hilo, kwa ajili ya mjadala katika Masjid Shahi, wakateuliwa Khan Mulla Khan na Mamufti wanne. Na daktari mmoja aliyekuwa mpinzani mkali kwa sababu ya kuwa Mpanjabi alitumwa akiwa mwamuzi. Wakati wa mjadala walikuwepo mkusanyiko mkubwa ya watu. Walioshuhudia wanasema kwamba tulikuwepo katika mjadala. Mjadala ulikuwa kwa kimaandishi, wakaandikiana tu na wahudhuriao walikuwa hawapati kusikia lolote. Kwa hiyo haikujulikana hali yoyote ya mjadala. Kuanzia saa moja asubuhi mpaka saa tisa alasiri mjadala uliendelea. Kisha ulipokuwa mwisho wa wakati wa alasiri, alitolewa fatuwa ya kukufurishwa. Na mwisho wa mjadala marehemu shahidi aliulizwa hii pia kwamba kama huyo Bwana Qadiani ndiye Masihi Mau'udi, basi unasemaji juu ya Isa[as], je atarudi duniani au la? Hapo alijibu kwa uimara sana kwamba Hadhrat Isa[as] ameshafariki, hatarudi kamwe sasa. Kurani Tukufu ni shahidi juu ya kufariki na kutorudi kwake. Hapo watu hao, jinsi masheikh walivyorarua mavazi yao wakisikiliza kauli hii kuhusu Hadhrat Isa[as], wakaanza kutusi na wakasema kwamba sasa haikubaki shaka yoyote katika kufuru ya mtu huyu, na katika hali ya ghadhabu sana fatuwa ile ya kufuru iliandikwa… Kisha, baada yake wakati wa usiku fatuwa hiyo ya kufuru alipelekewa Bwana Amiri na ukafanywa ujanja

huu kwamba hakupelekewa kusudi maandishi ya mjadala, wala watu hawakuambiwa madhumuni yake. Hiyo ilikuwa dalili wazi kwamba masheikh wapinzani hawakuweza kujibu hoja zilizoletwa na marehmeu shahidi. Lakini ni masikitiko kwamba Amir akatoa amri sawa na fatuwa ya kufuru na hakuagiza kuleta maandishi ya mjadala... Marehemu shahidi kila mara alipoambiwa kutubu kwa itikadi zake, akakata. Hapo Amir akikata tamaa, akaandika kwenye karatasi kubwa maandishi kwa mkono wake na humo akaandika fatuwa ya masheikh, na ndani yake akaandika kwamba adhabu ya kafiri wa aina hii ni kuuawa kwa kupigwa mawe. Basi, fatuwa hiyo ilininginizwa shingoni mwa marehmeu Sahibzada. Kisha, Amir akaamuru kwamba marehemu akitobolewa pua atiliwe kamba mle ndani na akivutwa na kamba hiyo afikishwe penye kuuawa yaani mahali pa kuuawa kwa kupigwa mawe. Basi, kwa amri ya Amir huyo mdhalimu ikafanywa hivyo, pua ikatobolewa na kamba ikatiwa kwa adhabu kali sana. Kisha kwa kamba hiyo akavutwa mpaka penye kuuawa akifanyiwa mzaha, na kuchekwa na kutukanwa na kuapizwa. Na Amir, pamoja na masahibu wake, makadhi, mamufti na maafisa wengine, akitazama hali hiyo ya mateso akafika mpaka mahali pa kuuawa. Na halaiki kubwa ya watu maelfu wa mji wasiohesabika, walienda huko kuona tamasha hilo. Walipofika penye kuuawa, Bwana Sahibzada alizikwa ardhini mpaka kiunoni. Kisha katika hali ya kuzikwa ardhini mpaka kiunoni, Amir alimwendea na akasema kwamba ukimkataa Bwana Mirza anayedai kuwa Masihi Mau'udi, hata sasa nitakuokoa. Sasa ni wakati wako wa mwisho na hii ni nafasi ya mwisho unayopewa, ujihurumie na familia yako. Hapo marehemu shahidi akajibu, 'Mungu apishe mbali, nawezaje kukataa ukweli, na uhai ni kitu gani, na familia na watoto ni kitu gani ambao kwa ajili yao niache imani; sitafanya hivyo kamwe, nami nitakufa kwa ajili ya haki. Ndipo makadhi na mamufti walipiga makelele, 'yu kafiri, yu kafiri, mtupieni mawe haraka.' Wakati huo Amir na nduguye Nasrullah Khan, Kadhi na Abdul Ahad, Mkuu wa kikosi, walikuwa wamepanda mafarasi na watu

wengine wote walikuja kwa miguu. Katika hali hiyo ya hatari, marehemu shahidi mara kwa mara aliposema kwamba natanguliza imani juu ya uhai, ndipo Amir alimwamuru kadhi wewe umtupie jiwe la kwanza, kwani wewe umetoa fatuwa ya kufuru. Kadhi akasema, u mfalme wa zama hizi, utupe wewe. Hapo Amiri akajibu kwamba mfalme wa sheria ni wewe na fatuwa pia ni yako, mimi simo humu. Ndipo, Kadhi akishuka kutoka juu ya farasi na akapiga jiwe ambalo kwalo marehemu shahidi alijieruhiwa vibaya na shingo yake ikainama. Kisha baada yake Amir, mwenye bahati mbaya alimtupia jiwe kwa mkono wake, hapo kwa kumfuata yeye, maelfu ya mawe yalirushwa kumpiga shahidi. Na kulikuwa hakuna yeyote kati ya wahudhuriao ambaye hakumtupia jiwe shahidi hata kwamba mawe mengi sana yakarundikana juu ya kichwa cha marehemu shahidi. Kisha wakati wa kurudi Amir alisema kwamba mtu huyu alisema kuwa katika siku sita nitafufuka, kwa hiyo yapasa hapa palindwe kwa siku sita. Imeelezwa kwamba dhuluma hiyo, yaani kuua kwa kupiga mawe, ilitokea tarehe 14 Julai 1903… Kifo cha kishahidi kilichokadiriwa kwa Shahzada Abdul Latif kimetokea, sasa iliyobaki ni kumwadhibu dhalimu... Ee Abdul Latif, rehema maelfu ziwe juu yako kwamba umeonyesha mfano wa ukweli wako katika uhai wangu, na watu wa Jumuiya yangu ambao watabaki baada ya kifo changu, sijui watafanya nini."

Hudhur[as] akieleza habari zilizobaki za Bwana Sahibzada Shahidi, ameandika mwishoni mwa kitabu chake *Tadhkiratush Shahadatain*:

"Mian Ahmad Nur aliye mwanafunzi maalum wa Hadhrat Sahibzada Maulawii Abdul Latif, amefika Qadian kutoka Khost pamoja na familia yake leo tarehe 8 Novemba 1903. Yeye ameeleza kwamba mwili wa Bwana Maulawii ulibaki kwa siku arobaini ndani ya mawe aliyotupiliwa kwa kumuua. Baada yake, mimi pamoja na ndugu wachache tulitoa mwili wakati wa usiku, tukauleta kwa kuficha-ficha mjini. Ilihofiwa kwamba Amir na wafanyakazi wake watazuia, lakini kwa sababu ya kuenea

kipindupindu mjini, kila mtu alikuwa amenaswa katika balaa yake. Kwa hiyo, bila shida tulipeleka mwili wake makaburini, tukasali jeneza humo na kumzika. Ni la ajabu kwamba Bwana Maulawii alipotolewa kutoka katika mawe, mwili wake ulikuwa unanukia kama miski. Watu waliathirika sana na jambo hilo."

MATOKEO YA MAUAJI HAYO PASIPO HAKI

Hudhur[as] ameandika katika sehemu fulani ndani ya kitabu chake hicho *Tadhkiratush Shahadatain*:

"Na ardhi ya Kabul itaona kwamba damu hii itazaa matunda gani ya aina aina. Damu hii haitapotea bure kamwe. Hapo kabla maskini Abdur Rahman wa Jumuiya yangu aliuawa kwa dhuluma, na Mungu Alinyamaza. Lakini kwa mauaji haya sasa hatanyamaza, na matokeo makubwa makubwa yatadhihirika. Basi, imesemekana kwamba marehemu shahidi alipouawa kwa kupigwa maelfu ya mawe, siku hizo hizo kipindupindu kikali kilizuka katika Kabul, na wakubwa wengi wa utawala walikufa nacho, na baadhi ya jamaa wa Amir pia waliaga dunia. Lakini hiyo siyo basi. Damu hii ilimwagwa kwa dhuluma kubwa, na katika zama hizi chini ya mbingu hautapatikana mfano wa mauaji ya namna hii. Amefanya nini huyo Amir mjinga! Amejiangamiza kwa kumwua kikatili mtu kama huyo asiye na kosa. Ee ardhi ya Kabul, uwe shahidi kwamba uhalifu mkubwa umetendwa juu yako. Ee ardhi yenye bahati mbaya, umedhalilika machoni mwa Mungu, kwani u mahali pa dhuluma hiyo kubwa."[445]

Katika mauaji hayo, alihusika zaidi ndugu wa Amir, Sardar Nasrullah Khan kuliko Amir wa Kabul. Anaandika Bwana Angus Hamilton kumhusu yeye:

(Siku ya pili ya kuuawa marehemu Shahid kwa kupigwa mawe, yaani tarehe 15 Julai 1903.)

"Katika Kabul, mji wa Afghanistan, na mikoa yake ya kaskazini

[445] Tadhkiratush Shahadatain uk. 72

na mashariki kipindupindu kilizuka kwa nguvu sana kilichokuwa kibaya zaidi kuliko kipindupindu cha mwaka 1879. Mkewe Sardar Nasrullah Khan na mwanaye mmoja na watu kadha wa familia ya mfalme na maelfu ya wakazi wa Kabul walikufa kwa maradhi hayo. Mambo yakavurugika vuruvuru mjini, na kila mtu alijihangaikia uhai wake na akasahau kabisa kuwajulia wengine hali zao."[446]

AMIR HABIBULLAH KHAN KAUAWA, 20 FEBRUARI 1919

Amir Habibullah Khan ambaye katika zama zake marehemu Hadhrat Shahid aliuawa kwa kupigwa mawe kwa njama ya ndugu yake, aliuliwa kwa kupigwa bastoli mara moja, tarehe 20 Februari 1919, wakati wa usiku akilala.

MWISHO WA SARDAR NASRULLA KHAN

Baada ya kuuawa kwa Amiri Habibullah Khan, alijitwalia Sardar Nasrullah Khan ufalme uliokuwa haki ya mrithi wa halali Sardar Inayatullah Khan. Kuona hali hiyo, Sardar Amanullah Khan aliyekuwa mwana wa tatu wa Amir Habibullah Khan akiungana na mawaziri wa utawala na masheikh, alishikilia utawala kwa nguvu na akaamuru kuwahudhurisha Sardar Nasrulla Khan na wenzake wakifungwa pingu za miguu, na tarehe 3 Aprili 1919 alifungwa katika ngome ya kifalme, na baadaye wakawekwa katika mnara. Inasemekana kwamba kwa huzuni hiyo akawa mwendawazimu. Baada ya muda kidogo aliuawa kwa kukabwa. Hii pia inesemekana kwamba Dkt. Ahmad Beg Mturuki msaidizi wa Dkt. Munir Izzat alimwua mwishoni mwa Aprili 1919 kwa kumlisha sumu kwa amri ya Amir Amanullah Khan.

MWISHO WA DAKTARI MPANJABI ABDUL GHANI

Dkt. Abdul Ghani, "Daktari Mpanjabi" aliyekuwa ametoa uamuzi katika hafla ya mjadala alifungwa pamoja na ndugu zake kwa miaka kumi na mmoja. Mkewe alipoondoka Kabul kurejea Panjab, njiani kwenye nyumba ya wageni katika Landikotal alifariki na watu

[446] Someni "Afghanistan" uk. 45 na Bwana Angus Hamilton

walikusanya fedha kwa ajili ya sanda na mazishi. Mwanaye Abdul Jabar alikuwa anarudi nyumbani baada ya kununua vitu kutoka soko, mtu fulani alikata kichwa chake akimpiga upanga kutoka nyuma. Mwanaye mwingine aliyekuwa msaidizi wa daktari katika hospitali za wanyama huko kwao katika wilaya ya Gujrat, sasa hana kazi, ameshakuwa mzee.

MWISHO WA KADHI SHEIKH ABDUR RAZZAK

Kadhi Sheikh Abdur Razzak aliyemtupia marehemu Shahidi jiwe la kwanza, hali yake ikawa kwamba Amiri wa Kabul, Habibullah Khan, alitoa amri kuwa mtu yeyote asitembee upande wa kuume wa barabara yoyote, bali watu wote watembee upande wa kushoto. Siku moja Amir wa Kabul alikuwa akipita barabarani, akaona kwamba Sheikh Abdur Razzak Khan, Sheikh Mkuu, anatembea barabarani upande wa kulia, na polisi aliye kazini anamkataza lakini yeye hamjali. Amir wa Kabul akiona hiyo alimfaini Rupia 1,000. Baadaye katika zama za Amir Amanullah Khan, Amir aliamuru kuwa haji Abdur Razzak achapwe mijeledi, na kumwamuru kuhudhuria kila siku kama mtu mhalifu.

Baada ya adhabu hiyo alipotea kutoka Kabul kana kwamba kazikwa akiwa hai.[447]

UTAWALA UKAITOKA FAMILIA YA AMIRI HABIBULLAH KHAN

Kama Mwenyezi Mungu Angetaka angeinyang'anya utawala familia ya Amir Habibullah Khan wakati uo huo, lakini aliipa muda fulani familia hiyo kujirekebisha. Lakini, familia hiyo isipoweza kutenda kitendo chochote kizuri, bali kwa kuwaua Waahmadiyya kadha, hao watu wakachemsha ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, basi mtu mmoja wa kawaidia sana, Bachcha Sakka, akamshambulia Amanullah Khan, Amir wa mwisho wa famili hiyo, na kumfukuza nchini. Naye mpaka leo anapitisha siku za maisha yake katika Italia kama mmiliki wa

[447] Kwa maelezo zaidi ya matukio hayo, someni "*Shuhadaul Hak*" cha Hadhrat Kadhi Muhammad Yusuf wa Peshawar, Amiri wa zamani wa Jumuiya za Ahmadiyya za mkoa wa Sarhad.

hoteli fulani. *Jifunzeni enyi wenye macho.*

TUKIO LA KIMWUJIZA LA KUKUBALIWA DUA, 25 OKTOBA 1903

Hadhrat Maulawii Abdul Karim[ra] Sialkoti anasema:

> "Mwana mdogo Abdur Rahim wa Nawab Muhammad Ali Khan akawa mgonjwa sana. Kwa siku 14 aliendelea kuugua homa, na hisia zake zikavurugika na akazimia. Hatimaye hali ikawa mwili kuwaka na homa... Hudhur Khalifatulllah[as] kila siku aliombwa kwa ajili ya dua, naye aliendelea kuomba. Tarehe 25 Oktoba, Hudhur[as] aliambiwa kwa huzuni sana kwamba Abdur Rahim hana alama nzuri kuishi. Hudhur[as] alipokuwa akimwombea katika sala ya tahajudi, akafunuliwa na Mungu:
>
> "Ni takdiri isiyoepukika, na kifo kimekwishaamuliwa."
>
> Hudhur[as] Kasema: Wahyi huu mkali uliposhuka, nikatawaliwa na huzuni sana. Wakati ule ghafula ikatoka mdomoni mwangu "Ee Mungu, kama huu sio wakati wa dua, basi nafanya maombezi, nafasi yake ipo. Hapo mara wahyi ikashuka:
>
> يُسَبِّحُ لَهٗ مَنۡ فِی السَّمٰوٰتِ وَمَنۡ فِی الۡاَرۡضِ مَنۡ ذَا الَّذِیۡ یَشۡفَعُ عِنۡدَهٗۤ اِلَّا بِاِذۡنِهٖ
>
> Yaani, wanamtukuza viumbe wote wa mbinguni na ardhini. Ni nani afanyaye maombezi mbele Yake bila ya idhini Yake!
>
> Kwa wahyi huo wa kijalali mwili wangu ulitetemeka na nikajawa na hofu na heba sana, kwani nilifanya maombezi bila idhini. Baada dakika 1-2, tena nilipata wahyi.
>
> اِنَّكَ اَنۡتَ الۡمُجَازُ
>
> Yaani, unayo idhini. Baada yake, Abdur Rahim alianza kupona haraka haraka. Kila mmoja aliyeona na kujua, akajaa shukurani kwa Mwenyezi Mungu kwa kumwona na akakiri kwamba bila shaka ni mfu aliyehuika."[448]

[448] Al Badr, J. 2, Na. 41-42, 29 Oktoba 1903

VITABU VYA MWAKA 1903

***Mawahibur Rahman*, 14 Januari 1903**: Gazeti moja la Kiarabu liitwalo "Al Liwaa" lilikuwa likitoka Misri. Mnamo Novemba 1902, mhariri wake aliandika katika toleo lake kwamba tumejua kutokana na gazeti la Kiingereza kuwa mtu fulani wa India amedai Umasihi na Unabii na anasema kwamba kudungwa sindano ya tauni haifai, hiyo ni kinyume cha kumtegemea Mungu. Gazeti hilo aliletewa Hudhur[as] tarehe 25 Novemba 1902. Hudhur[as] alisema:

> "Inaonekana Mwenyezi Mungu Ameshanuia kutangaza na kueneza (habari hii) katika Misri. Utangajazi wa (ujumbe wa) Mtume Mtukufu[saw] ulifanyika hivyo hivyo. Wapinzani walikuwa wanatangaza kwa njia mbaya. Kundi la watu wema likajitenga nao. Kwa vyovyote walikwishapata habari."

Hapo Hudhur[as] alinuia kwamba kwa kulijibu gazeti "Al Liwaa" aandike kitabu kimoja katika lugha ya Kiarabu. Basi, akaanza kuandika *Mawahibur Rahman*. Katika kitabu hicho, Hudhur[as] ameeleza kwa marefu na mapana imani na kutumia njia za dhahiri vilevile.

***Nasime Da'wat*, 28 Februari:** Kwa kuona shughuli za mahubiri za Hudhur[as], Waaria wa Qadian pia walipata harara. Wakatoa tangazo moja chafu sana dhidi ya Hudhur[as] tarehe 7 Februari 1903 kwa kichwa cha habari "Jibu kwa majivuno ya wafuasi wa Papa wa Qadian." Katika tangazo hilo wakatumia midomo michafu sana dhidi ya Mtume Mtukufu[saw], Hudhur[as] na waheshimiwa wa Jumuiya, Mungu Apishe mbali. Kwa kujibu tangazo hilo, Hudhur[as] alichapisha kitabu *Nasime Da'wat*. Katika kitabu hicho, kwanza Hudhur[as] aliwasihi wanajumuiya wake kusubiri, kisha akajibu kila swali la Waaria.

***Sanatan Dharm*, 8 Machi 1903:** Waaria wa Qadian walifanya mkutano tarehe mosi Machi 1903, Hudhur[as] alituma kitabu chake "Nasime Da'wat" katika mkutano. Kutoka katika kitabu hicho Pandit Ram Bhajdat akisoma habari za *Neyoga* alisema kwamba kama Bwana Mirza angejadili nami juu ya swala la *Neyoga* kabla ya kitabu hiki, ningemtuliza kwa kueleza faida za *Neyoga*. Kwa kusikiliza maneno hayo ya Bwana Pandit, Hudhur[as] aliandika kijitabu "Sanatan Dharm" ambamo alieleza waziwazi uchafu wa swala la *Neyoga*.

Kijitabu hicho kilichapwa 8 Machi 1903.

***Tadhkiratush Shahadatain*, 16 Oktoba 1903:** Hudhur[as] alichapisha kitabu hiki tarehe 16 Oktoba 1903. Ndani yake, Hudhur[as] alieleza kwa urefu vifo vya kishahidi vya Hadhrat Sahibzada Abdul Latif, Shahidi wa Kabul, na mwanafunzi wake mwema Hadhrat Mian Abdur Rahman.

***Siratul Abdaal*, 14 Desemba 1903:** Hiki ni kijitabu kidogo katika lugha yenye ufasaha sana ya Kiarabu lakini ngumu mno, alichoandika Hudhur[as] kwa kuwatahini masheikh ujuzi wao wa lugha ya Kiarabu. Katika kijitabu hiki, Hudhur[as] aliandika alama za *Abdaal,* yaani Mawalii wa Allah.

KUZALIWA KWA AMATUL HAFIIDH BEGAM, 25 JUNI 1904:

Tarehe 25 Juni 1904, binti wa Hudhur[as] alizaliwa, aliyeitwa Amatul Hafiidh Begam. Hudhur[as] alifunuliwa juu ya binti huyu "دُخْتِ کرام" Binti wa waungwana.[449]

SAFARI YA LAHORE, 20 AGOSTI 1904

Jumuiya la Lahore ilikuwa imemwomba Hudhur[as] mara nyingi kuitembelea Lahore, na Hudhur[as] akaahidi pia, lakini kwa shughuli za kesi za Maulawii Karmuddin, Hudhur[as] hakuweza kutimiza ahadi yake. Baada ya mahudhirio ya 18 Agosti 1904, tarehe ijayo iliyopangwa ya 5 Septemba 1904, akaona nafasi hii ya katikati ni ya kutosha, basi Hudhur[as] pamoja na familia yake akaja Lahore kutoka Gurdaspur tarehe 20 Agosti 1904. Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin, Hadhrat Maulawii Abdul Karim, Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan na Maulawii Muhammad Ali pia walikuwa na Hudhur[as]. Habari za Hudhur[as] kwamba anakuja, zilienea mjini kote

[449] Katika umri wa miaka 11, iliamuliwa aolewe na Hadhrat Nawab Mian Abdullah Khan bin Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan, Chifu wa Maler Kotla. Tarehe 7 Juni 1905 sawa na 23 Rajabu 1333 Hijria, siku ya Jumatatu, Hadhrat Maulawii Ghulam Rasul Rajeki alitangaza ndoa hiyo kwa mahari ya Rupia 15,000 katika Masjid Aqsa, baada sala ya alasiri. Na takriban baada ya miaka miwili tarehe 23 Februari 1917 sawa na 29 Rabii II 1335 Hijria, siku ya Alhamisi akasindikizwa kwenda kwa mumewe. Tarehe 23 na 24, Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan aliwakaribisha jamaa wa Qadian kwa karamu ya walima ya Mian Abdullah Khan.

haraka sana. Basi, Hudhur[as] alipofika kwenye stesheni, Mabaniani na Waislamu walijazana hapo hata kwamba haikubaki nafasi hata kidogo. Idadi kubwa ya Wazungu pia walikuja kumwona Hudhur[as]. Nyumba ya Hadhrat Mian Merajuddin Umar ilipendekezwa kwa ajili ya Hudhur[as] kukaa, iliyotambulika baadaye kwa jina la "Mubarak Manzil".

MAJI HAYAKUNAJISIKA

Keshoye, tarehe 21 Agosti 1904, wakati wa sala ya adhuhuri, Hudhur[as] akatoka akaja nje. Baada ya kusali sala ya jamaa wanajumuiya walisisitiza kwamba Hudhur[as] akae kitini ili watu wote waweze kumwona Hudhur[as] kwa urahisi. Siku ile Hudhur[as] alitoa hotuba yenye elimu ya ndani sana. Wanaume kwa wanawake wa wilaya nyingi za Panjab walikuwa wamejumuika. Hadhrat Mian Abdul Aziz Mughal alikuwa anasema kwamba kwa sababu ya kuhudhuria watu wengi, mitungi mikubwa mikubwa ya maji iliwekwa. Baadhi ya wanawake walipochukua maji humo kwa kuosha mikono na miguu ya watoto wao, mtu fulani akalalamika mbele ya Hudhur[as] kwamba akina mama wamenajisi maji. Hudhur[as] kwa makini sana aliiendea mitungi, alichota maji kutoka katika mtungi mmoja na akanywa na akasema maji ni baridi, kana kwamba Hudhur[as] akawaambia kwa kitendo chake kwamba maji hayajanajisika; kama yangekuwa yamenajisika nisingekunywa.

HOTUBA YA KUZIDISHA IMANI, NA WENGI WALIFANYA BAIATI

Tarehe 28 Agosti 1904, Hudhur[as] alitoa hotuba ya kuzidisha imani kuhusu hekima ya toba, imani na kushuka balaa. Siku hiyo watu wengi waliokuja kutoka matawi ya nje walifanya baiati, iliyofanywa kwa kushika vilemba, kwa sababu ya wingi wa wafanyao baiati.

HOTUBA YA LAHORE, 3 SEPTEMBA 1904

Tarehe 3 Septemba 1904, hotuba yake mashuhuri juu ya "Islam na dini nyingine za nchi hii" ilitolewa katika ukumbi ule uliopo nyuma ya ziara la Hadhrat Data Ganj Bakhsh, na siku hizo ulikuwa unaitwa ukumbi wa Mela Ram. Kuhusu hotuba, matangazo yaliyochapishwa

yalisambazwa katika mji mzima wa Lahore. Kwa hiyo, kabla ya kuanzia hotuba ukumbi mzima ulijaa. Karibu na mahali pa hotuba, masheikh wapinzani, kwa kuzuia watu wasiende mkutanoni, waliendelea kusema kwa kupaza sauti sana kwamba Mwislamu atakayesikiliza hotuba, ndoa yake itavunjika. Sheikh mmoja aliyekuwa akiupanda mti unaoitwa *Shisham* kwa Kiurdu na *Tahli* kwa Kipanjabi, kwa kuwazuia watu. Baadaye mtu huyo akawa mashuhuri kwa jina la "Sheikh Tahli". Ni kudra ya Mungu kwamba kadri masheikh walivyowazuia watu, ndivyo halaiki ya watu walivyozidi kuelekea penye mkutano kwa shauku kubwa. Usimamizi wa polisi pia ulikuwa mzuri mno. Hotuba ilianza kutolewa katika wakati wake uliowekwa, saa kumi na mbili u nusu. Hutuba ya Hudhur[as] iliyokuwa imeishachapwa aliisoma Hadhrat Maulawii Abdul Karim kwa sauti ya juu katika hafla ya watu maelfu. Hotuba ilikuwa imegawanywa katika sehemu mbili. Katika sehemu ya kwanza yalifanywa malinganisho kati ya Islam na dini zingine za nchi hii. Na katika sehemu ya pili, zikitolewa ishara hai za Mungu Aliye Hai ikathibitishwa kuwa Islam ni dini iliyo hai. Hadhrat Maulawii Abdul Karim alipomaliza kusoma hotuba ya Hudhur[as], wahudhuriao walisisitiza kwamba Hudhur[as] aseme chochote kwa ulimi wake pia. Hudhur[as] aliposimama, wapinzani walianza kupiga makelele. Kuona hali hiyo, Hadhrat Maulawii Abdul Karim alianza kusoma Kurani Tukufu kwa sauti nzuri. Hapo, watu waliathirika sana, wote wakanyamaza. Mara baada yake Hudhur[as] alianza kutoa hotuba. Kwanza Hudhur[as] aliwashukuru watu, kisha akasema kwamba msifanye hitilafu za dini kuwa sababu ya uadui na kuudhi. Huluka za Mungu ni zenye wasaa, nyinyi pia muwe na moyo mkunjufu. Siwaambieni kwamba msitaje hitilafu ya dini; tajeni na bila shaka tajeni, lakini kwa nia safi; msilete kati uadui na chuki.

Hotuba iliathiri vizuri sana, na juhudi zote za upinzani za masheikh zilipotea bure. Twamsifu Mungu kwa hayo.

SAFARI YA SIALKOT, 27 OKTOBA 1904

Miezi miwili baada ya safari ya Lahore, alienda Sialkot mnamo Oktoba 1904. Kwa ajili ya kutembelea Sialkot, ndugu wa hapo

walikwishamwomba wakati wa kukaa kwake Lahore. Hudhur[as] alikuwa amekubali. Basi, tarehe 27 Oktoba 1904, saa kumi za asubuhi Hudhur[as] aliondoka Qadian, ahli zake pia walikuwa pamoja naye. Kutoka stesheni ya Batala, behewa moja la daraja ya pili, na behewa moja daraja ya wastani, zikateuliwa. Gari lilipowasili Amritsar, wanajumuiya wa pale walimletea Hudhur[as] chakula kwa ikhlasi sana ambacho Hudhur[as] akakubali. Garimoshi lilipofika Lahore, watu walijumuika kwenye stesheni kiasi hiki kwamba ikawa vigumu kwa maafisa wa reli na polisi kuwasimamia. Kwenye stesheni ya Wazirabad pia watu wakajazana kiasi hiki kwamba ikawa vigumu kwa wafanyakazi wa reli kutenganisha behewa lake liliokuwa limeteuliwa, na kuunganisha na gari la Sialkot. Wanajumuiya wa Wazirabad pia waliwaletea Hudhur na wenzake soda na sharubati ya limau. Ingawa gari lilifika stesheni ya Sialkot baada ya magharibi, hata hivyo stesheni ilijaa sana wenye shauku ya kumwona. Hudhur[as] pamoja na wenzake walipopanda magari ili kwenda pahali pa kukaa, nje watu walionekana kila mahali. Mamia ya watu walikimbia pamoja na gari lake. Agha Muhammad Bakir Khan, Hakimu wa heshima, asiyelipwa, alitembea kando ya gari la Hudhur[as] kwa kupanga watu. Njiani kwa kuweka mwanga mbele ya gari la Hudhur[as] fashifashi zililipuliwa. Hudhur[as] alikaa katika nyumba ya Hadhrat Hakim Husamuddin.

UKARIMU WA WANAJUMUIYA WA SIALKOT

Kwa vile nyumba ya Hadhrat Hakim haikutosha kwa kukaa kwa ndugu wote, kwa hiyo wanajumuiya wengi wa maeneo yale waliwaachia nyumba zao wageni kwa njia hii kwamba mtaa wote ukawa kama nyumba moja. Katika kila chumba, maji ya kutosha yalikuwepo na mwanga pia. Jumuiya iliteua mjini maduka ya wafamasia kwa kupata dawa bure. Mpango wa chakula ulikuwa hivi kwamba wazee kutoka Qadian walikuwa wakipelekewa chakula pale walipokaa, na wageni wengine waliokuja kutoka wilaya za Sialkot, Gujaranwala, Lahore, Jhelum, Gujrat na kadhalika walipangwa kula chakula katika uga mmoja wenye wasaa.

MAPOKEZI

Nilisahau kutaja kwamba wakati wa ujio wa Hudhur[as] katika Sialikot,

Jumuiya iligawa mapokezi yaliyochapwa ambamo ziliandikwa beti hizi mbili:

> Ewe ambaye ujio wako ni raha kwetu, kukutaja ni wimbo wa kutufurahisha.
>
> Ee mola, tandaza juu ya moyo wetu usiotulia kivuli cha yule aliye Khidhiri wetu, Mahdi wetu, Isa wetu, Mirza wetu.

HOTUBA YA HUDHUR[as] BAADA YA SALA YA IJUMAA

Siku ya pili, tarehe 28 Oktoba, ilikuwa siku ya Ijumaa. Sala ya Ijumaa alisalisha Hadhrat Maulawii Abdul Karim katika Msikiti wa Hadhrat Hakim Husamuddin. Katika hotuba alitoa maelezo ya Sura Al-Jumu'a. Baada ya sala, watu wengi walifanya baiati. Kwa vile idadi ya wafanyao baiati ilikuwa kubwa sana, kwa hiyo vilemba 12 vilisambazwa kwa jeha mbalimabli, ambavyo watu wakivishika walirudia ahadi ya baiati. Baada ya baiati, Hudhur[as] alitoa hotuba fupi ambamo akatia mwanga juu ya uhakika wa baiati na akasihi kutanguliza dini juu ya dunia. Hotuba hiyo ilichapwa katika magazeti ya Jumuiya.[450] Baada ya sala ya Ijumaa akakaa na watu kwa muda mrefu, kwa hiyo afya ya Hudhur[as] iliathirika sana, kwa hiyo siku mbili zijazo, yaani 29 na 30 Oktoba, Hudhur[as] hakuweza kuja nje. Tarehe 31 Oktoba 1904, Hudhur[as] alidhihirisha nia yake ya kurudi, kwani wageni wengi sana walijumuika kuliko ilivyotarajiwa, na Hudhur[as] alihofia kwamba isije Jumuiya ya Sialkot ikaona shida kuhusiana na maakuli yao. Hadhrat Hakim alipojua habari hiyo, mara moja akamjia Hudhur[as] na akataja wingi wa vyakula na kumwomba Hudhur[as] kuahirisha nia yake. Hudhur[as] akajali sana furaha ya Bwana Hakim, kwani alikuwa na mahusiano naye tangu siku za kufanya kazi katika Sialkot, kwa hiyo aliahirisha nia yake ya kurudi.

PENDEKEZO LA HOTUBA KATIKA MKUTANO WA HADHARA

Iliamuliwa kwamba katika Sialkot mkutano wa hadhara ufanywe. Basi, kwa lengo hilo, baada ya kuweka tarehe 2 Novemba 1904,

[450] Al-Hakam, toleo la 10-17, Novemba 1904

ilienezwa kwa njia ya matangazo, na Hudhur[as] akashughulikia kutayarisha hotuba. Kwa hiyo, tarehe 31 Oktoba 1904 pia Hudhur[as] hakuweza kuja nje. Idadi ya wapendao kumwona iliendelea kuzidi. Kuona hali hiyo Hudhur[as] aliombwa akae kwa muda kidogo kwenye dirisha ili watu waweze kumwona kutoka mtaani. Hudhur[as] akaja dirishani, lakini kwa kujumuika maelfu ya watu, alihofia kwamba isije mzee, mtoto au dhaifu yeyote akakanyagwa kwa msongamano wa watu, hivyo akasimama kwa dakika moja tu na akaondoka.

Alikuwa anaandika haraka sana hata kwamba baadhi ya wakati aliandika kitabu cha mamia ya kurasa katika siku chache. Hotuba ya Sialkot iliyo hotuba ya hali ya juu sana, Hudhur[as] alianza kuiandika baada ya adhuhuri ya 31 Oktoba na tarehe mosi Novemba ilikwishachapwa tayari. Hotuba ilikuwa juu ya "Islam" iliyopangwa kusomwa katika nyumba ya wageni ya Maharaja wa Jammu, tarehe 2 Novemba 1904, saa moja asubuhi. Mkutano ulifanyika katika uga wa nyumba ya wageni ya Maharaja wa Jammu ambapo yalitandazwa mazulia mengi na kutiwa kivuli kwa kanopi nyingi.

Kwa vile Hadhrat Maulawii Abdul Karim akija kabla ya Hudhur[as], alikwishatoa hotuba mbili hadharani katika mji, na matangazo pia yalisambazwa kwa wingi, kwa hiyo masheikh wapinzani walifanya mpango wa kuzuia watu wasifike mkutanoni. Wakaanza kutoa hotuba siku hiyo asubuhi saa kumi na mbili na nusu katika sehemu mbalimbali za mji. Hata hivyo, watu walijumuika kusikiliza hotuba ya Hudhur[as] wengi sana kiasi hiki hata ikawa vigumu kupata nafasi ya kuwakalisha.

KWENDA MKUTANONI

Hudhur[as] alienda mkutanoni kwa sura ya maandamano, kwa magari 15-16. Hadhrat Maulawii Abdul Karim alikaa na Hudhur[as] kando ya gari la Hudhur[as], Sardar Muhammad Yusuf Khan, Hakimu wa mji, alikuwa akitembea kwa kusimamia mambo. Pande zote mbili za barabara halaiki ya watu walijumuika kwa wingi kiasi hiki kwamba kwa taabu sana njia ilikuwa inafanywa kupitia magari. Njiani vituo vya masheikh wapinzani pia vilionekana. Masheikh kwa kupaza sana sauti, walikuwa wanawazuia watu wasiende mkutanoni. Lakini

matokeo yake yakawa kwamba watu waliojua tayari mahali pa mkutano walielekea huko, lakini wale ambao hawakujua pia wakajua kwa hotuba za masheikh nao wakaenda mbio mkutanoni. Mungu Akitaka adui pia anasababisha heri.

HOTUBA YA MWENYEKITI, HADHRAT MAULANA HAKIM NURUDDIN

Hudhur[as] alipofika mkutanoni, aliona kwamba maelfu ya watu wa kila dini na kabila wameshajumuika. Waheshimiwa wa mji walikuwa na rai hii kwamba mpaka leo katika Sialkot watu wengi kiasi hiki hawajaonekana katika hotuba ya mtu yeyote. Kwenye jukwaa, pamoja na Hudhur[as] walikaa Hadhrat Maulawii Abdul Karim na wazee wengine. Baadhi ya waheshimiwa wa mji pia walikaa hapo. Kwa maoni ya Mian Fadhl Husain Wakili na kwa kuungwa mkono na wahudhuriao, Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin akawa mwenyekiti wa mkutano. Yeye papo kwa papo akawaambia katika hotuba yake fupi kwamba ndani ya Kurani Tukufu wametajwa katika aya لَوْ كُنَّا نَسْمَعُ اَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا فِيْ اَصْحٰبِ السَّعِيْرِ waja ambao kwa kutosikiliza maneno yao, watu watalazimika kusema siku ya kiyama 'Laiti tungalisikiliza maneno yao na kutafakari kwa kutumia akili, tusingalipata leo taabu.' Hotuba ya mja wa aina hiyo mtasikiliza sasa hivi. Kwa hiyo, sikilizeni kwa kutega masikio na kutenda sawa nayo.[451]

HOTUBA YA HUDHUR[AS]

Baada yake, Hudhur[as] alimwambia Hadhrat Maulawii Abdul Karim asome hotuba ya Hudhur[as]. Hadhrat Maulawii Abdul Karim kwanza alisoma fungu la mwisho la Sura Al-Hashr kwa sauti nzuri na kubwa, kisha akaanza kusoma hotuba ya Hudhur[as] kwa njia nzuri sana ya kuvutia. Kueleza mandhari ya wakati huo ni nje ya uwezo wetu. Watu kwa makini sana waliendelea kusikiliza hotuba ya Hudhur[as], na watu wengi walisimama juani pia.

Sifa maalum ya hotuba hii ilikuwa kwamba akieleza madai yake, ni mara ya kwanza kabisa alidai hadharani kuwa mithili wa Karishna. Kisha akiwaambia Mabaniani na Waaria kwamba nawasihini nikiwa

[451] Al-Hakam, 30 Novemba, 10 Desemba 1904.

Karishna kwamba kuamini kuwa mata na roho ni za tangu azali na za kudumu milele pamoja na Mwenyezi Mungu ni itikadi batili na imejaa ushirikina. Kwa hiyo, iacheni itikadi hii. Kadhalika akasema kwamba itikadi ya ***tanasukh*** pia ni batili, na ***Neyoga*** ni kitendo kichafu kiasi hiki kwamba ni aibu kuieleza pia.

Baada ya hotuba kumalizika, alipoondoka pamoja na wafuasi wake kurudi palipokaa, katika gari lililofungwa, njiani wapinzani walianza kulitupia gari mawe, lakini kwa fadhili na rehema ya Mwenyezi Mungu, Hudhur[as] alifikia makazi yake kwa usalama. Kwa kuona shari za wapinzani, Inspekta wa polisi Mzungu aliyekuwa wakati huo kazini, aliwaambia masheikh:

> "Twashangaa, kwa nini mnampinga mtu huyu, ilitupasa sisi (Wakristo) au Mabaniani kumpinga, kwani anapinga dini yetu. Yeye anathibitisha Islam kuwa dini ya kweli, anaangamiza dini yetu, mnampinga bure."[452]

WATU WENGI WALIFANYA BAIATI

Tarehe 3 Novemba 1904, Hudhur[as] alipanga kurudi, kwa hiyo tarehe 2 Novemba, yaani siku ile ya hotuba, watu wengi walifanya baiati kwa mkono wa Hudhur[as].

BAIATI YA HADHRAT CHAUDHARI NASRULLAH KHAN

Mheshimiwa Chaudhari Asadullah Khan Wakili, Amiri wa Jumuiya ya Waahmadiyya ya Lahore,[453] anasema kwamba baba yetu (Chaudhari Nasrullah Khan) pia alifanya baiati tarehe 2 au 3 Novemba, na mama yetu alitangulia siku chache kufanya baiati kwa sababu ya ndoto yake.[454] Baba alikuwa mtu mwenye tabia ya kuchunguza sana mambo na alijua vizuri mienendo ya Hudhur[as]. Katika kesi ya Maulawii Karmuddin, Hudhur[as] alimwita pia baba

[452] Al-Hakam, 30 Novemba, 10 Desemba 1904.

[453] Mdogo wa Chaudhari Sir Muhammad Zafrullah Khan.

[454] Mheshimiwa Chaudhari Sir Muhammad Zafrullah Khan, aliyekuwa mwenyewe sahaba wa Hudhur[as], ameandika katika kitabu chake, "Mama Yangu", kwamba wakati wa baiati ya baba na mama wote wawili, yeye alikuwa pamoja nao.

kama shahidi, na kabla ya ushahidi akasema, 'Bwana Chaudhari, katika ushahidi wako useme yale tu unayojua. Baba kwa hayo aliathirika sana. Na ukweli wa Jumuiya aliujua hivi kwamba katika Sialkot (Makao ya wanajeshi) ulikuwepo msikiti ambao imamu na msimamizi wake alikuwa Hadhrat Maulawii Abu Yusuf Mubarak Ali. Kwa vile akajiunga katika Jumuiya Ahmadiyya, kwa hiyo msikiti pia ukawa chini ya usimamizi wa Waahmadiyya. Baada ya muda fulani wasiokuwa Waahmadiyya walitaka kuteka msikiti huo. Hudhur[as] alipoambiwa, akasema kwamba kama Chaudhari Nasrullah Khan akikubali, basi mfanyeni wakili katika kesi yenu. Kwa kufuatilia kesi barabara ilibidi asome vitabu vya Hudhur[as], na akafanya hivyo. Alipohudhuria mahakamani, aliona kwamba kwa kuwapinga Waahmadiyya Masheikh wakubwa wakubwa wanakuja na wanasema uongo bila kusita; lakini kila shahidi Mwahmadiyya anasema jambo lile tu analojua kwa yakini na anachukia sana kusema uongo. Baba alichunguza kwa makini sana mwenendo wa Waahmadiyya na wasiokuwa Waahmadiyya, na akaathirika sana na ushahidi wa Waahmadiyya. Wakati fulani Hakimu alipomwuliza kwamba Bwana Chaudhari, je, u Mwahmadiyya? Hapo baba alisema sikuwa Mwahmadiyya, lakini sasa inaonekana nitalazimika kuwa Mwahmadiyya, na kwa kuthibitisha akaeleza matukio ya kesi. Akasema kwamba mtu ambaye wafuasi wake wanayo hali hii kwamba hawana cheo chochote cha kidini, lakini hata kuona hasara yao waziwazi hawakosi kusema ukweli, basi mtu ambaye wafuasi wake ni wa aina hii, hali yake mwenyewe itakuwaje!

Nilikuwa nikisema kwamba siku ile watu wengi walifanya baiati. Baada ya baiati, Hudhur[as] alitoa hotuba ya nasaha ambamo alieleza makusudio ya baiati.

Sialkot ni mji ambamo Hudhur[as] alikaa kikazi kwa miaka minne kuanzia mwaka 1864 hadi mwaka 1868, lakini katika zama zile watu wachache tu walijuana naye, na watu wengine hawakujua hata jina lake. Sasa Hudhur[as] alipoenda, alikuwa Mjumbe mwenye shani kubwa wa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, kabla alikuwa hajawasili, watu walijumuika kama vile kwa kupiga baragumu watu wanavyoamrishwa

kukusanyika. Na kwa kuona mandhari hiyo, mandhari ya Jhelum ikaja mbele ya macho.

KURUDI QADIAN, 3 NOVEMBA 1904

Tarehe 3 Novemba 1904 alipanga kurudi Qadian. Nje ya nyumba alimokaa Hudhur[as], watu walianza kujumuika kama kawaida tangu asubuhi. Kwa kutahadhari, Hudhur[as], alituma mapema akinamama waende stesheni pamoja na Hadhrat Mir Nasir Nawab. Jamaat ya Sialkot iliwapa wageni chakula kabla ya saa nne asubuhi. Karibu saa sita Hudhur[as] alishuka kutoka ghorofani. Halaiki kubwa ya watu walikuwa wamejumuika. Ingawa polisi walikuwa wanasimamia kwa juhudi sana, hata hivyo wakati mwingine wakashindwa. Kwa ajili ya gari la Hudhur[as], njia ilifanyika kwa taabu sana. Hudhur[as] alipowasili kwenye stesheni, watu walikuwa wamejazana ajabu. Kwa Hudhur[as] behewa moja la daraja ya pili ilikuwa imeteuliwa. Hudhur[as] pamoja na ahli zake walipanda behewa lile. Gari lilipoondoka, sauti ya ***Assalamu alaikum*** na ***Mungu awe mlinzi***, ilivuma stesheni nzima.

Ni tukio la stesheni hiyo kwamba gari lilipokwisha ondoka stesheni, baadhi ya wapinzani wakawa rabana kabisa upande mmoja wa stesheni, lakini haifai hapa kutoa maelezo yake. Kitendo hicho kilikuwa kinyume cha Islam bali kinyume cha ubinadamu, kiasi hiki hata kwamba gazeti 'Ahle Hadith' la wapinzani wa Jumuiya Ahmadiyya pia lililazimika kulalamika.[455]

MAZUNGUMZO NA PADRI MMOJA KWENYE STESHENI YA WAZIRABAD

Gari lilipofika Wazirabad, kwenye stesheni msongamano wa watu ulikuwa mkubwa zaidi kuliko awali. Hadhrat Hafidh Maulawii Ghulam Rasul Wazirabadi, kama awali, aliwahudumia ndugu zake kwa sharubati ya limau na soda. ***Mungu Ampatie ujira bora.***

Hapo mhubiri mmoja Mkristo wa Daska, Padri Scott, pia alionana na Hudhur[as]. Pamoja naye alikuwa Sheikh Abdul Hak, Mwislamu mpya,

[455] Gazeti "Ahle Hadithi", Amritsar la 11 Novemba 1904, sawa na Al-Hakam 17-24 Desemba 1904.

aliyekuwa Mkristo zamani. Bwana Padri akija tu akaanza kuongea na Hudhur[as] hivi kwamba umemchukua kijana wetu mmoja (Abdul Hak). Kisha alijaribu kufanya na Hudhur[as] mazungumzo ya kidini, lakini angewezaje kumkabili Hudhur[as]. Baada ya kuuliza mara chache na kujibiwa akaondoka.

Kwenye stesheni ya Wazirabad, ndani gari pia watu wengi walifanya baiati. Wakati wa kurudi, katika Lahore Dkt. Seyyid Muhammad Husain Shah aliwaletea Hudhur[as] na walio pamoja naye chakula cha jioni.

Usiku Hudhur[as] alikaa Batala. Asubuhi, Jumuiya ya Batala ilileta chai na chakula. Hatimaye karibu saa sita mchana, Hudhur[as] alifika Qadian pamoja na ahli na mahadimu. *Alhamdulillahi.*

"NGUVU MOJA YA MASHARIKI NA HALI YA HATARI YA KOREA," MWAKA 1904 TAKRIBAN

Nchi ya Korea ni peninsula inayotazamana na Japani. Mpaka 1904 hiyo ilikuwa chini ya ufalme wa China. Na ilikuwa nchi isiyojulikana hata kwamba wasomi wa kawaida pia hawakujua jina lake. Katika zama hizo Hudhur[as] alifunuliwa, "Nguvu moja ya Mashariki na hali ya hatari ya Korea". Ni dhahiri kwamba mtu asiyejua siasa ya kidunia aliyekaa katika kijiji kidogo cha Qadian ambacho hakiungani na mji wowote mkubwa, anadai kwamba Mwenyezi Mungu Ameniambia kwa ufunuo kwamba nguvu moja itazalika katika Mashariki ambayo itasababisha hali ya hatari ya Korea, ni ya kushangaza sana. Wanahistoria wanajua kwamba katika mwaka 1904 nguvu zote kubwa zilikuwa katika Magharibi tu; katika Mashariki haikuwepo nchi hata moja yenye nguvu. Baada ya ufunuo huo Japani ilianza kutambulika kuwa nguvu kubwa katika Mashariki. Wakati huo, hiyo ilikuwa nchi ndogo sana. Urusi ilitaka kuitwaa Korea kwa njia yoyote, lakini Japan iliona mauti yake kama Korea ikitekwa na Urusi. Hatimaye katika 1905 juu ya jambo hilo vita kali ilianza baina yao. Katika zama hizo vita kati ya Urusi na Japan ilikuwa ya kutaajabisha zaidi kuliko shindano baina ya ndovu na sisimizi, kwani Japani ilikuwa si chochote mbele ya Urusi. Lakini kwa vyovyote kauli ya Mwenyezi Mungu ilitakiwa kutimia. Katika vita hiyo, Urusi ilipata

kushindwa vibaya sana juu ya kuwa na nguvu kubwa ya vita na vifaa dhidi ya Japani. Armada yake yenye fahari ilizama katika bahari ya Japan. Na kwa kukubaliwa mamlaka ya Japan juu ya Korea, utabiri wa Hudhur[as] "Nguvu moja ya Mashariki na hali ya hatari ya Korea" ulitimia kwa shani kubwa.

VITABU VYA MWAKA 1904

Kwa vile wakati mwingi wa mwaka 1904 ulipita katika safari kwa sababu ya shughuli za kesi ya Maulawii Karmuddin, kwa hiyo mwaka huo kazi ya kuandika vitabu haikufanyika. Lakini kwa sababu ya safari hizo Hudhur[as] alipata nafasi nzuri ya malezi ya wanajumuiya. Masimulizi wanayoeleza masahaba wa Hudhur[as] kuhusu muda huo ni mengi kuliko masimulizi kuhusu zama zingine. Hata hivyo, hotuba mbili adhimu za Hudhur[as] ziitwazo "Hotuba ya Lahore" na Hotuba ya Sialkot" zilichapishwa katika mwaka huo.

ZILIZALA YA KANGRA, 4 APRILI 1905

Mwaka 1905 ulianzia na ushindi wa kesi ile aliyofungua Maulawii Karmuddin dhidi ya Hudhur[as]. Kesi hiyo imeshaelezwa hapo awali. Kwa fadhili na rehema ya Mwenyezi Mungu aliachiliwa Hudhur[as] kwa heshima sawa na utabiri wake, na Hakimu wa tarafa alitoa maoni makali dhidi ya Karmuddin. Kwani Maulawii Karmuddin alisisitiza jambo lile mara kwa mara kwamba Bwana Mirza ameniita ***Kadhabu,*** ilihali ***kadhabu,*** ni yule ambaye ni mwongo sana na mara kwa mara uongo wake umeishathibitika. Kwa hiyo, Hakimu wa tarafa aliandika katika uamuzi wake:

> "Sawa na maoni yetu matumizi ya maneno hayo makali yalikuwa barabara, hata kama yangekuwa makali zaidi kiasi fulani pia hatungemsaidia mshtaki."[456]

Baada ya uamuzi huo, sawa na utabiri wake, mwaka huo ishara kubwa iliyodhihirika ilikuwa zilizala katika maeneo ya Kangra iliyotokea tarehe 4 Aprili 1905 katika India kaskazini. Mwaka mmoja kabla ya tetemeko hilo Hudhur[as] alikuwa amechapisha ufunuo wake huu:

[456] Al-Hakam, J. 8, Na. 18 mwaka 1904

عَفَتِ الدِّيَارُ مَحَلُّهَا وَمُقَامُهَا

"Yaani karibuni maangamizi yatatokea ambayo kwayo makazi ya muda na makazi ya kudumu yatafutika."

Baadaye, siku za matetemeko yaliyoahidiwa zilipokaribia, alichapisha tangazo moja lenye kichwa cha habari "Al-Wasia" ambamo aliandika:

"Sasa naona kwamba wakati ule umekaribia. Wakati huu baada ya usiku wa manane, saa kumi, nimeona kashfi kwamba kuna makelele mengi ajabu kwa sababu ya vifo vinavyotia uchungu moyoni, nami natamka mdomoni mwangu ufunuo huu: '*Mauta mauti lag rahi hai*' — vifo vingi vinatokea. Hapo nikazinduka. Wakati huu, sehemu ya usiku imebaki kidogo nami nimeanza kuandika tangazo hili. Ndugu, amkeni na zindukeni kwani wakati umewadia wa msiba mkubwa kwa kizazi cha zama hizi. Sasa kwa kuvuka mto huu, hakuna safina yoyote isipokuwa uchamungu tu."[457]

Baadaye, tarehe 4 Aprili 1905 likatokea tetemeko lile la kuogofya ambalo likaleta mfano wa kiyama mbele ya dunia.

HUDHUR[AS] ALIKAA KATIKA BUSTANI, APRILI HADI JUNI 1905

Kwa vile alikuwa anafunuliwa mara kwa mara kuhusu matetemeko ya ardhi, kwa hiyo mara baada ya tetemeko la 4 Aprili 1905, siku hiyo hiyo aliamuru kwamba kwa muda kidogo ndugu wakae katika bustani ya Hudhur[as] inayoungana na *Bahishti Makbara*. Amri hiyo ya Hudhur[as] ikatekelezwa mara moja. Katika bustani hiyo kijiji kidogo kikapatikana. Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin, Hadhrat Maulawii Abdul Karim na ndugu wengine walianza kuishi katika bustani. Afisi za magazeti na Anjuman pia zilihamishwa bustanini, na kwa miezi mitatu mfululizo yeye pamoja na wanajumuiya alikaa katika bustani hiyo, na tarehe 2 Julai 1905 walirudi nyumbani kwao. Baadaye pia

[457] Kutoka katika tangazo la "Al-Wasia", lililoandikwa kati ya usiku wa 26-27 Februari 1905, lililoandikwa katika Tablighe Risalat, J. 10.

kwa njia ya matangazo "Mwito", "Onyo", "Mwito wa wahyi kutoka mbinguni" na "Habari za matetemeko mara ya tatu", aliwasihi watu kwamba wakiacha maovu washikilie njia za wema na uchamungu, kwani kwa kujiepusha na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu hiyo tu ni njia moja.

Watu walikasirika pia juu ya matangazo hayo yaliyojaa na huruma pia. Basi, *Paisa Akhbar* na baadhi ya watu wengine walipinga kwamba kwa kuchapisha habari za kutokea matetemeko watu wanahofishwa bure. Na wakaielekeza serikali pia kwamba habari za kutishia za namna hii zizuiliwe kuenezwa.

TANGAZO LA OMBI MUHIMU KWA KUZINGATIWA NA SERIKALI

Kwa kujibu shutuma za aina hiyo, Hudhur[as] alichapisha tarehe 11 Mei 1905 tangazo moja lenye kichwa cha habari "Ombi muhimu kwa kuzingatiwa na serikali", ambamo aliandika:

> "Zama hizi ni za ajabu kwamba hata huruma pia haishukuriwi. Baadhi ya wenye gazeti hasa wa *Paisa Akhbar* Lahore, amekasirika sana kwamba kwa nini nimechapisha habari za tetemeko la pili, ilihali anajua vizuri kwamba niliyochapisha hiyo si kwa nia mbaya, wala sikukusudia kumwudhi yeyote wala sikusudii kutia wasiwasini."[458]

Mwishoni mwa tangazo hilo, Hudhur[as] aliandika:

> "Baadhi yao wasiofahamu wanasema kwamba matangazo hayo yameandikwa kwa lengo hili kuwa watu wakiogopa wakubali kufanya baiati yake. Lakini nijibu nini kwa kuficha kwao haki. Nimeshaandika mara kwa mara katika matangazo hayo kwamba hapo kwa kujirekebisha na kutubu simaanishi kwamba Baniani au Mkristo yeyote asilimu au afanye baiati yangu. Bali ikumbukwe kwamba kama dini ya mtu si sahihi, basi kwa adhabu ya kosa hilo dunia hii si mahali pa kuhukumu, kwa ajili yake yamewekwa maisha ya ahera. Na mataifa yaliyoadhibiwa

[458] Tablighe Risalat, J. 10

kabla yake, kwa mfano walipigwa mawe kutoka mbinguni au waligharikishwa kwa tufani au waliangamizwa kwa zilizala, sababu yake haikukuwa kwamba hao walikuwa waabudu masanamu au wenye kuabudu moto au waabudu wa kiumbe kingine. Kama wangeshikilia makosa yao kwa kutojua na kwa wema, basi wasingeshukiwa adhabu. Lakini hawakufanya hivyo, bali walifanya madhambi makubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na kuonyesha ujeuri sana na kwa maovu yao ardhi ilichafuka, kwa hiyo adhabu iliwashukia katika dunia hii hii. Mungu ndiye Mkarimu na Mrehemevu na Mpole katika ghadhabu. Kama watu wa zama hizi wamche na wasijasiri kutenda maovu na mabaya na matendo mabaya ya aina aina, basi adhabu yoyote haitawashukia."[459]

UJAJI KATIKA QADIAN WA BWANA ABUN-NASR MAULANA GHULAM YASIN AAH, NDUGUYE MAULANA ABUL KALAM AZAD, APRILI 1905

Siku hizo ambapo Hudhur[as] alikaa bustanini mwake, Bwana Abun Nasr, nduguye Maulana Abul Kalam Azad, alikuja Qadian. Athari alizopata moyoni mwake alizichapisha katika gazeti "Wakil" la Amritsar. Anaandika:

"Niliona nini tena. Niliona Qadian, nilionana na Bwana Mirza, nilikuwa mgeni wake. Yanipasa nimshukuru Bwana Mirza kwa hulka yake na kunishughulikia. Nilipatwa na malengelenge kinywani mwangu kwa joto, kwa hiyo sikuweza kula chakula kikali, kwa hiyo Bwana Mirza (alipotoka nyumbani mwake mara moja) akanifanyia mpango wa maziwa na mkate.

Siku hizi Bwana Mirza anakaa nje ya Qadian katika bustani kubwa inayofaa (anayomiliki mwenyewe), wazee wa dini pia wapo hapo hapo. Wakazi wa Qadian ni watu karibu elfu tatu, lakini mazingira ni mazuri ya uchangamfu na shughuli nyingi. Katika kijiji kizima kuna jengo kubwa moja tu... njia si za lami wala si sawasawa hasa barabara ya Batala hadi Qadian ni mbaya zaidi kuliko zote. Wakati wa kuja kwa gari la farasi taabu

[459] Tablighe Risalat, J. 10

niliyopata ikawa nusu wakati wa kurudi kwa gari la farasi lenye magurudumu manne la Bwana Nawab. Kama nisingekuwa na shauku moyoni mwangu kumwona Bwana Mirza nisingeweza pengine kwenda hata hatua nane, achilia mbali maili nane.

Sifa ya kuwakirimu wageni haikuwa kwa watu maalum tu; kuanzia mdogo mpaka mkubwa kila mmoja alinitendea kama ndugu, kadhalika na Maulana Haji Hakim Nuruddin ambaye jina lake lenye heshima linatambulika katika India nzima na Maulana Abdul Karim ambaye hotuba yake ina umashahuri katika Panjab na Maulawii Mufti Muhammad Sadik, Mhariri wa Badr ambaye kwa makala zake Wazungu wengi katika Ulaya wameshasilimu.

Sura ya Bwana Mirza ni yenye shani sana inayoathari mno. Machoni mwake mna mng'ao na hali ya aina mahususi na mazungumzo yake ni laini sana. Ana tabia ya unyenyekevu lakini yenye kutawala, yu mpole lakini huhamasisha mioyo, shani ya uvumilivu imesawazisha hali ya unyenyekevu. Daima anaongea kwa upole sana hata inaonekana kana kwamba anatabasamu. Yu mweupe, anazipaka nywele zake rangi ya hina, ana mwili madhubuti na wenye kufanya kazi kwa bidii. Kichwani anafunga kilemba cha Kipanjabi, miguuni anavaa soksi na viatu vya kienyeji. Umri wake ni miaka 66 takriban. Nimeona imani kubwa katika wafuasi wa Bwana Mirza na wanafurahia itikadi yao. Nilipokuwepo hapo, wageni waheshimiwa wengi walikuja waliokuwa na mapenzi ya hali ya juu na wenye imani sana. Huu ni mfano mdogo wa hulka kubwa za Bwana Mirza kwamba siku za kukaa kwake baada ya kunikirimu mfululizo, nilipoomba ruhusa ya kuondoka akanena: "Tutakuruhusu kwa ahadi hii kwamba uje tena na ukae kwetu angalao kwa wiki mbili." (Uso uliojaa tabasamu wa wakati ule bado upo machoni mwangu). Kwa shauku niliyoenda, nimerudi nayo; na shauku hiyo hiyo pengine itanipeleka tena. Kwa kweli

Qadian imeelewa vizuri kauli hii: وَحَسِّنْ خُلُقَكَ وَلَوْ مَعَ الْكُفَّارِ[460]

MATANGAZO MENGINE KUHUSU MATETEMEKO YA ARDHI

Ingawa matukio ya 1905 yanaendelea kuelezwa, lakini kwa kufululizisha bishara zihusuzo matetemeko, yanatajwa hapa hapa matangazo ya miaka ijayo. Tarehe 20 Desemba 1905, Hudhur[as] alichapisha wasia wake na humo pia alitaja utabiri wa tetemeko na akaeleza ufunuo wake mpya pia "Majira ya kuchipua yakaja tena na usemi wa Mungu ukatimia tena." Na Hudhur[as] alibainisha majira ya kuchipua ni kuanzia mwisho wa Januari hadi mwisho wa Mei.[461] Basi, sawa nayo, tarehe 28 Februari 1906, saa saba na dakika ishirini ya usiku, likatokea tetemeko kali la ardhi, ambalo chanzo chake kilikuwa milima ya Simla. Zilizala hiyo iliharibu sana sehemu za Panjab mashariki. *Paisa Akhbar* Lahore liliandika kwamba watu wote wa kijiji Dadupur, tarafa ya Jagadhari, wilaya ya Ambala, walikufa wakilala, watu watatu tu walisalimika. Katika Tira, wilaya ya Saharanpur, kisima kikavu kilijaa maji. Hudhur[as] na wafuasi wake walifikiri kwanza kwamba tetemeko kubwa lililotabiriwa ni hilo tu, lakini haraka sana ufunuo wa Mungu uliiondoa dhana hiyo na kaeleza kwamba zilizala iliyoahidiwa iliyoitwa mfano wa kiyama itatokea baadaye.

TANGAZO LA UTABIRI WA TETEMEKO LA ARDHI

Tarehe 2 Machi 1906, Hudhur[as] alichapisha tangazo moja lenye kichwa cha habari "Utabiri wa Tetemeko la Ardhi" ambamo akieleza habari hiyo akaandika beti hizi:

> Marafiki, zindukeni, kwani zilizala iko karibu tena kutokea. Mungu Yu karibu kudhihirisha kudura yake haraka sana.
>
> Lile tetemeko mliloshuhudia mnamo mwezi Februari, hilo ─ mjue kwa yakini ─ lilikuwa ni onyo tu kuwafahamisha.

---

[460] Tafsiri: Onyesha hulka bora hata kwa makafiri.

Tanbihi: Nimepata habari kutoka kwa wanaoelewa kuwa Maulana Abun Nasr alifanya baiati pia. Badr, 25 Mei 1905.

[461] Al Wasiyyat, uk. 15

Itibuni kwa machozi ya jicho, maana mbingu iko tayari kushusha moto, Enyi mlioghafilika.

"Enyi wapendwa, pengine mliona tetemeko lile lililotokea usiku wa tarehe 28 Februari 1906, baada ya saa saba, lilikuwa tetemeko lile lile liliotajwa katika wahyi wa Mwenyezi Mungu "Majira ya kuchipua yakaja tena, na usemi wa Mungu ukatimia tena." Nami nilichapisha utabiri huo kwenye kurasa 3, 4, 14 za kijitabu Al-Wasia, vilevile katika matangazo yangu na gazeti Al-Hakam na Badr. Basi sifa njema ni za Mungu na hisani yake kwamba sawa nao tetemeko hilo likatokea katika siku za majira ya kuchanua. Lakini leo, tarehe mosi Machi 1906, wakati wa asubuhi tena Mungu Aliniteremshia wahyi ambao maneno yake ni haya: Tetemeko linakaribia kutokea." Na ilitiliwa moyoni mwangu kwamba tetemeko lile lilio mfano wa kiyama halijatokea bado, bali lakurubia kutokea. Na tetemeko hili lililotokea sawa na utabiri ni utangulizi wa tetemeko lile."

Baadaye, Hudhur[as] alikamilisha shairi lake hili katika kitabu chake "Chemchemu ya Ukristo" kwa kuongeza beti zingine pamoja na beti zilizotajwa juu.

UTABIRI WA VITA KUU, APRILI 1905

Siku hizo, Hudhur[as] alikuwa akiandika kitabu chake mashahuri "Barahine Ahmadiyya, sehemu ya 5". Katika kitabu hicho Hudhur[as] ametoa maelezo kiasi fulani katika shairi la Kiurdu, na katika maelezo ya pembeni, ya shairi hilo ameandika:

"Katika wahyi wa Mwenyezi Mungu neno 'zilizala' lipo mara kwa mara, na Akasema kwamba tetemeko litatokea litakalokuwa mfano wa kiyama, bali lapaswa kuliita tetemeko la kiyama ambalo kwalo inaashiria sura إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا . Lakini bado siwezi kuchukulia neno la tetemeko kidhahiri kwa yakini. Inayumkinika kwamba lisiwe tetemeko la kawaida, bali uwe msiba mwingine mkali uonyeshao onyesho la kiyama, ambao mfano wake hazijauona kamwe zama hizi, na ulete maangamio makali kwa watu na majengo. Naam, kama isidhihirike ishara

isiyo ya kawaida, na watu pia wasijirekebishe waziwazi, hapo nitakuwa mwongo. Lakini nimeshaandika mara kwa mara kwamba msiba ule mkali ambao Mwenyezi Mungu Aliuita kuwa tetemeko, hautamwathiri yeyote kwa sababu ya hitilafu ya dini, wala mtu hawezi kuadhibiwa kwa kuwa yu Baniani au Mkristo, wala hawezi kuadhibiwa kwa kutoingia katika baiati yangu. Watu hao wote wapo salama wasiwe na wasiwasi. Basi, mtu hata kama ni mfuasi wa dini yoyote aliye na tabia ya uhalifu na amezama katika ufasiki na maovu, ni mzinifu, mwuaji, mwizi, mdhalimu, mwenye nia mbaya pasipo haki, mwenye mdomo mchafu na mwendo mbaya, huyo anapaswa kuuogopa. Na akitubu, basi huyo naye hana huzuni yoyote, na yaweza pia adhabu hiyo kuondoka kwa sababu ya mienendo myema ya watu."[462]

Shairi lililotajwa juu lina beti 456 ambamo ameeleza kinaganaga kwa ufasaha sana madai yake, hoja zake, hali ya wapinzani na mwisho wao. Na mwishowe ametoa picha ya zilizala kwa beti zifuatazo:

Kule mbinguni kuna makelele, lakini ninyi hamna habari. Mchana ulikuwa mwangavu, lakini vumbi na ghubari limezidi.

Yaja ishara moja baada ya siku chache tangu leo, itakayosababisha vijiji, miji na machungani kufujika.

Yatatokea mapinduzi kwa mahuluku kwa ghadhabu ya Mungu, hata kwamba aliye rabana hatawahi kufunga mkanda wa suruali.

Ghafula watatetemeka vikali kwa zilizala wanadamu, miti, mawe na bahari.

Ardhi itapinduka chini juu kwa kupepesa macho; damu itatiririka miferejini kama maji mtoni.

Waliojivalia usiku mavazi ya rangi ya yasmini, asubuhi itayafanya mithili ya mipopla.

Binadamu atapigwa na bumbuazi, ndege watafadhaika. Njiwa

[462] Barahine Ahmadiyya, sehemu ya 5, uk. 120

na vinega wote watapitiwa kuimba.

Saa ile itakuwa ngumu kwa kila msafiri. Watapotea njia mafarasi waendao dalji wakiwa kama wamelewa.

Maji yapitayo ya mlimani yatakuwa mekundu kwa damu za maiti kama mvinyo ya ***mbistoti***[463].

Majini na wanadamu wataishiwa nguvu kwa hofu, hata akiwa mfalme Tzar (matamshi Zaar), huyo naye atakuwa na hali mbaya sana saa ile.

Ishara ile itakuwa ni mfano wa ghadhabu ya Mungu. Mbingu itafanya mashambulizi kwa kuchomoa hanjari yake.

Naam, usiharakie kukataa, Ewe mjinga usiyeelewa, kwani ukweli wangu unaitegemea hiyo kikamilifu.

Hii ndiyo habari ya wahyi wa Mungu itakayotokea isiyoweza kukosa. Subiri kwa siku chache ukiwa mcha Mungu na mvumilivu.

Usidhani kuwa dhana yako hii mbaya imesamehewa; ni deni hili, utarudishiwa deni hili lote kikamilifu.

Inaonekana kwamba katika kashfi Hudhur[as] alionyeshwa hali ya vita kuu. Basi, kuanzia 1914 hadi 1918 vita kuu iliyoendelea, maelezo yake mengi yametolewa katika beti hizo, hata Tzar wa Urusi aliyekubaliwa kuwa mfalme mkubwa wa dunia kuliko wote, hali yake mbaya pia imeelezwa kwa maneno wazi na dhahiri. Leo kila mtoto anajua kwamba katika vita kuu ya kwanza, mfalme mkubwa wa dunia na mwenye mamlaka zaidi kuliko wote, ambaye kuleta mfano wake historia ya Ulaya ilishindwa, ambaye alikuwa na heshima na nguvu kiasi hiki kwamba wafalme wakubwa wakubwa walikuwa wanapenda awaangalie kwa rehema; naam, mfalme aliyekuwa na nguvu na shani aliyejiita Tzar yaani yule asiyekubali utawala wa yeyote na anayewatawala wote, alilazimika tarehe 15 Machi 1917, saa tano na

[463] Mbistoti — kwa Kiingereza Bistort — ni mmea unaotumika kutengeneza dawa mbalimbali. Mfasiri

robo za mchana, kuandika kwa mkono wake kwamba yeye na kizazi chake wanaacha utawala wa Urusi. Wakati wa kutangaza kuacha utawala, Nicholas wa Pili (Tzar wa Urusi) alidhani kwamba hatanyang'anywa mali yake mwenyewe iliyokuwa Rupia mamilioni, na ataishi maisha yaliyobaki kwa kutegemea mali hiyo kwa amani bila tatizo lolote, lakini hakujua kwamba kwa kudura ya Mungu atapata mateso kiasi gani kwa kulipia dhuluma aliyofanya. Tarehe 15 Machi 1917 alijizulu utawala, na tarehe 21 Machi akafungwa na akapelekwa "Tsarsaoye Selo" ambapo alifungwa katika Jumba la Kifalme. Ingawaje hiyo pia ilikuwa adhabu kubwa kwa mfalme dikteta na ilikuwa ni uthibitisho wa kutosha ya kuwa na "hali mbaya" yake, lakini katika elimu ya Mungu taabu zingine zilikadiriwa kwake. Bado utawala wa Urusi ulikuwa mkononi mwa mtu mwanamfalme Lvov ambaye kwa sababu yake. Tzar alikuwa akatendewa vizuri katika jela. Lakini, katika Julai mwanamfalme huyo pia akalazimika kuondolewa na Bwana Kerensky alishikilia utawala ambaye hakuwa na huruma kwa Tzar wa Urusi. Hata hivyo, katika zama zake pia shida za Tzar wa Urusi hazikupita mipaka ya ubinadamu. Lakini tarehe 7 Novemba uasi wa Bolshevik ulimaliza utawala wa Kerensky. Sasa kipindi cha kutisha kilianzia kwa Tzar hata mtu wa moyo mgumu pia anatetemeka akisikia hali hiyo. Tzar akitolewa katika jumba la kifalme la 'Tsarsaoye Selo' aliwekwa katika sehemu mbalimbali. Kwa muda fulani akalazimika kukaa chumba kidogo kichafu chenye giza ambamo mlikuwa na matundu ya panya, viota vya shorewanda na tando za buibui. Baadaye alitumwa Ekaterinburg ulio mji mdogo upande wa mashariki ya mlima Ural. Hapo alifungwa katika nyumba yenye vyumba viwili vibovu. Na alikuwa akipewa mara mbili chapati ya unga mweusi iliyopikwa siku moja kabla na supu nzito ya mboga. Walikuwa na ruhusa kwa dakika tano tu katika masaa 24, ya kutembea katika bustani iliyoungana na nyumba ile. Mapolisi wachungaji walikuwa wakidhulumu sana familia ya kifalme. Siku moja askari mmoja dhalimu alinyang'anya pochi ya Tzarina —mkewe Tzar — akachukua fedha zote akisema kwamba "sasa huna haja ya fedha." Mabinti zake wakazomewa, wakatukanwa vibaya sana. Hatimaye, siku moja wasichana wa Tzarina walibakwa mbele ya macho yake.

Tarehe 16 Julai, katika kiza totoro la usiku, kamanda mmoja aliyefunika uso aliingia nyumbani. Akiamsha familia ya kifalme alisema kwa sauti kubwa kwamba mjini imetokea fujo sana na watu wanawajieni kwa kishindo ili kuwaueni. Kwa hiyo jivalieni haraka nguo na jificheni katika sela. Kutoka humo mtapelekwa haraka kwenye mahali pa usalama. Kwa kusikia maneno hayo ya kamanda, wote walitetemeka kwa hofu. Kwa Tzarina ikawa vigumu hata kusimama. Kwa taabu alishuka chini, alikalishwa juu ya kiti kilichokuwa kimevunjika. Waliposhuka tu chini, polisi waasi waliingilia sela na kuwaambia kwa kitisho:

> "Wenye kuwahamini wamejaribu sana kuwalindeni, lakini hawakuweza kufaulu. Sasa muwe tayari kufa."

Baada yake, mara askari mmoja alifyatua risasi iliyopasua ini la mfalme na kutoka nje upande wa pili. Tzar akianguka tu, risasi zilianzia kufyatuliwa mfululizo. Tzarina na mabinti zake wakilia wakajificha, kila mmoja nyuma ya mwingine, wakijiaribu kujiokoa, lakini maaskari wakiwapiga singe vifuani mwao wakanyamazisha makelele yao. Baada ya kufurukuta walipokufa, mbwa moja jike akaja baina ya maiti kumtafuta binti mdogo aliyemmiliki, mara askari mmoja akamdunga singe. Baadaye, maaskari walikata maiti zile vipande vipande na wakazimwagia kerosini na kuzichoma moto. Hivi kauli ya Nabii wa Mwenyezi Mungu ikatimia:

> "Hata akiwa mfalme Tzar, huyo naye atakuwa na hali mbaya sana."

MAANA YA TETEMEKO LILILOAHIDIWA

Kwa hali za Tzar, ikathibitika kwamba vita kuu ya kwanza bila shaka ilikuwa sehemu ya tetemeko lililoahidiwa. Na haya aliyoambiwa Hudhur[as] kwamba, "Nitaonyesha mng'ao wa ishara hii mara tano" muradi wake ni vita au yaweza kuwa zilizala pia, Mwenyezi Mungu Anayo elimu yake, lakini tuna imani imara kwamba kwa dunia yamekadiriwa maangamio makali mara tano, ambayo mfano wake hautapatikana katika historia iliyopita hata kwa kutafuta. Watu ambao

wameona zilizala za Behar na Quetta au wamesoma habari zake katika magazeti, bila shaka maonyesho hayo ya kutisha hayawezi kutoka machoni mwao katika maisha mazima. Siku za kutokea zilizala ya Quetta, nilikuwa Karachi. Zilikuwa siku za likizo ya kiangazi. Watu wengi wa Quetta walikufa, baadhi yao waliojeruhiwa waliobaki waliletwa Karachi. Kuwatazama kulitisha, ilikuwa vigumu kuwaona. Baadhi yao walikatika mikono, mwingine alijeruhiwa mgongoni, mwingine aliungua usoni. Ilmuradi, hali ya watu wengi ilikuwa mbaya sana isiyosemeka. Baadhi ya wanawake na watoto wakaja wakisalimika pia lakini wakalia sana wakisema kwamba jamaa yetu yeyote hakubaki, wote wamefariki katika zilizala. Bila shaka mandhari hayo yalikuwa ya kutia uchungu kiasi hiki kwamba ninapoyawaza hata sasa, mandhari ya kiyama yanakuja mbele ya macho.

WAKATI WA ZILIZALA KUBWA UMEAHIRISHWA

Zilizila iliyoahidiwa au zilizala kubwa ilipangwa kutokea katika uhai wa Hudhur[as], lakini kwa sababu ya maangamizo yake yaliyotazamiwa, Hudhur[as] aliomba dua kwamba zilizala hiyo isitokee katika uhai wake. Hudhur[as] anasema:

رَبِّ اَخِّرْ وَقْتَ هٰذَا, yaani, Ee Mungu wangu, zilizila inayokaribia Uahirishe kadiri fulani wakati wake."[464]

Kisha, siku ya pili, alifunuliwa: اَخَّرَهُ اللّٰهُ اِلٰى وَقْتٍ مُسَمًّى, yaani, Mwenyezi Mungu Ameiahirisha kwa muda maalumu. Kasema: zilizala ndogo ndogo zinatokea tu, lakini zilizala kali itakayotokea, wakati wake umeahirishwa, lakini haiwezi kusemwa kwamba taahiria ni kiasi gani."[465]

Hudhur[as] alifariki katika mwaka 1908 na zilizala kubwa ile ilianzia mara ya kwanza mnamo mwaka 1914 kwa sura ya vita kuu, na dunia ilishuhudia maangamizo yake kwa miaka minne mfululizo. Mataifa yaliyopigana yalipochoka kupigana, basi kwa muda fulani yakijitenga na vita yakashughulikia maandalizi mapya na kuvumbua silaha zenye

[464] Ufunuo wa 27 Machi 1906, uliopo katika Tadhkirah, uk.598-599

[465] Ufunuo wa 28 Machi 1906, uliopo katika Tadhkirah, uk. 599

kuangamiza. Basi katika mwaka 1939 yalipigana mara ya pili. Katika mwaka 1945 vita hiyo pia iliisha kwa muda. Na baada yake uvumbuzi wa kisanyasi uliendelea mbele sana hata kwamba kama si takdiri ya Mwenyezi Mungu kubakiza dunia hii, basi dunia inaweza kuangamizwa katika muda mfupi sana. Lakini, twajua kwamba Mwenyezi Mungu Anataka kuleta mabadiliko mapya duniani, na Anataka kwa kumpitia Masihi Mtukufu kumwagilia maji dini iliyoletwa na mpendwa wake Mtume Muhammad[saw]. Kwa hiyo dunia haitaisha kamwe. Naam, mabadiliko makubwa yatatokea ambayo kwa matokeo yake mataifa makubwa yote ya dunia yatakanyagiliwa mbali na kisha Islam itapokelewa duniani, Inshaallah. Ee Mungu, Ulete haraka siku zile ambapo nguvu za kishetani zikiinamisha kichwa mbele ya nguvu za Kirahmani zitakubali ufalme wa kimbingu. *Allahumma amin.*

UTABIRI WA ZILIZALA KISHAIRI

Kwa kueneza baina ya watu wote utabiri wa zilizala, Hudhur[as] alichapisha shairi moja katika gazeti la *Paisa Akhbar* la 31 Machi 1906, ambalo ubeti wake wa kwanza ni huu:

> Marafiki, tena zinakurubia siku za kutokea zilizala. Zilizala i nini? Ndiyo siku za kuondoka dunia hii.

UFUNUO "AAH, NADIR SHAH KAENDA WAPI", 3 MAI 1905

Kwa sababu ya kutaja matabiri ya zilizala kubwa pamoja, haikuweza kufululiza matukio kihistoria, kwa hiyo twaeleza sasa matukio yaliyobakia ya mwaka 1905.

Mwishoni mwa mwaka 1905, Hudhur[as] alichapisha wasia mmoja kwa Jumuiya ambamo alieleza kifo chake kukaribia. Twaona duniani kwamba kikawaida mtu anapofanya wasia, basi sawa na hali zake anawaachia warithi wake baadhi ya maandishi muhimu. Kwa vile Hudhur[as] alikuwa mjumbe kwa zama hizi, kwa hiyo akipata elimu kutoka kwa Mungu, Mjuzi wa ghaibu, alitangaza habari ambamo yalitajwa mabadiliko makubwa yatakayotokea. Na Hudhur[as] aliambiwa habari hizo ili kwa kuwaelekeza watu wa kila nchi kwenye ukweli wake, utabiri utolewe kuhusu nchi yao wenyewe. Utabiri

tunaotaja hapa chini pia ni mmoja wa aina ya matabiri yenye kuleta mapinduzi. Hudhur[as] alifunuliwa: "Aah, Nadir Shah Kahaan Geya" ─ Hae, Nadir Shah kaenda wapi?

Tumeshaeleza katika matukio ya mwaka 1903 kwamba sawa na utabiri wa Hudhur[as] "Mbuzi wawili watakaochinjwa", Hadhrat Sahibzada Abdul Latif[ra] na kabla yake mwanafunzi wake Hadhrat Maulawii Abdur Rahman waliuawa katika Kabul pasipo haki, bila sababu yoyote. Utabiri huo ulipotimia, basi kwa sababu ya dhuluma hiyo Afghanistan ilishikwa na kipindupindu kikali. Matokeo yake, maelfu ya wakazi wa hapo walikufa, ndipo Mwenyezi Mungu Alimwarifu Hudhur[as] tena kwa ufunuo kwamba

"Mbuzi watatu watachinjwa."[466]

Ufunuo huo ulitimia katika mwaka 1924 ambapo Amir Amanullah Khan, Mfalme wa mwisho wa familia ya kifalme, alikuwa akitawala Kabul. Katika zama zake Hadhrat Maulawii Ni'matullah Khan,[467] mbashiri wa Jumuiya Ahmadiyya, aliuawa kwa kupigwa mawe kwa sababu ya chuki ya dini tu. Kisha baada ya wiki chache, Hadhrat Maulawii Abdul Halim na Hadhrat Mulla Nur Ali[468] waliuawa kwa 'kosa' hilo.

Baada ya matukio hayo ya kuhuzunisha, Mwenyezi Mungu hakupenda kwamba utawala wa nchi ya Afghanistan ubaki mkononi mwa familia hiyo iliyowaua Waahmadiyya wasio na hatia. Basi, kwa kuangamiza familia hiyo, Akamwinua sio mfalme mkubwa au mtu aliye sawa naye, bali mtu wa kawaida sana aitwaye Habibullah, aliyejulikana kwa jina Bachcha Sakka, ili kuiangamiza. Yeye kwa kundi dogo sana la watu wasiozidi 300, alimshinda vibaya Mfalme Amanullah Khan aliyekuwa na jeshi lenye mizinga na baruti, hata kwamba akalazimika kukimbia nchi yake.

---

[466] Ufunuo wa 1 Januari 1906, Tadhkirah.

[467] Maulawii Ni'matullah Khan aliuawa tarehe 31 Agosti 1924 kwa kupigwa mawe. (Al-Fadhl, 4 Septemba 1924)

[468] Maulawii Abdul Halim na Qari Mulla Nur Ali waliuawa 12 Februari 1925, Tadhkirah, uk. 582, maelezo ya pembeni.

Utabiri ulioandikwa katika kichwa cha habari, ulitimia hivi kwamba Bachcha Sakka alipomwasi Jenerali Nadir Khan aliyeenda Ulaya mnamo mwaka 1923 kwa sababu fulani, na siku zile alikuwa mgonjwa huko Ufaransa, hakuweza kuvumilia maangamizi ya Afghanistan na katika hali ya kuugua akaondoka kwa nia ya kuelekea Kabul. Kupitia Bombay na Panjab alifika Peshawar. Lakini, alipofika tu Peshawar akaugua vikali sana. Kwa vile Mungu Alipanga hivi kwamba kabla ya Nadir Khan kufika, Amiri Amanullah Khan aondoke Kabul, kwa hiyo kabla ya Nadir Khan kupona na kuelekea Kabul, Amiri Amanullah Khan alikimbia Kabul. Hatimaye, tarehe 9 Machi 1929 Nadir Khan aliingia katika Afghanistan akiwa hohehahe hata kwamba alitaka kuanzisha kiwanda cha uchapaji kwa kuwaarifu wananchi hali sahihi za nchi, lakini hakuwa na uwezo wa kununua matbaa. Na kwa kutimiza lengo hilo alinunua mtambo wa *Stylo,* kitu cha kawaida cha rupia 40-50. Katika hali hiyo, kushindana na adui kama Bachcha Sakka aliyemshinda Mfalme kama Amanullah Khan na kushikilia utawala wa Kabul... ilikuwa si kazi ndogo. Lakini kwa vile Mwenyezi Mungu Alitaka kuonyesha ishara hiyo, kwa hiyo yeye alimshinda Bachcha Sakka, juu ya kuwa na hali mbovu, afya mbaya na vurugu nchini. Na akataka kwamba Waafghanistan wajichagulie wenyewe mfalme wao yeyote miongoni mwao, lakini Waafghani walimchagua huyo huyo kuwa mfalme wao. Nadir Khan akishikilia tu utawala, alitangaza kinyume cha desturi ya zamani kwamba tangu sasa yeye asiitwe Nadir Khan au Shah Nadir Khan, bali aitwe Nadir Shah. Utabiri huo wa Hudhur[as] ulipotimia, gazeti la Jumuiya Ahmadiyya "Al-Fadhl" liliutaja wazi wazi. Hapo gazeti "Ahli-Hadithi" lilileta upinzani kwamba:

> "Je, katika Afghanistan huitwa Nadir Shah? Je, katika istilahi ya Afghanistan mfalme aliitwa Shah siku yoyote? Je, mtu yeyote alisikia lakabu za Abdur Rahman Shah au Habibullah Shah au Amanullah Shah? Huko lakabu ya Shah haitumiki kwa mfalme, bali tutasema kwamba katika India majina Abdur Rahman Shah au Habibullah Shah hayapatikani katika maandishi

> yanayotegemewa. Basi, kama ufunuo huo ungeeleza dhamiri ya Afghanistan, isingetumika lakabu ya Shah bali ingetumika lakabu ya Nadir Khan. Hivyo, yaonekana kwamba ufunuo wa Nadir Shah unahusikanan a tukio lingine kumhusu Amiri Nadir Khan."[469]

Lakini wasomaji watashangaa kusikiliza kwamba muda si muda Sardar Walii Khan nduguye Nadir Shah, akaja Lahore, na alimwambia Seyyid Habib, mmiliki wa gazeti "Siasat", kwamba:

> "Katika India, watu wanakosea kuandika jina la mheshimiwa, kwani siku aliyotangaza utawala wake, siku hiyo hiyo badala ya Khan akawa Shah. Sasa jina lake ni Nadir Shah, Mfalme wa Afghanistan."[470]

Neno la Mungu likatimia, lakini ufunuo huo ulipangwa kutimia kwa njia nyingine pia. Baada ya kutawala miaka minne kamili, tarehe 8 Novemba 1933, Nadir Shah katika jumba lake, ***Dilkushaa***, alikuwa akiwagawia wanafunzi zawadi za mashindano ya mchezo, mara mwanafunzi mmojawapo alimpiga mfululizo risasi tatu kutoka umbali wa yadi moja, na mara moja hafla ile ye furaha ikawa hafla ya huzuni. Watu wakipigwa na butaa walikimbilia penye maduka wakisema "Shah amefariki, Shah amefariki." Maaskari walibaki wakisimama. Mtu yeyote hakuweza kumlinda mfalme wake mpendwa na shambulio la mauti. Kwa mauti hayo yasiyotazamiwa na ya ghafla, nchi nzima ilihuzunika na mara nyingine tena watu wakasema kwa sauti moja:

"Hae Nadir Shah kaenda wapi."

Allah, Allah, mambo ya Mungu huwa ya ajabu namna gani! Miaka mingi kabla, habari moja yasemwa katika hali ambayo hata mtoaji utabiri pia hajui kwa yakini kwamba utabiri wangu huo utatimia kwa sura gani na lini. Katika mwaka 1905, Hudhur[as] alipotoa utabiri huo, Nadir Shah kama mfalme hakuwepo kabisa. Hatimaye, baada ya miaka 28 utabiri huo ulitimia kwa shani kubwa namna gani!

---

[469] Eik Taza Nishan ka Dhuhuur, uk. 20

[470] Gazeti "Siasat", 11 Septemba 1929

Nilikuwa nikisema kwamba kwa mauti ya ghafla ya Nadir Shah, nchi nzima ilihuzunika na kila mtu alitamka kwamba "Hae, Nadir Shah kaenda wapi."

TAFSIRI MBILI ZA UTABIRI

Kwa kweli katika mauti hayo ya ghafla pia ilipangwa kutimia maana ya pili ya utabiri. Na hatusemi hivi baada ya kutokea tukio hilo, bali habari hiyo iliandikwa wakati ule kwa idhini ya Hadhrat Imam wa Jumuiya Ahmadiyya katika gazeti la Jumuiya "AL-Fadhl", ambapo Nadir Shah alishikilia tu utawala. Na kwa sababu ya kupendwa kwake, na ufahamu wake na akili na busara yake alikuwa hawezi kudhaniwa kwamba maafa hayo yatatokea baada ya miaka minne tu. Al-Fadhl liliandika kwamba:

> "Katika maana ya pili, inaonekana kwamba aliyetajwa atapata msiba fulani mkali na itapatikana huzuni kubwa kwa hasara ile."[471]

Kwa maandishi hayo yadhihirika kwamba Jumuiya Ahmadiyya tangu mwanzo ilichukua maana mbili za utabiri huo. Wamchao Mungu wakitafakari, jambo hilo pia lina sababu ya kutosha kwa mwongozo wao. Kwa vyovyote, Mwenyezi Mungu Alikuwa na haja gani kwamba kwa njia ya mtu wa kawaida Bachcha Sakka, Apindue utawala wa mfalme mwenye nguvu Amanullah Khan. Je, hakuweza kufanya kazi hiyo kwa njia ya Nadir Khan? Kwa yakini, Angeweza. Lakini, Alitaka kwamba kwa familia hiyo na kwa dunia Alete sababu za ibra kwamba mtu anapopita mipaka katika dhuluma na hajali hata kuwaua watumishi wetu, basi twamdhalilisha hivyo.

Kwa kumdhalilisha Amanullah Khan, Mwenyezi Mungu Alipanga hivi kwamba kabla ya tukio hilo, Alimfanya aitembelee Ulaya yote. Na wafalme wakubwa wakubwa wa dunia waliendelea kuhudhuria kwa kumpokea, na karamu kubwa ziliandaliwa kwa kumheshimu. Na kwa safari yake pia kwa shani yote mipango ya kifalme ilipangwa. Heshima zote hizo alipewa ili atakapokimbia nchi yake akidhalilika sawa na utabiri wa Hudhur[as], tukio hili lisichukuliwe kuwa dogo.

[471] Al-Fadhl, 3 Januari 1930

Na ndivyo hivyo ilivyotokea. Alipokimbia, magazeti ya dunia nzima yaliandika makala makubwa, na yakachukulia tukio la kukimbia kwake akishindwa mbele ya mtu wa kawaida sana kuwa kubwa kabisa.

Sasa tazameni, kama Mwenyezi Mungu Angetaka, Amanullah Khan angeangamizwa katika vita hiyo, na hivyo kwa siku chache watu wangetaja matukio hayo na kisha wangesahau. Lakini, Mwenyezi Mungu, sawa na ufunuo wa Hudhur[as], لَا يَمُوْتُ فِيْهَا وَلَا يَحْيٰى , Alitaka kumbakiza hai na kumdhalilisha. Kwa hiyo, akawekewa takdiri kwamba aishi siku zilizobaki katika hali ya uhamishoni. Ni kurda ya Mungu kwamba siku za uhai wake zikarefuka, na mpaka leo hii anapitisha siku za maisha yake katika Italia kama mmiliki wa hoteli moja. Laiti wamchao Mungu wapate ibra katika tukio hilo.

MARADHI YA HADHRAT MAULAWII ABDUL KARIM SIALKOTI, AGOSTI 1905

Katika matukio ya 1905, tukio moja muhimu ni kifo cha Hadhrat Maulawii Abdul Karim Sialkoti, Mwanachuoni aliye fahari wa Jumuiya Ahmadiyya, mfuasi na mwanafunzi mashuhuri mwenye ikhlasi wa Hudhur[as]. Hadhrat Maulawii alikuwa na shani kubwa katika usomaji wa Kurani Tukufu kwa sauti nzuri. Alikuwa na ghera sana hata kwamba wapinzani wakubwa pia walikuwa wakishindwa mbele ya sauti ya ujalali na akili yake aliyojaaliwa na Mungu. Alikuwa na maradhi ya sukari ambayo kwa sababu yake likatokea jipu mgongoni baina ya mabega mawili, mnamo Agosti 1905. Waganga mahiri kama vile Hadhrat Hakim Maulana Nuruddin, Bwana Dkt. Mirza Yakub Beg, Hadhrat Dkt. Khalifa Rashiduddin na Bwana Dkt. Seyyid Muhammad Husain Shah walifanya kila lililowezekana kwa kumtibu. Alipasuliwa mara kadha, lakini hakupata nafuu.

Hudhur[as] alijaribu kwa kumtibu na kujitahidi sana na akatumia fedha bila kujali. Chochote alichotamani Hadhrat Maulawii, Hudhur[as] alikiagiza kutoka Lahore au Amritsar akituma mtu maalumu. Hadhrat Maulawii alikuwa akipenda sana maji baridi, kwa hiyo Hudhur[as] alikuwa anaagiza barafu na kuhifadhi daima. Kwa mwezi mzima mfululizo supu ya kuku ilikuwa inatayarishwa kwa Hadhrat Maulawii

na dawa ghali zikatumika.

KIFO CHA HADHRAT MAULAWII, 11 OKTOBA 1905

Lakini kupona katika maradhi hakutegemei tiba ya hali ya juu. Kifo kinapokuja, kitu chochote hakiwezi kukizuia. Mwenyezi Mungu Akapenda kumweka Hadhrat Maulawii karibu Naye. Kwa hiyo, ingawaje jipu, yaani saratani, likapona, bali alipogusa mwenyewe sehemu ya jipu, akasema sasa nitaanza kutembea katika siku chache. Lakini alishikwa na maradhi ya ngozi ya nje ya mapafu, halijoto ilifikia 106 na tiba yoyote haikuathiri. Tarehe 11 Oktoba 1905, baada ya sala ya adhuhuri, Hadhrat Maulawii alifariki. ***Innaa lillahi wa innaa ilaihi raji'un.***

Siku hiyo hiyo karibu na jioni Hudhur[as] alisalisha sala yake ya jeneza na katika kiwanja cha makaburi ya kawaida kilichopo upande wa mashariki wa mji, karibu na bwawa, alizikwa kama amana. Baadaye, wakati wa Jalsa Salana ya mwaka 1905, ilipokwishatengwa ardhi kwa Bahishti Makbarah, sunduku lake lilitolewa kaburini, tarehe 26 Desemba, baada ya sala ya adhuhuri na alasiri. Kisha, tarehe 27 Desemba, karibu na saa nne, Hudhur[as] alisalisha sala yake ya jeneza pamoja na mkusanyiko mkubwa wa watu na aliendelea kumwombea kwa muda mrefu kwa daraja kubwa. Kisha akazikwa katika Bahishti Makbarah. Katika Bahishiti Makbarah, kaburi lake ni la kwanza. Shairi moja la Hudhur[as] alilotunga kutambua sifa za Hadhrat Maulawii, lilinakshiwa kwenye jiwe la kaburi lake. Tafsiri ya beti zake chache ndiyo ifuatayo:

> "Sifa za Maulawii Abdul Karim nielezeje! Abdul Karim aliyetoa uhai wake katika kupigana kwa ushujaa katika njia ya dini, alikuwa mpigaji mweleka mkubwa sana wa dini ambaye Mungu Mwenyewe Alimwita katika ufunuo Wake "Kiongozi wa Waislamu". Yeye alijua siri za haki na alikuwa hazina ya elimu ya dini. Ingawaje wamezaliwa watu wema wakubwa wakubwa chini ya mbingu hii, lakini lulu inayong'ara hivyo imeonekana kwa nadra. Moyo unahuzunika kwa kutengana na rafiki mwenye ikhlasi wa aina hii, lakini twamridhia na kumshukuru Mungu

wetu kwa kazi yake katika kila hali.[472]

JUHUDI YA KUMTIBU

Bidii aliyotia Hudhur[as] kwa kumtibu Bwana Maulawii msifiwa, aliikiri babake Bwana Maulawii akisema maneno haya:

> "Jinsi mwanangu alitibiwa vizuri sana mno katika Qadian, kama ningeuza mali zangu zote kwa kumtibu hivyo haingeyumkinika.

KIFO CHA HADHRAT MAULAWII BURHANUDDIN JHELUMI, 3 DESEMBA 1905

Muda mfupi kabla ya kifo cha Hadhrat Maulawii Abdul Karim, Hudhur[as] alifunuliwa kwamba

"Boriti mbili zimevunjika, Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun."

Kasema: ufunuo huu pia ni wa hatari. Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye maana yake."[473]

Baada ya kifo cha Hadhrat Maulawii Abdul Karim, alipofariki Hadhrat Maulawii Burhanuddin Jhelumi pia katika muda kidogo, ndipo ilijulikana kwamba maana ya boriti mbili ilikuwa wanachuoni hao wawili. Hadhrat Maulawii huyo pia alikuwa mwanachuoni mkubwa. Alifariki 3 Desemba 1905 saa za asubuhi. Alikuwa Mwahmadiyya wa zamani sana, mara ya kwanza kabisa alikutana na Hudhur[as] katika Hoshiarpur, ambapo Hudhur[as] aliwasili huko kwa kufanya ibada faraghani kwa siku arubaini. Alikuwa na tabia ya kisufii na saa zote alijishughulisha katika malezi ya Jumuiya.

PENDEKEZO LA KUANZISHA MADRASA AHMADIYYA QADIAN

Kwa sababu ya kifo cha hao wanachuoni wawili pengo lilionekana katika Jumuiya. Basi ilipendekezwa kwamba kwa kutayarisha wanachuoni katika Jumuiya, kianzishwe chuo cha dini mbali na idara nyinginezo, hapo Madrasa Ahmadiyya yalianzishwa. Na wanajumuiya walipojumuika kwa Jalsa Salana katika wiki ya mwisho ya Desemba

[472] Badr, Februari 1906

[473] Badr, 14 Septemba 1905

1905, Hudhur[as] aliwatolea hotuba kwa uchungu sana ambamo alipendekeza kwamba mbali na shule ya Kiingereza iliyopo, yanahitajika madrasa pia ambamo wanachuoni watayarishwe ambao pamoja na elimu ya Kiarabu wajifunze Kiingereza na elimu zingine pia kiasi fulani. Kwa kusikiliza hotuba hiyo ya Hudhur[as], watu wakaangua kilio, na baada ya hotuba ya Hudhur[as] kumalizika ndugu wote walisema kwa sauti moja kuwa mpango anaofikiria Hudhur[as], tupo tayari kuutekeleza na kuchukua jukumu lake kwa moyo wote. Kisha kushauriana kwa muda mrefu kuliendelea na ikaamuliwa kwamba kwa kutayarisha wanachuoni na wabashiri, tawi moja lianzishwe mbali na shule. Basi tangu mwaka 1906 tawi moja peke yake la elimu ya dini lilianzishwa.

SAFARI YA DELHI, 22 OKTOBA 1905

Mkewe Hudhur[as], Hadhrat Amman Jan, hakwenda kwao Delhi kwa muda mrefu. Mara kadha alinuia, lakini hakuweza kutimiza nia yake kwa baadhi ya vikwazo. Sasa nafasi hii pia ilitokea kwamba Hadhrat Dkt. Mir Muhammad Ismaili[ra] aliyekuwa mdogo wake alipewa jukumu la kutumikia katika hospitali ya Serikali mjini Delhi. Hadhrat Amman Jan alikuwa anajiandaa kwenda na baba yake, Hadhrat Mir Nasir Nawab[ra], hapo Hudhur[as], sawa na dasturi yake, alifanya istikhara na akaambiwa kwamba yeye pia anapaswa kwenda Delhi pamoja naye, hapo yeye akawa tayari pamoja na mahadimu wachache. Tarehe 22 Oktoba 1905, siku ya Jumapili, asubuhi, aliondoka Qadian. Kabla ya kuondoka aliona katika ruya hii:

> "Tumekwenda Delhi. Milango yote imefungwa. Kisha nikaona kwamba milango imetiwa kufuli. Kisha nikaona kwamba mtu fulani anatia kitu cha kuudhi sikioni mwangu. Nikasema kwamba ni udhia gani huu unaonisumbua nao, Mtume wa Mungu[saw] aliudhiwa zaidi ya hii."[474]

Kwa ruya hii ilijulikana kwamba kwenye mioyo wa Wadelhi zimetiwa kufuli kiasi hiki kwamba watakubali athari njema kidogo sana. Hudhur[as] akiondoka Qadian akafika Batala, behewa la daraja ya pili

[474] Badr, 27 Oktoba 1905

liliteuliwa kwa ajili yake. Kwenye stesheni ya Batala, sala za adhuhuri na alasiri zilisaliwa kwa kukusanywa pamoja. Katika Amritsar, nafasi baina ya magari ilikuwa ya masaa matano, kwa hiyo Hudhur[as] akitoka gari alienda kando ya platfomu kupumzika katika kivuli cha miti. Ingawa, Hudhur[as] aliamuru kwamba Waahmadiyya wa Amritsar wasipashwe habari, lakini walipata habari kwa njia hii au ile. Basi, mara moja watu wengi walijumuika na chakula cha jioni kililetwa kwenye stesheni na Jumuiya ya Amritsar.[475]

Saa tatu usiku garimoshi liliondoka stesheni ya Amritsar na karibu na saa tisa u nusu asubuhi lilifika Delhi. Kwenye stesheni za njiani wanajumuiya waliendelea kukutana na Hudhur[as]. Lakini wanajumuiya wa Ludhiana walipofika kwenye stesheni kwa kumwona mwongozi wao mpendwa, Hudhur[as] alikuwa amelala. Kwa hiyo, Dkt. Mirza Yakub Beg alikataa kumwamsha Hudhur[as], na kwa hiyo ndugu hawakuweza kukutana na Hudhur[as]. Baada ya kuwasili Delhi, Hudhur[as] alipopata habari, alisema kwamba wakati wa kurudi, lazima tutakaa Ludhiana. Katika Delhi, Hudhur[as] alikaa katika nyumba ya Alif Khan huko Chatli Kabr.

DUA KWENYE KABURI LA KHWAJA BAKI BILLAH[RH]

Asubuhi ya 24 Oktoba, Hudhur alimwambia Hadhrat Mufti Muhammad Sadik kwamba huku kuna makaburi ya baadhi ya mawalii wa Mungu. Tengeneza orodha yao, ili ipangwe kuyazuru. Basi, kwanza kabisa Hudhur[as] alifika kwenye kaburi la Khwaja Baki Billah[rh] akiinua mikono miwili alimwombea. Hapo, Hadhrat Mufti alimwuliza, "Hudhur, yapasa nini kuomba dua kwenye kaburi? Kasema:

"Yapasa kumwombea mwenye kaburi dua ya maghufira na pia yapasa kujiombea kwa Mungu."

Kwenye jiwe la kaburi la Bwana Khwaja[rh] shairi la Kiajemi lilikuwa limeandikwa. Hudhur akasema kwamba alinakili hili. Baadaye alizuru makaburi ya baadhi ya watawa wengine.

[475] Al-Hakam, 6 Desemba 1905

AKIONA JAMI‘ MASJID DELHI

Wakati wa kurudi, akiona Jami‘ Masjid Delhi, alisema:

> “Uzuri wa kweli wa misikiti si kwa majengo, bali ni kwa wasalio ambao wanasali kwa ikhlasi, waila misikiti hiyo yote ni mahame. Msikiti wa Mtume Mtukufu[saw] ulikuwa mdogo, uliezekwa kwa makuti na wakati wa kunyesha mvua msikiti ulikuwa unavuja...”

KAMWITA HADHRAT MAULAWII NURUDDIN AJE DELHI

Baada ya kufika Delhi, Hudhur[as] aliona kwamba afadhali Maulawii Nuruddin pia aitwe kuja Delhi. Basi Bwana Maulawii alitumiwa telegramu. Tarehe 28 Oktoba 1905 telegramu ilipofika Qadian Hadhrat Maulawii alikuwa katika kiliniki yake. Akifikiri asichelewe kutekeleza amri, papo kwa papo akaondoka kwenda safari, hakwenda nyumbani wala hakubadilisha mavazi wala hakuchukua tandiko, wala hakujiandaa kwa njia yoyote, bali hakusubiri hata gari la farasi, akaanza kutembea kuelekea Batala kwa miguu. Ndugu walipojua kwamba yeye ameenda safari kuchukua bila masurufu na mahitaji mengineyo, wakamfikishia baadhi ya mahitaji ya lazima akiwa njiani kuelekea Batala. Alifika Delhi kwa Imamu wake 29 Oktoba.

KWA NINI NI LAZIMA KUMWAMINI?

Tarehe 25 Oktoba, masheikh wachache pamoja na baadhi ya wanafunzi wao walimfikia Hudhur[as] na wakasema kwamba twasali, twafunga saumu, twaamini Kurani na Mtume[saw], kuna haja gani ya kukuamini? Akajibu:

> “Mtu anapopinga amri ya Mwenyezi Mungu, hayo yote yanageuka kuwa dhambi. Askari wa kawaida anapoleta amri kutoka kwa serikali, yule anayeikataa amri yake huhesabiwa kuwa mhalifu na huadhibiwa. Kama hii ndiyo hali ya watawala wa kidunia, basi kumwondolea heshima yule anayekuja kutoka kwa Hakimu Mkubwa kuliko mahakimu wote na kutokumthamini kutakuwa uasi mkubwa kiasi gani wa amri ya Mwenyezi Mungu! Mwenyezi Mungu Ana ghera sana. Yeye sawa na hekima yake Humtuma mtu sawa na haja ya wakati,

mwanzoni mwa karne potofu ili awaite watu kwenye mwongozo. Kukanyaga chini ya miguu mambo yake yote ni dhambi kubwa..."

WATU WANAOPASWA NIKUTANE NAO

Hudhur[as] alimwuliza saa za jioni Dkt. Mirza Yakub Beg kwamba leo umetembelea sehemu gani? Bwana Dkt. Akasema, 'Hudhur, nimeona Mnara wa Firoz Shah, Msikiti wa Mahabat Khan, Ngome Nyekundu na sehemu nyinginezo. Hudhur[as] akasema:

"Twataka kuzuru makaburi ya Hadhrat Bukhtiar Kaki[rh], Nidhamuddin[rh] Auliyaa, Hadhrat Shah Waliyullah[rh] na wengineo. Watu hawa wa Delhi walio juu ya uso wa ardhi hawakutani nami wala hawapaswi nikutane nao. Kwa hiyo, watu wema miongoni mwao walioishafariki na wamezikwa ndani ya ardhi tutakutana nao, ili tusirudi bila kukutana na mtu. Naona karama ya hawa watawa kwamba waliishi baina ya watu hao wenye mioyo migumu. Katika mji huu bado hatujapata kukubaliwa walivyopata watawa hao. Ubeti:

> Macho yapo wazi, na masikio pia, na akili ipo; nashangaa kwa kufunga macho yao upande wa Mungu.

Islam imefikiwa na msiba gani! Misiba ya ndani haina mwisho na ya nje pia haina mipaka. Hata hivyo, watu hao wanafikiri kwamba hakuna haja ya msuluhishi yeyote...

KUZURU MAKABURI

Basi, sawa na mpango huo, tarehe 26 Oktoba, Hudhur[as] aliyazuru makaburi ya Hadhrat Maulana Shah Abdur Rahim[rh] na mwanaye Hadhrat Shah Waliyullahi[rh], Hadhrat Maulana Shah Abdul Aziz[rh], Hadhrat Khwaja Mir Dard[rh], na makaburi ya watawa wengine. Kuhusu Hadhrat Shah Waliyullahi[rh], akasema kwamba mtawa huyo alikuwa mwenye kuona kashfi na kudhihirisha karama.

Tarehe 28 Oktoba, kuanzia adhuhuri mpaka alasiri, Hudhur[as] alitoa hotuba makazini pake. Na watu kumi walifanya baiati.

29 Oktoba 1905, wakati wa asubuhi, Hudhur alienda kuzuru kaburi la Mheshimiwa Nidhamuddin Auliyaa[rh]. Hapo palikuwa na kaburi la Amir Khusro[rh] pia. Hudhur[as] aliwaombea wote wawili. Khwaja Hasan Nidhami, kwa kusisitiza sana alimchukua Hudhur[as] kwenye chumba chake na akampa kitabu kimoja kiitwacho "Shawaahide Nidhami". Akamkirimu Hudhur[as] na mahadimu wake kwa chai.

Siku hiyo hiyo, baada ya sala ya adhuhuri, watu wachache wa Merat na Balbgad walifanya baiati. Baada yake, Hudhur[as] alitoa hotuba ndefu.

31 Oktoba, Hudhur[as] hakujisikia vizuri. Tarehe mosi Novemba 1905, Hudhur[as] alizuru kaburi la Khwaja Kutbuddin Bakhtiar Kaki[rh], na hapo akamwombea kwa kitambo kirefu.

MIRZA HAIRAT, MHARIRI WA KARZAN GAZETTE KAMTUPIA HUDHUR[AS] CHANGAMOTO

Mirza Hairat wa Delhi alikuwa mtu mwenye kupenda umashuhuri. Kwa kupata umashuhuri usio na thamani akamtupia Hudhur[as] changamoto ya kufanya mjadala, katika toleo la mosi Novemba 1905 la gazeti lake "Karzan Gazette". Kwa kumjibu, Hadhrat Sheikh Yakub Ali alichapisha tangazo tarehe 2 Novemba ambamo aliandika kwamba nikiwa mwandishi wa gazeti nipo tayari kwa kujadiliana na Mirza Hairat wa Delhi. Isitoshe, Jumuiya ya Delhi pia ilitoa tangazo moja ambamo iliandika kwamba wenzako waandishi gazeti Sheikh Yakub Ali na Mufti Muhammad Sadik wapo tayari kwa kujadiliana nawe, sharti masheikh maarufu wa Delhi, yaani Maulawii Muhammad Bashir, Maulawii Abdul Hak, Maulawii Abul Khair na wengine waliokulelea wakukubali kupitia tangazo lililochapwa. Tangazo hilo lilipotoka tu, Mirza Hairat ─ Hairat, maana yake 'mshangao' ─ akazama katika mshangao kiasi hiki kwamba hakuibuka tena.

KUONDOKA DELHI, 4 NOVEMBA 1905

Imeshatajwa juu kwamba wakati wa kwenda Delhi, ndugu wa Ludhiana hawakuweza kuonana na Hudhur[as], na Hudhur[as] aliijali sana habari hii. Mara baada ya kufika Delhi akasema kwamba wakati wa

kurudi lazima tutakaa Ludhiana. Jumuiya ya Ludhiana pia ilikuwa na huzuni kwa kukosa kumwona, na ikamtuma Hadhrat Maulawii Abdul Kadir Ludhianawii aende Delhi ili kwa niaba ya Jumuiya ya Ludhiana ampelekee Hudhur[as] ombi la mwaliko. Basi Hadhrat Maulawii alifika Delhi kwa lengo hilo, na kumfikishia ombi la Jumuiya la kumwalika, ambalo Hudhur[as] alikubali kwa furaha kubwa. 4 Novemba 1905, Hudhur[as] pamoja na mahadimu walifika kwenye stesheni ya Delhi kwa lengo la kurudi. Bwana Khwaja Hasan Nidhami, alikuwepo hapo mapema kwa kumsindikiza. Yeye alimwomba Hudhur[as] kwamba kuhusu cheo na daraja ya Hadhrat Khwaja Nidhamuddin Auliyaa[rh] na watawa wengine wa Delhi aandike na kututumia maandishi kutoka Qadian. Hudhur[as] akakubali ombi lake.

KAWASILI LUDHIANA, 5 NOVEMBA 1905

Hudhur[as] akiondoka Delhi kawasili Ludhiana tarehe 5 Novemba karibu saa tano za asubuhi. Hapo watu wapatao 1,000 walikuwepo kumpokea na kumwona Hudhur[as]. Watu wengi wa Jumuiya za Patiala, Rahun, Bangah, Hajipur, Bassi, Malerkotla na kadhalika walikuwepo kwenye stesheni. Wanajumuiya wa Ludhiana walikuwa wameweka tayari nyumba moja kubwa kwa Hudhur[as] kwa kukaa ambamo mahitaji yote yalikuwepo. Jioni ya 5 Novemba, Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin alitoa mawaidha katika Ludhiana yaliyopendwa sana. Asubuhi ya 6 Novemba, Hudhur[as] alitoa baadhi ya nasaha.

Maulawii Sa'dullah Ludhianwii ajulikanaye kwa mdomo wake mchafu na baadhi ya masheikh wengine walitoa matangazo machafu dhidi ya Hudhur[as] ambayo jibu lake likatolewa siku hiyo hiyo, 6 Novemba, na Sheikh Yakub Ali, Mhariri wa Al-Hakam.

HOTUBA YA LUDHIANA, 6 NOVEMBA 1905

Tarehe 6 Novemba 1905, katika mkusanyiko wa watu elfu kadha, Hudhur[as] alitoa hotuba. Katika hotuba hiyo, Hudhur[as] alieleza ukweli wa Islam, na hali yake ya siku hizi, na njia za urekebisho. Vilevile akaeleza hoja za madai yake. Hotuba hiyo kuanzia saa mbili na nusu

za asubuhi mpaka saa tano na nusu, kwa masaa matatu mfululizo, iliendelea na watu wakaendelea kuisikiliza kwa makini sana.

AWASILI AMRITSAR, 7 NOVEMBA 1905

Tarehe 7 Novemba 1905, asubuhi aliondoka Ludhiana, na karibu saa kumi akawasili Amritsar. Kwenye stesheni wanajumuiya wengi walikuwepo kwa kumpokea. Jumuiya ilimwomba Hudhur[as] akae katika Amritsar pia na atoe hotuba. Basi, kwa kibali cha Hudhur[as], tangazo la hotuba lilitolewa.

Sawa na tangazo, tarehe 9 Novemba, katika ukumbi wa Kanhayya Lal, saa mbili asubuhi, Hudhur[as] alianza kutoa hotuba. Ingawa kupitia matangazo, na kabla ya kuanzia mkutano pia, watu waliambiwa hii kwamba:

> "Mtu yeyote asilete ukizani dhidi yangu ama swali kabla ya hotuba yangu au katikati yake au baadaye,"[476]

na hiyo ilikuwa lazima, kwani lengo la Hudhur[as] lilikuwa mahubiri tu sio mjadala, lakini masheikh wa Amritsar sawa na mazoea yao walileta fujo sana mno na ufisadi. Hudhur[as] alikwisha pashwa habari ya fujo hiyo kwa njia ya ruya. Hudhur[as] aliona katika ruya shamba la miwa, na muradi wake huwa ufisadi na fujo. Sawa na wakati uliowekwa, ukumbi ulijaa wasikilizaji. Kwanza Hudhur[as] alisema, tazameni, kabla ya miaka kumi na minne nilipokuja hapa, watu wachache tu walikuwa pamoja nami. Masheikh walinitolea fatuwa ya kufuru. Sheikh Abdul Hak Ghaznawii alifanya mubahala nami ambamo nilijiombea tu kwamba kama mimi ni mwongo na mzushi katika madai yangu, basi Mwenyezi Mungu Anifedheheshe na kuniangamiza; sikuomba dhidi yake. Lakini, baada ya mubahala huo, Mwenyezi Mungu Alinisaidia kiasi hiki kwamba leo maelfu ya watu ni wafuasi wangu. Tena katika mashtaka ya wapinzani dhidi yangu, daima Alinishindisha na kunilinda na shari na ufisadi wao. Ilmuradi, bado Hudhur[as] alikuwa ametoa hotuba kwa dakika 45 tu, mfuasi mmoja wa Hudhur[as] akiona koo la Hudhur[as] limekauka, akampa

[476] Al-Hakam, 10 Novemba 1905

kikombe cha chai. Ulikuwa ni mwezi wa Ramadhani, Hudhur[as] alikuwa msafiri na mgonjwa pia, kwa hiyo ilikuwa si faradhi kwa Hudhur[as] kufunga saumu, hata hivyo alikataa kuinywa. Baada ya muda kidogo mara ya pili na kisha mara ya tatu akaletewa chai. Hapo hakuona vizuri kukataa na akanywa chai. Mara fujo ikatokea. Mungu tu Atulinde! Masheikh wapinzani walipata nafasi hiyo, wakaleta machafuko. Mungu Apishe mbali!! Hudhur[as] aliwafahamisha sana kwamba mimi ni msafiri na ni mgonjwa pia, na sawa na Kurani Tukufu saumu si faradhi juu yangu. Kurani Tukufu inaeleza kwa maneno wazi: فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَرِيْضًا اَوْ عَلٰى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ اَيَّامٍ اُخَرَ , yaani, miongoni mwenu awaye mgonjwa au katika safari, basi atimize hesabu katika siku zingine." Lakini wakati nia yenyewe iwe mbaya, nani anasikiliza jambo la akili. Wafisadi waliendelea kupiga makelele, hawakuacha nafasi ya kuvuruga mkutano kwa kupiga mbinja na makofi. Baadhi ya waovu waliendelea kutumia mdomo mchafu sana. Wazee wa Amritsar na polisi walijaribu sana kuwatuliza watu kwa njia ya amani, hakuna aliyewasikiliza. Hatimaye, ilionekana yafaa Hudhur[as] apelekwe makazini mwake katika gari lililofungwa. Basi gari lililofungwa lililetwa na Hudhur[as] akalipanda. Gari la Hudhur[as] lilipoondoka tu, wapinzani wakaanza kulirushia mawe gari. Ulikuwa ni ulinzi wa Mwenyezi Mungu kwamba Hudhur[as] hakupata shida, lakini hao hawakuacha njia yoyote ya kumwudhi Hudhur[as]. Njiani Hudhur[as] alisema:

"Ilikuwa hakuna budi kutimia suna hii pia."

KUFIKA QADIAN, 10 NOVEMBA 1905

Hatimaye, tarehe 10 Novemba 1905, saa sita mchana, Hudhur[as] alifika Qadian Darul Amaan kwa amani pamoja na mahadimu wake. *Alhamdulillahi alaa dhalika*. Ilikuwa ni siku takatifu ya Ijumaa. Baada ya kufika Qadian, Hudhur[as] alisali sala ya Ijumaa pamoja na jamaa. Maandishi ya Khwaja Hasan Nidhami yalimfikia Hudhur[as] ili kumkumbusha ombi lake. Kwa kujibu Hudhur[as] aliandika:

"Katika Delhi, moyo wangu ulipata jazba kwamba waja wakweli na wapenzi wa Mola waliotesewa sana na wakazi wa ardhi hiyo

kama mimi na wakafariki na kumlaki Mpendwa wa kweli, nichangamshe moyo wangu kwa ziara ya makaburi yao yenye baraka. Basi, kwa nia hiyo nikaenda kwenye kaburi lenye baraka la Hadhrat Khwaja Sheikh Nidhamuddin[rh], walii wa Mungu, na kadhalka kwenye makaburi yenye baraka ya watawa wengine wachache pia. Mungu Atujaalie sote rehema Yake."

MLANGO WA SITA

KUANZIA FUNUO ZA KUKARIBIA KIFO, MPAKA HUDHUR[AS] KUFARIKI

FUNUO ZA KUKARIBIA KIFO, DESEMBA 1905

Mwishoni mwa mwaka 1905, Hudhur[as] aliarifiwa kupitia ruya na funuo kwamba sasa wakati wa kifo chake umekaribia. Kwanza kabisa aliona kwamba amepewa katika chombo kipya cha udongo uliookwa, maji safi yaliyobaki kiasi cha mafunda mawili matatu na papo hapo akafunuliwa "maji ya uhai"[477] — kana kwamba Mwenyezi Mungu mwenyewe Alimwambia kwamba uliyoonyeshwa mafunda mawili matatu ya maji katika birika la udongo, hayo ni maji ya uhai, yaani sasa umri wako umebaki miaka miwili mitatu tu.

Baada yake alifunuliwa: قَلَّ مِيْعَادُ رَبِّكَ , siku chache sana zimebaki. Siku hiyo wote watahuzunika. [478]قَرُبَ اَجَلُكَ الْمُقَدَّرُ وَ لَا نُبْقِيْ لَكَ مِنَ الْمُخْزِيَاتِ ذِكْرًا yaani wakati wa kifo chako ulichowekewa umeshakaribia. Na hatutabakiza jambo la kufedhehesha nyuma yako. Kisha alifunuliwa: [479]جَاءَ وَقْتُكَ وَنُبْقِيْ لَكَ الْاٰيٰتِ بَاهِرَاتٍ , yaani, wakati wako umewadia na tutabakisha nyuma yako ishara zing'aazo kukusaidia. Na ufunuo huu pia ulifunuliwa: تَمُوْتُ وَ اَنَا رَاضٍ مِّنْكَ , yaani utafariki ilhali nitakuwa nimekuridhia. Kadhalika ufunuo mmoja nilifunuliwa: Siku chache sana zimebaki. Siku hiyo wote watajawa na huzuni. Hii itakuwa, hii itakuwa, hii itakuwa. Baadaye tukio kuhusu wewe litatukia. Baada ya matukio yote na kuonyeha maajabu ya kudra, litatokea tukio lako."[480]

Baadhi ya funuo zingine pia kama hizo zilifunuliwa ambazo sawa na kauli ya Hudhur[as], zilitetemesha msingi wa uhai wake, na zikapoza maisha haya. Kwa kuona wingi wa funuo kama hizo, Hudhur[as] akafahamu kwamba sasa zama za kifo chake ni karibu. Hapo kwa

---

[477] Ufunuo wa 18 Desemba 1905, *Review* la Desemba 1905.

[478] Ufunuo wa 29 Novemba 1905, Al-Hakam, J. 9, Na. 42

[479] Ufunuo wa 14 Desemba 1905, Badr, J. 1, Na. 39

[480] Al-Wasiyyat, uk. 2

kuitolea Jumuiya yake nasaha, Hudhur aliandika kijitabu kidogo "Al-Wasiyyat" ambamo aliandika:

"Ni sunna ya Mwenyezi Mungu ambayo sunna hii tangu Alipomwumba binadamu katika ardhi Aliendelea kudhihirisha ya kwamba Yeye Huwasaidia manabii na mitume wake… Na kweli ile wanayotaka kuizagaza kote duniani Anapanda mbegu zake kwa mikono yao. Lakini Haitimizi kazi hii kikamilifu kwa mkono wao, bali kwa kuwafisha katika wakati ambao kidhahiri huwa na hofu ya kushindwa, Huwapa wapinzani nafasi ya kucheka na kudhihaki na kufanya masihara na kuaibisha. Na pindi wanapokwisha kudhihaki, hapo Huonyesha mkono wa pili wa kudra yake… Hudhihirisha kudra ya namna mbili:

(1) Kwanza, kwa mkono wa manabii wenyewe huonyesha mkono wa kudra yake.

(2) Pili, katika wakati ambapo matatizo yanazuka baada ya kifo cha manabii na maadui hupata nguvu na hudhani kwamba mambo yameharibika… hapo Mwenyezi Mungu Hudhihirisha mara ya pili kudra yake yenye nguvu na kuimarisha Jumuiya iliyokuwa inaanguka. Basi yule anayesubiri mpaka mwisho, huona mwujiza wa Mwenyezi Mungu, kama ilivyotendeka katika enzi ya Hadhrat Abu Bakr Siddik[ra]. Wakati huo kifo cha Mtume Mtukufu[saw] kilipofikiriwa kutokea wakati usiofaa na mabedui wengi wakaritadi, na masahaba kwa sababu ya huzuni kubwa wakawa kana kwamba wameshikwa na wazimu, hapo Mwenyezi Mungu kwa kumsimamisha imara Hudhrat Abu Bakr Siddik[ra] Akaonyesha mara ya pili onyesho la kudra yake na Akanusuru Islam iliyokurubia kufutika…"

"Basi, enyi wapenzi, kwa kuwa hii ndiyo sunna ya Allah tangu kale ya kwamba Mwenyezi Mungu Huonyesha kudra mbili ili kuzikanyagilia mbali furaha mbili za bandia za wapinzani, hivyo haiwezekani sasa ya kuwa Mwenyezi Mungu Aziache sunna yake ya zamani. Kwa hiyo msihuzunike kwa habari niliyowaambieni wala nyoyo zenu zisifadhaike, kwani hamna budi kuiona kudra ya pili vilevile. Na kuja kwake ni bora kwenu

kwa sababu hiyo itadumu, nayo itaendelea bila kukoma mpaka kiama… Mimi nimedhihirika nikiwa kudra moja kutoka kwa Mungu, nami ndimi kudra hasa ya Mungu na baada yangu watakuwepo wengine watakaokuwa onyesho la kudra ya pili."

Katika maandishi hayo, Hudhur[as] akitaja mfano wa Hudhrat Abu Bakr Siddik[ra] akauita ukhalifa utakaopatikana baada yake kuwa kudra ya pili, na akasema hii itafululiza bila kukatika mpaka kiama.

KUANZISHA BAHISHTI MAKBARA

Zaidi ya hayo, sawa na bishara za Mungu, Hudhur[as] alipendekeza kuteua kiwanja cha makaburi pia ambacho utashi wa Hudhur[as] ulikuwa kwamba humo yawepo makaburi ya watu waaminifu ambao walikuwa wameishi maisha yao kwa wema, uchamungu na utakaso na waliweka mfano mzuri kutoa dhabihu za mali na uahi. Na Hudhur[as] sawa na ridhaa ya Mungu aliyaita mava hayo kuwa Bahishti Makbara. Akasema:

"Nami nikaonyeshwa mahali fulani kwamba ndipo mahali pa kaburi langu. Nikamwona malaika mmoja akipima ardhi, na alipofika mahali fulani akasema: Hapa ndipo mahali pa kaburi lako! Kisha nikaonyeshwa kaburi moja mahali pamoja ambalo liling'aa zaidi kuliko fedha, na udongo wake wote ulikuwa wa fedha. Ndipo nikaambiwa, 'Hili ni kaburi lako.' Na nikaonyeshwa mahali pamoja napo pakaitwa 'Bahishti Makbara' (Mava ya Kipeponi) na nikajulishwa kwamba hayo ndiyo makaburi ya watu wema wa Jumuiya watakaokwenda Peponi."

MASHARTI YA KUZIKWA KATIKA BAHISHTI MAKBARA

Kwa kuzikwa katika mava hayo, Hudhur[as] kwa kuelekezwa na Mungu aliyaweka masharti machache pia ambayo ni haya:

1. Sharti la kwanza ndilo hili ya kwamba mtu yeyote anayetaka azikwe humo achangie chochote sawa na uwezo wake kwa matumizi hayo.

2. Sharti la pili ni kwamba miongoni mwa wanajumuiya, yule tu atazikwa makaburini humo atakayefanya wasia ya kwamba

baada ya kifo chake sehemu ya kumi ya mali atakayoacha itatumiwa kwa kueneza Islam na kuhubiri maamrisho ya Kurani sawa na maagizo ya Jumuiya hii. Na kila mkweli mwenye imani kamilifu atakuwa na hiari ya kuandika katika wasia wake zaidi yake vile vile, lakini siyo kidogo kuliko sehemu hiyo.

3. Sharti la tatu ni kwamba mwenye kuzikwa makuburini humo awe mtawa na ajiepushe na yaliyoharamishwa wala asifanye ushirikina wala mambo yoyote yaliyo bidaa. Awe Mwislamu mkweli na safi.

Zaidi ya masharti hayo Hudhur[as] akaongeza mwishoni jambo moja katika maneno haya pia kwamba:

"Kila mtu mwema asiye na milki yoyote, asiyeweza kutoa mali, ikiwa itathibitika kwamba alijitoa wakfu maisha yake kwa kutumikia dini, naye alikuwa mwema, aweza kuzikwa makaburini humo."

KUANZISHA KAMATI YA WASIMAMIZI WA MASILAHI YA MAKBARA

Kwa kusimamia mava hayo, Hudhur[as] aliunda kamati moja pia aliyoita "Kamati ya wasimamizi wa masilahi ya Mava" Hudhur[as] alimteua Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin kuwa Sadr (mwenyekiti) wa kamati hiyo. Na akalazimisha kwamba wapaswa angalao wanakamati wawili wa kamati hiyo wawe wataalamu wa dini. Hudhur[as] akafafanua pia kwamba si maana ya kuanzisha mava hayo kwamba ardhi hii itamfanya mtu aende peponi. Bali, maana yake ni hii kwamba Mwenyezi Mungu Atajaalia kwa fadhili na rehema yake kwamba aendaye Peponi tu ataweza kuzikwa katika mava hayo."[481]

MAANA YA UNAIBU WA SADR ANJUMAN

Hudhur[as] aliandika kwamba "Anjuman ni naibu wa Khalifa aliyewekwa na Mungu." Baadhi ya watu wanaieleza sentensi hii ya Hudhur[as] kwamba Hudhur[as] aliweka kamati moja baada yake kwa kupokea mali ya wasia na kuitumia kwa kueneza na kuhudumia Islam

[481] Someni Al Wasiyyat.

na kusimamia nidhamu ya Jumuiya, ambayo akaiita naibu wake, na ambayo uamuzi wake utakaofanyika kwa rai ya wengi, akaufanya kuwa wa mwisho baada ya kifo chake. Hapo ni dhahiri kwamba kamati hiyo itakuwa lazima itiiwe na wanajumuiya wote, na uamuzi utakaokuwa kwa rai ya wengi hakuna budi wanajumuiya wautii. Kwa kujibu hoja hiyo ya wapinzani, inapaswa kuzigatia daima kwamba katika kijitabu Al-Wasiyyat Hudhur[as] alilazimisha vitu viwili kwa kuendesha nidhamu ya Jumuiya:

1. Kudra ya pili, ambayo haikuwepo katika uhai wa Hudhur[as]. Kwani kuja kwake kulipangwa baada ya kifo cha Hudhur[as], na kazi yake ilikuwa ile ile aliyofanya Hadhrat Abu Bakr Siddik[ra]. Na ni dhahiri kwamba hiyo haiwezi kuitwa kwa jina lolote minghairi ya Ukhalifa.
2. Anjuman, iliyowekwa katika uhai wa Hudhur[as]. Lakini Hudhur[as] aliikabidhi kazi hii tu kwamba itafakari mapendekezo yafaayo ya kupokea michango na kuitumia sawa na agizo la Jumuiya.[482]

Basi, wakati wa kifo cha Hudhur[as], mtu yeyote kati ya Jumuiya nzima hata hakuwaza kwamba baada ya Hudhur[as], Ukhalifa hautafululiza, bali Anjuman itakuwa ni Khalifa wake. Watu ambao baadaye walikanusha Ukhalifa, hata hao pia walifanya baiati kwa mkono mtakatifu wa Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin akiwa Khalifa wa Hudhur[as] na wakakiri kuwa hiyo ni "sawa na kijitabu Al-Wasiyyat". Na wakatangaza jambo hilo kwa saini zao katika Jumuiya nzima, kama itakayobainishwa mbele.

VITABU VYA MWAKA 1905

1. Uandishi wa **Barahine Ahmadiyya,** sehemu ya 5: Bishara zilizotajwa katika sehemu nne za awali za Barahine Ahmadiyya, nyingi katika hizo zilikuwa zimekwishatimia. Kwanza, Hudhur[as] alizitaja katika kitabu hiki. Pili, alifafanua uhakika na haja ya mwujiza. Ya tatu, ukinzani lilioleta *Paisa*

[482] Someni kijitabu Al Wasiyyat.

Akhbar Lahore dhidi ya utabiri wa tetemeko la ardhi, aliujibu kwa urefu. Zaidi ya hayo, jinsi alivyotoa maelezo kwa elimu ya ndani ya aya chache za Sura Al-Mu'min, haupatikani mfano wake.

Alianza kuandika kitabu hiki mwanzoni mwa mwaka 1905, na zaidi ya kukiita Barahine Ahmadiyya, alikiita Nusratul Hak pia. Kitabu hiki, baada ya kifo cha Hudhur[as], kilichapwa tarehe 15 Oktoba 1908.

2. Uandishi na uchapaji wa **Al-Wasiyyat**, kijitabu hiki kimeshaelezwa kireru hapo juu.

LIMETOKEA TETEMEKO KATIKA KASRI YA KISRA

Irani ni nchi ya zamani sana ya kihistoria. Tangu zamani sana wafalme wa nchi hiyo walikuwa wanaitwa Kisra. Tarehe 15 Januari 1906, Hudhur[as] alifunuliwa: "Limetokea tetemeko katika kasri ya Kisra". Wakati wa kuchapishwa ufunuo huo, mtawala wa Irani alikuwa Shah Mudhaffaruddin. Miezi michache kabla ya ufunuo huo katika mwaka 1905, akikubali maombi ya wananchi alishatangaza kuanzisha bunge. Kwa tangazo hilo la mfalme watu wa Irani walifurahi sana na mfalme pia alikuwa akifurahia kupendwa kwake. Lakini Mungu wa Arshi Aliyeteremsha ufunuo "Limetokea tetemeko katika kasri ya Kisra", Alitaka kutimiza ufunuo huo. Mudhaffaruddin Kachaar, mfalme wa Irani, akafariki katika mwaka 1907 na mwanamfalme aliyetakiwa kurithi, Mirza Muhammad Ali, akashikilia ufalme pahali pa baba yake. Ingawa mara baada ya kushikilia utawala, alitangaza kuanzisha kuimarisha Halmashauri na kuimarisha utawala wa kiniaba, lakini kwa kudra ya Mungu mambo yakazuka nchini yaliyoanzisha hitilafu baina ya mfalme na Halmashauri. Halmashauri iliona kwamba baadhi ya wafuasi wa mfalme ndio chanzo cha fitina na ikaomba kwamba hao waondolewe katika baraza. Ingawa mfalme aliahidi kukubali ombi la halmashauri, lakini papo hapo alinuia pia kwamba hao waende Tehran. Wakati wa kuhama, Ma-kosaki (Cossack) waliokuwa wapambe wa mfalme, na wasaidizi wa wazalendo walikosana. Ufunuo wa Hudhur[as] ulitimia hivi kwamba jengo la bunge la Irani lilibomolewa kwa mizinga, na mfalme akavunja bunge. Kwa sababu ya kitendo hicho cha mfalme uasi

ulitokea kote nchini. Hatimaye, wapambe wa mfalme ambao mfalme pia aliona fahari sana kwa hao, waliungana na waasi. Kasri ya Mirza Muhammad Ali Kachaar, Kisra wa Irani, ikatetemeka kiasi hiki kwmba tarehe 15 Julai 1909 mfalme akakimbilia pamoja na mkewe ubalozi wa Urusi. Matokeo yake ni kwamba utawala ukauondoa ukoo huo kwa kudumu, na uwepo wa Kisra ulifutika duniani.

KUWAFARIJI WABANGALI, 11 FEBRUARI 1906

Tarehe 11 Februari 1906, Hudhur[as] alipata ufunuo huu:

"Amri iliyokuwa imetolewa hapo kabla kuhusu Bangal, sasa hao watafarijiwa".[483]

Maelezo ya utabiri huu ni kwamba mnamo Oktoba 1905, Gavana Mkuu wa India, Lord Curzon, akiufikiria mkoa Bangal kuwa ni mkubwa, aliugawa katika sehemu mbili: 1. Sehemu moja ilikuwa Bangal mashariki na Asaam. 2. Sehemu ya pili, Bangal magharibi ambamo ilikuwepo Bihar na Urisa pia. Mji mkuu wa sehemu ya kwanza ulikuwa Dhaka, na wa sehemu ya pili, Calcutta. Kwa vile katika Bangal mashariki Waislamu walikuwa wengi, hivyo kwa namna fulani ikawa ni mkoa wa Kiislamu, ambao ulikuwa kama kidonda kwa Mabaniani, kwani Mabaniani walitaka kutawala Bangal nzima isiyogawanyika. Na kwa Bangal mashariki kutengwa, Waislamu pia walipata hadhi kubwa katika mkoa ambayo Baniani yeyote mwenye chuki hakuweza kustahimili. Kwa hiyo, Mabaniani walipiga makelele sana juu ya ugawanyaji huo. Walifanya mikutano, wakafanya maandamano, wakaharibu majengo ya serikali, wakayatupia magarimoshi mabomu, wakawaua pia baadhi ya Waingereza. Na kwa kufutiliwa mbali ugawanyaji huo wakatia bidii yote, lakini serikali haikuathirika. Lord Curzon alienda Uingereza mwishoni mwa mwaka 1905 akimaliza muda wa kazi yake. Pahali pake akaja Lord Minto na yeye pia hakukubali ombi la Mabaniani. Ilipofahamika kuwa katika India nzima kugawanywa huku kumeimarika na kidhahiri hayakuyumkinika mabadiliko kutokea ndani yake, hapo ufunuo huo ulifunuliwa, na kama kawaida ulitangazwa katika magazeti ya

[483] Badr, 16 Februari 1906

Jumuiya. Watu wliupinga kwa namna mbalimblai, wakafanya dhihaka, wakacheka, kwamba wakati hatua zote zimeishachukuliwa na mgawanyiko huo umebaki pale, sasa kutangaza ufunuo kinyume chake kuna maana gani? Katika mwaka 1910 Lord Minto pia alikwenda na Lord Hardinge akaja India akiwa Gavana Mkuu. Katika zama zake, kinyume cha kawaida ikaamuliwa kufanya sherehe ya kumtawaza George wa Tano katika India. Mnamo mwaka 1911 yalianzia maandalizi ya mkutano wa kutawazwa. Lord Hardinge mwenyewe alimpelekea Waziri wa India pendekezo moja ambamo aliandika kwamba "kwa kuwafariji Wabangali ni lazima kwamba mgawanyiko wa Bangal ufutiliwe mbali, na wakati ufaao sana wa kutangaza uwe wakati wa kutawazwa kwa George V. George V pamoja na Malkia akaja Delhi akisafiri maelfu ya maili, na katika Baraza la Delhi ambapo walijumuika Maamiri wa India nzima na Machifu, viongozi na watawala wa majimbo, alitangaza kufuta mgawanyiko huo, na katika tangazo alitumia maneno haya kwamba "kufutwa kwa mgawanyiko wa Bangala ni kwa kuwafaraji tu Wabangali."

KUANZISHA JARIDA TASH-HIZUL ADH-HAN, 1 MACHI 1906

Tarehe mosi Machi 1906, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad alianza kutoa jarida moja la Kiurdu lililoitwa Tash-hizul Adh-han. Katika zama zile, jarida hili lilifanya kazi nzuri sana kwa kulea vijana na kwa kujibu kikamilifu wapinzani wa Jumuiya, na kwa kueneza Uahmadiyya.

PADRI AHMAD MASIHI KAKATAA KUFANYA MUBAHALA, MEI 1906

Katika Delhi alikuwepo Padri mmoja kipofu, Ahmad Masihi, aliyeanzisha mjadala na Hadhrat Mir Kasim Ali juu ya swala la kufa au kutokufa kwa Bwana Yesu juu ya msalaba. Hadhrat Mir kwa hoja madhubuti akathibitisha kwamba Bwana Yesu hakufa kabisa msalabani, bali akiwa amezimia akaondolewa msalabani akiwa mzima. Mjadala huu wa kuvutia uliendelea mfululizo siku kadha. Hatimaye wasikilizaji walishuhudia kwa kuapa kwa kauli moja kwamba katika mjadala huu padri Ahmad Masihi ameshindwa kabisa.

Na padri Ahmad Masihi mwenyewe pia alilazimika kugeuka na kukiri kushindwa kwake katika mkutano wa hadhara wa 4 Aprili 1906. Akasema:

> "Enyi wasikilizaji, katika mkutano uliopita mlimwamulia Mwahmadiyya ushindi dhidi yangu. Sikuhuzunika, bali nimefurahi kwa namna fulani kwamba bila kutafakari mlimpa haraka Bwana Seyyid ushindi, lakini hamkutambua kwamba kwa kuamua hivyo, ikawa lazima kwetu kukubali dini na itikadi pia za Bwana Seyyid. Basi mimi nami pia namwamulia Bwana Seyyid kwamba yeye amewakubalisha watu wengi itikadi za Kiahmadiyya."[484]

Baada ya mjadala huo, Hadhrat Mir Kasim Ali alimpa Bwana Padri changamoto ya kufanya mubahala, lakini yeye hakuridhia, bali kwa kujibu alitoa tangazo kwamba nipo tayari kufanya mubahala na Bwana Mirza Ghulam Ahmad, kiongozi na Imamu wa Bwana Mir. Kwa kujibu, Hudhur[as] aliandika kwamba padri Ahmad Masihi ni mtu asiyejulikana baina ya watu, kwa hiyo haitafaa kufanya mubahala naye. Yeye anapaswa awatayarishe maaskofu wa Lahore, Calcutta, Madras na Bombay kwa kufanya mubahala nami, kwani kwa njia hii kaumu yote itaathirika na mubahala. Na kama ifikiriwe kwamba wote wanne hawawezi kujumuika pamoja basi nadhihirisha hii pia kwamba mubahala unaweza kufanyika kimaandishi pia. Litakaponifikia ombi lao, ndipo habari za mubahala zitatangazwa magazetini na makundi yote mawili, matokeo yatakuwa ni uamuzi wa mwisho. Nakubali hii pia kwa lengo la kufikisha haki kwamba kama askofu wote wanne wakikataa, basi kwa niaba ya wengine hata mubahala utafanywa kwa mmoja wao, lakini ombi hilo lapaswa litoke kutoka kwao. Kwa jambo hilo nitasubiri kwa miezi mitatu.[485] Kisha baada ya siku chache Hudhur[as] alichapisha tangazo lingine, humo aliandika:

> "Kama maaskofu hawapendi, basi wasileta majina yao kwa

[484] Al-Hakam, 7 Aprili 1906

[485] Tangazo la 5 Mai 1906 lililoandikwa katika Tablighe Risalat, J. 10 uk. 110, kimuhtasari.

kushindana, bali wakitoa kibali cha kimaandishi kupitia tangazo lililochapwa, watangaze hii tu katika gazeti la *Pioneer* au *Civil* kwamba kushindwa kwa Ahmad Masihi kutachukuliwa kushindwa kwa maaskofu wote wanne. (Katika hali hiyo nipo tayari kufanya mubahala na padri Ahmad Masihi.) Hilo pia twasema kwa sababu Ahmad Masihi si mtu anayejulikana, na mpaka maaskofu wamfanyie makamu wao, kaumu haiwezi kuathirika. Lakini, sasa jambo limewekwa wazi sana. Ni matarajio kwamba mabwana maaskofu watakubali mubahala baada ya kutafakari kikamilifu. Narudia kwamba kama maaskofu wote wanne wasikubali basi, maandishi ya Bwana Askofu wa Lahore pekee yatatosha."[486]

Baada ya kutolewa tangazo hilo, Bwana Padri alinyamaza kimya, kana kwamba alikuwa hakunena hata neno moja kwa kufanya mubahala na Hudhur[as].

HARUSI YA HADHRAT MIRZA BASHIR AHMAD, 10 MEI 1906

Imeshaandikwa mapema kwamba ndoa ya Hadhrat Mirza Bashir Ahmad ilitangazwa tarehe 12 Septemba 1902 na Bi Sarwar Sultana binti wa Hadhrat Maulana Ghulam Hasan Khan, msajili wa Peshawar, lakini harusi haikufanyika. Sasa tarehe 10 Mei 1906 Hadhrat Mir Nasir Nawab[ra], Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, Hadhrat Maulawii Seyyid Sarwar Shah, Khwaja Kamaluddin na baadhi ya ndugu wengine walienda naye Peshawar kwa harusi na wakarudi Qadian jioni, 16 Mei 1906.

DKT. ABDUL HAKIM KHAN KAONDOLEWA KATIKA JUMUIYA, MWAKA 1906

Dkt. Abdul Hakim Khan alikuwa mkazi wa kijiji cha Taravarii, Wilaya ya Karnal, na alikuwa amekwisha fanya baiati ya Hudhur[as], na katika vitabu vyake vya Tafsirul Quran na kadhalika alikwishaandika makala kumwunga mkono Hudhur[as]. Yeye kwa kutoelewa maelezo sahihi ya baadhi ya aya za Kurani Tukufu, alishika itikadi hii mbovu kwamba kumwamini Mtume Mtukufu[saw] ni njia

[486] Tangazo la 11 Mei 1906 lililoandikwa katika Tablighe Risalat, J. 10 uk. 112

rahisi ya kupata wokovu, lakini hii siyo sawa kwamba bila kumwamini yeye wokovu hauwezi kupatikana. Kama mtu akiamini umoja wa Mungu na atende vitendo vizuri na atekeleze faradhi ya kutumikia viumbe, basi huyu pia lazima atapata wokovu.

Hudhur[as] alipojua itikadi hiyo ya Bwana Daktari, akamsihi kupitia barua, lakini yeye akaendelea kuzidi katika mawazo yake, ndipo akamwondoa katika Jumuiya yake.

Aya za Kurani Tukufu alizotaja kwa kuthibitisha usahihi wa itikadi yake ni hizi:

Kwanza:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَ الَّذِينَ هَادُوا وَ النَّصَارَى وَ الصَّابِئِينَ مَنْ اٰمَنَ بِاللّٰهِ وَ الْيَوْمِ الْاٰخِرِ وَ عَمِلَ صَالِحًا فَلَهُمْ اَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ [487]

Ya pili:

بَلٰى مَنْ اَسْلَمَ وَجْهَهٗ لِلّٰهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَلَهٗ اَجْرُهٗ عِنْدَ رَبِّهٖ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ [488]

Ya tatu:

تَعَالَوْا اِلٰى كَلِمَةٍ سَوَآءٍ بَيْنَنَا وَ بَيْنَكُمْ اَنْ لَّا نَعْبُدَ اِلَّا اللّٰهَ وَ لَا نُشْرِكَ بِهٖ شَيْئًا وَّ لَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا اَرْبَابًا مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ [489]

Katika kitabu chake mashuhuri Hakikatul Wahyii[490], Hudhur[as] alieleza maelezo sahihi ya aya hizo, ambayo muhtasari wake katika maneno ya Hudhur[as] mwenyewe ni huu:

> "Katika Kurani tukufu ni suna ya Mungu kwamba katika baadhi ya sehemu maelezo marefu yanapatikana na katika baadhi ya sehemu habari inatolewa kwa ufupi. Na kwa msomaji hakuna budi atoe tafsiri ya aya yenye maana fupi isiyo kinyume cha aya zitoazo maelezo marefu. Kwa mfano, Mwenyezi Mungu Amesema waziwazi kwamba ushirikina hautasamehewa, lakini

[487] Al-Baqara, 2:63

[488] Al-Baqara, 2:113

[489] Aali Imran, 3:65

[490] Tazameni ukurasa 168

aya hii ya Kurani Tukufu إِنَّ اللّٰهَ يَغْفِرُ الذُّنُوْبَ جَمِيْعًا inaenda kinyume cha aya ile ambamo imeandikwa kwamba ushirikina hautasamehewa. Basi hiyo itakuwa kuachana na imani kwamba aya hiyo itolewe maana yake iliyo kinyume cha aya imara zilizo wazi sana." [491]

Na kuhusu aya zilizotajwa juu akasema:

"Siyo maana ya kutaja aya hizo kwamba bila kumwamini Mtume wokovu unaweza kupatikana, bali maana ndiyo hii kwamba bila kumwamini Mungu Mmoja asiye na mshirika na siku ya akhera, wokovu hauwezi kupatikana, na imani juu ya Allah inaweza kukamilika tu kwa kuwaamini mitume wake. Sababu yake ni hii kwamba hao ndio wanadhihirisha sifa Zake. Na uwepo wa kitu chochote hauthibitiki bila uwepo wa sifa zake. Kwa hiyo, pasipo elimu ya sifa za Mwenyezi Mungu, utambuzi wa Mungu hubaki mpungufu. Kwani, kwa mfano, sifa hizi za Mwenyezi Mungu kwamba Yeye Huongea, Husikia, Hujua mambo ya siri, Anao uwezo wa kurehemu na kuadhibu, inawejaze kupatikana yakini juu ya hizo bila kupitia mtume! Na kama sifa hizo zisithibitike kwa kushuhudiwa, basi hata uwepo wa Mwenyezi Mungu hauthibitiki. Katika hali hiyo, itakuwa na maana gani kumwamini Yeye. Na yule mtu anayemwamini Mungu, hana budi kuamini sifa Zake pia, na imani hiyo itamlazimisha kuwaamini manabii. Kwani, kwa mfano, kuongea kwa Mungu na kunena bila uthibitisho wa maongezi na Mungu kunawezaje kueleweka. Na waletaji Neno Lake pamoja na uhakikisho wake ni manabii tu."[492]

Kwa kuthibitisha kwamba sawa na Kurani Tukufu ni lazima kuwaamini manabii, Hudhur[as] ameleta aya 16.[493] Kwa mfano aya 5 miongoni mwa hizo zinaandikwa hapa chini:

1. قُلْ اَطِيْعُوا اللّٰهَ وَاَطِيْعُوا الرَّسُوْلَ۔

(Sura An-Nur, 24:55)

[491] Hakikatul Wahi, uk. 169, maelezo ya pembeni.

[492] Hakikatul Wahi, uk. 168-169.

[493] Hakikatul Wahi, uk. 124-130.

Tafsiri: Sema: Mtiini Allah na mtiini Mtume. Jambo hili limekubalika na ni wazi kwamba kuzihalifu amri za Mungu ni dhambi na ni sababu ya kuingia motoni. Na katika sehemu hii, kama anavyoamrisha kumtii Mungu ndivyo Anavyoamuru kumtii Mtume. Basi, mtu aipaye kisogo amri yake, anatenda dhambi ambayo adhabu yake ni jahanamu."

2. يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تُقَدِّمُوْا بَيْنَ يَدَيِ اللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَاتَّقُوا اللّٰهَ اِنَّ اللّٰهَ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ۔

(Sura Al-Hujuraat, 49:2)

Tafsiri: Enyi mlioamini, msiseme katu mkiitangulia amri ya Allah na Mtume wake, yaani, tekelezeni barabara amri za Mungu na Mtume, bali mcheni Allah msimwasi. Hakika Allah ni Mwenye kusikia, na pia Mwenye kujua.

Sasa ni dhahiri kwamba mtu ambaye akitegemea Tauhidi yake kavu (ambayo kwa kweli hiyo siyo Tauhidi), na anafikiri kuwa yeye hamhitaji Mtume[saw] na anajitenga na Mtume[saw] na kujiweka mbali naye kabisa na anazidi katika utovu wa adabu, yeye mtu huyo anamwasi Mungu na anakosa wokovu."[494]

3. كُلَّمَا اُلْقِيَ فِيْهَا فَوْجٌ سَاَلَهُمْ خَزَنَتُهَآ اَلَمْ يَاْتِكُمْ نَذِيْرٌ۔ قَالُوْا بَلٰى قَدْ جَآءَنَا نَذِيْرٌ فَكَذَّبْنَا وَ قُلْنَا مَا نَزَّلَ اللّٰهُ مِنْ شَيْءٍ۔

(Sura Al-Mulk, 67:9-10)

Maana yake: Na kundi la makafiri litakapoingia motoni, walinzi wa motoni watawauliza: "Je, hakuwafikieni Mwonyaji? Watasema: Naam! Alifika, lakini tulimkadhibisha na tukasema: Mungu Hakuteremsha kitu".

Sasa, tazameni, kwa aya hizo inathibitika wazi kwamba watu wa motoni wataingia motoni kwa sababu ya kutokubali manabii wa zama zao.[495]

4. اِنَّمَا الْمُؤْمِنُوْنَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوْا۔

(Sura Al-Hujuraat, 49:16)

[494] Hakikatul Wahyi, uk. 125

[495] Baadhi ya aya zimeshatajwa mapema pia zinazoeleza madhumuni hayo. Mwandishi

Maana yake ni kuwa waaminio ni wale waliomwamini Mungu na Mtume, na baada yake wakaimarika katika imani na hawakuingiwa na shaka.

Tazameni, katika aya hizo Mwenyezi Mungu anaweka sharti kwamba mbele ya Mungu waaminio ni wale ambao si tu wanamwamini Mungu pekee, bali wanawaamini Mungu na mitume, wote wawili. Basi, wokovu wawezaje kupatikana bila kumwamini mtume! Na bila kumwamini mtume, Umoja pekee wa Mungu utasidiaje![496]

5. إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيَقُولُونَ نُؤْمِنُ بِبَعْضٍ وَنَكْفُرُ بِبَعْضٍ وَيُرِيدُونَ أَنْ يَتَّخِذُوا بَيْنَ ذَٰلِكَ سَبِيلًا ۔

(Sura An-Nisaa: 4:151-153)

Tafsiri: Wale wanomkataa Mungu na Mitume wake, na wanataka kutofautisha baina ya Mungu na Mitume wake, na husema: Baadhi yao tutawaamini na wengine tutawakataa — yaani inatoshi kumwamini Mungu pekee au baadhi ya mitume pekee, na si lazima kumwamini Mtume pamoja na Mungu, au kuwaamini manabii wote — na wanataka kushika njia ya kati, hao ndio makafiri hasa, na tumewaandalia makafiri adhabu ifeheheshayo. Na wale wanaomwamini Mungu na Mtume wake, wala hawafarikishi baina ya Mungu na mitume — yaani hawapendi tofauti hii kwamba wamwamini Mungu tu lakini wasiwaamini mitume, wala hawapendi tofauti hii kwamba wawaamini baadhi ya mitume na kuwakataa wengine — Mungu Atawapa ujira wao.

Sasa yupo wapi Mian Abdul Hakim Khan aliyeritadi, aliyetengana nami kwa maandishi yangu hayo. Yampasa aone akifumbua macho kwamba jinsi Mungu Alivyounganisha kuwaamini Mitume kwa kumwamini Yeye. Ndani yake mna siri hii kwamba ndani ya binadamu kipaji cha kupokea Tauhidi ni kama ule moto uliofichika katika jiwe, na dhati ya mtume huwa kama ***chakmaki***[497] ambayo

[496] Hakikatul Wahyi, uk. 129

[497] Chakmaki ni jiwe gumu la aina fulani linalopigwa juu ya jiwe la kawaida kutoa moto. Kwa Kiingereza laitwa *flint*.

yatoa moto ikipigwa juu ya jiwe la kawaida. Basi haiyumkiniki kuwa moto wa Tauhidi uweze kuzalika moyoni mwa mtu bila ya *Chakmaki* ya Mtume. Mtume tu huleta Tauhidi ardhini, na kwa njia yake Tauhidi hupatikana. Mungu Haonekani, Yeye Huonyesha uso wake kwa njia ya Mtume."

Ingawaje kwa aya hizo ilithibitika waziwazi kwamba bila kumwamini Mtume, mtu hawezi kuokoka, kwani Tauhidi yaweza kupatikana kwa kumwamini Mtume tu. Tauhidi iliyobuniwa haina hakika yoyote. Lakini Abdul Hakim Khan alikuwa amezidi katika mawazo yake potevu kiasi hiki kwamba hakufaidika nayo. Na kama Hudhur[as] alivyosema katika Hakikatul Wahyi, uk. 148, kwamba "Abdul Hakim Khan amepiga muhuri juu ya kuritadi kwake hata kwamba pengine atafariki katika hali hiyo",[498] ndivyo ilivyotokea, na akafariki bila kutubu. Alifuata njia mbili za upinzani katika uhai wake. Moja, kuandika makala za upinzani na kutoa hotuba hadharani. Pili, kwa njia ya kutabiri. Na kutabiri huko alianza kwa msingi wa kitabu "Al-Wasiyyat" cha Hudhur[as]. Kwani Hudhur[as] alichapisha ndani yake habari za kufariki kwake katika muda usio mrefu, kulingana na funuo za Mungu na haiwezekani kufichika jambo hili kwa anayesoma kwa makini kwamba sawa na madhumuni za kitabu hicho, umri wa Hudhur[as] unaonekana umebaki kwa wingi ni miaka mitatu tu. Kwa msingi huo Bwana Dkt. alianza kutangaza matabiri ya kifo cha Hudhur[as].

Lakini kwa kudhihirisha kuwa yu mwongo, Mwenyezi Mungu Akazalisha sababu ya kubatilisha kila utabiri wake kwa kalamu yake mwenyewe. Kwanza kabisa Bwana Dkt., kupitia barua, alimwarifu Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin kuwa Hudhur[as] atafariki katika miaka mitatu.[499] Kisha alichapisha kwamba kifo kitatokea katika miezi 14.[500] Kisha mara ya tatu kinyume cha matabiri ya awali, alichapisha kwamba Bwana Mirza atafariki mpaka 21 Sawan[501] 1965,

[498] Hakikatul Wahyi uk. 127-128

[499] Tangazo la 16 Agosti 1906, lililoandikwa katika Tablighe Risalat, J. 10

[500] Takmila, uk.6, na Dakt. Abdul Hakim Khan

[501] Sawan ni mwezi wa 5 katika kalanda ya Bikrami, ya Kibaniani

yaani, hadi 4 Agosti 1908.[502] Kisha haraka akiufuta pia, akatoa utabiri huu wa mwisho kwamba Hudhur[as] atafariki tarehe 21 Sawan 1965, yaani 4 Agosti 1908.[503] Tuseme kuwa akifuta matabiri matatu ya awali kwa kalamau yake akaleta tarehe maalum ya 4 Agosti 1908, lakini matukio yalibatilisha utabiri wake huu pia. Hata ***Paisa Akhbar*** na ***Ahle Hadith*** na wapinzani wengine pia walikiri kubatilisha kwake. ***Paisa Akhbar*** la Lahore liliandika kwamba kama ingekuwa "mpaka 21 Sawan" badala ya "21 Sawan" katika ufunuo wa Dakt. Abdul Hakim Khan, ingekuwa vizuri sana.[504]

Na ***Ahle Hadith*** liliandika kwamba:

"Hatuweza kujizuia kusema ukweli kwamba kama Bwana Daktari angeishia hapo tu, yaani baada ya kutabiri miezi 14, kama asingeweka tarehe maalumu ya 4 Agosti 1908 ya kifo cha Bwana Mirza…, hapo leo usingeletwa upinzani ule wa kuchoma alioleta mheshimiwa mhariri wa ***Paisa Akhbar*** katika toleo lake la 27 dhidi ya ufunuo wa Bwana Daktari kwamba kama ingekuwa "mpaka 21 Sawan" badala ya "21 Sawan" ingekuwa vizuri sana.[505]

Hudhur[as], ndani ya muda aliochapisha katika kitabu chake "Al-Wasiyyat" na kinyume kabisa na tarehe aliyoweka Bwana Daktari, alifariki tarehe 26 Mei 1908. ***Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun***. Na hivyo ikadhihirika waziwazi sana kuwa Bwana Daktari yu mwongo katika utabiri wake. Sasa sikilizeni hali ya Dakt. Abdul Hakim Khan. Tarehe 30 Oktoba 1906 alichapisha ufunuo wake: "Mirza amefariki kwa maradhi ya mapafu", lakini yeye mwenyewe alikufa kwa maradhi ya mapafu. Tena alitangaza ufunuo wake kujihusu mwenyewe, "You will succeed", yaani utashinda. Na kumhusu Hudhur[as], alitabiri kwamba "Mzizi wa Mirza utang'oka."[506]

---

[502] I'lanul Hak wa Itmamul Hujja, uk.26

[503] Paisa Akhbar, 15 Mei 1908, na Ahle Hadith, 15 Mei 1908.

[504] Paisa Akhbar, 27 Mei 1908.

[505] Ahle Hadith, 12 Juni 1908

[506] I'lanul Hak, uk.7

Lakini Mwenyezi Mungu aling'olea mbali mzizi wake hata kwamba jina lake likafutika kabisa. Lakini Mungu Alimbariki Hudhur[as] kiasi hiki kwamba hakuna sehemu yoyote muhimu duniani ambapo mahadimu wake hawapo kushughulikia kutumikia Islam. *Alhamdulillahi alaa dhalika.*

NDOA YA HADHRAT MIRZA SHARIF AHMAD, 15 NOVEMBA 1906, SAWA NA 27 RAMADHAN 1324 HIJRIA

Tarehe 15 Novemba 1906, sawa na 27 Ramadhan 1324 hijria, ilitangazwa ndoa ya Hadhrat Mirza Sharif Ahmad na Bu Zainab Begam binti wa Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan wa Maler Kotla, kwa mahari ya Rupia 1,000. Hadhrat Maulana Nuruddin alitangaza ndoa hiyo katika uga wa nyumba 'Darul Barakaat, iliyokuwa juu ya paa la Nyumba ya Wageni, wakati Hudhur[as] alikuwepo. Funuo alizofunuliwa Hudhur[as] kuhusu shani ya huyo mwanaye tumeshaandika pale tulipotaja habari za kuzaliwa kwake. Hudhur[as] alitaka kwamba harusi ya Bu Zainab Begam ifanyike haraka ili apate nafasi ya kumwombea akiwa pamoja naye. Lakini Hadhrat Nawab hakuweza kujiandaa haraka, kwa hiyo harusi hiyo haikufanyika katika uhai wa Hudhur[as], bali ilifanyika baada ya kufariki kwake, tarehe 9 Mei 1909. Sherehe ya harusi ikafanyika kikawaida sana. Hadhrat Bi Nawab Mubaraka Begam anasimulia kwamba harusi ya Bu Zainab Begam ilifanyika kikawaida sana katika nyumba yetu iliyoungana na Darul Masihi. Hadhrat Amman Jan alitutumia vitu kama vile nguo na mapambo na kadhalika. Kwa vile Bwana Nawab alitaka kwamba harusi iwe kama ilivyokuwa ya Hadhrat Fatima[ra], Basi, Bi harusi alipojiandaa, Bwana Nawab akimkalisha karibu naye kamtolea nasaha. Kisha akaniambia kwamba nimpeleke kwa Hadhrat Amman Jan. Penye ngazi iliyopo katika uga wa Seyyida Ummi Nasir inayoteremeka kutoka upande wa sayyida Ummi Wasim, pale Hadhrat Amman Jan alitupokea na kampeleka Bi Harusi kwenye Darul Barakaat.[507]

[507] Ashabe Ahmad J. 2 uk. 269

ISHARA YA MUNGU KUHUSU MIAN ABDUL KARIM, MWAKA 1906

Mwanafunzi mmoja, Abdul Karim, kutoka Yadgir, wilaya Gulbarga, utawala wa Haidarabad Deccan, alikuja Qadian Darul Aman kwa masomo. Kwa bahati, aliumwa na mbwa mwenye kichaa. Naona vizuri kwamba nieleze tukio la kupona kwake kwa maneno ya Hudhur[as] tu. Hudhur[as] anasema:

> "Tulimpeleka Kasauli kwa kutibiwa. Kwa siku chache alitibiwa huko Kasauli, kisha akarudi Qadian. Baada ya kupita siku chache, alama za wazimu zikadhihirika ndani yake zinazodhihirika baada ya kuumwa na mbwa mwenye kichaa. Akaanza kuyaogopa maji, na hali ya kutisha ikapatikana. Ndipo moyo wangu ukatukuta kwa ajili ya huyo maskini aliye mbali kutoka nchi yake, na nilipata nafasi nzuri ya kumwombea. Kila mtu akafahamu kwamba huyo maskini atafariki baada ya masaa machache. Kwa kulazimika sawa na hali aliondolewa katika hosteli na kuwekwa katika nyumba nyingine kwa uangalifu sana kwa kutengwa na wengine. Na madaktari Waingereza wa Kasauli walitumiwa telegramu na wakaulizwa kwamba je, kuna tiba katika hali hiyo? Kutoka kwao jibu likaja kwa telegramu kwamba sasa hakuna tiba yake yoyote. Lakini moyo wangu ulielekea sana kumwombea kijana huyo maskini na mgeni, na rafiki zangu pia walisisitiza sana kumwombea, kwani katika hali ya ugeni kijana huyo alistahili kuhurumiwa. Na vile vile hofu ilizuka moyoni kwamba akifa huyo, kifo chake kwa sura mbaya kitasababisha maadui kufurahia kifo chake. Ndipo moyo wangu ulishikwa na uchungu na kukosa utulivu na nilipata mwelekeo mkubwa usio wa kawaida ambao si katika hiari ya mtu, bali hupatikana kutoka kwa Mungu tu. Na kama ukipatikana huo, basi kwa idhini ya Mwenyezi Mungu unaonyesha athari sana hata kwamba ni karibu mtu ahuike. Ilmuradi, hali ile ilipatikana ya mwelekeo ule uliofika keleleni na uchungu ukatawala moyo wangu wote, hapo mgonjwa yule ambaye kwa kweli alikuwa

amekufa, ndani yake zilianza kudhihiri athari za mwelekeo huo. Yeye alikuwa akiogopa maji na kukimbia mwanga, lakini sasa mara moja akaanza kupona na akasema kwamba sasa siogopi maji. Hapo akapewa maji, naye akanywa bila hofu yoyote, bali akitawadha kwa maji, akasali pia, na akalala usiku kucha na ikaondoka hali ya kuogofya, hata kwamba katika siku chache alipona kabisa. Mara moyoni mwangu mlitiliwa kwamba hali hiyo ya wazimu iliyozalika ndani yake, haikuwa ili wazimu huo umwangamize, bali ilikuwa ili ishara ya Mwenyezi Mungu idhihirike. Na watu wenye uzoefu wanasema kuwa haijaonekana duniani kwamba katika hali ambapo mtu ameumwa na mbwa mwenye kichaa na zikadhihirika alama za wazimu kisha mtu huyo akaweza kupona. Na waweza kuwa uthibitisho gani zaidi ya jambo hilo kwamba madaktari mahiri wa utaalamu huo huko Kasauli, waliowekwa na serikali kwa kutibu walioumwa na mbwa mwenye kichaa, waliandika wazi wazi kwa kujibu telegramu yetu kwamba sasa hakuna tiba yake yoyote.

Hapa iliyobaki kuandika ni kwamba nilipomwombea kijana huyo, Mungu alinitilia moyoni kwamba yapasa apewe dawa fulani. Basi nilimpa mgonjwa dawa ile mara chache. Hatimaye, mgonjwa alipona, au tuseme kwamba mfu akahuika."[508]

Baada ya tukio hilo, Mian Abdul Karim aliishi kwa miaka 28, na hatimaye katika Desemba 1934 alifariki. *Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun.*

ISHARA KUHUSU HADHRAT SETH ABDUR RAHMAN MADRASI, MEI 1906

Hadhrat Seth Abdur Rahman Madrasi alikuwa mwenye ikhlasi sana, mnyofu na mtawa. Alikuwa na maradhi ya sukari. Kwa sababu ya ugonjwa wa sukari alipopata jipu kubwa, akapata wasiwasi sana. Akamtumia Hudhur[as] telegramu kwa kuombewa. Hudhur[as] anasema:

[508] Tatimma Hakikatul Wahyi, uk. 46-47

"Kwa sababu ya maradhi yake nikawa na kiherehere na wasiwasi sana. Ulikuwa wakati wa karibu saa tatu nami nilikuwa nimekaa katika ghamu na huzuni, mara kwa lepe la usingizi kichwa changu kiliinama na papo hapo ukaja wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu: "alama za uhai". Baadaye telegram nyingine ikaja kutoka Madras kwamba sasa hali ni njema, hakuna wasiwasi."[509]

ISHARA KUHUSU HADHRAT NAWAB MUHAMMAD ALI KHAN, CHIFU WA MALER KOTLA, MWAKA 1906

Hudhur[as] anasema:

"Nawab Muhammad Ali Khan, Chifu wa Maler Kotla, pamoja na ndugu zake, alishikwa na matatizo makali. Tatizo mojawapo lilikuwa ni hili kwamba walihesabiwa kama raia chini ya mwanamfalme atakayerithi ufalme. Na walijaribu sana, lakini hawakufaulu. Na juhudi ya mwisho iliyobaki ilikuwa kwamba Nawab amwombe Gavana Mkuu kumwondolea shida, lakini kulikuwa hamna matarajio yake, kwani mahakimu wa chini walishatoa uamuzi wa mwisho dhidi yake. Katika tufani hii ya huzuni, ilivyo tabia ya mwanadamu, yeye si tu akaniomba kuwa nimwombee, bali akaahidi pia kwamba kama Mwenyezi Mungu Akimrehemu na kumwokoa katika adhabu hiyo, basi atatoa Rupia 3,000 taslimu baada ya kufaulu bila kuchelewa, kwa kusaidia Nyumba ya Wageni. Basi, baada ya maombi mengi nilifunuliwa:

"Ewe upanga, ugeuke upande mwingine"

Hapo nikamjulisha Nawab Muhammad Ali Khan kuhusu wahyi huu wa Mungu. Baadaye, Mwenyezi Mungu Alimrehemu.[510] Naye akatumia Rupia 3,000 bila kuchelewa kwa Nyumba ya Wageni.

[509] Hakikatul Wahyi, uk. 325

[510] Chashmae Maarifat, uk. 324

ISHARA KUHUSU HADHRAT MIR MUHAMMAD IS'HAK, MWAKA 1906

Mdogo wa Hadhrat Amman Jan, mwalimu wangu mheshimiwa Hadhrat Mir Muhammad Is'hak akawa mgonjwa sana katika mwaka 1906. Pamoja na homa kali alipatwa na mitoki mapajani na ikayakinika kwamba ni tauni. Hudhur[as] akapata habari, akafanya maombi, na Mwenyezi Mungu Akamponya Hadhrat Mir kimwujiza. Hudhur[as] ametaja ishara hiyo katika kitabu chake Hakikatul Wahyi, inayoandikwa hapa chini jinsi alivyoandika Hudhur[as] mwenyewe:

"Baadaye Mwenyezi Mungu Alinipa ishara nyingine ya furaha, nayo ndiyo hii kwamba katika siku zile safari moja niliomba kwamba Mwenyezi Mungu Anionyesha ishara yoyote mpya. Ndipo, kama vile ilivyochapwa katika gazeti la Badr la 30 Agosti 1906, nilifunuliwa kwamba siku hizi ishara itadhihirika. Yaani karibuni ishara itadhihirika. Basi ishara ile ilidhihirika hivi kwamba mara kadha niliota ndoto za kuogofya ambamo ilielezwa wazi wazi kwamba msiba fulani utawasibu wazao wa Mir Nasir Nawab aliye mkwe wangu. Safari moja niliota mguu wa mbuzi ukining'nia nyumbani, ulioashiria kwenye kifo cha mtu. Na safari moja niliona kwamba Dkt. Abdul Hakim Khan, daktari msaidizi mpasuaji, amesimama mlangoni, nje ya ghorofa ile ninamoishi. Hapo mtu fulani aliniambia kwamba mama Is'hak amemwita Abdul Hakim Khan aje nyumbani. (Mama Is'hak ndiye mke wa Mir Nasir Nawab, na Is'hak ni mwanaye) Na hao wote wanaishi nyumbani mwetu. Basi, nikisikia maneno yake nikajibu kwamba sitamruhusu kamwe Abdul Hakim Khan kuja nyumbani kwangu, maana hiyo ni fedheha kwetu. Hapo, yeye alipotea machoni mwangu, wala hakuingia ndani."

"Ikumbukwe kwamba katika elimu ya kuagua ndoto, waaguzi wa ndoto wameandika, na imeshuhudiwa mara nyingi, kwamba adui akiingia nyumbani mwa mtu, hutokea balaa au mauti katika nyumba ile… Ilmuradi nilipopata funuo kiasi hiki ambazo nilielewa kwazo kwamba watoto wa Bwana Mir watapata mkasa wowote, nilishughulikia kuomba dua, na yeye pamoja na

mwanaye Is'hak, na ahli zake walikwishajiandaa kwenda Lahore. Nikamwelezea ndoto hizo na kumzuia asiende Lahore, na yeye alisema kwamba bila idhini yako sitaenda kamwe. Asubuhi ya siku ya pili, Is'hak, mwanaye Bwana Mir, alishikwa na homa kali, na wasiwasi mkubwa ukaanza na ilitokea mitoki mapajani na iliyakinika kwamba hii ni tauni, kwani katika baadhi ya vijiji vya wilaya hii tauni iliishazuka. Ndipo ikajulikana kwamba hii ilikuwa ni maana ya ndoto zilizotajwa juu. Moyo wangu ukahuzunika sana, na nikawaambia watu wa nyumbani mwa Bwana Mir kwamba mimi naomba dua, nanyi mfanye toba na kuomba ghofira, kwani niliona ndotoni kwamba mmemkaribisha adui nyumbni mwenu, na hiyo inaashiria kwenye kosa fulani. Ingawa najua kwamba kifo ni kanuni ya Mungu tangu kale, lakini nikafikiria kwamba mtu akifa nyumbani mwangu kwa tauni, basi makelele yatapigwa sana kunikadhibisha. Na hapo hata kama nikileta ishara elfu pia, hata hivyo mbele ya upinzani huo hazitaleta athari yoyote. Kwani, nimeshaandika mara mamia na nimeshachapisha na nimeishawaelezea maelfu ya watu kwamba watu wote wa nyumbani mwangu watasalimika na tauni. Ilmuradi, wakati ule hali iliyokuwa ya moyo wangu siwezi kuieleza. Mara moja nikashughulikia dua, na baada ya dua nikaona jambo la ajabu la kudra kwamba katika masaa 2-3 homa ya Is'hak iliondoka kimwujiza na haikubaki hata alama ya mitoki, naye alikaa. Siyo hiyo tu, bali akaanza kutembea, kucheza na kukimbia, kana kwamba hakuwa na maradhi yoyote kamwe. Hiyo ndiyo kuhuisha wafu. Naweza kusema kwa kuapa kwamba katika kuhuisha wafu kwa Hadhrat Isa[as] kulikuwa hamna zaidi ya hiyo hata kidogo. Sasa ni hiari ya watu kupiga chuku katika miujiza yake, lakini hakika yenyewe ilikuwa ni hiyo tu. Mtu anayekufa kikweli na anaaga dunia hii, na malaika wa mauti anachukua roho yake, huyo harudi tena kabisa. Angalieni, Mwenyezi Mungu Anasema katika Kurani Tukufu: فَيُمْسِكُ الَّتِيْ قَضٰى عَلَيْهَا

الْمَوْتَ"[511]

BAADHI YA MATUKIO MBALI MBALI YA MWAKA 1906

Katika mwaka huo baadhi ya mipango ya awali ya Bahishti Makbara ilipangwa. Sadr Anjuman Ahmadiyya Qadian pia ilianzishwa mwaka huo. Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad alipata mtoto wa kwanza katika mwaka huo aitwaye Nasiir Ahmad aliyefariki haraka, na kadha wa kadha.

VITABU VYA MWAKA 1906

3. **Dhamima Al-Wasiyyat:** Katika Dhamima hii (Nyongeza), baadhi ya masharti yameandikwa kuhusu wafanyao wasia, mengine kuhusu Anjuman na mengine kuhusu kuleta maiti kutoka nje. Na mwishoni Hudhur[as] amewahimiza wanajumuiya kufanya wasia kwa maneno yenye uchungu.
4. **Chashmae Masihi:** Tarehe 9 Machi 1906, Hudhur[as] alichapisha kitabu (Chashmae Masihi). Katika kitabu hicho, Hudhur[as] amejibu kwa njia nyepesi sana kitabu cha Wakristo "Yanaabi'ul Islam". Sababu ya kuandika kitabu hicho ni kwamba mtu fulani[512] wa ukoo wa Ki-Nawab mwenye heshima sana, wa Bareilly (U.P.) alimwandikia Hudhur[as] kwamba kwa kusoma kitabu cha Wakristo "Yanaabiul Islam" nimepata shaka na wasiwasi sana juu ya Islam. Hudhur[as] akimsihi ameandika jibu la "Yanaabiul Islam".
5. **Tajalliyate Ilahiyya**: Tarehe 15 Machi 1906, Hudhur[as] alianza kuandika kitabu kiitwacho "Tajalliyate Ilahiyya". Na humo alitaka kuandika kwa kirefu juu ya utabiri huu wa Mwenyezi Mungu: "Nitakuonyesha mng'ao wa ishara hii mara tano." Katika kitabu hicho, Hudhur[as] alianza kujadili juu ya hekima ya matabiri ya adhabu, lakini ni sikitiko kwamba kwa baadhi ya

[511] Hakikatul Wahyi, uk. 327-329

[512] Huyo alikuwa akionana na Hadhrat Hafidh Seyyid Mukhtar Ahmad Shah Jahanpuri alipokuwa akifika Bareilly na aliafikiana na itikadi za Jumuiya Ahmadiyya. Lakini bado alikuwa hajajiunga na Jumuiya akafariki. Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun. (Mwandishi)

vizuizi kitabu hicho hakikukamilika. Na kurasa 32 zilizochapwa awali zikachapwa kwa sura ya kitabu cha saizi ndogo kwa kuwekwa jalada baada ya kifo cha Hudhur[as].

SAADULLAH LUDHIANAWII KAANGAMIA, 3 JANUARI 1907

Katika Ludhiana kulikuwa na mtu mmoja Mwislamu mpya aitwaye Saadullah aliyejua Kiarabu pia kiasi fulani. Yeye alikuwa katika safu ya mbele daima kwa kumpinga Hudhur[as]. Alikuwa akitumia lugha chafu sana ambayo hata watu waovu sana pia hawaitumii. Aliandika kitabu kimoja kiitwcho "Kimondo king'aracho cha kumwangukia masihi mwongo," ambacho beti mbili kutoka katika kitabu hicho ni hizi:

اخذ یمین و قطع وتین است بھر تو　　بے رونقی و سلسلہ ہائے مزوّری

اکنوں بہ اصطلاحِ شما نام ابتلا است　　آخر بروزِ حشر و بہ این دار خاسری

Ndani ya beti hizo alimwandikia Hudhur[as] kwamba "Umepangiwa na Mungu kwamba Yeye Atakushika na Atakata mshipa wako wa uhai, ndipo baada ya kifo chako Jumuiya yako, iliyo ya uongo kabisa, itaangamia. Na ingawa nyinyi mwasema kwamba mitihani pia hutokea, lakini hatimaye siku ya kufufuka pia na katika dunia hii pia utashindwa na utafariki bila mafanikio."

Baadaye Saadullah aliendelea kuzidi katika mdomo mchafu na matusi. Hatimaye, tarehe 16 Septemba 1894 alichapisha kuhusu Hudhur[as] maandishi machafu sana ambamo alimwita Hudhur[as] kuwa mkiwa. (Mungu Apishe mbali). Kitendo chake hicho, akieleza Hudhur kwa huzuni sana mbele ya Mwenyezi Mungu akaomba dua. Na yale Mwenyezi Mungu Aliyomdhihirishia kuhusu huyo, aliyachapisha kwa sharti ya zawadi ya rupia elfu tatu, katika tangazo la tatu miongoni mwa matangazo yaliyomo katika "Anwarul Islam", kwa maneno haya:

"Endelea kupigana na haki. Ee mzoga, hatimaye utaona kwamba mwisho wako utakuwaje. Ee adui wa Mungu, hupigani nami, bali unapigana na Mungu. Wallahi, sasa hivi, 29 Septemba 1894, nimefunuliwa kuhusu wewe: إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ Tafsiri ya ibara

> hii ya ufunuo ni kwamba Saadullah anayekuita mkiwa na anadai kwamba kizazi chako na baraka zingine zitakatika, haitafanyika hivyo kamwe, bali yeye mwenyewe atabaki mkiwa."[513]

Baada ya uchapaji wa maandishi hayo wana watatu walizaliwa kwa Hudhur[as], lakini Saadullah Mwislamu mpya hakujaaliwa hata mwana mmoja. Na watoto waliokuwa wamezaliwa hapo kabla hao wote walikuwa wamefariki mapema. Basi, anadhihirisha huzuni yake katika beti hizi alizoandika katika dua yake iitwao "Kadhil Hajaat":

> "Yaani, Ewe Usiyehitaji kitu, Wewe ulinipa kizazi, lakini baadhi yao miongoni mwao uliwachukua. Sasa unifurahishe moyo wangu kwa kunipa badala yao watoto wengine wazuri na kwa rehema yako uniondolee huzuni. Ewe Mwenye hisani, Uburudishe macho yangu kwa wake na watoto wangu. Moyo wangu umekatika vipande vipande kwa huzuni ya watoto wangu waliofariki."

Kwa kusoma beti hizo zenye kutia uchungu za Saadullah Mwislamu mpya, kila mtu anaweza kufikiri kwamba huzuni na uchungu kiasi gani ulijaa moyoni mwake kwa kukosekana watoto na kufa kwa waliokuwepo, na alikuwa hana utulivu kwa huzuni kiasi gani! Lakini hakuweza kuondolewa huzuni hiyo, na kwa kuomba pia kwa unyenyekevu sana kwa miaka na miaka hakupata mtoto. Na wakati Hudhur[as] aliposema hayo yaliyoelezwa hapo juu, yeye alikuwa na mwana mmoja aitwaye Mahmud, mwenye umri wa miaka 14-15. Saadullah akaishi baadaye hadi miaka 12, lakini hakupata mtoto. Na yule mtoto aliyekuwepo juu ya kuwa umri mkubwa hakuoa pengine alikuwa hafai kuoa, au kwa sababu nyingine hakupata kuoa, hata kwamba si masheikh wengine tu, bali baadhi ya Waahmadiyya pia wakamshauri amfanye mwanaye kuoa. Basi alipokuwa mwenye umri wa miaka 29 au zaidi, babake akamchumbia mwanaye bintiye Haji Abdur Rahim. Saadaullahi mwenyewe akafanya matayariso yote ya arusi ya mwanaye, lakini hakuweza kushiriki katika furaha ya ndoa ya mwanaye wa pekee, bali akafa kabla ya ndoa kwa tauni tarehe 3

[513] Kutoka tangazo la 5 Oktoba 1894 lililomo katika "Anwarul Islam"

Januari 1907. Lakini ni kudra ya ajabu ya Mungu kwamba mwanaye Saadullah hakujaliwa kizazi kutokana na ndoa hiyo. Baada ya kupita muda mrefu na kwa kukata tamaa kupata kizazi, Maulawii Thanaullah na wengine walianza kujaribu kuwa afunge ndoa yake ya pili, lakini aliendelea kukataa. Lakini kwa kufikiria huenda akapata kizazi kwa ndoa ya pili, alilazimishwa kuoa mara ya pili, lakini matarajio hayo hayakutimia hata kwa ndoa hii pia, na mwana huyo wa Saadullah akafariki kijijini Kom Kalaan, Wilaya ya Ludhiana tarehe 12 Julai 1926 bila kupata kizazi. Kama kijana yule angefariki katika utoto wake, mtu angeweza kusema kwamba hiyo ilikuwa ni bahati tu. Lakini baada ya utabiri, kwanza kwa miaka 15 baba hakupata kizazi, na kijana aliyekuwepo naye hakupata mtoto juu ya kuoa mara mbili ili kama hakupata kizazi kutoka kwa mmoja apate kutoka kwa wa pili, na utabiri kumhusu Saadullah kuwa mkiwa usitimie. Lakini juhudi zote zikapotea bure, na yeye pia hakupata kizazi. Na yule aliyetabiriwa kuwa atakuwa mkiwa, ukiwa wake haukuweza kufichwa na mwenye kujaribu kuficha na akathibitika kuwa mkiwa. *Jifunzeni enyi wenye macho.*

Kijana wa Saadullah alikuwa mchoraji ramani katika idara ya mifereji na kwa muda mrefu alikaa kikazi katika Sheikhupura na Lyallpur. Maulawii Malik Muhammad Shafii‘, mwanajumuiya mwenye ikhlasi sana anayeishi siku hizi katika Nankana Sahib, alinihadithia habari hii mara nyingi kwamba kijana wa Saadullah alikuwa anamlea msichana mmoja. Yule msichana alikuwa akimwita baba, na yeye alikuwa akisema kwamba huyo ni binti yangu. Lakini sisi tulikuwa tukimwambia kwamba Hudhur[as] alifunuliwa kuwa babako atakuwa mkiwa, hivyo inawezekanaje kuwa huyo ni binti yako, yeye si binti yako kamwe. Kama u mkweli katika jambo hili, basi twende Ludhiana, tutatoa sisi nauli yako ya kuenda na kurudi na matumizi mengine yote, na ikithibitika kwamba yu binti yako, basi tutakupa zawadi kubwa pia, lakini hakuridhia kuenda nasi Ludhiana juu ya kuomba kwetu mara kwa mara. Hatimaye, kwa kujua hali halisi tuliwaandikia wanajumuiya wetu wa huko Ludhiana. Jibu likaja kutoka huko kwamba kijana wa Saadullah anasema uongo, yu binti wa dada ya mkewe. Tulipomwambia kuhusu jibu hilo, akanyamaa

kimya kabisa kana kwamba hana roho mwilini.

HUDHUR[AS] AELEZA ISHARA KUHUSU SAADULLAH, NOVEMBA 1906

Kwa kuimarisha imani ya wasomaji watukufu twatoa hapa chini tafsiri ya ibara ya Kiarabu ya sehemu ya mwisho ya Hakikatul Wahyi, yaani "Al-Istiftaa". Katika ibara hiyo Hudhur[as] amechapisha maelezo ya habari za Saadullah kufariki akiwa mkiwa. Hudhur[as] anasema:

> "Matukio ya udhia mwingi wa wenye kuudhi ni kwamba Mwenyezi Mungu Alionyesha kuwapitia hao baadhi ya ishara. Kwa kuelewesha watafutao haki tumeshataja watu hao katika Hakikatul Wahyi. Na tukio jipya la aina hiyo ni la kifo cha mtu mmoja, lililotokea siku hizi katika Dhulkaada 1324 hijria. Mtu mmoja alikuwa akitumia lugha chafu dhidi yangu na alikuwa akinilaani, aitwaye Saadullah[514] (Ludhianawii). Mtu huyo alikuwa akiumiza sana kwa lugha yake chafu sawa sawa na mkuki. Wakati matusi yake yalipofikia upeo wake na akawashinda wote katika kuudhi, Mwenyezi Mungu Akaniarifu kudra yake kuhusu kufa kwake haraka na kudhalilika na kuwa mkiwa, na Akasema: إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ . Yaani, adui wako huyo atakuwa mkiwa na atashindwa kabisa. Nikatangaza wahyi huu wa Mungu baina ya watu. Baadaye, Mwenyezi Mungu Akadhihirisha ukweli wa wahyi wake Alionifunulia na Akatimiza kauli yake. Kwa hiyo, nikataka kuieneza habari hii baina ya watu kwa kutoa maelezo yake, lakini wakili mmoja aliye katika Jumuiya yangu alinizuia nisichapishe. Akadhihirisha hofu na hatari yake na akasema kwamba kwa kutangaza, jambo hili lazima litawafikia watawala. Hapo haitakuwa njia yoyote ya kusalimika na pigo la sheria na adhabu, na matatizo yataanzia mfululizo yasiyoishia. Na baada ya kupata taabu kubwa ya kesi matokeo yake yatakayokuwa ni dhahiri, na katika hali hiyo lazima serikali itaadhibu. Kwa hiyo,

[514] Saadullah Ludhianawii ndiye yule ambaye kuhusu lugha yake chafu Dkt. Sir Muhammad Iqbal aliyekuwepo katika zama zile huko Murray College Sialkot, alilazimika kuandika shairi refu ambalo ubeti wake wa kwanza ni huu: Ewe Saad, nimeshaona mdomo wako mchafu, utaheshimika sana baina ya matopasi.

ni bora kujitahadhari ufiche wahyi huu. Nikamwambia kwamba nionavyo mimi njia sahihi ni kwamba heshima ya ufunuo wa Mungu itangulizwe, na kwangu mimi kuuficha ni uasi wa Mungu na ni kitendo duni. Na minghairi ya Mwenyezi Mungu hakuna yeyote awezaye kudhuru. Na baada ya amri ya Mungu, siogopi onyo la watawala. Naam, tutamwomba Mwenyezi Mungu Aliye chanzo cha fadhili na rehema kwamba Atuhifadhi na kila msiba na fitina. Na kama imeshapangwa katika kudra kwamba tupate msiba huo, basi twaridhika juu ya maisha hayo ya dhila. Nasema kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba Hatamfanya mtu huyo mkorofi anitawale; bali mimi niliye mtumishi Wake ninayetaka kimbilio Kwake, Atanilida na shari yake kwa kumtia katika balaa fulani. Aliposikia kauli yangu hii mwenye ikhlasi wa pekee, mwanachuoni, mahiri wa elimu ya dini, Maulawii Hakim Nuruduin, mara moja alitamka hadithi hii: رُبَّ اَشْعَثَ اَغْبَرَ . Kwa kusikiliza jibu langu na kusikiliza Hadithi hii kutoka kwa Bwana Maulawii, wanajumuiya walipata kutulia, na wakasema kuwa alikosea wakili yule aliyenihofisha, na hawakujaali kuhofisha kwake. Baadaye, kwa siku 2-3 nilimwomba Mwenyezi Mungu Amfishe Saadullah. Baada yake Mwenyezi Mungu Akaniletea wahyi huu: رُبَّ اَشْعَثَ اَغْبَرَ لَوْ اَقْسَمَ عَلَى اللهِ لَاَبَرَّهٗ , Yaani baadhi ya watu ambao machoni mwa watu ni wenye nywele timtimu, zenye mavumbi, lakini mbele ya Mwenyezi Mungu wanayo daraja ile kwamba wakiapa kuhusu jambo fulani, Mwenyezi Mungu lazima hukitimiza kiapo chao. Na muradi wake ulikuwa ni kwamba Mwenyezi Mungu Atakulinda na shari ya mtu huyo. Naapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba zilipofika siku chache tu, ilifika habari ya kifo chake.[515]

KIFO CHA MMILIKI NA MHARIRI WA GAZETI 'SHUBH CHINTAK'

Kwa vile kusudio la kutumwa kwa Hudhur[as] lilikuwa kutangaza dini ya haki, ambalo Wakristo na Waariya hawakulipenda, kwani kaumu hizo zilidhani kwamba kama mtu huyo asingekuwepo, tungewafanya

[515] Al-Istiftaa, uk. 35-36, Tafsiri kutoka Kiarabu

Waislamu wa India katika muda mfupi kuwa Wakristo au Waariya, kwa hiyo watu hao walikuwa maadui zake wakali. Hapa twataka kutaja Aria Samaj ya Qadian. Watu hao wakachagua njia hii kwa kufikisha uadui wake keleleni kwamba katika mwaka 1906 walianzisha kutoa gazeti moja liitwalo "Shubh Chintak" kutoka Qadian. Na katika gazeti hilo walianzisha propaganda ya hali ya juu ya uongo ule dhidi ya Hudhur[as] na Jumuiya yake ambao Mungu tu Atulinde na huo. Na watu watatu hasa walikuwa katika mstari wa mbele katika kusambaza uongo huo, yaani (1) Ichar Chand, Mmiliki na Meneja wa gazeti (2) Pandit Somraj, Mhariri wa gazeti (3) Bhagat Ram, msaidizi wao katika kila jambo.[516]

LALA SHARMPAT NA MALAVAMAL WALIKIMBIA KUAPA

Katika siku chache watu hao walipata nguvu kiasi hiki kwamba wakawachanganisha nao Lala Malavamal na Lala Sharmpat, Waaria wa zamani wa Qadian waliokuwa mashahidi wa ishara nyingi za Hudhur[as]. Na wakachapisha katika gazeti lao kauli ya Lala Sharmpat kwamba Lala Sharmpat anasema kwamba hatukuona ishara yoyote ya kimbingu ya Bwana Mirza.

Hudhur[as] aliposoma kauli hiyo ya Lala Sharmpat, Hudhur[as] aliudhika sana. Basi, katika kitabu kiitwacho "Qadian Ke Aria Aur Ham" kilichokuwa kikiandikwa siku zile, Hudhur[as] aliandika:

> "Matabiri haya machache nayaeleza wakati huu hapa kama mfano, nami nasema kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba maelezo haya yote ni sahihi, na Lala Sharmpat ameishasikia mara kadha. Na kama nimesema uongo, basi Mungu Aniteremshie adhabu mimi na wanangu katika mwaka mmoja. ***Amin, na Laana ya Mungu iwe juu ya waongo***. Kadhalika Sharmpat pia anapaswa kwamba kinyume cha kiapo changu hicho aape na aseme kwamba kama nimesema uongo katika kiapo changu basi Mungu Aniteremshie adhabu mimi na watoto wangu katika mwaka mmoja. ***Amin, na Laana ya Mungu***

[516] Ichar Chand na Bhagat Ram walikuwa ndugu, wazazi wamoja.

iwe juu ya waongo.”[517]

Baadaye aliandika baadhi ya ishara kwa Lala Malavamal ambazo yeye alikuwa shahidi wake, na kisha akaandika:

> “Nasema kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba maneno haya yote ni sahihi, na kama hayo ni uongo, basi Mungu Aniteremshie adhabu mimi na wanangu katika mwaka mmoja na Atuadhibu kwa kuongopa. *Amin, na Laana ya Mungu iwe juu ya waongo.* Kadhalika Malavamal anapaswa kwamba asiwe na mapenzi ya dunia iliyo kwa siku chache. Na kama anakana maneno hayo, basi aape sawa nami kwamba hayo yote ni uzushi; na kama mambo hayo ni ya kweli, basi Mungu Aniteremshie adhabu mimi na watoto wangu katika mwaka mmoja. *Amin, na Laana ya Mungu iwe juu ya waongo.”* [518]

Kwa kutangazwa kauli hiyo ya Hudhur[as], Lala Sharmpat na Lala Malavamal walinyamaza kabisa. Ni dhahiri kwamba Waaria walifanya juu chini kuwahamasisha, kwani hili lilikuwa ni jambo ambalo lilikuwa kwao pigo kubwa sana. Lakini, Lala Sharmpat na Lala Malavamal hawakukubali kwa njia yoyote kwamba waape sawa na kiapo kilichoombwa na Hudhur[as] au kutoa jawabu lolote. Na mwenendo wao huu usio wa kawadia ulithibitisha kuwa sahihi mara ya tena kwamba Hudhur[as] alipoandika kwa Lala Sharmpat na Lala Malavamal ni mashahidi wa ishara zake na zile alizozitaja mara kwa mara katika Tiryaqul Quluub na vitabu vinginevyo lazima hao walikuwa mashahidi wa ishara hizo. Waila wakati wa hali hiyo ngumu iliyotokea kwa kuambiwa na Hudhur[as] kuapa, hawangeweza kunyamaza. Kwa matokea ya kimya hicho walisalimika na adhabu ya Mungu. Lakini wafanyakazi watatu wa “Gazeti Shubh Chintak” waliotajwa hapo juu wakafa kwa tauni kwa sababu ya kuzidi katika ujanja na ukorofi.[519]

---

[517] Qadian Ke Aria Aur Ham, uk. 36

[518] Qadian ke Aria Aur Ham, uk. 37-38

[519] Mheshimiwa Mirza Islamullah anasimulia kwamba Pandit Somraj aliposhikwa na tauni, alimwita Hadhrat Hakim Maulawii Abdullah Bismil kwa kutibiwa. Bwana Hakim alipomwuliza Hudhur[as], basi alijibu kwamba mtibu lakini

MAULAWII THANAULLAH AMRITSARI KAUOGOPA MUBAHALA NA KUKATAA

Wasomaji pengine wanakumbuka kwamba tumeshaeleza katika matukio ya mwaka 1896 kuhusu changamoto ya mubahala ambayo Hudhur[as] aliwatupia maulamaa na masufii. Katika changamoto hiyo, Hudhur[as] aliwaita kwa mubahala masheikh 58 maarufu wa India na masufii 49 mashuhuri akiandika majina yao. Na kati ya majina ya maulamaa, jina la 11 lilikuwa la Maulawii Thanaullah pia. Jinsi maulamaa wote wasivyokuwa na ushujaa kuingia uwanjani, ndivyo alivyokuwa Maulawii Thanaullah pia. Lakini katika jambo hilo Maulawii Thanaullah alikuwa tofauti kuliko maulamaa wengine wote. Yeye kinyume cha baadhi ya maulamaa hakunyamaza baada ya kuleta udhuru mbovu kuhusu kufanya mubahala, bali akashika njia ya kauleni na akaendelea kuishikilia na hakuiacha kamwe. Na njia ile ilikuwa ni kwamba hakutaka kwa moyo kufanya mubahala na Hudhur[as], lakini alitaka kuwadhihirishia watu kwamba nipo tayari kabisa kufanya mubahala. Alipoulizwa na wafuasi wake kwa nini hufanyi mubahala, unapaswa kufanya mubahala, alikuwa anadhihirisha nipo tayari kufanya mubahala. Na baadhi ya wakati alikuwa akipiga kelele za 'mubahala', 'mubahala', kwa fahari. Lakini, alipokuwa anajibiwa na Hudhur[as], basi alikuwa hana aibu kusema kwamba sijasema kamwe kufanya mubahala. Na sio kwamba alikuwa akikanusha tu, bali akiacha kabisa uungwana na ubinadamu alikuwa akitusi sana. Hapa chini inaandikwa mifano yake michache. Bwana Maulawii, sawa na mwenendo wake akawadhihirishia marafiki zake kuwa yupo tayari kwa mubahala, kwani marafiki zake walikuwa wakimwambia kwa midomo pia na kwa maandishi pia kufanya mubahala. Na asipoishia kudhihirisha kwa mdomo tu akamwandikia pia rafiki yake mmoja kuwa yupo tayari kufanya mubahala. Maandishi hayo yalipomfikia Hudhur[as], yeye katika kitabu chake ***Ijaze Ahmadi*** alichokuwa anakiandika siku zile, akaandika:

> "Nimesikia, bali nimeona maandishi pia ya Maulawii Thanaullah Amritsari yaliyotiliwa saini yake ambamo anaomba

hatapona. Basi juu ya kutibiwa, jioni hiyo hiyo akafa.

> kwamba napenda kwa moyo kwa uamuzi wa njia hii kwamba sisi wawili, yaani mimi na yeye, tuombe dua kwamba kati yetu wawili yule aliye mwongo afe katika uhai wa mkweli… Kama Maulawii Thanaullah amedhihirisha matakwa yake hayo kwa moyo, sio kwa unafiki, basi kuna nini iliyo bora kuliko hiyo. Yeye atafanya hisani kubwa juu ya umati huu katika zama hizi za mafarakano kwamba akiwa shujaa atapata uamuzi kati ya haki na batili kwa njia hizo mbili. Ameleta pendekezo zuri. Sasa ni bora abaki imara juu yake."[520]

Mbele kidogo Hudhur[as] aliandika:

> "Kama yeye (Maulawii Thanaullah) akiwa tayari kutekeleza mwito huu kuwa mwongo afe kabla ya mkweli, basi lazima yeye atakufa kabla."[521]

Baada ya kuchapwa kitabu hiki cha Hudhur[as], Bwana Maulawii hakutaja kuandika maandishi kwa kufanya mubahala wake, na kwa kujibu maandishi ya Hudhur[as] aliandika hii tu:

> "Kwa vile mimi sio kwa hakika, wala kama wewe, nabii, mtume au mwana wa Mungu au mpokeaji wahyi, kwa hiyo siwezi kujasiri kufanya shindano la namna hii."[522]

Lakini juu ya hayo baada ya muda fulani Bwana Maulawii aliandika tena:

> "Kwa kufuata aya ya pili (yaani قُلْ تَعَالَوْا نَدْعُ أَبْنَآءَنَا) tupo tayari. Hata sasa nipo tayari kufanya mubahala wa aina hii unaothibitika kutokana na aya iliyoandikwa ambayo imekubaliwa na Bwana Mirza mwenyewe."[523]

Baada ya maandishi hayo ya Bwana Maulawii, Hudhur[as] alipochapisha katika Februari 1907 kitabu chake "Qadian Ke Aria

[520] Ijaze Ahmdi, uk. 14

[521] Ijaze Ahmdi, uk. 37

[522] Ilhamate Mirza, chapa ya mara ya pili, uk. 85

[523] Ahle Hadith, 22 Juni 1906, uk. 4

Aur Ham" dhidi ya Waaria wa Qadian, na ndani yake aliwaita Lala Sharmpat na Lala Malavamal waje kuapa, basi nakala moja ya kijitabu hicho alimtumia Maulawii Thanaullah pia, ambacho kuhusu hicho mhariri wa Al-Hakam aliandika:

> "Nakala moja ya kijitabu hicho imetumwa kwa Maulawii Thanaullah Amritsari pia. Jinsi Waaria wa Qadian walivyokadhibisha wakiona ishara na bado wanakadhibisha, katika kijitabu hicho mubahala umefanywa nao… Na kama Thanaullah hajaiona ishara ya kimwujiza ya ukweli, basi yeye pia ajaribu kwa kuapa, ili ijulikane kwamba Mwenyezi Mungu Anamsaidia nani na Anasadikisha kiapo cha nani."[524]

Kwa kujibu maandishi ya mhariri wa Al-Hakam, Maulawii Thanaullah Amritsari akaandika:

> "Enyi Wamirzai, njooni kama m wakweli, na mleteni kiongozi wenu. Kipo kiwanja kile kile cha sala ya Idi cha Amritsar ambapo zamani mlifedheheka kwa kufanya mubahala na Sufii Abdul Hak Ghaznawii. Na kama si Amritsar, basi njooni huko Batala, mambo yafanyike hadharani, lakini maelezo na ufafanuzi wa matokeo yake mpate kwanza kutoka kwa Karishna wa Qadian. Na mleteni mbele yetu yule aliyetuita kwa mubahala katika kijitabu chake "Anjame Atham".[525]

Juu ya hayo, usemi huu wa Bwana Maulawii kwamba sijasema kufanya mubahala ni porojo na batili kabisa hata kwamba hakuna haja ya kueleza. Hii ni kweli kwamba yeye hakuwa siku yoyote tayari kamwe kwa moyo kufanya mubahala, lakini kwa kuwadanganya marafiki zake, lazima akajifanya kwamba yupo tayari kwa mubahala. Kama hilo si kweli, basi kwa lengo gani akaandika, "Kipo kiwanja kile kile cha sala ya Idi cha Amritsar ambapo zamani mlifedheheka kwa kufanya mubahala na Sufii Abdul Hak Ghaznawii… Na mleteni mbele yetu yule aliyetuita kwa mubahala katika kijitabu chake Anjame Atham".

[524] Al-Hakam, 17 Machi 1907

[525] Ahl Hadith, 29 Machi 1907

Kwa vyovyote, Hudhur[as] alipopata habari ya maandishi ya juu ya Maulawii Thanaullah Amritsari aliyochapisha katika Ahle Hadith la 29 Machi 1907, Hudhur[as] alimwambia Hadhrat Mufti Muhammad Sadik kuandika jibu lake. Hadhrat Mufti aliandika:

"Kwa mubahala changamoto ya Maulawii Thanaullah Amritsari imekubaliwa."

"Imeandikwa kwa amri ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as]."

Chini ya kichwa hicho cha habari, kwanza maandishi ya Maulawii Thanaullah yalinukuliwa, kisha jibu lilitolewa ambalo ni refu, kwa hiyo twaandika muhtasari wake ambao ndio huu:

"Kwa kujibu makala hiyo nampa habari njema Maulawii Thanaullah kwamba Hudhur[as] amekubali changamoto yake. Anaweza kusema kwa kuapa kwamba mtu huyo ni mwongo katika madai yake na bila shaka aseme kwamba kama mimi ni mwongo katika jambo hilo basi laana ya Mungu iwe juu ya waongo. Na zaidi ya hayo, ana hiari ya kujiombea mauti na kadhalika adhabu yoyote aitakayo yeye akiwa mwongo... Hata hivyo, Hudhur[as] akimhurumia akasema kwamba mubahala huu uwe baada ya siku chache, wakati kitabu chetu Hakikatil Wahyi kitakapoishachapishwa… Pamoja na kitabu hicho litakuwepo tangazo pia kutoka kwetu ambamo tutadhihirisha kwamba tumeshakubali changamoto ya mubahala ya Maulawii Thanaullah. Na kwanza twaapa kwamba funuo zote tulizoandika katika kitabu hicho ni kutoka kwa Mungu.

Na kama ni uzushi wetu, basi laana ya Mungu iwe juu ya waongo. Kadhalika Maulawii Thanaullah pia baada ya kusoma tangazo na kitabu aandike kwa kuapa kwa kupitia tangazo la kuchapwa kwamba 'nimeshasoma kitabu hiki kwa makini kutoka mwanzo mpaka mwisho, na kwamba funuo zilizomo ndani yake sio kutoka kwa Mungu bali ni uzushi wa Mirza Ghulam Ahmad, na kama mimi ni mwongo kusema hivyo, basi laana ya Mungu iwe juu ya waongo. Na pamoja na hayo, ajiombee kwa Mungu adhabu yoyote atakayo kwake. Baada ya

> kuchapishwa matangazo hayo, Mwenyezi Mungu mwenyewe Ataamua na Atapambanua kati ya mkweli na mwongo…
>
> Twaamini kwamba kama Maulawii Thanaullah kwa ujanja wake hakuepa mubahala huo, basi Mwenyezi Mungu lazima Atadhihirisha kwa Maulawii huyo ishara itakayopambanua kikamilifu kati ya ukweli na uongo… Natumai kwamba sasa Maulawii Thanaullah hatasikia haja ya kutafuta njia za kuukimbia mubahala aliopendekeza yeye mwenyewe."[526]

Aliyokuwa ameandika Bwana Maulawii, Hadhrat Mufti alijibu kikamilifu na akaleta urahisi huu pia kwamba mubahala uwe kimaandishi. Lakini Maulawii Thanaullah kwa kuwaonyesha tu watu akiandika katika maandishi yake maneno haya pia kwamba: "Enyi Wamirzai, njooni kama m wakweli na mleteni kiongozi wenu. Kipo kiwanja kile kile cha Idi cha Amritsar ambapo zamani mlifedheheka kwa kufanya mubahala na Sufii Abdul Hak Ghaznawii." Kwa hiyo, Hadhrat Mufti alitoa pendekezo lake juu yake pia kwamba:

> "Lakini, kama upo tayari kwamba mubahala uwe kwa mdomo kwa kusimama ana kwa ana, hapo waweza kuja Qadian na waweza kuleta pamoja nawe mpaka watu kumi. Nasi twaweza kukupa matumizi ya safari yako mpaka rupia 50 baada ya kuja hapa na kufanya mubahala. Lakini jambo hili litakuwa lazima katika hali yote kwamba kabla ya mubahala masharti yataandikwa kati ya makundi mawili. Na maneno ya mubahala yakiandikwa yatawekewa saini za makundi mawili na za mashahidi."[527]

Baada ya jibu la Hadhrat Mufti kwa niaba ya Hudhur[as], Maulawii Thanaullah alichapisha tarehe 12 Aprili 1907 matoleo mawili pamoja ya 12 na 19 Aprili 1907 ambamo Bwana Maulawii tena aliandika kwamba:

> "Sijakuita kwa mubahala, bali nipo tayari kwa kuapa lakini unaiita mubahala, ilihali mubahala ndio makundi mawili

[526] Badr, 4 Aprili 1907

[527] Badr, 4 Aprili 1907

kuapiana. Nimesema kuapa, sijasema kufanya mubahala. Kiapo ni kitu kingine na mubahala ni kitu kingine."[528]

Wakati ilipodhihirika kwamba Bwana Maulawii anarudia mara kwa mara jambo lile lile lisilofaa kwamba ataendelea kudhihirisha kuwa yu tayari kwa mubahala, lakini hatakuja kamwe katika uwanja wa mubahala, hapo Hudhur[as] alichapisha dua ya mubahala kutoka kwake kwa kichwa cha habari "Kwa Maulawii Thanaullah uamuzi wa mwisho", akiona kwamba si lazima kumtumia Hakikatul Wahyi. Na alitaka kwamba Bwana Maulawii kwa kujibu aandike chochote kutoka kwake chini ya maandishi hayo kama dua ya mubahala na aichapishe katika gazeti lake. Dua ile ya Hudhur[as] ndiyo ifuatayo:

"Uamuzi wa mwisho kwa Maulawii Thanaullah"

Kwa Maulawii Thanaullah, amani iwe juu ya afuataye mwongozo.

Tangu muda fulani, katika gazeti lako, Ahle Hadith, nakadhibishwa na kuitwa fasiki. Daima unaniita katika gazeti lako kama mtu aliyekataliwa na Mungu, mwongo, dajali na mfisadi. Na unatangaza duniani kwamba mtu huyo ni mzushi, mwongo na dajali, na kwamba madai ya mtu huyo ya kuwa Masihi Mau'udi ni uzushi mtupu. Nimeudhika sana nawe na nikaendelea kusubiri. Lakini kwa vile naona kwamba nimetumwa kwa kueneza haki, na ukinizushia uzushi mwingi unaizuia dunia kuja kwangu, na unanitukana na kutuhumu na kutumia maneno makali ambayo hakuna neno kali kuliko hayo. Kama mimi ni mwongo na mzushi, jinsi unavyonitaja mara nyingi katika kila toleo lako, basi nitakufa katika uhai wako. Kwani najua kwamba mfisadi na mwongo hapati umri mrefu, na hatimaye anafariki kwa dhila na majuto katika uhai wa maadui zake, na ni bora afe ili asiangamize watumishi wa Mungu. Na kama mimi si mwongo na mzushi, bali nina heshima ya kuongea na Mungu na ni Masihi Mau'udi, basi natarajia kwa fadhili ya Mungu kwamba sawa na suna ya Mungu hutasalimika na adhabu wanayopewa wakadhibishao. Basi ile adhabu ambayo si kwa mikono ya watu bali ni kwa mikono ya

[528] Ahle Hadith, 19 Aprili 1907

Mungu tu, kama vile tauni, kipindupindu na maradhi yanayofisha, kama hukupata katika uhai wangu basi mimi sikutoka kwa Mwenyezi Mungu. Huu sio utabiri ninaotoa kwa sababu ya ufunuo au wahyi, bali nimetaka uamuzi kutoka kwa Mungu kwa kuomba dua tu. Na namwomba Mungu kwamba Ee Mmiliki wangu, Mwonaji, Uliye Mjuzi na Mwenye habari, Unayejua hali za moyo wangu, kama madai haya ya kuwa Masihi Mau'udi ni uzushi wa nafsi yangu tu na mimi ni mfisadi na mwongo katika macho yako na mzushi, na ni kazi yangu kuzua usiku na mchana, basi Ee Mmiliki wangu mpendwa, nakuomba kwa unyenyekevu kwamba unifishe katika uhai wa Maulawii Thanaullah, na kwa kifo changu mfurahishe yeye na kundi lake. Amin. Lakini, Ee Mungu mkamilifu na Mkweli, kama Maulawii Thanaullah si mkweli katika tuhuma zile anazonitupia, basi nakuomba kwa unyenyekevu kwamba mhilikishe katika uhai wangu, lakini si kwa mikono ya watu, bali kwa tauni, kipindupindu na kadhalika kwa maradhi yanayohilikisha, isipokuwa kama atubie waziwazi matusi na maneno makali mbele yangu na mbele ya Wanajumuiya wangu, ambayo kwayo daima ananiudhi akiyaona ni faradhi yake. Amin, Ee Mola wa walimwengu wote.

Nilisumbuliwa sana naye, na nikaendelea kusubiri. Lakini, sasa naona kwamba lugha yake chafu imepita mipaka. Ananiona mbaya zaidi kuliko wezi na majambazi pia ambao uwepo wao unaleta hasara sana duniani. Na katika tuhuma na lugha chafu hakutenda sawa na aya لَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهٖ عِلْمٌ , na akaniona mbaya zaidi kuliko dunia nzima. Na akasambaza kunihusu mimi mpaka nchi za mbali kwamba kwa hakika mtu huyo ni mfisadi, mlaghai mdanganyifu, mwongo, mzushi na mtu mwovu sana. Kama maneno ya aina hii hayangeleta athari mbaya kwa watafutao haki, basi ningesubiri juu ya tuhuma hizo. Lakini naona kwamba Maulawii Thanaullah anataka kuangamiza Jumuiya yangu kwa tuhuma hizo, na anataka kubomoa jengo hili ambalo Umejenga kwa Mkono Wako, Ee Mola wangu na Mwenye kunituma. Kwa hiyo, sasa, kwa kushika utukufu na rehema yako nakuomba kwamba Utoe uamuzi wa kweli kati yangu mimi na Thanaullah. Na yule aliye mfisadi na mwongo machoni mwako, U -

mwondoe duniani katika uhai wa mkweli, au Umletee msiba mkali ulio sawa na kifo. Ee Mmiliki wangu Mpendwa, fanya hivyo. Amin thumma Amin. رَبَّنَا افْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِالْحَقِّ وَأَنْتَ خَيْرُ الْفَاتِحِيْنَ Amin.

Mwishoni, ni ombi kwa Bwana Maulawii kwamba achapishe makala yangu hii katika gazeti lake na aandike chini yake atakayo. Sasa uamuzi upo mkononi mwa Mungu."

Mwandishi:

Mtumishi wa Mungu Asiyehitaji kitu, Mirza Ghulam Ahmad Masihi Mau'udi, *Mungu Amsamehe na Amsaidie.*

Iliandikwa 15 Aprili 1907, 1 Rabiul Awwal 1325 hijriyya.

Baada ya kuchapishwa dua hii ya Mubahala ya Hudhur[as], sawa na uadilifu na haya ilitakiwa kwamba yeye pia chini yake angeandika dua yake ya mubahala na angechapisha katika gazeti lake. Na kama Hudhur[as] alivyomwachia Mungu uamuzi, Bwana Maulawii pia angemwachia Mungu uamuzi. Lakini angewezaje kupata uwezo huu! Njia ya kauleni aliyoendelea kufuata tangu mwanzo akatumia ile ile sasa pia. Akanukuu maandishi ya Hudhur[as] katika gazeti lake la 26 Aprili 1907, na kumwambia naibu mhariri aandike chini yake kwamba:

> "Katika madai yako haya unasema kinyume kabisa na Kurani Tukufu. Kurani Tukufu inasema kwamba Mungu Anawapa waovu muda. Sikiliza: مَنْ كَانَ فِي الضَّلٰلَةِ فَلْيَمْدُدْ لَهُ الرَّحْمٰنُ مَدًّا (Juzu 16, Fungu 8) وَإِنَّمَا نُمْلِي لَهُمْ لِيَزْدَادُوْا إِثْمًا (Juzu 4, Fungu 9) na وَيَمُدُّهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُوْنَ (Juzu 1, Fungu 2) Aya hizo zinakadhibisha udanganyifu wako, na sikiliza: بَلْ مَتَّعْنَا هٰؤُلَاءِ وَاٰبَاءَهُمْ حَتّٰى طَالَ عَلَيْهِمُ الْعُمُرُ (Juzu 17, Fungu 4) Hizo zinamaanisha waziwazi kwamba Mwenyezi Mungu Anawapa umri mrefu watu waongo, wadanganyifu, walaghai, wafisadi na waasi, ili katika muda huo watende maovu zaidi. Unatuambiaje kanuni za kubuniwa kwamba watu wa aina hiyo hawapati umri mrefu. Kwa nini isiwe hivyo kwani unadai kuwa Masihi, Karishna, Muhammad na Ahmad, na ujuzi wa Kurani ndio huu? ذٰلِكَ مَبْلَغُهُمْ مِنَ الْعِلْمِ — Huo ndio upeo wao katika elimu. Naibu Mhariri".

Na katika *Ahle Hadith* la 31 Julai 1907, kuhusu maandishi hayo

aliandika kwamba "nayaona kuwa sahihi". Ilihali maandishi hayo ya naibu mhariri hayana uhakika wowote isipokuwa kuongopa na kudanganya. Kwani katika aya hizo haikutajwa kupata umri mrefu kwa amzuliaye Mungu uwongo, bali wametajwa waongo wengine minghairi yao. Hudhur[as] alieleza kutopata umri mrefu kwa amzuliaye Mungu uwongo. Na tofauti kati ya hao wawili ni dhahiri kabisa.

Hapa yapasa kutaja kwamba kuandika hivyo kusudio la naibu mhariri lilikuwa nini? Na kwa lengo gani Maulawii Thanaullah alimwunga mkono? Kwa kutafakari kidogo tu yaeleweka kwamba wote wawili walikuwa na yakini moyoni kwamba kama shindano likitokea, Maulawii Thanaullah lazima atakufa kwanza na hapo tutapata nafasi ya kusema kwamba tumeshaandika mapema kwamba mwongo hupewa umri mrefu. Na kama mubahala haukufanyika na Bwana Mirza akifarika kwanza, basi tutasema kwamba hayo ni matokeo ya kufanya dua kwa upande mmoja.

Baada yake, Maulawii Thanaullah, badala ya kuandika dua yake ya mubahala chini ya dua ya Mubahala ya Hudhur[as], akaandika ibara yake iliyojaa laana, dhihaka, matusi, lugha chafu, mdomo mchafu, udanganyifu. Tukiacha porojo na maneno yake ya kishenzi twaandika maneno yake machache kutoka katika maandishi yake:

1. "Kwanza kabisa hujachukua kibali changu kuhusu dua hii, na uliichapisha bila kibali."

2. "Maandishi yako haya hayawezi kuleta umuzi wa mwisho."

3. "Nashindana nawe. Nikifa, kifo changu kitakuwaje hoja kwa watu wengine."

4. "Kwa kuwa Mitume wa Mungu huwa wenye rehema na huruma, na kila wakati wanataka kwamba mtu yeyote asiangamie, sasa kwa nini unaniombea kifo changu."

5. "Mwenyezi Mungu huwapa watu waongo, wadanganyifu, wafisadi na waasi umri mrefu ili katika muda huo watende maovu zaidi."

Tanbihi: Ibara hiyo ya mwisho iliandikwa na naibu mhariri, lakini

Maulawii Thanaullah aliisadikisha na akaandika kwamba "naiona kuwa sahihi."[529]

6. "Kwa kifupi ni hii kwamba… maandishi yako haya sikubali, wala yeyote mwenye akili hawezi kuyakubali."[530]

Kisha Maulawii Thanaullah anaandika:

7. "Mtume Mtukufu[saw] juu ya kuwa mtume mkweli alifariki kabla ya Musailama Kadhdhab, na Musailama juu ya kuwa mwongo alifariki baada ya mkweli."[531]

8. "Onyesha ishara ambayo sisi pia tupate somo tukiiona. Tukifa tutaona nini na tutapataje mwongozo."[532]

Basi, Maulawii Thanaullah sawa na mwenendo wake wa zamani aliukimbia mubahala, kwa hiyo mubahala haukufanyika. Na sawa na kanuni yake aliyokubali Bwana Maulawii huyo mwenyewe, Mwenyezi Mungu alimpa umri mrefu kama watu waongo, wadanganyifu, wafisadi na waasi", ili afanye vitendo vibaya zaidi katika muda huo.

Kama angejasiri kufanya mubahala, kwa yakini angekufa kabla ya Hudhur[as] . Lakini aliuepa mubahala walivyoepa[533] Wakristo wa Najran, kwa hiyo alisalimika kufa katika uhai wa Hudhur[as].

---

[529] Ahle Hadith, 31 Julai 1907

[530] Maandishi kutoka Ahle Hadith, 26 Aprili 1907

[531] Muraqqa' Qadiani, uk. 9, Agosti 1907

[532] Maandishi ya Bwana Maulawii huyo yaliyoandikwa katika gazeti la Watan, 26 Aprili 1907, uk. 11

[533] Mtume Mtukufu[saw] aliwaita Wakristo wa Najran kwa mubahala kwa kutimiza hoja mara ya mwisho, kama vile aya ya Kurani Tukufu: لَعْنَةُ اللهِ عَلَى الْكَاذِبِيْنَ ni shahidi juu yake, lakini hawakuhudhuria katika uwanja wa mubahala. Kwa kuona kukimbia kwao Mtume Mtukufu[saw] alisema: لَمَّا حَالَ الْحَوْلُ عَلَى النَّصَارٰى كُلِّهِمْ حَتّٰى يَهْلِكُوْا (Tafsir Kabir, J. 2 uk. 299) Yaani kama Wakristo wangefanya mubahala, wote wangefariki katika mwaka mmoja. Kadhalika Hudhur[as] alisema kuhusu Maulawii Thanaullah kwamba "Kama (Maulawii Thanaullah) akiwa tayari kwamba mwongo afe kabla ya mkweli, basi lazima yeye atafariki kabla." Ijaze Ahmadi, uk. 36

Basi, kama vile huko kukimbia kwa Wakristo wa Najran kukasababisha uzio njiani mwa "Uamuzi wa Mungu kupitia mubahala", hivyo ndivyo hapa pia kukimbia kwa Maulawii Thanaullah kulivyomsalimisha na kifo.

JIBU LA UPINZANI HUU KWAMBA TANGAZO LA HUDHUR[AS] HALIKUWA MUSWADA WA MUBAHALA

Maulawii Thanaullah na baadhi ya wapinzani wengine, muda mfupi baada ya kifo cha Hudhur[as], walianza kusema kwa kuweka pazia juu ya "ukimbizi kutoka mubahala" wa Maulawii Thanaullah kwamba dua ya Hudhur[as] ilikuwa siyo "dua ya mubahala", lakini udhuru huu ni batili kwa sababu zifuatazo:

1. Maulawii Thanaullah mwenyewe wakati wa kuchapishwa tangazo hilo alilichukulia kama "dua ya mubahala", waila ilikuwa haja gani ya kuandika "sababu" za kukana zilizoandikwa juu. Hususan tangazo la kutokubali dua ya upande mmoja lilikuwa kinyume cha akili.
2. Mwezi mmoja baada ya kifo cha Hudhur[as], Maulawii Thanaullah aliandika:

"Krishna wa Qadian alichapisha tangazo la kufanya mubahala nami, tarehe 15 Aprili 1907.[534]

3. Kichwa cha tangazo la Hudhur[as] ni: "Uamuzi wa mwisho kwa Maulawii Thanaullah", sio "Uamuzi wa mwisho kuhusu Maulawii Thanaullah". Na uamuzi wa mwisho kwa mtu fulani daima unamaanisha kwamba mpaka makundi yote mawili yakubaliane njia ya uamuzi, uamuzi wowote hauwezi kufanyika.
4. Ni dhahiri kwa mambo ya kweli yaliyoandikwa juu kwamba katika tangazo la "Uamuzi wa mwisho kwa Maulawii Thanaullah", Hudhur[as] alichapisha "dua ya mubahala" kwa upande wake na Bwana Maulawii pia akiichukulia kuwa dua ya mubahala aliepa kuchapisha dhidi yake "dua ya mubahala".

[534] Muraqq'a Qadiani, 18 Juni 1908

MAREJEO YA HUDHUR[AS] YA UAMUZI WA MWISHO

Hudhur[as] katika uhai wake, akijibu swali la mtu fulani, alisema kwamba:

> "Imeandikwa wapi kwamba mwongo anafariki katika uhai wa mkweli. Niliyoandika ni hii tu kwamba miongoni mwa wafanyao mubahala yule aliye mwongo anafariki katika uhai wa mkweli. Je, maadui wote wa Mtume Mtukufu[saw] walikufa katika uhai wake? Maelfu ya maadui walibaki hai baada ya kifo chake. Naam, mwongo afanyaye mubahala anakufa katika uhai wa mkweli. Kadhalika wapinzani wangu pia watabaki hai baada ya kifo changu. Tunashangaa kwa kusikiliza mambo ya namna hii. Tazameni, mambo yetu yanapinduliwaje! Wametumia ujanja ule wa kugeuza maneno hata kushinda Wayahudi."[535]

MAANGAMIO YA ALEXANDER DOWIE, 9 MACHI 1907

Katika Marekani, mtu mmoja alikuwa maarufu aitwaye jina Dkt. John Alexander Dowie. Mwishoni mwa mwaka 1899 au mwanzoni mwa mwaka 1900 alidai kwamba:

> "Yoyote nitakayowaambieni, mtalazimika kuyatekeleza, kwani mimi ni mtume sawa na ahadi ya Mungu."[536]

Huyo alikuwa mtu maarufu na tajiri wa Marekani. Yeye alianzisha mji wa Zion katika mwaka 1901, ambao kwa uzuri, wasaa na majengo yake ulianza kuhesabiwa katika miji maarufu ya Marekani katika muda mfupi. Gazeti lake "Leaves of Healing" lilikuwa likitoka kwa shani kubwa, ambalo kwa sababu hiyo katika Marekani nzima umaarufu wake ukaenea. Idadi ya wafuasi wake ilifikia malaki.

Mtu mmoja aitwaye Parlan ameandika habari za maisha ya Dkt. Dowie. Profesa Franklin Johnson wa Chicago aliandika katika dibaji ya kitabu hicho:

---

[535] Al-Hakam, 10 Oktoba 1907 uk. 4

[536] Ibratnak Anjaam, uk. 25 na Dkt. Chaudhari Khalili Ahmad Nasir, Mbashiri wa huko Marekani, akirejesha kwa Parlan.

> "Katika muda wa miaka 12 iliyopita watu wachache sana wamepita waliopata nafasi kubwa katika magazeti ya Marekani jinsi alivyopata John Alexander Dowie."

Alimaanisha kuwa Bwana Dowie alipata umaarufu sana katika Marekani na magazeti ya huko. Bwana Dowie alikuwa adui mkali sana wa Mtume wetu Mtukufu[saw] na alikuwa mwenye mdomo mchafu. Daima alikuwa anafikiria kwamba kwa njia yoyote iwezekanayo aangamize Islam duniani. Anaandika katika gazeti lake:

> "Nawatahadharisha mataifa ya Kikristo ya Marekani na Ulaya kwamba Islam haijafa; Islam imejaa nguvu. Ingawaje yapasa lazima Islam ifutike, dini ya Muhammad lazima iangamie, lakini maangamio ya Islam hayataweza kwa njia ya Ukristo wa Magharibi (Kilatini) uliodhoofika wala kwa Ukristo wa Mashariki (Kiyunani) usio na nguvu, wala kwa Ukristo uliochoka wa watu ambao wanamwamini Yesu kwa jina tu na wanaishi maisha ya watu walafi, walevi, waovu, waasherati na wadhalimu."[537]

Hudhur[as] alipojua madai ya mtu huyo, basi tarehe 8 Agosti 1902 alimwandikia barua[538] ambamo akitaja kifo cha Hadhrat Masihi[as] na kaburi lake katika Srinagar, Kashmir, akampa changamoto ya mubahala. Akaandika:

> "Ilmuradi, Dowie anasema mara kwa mara kwamba karibuni hao wote wataangamia isipokuwa kundi lile ambalo linaamini uungu wa Yesu Kristo na utume wa Dowie. Katika hali hiyo, Wakristo wote wa Ulaya na Marekani wanapaswa kwamba haraka sana wamkubali Dowie ili wasiangamie. Na maadamu wameishakubali jambo kinyume na akili, yaani Uungu wa Yesu Kristo, basi na wakubali jambo la pili pia lililo dhidi ya akili kuwa Dowie ndiye mtume wa huyo mungu. Kuhusu Waislamu,

[537] Leaves of Healing, 25 Agosti 1900

[538] Katika zama zile padre mmoja, Bwana Pigott wa London, alijidai kuwa Mungu ambaye Hudhur[as] alimwonya na adhabu ya Mungu. Matokeo yake yakawa akanyamaza kabisa na akafa baada ya kuishi maisha yasiyojulikana.

> twamwambia Dowie kwa adabu kwamba katika kesi hiyo kuna haja gani ya kuwaangamiza mamilioni ya Waislamu. Ipo njia rahisi ambayo kwa njia hiyo itaamuliwa kwamba je, Mungu wa Dowie ni Mungu wa kweli au Mungu wetu. Na njia yenyewe ni kwamba Bwana Dowie asikariri kuwaambia utabiri wa maangamio ya Waislamu wote, bali akinilenga mimi pekee moyoni mwake aombe kwamba miongoni mwetu sisi wawili yule aliye mwongo Mungu Amfishe kwanza."[539]

Bwana Dowie hakuijibu changamoto hiyo ya Hudhur[as], lakini magazeti ya Marekani yalitaja utabiri huo kwa maneno mazuri. Gazeti Argonaut la San Francisco, likaandika katika toleo lake la 1 Desemba 1902, chini ya kichwa cha habari "Shindano la dua kati ya 'Kiingereza' na 'Kiarabu' (yaani Ukristo na Islam)"

> "Muhtasari wa madhumuni ya Bwana Mirza aliyomwandikia Dowie ni kwamba u kiongozi wa kundi moja, nami pia nina wafuasi wengi. Basi uamuzi wa jambo hili kwamba nani kati yetu ametoka kwa Mungu, unaweza kuwa hivi kwamba kila mmoja wetu amwombe Mungu wake dua na atakayekubaliwa maombi yake afahamike kuwa ametoka kwa Mungu wa kweli. Dua yenyewe itakuwa hii kwamba aliye mwongo kati yetu Mungu Amfishe kwanza. Bila shaka pendekezo hili ni la akili na uadilifu."[540]

Hudhur[as] alikuwa akiagiza gazeti lake na kuona kwamba anaendelea kuzidi katika uadui wa Islam. Hapo, katika mwaka 1903 pia kwa kupitia barua alirudia changamoto ya mubahala. Basi akaandika:

> "Nina umri karibu miaka 70, na Dowie, kama anavyoeleza, ni wa miaka 50, lakini sijajali umri wangu mkubwa. Kwani uamuzi wa mubahala hautafanyika kwa kutegemea umri, bali Mungu Aliye Hakimu wa mahakimu, Atatoa uamuzi. Na kama Dowie akikimbia shindano… hata hivyo eleweni kwa yakini kwamba

[539] The Review of Religions, toleo la Septemba 1902, uk 344.

[540] Tatimma Hakikatul Wahyi, uk. 71, maelezo ya pembeni.

karibuni balaa itaiangukia Zion yake.[541]

Barua ambayo Hudhur[as] alikuwa anampelekea, nakala zake akayatumia magazeti ya Kiingereza ya Marekani pia. Kwa hiyo, katika mwaka 1903 magazeti yalitaja kwa wingi changamoto hiyo ya mubahala ya Hudhur[as]. Muhtasari wa makala za magazeti 32 Hudhur[as] aliandika katika Tatimma Hakikatul Wahyi, uk. 70 hadi 72, maelezo ya pembeni. Watu walipomsumbua sana Dowie na kung'ang'ania ajibu changamoto ya mubahala huo, ndipo katika baadhi ya matoleo ya Septemba na Desemba 1903 aliandika kwamba:

> "Katika India yupo Masihi mjinga wa Muhammad, anayeniandikia mara kwa mara kwamba kaburi la Yesu Kristo lipo katika Kashmir na watu wananiuliza kwamba kwa nini hulijibu, na kwamba kwa nini humjibu. Lakini je, mnadhani kwamba nitawajibu hao mbu na nzi. Kama nikiweka tu mguu wangu juu yao, nitawakanyaga na kuwaangamiza."[542]

Hudhur[as] alipopata habari ya ujeuri, utovu wa adabu na ujasiri, akaanza kumwomba sana Mwenyezi Mungu kwa kupata ushindi katika uamuzi huo. Katika muda huo huyo alikwishapata umaarufu na heshima katika Marekani, Ulaya na Australia. Na kwa kuwa alikuwa na afya nzuri sana, kwa hiyo katika mikutano mara nyingi alikuwa akiona fahari kwa afya yake nzuri. Inayumkinika kuwa alikuwa na furaha kwamba siku hadi siku ninapanda juu. Lakini Mungu wa Hudhur[as] alitaka kumdhalilisha vibaya baada ya kumpatia umaarufu duniani kote, ili dunia ipate ibra na ijue kwamba upi unakuwa mwisho wa watu wakubwa kabisa wanaokabiliana na Mitume wa Mungu?

Kwa vile Bwana Dowie alikuwa mtu mpenda anasa, na alijenga mji wa Zion pia kwa kukopa pesa kutoka kwa wafuasi wake, kwa hiyo, upande mmoja maendeleo ya mji yalianza kupungua na upande wa pili pesa zilizokuwa zimekusanywa zilianzia kutumika katika anasa za

[541] Tangazo la 23 Agosti 1903 sawa na Tatimma Hakikatul Wahyi, uk. 71, maelezo ya pembeni.

[542] Tatimma Hakikatul Wahyi, uk. 73

Dowie. Matokeo yake yakawa kwamba heshima ya Bwana Dowie ilianza kupungua. Kwa kuondoa upungufu huu wa hatari wa mali, Dowie alitaka kununua ardhi huko Maxico. Alidhani kwamba akinunua ardhi ile, basi matatizo yote ya kifedha ya Zion yatakwisha. Basi, kwa kununua ardhi ile alitaka kukopa kutoka kwa wafuasi wake wa Zion, na kwa lengo hili alitangaza mkutano mkubwa sana utakaofanyika Jumapili ya mwisho ya Septemba 1905. Maandalizi ya mkutano yalifanywa vizuri. Dowie akivaa mavazi ya heshima aliyoita mavazi ya kiutume alipokaa juu ya kiti chake, wahudhuriao wote walianza kusubiri kwa hamu sana kwamba tuone sasa Bwana John Alexander Dowie atatangaza nini.

Bwana Newcomb, mwandishi wa maisha ya Bwana Dowie anaandika:

> "Dowie siku ile alikuwa kileleni mwa fasaha yake. Mada ya mawaidha ilikuwa hafla ya Mlo wa Bwana. Baada yake Dowie akivaa mavazi meupe akajitokeza tena mbele ya wafuasi wake. Kwanza uliimbwa wimbo wa maombi. Baada ya usomaji wa baadhi ya aya za Biblia, damu na nyama ya Yesu, kwa sura ya mkate na kileo, iligawanywa na manaibu waliovaa mavazi maalumu baina ya wafuasi waliohudhuria. Sasa sherehe yenyewe ilikaribia kwisha. Maneno machache tu ya mwisho ya Dowie yalibaki kwa kufunga mkutano. Kwa kusikiliza maneno ya mwisho, watu walikuwa wakisubiri kwa hamu.
>
> Mara Dowie akatingisha mkono wake wa kulia kana kwamba mdudu mchafu amejikalia juu ya mkono wake. Kisha alipiga mkono wake kwa nguvu juu ya mkono wa kiti. Watu walishangaa kwa kitendo chake kisicho cha kawaida.
>
> Dowie akasawajika, akawa karibu aanguke, wafuasi wake wawili wakamsaidia na wakimvuta wakampeleka nje ya ukumbi."

Ilmuradi, Dowie akapooza ghafula mwili wake wakati ambapo mpango ulikuwa kileleni, wa kununua ardhi katika Maxico kwa kuondoa mgogoro wa mali wa mji wa Zion. Mungu Mwenye kulipiza kisasi na Mweza kamili leo alifumba mdomo wake aliokuwa

akiutumia vibaya dhidi ya shani kubwa ya Mtume Mtukufu[saw]. Akaweza kuongea pole pole tu. Afya yake ilipoanza kuharibika siku hadi siku, akalazimika sawa na shauri la daktari kwenda Maxico na Jamaica ili kupata kupona. Lakini sasa hakuwaamini manaibu wake, alihofia kwamba katika kutokuwepo kwake siri zote zitafichuka. Kwa hiyo, aliamua kwamba msimamizi atakuwa makamu wake Voliva aliyekuwa mkuu wa Misheni ya Australia kutoka kwake. Lakini, kwa kuwa yeye asingeweza kufika haraka, kwa hiyo aliikabidhi kamati ya wafuasi wake watatu watakaosimamia mambo ya Zion.

Katika Zion donda la uasi dhidi ya Dowie liliendelea kuiva tangu muda mrefu. Hilo lilihitaji tu kutumbuliwa, nalo likatumbuliwa hivi kwamba afisa mmoja miongoni mwa wafanyakazi wake alitaka kumwoa mwanamke Mzioni. Kwa kupata kibali chake alisafiri pamoja na Dowie katika garimoshi mpaka Chicago. Njiani akamwomba ruhusa ya kumwoa huyo, lakini Dowie akakataa kabisa. Afisa yule aliporudi Zion, akamwambia mwanakamati mmoja kwamba nimeshapata idhini, uitangaze. Basi, mwanakamati huyo akatangaza. Dowie alishafika Jamaica tarehe 1 Januari 1906. Alipojua jambo hilo, yeye kwa kutuma telegramu akamwondolea cheo chake yule mwanakamati aliyetangaza. Sasa, watu wakafahamu kwamba mwanakamati huyo hana kosa, wakamwonea huruma. Kwa hiyo, Mhariri wa *Leaves of Healing* akaleta upingamizi wa kwanza kwamba akakataa kuchapisha telegramu hiyo ya Dowie. Dowie alipojua mwenendo wa uasi wa gazeti lake binafsi, alimtuma mfanyakazi wake mmoja aende Zion kwa barua yake binafsi ambamo alimwamuru Mhariri kwamba mara moja atangaze adhabu hiyo katika gazeti. Mhariri alipopokea barua, akaichana vipande vipande mbele ya mjume wa Dowie na kuitupa kikapuni na kamwambia nenda ukamwambie Dowie kwamba hili ndilo jibu la barua yake.

Naibu aliyeitwa kutoka Australia, Bwana Voliva, pia alifika Zion tarehe 12 Februari 1906. Baada ya kufika huko alijua kwamba usimamizi wa mamlaka aliyopewa hali yake ni mbovu kabisa. *Leaves of Healing* limeshafungwa kwa upungufu wa fedha. Haukuwa mpango wowote wa kuwalipa mishahara wafanyakazi wengine. Watu ambao waliweka pesa zao katika hazina ya Zion, walikuwa na hamu ya

kupata chochote katika pesa zao. Ilmuradi, hali ilikuwa mbaya mno.

Katika hali kama hizo, Dowie alikuwa na nia ya safari ya Cuba kutoka Jamaica, kisha kutoka Cuba mpaka Maxico. Kwa vyovyote fedha zilitakiwa kuletwa kutoka Zion. Yeye alipomwambia Bwana Voliva kuhusu nia yake hiyo, yeye alikataa kabisa kuwa mshiriki wa Dowie katika kosa hilo. Hapo Dowie akaghadhibika sana. Mwishoni mwa Machi 1906, alimwondoa Voliva pia katika cheo chake cha unaibu wake kwa kumtumia telegramu. Lakini sasa kulikuwa hakuna aliyekuwa anamsikiliza. Telegramu ya kumwondolea Voliva ikaleta dhoruba kubwa katika Zion. Kwa uamuzi huu wa Bwana Dowie, watu wote wakawa wapinzani wake.Tarehe 31 Machi 1906 telegramu hiyo ilifika, na tarehe 1 Aprili, Voliva akaitisha mkutano wa hadhara. Wazioni 3500 walishiriki katika kikao hicho. Bwana Voliva akatoa maelezo yote ya tukio hilo. Wafuasi wa Dowie walipojua kwamba Dkt. Dowie ameshachukua binafsi Dola laki sita za Zion, na katika viwanda vya Zion mpaka tarehe ile hisa za Dola laki 25 zimeshauzwa, lakini miongoni mwake Dola laki 5 tu zimetiwa katika shughuli ya kuendesha kazi. Kwa kiwanda cha kutengeneza tamutamu, hisa zaidi ya Dola laki moja na nusu ziliuzwa, lakini Dola 17,000 pekee zilitiwa katika biashara, hapo watu walikasirika sana.

Baada yake, Voliva alimwita naibu yule wa Dowie aliyekuwa ameondolewa kwa kosa la kutangaza ndoa ya Mzioni fulani, na kasema kwamba natangaza kumrudisha kwenye cheo chake tena. Watu walipokea tangazo hilo kwa furaha na shangwe.

Baadaye Bwana Voliva alitangaza kwamba kwa vile Dowie ni mwenye kosa la kujivunia, kiburi, ufujaji wa mali na mambo ya anasa na kutumia fedha ya watu kwa maisha ya anasa, kwa hiyo natangaza kwamba yeye hafai kabisa kuwa mwongozi wetu. Kwa tangazo hilo, watu walifurahika sana. Baada yake kikao kingine kilifanyika cha kamati ambayo baada ya kushauriana ilimtumia Dowie telegramu ifuatayo:

> "Wajumbe wote wa kamati kuu wanakubali uongozi wa Voliva na maafisa uliowafukuza wanawarudisha tena katika vyeo vyao.

> Na wanapinga vikali ufujaji wako wa fedha, unafiki, uwongo, kupiga chuku, matumizi mabaya ya fedha za watu, dhuluma yako na kutofanya uadilifu."[543]

Dowie aliposoma telegramu hii, akaduwazwa. Afya ilikuwa imeshaharibika tayari, heshima iliyobaki ilionekana kuvunjika, mara moja akafunga safari ya kuelekea Chicago. Baada ya kufika Chicago kwa fedha zile za watu, alizokuwa ametwaa bila haki, aliwaajiri mawakili kwa kufungua kesi dhidi ya Bwana Voliva. Katika mahakama ya Chicago kesi iliendelea kwa wiki mbili. Mahakama badala ya kumrudishia Dowie mali ya Zion, iliweka mfilisi mmoja, na iliagiza kwamba wafuasi wa kanisa la Zion wajichagulie kiongozi wao mpya kwa kupiga kura. Uchaguzi huo ulifanyika tarehe 18 Septemba ambamo Voliva alishinda kwa kupata maelfu ya kura dhidi ya kura mia moja tu za Dowie.

MWISHO WA DOWIE

Sasa sikilizeni mwisho wa Bwana Dowie. Mwaminio wake mmoja Bwana Lindsay anaandika kwamba siku hizo kulikuwa hamna maradhi yoyote asiyoshikwa nayo Dowie. Alikuwa akiendelea kupungukiwa nguvu yake pia haraka sana. Katika siku za maradhi, Wahabeshi wawili pekee walioajiriwa walikuwa wakimtumikia. Hao walikuwa wakimbeba kwa kumpeleka kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine. Wakati mwingine mwili wake uliopooza na usio na hisia ulikuwa unaanguka kutoka mikononi mwao kama jiwe zito, na Dowie alikuwa akianguka ardhini kama vile jiwe linavyomponyoka mtu na kuanguka chini. Dowie akipata maelfu ya shida ya namna hii, hatimaye aliaga dunia hii tarehe 9 Machi 1907. Mji wake uliangamia, mke na watoto wake walitengana naye kiasi hiki kwamba hata hawakushiriki katika sala yake ya jeneza. Watu wachache tu walishughulikia mazishi yake. Ilmuradi, alishuhudia katika uhai wake kushindwa katika mpango wake wote. Alifikiri kwamba ni rahisi kujenga mji mkubwa kwa kukopa kutoka kwa watu, lakini dhana yake hiyo ikawa batili. Alifikiri ni rahisi kudai unabii, lakini alishindwa

[543] Dowei ka 'Ibratnak Anjam, uk. 85

vibaya katika jambo hili pia. Kisha alipokuwa bado katika Jamaica, zilipatikana nyumbani mwake chupa za pombe na barua za mapenzi za wasichana, ilihali alikuwa alikataza mambo hayo. Alikuwa tayari kabisa kufunga ndoa ya pili, ilihali jambo hilo ni kinyume kabisa na Ukristo uliopo. Ilmuradi, alipata dhila kutoka kila upande. Ni kweli kwamba mtu mwongo hawezi kufaulu kamwe katika mipango yake.

Hudhur[as] alikwisha pata habari za ushindi wake adhimu kutoka kwa Mwenyezi Mungu wiki mbili kabla ya kifo cha Dowie. Basi, kwenye jalada la kijitabu alichokuwa akiandika siku zile, yaani 'Qadian Ke Aria Aur Ham' alichapisha tangazo hili:

"UTABIRI WA ISHARA MPYA"

> "Mungu Anasema kwamba Mimi Nitadhihirisha ishara moja mpya itakayokuwa na ushindi adhimu. Itakuwa ishara kwa dunia nzima, na itatokea kwa mikono ya Mungu na kutoka mbinguni. Yapasa kila jicho liisubiri, kwani Mungu Ataidhihirisha karibuni, ili Athibitishe kwamba mimi, ninayetukanwa na mataifa yote nimetoka Kwake. Amebarikiwa ajifaidishaye kwayo. Amin."

Mtangazaji: Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Mau'udi. (Tangazo la 20 Februari 1907)

MAONI YA HUDHUR[AS] JUU YA KIFO CHA DOWIE

Hudhur[as] alipopata habari ya kifo cha kusikitisha cha Dowie, alikiita kuwa mwujiza mkubwa wa Mtume Mtukufu saw. Alisema:

> "Sasa ni dhahiri kwamba ishara (iliyosababisha ushindi adhimu) inayoweza kuwa ishara wazi kwa dunia nzima — Asia, Marekani, Ulaya na India — ndiyo ishara ile ya kifo cha Dowie. Kwani, ishara zingine zilizodhihiri kwa matabiri yangu zilikuwa kwa Panjab na India tu, na mtu yeyote wa Marekani na Ulaya hakupata habari ya kuzidhihiri. Lakini, ishara hii ikidhihirika kutoka Panjab kwa sura ya utabiri, ikafika Marekani, ikatimia kwa mtu ambaye alijulikana kwa kila mtu wa Amerika na Ulaya, na alipokufa, mara moja habari ikapelewa kwa magazeti ya Kiingereza ya nchi hii kupitia telegramu. Basi "Pioneer"

(linalotoka Ilahabad) likachapa habari hii katika toleo lake la 11 Machi 1907, "The Civil and Military Gazette" (litokalo Lahore) katika toleo lake la 12 Machi 1907 na "The Indian Telegraph" (litokalo Lucknow) katika toleo lake la 12 Machi 1907. Basi, hivyo habari hiyo ilitangazwa takriban duniani kote. Na mtu huyo mwenyewe, sawa na daraja yake ya kidunia, alitambulika kama ma-Nawab wenye shani na wanamfalme. Basi, Webb, aliyesilimu kule Marekani , aliniandikia barua kuhusu habari hii kwamba Dkt. Dowie anaishi katika nchi hii kama waheshimiwa sana na kama wanamfalme. Na juu ya heshima na umaarufu aliopata katika Marekani na Ulaya ikawa hivi kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu kwamba magazeti makubwa maarufu yatokayo kila siku yalichapa makala yangu ya kufanya mubahala naye na kuyaeneza kote katika Marekani na Ulaya. Kisha baada ya habari hiyo kuenea sana, mauti na maangamio yake yaliyokuwa yametabiriwa, yalitimia wazi wazi kiasi hiki kwamba haiwezi kuwazwa kudhihirika kikamilifu, kitimilifu zaidi ya hiyo. Balaa iliangukia kila jiha ya maisha yake. Ikathibitika uhaini wake. Alikuwa akisema kileo ni haramu katika mafundisho yake, lakini ikathibika kuwa yu mlevi. Alifukuzwa akiwa na majuto sana katika mji wa Zion aliojenga kwa gharama ya rupia malaki kadha, na vile vile rupia milioni 70 taslimu zilizokuwa mkononi mwake alinyng'anywa. Mkewe na mwanaye wakawa maadui zake, na baba yake alitangaza kwamba yu mwanaharamu.[544] Hivyo alithibitika baina ya watu kuwa yu mwanaharamu. Na madai yake kwamba nawaponya wagonjwa kwa mwujiza, madai hayo yote yalithibitika kuwa uwongo na alipata dhila ya kila aina. Na hatimaye alipooza, na watu wachache walikuwa wakimbeba kama mbao. Kisha akawa mwendawazimu kwa huzuni nyingi, na akapotewa na akili. Na madai yake kwamba bado ninao umri mrefu na ninazidi kuwa kijana siku hadi siku ilhali watu wengine wanazeeka, ikathibitika kuwa ulaghai. Mwishowe katika wiki ya kwanza ya Machi 1907 alikufa kwa majuto makubwa, udhia na taabu.

[544] Kwa maelezo ya mambo haya someni 'Dr. Dowie ka Ibratnak Anjam'.

Sasa ni dhahiri kwamba mwujiza upi utakuwa mkubwa zaidi kuliko huu. Kwa vile kazi yangu ndiyo kuvunja msalaba, sehemu kubwa ya msalaba imevunjika kwa kifo chake. Kwani yeye alikuwa msaidizi wa kwanza duniani kuusaidia msalaba ambaye alidai kuwa mtume na kasema kwamba kwa dua yangu Waislamu wote watahilikika, na Islam itaangamia, na Kaaba haitaendewa na watu. Mwenyezi Mungu Alimwangamiza kwa mkono wangu. Najua kwamba kwa mauti yake utabiri wa kuua nguruwe ulitimia wazi wazi. Kwani, nani anaweza kuwa hatari zaidi kuliko mtu yule aliyejidai kuwa mtume na akala uchafu wa uongo kama nguruwe. Na kama alivyosema yeye mwenyewe, watu karibu laki moja walikuwa pamoja naye ambao walikuwa matajiri, bali ukweli ni huu kwamba Musailama Kadhdhab na Aswad 'Ansi walikuwa si kitu mbele yake, wala hawakuwa na umaarufu sawa naye wala hawakuwa na rupia mamilioni. Basi, naweza kula kiapo kwamba huyo alikuwa ndiye yule nguruwe ambaye kumhusu yeye Mtume Mtukufu[saw] alitabiri kwamba atauawa kwa mkono wa Masihi Mau'udi.[545] Kama nisingemwita kwa mubahala, na kama nisingeomba dhidi yake, na kama nisingetangaza utabiri wa kifo chake, hapo kifo chake kisingekuwa dalili yoyote ya ukweli wa Islam. Lakini kwa kuwa niliishatangaza mapema katika mamia ya magazeti kwamba atakufa katika uhai wangu, mimi ni Masihi Mau'udi, na Dowie ndiye mwongo, na niliandika mara kwa mara kwamba dalili yake ni hii kwamba atakufa kwa dhila na majuto katika uhai wangu. Basi, akafa katika uhai wangu. Utakuwa ni mwujiza gani ulio wazi zaidi kuliko huu unaosadikisha utabiri wa Nabii[saw]. Sasa yule tu atakataa atakayekuwa adui wa ukweli."[546]

[545] Alhamdulillahi, leo sio tu utabiri wangu, bali utabiri wa Mtume Mtukufu[saw] umetimia dhahiri shahiri.

[546] Tatimma Hakikatul Wahyi, uk. 75-80

MAONI YA MAGAZETI YA MAREKANI JUU YA KIFO CHA DKT. DOWIE

Dkt. Alexander Dowie alipokufa, magazeti mengi ya Marekani yalikubali kwamba utabiri wa Hudhur[as] umetimia:

1. Gazeti la 'Dunnville' likitaja tukio hilo liliandika:

"Kama Ahmad na wafuasi wake, juu ya utabiri uliotimia miezi michache kabla, waone fahari kwa kuutimia wazi wazi sana, basi hawana lawama yoyote."[547]

2. Gazeti "Truth Seeker" liliandika:

"Hali za kidhahiri zilikuwa kinyume cha mtoaji changamoto kuishi muda mrefu, lakini akashinda." Yaani umri wa Hudhur[as] ulikuwa mkubwa kuliko Dkt. Dowie.

3. Gazeti "Herald" la Boston, Marekani, liliandika:

"Baada ya kifo cha Dowie, umaarufu wa Nabii wa India umezidi sana. Kwani, je, hii si kweli kwamba alitabiri kifo cha Dowie kwamba atakufa katika uhai wake yeye aliye Masihi, na huyo atakufa kwa majuto makubwa na taabu sana? Umri wa Dowie ulikuwa miaka 65 na wa mtoa utabiri, miaka 75."

KAMHESHIMU MKEWE MHESHIMIWA

Hadhrat Amman Jan na Hadhrat Amman Ji[548] pamoja na watoto wao wakaenda Lahore pamoja na Hadhrat Mir Nasir Nawab[ra] kwa siku chache kwa kubadilisha hewa. Msafara huu uliondoka kuelekea Lahore tarehe 4 Julai 1907, na tarehe 15 Julai 1907 ulirudi Batala. Hudhur[as] aliyekuwa mfano kamili wa kuishi vizuri nyumbani, alienda Batala pamoja na mahadimu wachache kwa kumpokea mke wake. Hudhur[as] alipanda gari la farasi, akafungua Kurani akaanza kusoma Sura Al-Faatiha. Mahadimu wanasimulia kwamba mpaka Batala Hudhur[as] aliendelea kutafakari katika Sura Al-Faatiha tu. Njiani kwenye mto akishuka alitawadha tu na tena akaanza kusoma ile ile

[547] Toleo la 7 Juni 1907

[548] Mke wa Hadhrat Khalifatul Masihi[ra] I.

Sura Al-Faatiha. Allah, Allah, mapenzi makubwa yalioje ya aliyetumwa na Mungu kwa Kitabu cha Mungu! Katika safari ndefu ya maili 11 aliendelea kutafakari katika Sura moja ndogo ya Kurani tukufu. Amesema kweli katika ubeti kwamba:

> Moyo wangu unataka kuubusu saa zote msahafu Wako, na kuizunguka Kurani, hiyo ndiyo Kaaba yangu.

Alipofika Batala, Rai Jasmal Khan, Mkuu wa tarafa ya Batala, alimwekea karibu na stesheni ya garimoshi nyumba ya kupumzika iliyoungana na nyumba yake mwenyewe, na pia akapata heshima ya kukutana na Hudhur[as]. Hudhur[as] alimshukuru kwa hisani yake hiyo. Baada ya kula chakula cha mchana, Hudhur[as] akaenda stesheni kwa kumpokea mkewe. Kabla ya yeye kufika stesheni, garimoshi liliishafika, na Hadhrat Amman Jan alikuwa akimtafuta. Kwa vile watu walikuwa wengi, kwa hiyo hakuweza kuonekana kwa muda kidogo. Kisha alipomwona, akamwita akisema "babaye Mahmud". Hapo Hudhur[as] akasonga mbele na kupeana mkono na mkewe. Baadaye, Hudhur[as] akarudi makazini. Baada ya kupitisha saa za adhuhuri akaelekea Qadian kabla ya alasiri, na kufika kabla ya jua kutua salama salimini.

MARADHI YA HADHRAT MIRZA MUBARAKA AHMAD, 21 AGOSTI 1907

Imeshatajwa katika matukio ya mwaka 1899 kwamba Hadhrat Mirza Mubaraka Ahmad mwana mdogo wa Hudhur[as] aliyezaliwa tarehe 14 Juni 1899 alikuwa na sura nzuri na tabia njema. Alikuwa na umri zaidi ya miaka 8. Tarehe 21 Agosti 1907, yeye alipata homa. Homa ilikuwa kali kiasi hiki kwamba baadhi ya wakati alizimia na kuweweseka. Hudhur[as] alimwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu sana kwa afya yake. Hapo tarehe 27 Agosti 1907, yaani siku ya saba, Mwenyezi Mungu Alimfunulia kwamba "Limekubaliwa. Homa ya siku tisa imeondoka." Hiyo ilimaanisha kwamba homa bado itaendelea kwa siku mbili kisha itaondoka. Basi baada ya siku 9 kamili siku ya kumi yaani tarehe 30 Agosti 1907 homa ya kijana iliondoka na kijana alipona kiasi hiki kwamba alienda bustanini kupunga hewa.

NDOA YA MUBARAK AHMAD, – 30 AGOSTI 1907

Hadhrat Amman Jan alimpenda sana Mariamu Begam binti wa Hadhrat Dkt. Seyyid Abdus Sattar Shah. Kwa hiyo, alitaka kwamba haraka iwezekanavyo ndoa yake na Mubarak Ahmad itangazwe na hivyo amfanye awe kama binti yake tangu utotoni. Njia ya Hudhur[as] sikuzote ilikuwa kwamba alikuwa akiheshimu sana matakwa ya Hadhrat Amman Jan. Kwa hiyo, aliidhinisha ndoa hiyo baada ya ridhaa ya Bwana Daktari. Basi, tarehe 21 Agosti 1907 baada ya sala ya alasiri, Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin alitangaza ndoa ya Mubarak Ahmad. Katika hotuba ya ndoa Hadhrat Maulana Nuruddin alitangaza ndoa pia ya mwanaye Mian Abdul Hayyi kwa Bi Haamida Begam binti wa Hadhrat Pir Manzur Muhammad.

KIFO CHA MUBARAK AHMAD, 16 SEPTEMBA 1907

Baada ya ndoa, kwa siku 13 afya ya kijana ilikuwa nzuri, lakini siku ya 14 yaani tarehe 14 Septemba 1907, mara akawa mgonjwa. Siku hiyo Hudhur[as] alifunuliwa:

لَا عِلَاجَ وَلَا يُحْفَظُ Yaani, sasa hakuna tiba wala hatasalimika. Basi, baada ya siku mbili tu tarehe 16 Septemba 1907 kijana Mubarak Ahmad alifariki. *Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun.*

Wakati alipozaliwa Mwenyezi Mungu alimwambia Hudhur[as] kwamba mtoto huyu atafariki haraka, lakini aliendelea kuifasiri. Aliandika:

> "Mwenyezi Mungu Alinipasha habari kwamba Nitakupa mwana mmoja mwingine, na ndiye huyu mwana wa nne aliyezaliwa sasa ambaye amepewa jina Mubarak Ahmad. Habari ya kuzaliwa kwake nilipewa takriban miaka miwili kabla. Kisha nikaambiwa ambapo miezi miwili ilibaki katika kuzaliwa kwake. Alipokaribia kuzaliwa nilipata ufunuo huu: اِنِّیْ اَسْقُطُ مِنَ اللّٰہِ وَ اُصِیْبُہٗ . Yaani, naanguka ardhini kwa mkono wa Mungu na nitarejea Kwake. Kwa *ijtihadi* yangu niliifasiri kwamba mwana huyu atakuwa mwema na ataelekea kwa Mungu, au atafariki haraka. Mwenyezi Mungu Anajua kwamba kati ya mambo hayo mawili jambo lipi ni sawa

na takwa lake."[549]

Hatimaye, matukio yalithibitisha kwamba jambo la mwisho tu lilikuwa sahihi, yaani "Mwana huyu atafariki haraka". Hudhur[as] alimpenda sana mwanaye, Mubarak Ahmad, na kijana pia alimpenda yeye sana. Muda kidogo kabla ya kifo, kijana alipeana na Hudhur[as] mkono mara ya mwisho na kasema kwamba sasa nataka kulala na mara baada yake akafariki. *Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun*.

Shairi aliloandika Hudhur[as] kuhusu kifo chake, ndani ya ubeti wake mmoja ameashiria kwenye jambo hilo. Shairi lenyewe ndilo lifuatato:

> Mwanangu mpendwa, Mubarak Ahmad, aliyekuwa na sura nzuri na tabia njema, ametuaga leo akituhuzunisha moyo wetu.
>
> Akasema nataka kulala, hiyo ilikuwa kauli yake ya mwisho. Lakini, akalala hata kwamba hakuamka tena, na tukashindwa kumwamsha.
>
> Alikuwa na umri wa miaka minane na miezi michache wakati Mungu Alipomwita. Mwitaji ni Mpendwa kuliko wote, Ee moyo, ujitolee Kwake tu.

MAKALA YA HUDHUR[AS] NA MKUTANO WA ARIA SAMAJ YA WACH-CHOWALI, LAHORE, 2-4 DESEMBA 1907

Mnamo mwaka 1907, Aria Samaj ya Lahore, baada ya kufanya mkutano wao wa mwaka waliamua kwamba katika Desemba 1907 mkutano wa dini ufanyike ambamo waalikwe viongozi wa dini mbalimbali na waombwe kutoa hotuba juu ya "Kitabu kipi kinaweza kuwa cha kufunuliwa na Mungu".Wajumbe wa Waaria walimfikia Hudhur[as] pia. Hudhur[as] akikumbuka mwenendo na hulka za Waaria, alitaka kuepa, lakini kwa sababu ya wao kung'ang'amia sana, akasema vizuri, mimi pia nitaandika makala moja juu ya mada hiyo. Waaria walipanga tarehe 2, 3, 4 Desemba 1907 kwa mkutano na kwa kushiriki mkutanoni kila mmoja alitakiwa kununua tiketi ya Anna 4.

Kutoka Qadian ujumbe mmoja ulishiriki mkutanoni chini ya uongozi

[549] Tiryaqul Quluub, uk. 40

wa Hadhrat Maulana Nuruddin. Ilipangwa kwamba hotuba za Mabaniani, Wakristo, Mabarhamu na Waislamu zitatolewa mkutanoni.

Siku ya pili ilipangwa kusomewa makala ya Hudhur[as]. Kwa hiyo, Waahmadiyya wengi kutoka sehemu za mbali na karibu walihudhuria mkutanoni. Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin alisoma makala ya Hudhur[as]. Kwa kusoma makala hiyo kwa jumla yalitumika masaa mawili na dakika 15. Makala hiyo ilikuwa ni nini?! Hiyo inaweza kujulikana hali yake kwa kuiona tu. Hudhur[as] alitoa mapendekezo machache ndani ya makala hiyo; kama Waaria wangeahidi kuyafuatilia, mlango wa upinzani wa kidini na ukinzani ungeweza kufungwa. Lakini badala ya kuyazingatia mapendekezo hayo yaliyoandikwa kwa kuiondoa kupingana na kukinzana, Waaria, katika makala yao ya mwisho iliyosomwa siku ya tatu, hawakuacha kasoro yoyote katika kuudhi kwa matusi na maneno makali, ilihali waliishaahidi hapo kabla kwamba katika mkutano kutakuwa hamna jambo lolote kinyume cha ustaarabu wala kuwaudhi wafuasi wa dini yoyote. Hudhur[as] alipojua habari hiyo, aliudhika sana na akadhihirisha huzuni na kutopenda kwake. Akasema kwa nini wanajumuiya wetu waliendelea kusikiliza makala katika hali hiyo, na kwa nini hawakuondoka.

Shutuma walizoleta Waaria dhidi ya Islam na Mtume Mtukufu[saw] katika makala yao, kwa kuzijibu, Hudhur[as] aliandika kitabu kiitwacho *Chashmae Ma'rifat* ambamo mwanzoni mwake alieleza hali ya mkutano, na akajibu kwa kirefu mashambulizi dhidi ya Mtume Mtukufu[saw] na shutuma dhidi ya Islam. Na mwishoni kuna makala ile pia iliyoandikwa kwa kusomwa mkutanoni.

MKUTANO WA MWAKA 1907

Mwishoni mwa Desemba 1907 pia kama kawaida Mkutano wa Mwaka ulifanyika katika Qadian. Watu walioshiriki katika mkutano huo hawakujua kwamba katika Mkutano wa mwaka ujao aliyetumwa na Mungu hatakuwepo baina yetu. Huo ulikuwa Mkutano wa mwisho ambamo wanajumuiya walipata kusikiliza nasaha na maneno matakatifu mdomoni mwa Hudhur[as].

VITABU VYA MWAKA 1907

1. ***Qadian ke Aria Aur Ham***: Kuhusu kitabu hicho kimeshaelezwa juu.
2. ***Hakikatul Wayhi:*** Hiki ni kitabu kikubwa cha mwisho cha Hudhur[as] kilichochapwa katika uhai wa Hudhur[as]. Humo mmeelezwa hali ya Dkt. Abdul Hakim Khan kuritadi, na pia majibu ya shutuma zao ya kuwanyamazisha na kwa watafiti kuwaelimisha na kuwatuliza. Njia za kuwatambua Mawalii wa Mungu na daraja zao pia zimeelezwa katika kitabu hicho na ishara karibu 200 pia. Nina yakini kwamba kama mtu kwa moyo safi, kwa ajili ya Mungu, akisoma kitabu hicho kizuri, yeye kwa yakini atapata nuru moyoni mwake na, zitaondoka kabisa moyoni mwake giza zote za kutoamini uwepo wa Mungu. Laiti watafutao haki wakisome kwa makini kamili.
3. ***Chashmae Ma'rifat:*** Kitabu hiki kimeshaelezwa juu.

NDOA YA HADHRAT NAWAB MUBARAKA BEGAM, 17 FEBRUARI 1908

Amatul Hamid mke wa Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan, Chifu wa Malerkotla, aliyekuwa mke wake wa pili, alifariki tarehe 27 Novemba 1906, katika umri wa miaka 20 akiugua kwa miezi mitano. Na ilihitajika kumtafutia Bwana Nawab mke. Hudhur[as] pia alijaribu kwa ajili yake katika sehemu kadha, lakini ikashindikana kwa sababu ya kizuizi hiki au kile. Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin alifikiria moyoni mwake kuhusu binti fulani lakini kwa sababu kadha akakaa kimya mpaka siku moja Hadhrat Nawab Muhammad Ali Khan akamjia na akaomba kuandika barua kwa fulani kuhusu habari hiyo. Hadhrat Maulawii alisema: "Sawa, naandika, lakini moyo haukubali, moyo wangu unataka kitu kingine, lakini nashindwa kunena." Hadhrat Nawab alielewa fikara yake kwa kauli hiyo, na nia ya kuandikisha barua akaacha na bila kusema lolote akaondoka. Kisha alimweleza habari hiyo mke wa Hadhrat Maulawii Abdul Karim, aliyekuwa anakwenda kwao sana, kwamba ujaribu mwenyewe kujua ridhaa ya Hudhur[as] na usinitaje katika habari hii. Lakini kwa vile mama huyo alikuwa mwenye kusema mambo yalivyo, alieleza yote

aliyoyasema Bwana Nawab. Baada yake kwa njia ya Hadhrat Pir Manzur Muhammad mazungumzo yaliendelea na hatimaye ombi lilikubaliwa. Tarehe 17 Februari 1907, baada ya sala ya alasiri, Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin alitangaza ndoa kwa mahari ya rupia 56,000. Katika hotuba ya ndoa baada ya kueleza makusudio, malengo na hekima ya ndoa, alisema hii pia:

> "Nawab Muhammad Ali Khan amepata uhusiano huu na Imamu wa zama a.s., hii heshima na fahari hiyo ni sababu ya bahati yake njema. Kulikuwa na mzee wake mmoja jina lake Sheikh Sadr Jahan[rh]. Mfalme mmoja wa kidunia akimfahamu kuwa mtu mwema, alimwozesha binti yake. Lakini hii ni fadhili kubwa ya Mwenyezi Mungu na hisani yake kwamba leo Mfalme wa dini amempa Muhammad Ali Khan binti yake. Huyu ni mwenye bahati nzuri zaidi kuliko jadi yake. Elimu yangu, dini yangu na imani yangu inaniambia kwamba mheshimiwa huyu ni mwenye bahati nzuri zaidi kuliko Hadhrat Sadr Jahan[rh]."[550]

HADHRAT NAWAB MUBARAKA BEGAM ASIMULIA KUHUSU KUPANGA MAHARI

Kuhusu kupanga mahari Hadhrat Nawab Mubaraka Begam anasimulia kwamba:

> "Hadhrat Nawab alieleza kwamba Hudhur alipopanga mahari yako rupia 56,000 sawa na mapato ya miaka miwili, wakati ule mapato yangu yalikuwa kidogo, lakini nilikaa kimya na sikuona sawa kupinga makisio ya Hudhur[as]. Lakini katika mwaka huo huo kwa kupata mali ya urithi fulani mapato yangu yakawa sawa na rupia 56,000 ya miaka miwili. Yeye alinielezea habari hiyo mara kadha. Baadaye mapato yake ya mwaka yakazidi zaidi, karibu na 37,000 kwa mwaka."[551]

HARUSI, 14 MACHI 1909

Sherehe ya harusi hii ilifanyika hivi kwamba miezi tisa na nusu baada

[550] Kwa maelezo zaidi someni As'habe Ahmad, sehemu 2, uk. 230-231

[551] As'habe Ahmad sehemu 2, Hashia uk. 237

ya kufariki Hudhur[as], tarehe 14 Machi 1909, siku ya Jumapili, saa nane mchana, Hadhrat Amman Jan alimpeleka Hadhrat Nawab Mubaraka Begam kwenye nyumba ya Hadhrat Nawab, iliyoungana na nyumba ya Hudhur[as]. Hadhrat Nawab anasema kwamba wakati ule Hadhrat Amman Jan alisema, "Nakukabidhi binti yangu yatima." Kisha akajawa na majonzi, na akisema Assalamu alaikum akaenda.

KARAMU YA WALIMA, 15 MACHI 1909

Tarehe 15 Machi 1909, Hadhrat Nawab aliwaalika Waahmadiyya wote wa Qadian na baadhi ya wazee wengine wa mji kwenye karamu ya walima.

BAADHI YA FUNUO ZA HUDHUR[AS] ZIKATIMIA KWA NDOA HIYO

Hapa naona wema kusema kwamba kuhusu Hadhrat Nawab Mubaraka Begam alipokuwa na umri wa miaka minne tu, Hudhur[as] alifunuliwa, "Nawab Mubaraka Begam".

UJIO WA KAMISHNA WA FEDHA KATIKA QADIAN, 21 MACHI 1908

Katika mwaka wa 1908 Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, kwa fadhili na hisani ya Mwenyezi Mungu, ilipata maendeleo sana. Wapinzani walikuwa wakituma kwa serikali habari dhidi ya Jumuiya. Inaonekana kwamba kwa kupeleleza ripoti hizo, serikali ilimwagiza Sir James Wilson, Kamishna wa fedha, kuingiza Qadian pia katika matembezi yake kwa kupata habari sahihi kuhusu Jumuiya, waila haionekani sababu ya ujio wa afisa mkubwa kama huyo katika kijiji kidogo. Basi, Kamishna wa fedha wa Panjab alitia Qadian pia katika ratiba ya ziara yake. Hudhur[as] aliishapata taarifa, kwa hiyo Hudhur[as] aliwaita ndugu waheshimiwa wa nje kwa kumpokea Kamishna wa fedha. Na pia alimwalika Bwana Kamishna kwenye chakula, na Bwana Kamishna akakubali. Kwa kupiga mahema ya Bwana Kamishna, ilipangwa sehemu ambapo siku hizi pana jengo kubwa la Talimul Islam College. Sawa na ratiba, tarehe 21 Machi 1908, Kamishna wa fedha pamoja na Bwana King, Disii wa Gurdaspur na Msimamizi wa Mpangaji alifika Qadian. Waheshimiwa wa Jumuiya

waliwapokea. Bwana Mkubwa alikuwa ameshakubali mwaliko wa Hudhur[as] kwenye chakula cha usiku. Yeye pia alitaka kwamba kama Hudhur[as] asione shida ningependa kuonana naye. Hudhur[as] alipoambiwa, akasema kwamba Bwana huyo ni mgeni wetu, kwa hiyo baada ya sala alasiri, mimi mwenyewe nitaenda kuonana naye. Bwana mheshimiwa akapashwa habari hiyo. Basi, saa 11 jioni, Hudhur[as] pamoja na mahadimu wachache akawasili katika kambi la Bwana Kamishna wa fedha. Kwa dakika 45 kikao kiliendelea. Wakaongea juu ya mambo mbalimbali. Bwana mheshimiwa aliuliza maswali kadha kuhusu Jumiya pia, ambayo Hudhur[as] aliyajibu. Hudhur[as] alipokuwa aondoke, Kamishna wa fedha na Disii, wote wawili, walimshukuru. Baada ya kutoka hemani, Hudhur[as] aliona kwamba Waahmadiyya wengi wamejumuika na wanataka kupeana naye mkono. Hapo, Hudhur[as] nje ya mji wa Qadian alisimama sehemu fulani na alipeana mkono na mahadimu wote.

UJIO WA WATALII WAWILI WAMEREKANI KATIKA QADIAN, 7 APRILI 1908

Tarehe 7 Aprili 1908, watalii wawili Wamerekani pamoja na mama mmoja wakaja Qadian kumwona Hudhur[as]. Wakamwuliza Hudhur[as] maswali mengi kuhusu mubahala na Dkt. Dowie, ishara za ukweli wa Hudhur[as] na makusudio ya ujio, ambayo Hudhur[as] aliyajibu kirefu. Katika ishara, Hudhur[as] alitaja kuwa ujio wao pia kutoka mbali ni ishara. Hudhur[as] akasema:

> "Nyinyi wenyewe ni ishara ya ukweli wangu. Miaka 26 kabla, wakati nilipokuwa mtu nisiyetambulika katika kijiji hiki na sikuwa na njia yoyote kujitangaza na kupata umaarufu, Mwenyezi Mungu Alidhihirisha kwa ulimi wangu kwamba يَأْتُوْنَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيْقٍ Yaani, watu kutoka njia za mbali watakufikia. Sasa tazameni, nyinyi hamjui kuhusu utabiri huu, hata hivyo mmeutimiza. Pengine, kama mngeujua, mngesita kuutimiza, lakini Aliyotaka Mungu kufanya Akaifanya tu. Nchi gani inaweza kuwa mbali na Marekani, hata kutoka kuko watu walinifikia, tena katika sehemu ambapo hakuna chochote cha kuvutia. Mkitafakari, basi jambo hili ni zaidi kuliko kuhuisha

mfu. Kuhuisha wafu kumekuwa ni hadithi tu. Na hili ni jambo la juzi. Utabiri umeishachapishwa kabla, na ukweli wake mmeona kwa macho yenu.”[552]

SAFARI YA LAHORE NA KUKARIRIWA KWA FUNUO ZA KIFO, 27 APRILI 1908

Siku zile afya ya Hadhrat Amman Jan ilikuwa si nzuri. Kwa hiyo, alitaka atibiwe na daktari wa kike huko Lahore. Hudhur[as] kwa athari iliyofichika alikuwa anasita kwenda safarni, lakini kwa kusisitizwa na Hadhrat Amman Jan akawa tayari. Tarehe 26 Aprili, asubuhi na mapema alifunuliwa: ‘Usijione salama katika hila za zama’.[553]

Hapo alisubiri siku hiyo, na tarehe 27 Aprili 1908 alisafiri kuelekea Lahore. Hudhur alipofika Batala, akajua kwamba leo behewa la kuteuliwa haliwezi kupatikana. Hapo, kwanza alinuia kurudi Qadian, lakini baada ya kufikiria alikaa hapo hapo Batala kusubiri behewa la kuteuliwa. Tarehe 29 Aprili 1908 alipopata gari, alienda Lahore. Huko Lahore alikaa katika nyumba ya Khwaja Kamaluddin, na akaifanya nyumba ya Bwana Khwaja kuwa marejeo ya halaiki. Waahmadiyya na wasiokuwa Waahmadiyya walianza kuja kwa kumzuru Hudhur[as]. Mheshimiwa mmoja asiyekuwa Mwahmadiyya aliyekuwa miongoni mwa wanamfalme wa Kabul aitwaye Muhammad Ibrahim Khan alimwalika Hudhur[as] nyumbani mwake kwa chakula, lakini kwa sababu fulani Hudhur[as] hakuona sawa kwenda makazini mwake. Hapo, mwanamfalme huyo akamtumia Hudhur[as] rupia 50 kwa ombi hili kwamba Hudhur[as] atayarishe chakula kutoka kwangu na kula makazini mwake. Kwa vile muda wa kukaa ulizidi, kwa hiyo Hadhrat Maulana Nuruddin, Hadhrat Maulana Muhammad Ahsan Amrohi na ndugu wengine pia wakafika Lahore. Gazeti Badr pia lililetwa Lahore kwa muda ili Wanajumuiya waweze kupata habari mpya mpya kila siku.

Katika Lahore upinzani ulikuwa mkali sana, na Hudhur[as] alipofika huko, upinzani huo ulizidi sana. Kila siku nje ya makazi yake

[552] Badr, J. 7, Na. 14, toleo la 19 Aprili 1908

[553] Badr, J. 7, Na.17, Al-Hakam, J. 12, Na.30

wapinzani wakorofi walianza kutoa hotuba chafu na za kuchokoza. Baadhi ya wanajumuiya wakiona fujo zao walikasirika sana. Hapo Hudhur[as] aliwajumuisha wanajumuiya, akawasihi kuvumilia kwa subira na kujizuia, na akasema kuwa mtu aliye mwepesi wa kupandwa na hamaki si shujaa; shujaa ni yule ambaye anazuia hasira na kujitawala nafsi yake. Basi mahadimu wakatenda sawa na nasaha zake na wakaonyesha subira. Watu wenye hulka mbovu walishughulikia matendo mabaya, lakini Mwenyezi Mungu alitia nyoyoni mwa waungwana mawazo ya kumwendea Hudhur. Basi, watu waheshimiwa wakaendelea mfululizo kumfikia na kujifaidisha. Katika muda huo, tarehe 9 Mei 1908, tena alipata ufunuo huu: اَلرَّحِيْلُ ثُمَّ الرَّحِيْلُ۔ اِنَّ اللّٰهَ يَحْمِلُ كُلَّ حِمْلٍ Yaani, kuondoka tena kuondoka, Mwenyezi Mungu Mwenyewe Atabeba mzigo wote.”[554]

Hiyo ilikuwa ishara wazi ya kukaribia wakati wa kifo cha Hudhur[as], lakini Hudhur[as] aliendelea kufanya kazi yake kwa makini na hakudhihirisha wasiwasi wowote. Naam, sawa na suna ya manabii alibadilisha makazi yake kwa kutimiza ufunuo huo kidhahiri na kasema kwamba hii pia ni namna ya kuondoka tu. Lakini Mwenyezi Mungu Alikuwa anataka vingine. Basi akahama nyumba ya Bwana Khawaja na kuhamia nyumba ya Dkt. Seyyid Muhammad Husain Shah. Baada ya siku chache habari ya kifo cha Babu Shah Din, Stesheni Masta, aliyekuwa Mwahmadiyya mwenye ikhlasi, wa Qadian, fikara ya watu kaelekea huko kwamba ufunuo wa kuondoka uliashiria kifo cha Bwana Babu tu. Lakini zipo dalili za kuhakikisha kwamba Hudhur[as] alijua vizuri kwamba ufunuo huo unamhusu Hudhur[as].

Kwa kupata habari ya ujio wa Hudhur[as] katika Lahore, wanajumuiya wengi wa matawi ya nje walihudhuria. Katika Ahmadiyya Buildings ambapo kuna msikiti sasa, sehemu hiyo ilikuwa wazi, hapo kwa kupigwa mahema makubwa ilikuwa inapangwa kusali sala ya Ijumaa.

PROFESA CLEMENT WRAGGE ALIKUTANA NA HUDHUR[AS]

Hudhur[as] alipofika Lahore, mtalii mashuhuri, mwanafalaki na profesa wa Uingereza aliyekaa kwa muda mrefu katika Australia akiajiriwa na

[554] Al-Hakam, J. 12, Na.35, Badr, J. 7, Na. 210

serikali katika idara ya falaki, yeye pia alikuwa amewasili Lahore kwa bahati. Yeye alitoa hotuba juu ya elimu ya falaki karibu na stesheni ya garimoshi ya Lahore. Hadhrat Mufti Muhammad Sadik pia alikuwepo katika hafla hiyo. Baada ya kwisha hotuba, Hadhrat Mufti alimweleza Bwana Profesa madai ya Hudhur[as] na hoja zake. Bwana Profesa alionyesha shauku ya kumwona Hudhur[as]. Basi, yeye na mke wake wakaja mara mbili katika Ahmadiyya Buildings kwa kumwona Hudhur[as], na majibu ya kutuliza ya maswali yake ambayo alikwua hakupata kutoka kwa mtu yeyote, sasa kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu akapata kwa kuonana na Hudhur[as]. Wakati wa kuaga akimshukuru Hudhur[as] akasema kwamba "Nimefurahi sana kwa kupata majibu ya kutosheleza na ya kutuliza ya maswali yangu, nami nimepata utulivu, na kutuliza hivyo si kazi ya mtu yeyote isipokuwa nabii wa Mungu."[555]

WAKILI MIAN FADHL HUSAIN KAONANA NA HUDHUR[AS], 15 MEI 1908

Wakili Mian Fadhl Husain aliyeitwa baadaye Sir Fadhl Husain na kwa miaka mingi alikuwa waziri wa serikali ya India, alikuwa mtu mwungwana. Ingawaje alikuwa na huruma kwa wanadamu wote, lakini hakuweza kuvumilia dhuluma waliyofanyiwa Waislamu. Kwa hiyo, alijaribu sana kurekebisha hali ya kidunia ya Waislamu. Mungu Ampatie malipo bora. Yeye alimjia Hudhur[as] tarehe 15 Mei 1908 na kuuliza baadhi ya maswali ambayo Hudhur[as] alitoa majibu yake ya kutuliza sana."[556]

Kwa mfano, swali lake moja lilikuwa hili kwamba kama wote

[555] Badr, 26 Mei 1908. Maswali maarufu ya Bwana Profesa yalikuwa haya: 1. Ulimwengu huu upo tangu lini. 2. Uhakika wa dhambi ni nini? 3. Kwa nini dhambi yenyewe ipo? 4. Je, baada ya kifo mtu atapata uhai? 5. Je, inawezekana kukutana na roho? 6. Unasemaje juu ya Dhati ya Mungu na sifa zake? 7. Je, Mungu ni upendo? 8. Kwa nini mnyama wa daraja ya juu anakula mnyama wa daraja ndogo. 9. Mwanadamu yupo tangu lili? 10. Unasemaje juu ya nadharia ya Darwin? 11. Je, jua, mwezi na sayari zote zina athari fulani ndani yake? 12. Roho ni za aina ngapi? 13. Unasemaje juu ya itikadi ya kafara? na kadhalika.

[556] Someni gazeti Badr, 24 Mei 1908

wasiokuwa Waahmadiyya waitwe makafiri, basi hakibaki chochote katika Islam. Kwa kujibu Hudhur[as] alisema:

"Simtoi katika Islam anayetamka لَا اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ mpaka kwa kuniita kafiri, yeye mwenyewe awe kafiri. Labda hujui kwamba nilipodai kutumwa na Mungu, basi Muhammad Husain Maulawii Abu Said wa Batala alitayarisha fatuwa kwa juhudi kubwa ambamo iliandikwa kwamba mtu huyu ni kafiri, ni dajali, amepotea, asisaliwe sala yake ya jeneza; atakayemsalimia, au kupeana naye mkono au kumwita Mwislamu, basi huyo pia ni kafiri. Sasa sikilizeni, swali hili limekubaliana na wote kwamba amwitaye mumini kuwa kafiri, huyo mwenyewe huwa kafiri. Basi swala hilo twawezaje kulikanusha. Nyinyi mseme wenyewe kwamba katika hali hiyo tunayo njia gani ya kushika. Hatukuwatolea fatuwa yoyote kwanza. Sasa wanapoitwa makafiri, hayo ni matokeo ya kutuita makafiri. Mtu mmoja aliniomba kufanya mubahala, nilimjibu kwamba kati ya Waislamu wawili mubahala haujuzu. Kwa kujibu aliandika kwamba tunakufahamu u kafiri kabisa. Mtu huyo (Mian Fadhl Husain, Wakili) alisema kwamba wanakuita kafiri, acha waite, lakini kama usiwaite, basi kuna shida gani? Akasema kwamba asiyetuita makafiri, sisi pia hatumwiti kafiri. Lakini anayetuita kafiri, kama tusimwite kafiri basi twalazimika kupinga Hadithi na swala lililokubaliwa na wote, na hatuwezi kufanya hivyo.

Mtu huyo akasema kwamba wale ambao hawakuiti kafiri, kuna tatizo gani kusali nao? Akasema: لَا يُلْدَغُ الْمُؤْمِنُ فِيْ جُحْرٍ وَاحِدٍ مَرَّتَيْنِ . Tumeshajaribu sana kwamba watu wa aina hii kwa kweli huwa wanafiki. Hali yao ndiyo hii: وَاِذَا لَقُوا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا قَالُوْا اٰمَنَّا وَاِذَا خَلَوْا اِلٰى شَيٰطِيْنِهِمْ قَالُوْا اِنَّا مَعَكُمْ اِنَّمَا نَحْنُ مُسْتَهْزِؤُوْنَ Yaani, mbele yetu wanasema hatuhitilafiani nanyi, lakini wanapokutana na watu wao faraghani, husema kwamba sisi tulikuwa tukiwafanyia tu dhihaka. Basi watu hao mpaka watangaze kwamba twawaona wafuasi wa Jumuiya Ahmadiyya kuwa waminio, bali twawaona makafiri wale wawaitao makafiri, basi nitawaamuru wanajumuiya wangu leo hii kwamba wasali pamoa nao. Twashikilia ukweli, huwezi kutulazimisha kufuata mambo yaliyo

nje ya Islam. Imo katika Kurani Tukufu فَمِنْهُمْ ظَالِمٌ لِّنَفْسِهٖ وَمِنْهُمْ مُّقْتَصِدٌ وَمِنْهُمْ سَابِقٌ بِالْخَيْرَاتِ Twawaita watu wa tabaka zote tatu kuwa Waislamu, lakini tutawawaita jina gani wanaomwita mumini kuwa kafiri. Wale ambao hawatuiti makafiri, tutawachukulia pia pamoja nao mpaka watangaze kupitia tangazo la kuchapwa la kujitenga nao na waandike kwa kutaja majina yao kwamba twawaona hao wakufurishao sawa na Hadithi ndio makafiri kweli."[557]

Tarehe 16 Mei 1908, usiku alifunuliwa ufunuo huu: "Usitegemee uhai usio wa kudumu", uliojulisha kwamba wakati wa kifo ni karibu sana, lakini Hudhur[as] kwa utulivu kamili aliendelea kushughulikia kazi yake.

MWALIKO KWA MACHIFU NA WAHESHIMIWA VIONGOZI WA LAHORE NA MAHUBIRI YA MWONGOZO, 17 MEI 1908

Tarehe 17 Mei 1908, sawa na pendekezo la Hudhur, machifu na viongozi wa mji walialikwa kwenye chakula. Mpango wa kuonana na Hudhur[as] ulipangwa ugani mwa nyumba ya Dkt. Seyyid Muhammad Husain Shah. Watu wote walipojumuika ndani ya hema kubwa, kwa kusisitizwa sana na watu, Hudhur[as] alianza kutoa hotuba saa tano ambamo alijibu vya kutuliza sana shutuma za wapinzani juu ya madai na mafundisho yake. Alitimiza hoja juu ya wapinzani kwa njia ya dalili imara sana. Saa sita Hudhur[as] akauliza "muda wa kula chakula unapita, mkitaka nikome kuhutubia." Lakini watu wengi kwa sauti moja wakasema kwamba "chakula tunakula kila siku, lakini chakula hiki cha kiroho hakipatikani kila siku, kwa hiyo Hudhur aendelee kutoa hotuba. Hotuba yake hiyo adhimu[558] iliishia saa 7 mchana. Baadaye, Hudhur[as] pamoja na wageni wakaenda kula chakula katika uga wa marehemu Khwaja Kamaluddin uliokuwa hatua chache mbali.

[557] Badr, 24 Mei 1908

[558] Hotuba hiyo kamili ilichapwa katika Badr la 25 Juni 1908.

KUONDOA KOSA LA AKHBARE AAM KUPITIA BARUA, 23 MEI 1908

Kwa hotuba hiyo ya Hudhur[as] baadhi ya watu walidhani kwamba ameachilia mbali dai lake la unabii. Katika "Akhbare Aam" la 23 Mei 1908, habari hiyo ilichapishwa, lakini hiyo ilikuwa kwa sababu ya kutokuelewa tu. Hudhur alikataa unabii wenye sheria mpya tu sio unabii wenyewe. Alipopata gazeti hilo, aliona lazima kudhihirisha ubatili wake na uhakika wake wenyewe, na akaliandikia "Akhbare Aam":

> "Katika msitari wa pili, safu ya kwanza ya toleo la Akhbare Aam la 23 Mei 1908, imeandikwa habari hii kunihusu mimi kuwa kana kwamba nimekanusha unabii wangu katika mkutano wa mwaliko. Kwa kujibu hiyo ibainike kwamba nilisema mkutanoni katika hotuba kwamba sikuzote niliendela kuwaarifu watu kupitia vitabu vyangu, na hata sasa pia nadhihirisha kwamba ninatuhumiwa kuwa nadai ule unabii ambao kwa sababu yake sihusiki kabisa na Islam, yaani najiona kuwa nabii wa kujitegemea wa aina hii kwamba sioni haja yoyote ya kuifuata Kurani Tukufu na nimezusha shahada yangu na kibla tofauti, na naona sheria ya Islam kana kwamba imetanguka na natoka nje ya utii na ufuasi wa Mtume Mtukufu[saw]. Tuhuma hiyo si sahihi, bali kwangu dai la unabii wa namna hii ni kufuru. Sio leo tu, bali katika kila kitabu nimeandika daima kwamba sina dai la unabii wa namna hiyo, na hiyo ni tuhuma kabisa juu yangu. Na ninapojiita nabii maana yake ni hii tu kwamba nina heshima ya kuongea na Mungu. Yeye Anaongea nami sana, na Ananijibu ninapomwuliza na Ananidhihirishia mambo mengi ya ghaibu, na Ananifichulia siri za zama zijazo. Mpaka mtu awe na ukaribu mahususi, Yeye Hadhihirishi siri hizo kwa wengine. Na kwa sababu ya wingi wa mambo hayo Ameniita nabii. Basi, mimi ni nabii sawa na amri ya Mungu; na kama mimi niikanushe, hiyo itakuwa dhambi yangu. Na Mungu Anaponiita Nabii, basi nawezaje kukanusha. Nipo imara juu yake mpaka wakati ule niage dunia hii. Lakini mimi si nabii kwa maana hii kwamba najitenga na Islam au natangua amri yoyote ya Islam. Shingo

yangu ipo chini ya nira ya Kurani Tukufu. Yeyote hana nguvu kwamba aweze kufuta hata nukta moja au alama moja ya Kurani Tukufu... Mimi nasema si kwa kujisifu, bali kwa fadhili ya Allah na kwa sababu ya ahadi yake kwamba kama dunia nzima iwe upande mmoja na upande mwingine nisimamishwe mimi peke yangu, na jambo fulani liletwa ambalo kwalo hujaribiwa waja wa Mungu, basi katika shindano hilo Mungu Atanishindisha, na kwa kila jiha Mungu Atakuwa nami. Basi, kwa sababu hii hii Mungu Ameniita jina nabii, kwani katika zama hizi mimi pekee nimejaliwa kuongea Naye kwa wingi na kupewa elimu za mambo ya ghaibu kwa wingi."[559]

PENDEKEZO LA KUTOA HOTUBA KATIKA MKUTNAO WA HADHARA, NA "PAIGHAME SULH"

Hotuba aliyotoa Hudhur[as] kwenye karamu kwa vile ilikuwa kwa watu maalumu, kwa hiyo baadhi ya waheshimiwa walipendekeza kwamba Hudhur[as] atoe hotuba katika mkutano wa hadhara pia ambamo watu wakishiriki kwa wingi wanufaike. Hudhur[as] alikubali pendekezo hilo na akaanza kuandika makala. Kichwa cha maneno ya makala kilikuwa ni "Paighame Sulh". Hudhur[as] alitaka kwa kupitia ujumbe huu suluhu ipatikane kidini kati ya kaumu mbili mashuhuri za India, yaani kati ya Mabaniani na Waislamu. Na kwa ajili yake Hudhur[as] alitoa mapendekezo machache pia, lakini kabla ya kupatikana nafasi ya kusomwa makala hiyo, alifariki.

NASAHA YA MWISHO

Hadhrat Dkt. Hashmatullah Khan anasema:

"Siku mbili kabla ya kufariki, Hudhur[as] alikaa siku moja katika ukumbi wa nyumba ya marehemu Khwaja Kamaluddin baada ya sala ya adhuhuri na alasiri. Wakati huo, watu 15-20 walikuwepo mbele ya Hudhur[as], na mimi pia nilikuwepo … Wakati huo, Hudhur[as] alieleza mambo machache kama nasaha. Katika maneno hayo ya Hudhur[as] nakumbuka vizuri mpaka leo hii maneno haya: "Jumuiya Ahmadiyya inapaswa kufikiria

[559] Tablighe Risalat, J. 10 uk. 132

kwamba upande mmoja malaki ya watu wanawaita makafiri, kama upande wa pili hawa pia wasingekuwa waaminio machoni mwa Mwenyezi Mungu, basi hii itakuwa hasara marudufu."

Bwana Daktari anasema:

Kadri ninavyokumbuka, hiyo ilikuwa nasaha au wasia wa mwisho wa Hudhur[as] niliosikia kwa masikio yangu."[560]

VITABU VYA 1908

1. ***Chashmae Ma'rifat*:** Sababu ya kuandika kitabu hiki imeshaelezwa juu kwamba Waaria walifanya mkutano mjini Lahore, tarehe 2-3-4 Desemba 1907. Shutuma zilizoletwa mkutanoni zimejibiwa kikamilifu ndani yake. Hudhur[as] aligawa kitabu hicho katika sehemu tatu. Katika sehemu ya kwanza yamebatilishwa majisifu ya Waaria na kuongopa kwa kuihami Veda na kudhihirisha mazuri yake. Katika sehemu ya pili, shutuma zilijibiwa alizoleta Mwaria dhidi ya Kurani Tukufu na Mtume Mtukufu[saw]. Katika sehemu ya tatu sifa teule za Islam zimeelezwa. Na mwishoni, makala ile imeunganishwa iliyosomwa katika mkutano huo kwa niaba ya Hudhur[as].

MWITO WA KUSHINDANA KATIKA KUKUBALIWA DUA:

Katika kitabu hicho, kwa kutimiza hoja juu ya maulamaa, alichapisha tangazo moja pia lenye kichwa cha maneno: رَبَّنَا افْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِالْحَقِّ وَأَنْتَ خَيْرُ الْفَاتِحِيْنَ , yaani Ewe Mungu wetu, Utoe hukumu baina yetu na baina ya kaumu yetu kwa haki. Nawe ndiwe Mbora wa wanaohukumu. Kisha Hudhur[as] aliandika:

"Leo, tarehe 15 Mei 1908, nilifikiria moyoni kwamba kuna njia nyingine ya uamuzi. Labda mchamungu yeyote anufaike nayo na ajitoe katika mzunguko wa hatari wa kukana. Na njia yenyewe ni hii kwamba miongoni mwa wapinzani wangu aliye mpinzani mkali zaidi anayeniona kuwa kafiri na mwongo ashindane nami akichaguliwa na masheikh 10 kwa akali walio maarufu na wakuu 10 mashuhuri kwamba tujaribu ukweli au

[560] Al-Fadhl, 12 Novemba 1959

uongo wetu juu ya wagonjwa wawili wenye maradhi makali. Yaani, hivi kwamba tuchukue wagonjwa wawili walioshikwa na maradhi mbali mbali, tugawe wagonjwa hao wawili kwa kipiga kura na kila mmoja wetu amwombee mgonjwa wake. Basi yule ambaye mgojwa wake apone kabisa au apate umri mrefu kuliko mgonjwa wa pili, mtu huyo atafahamika kuwa mkweli. Hayo yote ni katika hiari ya Mungu. Nami nikitegemea ahadi ya Mwenyezi Mungu natangulia kutoa habari hii kwamba mgonjwa wangu, Mungu Atamponya au Atamzidishia umri wake kuliko mgonjwa mwingine, na jambo hili litakuwa shahidi wa ukweli wangu... lakini itakuwa sharti hii kwamba mtu mpinzani atakayesimama kunikabili yeye mwenyewe na masheikh 10 wengine au wakuu 10 wenye itikadi kama yake watangaze kwamba nikishinda wataniamini na watajiunga na Jumuiya yangu. Ikirari hii ni lazima waitangaze katika magazeti matatu mashuhuri. Hiyo ndiyo itakuwa sharti upande wangu pia... Shindano la aina hii litaleta faida hii kwamba mtu mwenye ugonjwa wa hatari aliyekata tamaa kuishi, Mwenyezi Mungu Atasalimisha uhai wake na ishara itadhihirika ya aina ya kuhuisha wafu. Kwa kupambanua ukweli na batili, hili lilikuwa shindano zuri sana, lakini hata mtu mmoja hakudhihirisha kujitokeza kwa shindano hilo.

2. **Paighame Sulh** (Ujumbe wa Suluhu): Kwa lengo la kusuluhisha kaumu mbili mashahuri za India, yaani Mabaniani na Waislamu, Hudhur[as] alianza kuandika hotuba juu ya mada hiyo, ambayo kabla haijakamilika, Hudhur[as] alifariki. *Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiun*. Hata hivyo, sehemu iliyoishaandikwa ilitosha kwa kusuluhisha. Baada ya Hudhur[as] kufariki hotuba hiyo ilisomwa na Khwaja Kamaluddin, tarehe 21 Juni 1908, siku ya Jumapili, saa moja asubuhi, katika ukumbi wa Chuo Kikuu, katika hafla kubwa. Mwenyekiti wa mkutano huo ambamo hotuba hiyo ilisomwa, alikuwa Jaji Sir Pratul Chandra Chatterjee wa mahakama kuu. Ukumbi ulijaa kabisa, hata nje pia watu walisimama kwa wingi. Watu walipenda sana mapendekezo

ya suluhu yaliyoandikwa katika hotuba. Wakati huo watu walikuwa tayari kutia saini pia, lakini kwa kufikiri kwamba nia hiyo isiwe kwa sababu ya athari ya mara moja ya hotuba, kwa hiyo kutia saini kuliahirishwa hadi wakati mwingine. Lakini saini hazikutiwa, na ikasikika kwamba Waaria wakiona ni kinyume cha makusudio yao hawakutaka kutia saini.

MARADHI ALIMOFIA

Hudhur[as] alikuwa ameshughulikia kuandika hotuba yake "Paighame Sluh", tarehe 20 Mei 1908, alipopata ufunuo huu: اَلرَّحِيْلُ ثُمَّ الرَّحِيْلُ وَالْمَوْتُ قَرِيْبٌ yaani wakati wa kuondoka umewadia. Naam, wakati wa kuondoka umewadia na kifo kipo karibu.[561]

Ufunuo huu ulieleza wazi wazi kuwa kifo cha Hudhur[as] kimekurubia sana. Kwa hiyo, Hudhur[as] hakuufasiri ufunuo huo. Kwa kuona funuo za aina hii mfululizo, Hadhrat Amman Jan akapata wasiwasi, akasema sasa turudi Qadian. Akajibu: "Sasa tutaenda Atakapotupeleka Mungu." Siku hizo Hudhur[as] alishughulikia kuandika hotuba ya Paighame Sulh".[562] Baada ya kupata ufunuo huo, Hudhur[as] akajitahidi zaidi na kuharakia kuandika hotuba. Hatimaye, jioni ya 25 Mei akikamilisha madhumuni haya akamkabidhi mwandishi. Dalili zinaonyesha kwamba akifahamu kwamba baada ya leo atapata nafasi au la ya kuandika madhumuni hayo akaahirisha kuandika kulingana na kumbukumbu zilizobaki, alimkabidhi mwandishi aliyoandika. Baada ya sala ya alasiri, Hudhur[as] alitoa hotuba fupi juu ya kifo cha Nabii Isa[as] iliyokuwa hotuba ya mwisho ya Hudhur[as]. Kisha sawa na kawaida yake alitoka nje kupunga hewa. Lilikuwepo gari la farasi la kukodishwa, Hudhur[as] alimwambia Hadhrat Sheikh Abdur Rahman Qadiani, mfuasi wake mwenye ikhlasi kwamba mwambie mwenye gari[563] kwamba twataka kurudi baada ya kupunga hewa kwa muda wa saa moja tu. Atupeleke

[561] Badr, J. 7 Na. 22

[562] Silsila Ahmadiyya, uk. 182

[563] Pamoja na mwenye gari aliketi marehemu Mian Shadi Khan na kwenye ngazi ya nyuma ya gari alisimama Hadhrat Bhai Abdur Rahman Qadiani kama mlinzi.

mbali kiasi hiki tu kwamba turudi nyumbani katika muda huo. Basi amri hiyo ya Hudhur[as] ikafuatwa, na akarudi baada ya kupunga hewa. Wakati huo, Hudhur[as] alikuwa hana maradhi, isipokuwa kwa sababu ya kuandika mfululizo alikuwa na udhaifu kidogo, na pengine kwa athari iliyofichika ya tukio lijalo alikuwa na lepe la usingizi. Akasali sala za Magharibi na Isha, kisha akala chakula kidogo akalala kupumzika.

USIMULIZA WENYE KUONGEZA IMANI

Mimi mwandishi wa maneno haya nimesikia usimulizi huu kutoka kwa masahaba kadha wa zamani wa Hudhur[as], kati yao nakumbuka hasa majina ya Hadhrat Babu Ghulam Muhammad wa Lahore, Mnyapara, na Hadhrat Mian Abdul Aziz Mughal kwamba safari moja Hudhur[as] alipokuja Lahore, sisi vijana wachache tulishauriana kwamba viongozi wakubwa wa mataifa mengine wanapokuja hapa vijana wa mataifa yao wenyewe wanayavuta magari yao badala ya mafarasi. Na kiongozi ambaye Mwenyezi Mungu Ametupatia ni adhimu sana hata wafalme wakubwa pia hawana thamani mbele yake. Kwa hiyo, yatupasa leo tuvute gari lake badala ya farasi. Basi tulimwambia mwenye gari kwamba ondoa farasi wako, leo sisi tutavuta gari. Mwenye gari akafanya hivyo. Hudhur[as] alipokuja nje, aliuliza kwamba mafarasi wako wapi? Tukasema, kwamba Hudhur, viongozi wa mataifa mengine wanapokuja, vijana wa kaumu yao wanavuta magari yao. Leo sisi tutapata heshima ya kuvuta gari la Hudhur[as]. Akasema: Tieni farasi mara moja; sikuja duniani kuwafanya wanadamu kuwa wanyama, bali nimekuja kuwafanya wanyama kuwa wanadamu. Allah, Allah, ni mawazo mema yaliyoje ya Masihi[as] wa Mungu. Wako wengi wanaopata ladha na wanaona fahari kwamba gari lao livutwe na wanadamu badala ya wanyama, lakini Hudhur[as], aliyetumwa kwa kuwafanya wanyama kuwa wanadamu akakatalia mbali heshima hiyo isiyo na maana isiyotakikana, na akapenda kuimarisha heshima sahihi ya binadamu.
اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَعَلٰى اٰلِ مُحَمَّدٍ وَبَارِكْ وَسَلِّمْ اِنَّكَ حَمِيْدٌ مَّجِيْدٌ

Nilisahau kuandika usimulizi huu, lakini Mwenyezi Mungu Ampe

Kureshi Muhammad Sadik fadhili zake, aliyenikumbusha na nimejaaliwa kuuandika kwa sababu yake. Mungu Ampatie malipo bora.

KIFO, 26 MEI 1908

Sasa twaandika tukio la kifo cha Hudhur[as]. Katika maisha ya Hudhur[as], hili ni tukio la mwisho, kwa hiyo inaonekana yafaa kuandika maelezo ya tukio hili yanukuliwe kutoka katika kitabu "Silsila Ahmadiyya" cha Mirza Bashir Ahmad, mwanaye Hudhur[as], ambaye zaidi ya kuwa mwanahistoria wa kutegemewa ni shahidi aliyeona kwa macho yake pia. Anasema:

> "Karibu na saa tano alisikia haja ya kujisaidia. Akasimama na akaenda kujisaidia. Alikuwa mara nyingi akipata tatizo la kuhara, sasa pia alihara na akahisi udhaifu. Baada ya kurudi akamwamsha mama yangu na akasema kwamba nimehara, nami nimedhoofika sana. Mara moja yeye akainuka na akajikalia karibu naye. Kwa vile alikuwa akijisikia vizuri kwa kukandwa miguu, kwa hiyo akikaa kitandani akaanza kumkanda miguu yake. Katika hali hiyo, tena alisikia haja ya kujisaidia, kwa hiyo akaenda kujisaidia. Aliporudi akawa na udhaifu kiasi hiki kwamba hakujiweza wakati wa kujilaza kitandani, na akaanguka tu kitandani. Hapo mama akiwa na wasiwasi akasema "Allah! yaelekea nini kutokea"? Hudhur akasema: 'Hii ni ile ile niliyokuwa nikisema." Yaani, wakati uliowekwa umeshawadia. Pia akasema, mwite Bwana Maulawii. (Yaani Hadhrat Maulawii Hakim Nuruddin ambaye juu ya kuwa karibu naye sana alikuwa tabibu mahiri.) Na akasema hii pia kwamba waamshe Mahmud (yaani kaka yetu Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad) na Bwana Mir (yaani, Hadhrat Mir Nasir Nawab aliyekuwa mkwe wa Hudhur[as]). Basi, watu wote wakajumuika. Na baadaye Dkt. Seyyid Muhammad Husain Shah na Dkt. Mirza Yakub Beg pia waliitwa. Jitihada yote iliyowezekana kwa binadamu ya kumtibu ilifanywa lakini mtu hawezi kubadilisha takdiri ya Mungu. Udhaifu uliendelea kuzidi kwa kupita muda. Baada yake alihara tena, kwa sababu hiyo udhaifu ulizidi kiasi hiki kwamba papo halikuhisika. Na kwa sababu ya kuhara, ulimi na

koo lilikauka, na kwa sababu hiyo alipata shida kuongea. Lakini maneno yaliyosikika wakati huo mdomoni mwake yalikuwa ni haya matatu: "Mungu, Mungu wangu Mpendwa. Hakusema zaidi ya hayo."

"Wakati wa sala ya alfajiri uliwadia. Wakati huo mimi mwandishi (Hadhrat Mirza Bashir Ahmad M.A.) pia nilikuwa nimesimama karibu naye. Akauliza kwa sauti hafifu, "Je, wakati wa sala umewadia." Hadimu mmoja akajibu, naam, Hudhur, wakati umewadia.' Hapo yeye akifanya tayamamu kwa kugusa mikono yake miwili kwa tandikio alianza kusali akilala kitandani, lakini akazimia katika hali hiyo. Alipopata fahamu, tena akauliza: "Je, wakati wa sala umewadia." Hapo aliambiwa, naam, Hudhur, wakati umewadia.' Tena akanuia na kusali akiwa amelala kitandani. Baadaye hali ya kuzimia kiasi kidogo iliendelea. Lakini kila alipozinduka maneno yale yale yalisikika: "Mungu, Mungu wangu Mpendwa." Na kwa kupita wakati udhaifu uliendelea kuzidi. Hatimaye wakati wa saa nne za asubuhi akapata hali ya gharighari ya mauti na iliyakiniwa kwamba kidhahiri sasa hakuna njia ya kusalimika. Mpaka wakati huo mama alikuwa akiomba kwa subira na hakutamka neno lolote isipokuwa maneno haya, "Ee Mungu , uhai wake umetumika katika huduma ya dini, basi mpe uhai wangu pia." Lakini, sasa ilipopatikana hali ya gharighari ya mauti, akasema kwa huzuni kubwa akilia: "Ee Mungu, sasa huyu anatuacha, lakini usituache." Hatimaye, karibu na saa nne na nusu Hadhrat Masihi Mau'udi[as] alipumua pumzi ndefu moja au mbili na roho yake ikiacha mwili wake ilimfikia Mola wake wa kudumu.[564]

اِنَّا لِلّٰہِ وَاِنَّاۤ اِلَیۡہِ رٰجِعُوۡنَ۔ کُلُّ مَنۡ عَلَیۡہَا فَانٍ وَّیَبۡقٰی وَجۡہُ رَبِّکَ ذُو الۡجَلٰلِ وَالۡاِکۡرَامِ

UMRI WAKE

Sawa na ufunuo wake maarufu: ثَمَانِیۡنَ حَوۡلًا اَوۡ قَرِیۡبًا مِّنۡ ذٰلِکَ اَوۡ تَزِیۡدُ عَلَیۡہِ سِنِیۡنًا [565] wakati wa kifo umri wake ulikuwa miaka 74 sawa na kalenda ya jua,

[564] Silsila Ahmadiyya, uk. 182 hadi 184

[565] Yaani, umri wako utakuwa miaka 80, au itapungua miaka michache au itazidi.

na miaka 76 sawa na kalenda ya mwezi.

SUBIRA YA WATU WA NYUMBANI

Mfano wa subira alioonyesha Hadhrat Amman Jan umeshatajwa juu. Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad pia alivumilia huzuni hiyo kwa subira sana na hakutamka neno lolote isipokuwa Ya Hayyu na Ya Kayyumu. (yaani Ee Mwenye Uzima na Ee Mhifadhi wa milele). Hadhrat Mir Nasir Nawab pia juu ya kupata msiba huo mkubwa alishughulikia kupanga mambo muhimu kwa uimara sana.

HUZUNI KWA KIFO CHA GHAFLA

Habari ya kifo cha Hudhur[as] ilienea mara moja kote mjini. Lakini kwa vile mpaka 25 Mei 1908 Hudhur[as] alishughulikia kazi yake aliyopenda ya kuandika na siku hiyo jioni alienda kwa kupunga hewa pia sawa na kawaida, kwa hiyo licha ya watu wa nje, hata Waahmadiyya wa Lahore pia hawakuwa na yakini juu ya kifo cha Hudhur[as]. Walikuwa wakijumuika katika Ahmadiyya Buildings wakiomba kwamba habari hiyo iwe ni uvumi tu, lakini walipofika katika Ahmadiyya Buildings wakipata ukweli wa habari hiyo, wakafadhaika na wakaonekana kama wendawazimu kwa huzuni kubwa sana. Watu waliolelewa hasa na Hudhur[as], ingawa macho yao yalitiririsha machozi, lakini kwa kuona hali ilivyo wakakaza roho zao, na baada ya kifo cha Hudhur[as] walishughulikia majukumu waliyokuwa nayo kuyatekeleza.

HALI YA WAPINZANI

Hiyo ilikuwa ni hali ya Wanajumuiya. Na wasiokuwa Waahmadiyya, hao walikuwa wa aina mbili. Sehemu moja ya watu waungwana walihuzunika kwa kifo cha Hudhur[as] akiwa jenerali wa Kiislam na idadi yao kubwa ilifika katika Ahmadiyya Buildings kwa kumwona Hudhur[as] mara ya mwisho na kwa kushiriki katika huzuni. Mwenyezi Mungu Awapatie malipo bora. Watu wa aina ya pili walikuwa kinyume cha aina ya kwanza. Walitenda viovu visivyoweza hata kuwazwa. Watu hao chini ya uongozi wa viongozi wao wlijumuika katika uwanja wa Islamia College. Watu hao wakipiga kelele wakitamka maneno machafu na kutukana sana walikuwa wanasogelea nyumba ya Dkt. Seyyid Muhammad Husain Shah kushambulia,

ambamo ulikuwepo mwili wa Hudhur[as], na kila mara wakashindwa. Mwenendo wao ulionyesha kwamba wanayo nia ya kutenda mambo ambayo ni vigumu kutendwa hata na watu duni na dhalili kabisa wa taifa lolote.

KUMWOSHA NA KUMKAFINISHA

Wanajumuiya pamoja na kuzuia ghasia hiyo walikuwa wanafanya matayarisho kupeleka mwili wa Hudhur Qadian. Kati ya saa nane na saa tisa kwa juhudi sana walimaliza kuosha na kuvisha sanda. Kisha jeneza likaletwa kutoka ghorofa ya Dkt. Seyyid Muhammad Husain Shah katika uga la chini. Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin alisalisha sala ya jeneza, na hiyo ilikuwa sala ya kwanza ya jeneza iliyosaliwa hapo hapo katika Lahore.

Zaidi ya matendo maovu na yaliyo kinyume cha ubinadamu, wapinzani waliwafikishia maafisa wa idara ya reli habari hii ya uongo kwamba Bwana Mirza amefariki kwa kipindupindu. Walifanya hivi kwani kupeleka mwili wa aliyefariki kwa kipindupindu kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine ilikuwa ni kinyume cha kanuni ya idara ya reli, kwa sababu ni maradhi ya kuambukiza. Wapinzani walitaka kwamba mwili usiweze kupelekwa Qadian, na watie vikwazo wawezavyo kumzika Lahore. Waahmadiyya waliishajua njama hiyo ya wapinzani. Kwa hiyo, Sheikh Rahmatullah alimwendea Dkt. Meja Sutherland, Principal Medical College Lahore, aliyekuwa ameitwa katika saa za mwisho kwa kumtibu Hudhur[as], na akamwelezea njama ya wapinzani na alimtaka daktari atoe hati ya maradhi alimofia Hudhur[as]. Basi akatoa hati kwamba Hudhur[as] hakufa kamwe kwa kipindupindu, bali amefariki kwa uchovu wa neva kwa sababu ya kuhara. Na ndivyo ulivyokuwa uhakika kwamba Hudhur[as] alikuwa na tatizo hilo la zamani na mara kwa mara alikuwa akipata kuhara. Basi jeneza lilipofika kwenye stesheni, maafisa wa idara ya reli walisema kwa kutegemea habari hiyo ya uongo kwamba tumeshapata taarifa kwamba Bwana Mirza amefariki kwa kipindupindu. Kwa hiyo haiwezekani kupewa behewa. Lakini

walipopewa hati ya Meja Dkt. Sutherland,[566] wakaidhinisha, na jeneza liliwekwa katika behewa la daraja la pili lililoteuliwa.

KITENDO KINGINE CHA KULAUMIWA CHA WAPINZANI

Baada ya jeneza kusafirishwa, wapinzani walifanya kitendo hiki pia kiovu kwamba walimpaka usoni mwa mtu mmoja miongoni mwao rangi nyeusi, wakamlaza kitandani, wakatayarisha jeneza la bandia, na wakibebea, wakapiga makelele ya 'Hae, hae, Mirza. Hae, hae, Mirza'. Na wakaelekea stesheni toka Mochi Darvaza. Jinsi yalivyokuwa matendo yao hayo, anaweza kuyafahamu kila mtu mwenye hisia kidogo za wema. Waahmadiyya walisubiri juu ya fidhuli zao hizo na hawakutenda chochote kinyume cha sheria, ilihali katika hali ya huzuni mwenendo wa wapinzani uliokuwa wa kuudhi mioyo na kuchokoza hauhitaji kuelezwa. Hayo yalikuwa matendo ya watu hao waliompinga Hudhur[as] kwa jina la Islam. Hapa hatutaki kusema lolote kuhusu mienendo ya wapinzani wala hakuna haja yake. Naam, twaweza kusema kwamba wasomaji wa kitabu hiki wataamua wenyewe kwamba wakati huo waliyofanya wapinzani wa Hudhur[as], wanaojiita Waislamu, yahusikaje na mafundisho ya Islam, uungwana na ubinadamu?

JENEZA LIKAFIKISHWA QADIAN

Imeshaelezwa hapo juu kwamba mwili wa Hudhur[as] uliwekwa katika behewa la daraja la pili lililoteuliwa. Garimoshi liliondoka Lahore saa kumi na mbili kasa robo jioni, na usiku saa nne lilifka Batala. Jeneza lilibaki katika behewa na Khuddam walikuwepo kwa kulinda. Saa nane usiku mwili ulitolewa kutoka sanduku, ukawekwa kitandani na Khuddam wakabeba mabegani. Wakitembea maili 11, saa mbili asubuhi wakaufikisha Qadian. Njiani hali ilikuwa ya ajabu.

[566] Kwa hakika Dkt. Sutherland alimtibu Hudhur, kwa hiyo kwa kusadikisha kwake, Dkt. Cunningham akatoa hati hiyo. Tazameni Tarikh Ahmadiyyat, J. 2, uk. 554. — Mwenezi.

Wanajumuiya wenye ikhlasi wakibeba jeneza la mpendwa wao, walitembea, huku macho yao yakitiririsha machozi wakimsalia Mtume Mtukufu[saw]. Na kila mmoja wao alitaka kwamba kwa muda mwingi yeye abebe jeneza begani. Kwani walijua kwamba baada ya miaka 1300 Mwenyezi Mungu Amemtuma Mrekebishaji adhimu na naibu wa Mtume[saw] kwa kurekebisha dunia hii. Basi, miongoni mwa watu wote wa duniani, kwa kubeba jeneza lake Mungu Aliwachagua kwa fadhili na rehema yake. Hivyo, hilo lilikuwa si jambo dogo kwao. Kwa vyovyote, wapenzi wa Masihi[as] wa Muhammad[saw] walifikisha maiti yake Qadian katika masaa machache tu. Na mwili huo uliwekwa kwa uhifadhi wote katika bustani inayoungana na Bahishti Makbara. Na wanajumuiya wote 1200 ambao miongoni mwao watu wengi walifika kutoka sehemu za Ambala, Jalandhar, Kapurthala, Amritsar, Lahore, Gujranwala, Wazirabad, Jammu, Gujrat, Gurdaspur na kadhalika, walipewa nafasi ya kumwona mpendwa wao mara ya mwisho.

Tarehe 27 Mei 1908, wanajumuiya wote waliohudhuria, kwa kauli moja wakimchagua Hadhrat Maulana Hakim Hafidh Nuruddin kuwa Khalifa wa kwanza wa Masihi Mau'udi[as] walifanya baiati kwa mkono wake. Na hivyo ulitimia ufunuo ule wa Hudhur[as] kwamba "Tukio moja litatokea 27".[567]

Mandhari ya baiati ya kwanza pia ilikuwa ya hali ya ajabu. Mioyo ya masahaba wa Masihi Mau'udi[as] ilijeruhiwa sana kwa kifo chake na marhamu yoyote hayangeweza kuponya mioyo yao iliyojeruhiwa, isipokuwa tu wakijumuika tena juu ya mkono mmoja waweze kuendeleza kazi ya Hudhur[as]. Basi Jumuiya yote ya Qadian ilimwomba Hadhrat Maulana Nuruddin kimaandishi kwamba:

> "Sawa na kauli ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as] iliyopo katika kijitabu Al-Wasiyyat, sisi Waahmadiyya tuliotia saini hapa chini, tunaafikiana kwa moyo safi juu ya jambo hili kwamba mhamiaji wa kwanza Hadhrat Al-Haji Maulawii Hakim Nuruddin aliye

[567] Badr, J. 6, Na. 51; Al-Hakam, J. 11, Na. 46 la tarehe 24 Desemba 1907

mjuzi na mchamungu zaidi kati yetu na aliye mwenye ikhlasi sana kwa Hadhrat Imam[as] na rafiki yake kuliko wote na ambaye Hudhur[as] akasema kuwa yeye ni mfano mwema, kama ilivyo dhahiri katika ubeti wake:

Itakuwa vizuri ilioje kama kila mmoja wa umati akiwa Nuruddin;
Na hii itawezekana hapo tu utakapojaa kila moyo nuru ya yakini,

kwamba wafanye baiati kwa mkono wake, kwa jina la Ahmad, wanajumuiya wote wa sasa na wa baadaye wale wapya watakaojiunga katika Jumuiya. Na tangu sasa amri ya Hadhrat Maulawii Sahib itakuwa kwetu kama ilivyokuwa amri ya Hadhrat Masihi Mau'udi na Mahdi[as]."

Basi, sawa na ombi hilo, wakati huo huo Waahmadiyya wote waliokuwepo Qadian, ambao idadi yao ilikuwa 1200, walifanya baiati kwa mkono wa Hadhrat Maulawii.[568]

Na hivyo, baiati hiyo ilisababisha umoja kamili wa Jumuiya. Familia nzima ya Hudhur[as] pia ilikubali ukhalifa wake. Wanajumuiya wa Qadian na waliokuja kutoka matawi ya nje pia walifanya baiati kwa mkono wake. Na wanakamati wote wa Sadr Anjuman Ahmadiyya pia kumpitia katibu wao wa wakati huo Khwaja Kamaluddin walitoa tangazo hili kwa kuwaarifu Wanajumuiya wote:

TANGAZO KUTOKA KWA SADR ANJUMAN

Ndugu, Assalamu Alaikum wa Rahmtullahi wa Barakatuhu.

Hapa Qadian, kabla ya kusali sala ya jeneza la Seyyidi, Kiongozi wetu,

[568] Chini ya ombi hilo, majina yaliyoandikwa, baadhi yao ndiyo yafuatayo:

Rahmatullah (Mmiliki wa English Warehouse), Hadhrat Mirza Mahmud Ahmad, Mufti Muhammad Sadik, Seyyid Muhammad Ahsan Amrohi, Seyyid Muhammad Husain (Asistant Surgeon Lahore), Maulawii Muhammad Ali (Mhariri wa 'Review of Religions'), Khwaja Kamaluddin, Dkt. Mirza Yakub Beg, Khalifa Rashiduddin (Asistant Surgeon), Mirza Khuda Bakhsh, Sheikh Yakub Ali (Mhariri wa Al-Hakam) Nawab Muhammad Ali Khan, Chifu wa Malerkotla, Hadhrat Mirza Bashir Ahmad, Hadhrat Mir Nasir Nawab, Maulawii Ghulam Hasan (Msajili mdogo wa Peshawar), Dkt. Bisharat Ahmad (Asistant Surgeon) na kadhalika.

Hadhrat Masihi Mau'udi na Mahdi[as], sawa na wasia wake ulioandikwa katika kijitabu Al-Wasiyyat, sawa na shauri la wakuu wa Anjuman Ahmadiyya waliopo Qadian na jamaa wa karibu wa Hadhrat Masihi Mau'udi[as], kwa idhini ya Hadhrat Amman Jan, wanajumuiya wote waliopo Qadian, ambao idadi yao ilikuwa 1200, wamemkubali Mheshimiwa Hadhrat Al-Haj Hakim Nuruddin kuwa Khalifa wao na wamefanya baiati kwa mkono wake. Miongoni mwa wakuu hao watu wafuatao walikuwepo: Maulana Hadhrat Maulawii Seyyid Muhammad Ahsan, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, Nawab Muhammad Ali Khan, Sheikh Rahmatullah, Maulawii Muhammad Ali, Dkt. Mirza Yakub Beg, Dkt. Seyyid Muhammad Husain Shah, Khalifa Rashiduddin, mimi Khwaja Kamaluddin. Wahudhuriao wote waliotajwa juu ambao idadi yao imetajwa kabla, kwa kauli moja wamemkubali Mheshimiwa Hakimul Ummat kuwa Khalifatul Masihi. Barua hii inaandikwa kwa wanajumuiya wote kwa kuwaarifu kwamba baada ya kusoma barua hii mara moja wafanye baiati ya Hadhrat Hakimul Ummat, Khalifatil Masihi wal-Mahdi kwa kuhudhuria binafsi au kwa kupitia maandishi.[569]

Baada ya baiati ya Ukhalifa iliyofanyika katika bustani ya Hudhur[as] chini ya mwembe, Hadhrat Khalifatul Masihi I[ra] aliwasalisha Waahmadiyya wote waliohudhuria wakati ule sala ya jeneza ya Hadhrat Masihi Mau'udi[as]. Watu wote kwa huzuni walikuwa wakilia sana mbele ya Mola wao. Pengine wakakumbuka kukaa na Hudhur[as] katika zama zilizopita, na pia kwa kuondoka kwa Hudhur[as] ghafla hivyo huzuni nyingi ilifanya kutiririka machozi machoni na pia kwa kufikiria fikara za ajabu ajabu za aina aina kuhusu hali za siku zijazo. Masahaba wa zamani wanaeleza kwamba hali ya wakati huo ni vigumu kueleza kwa maneno.

Baada ya sala ya jeneza, karibu saa kumi na mbili jioni jeneza likapelekwa Bahishti Makbara na kuzikwa. Hivyo, mja mtakatifu aliyebashiriwa na manabii wote ambaye alileta mapinduzi ya kiroho katika ulimwengu mzimu wa kidini kwa kuuarifu dini iliyo hai,

[569] Al-Hakam, 29 Mei 1908 na Badr, 2 Juni 1908

Mungu Aliye Mzima wa milele, Kitabu kilicho hai na Mtume aliye hai, na aliyeshindisha dini ya Kiislamu juu ya dini zote, si kwa hoja na dalili pekee bali kwa kuonyesha miujiza iliyo hai, ndugu wakamkabidhi Mola wao Aliye Mzima na Mhifadhi wa milele wakarudi nyumbani wakimwombea mara nyingine dua ya mwisho kwa macho yatiririshayo machozi na mioyo yenye huzuni. Sawa na ubeti wa Hadhrat Hassaan bin Thabit[ra], sahaba mkubwa wa Mtume Mtukufu[saw]

كُنْتَ السَّوَادَ لِنَاظِرِيْ فَعَمِيَ عَلَيْكَ النَّاظِرُ
مَنْ شَاءَ بَعْدَكَ فَلْيَمُتْ فَعَلَيْكَ كُنْتُ أُحَاذِرُ

> Yaani Ee Mtume Muhammad[saw], ulikuwa mboni ya jicho langu, leo kwa kifo chako jicho langu limepofuka; sasa baada ya kifo chako afe tu mtu yeyote; mimi sijali mauti yake

wakati huo kila mtu kwa hali yake alikuwa akisema: Ee Masihi wa Mungu, bila wewe sasa duniani mmekuwa na utusitusi machoni mwetu. Sasa afe tu yeyote atakaye hatumjali sisi. ***Allahumma Salli alaa Muhammad wa aali Muhammad.***

Ee Masihi Mtukufu wa Mungu, baraka na amani ziwe kwako mara maelfu kwa maelfu kwamba umepanda mbegu ya mapinduzi ya kiroho kwa mafundisho yako matukufu na mfano mwema, ambayo sasa itaendelea kukua kuchanua na kuzaa matunda, na hakuna awezaye kuleta kikwazo njiani mwa maendeleo yake. Wafalme wakubwa wa dunia watakusalia na watatafuta baraka katika nguzo zako, na jina lako litatajwa duniani kote kwa heshima na takrima, bali na ya wale pia ambao wameungana nawe. Hakuna shaka ndani yake kwamba sawa na ahadi za Mwenyezi Mungu, baraka zote za kiroho na kimwili zimeunganishwa nawe. Basi, wamebarikiwa wale watambuao hali ya wakati na waimarishe ahadi ya kuwa mwaminifu kwa Jumuiya. Ee Allah, Unijaalie mimi, kizazi changu, jamaa wa karibu na Jumuiya yote, bali dunia nzima, kwa fadhili na rehema yako kufuata njia hiyo, kwani bila fadhili na rehema yako juhudi hazifai na bidii zote hupotea bure. ***Allahumma Amin.***

MAONI YA BAADHI YA MAGAZETI WAKATI WA KIFO CHA HUDHUR[AS]

Alipofariki Hudhur[as], baadhi ya watu walifanya matendo yaliyo kinyume cha ubinadamu, lakini watu wengi waungwana wakaja katika Ahmadiyya Buildings kuwapa Waahmadiyya mkono wa tanzia na kumtazama Hudhur uso wake mara ya mwisho. Kadhalika ndani ya magazeti pia baadhi ya watu walionyesha undani mwao kwa matusi na lugha mbaya, lakini watu wataratibu na waungwana walidhihirisha huzuni wakati wa kifo chake. Maoni ya watu wachache miongoni mwao yanaandikwa hapa chini:

1. Maulana Abul Kalaam Aazaad, mhariri wa gazeti la Wakil la Amritsar aliandika:

> "Mtu yule, mtu mkubwa sana, ambaye kalamu yake ilikuwa na umbuji wa maandishi yenye kuathiri, na alikuwa na ulumbi mkubwa kabisa, yule aliyekuwa mfano wa akili ya maajabu, ambaye mtazamo wake ulikuwa wenye kushawishi na sauti yake ilikuwa ufufuo, ambaye nyaya za mapinduzi zilikuwa zimezongomezwa vyandani mwake, na ambaye mikono yake miwili ilikuwa betri mbili za umeme, yule aliyeendelea kuwa tetemeko na tufani katika ulimwengu wa kidini kwa miaka thelathini, ambaye aliendelea kuwaamsha waliolala akiwa baragumu la Kiama ... ameiaga dunia, ... Kifo cha Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian hakistahili kuwa tusijipatie somo ndani yake. Watu kama huyo ambao kwa njia yao mapinduzi ya kidini na kiakili yanatokea duniani hawaji sikuzote katika dunia. Hawa fahari ya wafanyao mambo ya kihistoria huja kwa nadra sana ulimwenguni, na wajapo huonyesha wameishaleta mapinduzi duniani. Ukuu huu wa Mirza Sahib, licha ya hitilafu sana kuhusu baadhi ya madai yake na itikadi zake, kifo chake kimewatambulisha Waislamu, hasa wale walioelimika na wenye maarifa mapana, kwamba mtu wao mkubwa ametengana nao, na kuondoka kwake utetezi wa Islam wenye shani uliofungamana na dhati yake dhidi ya wapinzani wa Islam umekwisha. Sifa yake hii ya pekee kwamba dhidi ya wapinzani wa Islam yeye aliendelea kutekeleza jukumu la Jenerali mshindi,

> inatulazimisha tukiri waziwazi maono haya... Vitabu alivyoandika Mirza Sahib kukabiliana na Wakristo na Waaria vimeishakubaliwa na watu wote. Katika sifa hii ya pekee, yeye hahitaji utambulisho wowote. Thamani ya vitabu hivyo, leo alipoishatimiza wajibu wake, twalazimika kukiri kwa moyo wote... Hakuna matarajio ya kuzaliwa mtu mwenye shani hiyo katika siku zijazo ndani ya ulimwengu wa dini.[570]

Katika siku hizo katika gazeti hilo la Wakil ilitolewa makala nyingine pia ambayo sehemu yake moja inaandikwa hapa chini:

> "Kuhusiana na khulka zake halionekani hata doa moja dogo kabisa ndani yake. Aliishi maisha akiwa mtu mwema, na alipitisha maisha akiwa mcha-Mungu. Ilmuradi, kihulka na kitabia na kuihudumia na kuihami dini, miaka 50 ya awali ya Mirza Sahib ilimfikisha kwenye daraja teule, ya kipekee yenye kutia wivu."[571]

2. Mhariri Mirza Hairat Delhawii wa gazeti la Delhi, 'Curzon Gazette' aliandika:

> "Huduma bora sana za hali ya juu za Islam alizotoa marehemu katika kukabiliana na Waaria na Wakristo zinastahili kwa hakika kusifiwa mno. Yeye alibadili kabisa njia ya kujadiliana na akaimarisha katika India msingi wa kutunga vitabu kwa njia mpya. Sisi sio tukiwa Waislamu bali na kuwa wahakiki, twalikiri jambo hili kwamba padri au Mwaria hata mkubwa namna gani alikuwa hawezi kufumbua mdomo kukabiliana na marehemu... Ingawa alikuwa Mpanjabi, lakini kalamu yake ilikuwa na nguvu kiasi hiki kwamba leo katika Punjab nzima, bali hata katika India bara hakuna mwenye kuandika kwa ufasaha kama yeye. Maandishi yake yenye nguvu yalikuwa na shani ya kipekee, na ni kweli kwamba hali fulani ya kiroho inatawala kwa kuzisoma baadhi ya ibara zake. Yeye akajitengenezea njia yake safi kwa kupitia matabiri ya hilaki, makinzani na moto wa kukusolewa,

[570] Akhbar Wakil, Amritsar

[571] Akhbar Wakil, 30 Mei 1908

na akafikia upeo wa mwisho kabisa wa maendeleo."[572]

3. Mhariri wa gazeti mashuhuri la wasio Waahmadiyya la Lahore, Tahdhiibun Niswan, aliandika:

"Marehemu Bwana Mirza alikuwa mtakatifu sana, mteule na mtawa wa kiwango cha juu sana, na alikuwa na nguvu ya wema iutiishayo hata moyo mgumu mno. Yeye alikuwa mwanazuoni mjuzi sana, mrekebishaji shujaa na mfano wa maisha matakatifu. Sisi, kidini, hatumwamini yeye kuwa Masihi Mau'udi, lakini mwongozo wake na maelekezo yake kwa wafu wa kiroho yalikuwa ni ya Kimasihi kweli."

4. Baba mzazi wa mhariri wa gazeti la Zamindar, Maulawii Zafar Ali Khan, na pia mwasisi wa gazeti hilo la Zamindar, Munshi Sirajuddin Ahmad aliandika:

"Bwana Mirza Ghulam Ahmad alikuwa karani katika wilaya ya Sialkot mnamo mwaka 1860 au 1861. Wakati huo umri wake pengine ulikuwa miaka 22 au 23 hivi. Nasi twaweza kusema kutokana na kushuhudia kwa macho kwamba yeye hata katika ujana wake alikuwa mwema mno na mtawa, mchamungu sana. Baada ya saa za kazi, wakati wake wote ulikuwa ukitumika katika kutalii elimu ya dini. Kwa nadra sana alikuwa akikutana na watu. Mnamo 1877 nilipata heshima ya kuwa mgeni wake huko Qadina kwa usiku mmoja. Siku hizo pia alikuwa anazama ndani ya ibada na nyiradi kiasi hiki kwamba alikuwa akiongea kidogo sana hata na wageni. Ingawa, hatukupata heshima ya kukubali na kuamini madai au funuo zake, lakini tulikuwa tukimtambua kwa Mwislamu imara.

5. Gazeti la Kiarya, 'Indar' la Lahore, liliandika:

"Bwana Mirza alikuwa anafanana sana na Muhammad[saw] katika sifa moja. Na sifa hiyo ilikuwa uthabiti, hata kama ulikuwa kwa kusudio gani. Nasi tunafurahi kwamba hadi mwisho alikaa imara juu yake, na licha ya makinzani maelfu hakutetereka hata

[572] Curzon Gazette, Delhi, 1 Juni, 1908

kidogo."

6. Mhariri wa gazeti la 'Aria Patrika', Lahore, aliandika:

"Kuliko ule Uislamu upatikanao kwa jumla katika Waislamu wengine, fikara za Mirza Sahib kuhusiana na Islam zilikuwa pana zaidi zenye kuvumilika. Uhusiano wa Bwana Mirza na Waaria haukuwahi kuwa wa kirafiki katu. Na sisi tuikumbukapo historia iliyopita ya Aria Samaj, dhati yake huzalisha mioyoni mwetu harara kubwa sana."

7. Gazeti la Kiingereza "Poineer" la huko Illahabad liliandika:

"Bwana Mirza hakuwa na shaka iwayo yoyote ile kuhusu madai yake. Naye alikuwa na yakini kwa ukweli mkamilifu na ikhlas ya kuwa maneno ya Mwenyezi Mungu yanamteremkia na kwamba alikuwa amejaaliwa nguvu isiyo ya kawaida... Safari moja, yeye alimtupia Askofu Weldon mwito (uliomshtusha) kwamba ashindane naye katika kuonyesha ishara. Na Bwana Mirza alikuwa tayari kwamba sawa na hali za zama, Askofu ajiridhishe kwa njia apendayo kwamba kusiwe na ujanja au udanganyifu wowote katika kuonyesha ishara... Wale watu walioanzisha duniani harakati katika uwanja wa dini, hao katika silika yao, wanashabihiana zaidi sana na Mirza Ghulam Ahmad kuliko Askofu mkuu wa Uingereza. Kwa vyovyote, Nabii wa Qadian alikuwa miongoni mwa watu ambao hawaji duniani sikuzote."[573]

8. Taasisi ya Aligarh, baada ya kuandika kwa kifupi habari za kifo cha Hadhrat Ahmad[as], ikaandika kwamba:

"Bila shaka marehemu alikuwa mpigaji mweleka mkubwa sana wa Islam."

Hali kadhalika, magazeti mengi ya Kiingereza na Kiurdu yaliandika maoni na fikara zao zenye thamani sana, lakini nasikitika kwamba nafasi hamna ndani ya kitabu hiki kuziandika. Na kadiri Jumuiya yake inavyozidi kuenea duniani na kazi yake inavyoendelea kupanuka, ndivyo waandishi habari wakubwa wakubwa wanavyoendela kueleza

[573] Gazeti "Poiner", Ilahabad, 30 Mei 1908

vizuri sifa zake njema. Yakijumuishwa maandishi ya aina hiyo ya magazeti na majarida kuanzia wakati ule hadi wakati huu, kitabu kikubwa chaweza kutayarishwa.

9. Hivi karibuni, mwandishi mashuhuri wa India mwenye jina, Niaz Fatehpuri, mhariri wa gazeti la "Nigaar" la Lucknow, aliandika:

> "Kutalii kwangu kuhusiana na mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya bado hakujakamilika, nami siwezi kusema kwamba muda gani utahitajika kwa kuifahamu sera ya Bwana Mirza na mafundisho yake, mwito wake wa kurekebisha, maelezo yake ya Kuran, nadharia zake za itikadi na mafanikio yake yote kwa kitendo, kwani kutalii hivyo vyote kwa mapana na marefu ni kama kuinywa bahari nzima, na hiyo nafikiri siwezi. Hata hivyo, kama nilazimishwe kueleza maoni yote hadi wakati huu kwa muhtasari tu, basi mimi bila ya kujikalifisha nitasema: Yeye alikuwa ni mtu mwenye azma na uthabiti usio wa kawaida, mwenye akili na busara, aliyekuja na nguvu fulani maalum ya batini, na madai yake ya kuwa Mujadidi na Mahdi hayakuwa mambo yasiyo na msingi. Hakuna shaka kwamba alizihuisha tena kwa yakini khulka za Kiislamu, na ameonyesha kufanyiza Jumuiya ambayo kwa hakika maisha yao tunaweza kusema kwamba ni picha ya mfano mwema wa Mtume[saw]."[574]

[574] Jarida "Nigaar", Luchnow, Novemba 1959

MLANGO WA SABA

SIFA ZA HADHRAT MASIHI MAU'UDI[AS]

Mwishoni, kuhusu sifa za Hadhrat Masihi Mau'udi[as] wakati huu twaona kuwa yatosha kutoa makala moja tu iliyoandikwa na Hadhrat Dkt. Mir Muhammad Ismail. Yeye amesema:

> Kwa fadhili ya Mungu, Waahmadiyya wapo katika kila kona ya India, bali wapo katika nchi za nje pia. Lakini kuna tofauti kati ya Waahmadiyya waliomwona Ahmad[as] na wale wasiomwona. Katika moyo wa wale waliomwona, mpaka sasa inabaki sururi na ladha ya kumwona na kukaa naye. Wale ambao hawakumwona wamekutwa mara nyingi wakisikitika kwa nini hawakufanya haraka na kwa nini hawakuwahi kuona wenyewe uso wa mpendwa huyo katika uhai wake. Kuna tofauti kubwa kati ya picha na mwenye picha. Na tofauti hiyo pia wanatambua wale tu waliomwona mwenyewe. Moyo wangu unataka kwamba niandike kuhusu sura na mazoea ya Seyyidna Ahmad[as] ili ndugu zetu ambao hawakujaaliwa kumwona huyo mwenye baraka wapate nyemi.

SURA TAKATIFU

Badala ya kueleza sura yake na kuandika kuhusu kila kitu, afadhali nitupie macho tu na natija niwaachie wasomaji. Kimuhtasari sura yake yote inaweza kuelezwa kwa sentensi moja hivi: "Alikuwa mfano bora wa uzuri wa kiume." Lakini sentensi hiyo haitakamilika mpaka ya pili iwe pamoja nayo kwamba "Uzuri huo wa kibinadamu ulikuwa na mwanga wa kiroho na nuru."

Na kama alivyotumwa kwa umati huu kijamali, ndivyo ujamali wake ulivyokuwa mfano wa kudra ya Mungu na ulikuwa ukivutia kwake moyo wa mtazamaji. Usoni mwake pamoja na nuru kulikuwa hamna majivuno, tishio na kiburi, bali kulikuwa na unyenyekevu, upole na upendo. Naeleza habari moja kwamba Hudhur[as] alipoenda Dera Baba Nanak kwa kuona Chola Sahib (kanzu ya Baba Nanak), hapo

chini ya mti mmoja shuka lilitandazwa na watu wote wakakaa. Watu wa vijiji vya karibu na wa mji ule hasa walianza kufika kwa kuonana naye na kupeana naye mkono, kila mtu aliyekuja akaelekea kwa Maulawiii Seyyid Muhammad Ahsan na kwa kudhani kwamba huyu ndiye Hudhur[as] akapeana naye mkono na kukaa. Kwa muda fulani watu hawakujua mpaka Bwana Maulawii mwenyewe aliwaashiria na kuwaelezea kwamba "Hudhur[as] ndiye huyo". Hivyo ndivyo ilivyotokea kumhusu Mtume Mtukufu[saw] huko Madina wakati wa kuhamia. Hapo pia watu waliendelea kupeana mkono na Hadhrat Abu Bakar[ra], mpaka yeye aliwaelezea kosa lao kwa kumtilia Mtume[saw] kivuli kwa shuka.

MWILI NA KIMO

Mwili wake haukuwa mwembamba wala mnene sana; naam, alikuwa mnene kiasi. Kimo chake kilikuwa cha wastani ingawa hakikupimwa lakini kilikuwa kiasi cha futi 5 na nchi 8 takriban. Mabega na kifua kilikuwa kipana. Mpaka mwisho wa umri alikuwa anasimama wima hakupindika mgongo wala mabega. Viungo vyote vya mwili vililingana, sio kwamba mikono iwe mirefu sana au miguu, au tumbo liwe limejitokeza mbele. Ilmuradi, hakuwa na ubaya wowote mwilini mwake. Ngozi ilikuwa ya hali ya wastani, si ngumu wala si wa kukwaruza wala si nyororo sana kama ya akinamama. Mwili wake haukuwa mtepetevu, bali ulikuwa madhubuti na mgumu kama wa kijana. Katika umri wa mwisho, ngozi yake haikulegea sehemu yoyote wala haikupata makunyanzi.

RANGI YAKE

> Rangi yangu ni ya ngano na katika nywele pia ni tofauti wazi, kama ilivyobashiriwa katika Hadithi za Mtume[saw] wangu.

Rangi yake ilikuwa ya ngano, ngano ya daraja ya juu, yaani ndani mwake mlimulika nuru na wekundu. Na mng'ao huo wa uso wake haukuwa wa muda bali ulikuwa wa kudumu. Hatukumshuhudia yeye kusawajika kamwe hata wakati wa madhara yoyote, huzuni, majaribio, kesi na misiba. Na daima uso wake uliendelea kung'ara kama dhahabu halisi. Msiba au taabu yoyote haikuondoa mng'ao huo.

Zaidi ya mng'ao huo na nuru hiyo, bashasha na tabasamu ilidumu usoni mwake. Watazamaji walikuwa wakisema kwamba kama mtu huyo ni mzushi na moyoni mwake anajiona ni mwongo, inawezekanaje usoni mwake ziwepo athari za bashasha, furaha, ushindi na utulivu wa moyo. Wema huu wa kidhahiri hauwezi kuungana na mwovu wa batini, na nuru ya imani haiwezi kung'ara usoni mwa mwovu. Siku ya mwisho ya utabiri kuhusu Atham ikaja, na watu katika Jumuiya walikuwa na huzuni usoni, na mioyoni mlikuwa na majonzi sana. Baadhi ya watu kwa kutojua waliwekeana masharti na wapinzani juu ya kifo. Pande zote alama za huzuni zilidhihirika. Watu walikuwa wakilia sana katika sala kwamba Ee Mungu, Usitufedheheshe. Ilmuradi, kulikuwa na makelele hata watu wengi pia wakaonekana kusawajika. Lakini huyu simba wa Mungu anatoka nyumbani akicheka, anawaita wazee wa Jumuiya akitabasamu. Wahudhuriao wanahuzunika, lakini yeye anasema tazameni utabiri umetimia. Nimefunuliwa: اِطَّلَعَ اللهُ عَلٰى هَمِّهٖ وَغَمِّهٖ — Mungu Alijua huzuni na ghamu yake. — Amerejea kwenye haki, na haki imerejea kwake. Watu walimwamini au la, yeye aliishasema yake. Na wasikilizaji wakiona uso wake walipata yakini kwamba yu mkweli; tuna huzuni kubwa na huyu hajali, hana huzuni na anaongea akitabasamu, kana kwamba uamuzi wa jambo la Atham, Mwenyezi Mungu Amemwachia yeye. Kisha yeye akiona kurejea kwake na mhangaiko yake, mwenyewe akampa muda. Na sasa anafurahi kama vile baada ya kumshinda adui, mshindi anavyomwacha kwa ukarimu wake kwamba nenda nakuhurumia, naona aibu kumwua aliyekufa tayari.

Utabiri kuhusu Lekhram ulipotimia, watoa habari haraka sana walianza kutuhumu, ombi la upekuzi lilipelekwa kwa polisi. Mara Mkuu wa Polisi akaja kupekua. Watu wakatenganishwa, waliokuwa ndani ya nyumba hawakuweza kutoka nje, na walio nje hawakuweza kuingia ndani. Wapinzani wakatia bidii kwamba hata kama herufi moja yenye kutia shaka ikipatikana, akamatwe. Lakini hali yake ni ile ile ya furaha na uchangamfu usoni mwake. Mwenyewe anawaleta maafisa wa polisi kuwaonyesha mifuko yake, vitabu, maandishi na barua. Anawaonyesha vyumba na sehemu mbalimbali za nyumba.

Baadhi ya barua walizichukua pia wakidhani kuwa ni zenye kutia shaka, lakini yeye anao uso ule ule na tabasamu ile ile. Kana kwamba sio kutokuwa na kosa bali unasogelea karibu wakati wa ushindi waziwazi na kukamilisha hoja. Kinyume chake watu wanaokaa nje, tazameni nyuso zao. Hao wakiona kila askari akienda ndani na kutoka nje wanahofia, wamekwajuka rangi yao. Hawajui kwamba wanaomhofia heshima yake, yeye humo ndani mwenyewe akiwaita maafisa anawaonyesha mifuko yake na maandishi yake, na ana tabasamu usoni mwake inayomaanisha kwamba sasa hakika ya utabiri itabainika kikamilifu na itathibitika kwamba sihusiki na njama yoyote.

Ilmuradi, hali hiyo ilikuwa katika kesi zote, majaribio na mijadala yote. Na huo ulikuwa mfano bora na kamili wa utulivu wa moyo ambao watu wema wengi wakiuona wakaamini.

NYWELE ZAKE

Nywele zake za kichwani zilikuwa nyembaba sana za singa, lakini, nyangavu, nyororo zilizopakwa rangi ya hina. Hazikusongamana, bali zilikuwa kidogo na nyororo sana, ndefu mpaka shingoni. Alikuwa hanyoleshi nywele za kichwani wala kukatisha fupi sana wala fupi, bali akazifuga kama zinavyofugwa kikawaida hadi ndeweni au shingoni. Alikuwa akipaka kichwani mafuta, ya yasmini, au hina na kadhalika. Hii ilikuwa kawaida yake kwamba alikuwa haachi nywele zikiwa kavu.

NDEVU

Ndevu zake zilikuwa nyingi, zilikuwa madhubuti, nene, nyangavu zilizonyooka na nyororo zilizopakwa rangi nyekundu ya hina. Alikuwa na ndevu ndefu, akakatisha zilizozidi, yaani hakuacha bila kuzisawazisha, bali akazifanya zielekee chini kwa usawa. Akapaka mafuta daima ndevuni pia. Safari moja kwa sababu ya kupata kipele kidogo shavuni, akakatisha nywele zote za sehemu hiyo, ambazo watu wanazo mpaka sasa kama baraka. Ndevu zilikuwa sehemu zote tatu za uso na zilikuwa nzuri sana, si ndogo sana, wala si kidevuni pekee, wala si nyingi kiasi cha kufika mpaka macho.

MNILI NA HINA

Siku za awali alikuwa akitumia mnili na hina. Kisha kwa sababu ya maumivu ya kichwa aliendelea kutumia hina tu kichwani na ndevuni mpaka mwisho wa umri, akaacha mnili. Hata hivyo alitumia kidogo dawa ya kizungu ya kutia rangi katika nywele, kisha kaiacha. Katika siku za mwisho Bwana Mir Haamid Shah Sialkoti alitengeneza dawa ya kutia rangi katika nywele na akamletea Hudhur. Hiyo akatumia. Kwa dawa hiyo, ndevu zikawa nyeusi. Lakini mbali na hiyo akatosheka na kutumia hina tu kwa miaka, ambayo siku ya Ijumaa au baadhi ya wakati katika siku zingine pia, alikuwa akipakwa na kinyozi.

Kama ndevu, masharubu pia yalikuwa madhubuti, manene na maangavu. Alikuwa akiyapunguza lakini si sana kama Mawahabi hata yaonekane yamenyolewa, wala si marefu hata yauguse mdomo.

Mwilini mwake, malaika yalikuwa upande wa mbele tu, hayakuwepo mgongoni. Na baadhi ya wakati alikuwa akinyoa malaika ya kifuani na tumboni au kuyakata. Kwenye miundi alikuwa na malaika kidogo sana nayo yalikuwa mororo na mafupi, kadhalika ya mikono pia.

USO WAKE

Alikuwa na uso mrefu kiasi kidogo. Ingawaje alikuwa na umri kati ya miaka 70 na 80, lakini kulikuwa hamna alama yoyote ya makunyanzi, wala hakuwa na alama za mikunjo kwenye paji la uso kama yanavyokuwa kwa watu wenye kuzama katika mawazo na wenye tabia ya kukasirika. Badala ya kuona alama za huzuni, dukuduku, wasiwasi au majonzi, mwenye kumtembelea alikuwa akiona alama za tabasamu na furaha tu.

Weusi wa macho yake ulielekea kwenye rangi ya manjano — hudhurungi. Macho yake yalikuwa makubwa. Vigubiko vyake vya macho vilikuwa namna ambavyo macho yake yalitazama chini isipokuwa alipoyafumbua kusudi. Hata wakati wa kuongea pia macho yalitazama chini. Kadhalika alipokwenda katika hafla za wanaume, macho yake yalitazama chini. Akikaa nyumbani pia mara nyingi alikuwa hajui kwamba kinanani wapo nyumbani. Yafaa hapa kueleza pia kwamba hakutumia kamwe miwani, na macho yake yalikuwa

hayachoki kufanya kazi. Mwenyezi Mungu aliahidi kulinda macho yake, hivyo, macho yake yalisalimika mpaka mwisho kuugua na kuchoka. Lakini alikuwa akisema kwamba hilali ya usiku wa kwanza haionekani kwangu. Pua ya Hudhur[as] ilikuwa nzuri sana iliyoinuka ya kutosha, nyembamba, iliyonyooka, iliyonyanyuka na ya kustahiki, siyo pana wala nene. Masikio ya Hudhur[as] yalikuwa ya wastani au makubwa kidogo kuliko wastani, hayakujitokeza nje sana, wala hayakugusana na kichwa, yalikuwa makubwa upande wa juu kama kipande cha embe ya mwemba uliopandikiziwa na madogo upande wa chini. Hisia yake ya kusikia kwa fadhili ya Mungu ilibaki nzuri mpaka mwisho.

Mashavu yake hayakubopa wala kunenepa kiasi cha kujitokeza nje wala mifupa ya mashavu haikuinuka. Nyushi zake zilitengana, hazikuungana.

PAJI LA USO NA KICHWA

Paji lilinyooka liliinuka kidogo na lilikuwa pana. Paji lake lilidhihirisha busara na akili ya hali ya juu. Sawa na elimu ya ***fizianomi***[575] paji la aina hii ni mfano mzuri wa sifa bora na hulka nzuri, yaani lile lililonyooka lisilojitokeza nje wala kuingia ndani na liwe limeinuka kidogo yaani liwe kubwa na pana. Kuna baadhi ya mapaji yaliyoinuka lakini si mapana. Sifa zote tatu zilijumuika ndani yake. Tena lilikuwa na uzuri huu pia kwamba lilikuwa halipatwi na mkunjo ila kidogo tu. Kichwa chake kilikuwa kikubwa na kizuri. Sawa na elimu ya ***fizianomi*** kilikamilika kwa kila upande, yaani kilikuwa kirefu pia, kipana pia, kiliinuka kidogo na sehemu kubwa ya upande wa juu ilikuwa sawasawa, na mviringano pia ulikuwa sawa upande wa nyuma. Mapanja yake yalikuwa mapana yaliyodokeza kwenye akili yake ya hali ya juu.

MIDOMO

Midomo yake haikuwa myembamba wala minene kiasi cha

[575] Elimu ya fizianomi (physiogonomy) ni elimu ya kujua khulka za mtu kutokana na sura yake.

kutopendeza. Kinywa chake kilikuwa cha wastani. Wakati wa kutosema, kinywa hakikubaki wazi. Baadhi ya wakati alipokaa kimya kikaoni, alikuwa akifunika kinywa chake kwa sehemu isiyoviringishwa ya kilemba chake.

Katika mwisho mwisho wa umri wake meno yake yaliharibika kidogo, yaani baadhi ya magego yaliharibika yaliyomwumiza wakati mwingine. Safari moja ncha ya gego moja ikawa kali iliyojeruhi ulimi, hapo aliisawazisha kwa kusuguliwa na tupa, lakini jino lolote halikung'olewa kamwe. Alikuwa akipiga sana mswaki. Baadhi ya wakati visigino vyake vilikuwa vikipasuka katika kiangazi ingawaje alikuwa akivaa nguo za majira ya kipupwe katika siku za baridi na za joto, hata hivyo katika majira ya kiangazi alikuwa akipata jasho pia sana lakini jasho lake halikunuka katu hata akibadilisha shati refu baada ya siku kadha hata msimu uwe wa namna gani.

SHINGO

Urefu na unene wa shingo yake ulikuwa wa wastani. Kwa kumfuata Mtume Mtukufu[saw] alikuwa akizingatia kujipamba mwili wake kiasi fulani. Sawa na suna alikuwa anaoga siku ya Ijumaa, kukata nywele, kuzipaka nywele hina, kupiga mswaki, kutia mafuta katika nywele, kutumia manukato, kitana na kioo, lakini kushughulikia sana mambo hayo kulikuwa mbali sana na shani yake.

MAVAZI

Kwanza kabisa yapasa kuzingatia kwamba yeye hakuwa na shauku ya mavazi ya aina fulani maalum. Katika miaka michache ya mwisho alikuwa akiletewa kama zawadi mavazi ya kawaida yaliyoshonwa tayari, hasa koti, kizibau, suruali, shati refu mpaka magoti na kadhalika. Mavazi hayo Sheikh Rahmatullah Lahori alikuwa akimletea kama zawadi kila idi ndogo na idi kubwa. Hayo alikuwa akitumia. Lakini zaidi ya hayo alikuwa akishonesha mwenyewe pia baadhi ya mavazi; hususan kilemba alichotumia mara nyingi alikuwa akinunua mwenyewe. Kama vile mavazi yalivyokuwa yanashonwa na kutumiwa, ndivyo hivyo yalivyotolewa kwa wengine pia, kwani wakati wote watakao kitu cha baraka walikuwa wakiendelea

kumwomba. Baadhi ya wakati alipokuwa akitoa nguo fulani kwa mtu kama baraka, alilazimika kushonesha nyingine ili kuvaa. Na baadhi ya wenye busara walikuwa wakifanya hivi pia kuwa wakamletea nguo mpya na kumwomba Hudhur kupewa nguo yake kama baraka aliyokwishatumia.

Maelezo hayo yaliingizwa tu katikati, sasa sikilizeni kuwa mavazi ya aina gani alikuwa akitumia. Kikawaida alikuwa akitumia mavazi haya: ***Kurta***[576] au ***Qamis, suruali,*** kizibau koti, na kilemba. Zaidi ya hayo lazima alikuwa na hanchifu na katika majira ya baridi alikuwa akitumia soksi pia. Mavazi yake yote yalikuwa na sifa hii kwamba yalikuwa mapana na marefu. Ingawa makoti yaliyoletwa na Bwana Sheikh yalikuwa ya kizungu lakini hayo pia yalikuwa mapana sana na marefu, yaani yalikuwa mpaka chini ya magoti. Na juba alilotumia pia lilikuwa refu kufika pengine mpaka vifundoni mwa miguu, Kadhalika mashati na vizibaa pia vilikuwa vipana.

Alikuwa havai kamwe fulana, alikuwa haoni raha kwa kubanwa nayo. Shati refu nene alilokuwa analivaa, mara nyingi aliacha wazi kifungo cha juu, kadhalika cha kizibau na cha koti pia. Na kama vipo vifungo katika mikono ya shati lake refu, basi daima aliviacha wazi. Matendo yake yalikuwa sawa na مَا اَنَا مِنَ الْمُتَكَلِّفِيْنَ , kwamba ilikuwa kinyume cha tabia yake kujibana katika jambo ambalo si la lazima sawa na sheria, wala alikuwa hajali kamwe kwamba mavazi ni maridadi au yamepigwa burashi au vifungo vimefungwa sawasawa au la. Alihusikana na kupata shabaha hasa tu ya mavazi. Mara nyingi ilionekana kwamba vifungo vilifungwa katika matundu ya vifugo tofauti, pia ilionekana vifungo vya kizibau kufungwa katika matundu ya koti. Muda wote alimakinikia jukumu lake na akazama katika kurekebisha umati kiasi hiki kwamba hakujali kurekebisha mavazi. Katika sehemu ya mwisho ya umri wake, kwa miaka michache mavazi yake yalikuwa mazito tu, yaani katika joto pia alikuwa akitumia koti, kizibau na suruali nzito, na hiyo ilikuwa kwa sababu ya maradhi. Baridi haikuafikiana na afya yake, kwa hiyo mara nyingi

[576] ***Kurta***: Shati pan refu mpaka magoti lisilo na kola, kama hili lina kola, huitwa ***Qamis***.

alikuwa akitumia mavazi mazito. Lakini, katika kiangazi alikuwa akitumia shati refu la melimeli badala ya shati refu nene alilotumia katika kipupwe. ***Pajama***[577] lake lilikuwa la kikawaida la aina ya kisheria (Mwanzoni alikuwa akitumia suruali pana lakini katika miaka ya mwisho ya umri wake akaiacha.) Katika majira ya kiangazi alikuwa akivaa nyumbani shuka wakati mwingine saa za mchana, na kikwaida kavaa shuka saa za usiku akilala.

Nyumbani mara nyingi alikuwa akivaa kizibau, lakini wakati wa kutoka nje, akavaa koti. Na katika siku za baridi kali akavaa makoti mawili, bali baadhi ya wakati kavaa koti la manyoya pia.

Katika mfuko wa kizibau au baadhi ya wakati katika mfuko wa koti alikuwa akiweka leso yake. Daima alikuwa akiweka leso kubwa siyo ndogo wanavyokuwa nayo vijana wa siku hizi. Katika kona zake alikuwa akifunga miski na dawa za lazima alizokuwa akitumia na barua za muhimu. Na katika leso hiyo akafunga sarafu pia walizokuwa wakimtolea watu msikitini kama zawadi. Lazima alikuwa na saa pia, lakini mara nyingi kwa sababu ya kutojaza ufunguo haikuonyesha wakati sawasawa. Kwa kuwa saa ilikuwa ikitoka mfukoni, kwa hiyo alikuwa akiifunga pia katika leso. Alikuwa akiweka saa kwa haja sio kama mapambo.

Kwa kumwona yeye, mtu alikuwa hawezi kusema hata kidogo kwamba katika maisha na mavazi ya mtu huyu kuna kujikalifisha au kwamba anapenda mapambo ya kidunia. Naam, sawa na وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ alikuwa akipenda kitu safi na kuchukia sana kitu kichafu. Alizingatia usafi kiasi hiki kwamba baadhi ya wakati kama hayupo mtu mwingine, yeye mwenyewe akatia dawa msalani.

Alikuwa anajivalia kilemba cha melimeli na hicho mara nyingi

[577] Pajama: Kwa Kiurdu, 'Pa' ndiyo mguu, na 'jama' ni vazi. Pajama ni vazi la kitambaa linalovaliwa kama suruali, na inafungwa kunoni kwa mkanda uliofungwa na nyuzi. Kiingereza kimechukua neno hili katika maana ya vazi linalojumuisha shati na suruali pamoja linalovaliwa wakati wa kulala. Kiswahili kimechukua maana hiyo ya Kiingereza. Katika kitabu hiki pajama limetumika katika maana ya asili. Mwenezi.

kilikuwa yadi 10 au zaidi kidogo. Sehemu ya mwisho ya kilemba isiyoviringishwa ilikuwa ndefu, na baadhi ya wakati alikuwa akiiweka mbele na baadhi ya wakati alikuwa akaiweka sehemu yake juu ya kinywa chake pia wakati wa kuwa kimya kikaoni. Kwa kufunga kilemba alikuwa na njia yake, kona lazima ilikuwa mbele, lakini kichwani alikuwa akiviringisha bila kukaza. Mara nyingi chini ya kilemba alikuwa akitumia tarabushi. Na nyumbani akavaa tarabushi tu akivua kilemba, lakini hiyo ilikuwa nene na laini, siyo ngumu.

Katika majira ya baridi, alikuwa akitumia soksi na wakati wa kutawadha akapitisha mkono ulioloa juu yao. Baadhi ya wakati katika baridi kali akavaa soksi mbili. Lakini mara nyingi alivaa soksi bila miguu kuingia kikamilifu, ikazidi mbele kidogo au sehemu ya kisigino ikawa juu mguuni. Pengine soksi moja alivaa sawasawa na nyingine iliyopinduka. Kama soksi ikipasuka sehemu fulani, alikuwa akipangusa tu juu yake akitawadha, bali akasema kwamba masahaba wa Mtume Mtukufu[saw] pia wakitawadha wakapangusa juu ya soksi za ngozi ambamo sehemu za vidole vyao zilitojikeza nje.

Viatu vyake vilikuwa vya kienyeji vya aina yoyote ya Pathwari, Lahori, Ludhianawii, Salimshahi; akatumia ya aina yoyote, vikiwa vipana kidogo. Hakuvaa mabuti ya Kizungu. Sikumwona Hudhur[as] akitumia viatu vya aina ya sapatu.

Kama viatu vikiwa vinakaza, akafinya visigino vyake, lakini hakwenda nje kwa viatu kama hivyo. Ningetaja kitu kingine pia pamoja na mavazi yake, nacho ni kwamba lazima alikuwa na fimbo. Nyumbani na wakati wa kwenda Masjid Mubarak kila siku kusali hakuishika, lakini wakati wa kwenda Masjid Aqsa au wakati wa kwenda nje kwa kupunga hewa, lazima alikuwa akiishika mkononi. Alikuwa akipenda fimbo ya mti mnene na madhubuti, lakini hakuiegemea akitembea kama yalivyo mazoea ya wazee.

Katika majira ya baridi alikuwa akija msikitini kusali akiwa na shali nzito ambayo mara nyingi ilikuwa begani mwake na akaiweka mbele yake. Baada ya kukaa akaitia juu ya miguu yake. Hali ya kutunza mavazi yake ilikuwa kwamba akivua koti, kizibau, tarabushi na kilemba, alikuwa akiweka chini ya mto, na usiku mzima nguo hizo

zilikuwa zikibaki chini ya kichwa na mwili, ambazo watu waangalifu wanazining'iniza kwa kibanio isije zikapata mikunjo na uchafu. Na asubuhi hali ya nguo ikawa kwamba mpenda mtindo wa kisasa asiyependa mikunjo kama angeziona angechukia.

Katika majira ya kiangazi, mchana pia, lakini mara nyingi usiku alikuwa akivua nguo na akavaa shuka tu. Baadhi ya wakati alikuwa akipata vipele vya harara, kwa hiyo pia alikuwa akivua ***kurta*** pia. Shuka lilikuwa likifikia nusu ya muundi, na sikumbuki kabisa akifunua sehemu juu ya magoti.

Mara nyingi alikuwa na funguo pia, hizo alikuwa akizifunga katika leso au kwa mkanda wa suruali. Hakuwa na kawaida ya kuvaa koti lilojazwa pamba ndani yake, wala alikuwa hatoki nje akijivalia mfarishi, bali alikuwa akitumia shuka la sufu au shali hata hiyo pia hakujivalia kichwani katu, bali ikawekwa mabegani hata shingoni. Hakuwa na mazoea ya kitambaa cha shingoni wala glavu. Kitanda chake kilikuwa na mfarishi uliojazwa pamba kilo 5-6 kwa akali nao ulikuwa mrefu na mpana, godoro na juu yake shuka na mto. Katika kiangazi na kipupwe, majira yote mawili, alikuwa akitandika godoro kwa sababu ya afya yake isiyoafikiana na baridi.

Kazi ya kuandika mara nyingi alikuwa akifanya kitandani. Kidau, kalamu, tandiko na vitabu, vitu hivyo vyote, vikabaki kitandani, kwani sehemu hiyo ilikuwa ikitumika kama meza, kiti na maktaba, na mandhari ya مَا اَنَا مِنَ الْمُتَكَلِّفِيْنَ kwa kitendo ilikuwa ikionekana waziwazi.

Nimesahau kutaja jambo moja, nalo ni hili kwamba alikuwa habadilishi mavazi yake kila siku kama matajiri, bali alikuwa akibadili wakati usafi wake ulipoonekana umeathirika.

KIASI CHA CHAKULA

Katika Kurani Tukufu kuhusu makafiri imetajwa يَأْكُلُوْنَ كَمَا تَأْكُلُ الْاَنْعَامُ — wanakula walavyo wanyama, na katika Hadithi ipo kwamba kafiri anakula katika matumbo saba, na mumini katika moja tu. Muradi wake ni kwamba muminina anakula kitu taibu na anakula kidogo kuliko mtu wa dunia au kafiri. Kama hiyo ndiyo hali ya muminina basi hali ya manabii na mitume itakuwaje! Kwenye tandiko la chakula

cha Mtume Mtukufu[saw] pia mara nyingi kulikuwa na kitoweo kimoja tu, bali chakula chake kilikuwa shayiri zilizokaushwa na kuchomwa na kusagwa, au tende pekee au bakuli la maziwa. Sawa na suna hiyo, Hudhur[as] wetu pia alikuwa anakula kidogo sana, na kwa kulingana na kazi na juhudi alizoshughulikia Hudhur[as] usiku na mchana, mara nyingi kwa kuona chakula cha Hudhur[as] , baadhi ya wakati watu walikuwa wakishangaa na mara wakasema anawezaje mtu huyu kuishi kwa kiasi hiki cha chakula. Hata kama chakula ni kizuri na chenye ladha na hata akisikia njaa sana alikuwa hali kwa kujaza tumbo. Katika siku nzima, kikawaida alikuwa akila chakula mara mbili, lakini baadhi ya wakati alipokuwa hajisikii vizuri akala mara moja pekee. Vilevile asubuhi alikuwa akinywa kikombe kimoja cha chai pia kama kifungua kinywa. Lakini, nifikirivyo, alikuwa hana shauku kabisa ya kula chakula kinono chenye ladha sana.

NYAKATI ZAKE

Kikawaida alikuwa akila chakula cha mchana wakati wowote kuanzia saa 4 hadi adhana ya Adhuhuri, na cha jioni kuanzia baada ya sala ya magharibi hadi wakati wa kulala. Kwa nadra alikula chakula cha mchana baada ya Adhuhuri. Hakuwa na mazoea ya kuka chakula cha jioni kabla ya Magharibi, lakini wakati mwingine akala kabla. Lakini alikuwa na kawaida ya aina mbili. Katika zile siku alipokuwa akikaa nje mpaka baada ya sala za Magharibi na Isha na akala nyumbani, katika siku hizo wakati wa chakula ulikwa baada ya Isha, waila baina ya Magharibi na Isha.

Siku nyingi alikuwa akila chakula nje pamoja na wageni. Na tandiko la chakula lilikuwa likitandikwa katika chumba cha duara au katika Masjid Mubarak. Na wageni maalumu walikuwa wakikaa naye kwenye tandiko la chakula, na watu hao walikuwa wakichaguliwa na Hudhur[as] na idadi yao ilikuwa kutokea watu 10 hadi 20-25.

Alipokuwa akila nyumbani akala pengine pekee yake, lakini mara nyingi pamoja na Hadhrat Amman Jan au mmojawapo wa watoto ama pamoja na watoto wote. Wakati mwingine mimi nikiwa Qaidan, nilikuwa nikipata heshima hiyo ya kukaa kwenye tandiko la chakula cha nyumbani.

Daima alikuwa akila daku nyumbani tu pamoja na mtu mmoja au wawili waliokuwepo, au pekee yake. Lakini nje ya nyumba, alipokula hakula na yeyote. Hiyo haikuwa amri yake, bali kwa heshima yake mahadimu walikuwa wakimpa chakula katika chombo chake peke yake, ingawaje wageni wengine pia walikuwa wakila chakula katika vyombo vyao mbalimbali isipokuwa baadhi ya wakati.

JINSI ALIVYOKULA CHAKULA

Chakula kilipoletwa mbele yake, au tandiko la chakula lilipotandikwa, basi Hudhur[as] akiwa kikaoni, alikuwa akiuliza: Je, tuanze? Alimaanisha kuwa je wageni wote wamekwishaletewa chakula au yupo ambaye hajapata bado. Kisha kwa kupata jibu, alikuwa akianza kula. Kwa muda wote alikuwa akila pole pole akitafuna. Alikuwa hali haraka haraka. Alikuwa akiongea kila aina ya mambo pindi akilapo chakula. Alikuwa akila kitoweo kidogo sana. Na kama katika karamu maalumu, vyakula vya aina mbili tatu vikiletwa mbele yake yeye mara nyingi alikuwa akila aina moja tu. Na dishi lake lililoondolewa baada ya kula mara nyingi lilionekana kana kwamba halijaguswa na yeyote. Hakuwa na mazoea ya kula nyama sana au mboga nyingi, bali alikuwa akila kipande cha chapati kwa kuigusia tu rojo. Alikuwa akitumia kipande kidogo. Alikuwa akikata chapati vipande vidogo vidogo kadha, na hiyo ilikuwa kawaida yake. Na baada ya kuondoka watu, vipande vingi vilipatikana mbele yake kuliko watu wengine, na watu walikuwa wakivichukua wakala kama baraka. Alikuwa akila kidogo sana hata kwamba ingawa akiwekewa chakula sawa na wageni wengine, lakini hata hivyo chakula kingi kilikuwa kikibaki mbele yake.

Wakati mwingine ilionekana kwamba akaweka kipande cha chapati kavu tu kinywani kisha kwa kugusa mchuzi na ncha ya kidole akaugusa ulimi ili kipande kipate kuwa cha chumvi. Katika siku za nyuma alipokuwa akila chakula nyumbani, mara nyingi saa za mchana alikuwa akila chapati ya unga wa mahindi kwa ***Saag*** — aina ya mchicha — au ***Lassi***, yaani maji meupe yanayobaki baada ya kutoa siagi katika maziwa, au alitumia siagi au pengine achari. Alikula ili kupata nguvu tu kwa kutekeleza kazi yake si kwa kupata ladha ya nafsi yake. Mara nyingi alisema kwamba baada ya kula sikujua

kilipikwa nini na nimekula nini. Hakuwa na tabia ya kuiramba mifupa, kutumia vipande vikubwa, kutoa sauti wakati wa kula, kuteuka au kulamba sehani au kutaja uzuri na ubaya wa chakula na ladha zake. Bali kilichopikwa akala. Pengine alikuwa akishika bilauri ya maji au kikombe cha chai kwa mkono wa kushoto na akanywa na akasema kwamba katika umri mdogo niliumia mkono wa kulia kiasi hiki kwamba mpaka sasa siwezi kuchukua kitu kizito kwa mkono huo. Hakuwa na tabia ya kuchutama wakati wa kula, bali alikuwa akikaa kitako au akalaza mguu wa kushoto na kusimamisha goti la kulia.

ALIKUWA AKILA NINI

Nimeshaeleza mapema kwamba lengo lake la kula lilikuwa kupata nguvu tu mwilini sio kupata ladha na utamu. Kwa hiyo, alikuwa akila vitu vile tu vilivyoafikiana na hali yake na vya kuimarisha nguvu ya ubongo ili kazi yake isiathirike. Isitoshe, yeye alikuwa na baadhi ya maradhi pia, kwa hiyo alikuwa akilazimika kuwa mwangalifu kuhusu chakula chake. Lakini kama kawaida alikuwa akila vyakula vyote vizuri. Na ingawa alikuwa akiulizwa mara nyingi kwamba leo utakula nini, lakini, tujuavyo, alikuwa akila sawa na haja yake chochote kilichopikwa. Hakukasirika kamwe kwa sababu ya chakula kuwa na ladha isiyo nzuri, lakini hata akieleza kutopenda chakula na kitoweo kwa sababu ya kutopikwa vizuri, akasema kwamba pengine wageni hawakupenda chakula hicho.

Alikuwa akila chapati ya aina zote mbili, iliyopikwa katika oveni ya udongo au tawa, pia alitumia mkate kwa chai au biskuti na tosti pia, bali alikuwa akisema biskuti za ulaya pia zinajuzu, kwani twajuaje kwamba kuna shahamu ndani yake, maana madai ya mtengenezaji ni kuwa imetumiwa siagi tu, kwa nini tuingie katika dhana mbaya na shaka bila haki. Katika miaka ya mwisho alikula chapati ya unga wa mahindi kwa muda mrefu, kwani tangu miaka 7-8 ya mwisho alipata maradhi ya kuhara na alipungukiwa nguvu ya kumeng'enya chakula. Zaidi ya chapati hizo, alikuwa akila chapati ya unga mweupe uliokandwa kwa maziwa badala ya maji, na mkate wa unga uliochujwa sana uliokandwa katika maziwa badala ya maji pamoja na

sukari na siagi, na pia chapati laini ndogo iitwayo ***kulcha*** kwa Kiurdu na kadhalika. Tuseme aina yoyote ya chapati akiletewa akala tu wala hakuikatalia.

Alikuwa akila kitoweo kidogo sana. Nyama ilikuwa ikipikwa kila siku nyumbani mara mbili, lakini akapenda dengu zaidi kuliko nyama. Dengu hiyo ilikuwa ya ***Mash*** au ***Urd*** inayotambulika sana katika wilaya ya Gurdaspur. Kitoweo cha aina zote na mboga za kila aina zilionekana kikawaida kwenye tandiko lake la chakula. Nyama ya kila mnyama halali na safi alikuwa akila. Alipenda sana nyama ya ndege. Kwa hiyo, baadhi ya wakati alipokuwa na udhaifu mwilini, alikuwa akiagiza nyama ya kwara na tetere kutoka kwa Sheikh Abdur Rahim, Mwislamu mpya. Nyama ya jimbi na tombo pia alikuwa akipenda, lakini tangu ilipozuka tauni katika Panjab aliacha kula tombo, bali alikuwa akikataza. Na alikuwa akisema kwamba nyama yake ina sifa ya kueneza tauni, na kwa kula nyama yake, tauni ilizuka vikali baina ya wana wa Israeli. Safari moja au mbili Hudhur[as] aliletewa nyama ya kenge, akasema inajuzu ale atakaye, lakini kwa vile Mtume Mtukufu[saw] aliichukia kwa hiyo mimi pia naichukia. Na jinsi ilivyofanyika huko, hapa pia watu katika nyumba ya wageni, bali nyumbani pia baadhi ya watoto na watu walikula nyama ya kenge. Lakini, mwenyewe binafsi hakuipenda kabisa. Nyama ya aina yote ya kuku alikuwa akila, ikiwa ni kitoweo ama imechomwa, iwe kababu au pilau. Lakini mara nyingi aliridhika na paja moja tu na hilo lilimtosha, bali baadhi ya wakati sehemu yake ilibaki pia. Pilau pia alikuwa akila, lakini daima laini iliyopikwa vizuri. Wali mtamu baadhi ya wakati alikuwa akiagiza mwenyewe upikwe, lakini ya sukari guru, na hiyo alikuwa akipenda. Vyakula vizuri, yaani kababu, kuku, pilau au mayai na kadhalika ***firni***[578] na wali mtamu alikuwa akiagiza kupika wakati alipohisi udhaifu mwilini. Katika siku alipokuwa na kazi kidogo ya uandishi au afya ilipokuwa nzuri, katika siku hizo alikuwa akila chakula cha kawaida, na ile pia kwa wakati mmoja tu, na wakati wa pili alikuwa akitumia maziwa. Maziwa, malai, siagi bali hata mafuta ya

[578] Unga wa mchele uliopikwa ndani ya maziwa mpaka ukawa mzito na katiwa sukari ndani.

lozi alikuwa akitumia kwa kupata nguvu na kuondoa udhaifu, lakini daima katumia kidogo sana. Baadhi ya watu wameleta upinzani kuhusu vyakula vyake, lakini wapumbavu hao hawana habari hii kwamba mtu aliye mzee na anayo maradhi kadha na juu yake anaendelea kupigana na dunia nzima, anaunda Jumuiya ambayo anachunguza kila mmoja wake, anashughulikia kazi ya kurekebisha umati, vita ya aina tofauti inaendelea na kila dini, ana shughulikia kuandika usiku na mchana, sio katika Kiurdu pekee bali katika Kiajemi na Kiarabu pia, mwenyewe anaandika, mwenyewe anadurusu, mwenyewe anasahihisha na mwenyewe anasimamia uchapaji wake, kisha kusimamia makazi ya wageni na vyakula sawa na daraja zao, kusimamia mijadala, na wajumbe, kuhudhuria kusali, vikao vya msikitini kila siku, na hotuba, kukutana na maishirini ya watu kila siku, kisha kuongea nao kuhusu mambo ya aina aina, kufuatilia kesi, kusoma mamia ya barua kila siku, kisha kuandika majibu ya barua nyingi, kisha kukaa na watoto na mke nyumbani, na nje ya nyumba shughuli za kupokea baiati, kutoa nasaha na kufanya maombi, ilimuradi kwa kazi hizo kiasi hiki na bidii za ubongo na kwa fikara nyingi, kisha uzee na kwa maradhi, kwa jihadi hiyo adhimu kwa kupata nguvu kama mtu anatumia mafuta ya lozi, je ni vibaya? Je, hajui kwamba mafuta ya lozi si kitu cha ladha yoyote, na watu hawayatumii kwa kupata ladha. Hata kama akitumia kitu cha ladha, basi ni faradhi kwa mwenye nia ya namna hii na kwa mwenye kufanya kazi ya aina hii. Naam, kwa wazembe kama sisi vyakula hivyo ni vya anasa.

Kisha inapoangaliwa kwamba mtu huyu anatumia vyakula vya kutia nguvu ni kidogo sana ili kumbakiza hai tu kumkinga asife, basi asiye na akili tu atavihesabu vyakula hivyo kuwa ni kupata ladha za kinyama na furaha ya kibinadamu. Mwenyezi Mungu Ampishe kila muminina mbali na dhana mbaya.

Alikuwa akitumia maziwa, na wakati wa kulala lazima akanywa bilauri moja, na saa za mchana pia. Katika siku za nyuma alitumia zaidi, kwani ikawa hivi kwamba mara baada ya kunywa maziwa alikuwa akipata kuhara. Kwa hiyo akapata udhaifu sana. Ili kuuondoa udhaifu

huo alikuwa akinywa maziwa kidogo kidogo mara mbili tatu katika mchana kwa kupata nguvu.

Katika majira ya kiangazi, saa za chakula cha mchana alikuwa akinywa *lassi* pia, na kama ipo barafu alikuwa akiitumia pia.

Zaidi ya vitu hivyo, katika kiangazi alikuwa akinywa shira ya lozi. Hiyo alitengeneza kwa kusaga malozi machache pamoja na iliki ndogo chache na fuwele za sukari kisha kuvichuja hivyo vyote vizuri na kunywa kwa kuongeza maji. Si kama kawaida, bali wakati mwingine alikuwa akinywa mfululizo kwa siku chache supu ya nyama au ya makongoro. Supu hiyo pia ilikuwa na ladha mbaya, ni maji tu ya nyama iliyochemshwa.

Matunda alikuwa akiyapenda, na mara nyingi ndugu walikuwa wakimletea pia kama zawadi, na mara kwa mara alikuwa akiagiza mwenyewe pia. Miongoni mwa matunda aliyokuwa akipenda zaidi ni zabibu, ndizi ya Bombay, machenza ya Nagpur, tufaha, tikiti na maembe ya Saroli. Matunda mengine pia yaliyokuwa yakiletwa mara moja moja alikuwa akila. Alipenda muwa pia.

Katika msimu wa maforosadi, alikuwa akiyala kwa kuagiza kutoka bustani yake. Na mara moja moja katika siku hizo wakati wa kupunga hewa alikuwa akienda bustanini na kuyachumisha na kutia katika kikapo, akala pamoja na marafiki zake. Kati ya matunda makavu alikuwa akipenda zaidi lozi tu.

Nimeshaashiria nyuma kuhusu chai. Katika majira ya baridi, mara nyingi alikuwa anaagiza kutayarisha chai kwa wageni asubuhi na mwenyewe pia alikuwa akinywa lakini hakuwa na mazoea yake. Alikuwa akitumia chai ya kijani na hakupenda chai nyeusi. Alikuwa akinywa chai kwa kutia maziwa na sukari.

Vitu vya zama hizi, kwa mfano barafu, soda ya limau, soda ya tangawizi na kadhalika pia alikuwa akinywa katika siku za joto, bali katika joto kali mwenyewe alikuwa akiagiza barafu kutoka Amritsar na Lahore.

Hakukataa kula tamutamu za madukani wala hakuchunguza kwamba zimetengenezwa na Mabaniani au Mwislamu. Tamutamu ziletwazo

na watu kama zawadi pia alikuwa akila, na mwenyewe pia alikuwa akiagiza na kuziweka tamutamu za rupa 1-2. Tamutamu hizo zilikuwa kwa ajili ya watoto, kwani walikuwa wakimkimbilia Hudhur[as] mara nyingi kuomba vitu au hela. Sambusa tamu au forosadi, vitu hivi viwili tu, alikuwa akiagiza kwa ajili ya watoto, kwani hivyo vilikukwa vikitayarishwa vizuri siku hizo katika Qadian.

Jambo hili pia lapaswa kukumbuka kwamba alikuwa akijali zaidi chakula cha wageni wake kuliko chake mwenyewe binafsi, na alikuwa akiuliza kwamba mgeni fulani anapenda nini na amezoea kula kitu gani. Maulawii Muhammad Ali M.A. mpaka alipooa, Hudhur alikuwa anafariji kiasi hiki kwamba chini ya usimamizi wake kila siku asubuhi akafululiza kumpelekea maziwa, chai, biskuti, tamutamu, mayai na kadhalika, kisha alikuwa akimwuliza mpelekaji kwamba amekula pia vizuri, ndipo alikuwa akitulia. Kadhalika alikuwa anamtunza sana Bwana Khwaja. Na alikuwa akiuliza mara kwa mara kwamba je, wageni wote wameshakula au wafanyakazi wa nyumba ya wageni hawakughafilika kumtumikia yeyote. Baadhi ya wakati ikawa hivi kwamba hakikubaki kitoweo kwa mgeni fulani au ilisahaulika kumwekea chakula, hapo akampelekea kitoweo chake au chakula chake chote.

Mara nyingi ilitokea hivi pia kwamba aliletewa kitu cha kula kama zawadi, au aliagiza mwenyewe kitu fulani, kisha akakisahau na hicho kikaoza au kikaharibika ndani ya sanduku na kikatupwa chote. Hiyo siyo kazi ya mtu wa dunia. Vitu hivo vingi vilikuwa vikiletwa kama zawadi sawa na ahadi za Mungu, na mara nyingi ikawa hivi kwamba Hudhur alitamani kitu fulani na wakati huo huo mgeni au mfuasi yeyote mwenye ikhlasi akamletea.

Hakuwa na mazoea ya kitu chochote. Alikuwa anatumia tambuu siku moja moja kwa kutia nguvu moyo au kwa kusafisha kinywa baada ya kula, au pengine akipewa na mke, au wakati fulani kwa kikohozi, mafua au tatizo la koo pia alikuwa akiitumia. Alichukia sana kuvuta buruma, tumbaku, bali wakati fulani aliwatoa nje pia baadhi ya wavutaji tumbaku. Naam, wazee waliozoea tangu zamani aliwaruhusu pia kwa sababu ya udhuru wao. Waahmadiyya kadha

waliacha kuvuta buruma kwani wakalazimika kwenda pahali pa kuvuta buruma au wakalazimika kwenda kwenye kundi la Mirza Nidhamuddin. Na kuondoka kikao cha Hudhur[as] na kwenda huko kulikuwa sawa na kutoka peponi na kuendea jahanamu, kwa hiyo watu wenye ghera waliacha kuvuta buruma kwa kudumu.

KUNAWA MIKONO

Hudhur[as] alikuwa lazima akinawa mikono kabla na baada ya kula na katika siku za baridi mara nyingi alikuwa akitumia maji ya moto. Sabuni alikuwa akitumia kidogo sana, alikuwa akikausha mikono kwa kitambaa au taulo. Kama wafanyavyo baadhi ya masheikh, yeye alikuwa hana kabisa tabia ya kukausha kwa ndevu mikono yenye mafuta. Baada ya kula alikuwa akisukutua, na lazima alikuwa anachokonoa meno baada ya kula. Daku katika Ramadhani mara nyingi ilikuwa kitoweo au paja moja la kuku na *firni*, na badala ya chapati kavu ilikuwa chapati ya samli, ingawa alikuwa akila kidogo sana katika hiyo.

KUJINYIMA KULA

Hapa inaonekana itafaa kutaja kwamba katika miaka ya mwanzo ya ujana alijitahidi mno kufanya ibada akijitenga na watu. Safari moja alifunga kwa miezi sita[579] mfululizo kwa takwa la Mungu. Na chakula alicholetewa kutoka nyumbani alikuwa akimpa maskini fulani kwa siri ili watu wa nyumbani wasijue. Lakini, kwa Jumuiya yake hakupenda kujibidiisha vikali hivyo, bali badala yake alisema jihadi ya zama hizi dhidi ya wapinzani wa Islam ni mahubiri na huduma kwa kalamu. Kudhani kuhusu mtu kama huyo kwamba anataka ladha za kidunia, ni nini kama siyo dhuluma tupu?

Katika zama zake, ndani ya nyumba ya wageni mara nyingi ilikuwa ikipikwa dengu na kwa wageni maalumu ilipikwa nyama. Lakini katika siku za mikutano na Idi mbili au wakati wa akika ya watoto wake au wakati wa furaha fulani mara nyingi alikuwa akiamuru kupika pilau au wali mtamu ili maskini pia wapate nafasi ya kushiriki humo.

---

[579] Kutokana na maandishi ya Hudhur[as] saumu za miezi tisa zinathibitika. Mwandishi

UFUNUO

Kuhusu kulisha chakula, aliamriwa katika ufunuo: يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ أَطْعِمُوا الْجَائِعَ وَالْمُعْتَرَّ . Yaani, Ee nabii, mlishe mwenye njaa na mwombaji.

MADAWA

Alikuwa tabibu wa kurithi. Baba yake alikuwa tabibu maarufu wa maeneo haya. Yeye pia alijifunza utabibu, lakini hakuendesha kliniki rasmi, kwa sababu ya kuwa mgonjwa mwenyewe na pia kwa sababu ya ujio wa watu ili kuuliza tiba. Alikuwa akiweka madawa ya kufaa na mashuhuri nyumbani mwake, si ya Kiyunani pekee bali ya Kizungu pia. Na mwishowe yalikuwa yakibaki madawa mengi ya Kizungu tu katika kabati lake. Maelezo zaidi yatapatikana chini ya 'Utibabu'. Hapa ni muhimu kutaja hii tu kwamba alikuwa akitumia madawa ya aina mbalimbali ya kuongeza nguvu ya ubongo, kama mfano koka, kola, mafuta ya samaki, easton syrup, kwinini, *foladi* na kadhalika. Na dawa hata iwe chungu namna gani alikuwa akinywa bila shida.

Akisikia kizunguzungu na baridi, alikuwa akitumia zaidi miski na ambari na daima alikuwa akiagiza iliyo nzuri sana. Katika siku za mwisho jukumu la kununua miski lilikuwa la Hakim Muhammad Husain Lahori aliyevumbua dawa ya *Mufarrih Ambari*. Ambari na miski zote mbili kwa muda mrefu zilikuwa zikiletwa na Seth Abdur Rahman wa Madras pia. Miski alikuwa akihitaji kiasi hiki kwamba baadhi ya wakati alikuwa akifunga katika leso ili aweze kupata akihitaji."

Tanbihi: Makala hiyo ya thamani ya Hadhrat Mir nimenakili kutoka katika kitabu 'Siratul Mahdi', sehemu ya pili, cha Hadhrat Mirza Bashir Ahmad. Yeye aliandika:

"Bwana Mir alikuwa na nia ya kuikamilisha madhumuni hiyo, lakini ni masikitiko kwamba haikukamilika, na sehemu zake zingine hazijaandikwa."

Mimi, mwandishi wa kitabu hiki nasema kwamba kama ingekamilika madhumuni hiyo, ingekuwa kitabu kilichokusanya sifa za Hudhur[as].

Mwishoni, mimi mwandishi mwenye dhambi namwomba Mola wangu Mkarimu kwa unyenyekevu kwamba Ee Mola wangu wa

mbinguni, sawa na uwezo wangu nimejumuihsa baadhi ya habari za maisha ya Masihi wako Mtakatifu katika sura ya kitabu. Nia yangu na utashi wangu ni kwamba viumbe wako wakisoma habari za maisha ya Uliyemtuma wanufaike na kuniombea. Lakini, Ee Mungu wangu Mwumbaji na Mmiliki, jambo la asili ni ridha yako, basi unikubalie juhudi yangu hiyo duni. Unifunike katika shuka lako la maghufira ukinisamehe dhambi zangu, kwani huo ni utashi wangu wa kwanza na wa mwisho. Allahumma Amin.

Ni mimi

Abdul Qadir (Saudagar Mal wa zamani)

Siku hizi mkazi wa Masjid Ahmadiyya, Delhi Darwaza, Lahore. Siku ya Jumatano tarehe 5 Agosti 1959.

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ

MAISHA KWA KIFUPI YA MWANDISHI WA KITABU CHA MAISHA MATAKATIFU

(Na Maulana Abul Ataa Jalandhari)

Nafurahi sana moyoni nikimpongeza rafiki yangu mtaalamu, mpendwa Bwana Sheikh Abdul Qadir, Mwislamu Mpya, Maulawii Fadhil, kwa kuandika "Maisha Matakatifu", kuwajulisha wasomaji waheshimiwa habari za maisha yake.

Sawa na elimu na fikara yangu, Bwana Sheikh ana uhusiano wa moyo kwa Islam na Ahmadiyya, mwenye uchungu moyoni kwa kutumikia Islam, mwenye kuishi maisha ya kawaida na ya mwaminio na ni miongoni mwa wabashiri bora wa Islam. Namjua, bali yu rafiki yangu wa moyo, nami nampenda tangu yeye alipokuwa mwanafunzi. Tangu awali alikuwa na mwenendo mzuri na alijaa jadhaba ya kutumikia dini. Kwa kuwa maisha yake yaweza kuwahimiza vijana kufanya mema, kwa hiyo naona hakuna budi habari za maisha yake pia zitiwe ndani ya kitabu chake. Kwa nia hiyo na makusudio hayo naandika maneno haya:

Sehikh Abdul Qadir alizaliwa tarehe 15 Agosti 1909 katika nyumba ya Baniani Khatri kijinini Gorna Pathanaan, tarafa ya Bhalwal, wilaya ya Sargodha. Wazazi walimpa jina Saudagar Mal. Baba yake Lala Wazir Chand aliwezaje kujua kwamba mtoto wake anayeitwa Saudagar mal kulingana na shughuli zake za biashara, katika zama zijazo atakuwa mfanyabisashara wa kiroho kwa kutumikia Islam na siku moja atakuwa sababu ya kuwaongoza wengi.

Bwana Saudagar Mal alipata masomo katika shule ya msingi kijijini mwake. Alihitimu masomo yake ya darasa la nane katika shule ya Lalian, Wilaya Sargodha. Masomo ya baadaye yalikuwa bado yanafikiriwa, katika hali hiyo alihamia pamoja na familia yake Dhakhira Beranwala, tarafa ya Hafidhabad, wilaya Gujranwala, kutoka wilaya ya Sargodha, na alikuwa anasaidiana katika biashara ya familia yake. Katika hali hiyo, Mungu Alimtayarishia njia ya kuingia

katika Islam. Ilitokea hivi kwamba katika kijiji kile kile cha tarafa ya Hafidhabad ambapo alikuwa anaishi kijana Baniani Saudagar Mal mwenye akili, alikuwepo Mian Muhammad Murad, mwenye duka la nguo, Mwahmadiyya mwenye ikhlasi, Mwislamu mpole, aliyetambulika kwa wema na ukweli wake mpaka mbali. Rafiki yetu mpendwa Saudagar Mal ─ Sheikh Abdul Qadir ─ akapata kujuana na Mian Muhammad Murad. Yeye akiona dalili za mwongozo na wema katika kijana huyo, alianza kumhubiri Islam. Mafundisho ya Islam yaingiayo akilini yalianza kumwathiri moyoni.

Mian Muhammad Murad alipokwenda Qadian kuhuduria mkutanoni mwa mwaka 1924 alimchukua pamoja naye mwenyeji mmoja wa hapo, bwana Allah Javaya Musalli, aliyerudi kwa kuathirika vizuri kwa kuzuru Qadian na kuona mazingira ya hapo. Lakini baada ya kurudi alipoulizwa na watu, alianza kusema kwamba huko Qadian ni biashara tu na udanganyifu. Kwa Saudagar Mal habari ikawa kama fumbo. Aliona kwamba mkazi wa Qadian Mian Muhammad Murad anaishi maisha mema na watu wanamsifu hulka zake, lakini Allah Javaya Musalli anasema huko Qadian kuna biashara na udanganyifu. Kutatua tatizo hilo, Bwana Saudagar Mal aliona hakuna budi kumwona Allah Javaya faraghani. Akamwita Allah Javaya kwenye duka la ndugu zake, wakakaa juu ya rundo la pamba, akamwuliza kwamba unasema kule Qadian kuna biashara na udanganifu, lakini huyo Muhammad Murad ni mbali sana na hali hiyo na anaishi maisha mema; kuna nini hii? Mara Allah Javaya akasema kuwa kauli yangu ni uongo, mimi ni mtu duni wa kijiji. Makabaila wa kijiji wanawapinga watu wa Qadian, kwa hiyo siwezi kusema kweli mbele ya watu. Nawaambia watu wa kawaida sawa na upendo wao ili wafurahi, waila ukweli ni huu kwamba kama Islam ipo popote duniani basi ipo katika Qadian tu. Nakuambia jambo hili la kweli. Kama nikiwaambia watu wengine jambo hilo, makabaila wa kijiji watanifukuza kijijini wakinipiga viatu. Kwa hiyo, mbele yao nitasema jambo lile lile. Lakini ukweli ni huu niliokuambia.

Kwa maongezi haya ya Allah Javaya si tu kwamba tatizo la Saudagar Mal likatatuliwa, bali aliinuka hapo kwa azma hii kwamba mimi mwenyewe nitaenda Qadian na nitashuhudia mambo yote kwa

macho yangu. Ingawa, Saudagar Mal aliichukia Islam kwa kuona hali duni ya Waislamu wa kawaida, kutokuwa na elimu, kukosa hulka njema na hali mbaya ya kiuchumi. Lakini maneno safi ya kuingia moyoni ya Mian Muhammad Murad na mfano wake mwema wa kuvutia moyo ulimlazimisha kwamba aende Qadian akashuhudie mwenyewe hali ilivyo. Wakati huo, alikuwa na matatizo ya ajabu. Kwa mdomo alisema kwamba hata kama dunia nzima isilimu sitasilimu, lakini moyo wake ulikuwa unamvutia kuelekeza kwenye Islam.

Keshoye asubuhi baada ya maongezi ya Allah Javaya, Saudagar Mal akawa tayari kwenda Qadian. Akamwambia Mian Muhammad Murad kwamba naenda Qadian. Mian Muhammad Murad alisema kwamba maongezi yako ya jana usiku na Allah Javaya nilisikiliza kwa masikio yangu katika giza la usiku. Wakati uo huo nilinuia moyoni kwamba kama Saudagar Mal akiwa tayari kwenda Qadian, mimi nitaenda pamoja naye, kwa hiyo naenda nawe.

Basi baada ya muda mfupi, wote wawili wakaondoka kuelekea Qadian. Wakitoka Sangla Hill, badala ya Batala walishuka stesheni ya Chhina, stesheni[580] baada ya Batala, isije jamaa wa Saudagar Mal wakimfuata wakamkamata njiani wakitembea kati ya Batala na Qadian. Msafara huo kutoka Chhina ulifika Qadian. Saudagar Mal, mara baada ya kufika Qadian, alisema katika nyumba ya wageni kwamba mimi ni Baniani, kwa hiyo sitakula chakula kilichopikwa na Mwislamu yeyote. Siku hizo, mwalimu wetu Hadhrat Mir Muhammad Is'hak alikuwa msimamizi wa nyumba ya wageni na alikuwa amejaliwa kipawa maalumu cha kuwakirimu wageni. Yeye alipanga kuagiza chakula kwa Saudagar Mal kutoka kwa Mabaniani, na mpango huo uliendelea kwa wiki moja mfululizo. Katika muda huo Mian Muhammad Murad alimpeleka Saudagar Mal huko na huko ili apate kuonana na wazee walio Waislamu wapya ambao zamani walikuwa Mabaniani na Masingasinga. Kwa kuonana na

[580] Toka Batala reli inaelekea Gurdaspur. Chhina ni stesheni ya kwanza baada ya Batala. Siku hizo garimoshi lilikuwa haliendi Qadian. Waendao Qadian, kwa ajili yao Batala ilikuwa stesheni ya mwisho. Mwenezi.

Hadhrat Abdur Rahim[ra], Hadhrat Bhai Abdur Rahman Qadiani, Hadhrat Masta Sardar Abdur Rahman[ra] B.A., Hadhrat Sheikh Ghulam Ahmad Wa'idh[ra] na Hadhrat Sheikh Muhammad Yusuf[ra], mhariri wa gazeti 'Nur', Qadian, aliathirika sana moyoni Saudagar Mal, kwani watu hao walitokana na Masingasinga na Mabaniani, na kwa kusilimu walipata nuru maalumu na maisha ya kiroho. Mian Muhammad Murad alimpeleka pia kwa wazee Waislamu wa zamani ambao walikuwa wamepata baraka hasa za Jumuiya Ahmadiyya. Maongezi yaliyojaa ikhlasi na mifano bora ya Hadhrat Maulawii Rajeki[ra], mwalimu wangu Hadhrat Hafidh Roshan Ali[ra], Hadhrat Khalifa Rashiduddin[ra], Hadhrat Maulawii Dhulfakar Ali Khan[ra] na Hadhrat Maulawii Abdul Mughni[ra] yaliulazimu moyo wa Sadagar Mal kuwa Sheikh Abdul Qadir.

Ilipokuwa imepita wiki moja tu tangu Saudagar Mal aje Qadian, ujumbe wa watu saba wa jamaa zake wakaja Qadian ili kumrudisha. Watu hao wakaonana na Hadhrat Chaudhari Nasrullah Khan, aliyekuwa siku hizo Nadhir A'laa wa heshima, si wa kulipwa mshahara, na walisisitiza kwamba Saudagar Mal arudishwe nasi. Bwana Chaudhari alisema kwamba mafundisho ya Islam ni لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّيْنِ , kwamba hakuna karaha katika dini, wala hiyo haijuzu. Kama Saudagar Mal akitaka kwenda nanyi, mchukueni bila wasiwai.

Jamaa hao walimwambia Saudagar Mal twende kwetu kijijini, lakini yeye alishakuwa Abdul Qadir moyoni, kwa hiyo akakataa kwenda nao na akawa wa makao makuu ya kuzagaza Islam kwa kudumu.

Siku ya pili au ya tatu, Saudagar Mal alimwomba Khalifatul Masihi II akubali baiati yake na kumwingiza katika Jumuiya Ahmadiyya. Hudhur[ra] akasema, kuna haraka gani? Kaa tu kwa miezi 2-3. Lakini akasema kusisitiza, 'Hudhur, nimeshakuwa na yakini juu ya ukweli wa Islam.' Hapo Hudhur[ra] akamwambia mwalimu wangu Hadhrat Maulana Seyid Muhammad Sarwar Shah[ra] kwamba msomeshe shahada leo, kesho nitapokea baiati. Basi ikafanyika hivyo. Sasa Lala Saudagar Mal akawa Sheikh Abdul Kadir. Alhamdulillah, thumma Al-hamdulillah.

Utamaduni wa Kibaniani ulikuwa na athari kubwa kiasi hiki kwamba

baada ya kusilimu pia, mwanzoni Bwana Sheikh alikuwa akila chakula kilichopikwa na Mwislamu kwa kusitasita sana. Lakini baada ya siku chache akafungamanika kiasi hiki kwamba ikawa vigumu kutambua kwamba kijana huyu amesilimu kutoka kwa Mabaniani au ni Mwislamu wa kuzaliwa. Kwa kweli mabadiliko hayo kikamilifu yalikuwa ni natija ya lazima ya ikhlasi ile aliyokuwa nayo Saudagar Mal moyoni mwake kwa dini. Islam ilinurisha sana ikhlasi hiyo.

Ilipopita miezi michache tu tangu Sheikh Abdur Qadri alipozaliwa kiroho, Pandit mmoja mashuhuri wa Sanatan Dharm, Bwana Raj Narain Armaan akaja Qadian. Sheikh Abdur Qadir alikwisha kuwa mwanafuzi wa Madrasa Ahmadiyya. Mabaniani wachache wa Qadian walimleta Pandit Raj Narain kwa kumwonyesha Madrasa Ahmadiyya, kwani katika Madarasa Ahmadiyya tu wabashiri vijana walikuwa wanatayarishwa ambao walishindana na Aria Samaj na Ukristo kwa ushujaa sana. Kwa bahati tu wakati huo Sheikh Abdul Qadir, Mwislamu Mpya alikuwa amesimama uani, na Mabaniani wa Qadian walishajua kusilimu kwake. Baniani mmoja akiashiria kwa Bwana Sheikh, akamwambia Bwana Pandit kwamba kijana huyu pia alikuwa Baninai lakini sasa ameshasilimu. Bwana Pandit akamwendea Sheikh Abdul Qadir moja kwa moja na kumwuliza kwamba Islamu ina uzuri gani ambao unakosekana katika dini ya Kibaniani. Baada ya kutafakari kidogo, kijana Abdul Qadir akamwuliza Bwana Pandit, 'Niambie lengo la dini ni nini?' Bwana Pandit akajibu, 'Kukutana na Mungu'. Abdul Qadir akasema, 'Umeshapata kukutana na Mungu?' Bwana Pandit akajibu, 'Hapana'. Hapo Bwana Sheih alimwuliza kwamba sawa na elimu yako je, yupo Baniani yeyote hai aliyekutana na Mungu? Sasa pia Bwana Pandit alikana, lakini pia alisema kwamba naweza kusema kuhusu Bwana Ram Chandra na Bwana Karishna. Sheikh Abdur Qadir alisema kwamba nataka kumwona Baniani yeyote wa zama hizi. Hapo, Bwana Pandit akamwuliza kijana Mwislamu mpya kwamba je, waweza kuniambia kuhusu Mwislamu yeyote ambaye amepata kukutana na Mungu? Bwana Sheikh mara moja alitaja jina la Hadhrat Masihi Mau'udi[as] na kwa kuhakikisha ukweli wake akataja ufunuo: يَأْتُوْنَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيْقٍ . Hapo Mabaniani wenzake wakamwita Bwana Pandit na kwenda naye upande mwingine.

Maongezi hayo ya kawaida ambayo Sheikh Abdul Qadir alifanya na mjadili mkubwa wa Kibaniani, katika siku zake za awali yanaonyesha waziwazi kwamba Bwana Sheikh alikuwa imara kiasi gani katika itikadi yake na alikuwa kijana mwenye kuweka lengo lake mbele yake namna gani!

Sasa Bwana Sheikh alikuwa miongoni mwa wanafunzi wenye dalili za kusonga mbele wa Madrasa Ahmadiyya. Alikuwa mwanafunzi mwenye adabu sana na bidii. Mnamo mwaka 1931 alifaulu katika mtihani wa Maulawii Fadhil (Usheikh) wa Chuo cha Panjab (Panjab University). Na baada ya kupata mazoezi ya mahubiri kwa muda fulani, alianza kazi ya mahubiri mnamo mwaka 1934. Kwa miezi michache alifanya kazi chini ya usimamizi wa Hadhrat Maulawii Rajeki, kisha mpaka leo anatumikia dini mfululizo. Kwa muda fulani alikuwa Mbashiri Mkuu katika Karachi pia. Alihubiri katika Lyallpur, Shiekhupura, Sargodha na Lahore. Siku hizi anahubiri katika Lahore kama mbashiri wa Makao Makuu.

Tangu mwanzo Bwana Sheikh alikuwa mwenye uimara na heshima. Alinielezea mwenyewe kwamba mwanzoni tu nilipojuana naye, siku moja wakati wa kwenda msikitini nilimwambia kwamba ipo katika Hadithi ya Mtume[saw] kwamba yule unayempenda yakupasa umwambie. Basi, sawa na Hadithi hiyo nakuambia kwamba nakupenda.

Bwana Sheikh aliponitajia habari hiyo ya zamani, nikakumbuka maisha yake yote ya zama hizo.

Hotuba ya Bwana Sheikh ilikuwa yenye kuathiri, lakini alikuwa akiepa kutoa hotuba iwezekanavyo sawa na tabia yake ya kuona haya. Alikuwa akiongea kwa jadhba na sauti yenye kuathiri katika mjadala. Alikuwa akimbana vizuri mpinzani. Ana shauku ya kuandika pia, lakini mwelekeo wake zaidi ni kwenye mambo ya kihistoria. Alishiriki vya kutosha katika upangaji wa awali wa Tadhkira. Kwa muda fulani alikuwa msimamizi wa Nadharat ya mahubiri na uchapaji.

Mtume Mtukufu[saw] alisema: اَلْاَرْوَاحُ جُنُوْدٌ مُّجَنَّدَةٌ , yaani, roho za watu zikilingana zapendana. Roho zinazolingna zinaanza zenyewe kupendana. Waalimu wetu Hadhrat Maulana Muhammad Ismaili

Halalpuri na marehemu Hadhrat Maulawii Abdul Mughni Khan, Nadhir Da'wato Tabligh walikuwa na upendo maalumu kwa Bwana Sheikh. Na ukweli huu pia umeshuhudiwa kwamba Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (Mungu amweke salama) pia alikuwa akimpenda Bwana Sheikh kwa sababu ya wema na uchamungu wake. Naandika hayo kwa elimu yangu binafsi. Bwana Sheikh anapata sehemu kubwa ya ukarimu na huruma ya Seyyidna Hadhrat Amirul Muminin[atba].

Tangu robo karne takriban, nina mahusiano ya dhati na mapenzi kwa ajili ya Mungu kwa ndugu yangu Bwana Sheikh. Juu ya juhudi yangu sikuweza kumwona Bwana Sheikh akikosana na yeyote isipokuwa mara moja tu. Hayo ni matokeo ya kupenda kwake usalama. Alimwoa binti wa marehemu Sheikh Abdur Rab, Mwislamu mpya. Kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu alipata watoto wengi. Yeye siku zote alikuwa na hali ndogo, lakini alikuwa mwenye subira na kuridhika. Kwa hiyo aliishi kwa uvumilivu, na hakulalamika katu.

Wakati huu umri wa Bwana Sheikh pengine ni karibu miaka hamsini. Naomba, Mwenyezi Mungu Ambariki katika umri wake na Amjalie kutumikia dini zaidi sana, na Akubali sana kitabu chake hiki "Maisha Matakatifu". Amin.

Nampongeza kwa moyo uliojaa mapenzi.

Ni mimi Abul Ataa Jalandhari
17 mwezi mtukufu wa Ramadhani, 1379 hijria
Rabwah, Pakistan. Machi 16, 1960